# FADHILA ZA WATUKUFU WATANO KATIKA SAHIH SITA

## JUZUU YA KWANZA

**Kimeandikwa na:**
Sayyid Murtadha al-Husaini al-Firuzabadi

**Kimetarjumiwa na:**
Alhaj Hemedi Lubumba Selemani

**Kimehaririwa na:**
Alhaj Ramadhani S.K. Shemahimbo

ترجمة

# فضائل الخمسة من الصحاح الستة

## الجزء الأول

تأ ليف

السيد مرتضى الحسيني الفيروز آبادي

من اللغة العربية الى اللغة السواحلية

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN:** 978 - 9987 - 17 – 040 - 1

**Kimeandikwa na:**
Sayyid Murtadha al-Husaini al-Firuzabadi

**Kimetarjumiwa na:**
Alhaj Hemedi Lubumba Selemani

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Desemba, 2013
Nakala: 1000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L. P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** www.alitrah.info

# YALIYOMO


Neno la Mchapishaji ....................................................01

Utangulizi wa Jumuiya ....................................................02

Utangulizi wa Mwandishi ....................................................04


## KUSUDIO LA KWANZA: LAHUSU FADHILA ZA MTUKUFU MTUME (SAWW)


Mlango unaozungumzia nasaba ya Mtukufu Mtume (saww), na kwamba yeye hajatokana na tendo la bila ndoa, kuanzia kwa Adam (as) ....................................................05

Mlango unaozungumzia kuwa kundi, kabila, ukoo, nasaba na asili ya Mtukufu Mtume (saww) ndio bora kushinda za wengine wote ....................................................06

Mlango unaozungumzia kuwa Mtume (saww) aliandikiwa unabii tangu Adam angali baina ya roho na mwili ....................................................08

Mlango unaozungumzia kuzaliwa kwa Mtukufu Mtume (saww) ....................................................08

Mlango unaozungumzia sifa za umbile la Mtukufu Mtume (saww) ....................................................09

Mlango unaozungumzia sifa za Mtukufu Mtume (saww) katika Taurati na Injili....................................................10

Mlango unaozungumzia kuwa uongofu wa Mtukufu Mtume (saww) ndio uongofu bora ....................................................11

Mlango unaozungumzia majina ya Mtukufu Mtume (saww)....................................................12

Mlango unaozungumzia nakshi ya muhuri wa Mtukufu Mtume (saww)....................................................13

Mlango unaozungumzia uzuri wa Mtukufu Mtume na nuru ya uso wake ....................................................14

Mlango unaozungumzia uzuri wa harufu ya Mtukufu Mtume (saww), ulaini wa ngozi yake, tembea yake ya kuyumba, uzuri wa jasho lake, na ardhi kuficha uchafu utokao kwake ....................................................16

Mlango unaozungumzia watu kutabaruku kwa wudhu wa Mtukufu Mtume (saww), kwa mate yake na kwa nywele za kichwa chake....................................................18

Mlango unaozungumzia kuwa Mtukufu Mtume ndiye aliyeweka Jiwe Jeusi sehemu yake kabla ya kukabidhiwa unabii ....................................................19

Mlango unaozungumzia dalili za unabii wa Mtukufu Nabii (saww)....................................................20

Mlango unaozungumzia ushuhuda wa mapadri na makasisi na wengineo

juu ya unabii wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), kabla ya kukabidhiwa unabii wake na baada ya kukabidhiwa........24

Mlango unaozungumzia kuwa Mtukufu Mtume (saww) aliteuliwa kuwa Mtume katika karne bora kushinda zote, na alipoteuliwa majini walifukuzwa........31

Mlango unaozungumzia kuamini kwa an-Najashi pindi Mtukufu Mtume (saww) alipowapeleka baadhi ya Waislamu kwake........32

Mlango unaozungumzia kuwa Mtukufu Mtume (saww) ndiye bwana wa wana wa Adam, hababi wa Mwenyezi Mungu kushinda wote, khalili wa Mwenyezi Mungu na apendwaye zaidi na Mwenyezi Mungu na ndiye mbora zaidi kuliko wao mbele ya Mwenyezi Mungu........33

Mlango unaozungumzia kuwa Mtukufu Mtume alipewa vitu vitano ambavyo hakuna yeyote aliyepewa kabla yake, na kwa vitu sita akawashinda Manabii wote kwa ubora........35

Mlango unaozungumzia kuwa hakika Mtukufu Mtume (saww) ni bwana wa Manabii na Imamu wao, na wao wanamwamini........37

Mlango unaozungumzia kuwa Mtukufu Mtume (saww) ndiye Nabii mwenye wafuasi wengi kushinda Manabii wote........38

Mlango unaozungumzia kuwa Mtukufu Mtume (saww) ndiye mwisho wa Manabii........38

Mlango unaozungumzia kuwa Mtukufu Mtume (saww) huona hadi nyuma ya mgongo wake na huona hata gizani........39

Mlango unaozungumzia kuwa shetani hajifananishi na sura ya Mtukufu Mtume (saww)........40

Mlango unaozungumzia kuwa Mtukufu Mtume (saww) hulishwa na kunyweshwa na Mola Wake........41

Mlango unaozungumzia muujiza wa Mtukufu Mtume (saww) katika maji ya wudhu........42

Mlango unaozungumzia miujiza ya Mtukufu Mtume (saww) katika kunywesha maji........43

Mlango unaozungumzia miujiza ya Mtukufu Mtume katika kulisha chakula........46

Mlango unaozungumzia miujiza ya Mtukufu Mtume (saww) katika shina la mti ambao alikuwa akitolea hotuba hapo........52

Mlango unaozungumzia miujiza ya Mtukufu Mtume (saww) katika kupasuka kwa Mwezi........53

Mlango unaozungumzia miujiza ya Mtukufu Mtume (saww) katika mambo mbalimbali........54

Mlango unaozungumzia ushuhuda wa Ut’bah bin Rabia’h kwamba Qur’ani si mashairi wala si uchawi wala si ukuhani........64

Mlango unaozungumzia kitendo cha Mtukufu Mtume (saww) kuomba mvua ......................................65

Mlango unaozungumzia baadhi ya dua alizoomba Mtukufu Mtume na zikajibiwa ..............................66

Mlango unaozungumzia elimu ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ..............................................................67

Mlango unaozungumzia baadhi ya habari za ghaib alizotolewa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)...........................................................................................................69

Mlango unaozungumzia upasuaji wa kifua cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) .........................................74

Mlango unaozungumzia mwanzo wa kushuka Wahyi kwa Mtukufu Mtume (saww) na jinsi ulivyoshuka.........................................................................................................77

Mlango unaozungumziaMiraji ya Mtume (saww).................................................................................79

Mlango unaozungumzia kumpenda Mtukufu Mtume (saww)................................................................81

Mlango unaozungumzia ukarimu wa Mtukufu Mtume (saww) ............................................................82

Mlango unaozungumzia ushujaa wa Mtukufu Mtume (saww), kupenda kwake kufa kishahidi, na kulindwa kwake na Jibril na Mikail katika mapambano ...........................................84

Mlango unaozungumzia tabia za Mtukufu Mtume (saww) ....................................................................86

Mlango unaozungumzia staha ya Mtukufu Mtume (saww) ...................................................................94

Mlango unaozungumzia ushuhuda wa Abu Sufiyan alioutoa kwa mfalme wa Urumi Harqal wakati akiwa bado kafiri, kuwa hakika Mtukufu Mtume (saww) hasemi uwongo...........................................................................................................94

Mlango unaozungumzia jinsi Ibn Salam alivyotambua kuwa Mtukufu Mtume hasemi uwongo, na akataja jinsi anavyotekeleza ahadi yake .................................................................96

Mlango unaozungumzia kuwa hakika Mtukufu Mtume anawapenda masikini na anachukia kuwaona watu wakimsimamia, wakibusu mkono wake au kutembea nyuma yake..........................................................................................................97

Mlango unaozungumzia mizaha ya Mtukufu Mtume (saww) na tabasamu lake...................................98

Mlango unaosema kuwa Mtukufu Mtume (saww) alikuwa mbali na madhambi kuliko watu wote, na alikuwa akiharakisha ..........................................................100

Mlango unaozungumzia kuketi kwa Mtukufu Mtume (saww) na malaika kutembea nyuma yake..........................................................................................................101

Mlango unaozungumzia fadhila za kumswalia Mtukufu Mtume (saww) ............................................102

Mlango unaozungumzia swala ya Mtukufu Mtume (saww).................................................................103

Mlango unaozungumzia kulia kwa Mtukufu Mtume katika swala na pindi anaposoma Qur'ani tukufu....105

Mlango unaosema kuwa Mtukufu Mtume (saww) alibeba tofali la kujengea msikiti na alibeba udongo siku ya handaki. na unabainisha sehemu ya mashairi yake....106

Mlango unaozungumzia tawakali ya Mtukufu Mtume (saww) kwa Mwenyezi Mungu....00

Mlango unaozungumzia jinsi Mtukufu Mtume (saww) alivyowataka ushauri masahaba zake licha ya kuwa yeye ndiye mwenye akili zaidi kushinda watu wote....108

Mlango unaozungumzia maisha ya Mtukufu Mtume (saww) na kujinyima kwake....108

Mlango unaosema kuwa Mtukufu Mtume (saww) aliongezewa majaribu kama alivyoongezewa malipo....115

Mlango unaosema kuwa malaika wa mauti aliomba idhini kwa Mtukufu Mtume (saww) na hakuwahi kuomba idhini kwa yeyote kabla yake....116

Mlango unaosema kuwa Mola Mlezi ndiye aliyekuwa wa kwanza kumswalia Mtukufu Mtume – baada ya kufariki - juu ya Arshi Yake....118

Mlango unaosema kuwa Mtukufu Mtume (saww) ni mzuri wa harufu kuanzia alipokuwa hai hadi alipokuwa maiti....119

Mlango unaosema kuwa malaika hushuka katika kaburi la Mtukufu Mtume kila siku. na unabainisha fadhila za kumzuru....120

Mlango unaozungumzia kauthari ya Mtukufu Mtume na cheo kinachosifika, na kwamba huko peponi atamuoa kadhija, Mariam binti Imran, mke wa Firauni na dada yake Musa....121

## KUSUDIO LA PILI: LAHUSU FADHILA ZA ALI BIN ABU TALIB (AS)

Mlango unaozungumzia wingi wa fadhila za Ali (as)....123

Mlango unaosema kuwa nuru ya Mtukufu Mtume (saww) na ya Ali (as) ziliumbwa kabla ya Adam (as), na waliumbwa kutokana na udongo mmoja....124

Mlango unaosema kuwa Adam (as) alimuomba Mwenyezi Mungu kwa haki ya Muhammad, Ali, Fatimah, Hasan na Husein (as), toba yake ikakubalika....125

Mlango unaosema kuwa Mtukufu Mtume (saww) na Ali (as) wanatokana na mti mmoja....126

Mlango unaosema kuwa Mwenyezi Mungu alimteua Mtukufu Mtume (saww) na Ali (as)....127

Mlango unaosema kuwa Mwenyezi Mungu alimtia nguvu Mtukufu Mtume kupitia Ali (as)....129

Mlango unaosema kuwa hakika Ali (as) alizaliwa ndani ya Ka'aba na yeye ana cheo sawa na Ka'aba....130

Mlango unaosema kuwa Mtukufu Mtume (saww) alimchukua Ali (as) kutoka kwa Abu Talib ....131

Mlango usemao kuwa Ali ndiye wa kwanza kuukubali Uislamu....131

Mlango usemeao kuwa Ali (as) ndiye mtu wa kwanza kumwamini Mtukufu Mtume (saww) ....133

Mlango usemao kuwa imani ya Ali (as) itashinda ....142

Mlango usemao kuwa Ali (as) ndiye mtu wa kwanza kuswali....142

Mlango unaosema kuwa hakika Ali (as) huswali kama Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ....149

Mlango unaozungumzia uzuri wa uso wa Ali (as) na nakshi za pete zake....150

Mlango unaozungumzia majina ya ubaba ya Ali (as) na baadhi ya lakabu zake tukufu ....151

Mlango unaosema kuwa dua huzuiliwa mpaka atakaposwaliwa Muhammad na Aali Muhammad ....153

Mlango unaosema: swala haikubaliki mpaka atakaposwaliwa humo Muhammad na aali Muhammad (as) ....155

Mlango unaozungumzia namna ya kumswalia Muhammad na aali Muhammad....156

Mlango unaosema kuwa hakika Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as) ndio aali Muhammad ....163

Mlango unaokataza kumswalia Mtukufu Mtume (saww) swala kigutu....166

Mlango unaosema kuwa aya ya utakaso iliteremka kwa ajili ya Mtukufu Mtume (saww), Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as)....166

Mlango unaosema kuwa Mtukufu Mtume aliapizana kupitia Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as) ....181

Mlango unaosema kuwa Mtukufu Mtume (saww) alimwambia Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as): mimi ni mwenye kumpiga vita yule mwenye kuwapigeni vita na ni mwenye kuishi kwa usalama na yule mwenye kuishi kwa usalama na ninyi:....186

Mlango unaosema kuwa atakayempenda Mtukufu Mtume (saww), Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as) atakuwa pamoja na Mtukufu Mtume katika daraja lake....188

Mlango unaoeleza kuwa aya ya Mawadah imeteremshwa kwa ajili ya karaba wa Mtukufu Mtume (saww), nao ni Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as)....191

Mlango wenye kuelezea aya ambazo zimeteremshwa kwa ajili ya maadui wa Ali (as)....195

Mlango unaosema kuwa hakika Mwenyezi Mungu ameupunguzia ummah huu kwa kuwaondoshea (wajibu) wa sadaka ya mazungumzo ya siri kupitia Ali (as)..........................210

Mlango unaoelezea kuwa hakuna yeyote aliyeifanyia kazi aya ya mazungumzo ya siri isipokuwa Ali (as).........................................................................................................212

Mlango unaozungumzia cheo cha Ali (as) kwa Mtume (saww)...........................................................214

Mlango unaozungumzia kauli ya Mtukufu Mtume (saww) kwa Ali (as): cheo chako kwangu mimi ni sawa na cha Harun kwa Musa. ...............................................................216

Mlango unaosema kuwa Ali (as) ni ndugu wa Mtukufu Mtume (saww) .............................................229

Mlango usemao kuwa hakika Ali (as) ni waziri wa Mtukufu Mtume (saww).....................................240

Mlango unaozungumzia kauli ya Mtukufu Mtume (saww): Ali (as) ni sehemu yangu na mimi ni sehemu ya Ali (as)..........................................................................................243

Mlango unaosema kuwa hakika Ali (as) nyama yake ni nyama ya Mtume (saww) na damu yake ni damu ya Mtukufu Mtume (saww)....................................................248

Mlango unaosema hakika Ali (as) ni nafsi ya Mtukufu Mtume (saww)...............................................249

Mlango unaozungumzia kauli ya Mtukufu Mtume (saww) aliyosema siku ya ghadir khum kuhusu Ali (as): yeyote ambaye mimi ni mtawala wake Ali (as) ndiye mtawala wake.........................................................................................................251

Mlango unaozungumzia kauli ya Umar na Abu Bakri kwa Ali (as): umekuwa mtawala wa kila muumini mwanaume ..........................................................................................277

Mlango unaosema kuwa Mtukufu Mtume (saww) alimfunga kilemba Ali (as) siku ya Ghadir Khum kwa mtindo wanaofunga Malaika .....................................................................279

Mlango unaosema kuwa aya: "Ewe Mtume fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola Wako." iliteremka siku ya Ghadir Khum katika fadhila za Ali (as).........................280

Mlango unaosema kuwa aya: "Leo nimekukamilishieni dini yenu" iliteremka siku ya Ghadir Khum.........................................................................................................280

Mlango unaoeleza kuwa adhabu ilimteremkia Harith bin Nuuman pale alipokanusha Mtume (saww) kumsimika Ali (as) siku ya Ghadir Khum.............................................281

Mlango unaosema kuwa hadith ya Ghadir Khum ni dalili inayothibitisha ukhalifa wa Ali (as) baada tu ya Mtukufu Mtume (saww) ...................................................................282

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako asili yake ni cha Kiarabu na kinaitwa, *Fadha'ilu 'l-Khamsah min Sihah Sittah*, kilichoandikwa na mwanachuoni mahiri aitwaye Sayyid Murtadha al-Husaini al-Firuzabadi. Sisi tumekiita, *Fadhila za Watukufu Watano katika Sahih Sita.*

Kitabu hiki ni matokeo ya utafiti uliofanywa na mwanachuoni huyu juu ya utukufu na fadhila za watukufu watano kutoka katika vitabu sita maarufu vya wanavyuoni mashuhuri wa Kisunni viitwavyo, *Sihaa Sittah.*

Ni jambo la kupendeza kwamba pamoja na kuhitilafiana baina ya Sunni na Shia lakini kuna mambo mengi ya kimsingi ambayo wote wanakubaliana; na cha kufurahisha zaidi ni kwamba mambo hayo yamehifadhiwa vizuri katika vitabu vya historia na hadithi vya wanavyuoni wote Shia na Sunni.

Mwandishi wa kitabu hiki amechagua kufanya utafiti wake kwenye vitabu vya *Sahih Sita* vya Sunni ambavyo ni vitabu vikubwa vya hadithi kwa upande wa ndugu zetu Masunni. Utafiti huu ni kwa ajili ya kuelimishana tu na si vinginevyo. Kusema kweli ni muhimu sana kujua imani za watu wengine kupitia vyanzo vyao wenyewe vilivyo sahihi badala ya kutafuta habiri hizo kupitia vyanzo ambavyo sio sahihi na wala si vya kuaminika, na matokeo yake kuleta malumbano yasiyo na natija katika jumuiya yetu ya Waislamu.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Kutoka na ukweli huu, taasisi yetu ya Al-Itrah imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumini yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu Al-Haj Hemedi Lubumba Selemani kwa kazi kubwa aliyofanya ya kukitarjumi kwa Kiswahili; pia na wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah Mwenye kujazi awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera. Amin.

**Mchapishaji**
**Al-Itrah Foundation**

# UTANGULIZI WA JUMUIYA

Baada ya kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **"Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara,"**[1]mazungumzo kuhusu fadhila za watu watano yataendelea kuwa fadhila, kwani bila shaka sifa hii ya kimungu imekuwa ni alama inayowetanginisha Ahlul-Baiti (as) mbali na wasiokuwa wao pindi mawazo yanapogongana, fitina inapozuka na madhehebu kujitokeza, kwani ni lazima ummah uwe na alama iliyo wazi na taa iangazayo inayoongoza safari kadiri masafa yanavyozungukwa na upotevu na kuzingirwa na sababu za upotevu.

Hakika Ahlul-Bait (as) walitekeleza jukumu lao hili kubwa, bila kuchoshwa na giza lililokuwa likiuvamia msafara, hiyo ni kwasababu wao pembozoni mwao wamebeba asili ya ujumbe na msingi safi na imani ya kweli. Hakika kutaja fadhila za Ahlul-Baiti (as), licha ya kwamba ni sababu inayomfanya mtu kufuata athari zao na kuwafanya mwongozo wake, pia kwenyewe tu ni fadhila kubwa na ni neema isiyo na mbadala.[2] Na kwakweli kwa kutazama tu juu juu historia inatosha kutubainishia nafasi yao muhimu ndani ya karne zote. Na kwa ajili hii ndio maana Waislamu hawajazama kwa kina ndani ya pande zote za historia ya mtu baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kama walivyojihusisha na Ahlul-Baiti maasumina (as), hakika wamepokea fadhila zao na wametangaza ubingwa wao, na wametamani kila kilichotoka kwao, sawa iwe kauli au kitendo. Na hii si gharibu baada ya kuwepo kauli ya Mwenyezi Mungu: **"Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa jamaa zangu wa karibu."**[3]

Kuanzia hapa tunaviona vitabu vya tafsiri na hadithi vimesheheni ufafanuzi wa fadhila zao na ubainifu juu ya nafasi yao, licha ya kwamba maadui zao walifanya kila waliwezalo katika kuficha fadhila zao na kufunika maneno yao. Hakika hazina ya Bani Umaiyyah na Bani Abbas ilikuwa wazi kwa kila mwenye kuleta hadithi ya uwongo yenye kuficha nafasi yao au kupunguza hadhi yao, kama ambavyo tawala ovu zilimfuatilia kwa ubaya kila aliyepokea fadhila kuhusu wao au kusimulia jema lolote linalowahusu wao.

Si vitabu vya wafuasi wao, si vya ulamaa wa kambi ya Ahlul-Baiti (as) na wasimulizi wao ndio vilivyotaja fadhila zao tu, bali ni kwamba pia *Sahih Sita* za ndugu zetu Masunni na *Masanid* zao zimesheheni fadhila na sifa za Ahlul-Bait (as) baada ya kutaja fadhila za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Bali ni kwamba hakuna mtu aliyepokea fadhila za Sahaba yeyote kwa njia nzuri kama zilivyopokewa fadhila za Ali bin Abu Talib (as).[4]

Al-Allamah Sayyid Murtaza al-Fayruz Abad amefanya kazi ya kukusanya na kupangilia hadithi zilizopokewa kuhusu fadhila za Mtukufu Nabii (s.a.w.w.) na Ahlul-Baiti wake (as), kutoka kwenye vitabu zaidi ya arobaini na sita vya ndugu zetu Masunni,[5] na muhimu zaidi ni *Sahih Sita* zinazokubalika kwao, bali ni vitabu ambavyo wao wana yakini na usahihi wa yale yaliyomo ndani yake.[6] Bali kwao ndio vitabu sahihi baada ya Qur'ani kwa ijmai yao.[7]Hakika juhudi hizi za kielimu zinafaa kuleta umoja baina ya Waislamu na kuondoa tofauti zao za kimakundi kwa kuwafanya kitu kimoja, tofauti ambazo ugandamizaji wa kimataifa unajitahidi kuzitumia ili kummaliza yule aliyeshikamana na ummah na safu yake imara.

---

[1] Sura Ahzab: 33.

[2] Sura al-Maidah: 3.

[3] Sura Shura: 23.

[4] Kuna hadithi imepokewa kutoka kwa Muhammad bin Mansuri kutoka kwa Ahmad bin Hanbal na Ismail bin Ishaq al-Qadhi ndani ya *al-Istiab* Juz. 2, uk. 466. Na *Mustadrakus-Sahihayn* Juz. 3, uk. 107. Na *Sawaiqul-Muhriqah*uk. 72. Na katika *Nurul-Absar* ya Shablanjiy uk. 73. Na *Fathul-Bariy* Juz. 8 uk. 71.

[5] Mwandishi ameorodhesha rejea hizi katika juzuu la kwanza katika chapa ya pili. Nasi tumezitaja mwishoni mwa juu tatu za chapa hii iliyofanyiwa tahakuki.

[6] *Tadribur-Rawi* Juz. 1, uk. 131.

[7] *Sawaiqul-Muhriqah*, Mlango wa Kwanza, Faslu ya Kwanza, uk. 18.

Ili kukamilisha juhudi hizi, kamati ya tahakiki imetekeleza kazi zifuatazo:

1. Kuhakiki maelezo ya kitabu na kuyaoanisha na rejea na kusahihisha (palipohitaji kusahihishwa).
2. Kwa kuwa mwandishi alitegemea chapa za zamani, katika pambizo tumeashiria anwani za ndani za rejea husika, ili kwamba mtafiti aweze kurejea huko katika chapa tofauti.
3. Kutoa na kuthibitisha maelezo ambayo yalikuwa hayajathibitishwa.

Jumuiya ya Kimataifa ya Ahlul-Baiti kwakuwa inathamini juhudi hizi kubwa na ulinganiaji huu mzuri, inaona ni wajibu juu yake kuchapisha tena mistari hii ya kudumu, ikiamini kwamba hakika ummah wa Kiislamu ni jengo moja lililoshikana, hivyo baada ya kauli ya Mwenyezi Mungu: **"Kwa hakika huu ummah wenu ni ummah mmoja, na Mimi ni Mola wenu Mlezi. Kwa hivyo niabuduni Mimi."**[8]Halibomolewi na nguvu za mfarakano wala haliguswi na mikono ya upumbavu na ujinga.

**Jumuiya ya Kimataifa ya Ahlul-Bait (as)**
**Qum Tukufu.**

[8] Sura Anbiyai: 92.

# UTANGULIZI WA MWANDISHI

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu***.**

Mwenyezi Mungu anastahiki himidi nyingi, na utakatifu ni Wake asubuhi na jioni. Swala na salamu zimfikie yule aliyemtuma kubashiri na kuonya, Muhammad (saww). Ziwafikie pia watu wa nyumba yake ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na kuwatakasa barabara. Khususan binamu yake aliyesimikwa kama alama na kiongozi. Na laana ziwe juu ya maadui zao na juu ya yule mwenye kuwafanyia uadui vipenzi vyao, na ziwe juu ya yule mwenye mapenzi na maadui zao ambao Mwenyezi Mungu amewaandalia moto uchomao: **"Ule Moto ukiwaona tangu mahali mbali wao watasikia hasira yake na mngurumo wake."**[9]

Ama baada, huu ni muhtasari kuhusu fadhila za watu watano (as). Nimeuchukua kutoka kwenye *Sahih Sita* na vitabu vinginevyo vya Masunni, vile vyenye kukubalika kwao, nimeukusanya na kuuweka ndani ya karatasi, nikitaraji kwamba utawanufaisha Waislamu wote. Hivyo kama mwenye kuuchunguza ni katika wasiokuwa wao, inshaallah ataongoka. Na kama mwenye kuuchunguza ni katika watu wa uongofu na imani basi imani yake itazidi, na Mwenyezi Mungu ndiye mmliki wa taufiki.

Kitabu hiki kimepangiliwa katika makusudio matano na hitimisho. Mwanzoni mwa kitabu tumetaja rejea za kitabu, na tumeonesha chapa za rejea, kama ambavyo katika kila hadithi tunataja namba ya juzuu ya kitabu husika na namba ya ukurasa, isipokuwa kama ni kutoka kwenye Sahih mbili, Bukhari na Muslim, hapo tunataja chapa yake, kitabu na mlango. Au kama ni kutoka kwenye kitabu cha tafsiri, basi hapo tunataja Aya na Sura. Hivyo tunawataka wasomaji wapendwa watakapo kufanya tahakiki katika hadithi na rejea husika, basi warejee chapa ileile tuliyoitaja, kama itawezekana kufanya hivyo, hiyo ni ili kusiwepo tofauti katika namba ya juzuu na namba za ukurasa, na hatimaye wakanituhumu kwa sahau na usahaulifu, ijapokuwa mwanadamu (asiye maasumu) hakosi kusahau hata kama atajitahidi kiasi gani kudhibiti na kuchunga kwa umakini, na Mwenyezi Mungu ndiye mlinzi.

[9] Sura al-Furqan: 12.

# KUSUDIO LA KWANZA:

# LAHUSU FADHILA ZA MTUKUFU MTUME (SAWW)

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA NASABA YA MTUKUFU MTUME (SAWW), NA KWAMBA YEYE HAJATOKANA NA TENDO LA BILA NDOA, KUANZIA KWA ADAM (AS)

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 300:**

Amesema: Kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Mimi ni Muhammad bin Abdullah bin Abdul-Muttalib bin Hashim bin Abdumanaf bin Qusway bin Kilab bin Murah bin Kaabi bin Luayi bin Ghalib bin Fahri bin Malik bin Nadhir bin Kinanatah bin Khuzaymatah bin Mudrikatah bin Ilyasa bin Mudhiru bin Nazari bin Ma'di bin Adnan bin Adi bin Adudi bin al-Humaysau bin Yash'hab bin Nabtu bin Jamili bin Qaydari bin Ismail bin Ibrahim bin Tarikh bin Nahur bin Ashu'u bin Aru'us bin Faligh bin Abir – Nabii Hud- bin Shalikh bin Arfakhshad bin Sam bin Nuh bin Lameki bin Mutawashalakh bin Akhnukhu – Nabii Idirisa – bin Azdi bin Qaynan bin Anush bin Shaythu bin Adam (as)."

Amesema: Kaiandika Daylamiy.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 106:**

Alisema: "Nilikuwa na Adam peponi nikiwa katika mgongo wake. Na alinipandisha safina katika mgongo wa baba yangu Nuhu. Nikatupwa ndani ya moto nikiwa katika mgongo wa Ibrahim, kamwe wazazi wangu hawakukutana pasi na ndoa. Mwenyezi Mungu aliendelea kunihamisha toka migongo safi kwenda kwenye matumbo ya uzazi yaliyo tohara, nikiwa safi mwenye kuongozwa, hayakuzalika matawi mawili isipokuwa nilikuwa katika tawi bora zaidi. Hakika Mwenyezi Mungu kwa unabii alichukua agano langu na kwa Uislamu ahadi yangu, na akautangaza utajo wangu ndani ya Taurati na Injili, na kila Nabii alibainisha sifa yangu, ya kwamba ardhi itang'aa kwa nuru yangu na mawingu yatang'aa kwa wajihi wangu. Alinifundisha Kitabu chake na akanipaisha mpaka mbinguni kwake, na akanipa jina kutoka kwenye jina lake, hivyo Mkuu wa Arshi anaitwa Mahmudu nami ni Muhammad. Aliniahidi kunizawadia Hodhi na Kawthari, na kunifanya mwombezi wa kwanza na wa kwanza kukubaliwa uwombezi wake. Kisha alinitoa katika karne bora kwa ajili ya ummah wangu, nao ni wenye kumuhimidi, ni wenye kuamrisha mema na ni wenye kukataza maovu."'Amesema: Ibn Asakir ameiandika kutoka kwa Ibn Abbas.

**Tabaqat Ibn Sa'd Juz. 1, Sehemu ya kwanza, uk. 31:**[10] Kitabu hiki chajulikana kwa jina la *Tabaqatul-Kubra*:

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ja'far bin Muhammad kutoka kwa baba yake Muhammad bin Ali bin Husain (as) kwamba Mtukufu Mtume (saww) alisema: "Hakika nimetokana na ndoa na sikuto-

[10] *Tabaqatul-Kubra*: Ametaja mama zake na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

kana na tendo lisilo la ndoa tangu kwa Adam, na tendo lisilo la ndoa la ujahiliya halikunigusa hata kidogo, sikutoka isipokuwa kwenye usafi wake."

**Nasema:** Hakika habari zinazoonesha kuwa ametokana na ndoa na hakutokana na tendo lisolokuwa la ndoa tangu kwa Adam, ni nyingi sana, nasi tumetosheka na hizi mbili tulizozitaja.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA KUWA KUNDI, KABILA, UKOO, NASABA NA ASILI YA MTUKUFU MTUME (SAWW) NDIO BORA KUSHINDA ZA WENGINE WOTE

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2 Uk. 269:**[11]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwaal-Mutwalib bin Abi Wada'ah amesema: "Alikuja Abbas kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kana kwamba amesikia kitu, Mtume akasimama juu ya mimbari na kusema: 'Mimi ni nani?' Wakasema: 'Wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu salamu iwe juu yako.' Akasema (saww): 'Mimi ni Muhammad bin Abdullah bin Abdul-Muttalib, hakika Mwenyezi Mungu aliviumba viumbe na akaniweka katika kundi bora kuliko yote, kisha akawafanya makundi mawili, akaniweka katika kundi bora kuliko yote, kisha akawafanya makabila na akaniweka katika kabila bora kuliko yote, kisha akawafanya koo mbalimbali na akaniweka katika ukoo bora kushinda zote, na katika nasaba bora kushinda zote."

**Mustadrakus-Sahihayni Juz. 4 Uk. 73:**[12]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Umar, amesema: "Tukiwa tumeketi mbele ya uwanja wa nyumba ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, ghafla alipita mwanamke, mtu mmoja kutoka katika jamaa akasema: 'Huyu ni binti wa Muhammad.' Abu Sufiyan akasema: 'Hakika Muhammad kwa Bani Hashim ni mfano wa ua katikakati ya mabaki ya mashuke.' Mwanamke alikwenda na akamwambia Mtume habari hiyo, Mtume (saww) alitoka huku uso wake ukiwa na alama za ghadhabu, akasema: 'Zina nia gani kauli zilizonifikia kutoka kwa jamaa? Hakika Mwenyezi Mungu aliumba mbingu na akazinyanyua juu na humo akampa makazi amtakaye miongoni mwa viumbe vyake. Kisha akaumba viumbe, na akawachagua wanadamu kutoka katika viumbe hivyo, na akawachagua Waarabu kutoka kwa wanadamu, na akamchagua Mudhir kutoka kwa Waarabu, na akamchagua Kuraishi kutoka kwa Mudhir, na akawachagua Bani Hashim kutoka kwa Kuraishi, na akanichagua mimi kutoka kwa Bani Hashim. Hivyo mimi ni kutoka kwa Bani Hashim, kutoka kwa aliye bora zaidi kwenda kwa aliye bora zaidi. Hivyo atakayewapenda Waarabu basi ajue ni kwa kunipenda mimindio maana kawapenda, na atakayewachukia Waarabu basi ajue ni kwa kunichukia mimi ndio maana kawachukia."'

**Dhakhairul-Uqba Uk. 10:**[13]

Amesema: Kutoka kwa Wathilah bin al-As'qau amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): "Hakika Mwenyezi Mungu alimteua Ibrahim kipenzi kutoka katika kizazi cha Adam, na akamteua Ismail kutoka katika kizazi cha Ibrahim, na akamteua Nazar kutoka katika kizazi cha Ismail, kisha

[11] *Sahih Tirmidhiy*, kitabu cha fadhila, mlango wa ubora wa Mtume (s.a.w.w.), hadithi ya 3608.
[12] *Mustadrakus-Sahihayni*, kitabu cha kuwatambua Masahaba, mlango wa kutaja fadhila za Makuraishi.
[13] *Dhakhairul-Uqba*, mlango wa ubora wa Makuraishi, kutaja kuteuliwa kwao.

akamteua Mudhir kutoka katika kizazi cha Nazar, kisha akamteua Kinanah kutoka katika kizazi cha Mudhir, kisha akamteua Kuraish kutoka katika kizazi cha Kinanah, kisha akawateua Bani Hashim kutoka katika kizazi cha Kuraishi, kisha akawateua Bani Abdul-Muttalib kutoka katika kizazi cha Bani Hashim, kisha akaniteua mimi kutoka kwa Abdul-Muttalib."

Kisha akasema: Ameiandika kwa tamko hili Abu Qasim Hamza bin Yusuf as-Sahmiy. Na ameiandika Muslim na Tirmidhiy na Abu Hatim kwa muhtasari.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 108:**[14]

Tamko lake ni: "Mimi ni mbora kushinda watu wote kinasaba na si kwa kujifaharisha, na ni mtukufu kushinda watu wote kiheshima na si kwa kujifaharisha. Enyi watu! Anayekuja kwetu nasi huenda kwake, anayetukirimu nasi humkirimu, anayetuandikia barua nasi humwandikia barua, anayesindikiza wafu wetu nasi husindikiza wafu wake, na anayetutekelezea haki yetu nasi humtekelezea haki yake. Enyi watu! Watathminini watu kwa kadiri ya asili yao, na jichanganyeni na watu kwa kadiri ya dini zao, waheshimuni watu kwa kadiri ya murua wao, na amilianeni na watu kwa akili zenu."

Amesema: Ameiandika Daylamiy kutoka kwa Jabir, yaani kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.).

**As-As-Suyutiyiy katika ad-Durul-Manthur, Mwishoni mwa tafsiri ya Aya ya Utakaso katika Sura al-Ahzab:**

Amesema: Hakim, Tirmidhiy, Tabaraniyy, Ibn Mardawayhi, Abu Na'im, na al-Bayhaqii katika *ad-Dalail*, wote wameandika kutoka kwa Ibn Abbas (r.a.) kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Hakika Mwenyezi Mungu alivigawa viumbe mafungu mawili, akaniweka katika fungu bora kushinda jingine, na hiyo ndio kauli yake: **"Watu wa kuliani…. Na watu wa kushotoni."** Mimi ni miongoni mwa watu wa mkono wa kulia, na mimi ndiye bora kushinda watu wote wa mkono wa kulia. "Kisha akayaweka mafunguhayo mawili katika theluthi tatu, akaniweka katika theluthi bora kushinda nyingine, na hiyo ndio kauli yake:**"Basi watakuwepo wa kuliani; je, ni wapi wa kuliani? Na wa kushotoni; je, ni wapi wa kushotoni? Na wa mbele watakuwa mbele."** Mimi ni miongoni mwa watu wa mbele, na mimi ndiye bora kushinda watu wote wa mbele.

"Kisha theluthi hizo akazifanya makabila mbalimbali, na akaniweka katika kabila bora kushinda yote, na hiyo ni kauli yake: **"Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamungu zaidi katika nyinyi."** Na mimi ndiye mchamungu na mtukufu zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu kushinda wanadamu wote, na si kwa kujifaharisha.

"Kisha makabila hayo akayafanya koo na akaniweka katika ukoo bora kushinda koo zote, na hiyo ndio kauli yake: **"Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara."** Hivyo mimi na watu wa nyumbani kwangu ndio waliotakaswa dhidi ya madhambi.'"

[14] *Kanzul-Ummal*, kitabu cha fadhila, fadhila mbalimbali zinazoonesha kuzungumzia neema ni ukamilifu, hadithi ya 32044.

# MLANGO UNAOZUNGUMZIA KUWA MTUME (SAWW) ALIANDIKIWA UNABII TANGU ADAM ANGALI BAINA YA ROHO NA MWILI

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, uk. 282:**[15]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kuwa alisema: "Walisema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ni lini uliandikiwa unabii?' Akasema: 'Tangu Adamu angali baina ya roho na mwili.'"

**Mustadrakus-Sahihayni Juz. 2, uk. 600:**[16]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa al-Arbadh bin Sariyyah as-Salmiy kuwa alisema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Hakika mimi niliandikiwa na Mwenyezi Mungu mwanzo wa kitabu kuwa mwisho wa Manabii tangu Adam angali mchanga ndani ya udongo wake….'"

**Hilyatul-Awliyai Juz. 7, uk. 122:**[17]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Maysaratul-Fakhri amesema: "Nilimwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ni lini uliandikiwa kuwa Nabii? Watu wakaniambia nyamaza, Mtume (saww) akasema: 'Mwacheni, niliandikiwa kuwa Nabii tangu Adam angali baina ya roho na mwili.'"

**Tarikhu Baghdad Juz. 3, Uk. 70:**[18]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kuwa amesema: "Aliulizwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): Ni lini uliandikiwa unabii? Akasema: 'Baina ya kuumbwa Adam na kupuliziwa roho.'"

# MLANGO UNAOZUNGUMZIA KUZALIWA KWA MTUKUFU MTUME (SAWW)

**Tabaqat Ibn Saad, sehemu ya kwanza uk. 63:**[19]

Amepokea kwa njia mbalimbali kwamba Amina binti Wahbi alisema: "Niliposhika mimba yake sikupatwa na uzito wowote mpaka nilipojifungua, alipojitenga nami alitoka akiwa na nuru ambayo iliangaza Magharibi hadi Mashariki, kisha alisujudu ardhini kwa kutegemea mikono yake, kisha alichukua kufi la udongo akaushika na akanyanyua kichwa chake kuelekea mbinguni."Baadhi yao wanasema: "Alipiga magoti na akanyanyua kichwa chake kuelekea mbinguni, na akatoka akiwa na nuru ambayo iliangazia makasri ya Sham na masoko yake mpaka nikaziona shingo za ngamia kwa macho yangu."

---

15 *Sahih Tirmidhiy*, kitabu cha fadhila, katika ubora wa Mtume, hadithi ya 3609.
16 *Mustadrakus-Sahihayni*, kitabu cha historia, kutaja habari za bwana wa Mitume na mwisho wa Manabii (s.a.w.w.).
17 *Hilyatul-Awliyai*, katika wasifu wa Sufiyan at-Thawriy.
18 *Tarikh Baghdad*, wasifu wa Muhammad bin Ali al-Haffar ad-Dhariri, namba 1032.
19 *Tabaqat Ibu Saad:* Kutaja mazazi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.).

**Tabaqat Ibn Saad, sehemu ya kwanza Uk. 64:[20]**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas kutoka kwa baba yake Abbas bin Abdul-Muttalib kuwa alisema: "Mtume (saww) alizaliwa akiwa tayari keshafanyiwa sunna na ni mwenye furaha, hilo likamshangaza Abdul-Muttalib na akapata hadhi kwake na akasema: 'Hakika mtoto wangu huyu atakuwa na jambo kubwa.' Na kweli akawa na jambo kubwa."

**Al-Haythamiy katika Majmau yake Juz. 8 Uk. 220:[21]**

Amesema: Kutoka kwa Uthman bin Abul-Asw amesema: "Mama yangu alinieleza akasema: 'Nilimshuhudia Amina alipokuwa anajifungua Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), aliposhikwa na uchungu niliona nyota zikiteremka mpaka nikasema zitaniangukia, alipojifungua ilitoka pamoja naye nuru ambayo iliangaza nyumba ambayo tulikuwemo humo na nyumba nyingine, hakuna kitu nilichokuwa nakitazama isipokuwa kilikuwa nuru tupu."'- Amesema: Kaipokea Tabaraniy.

**Tarikh Baghdad Juz. 1, uk. 329:[22]**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa amesema: "Mtume waMwenyezi Mungu (saww) amesema:'Miongoni mwa heshima yangu ni kwamba nilizaliwa nikiwa nimefanyiwa sunna na hakuna yeyote aliyeuona utupu wangu."'

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA SIFA ZA UMBILE LA MTUKUFU MTUME (SAWW)

**Tabaqat Ibn Saad, sehemu ya pili uk. 120:[23]**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa mwanaume mmoja wa Kiansari, kuwa alimuuliza Ali (as) kuhusu sifa za Mtume wa Mwenyezi Mungu na umbile lake, akasema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa ni mweupe weupe wenye kuelekea kwenye wekundu, mwenye macho ya mviringo yenye weusi, mwenye nywele za kunyooka, mwenye ndevu za kujaa, mwenye mashavu membamba, mwenye nywele nyingi, shingo yake ni kama birika la fedha, mwenye msitari wa nywele unaoanzia mwanzo wa kifua mpaka kwenye kitofu, umenyooka kama tawi la mti lililonyooka, kifuani kwake na tumboni kwake hana nywele nyingine zaidi ya hizo, ni mwenye kitanga na nyayoimara, anapotembea ni kama mwenye kushuka kutoka kwenye mteremko, na anaposimama ni kama mwenye kuporomoka kutoka mlimani, anapogeuka hugeuka mwili mzima, jasho lake hung'aa usoni kwake kama lulu, harufu ya jasho lake ni nzuri kushinda miski. Si mfupi wala si mrefu, si mwenye kushindwa na jambo wala si muovu, sijapata kumuona mtu mfano wake si kabla yake wala baada yake."

**Kanzul-Ummal Juz. 4 Uk. 34[24]:**

Amesema: Imepokewa kutoka kwa Abu Huraira kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alifariki siku ya Jumatatu, mwezi kumi na mbili, Mfunguosita, ilipofika asubuhi ya Alhamisi mara tu-

[20] *Tabaqat Ibu Saad*: Kutaja mazazi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.).
[21] *Majmauz-Zawa'id Wamanbaul-Fawaid:* Kitabu cha alama za unabii, mlango wa mazazi yake, kunyonya kwake na kupasuliwa kifua chake.
[22] *Tarikh Baghdad*: Wasifu wa Muhammad bin al-Faraj, namba 237.
[23] *Tabaqat Ibu Saad:* Kutaja mazazi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.).
[24] *Kanzul-Ummal*: Kitabu kinachozungumzia maumbile, Mlango unaozungumzia pambo lake (saww), Hadithi ya 18560.

limuona mzee ambaye alikuja na kusema: ‘Mimi ni padri miongoni mwa mapadri wa Baytul-Maqdas.’ Akasema: ‘Ewe Ali nieleze sifa za Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kiasi kwamba iwe kama namuona kwa macho yangu.’ Ali (as) akasema:

“‘Naapa kwa haki ya baba yangu na mama yangu, hakuwa mrefu wa kupindukia wala hakuwa mfupi, alikuwa ni mtu wa wastani, mweupe weupe wenye kuelekea kwenye wekundu, mwenye nywele zenye misokoto miwili, nywele zake ni ndefu mpaka kwenye nyama za masikio yake, mwenye paji la uso lenye kunyooka na kuchomoza, mwenye mashavu ya kutoka, mwenye macho ya mviringo, mwenye kucha za kunyooka, mwenye pua nyembamba ya kunyooka, mwenye mwanya, mwenye ndevu za kujaa, shingo yake ni kama birika la fedha, yenye kung’ara kama dhahabu. Jasho lake hung’aa usoni kwake kama lulu, ni mwenye vitanga na nyayo imara, ni mwenye msitari wa nywele unaoanzia mwanzo wa kifua mpaka kwenye kitofu, umenyooka kama tawi la mti lililonyooka, hakuwa na nywele nyingine zaidi ya hizo, si kifuani kwake wala si tumboni kwake.

“Anatoa harufu ya miski na anaposimama huwazamisha watu, na anapotembea ni kama mwenye kushuka kutoka mlimani na anapogeuka hugeuka mwili mzima, na anapoteremka ni kama mwenye kuporomoka kutoka kwenye mteremko. Ni mwenye tabia takatifu kushinda watu wote na ni mwenye moyo wa ushujaa kushinda watu wote, na ni mwenye mkono wa ukarimu kushinda watu wote. Abadan hajawahi kupatikana mtu mfano wake kabla yake, na milele hatapatikana mtu mfano wake baada yake.’Padri akasema: ‘Ewe Ali hakika mimi nimezipata sifa hizi ndani ya Taurat, na nimepata yakini kuwa hapana mungu isipokuwa Allah, na hakika Muhammad ni Mtume wa Allah.’”

Amesema: Ameiandika Ibn Asakir.

**Nasema:** al-Muhibu Tabari ametaja ndani ya *ar-Riyadh an-Nadhrah* Juz. 2 uk. 195[25]hadithi kutoka kwa Ibn Umar, kuwa Mayahudi walikuja kwa Abu Bakr na kumwambia: Tuelezee wasifu wa rafiki yako. Akawaelekeza kwa Ali bin Abu Talib, naye akawatolea wasifu unaokaribiana na ule uliotajwa katika hadithi ya Abu Huraira. Na inshaallah tutataja hayo katika mlango wa Abu Bakr kurejea kwa Ali (as).

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA SIFA ZA MTUKUFU MTUME (SAWW) KATIKA TAURATI NA INJILI

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 2 Uk. 174:[26]**

Amepokea kutoka kwa Atau bin Yasar amesema: “Nilikutana na Abdullah bin Amru bin al-Aas, nikamwambia nielezee kuhusu sifa za Mtume wa Mwenyezi Mungu katika Taurat, akasema: ‘Wallahi hakika yeye kaelezewa ndani ya Taurat kama alivyoelezewa ndani ya Qur’ani: **“Ewe Nabii, hakika sisi tumekutuma uwe shahidi, mbashiri na mwonyaji.”** Na ngome ya wasiojua kusoma na kuandika, na wewe ni mja Wangu na Mtume Wangu, nimekuita Mwenye kutawakali, si mkali wala si mgumu na wala si mpiga makelele sokoni.’”

Yunus amesema: “Wala si mpiga makelele sokoni, halipi ubaya kwa ubaya, lakini anasamehe na kufumbia macho, na hatomtwaa mpaka anyooshe kupitia yeye mila iliyopinda, waseme: Hapana mungu isipokuwa Allah. Kwa mila hiyo atayafumbua macho yaliyofumba, atayazibua masikio yaliyoziba na atazifungua nyoyo zilizofunga.”Atau amesema: “Nilikutana na Kaabi, naye nikamuuliza, hawakutofautiana hata katika herufi moja, isipokuwa ni kwamba Kaabi alisema kwa lugha yake: ‘Macho yasiyoona, masikio yasiyosikia na nyoyo zilizo na kifuniko.”’

[25] *Ar-Riyadh an-Nadhrah:* Mlango wa fadhila za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib.
[26] *Musnad Ahmad bin Hanbal*; *Musnad Abdullah bin Amru bin Al-Aas*, hadithi ya 6585.

**Hilyatul-Awliyai Juz. 5, uk. 386:**[27]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa mtoto wa kaka yake na Kaabi, amesema: "Kaabi alisema: 'Hakika sisi tunazipata sifa za Nabii (saww) katika msitari wa kitabu cha Mwenyezi Mungu, tunamkuta katika msitari kaandikwa: Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu, na ummah wake ni watu wenye kuhimidi, wanamhimidi Mwenyezi Mungu kwa kila hali, na wanamtukuza kwa kila utukufu. Ni wenye kulichunga jua, wanaswali Swala tano ndani ya wakati wake hata kama ni juu ya uchafu, wanafunika miili yao na wanaosha viungo vyao, na wana mngurumo angani kama mngurumo wa nyuki. Na tunamkuta katika msitari mwingine: Muhammad mteule, si mkali wala si mgumu na wala si mwenye kupiga kelele sokoni. Halipi ubaya kwa ubaya lakini anasamehe na kufumbia macho, atazaliwa Makka na atahamia Twiba na atakuwa na ufalme Sham.'"

**Tabaqat Ibn Saad, sehemu ya pili Juz. 1, uk. 89:**[28]

Amepokea kwa njia yake kutoka Sahli mtumwa wa Utaybah kuwa yeye alikuwa mkiristo wa Maris, na kwamba yeye alikuwa yatima chini ya uangalizi wa mama yake na ami yake na alikuwa akisoma Injili, amesema: "Nilichukua kitabu cha ami yangu nikasoma mpaka nilipofika katika ukurasa ambao sikuyapenda maandishi yake na nikaugusa kwa mkono wangu, nikagundua kuwa karatasi zimeshikana kwa gundi, nikaziachanisha na ndipo nikakuta sifa za Muhammad, kuwa yeye si mfupi wala si mrefu, ni mweupe, mwenye nywele zenye misokoto miwili, na kati ya mabega yake ana muhuri, anapenda kukaa kwa kujikunja, hakubali sadaka, anapanda punda na ngamia, anakamua maziwa ya mbuzi, anavaa kanzu ya kushonwa, na atakayefanya hivyo huwa kajiepusha na kiburi, naye anafanya hivyo, naye ni kutoka katika dhuriya wa Ismail na jina lake ni Ahmad."

Sahlu amesema: "Nilipofika hapa kwa kumtaja Muhammad (saww), ami yangu alikuja na alipouona ukurasa huu alinipiga na kuniambia: Kwa nini umeufungua ukurasa huu na kuusoma? Nikamwambia: Humu mna sifa za Nabii Ahmad, akasema: Bado hajakuja."

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA KUWA UONGOFU WA MTUKUFU MTUME (SAWW) NDIO UONGOFU BORA

**Sahih Muslim, kitabu cha Ijumaa, mlango wa kukhafifisha Swala na hotuba:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ja'far bin Muhammad, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Jabir bin Abdullah amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa anapohutubia macho yake huwa mekundu, sauti yake huwa juu, na ghadhabu yake huongezeka mpaka anakuwa kama mwenye kulionya jeshi, na husema: 'Nimetumwa niwe mimi na muda kama viwili hivi – kidole shahada na kidole kati –' Kisha husema: 'Ama baad, hakika mazungumzo bora ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na uongofu bora ni uongofu wa Muhammad. Jambo baya zaidi ni lile la kuzushwa, na kila bidaa ni upotovu.' Kisha husema: 'Mimi ni mwenye mamlaka kwa kila muumini kuliko nafsi yake, atakayeacha mali ni kwa ajili ya familia yake,……'"

[27] *Hilyatul-Awliyai*: Wasifu wa Kaabul-Ahbar katika majlisi zake na mawaidha yake.
[28] *Tabaqat Ibu Saad*: Kutaja sifa za Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) katika Taurat na Injili.

**Sahih an-Nasaiy Juz. 1, uk. 234:** [29]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ja'far bin Muhammad, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Jabir bin Abdullah amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa katika hotuba yake baada ya kumhimidi Mwenyezi Mungu na kumsifu kama anavyostahiki, husema: 'Atakayeongozwa na Mwenyezi Mungu hana wa kumpoteza, na atakayempoteza hana wa kumwongoza, hakika mazungumzo ya kweli kabisa kushinda yote ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na uongofu bora ni uongofu wa Muhammad. Jambo baya zaidi ni lile la kuzushwa, na kila uzushi ni bidaa, na kila bidaa ni upotovu, na kila upotovu mahali pake ni motoni……."'

**Sahih an-Nasaiy Juz. 1, uk. 193:**[30]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ja'far bin Muhammad, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Jabir kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa akisema ndani ya Swala yake baada ya tashahudi: "Maneno mazuri kushinda yote ni maneno ya Mwenyezi Mungu, na uongofu bora kushinda wote ni uongofu wa Muhammad."

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA MAJINA YA MTUKUFU MTUME (SAWW)

***Sahih Bukhar*: Kitabu cha tafsiri, mlango wa kauli yake: "Baada yangu jina lake ni Ahmad" katika Sura Swaf:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Muhammad bin Jubair bin Muti'im, kutoka kwa baba yake, amesema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Hakika mimi nina majina mengi: Mimi ni Muhammad, mimi ni Ahmad, mimi ni mwenye kufuta, ambaye kupitia kwangu Mwenyezi Mungu ataufuta ukafiri, na mimi ni mkusanyaji ambaye watu watakusanywa chini ya nyayo zangu, na mimi ni Aqibu."'

**Nasema:** Kaipokea pia Muslim ndani ya *Sahih* yake katika kitabu cha fadhila, mlango wa majina yake (saww), amesema: "Mimi ni Aqibu, mwenye kufuatia ambaye hakuna Nabii baada yake."

**Musnad Ahmad bin Hanbal Juz. 4, uk. 404:**[31]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Musa al-Ash'ariy amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alitutajia majina yake, yapo tuliyoyahifadhi na yapo ambayo hatukuyahifadhi, alisema: 'Mimi ni Muhammad, mimi ni Ahmad, al-Muqfiy, al-Hashiru, Nabiyyut-Tawba, na Nabiyyul-Mulhimah.'"

**Musnad Ahmad bin Hanbal Juz. 5, uk. 405:**[32]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Hudhayfa, amesema: "Wakati nikiwa natembea katika barabara ya Madina, nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu akitembea, nikamsikia akisema: 'Mimi ni Muhammad, mimi ni Ahmad, Nabiyyur-Rahma, Nabiyyut-Tawba, al-Hashiru, al-Muqfiy, na Nabiyyul-Mulahimu."'

---

[29] *Sahih an-Nasaiy*: Kitabu cha Swala ya Iddi mbili, mlango wa namna ya kutoa hotuba, hadithi ya 1786.
[30] *Sahih an-Nasaiy*: Kitabu cha sifa ya Swala ya Iddi mbili, mlango wa namna nyingine ya dhikri baada ya tashahudi, hadithi ya 1234.
[31] *Musnad Ahmad bin Hanbal*: Hadithi ya Abu Musa al-Ash'ariy, hadithi ya 19124.
[32] *Musnad Ahmad bin Hanbal*: Hadithi ya Hudhayfa bin al-Yaman, hadithi ya 22935.

**Mustadrakus-Sahihayni Juz. 4, uk. 273:**[33]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Nafiu bin Jubair, kuwa aliingia kwa Abdul-Malik bin Mar'wan, akasema: "Je unaweza kuorodhesha majina ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ambayo Jubair bin Muti'imu alikuwa akiyahesabu?" Akasema: "Ndio ni sita: Muhammad, Ahmad, Khatam, Hashir, Aqibu, na Mahi. Ama Hashiri ni kwakuwa atafufuliwa siku ya Kiyama na kuwaonya ninyi kwamba mbele yangu kuna adhabu kali. Ama Aqibu ni kwakuwa yeye ndio mwisho wa Manabii. Na ama Mahi ni kwakuwa kupitia yeye Mwenyezi Mungu atafuta makosa ya wale watakaomfuata."

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 116:**[34]

Tamko lake ni: "Hakika kwa Mola Wangu nina majina kumi: Muhammad, Ahmad, Abul-Qasim, al-Fatihu, al-Khatimu, al-Mahi, al-Aqibu, al-Hashir, Yasin, na Twaha." - Amesema: Ameiandika Ibn Adiy, na Ibn Asakir kutoka kwa Abul-Fadhli.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA NAKSHI YA MUHURI WA MTUKUFU MTUME (SAWW)

***Sahih Bukhar*: Kitabu cha elimu, mlango wa yale yanayosemwa wakati wa kupokea:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik, amesema: "Mtume aliandika barua – au alitaka kuandika barua - akaambiwa: 'Hakika wao hawasomi barua isipokuwa inapokuwa imepigwa muhuri.' Ndipo akatengeneza muhuri utokanao na madini ya fedha, nakshi yake ilikuwa ni: 'Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Kana kwamba nauona weupe wake mkononi mwake. "

**Nasema:** Ameipokea pia an-Nasaiy ndani ya *Sahih*yake Juz. 2, uk. 289[35], na amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alitaka kuandika barua kwenda Urumi, wakamwambia: Hakika wao hawasomi barua isipokuwa iliyopigwa muhuri…." Hadithi.

**Sahih Tirmidhiy Juz. 1 Uk. 325[36]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik amesema: "Nakshi ya muhuri wa Mtume ilikuwa ni: Muhammad, katika msitari. Mtume, katika msitari mwingine, na wa Mwenyezi Mungu, katika msitari mwingine."

**Sahih an-Nasaiy Juz. 7, uk. 295:**[37]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Umar, amesema: "Hakika Mtume alikuwa akivaa pete ya dhahabu, kisha aliiacha na akavaa pete ya karatasi, na akiwekea nakshi isemayo: 'Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Kisha akasema: 'Haipasi kwa yeyote kuweka nakshi ya pete yangu hii katika nakshi ya pete yake.' Na akaweka jiwe lake ndani ya tumbo la kiganja chake."

---

[33] *Mustadrakus-Sahihayni*: Kitabu cha adabu, kutaja majina ya Mtume na maana zake.
[34] *Kanzul-Ummal:* Kitabu cha fadhila, katika majina ya Mtume, hadithi ya 32169.
[35] *Sahih an-Nasaiy*, Kitabu cha elimu, mlango wa barua ya wasomi kwenda miji mingine, hadithi ya 5860, Kitabu cha tafsiri, mlango wa Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu, hadithi ya 11512.
[36] *Sahih Tirmidhiy:* Kitabu cha mavazi, mlango unaohusu nakshi ya muhuri, hadithi ya 1747.
[37] *Sahih an-Nasaiy:* Kitabu cha mapambo, mlango wa sehemu ya pete katika mkono.

# MLANGO UNAOZUNGUMZIA UZURI WA MTUKUFU MTUME NA NURU YA USO WAKE

**Sahih Bukhari: Kitabu cha mwanzo wa uumbaji, mlango wa sifa ya Mtume (saww):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Is'haq, amesema: "Nilimsikia al-Barau akisema: 'Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa na uso mzuri kushinda watu wote, na umbile zuri kushinda watu wote, si mrefu sana wala si mfupi."'

**Sahih Bukhari:**

Amepokea katika mlango uliotangulia kutoka kwa al-Barau, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu hakuwa mrefu wala mfupi, si mwembamba si mnene, mwenye nywele zenye kugusa nyama ya masikio yake, nilimuona akiwa katika vazi jekundu, sijawahi kumuona mtu mzuri kushinda yeye."

**Sahih Bukhari:**

Amepokea katika mlango uliotangulia kutoka kwa Abu Is'haqa, amesema: "al-Barau aliulizwa: Je uso wa Mtume ulikuwa uking'ara kama upanga? Akasema: 'Hapana, ni kama mbalamwezi."'

**Sahih Bukhari:**

Amepokea katika mlango uliotangulia kutoka kwa Abdullah bin Ka'ab, amesema: "Nilimsikia Ka'ab bin Malik akisimulia, alisema: 'Nilipomsalimu Mtume wa Mwenyezi Mungu, niliona uso wake uking'ara kwa furaha, na ilikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu anapofurahi uso wake hutoa nuru kama vile mbalamwezi, na tulikuwa tunalijua hilo kutoka kwake.'"

**Sahih Muslim: Kitabu cha fadhila, mlango unaoeleza kuwa Mtume alikuwa mweupe mwenye uso wa kuvutia:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa al-Jaririy kutoka kwa Abu Tufayli, amesema: "Nilimwambia: Ulimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: 'Ndio, alikuwa mweupe mwenye uso wa kuvutia."'

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, uk. 133:**[38]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir bin Samrah, amesema: "Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika usiku wa mbalamwezi, nikawa namtazama Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na ninatizamambalamwezi huku akiwa kavaa vazi jekundu, kwangu mimi alikuwa ni mzuri kushinda mbalamwezi."'

**Musnad Ahmad bin Hanbal Juz. 2, uk. 350:**[39]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Hurayra, amesema: "Sikupata kukiona kitu kizuri kushinda Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), alikuwa kana kwamba jua latembea juu ya paji lake la uso.

[38] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha adabu, mlango unaoelezea ruhusa ya kuvaa vazi jekundu kwa wanaume, hadithi ya 2811.
[39] *Musnad Ahmad bin Hanbal*: Musnad Abu Huraira, hadithi ya 8397.

Na sikupata kumuona mtu mwenye mwendo wa haraka kumshinda Mtume wa Mwenyezi Mungu, kana kwamba ardhi inajikusanya kwa ajili yake. Hakika sisi tunakazana lakini yeye hata hajali."

**Sinan ad-Daramiy Juz. 1, uk. 30:**[40]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ubaydah bin Muhammad bin Ammar bin Yasir, amesema: "Nilimwambia Rabiu binti Maudhu bin Afrau: Tuelezee alivyokuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Akasema: 'Ewe mwanangu, lau ukimuona ni kama umeona jua lililochomoza."

**Sinan ad-Daramiy Juz. 1, uk. 30:**[41]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alikuwa na mwanya katika meno yake ya mbele, anapozungumza nuru huonekana ikitoka kwenye mwanya wake."

**Tarikh Baghdad Juz. 5, uk. 439:**[42]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir kutoka kwa Mtume (saww) kuwa alisema: "Jibril alinishukia na kuniambia: 'Ewe Muhammad, hakika Mwenyezi Mungu anakutolea salamu na anasema: 'Habibi, hakika Mimi nilimvisha Yusuf uzuri utokanao na nuru ya Kursiy, na nimeuvisha uso wako uzuri utokanao na nuru ya Arshi yangu, na sijaumba kiumbe kizuri kukushinda wewe ewe Muhammad.'"

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 297:**[43]

Amesema: Kutoka kwa Aisha, amesema: "Niliazima kutoka kwa Hafsa binti Rawaha sindano ambayo nilikuwa ninashonea nguo ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), sindano ikanidondoka na nikaitafuta bila kuipata, ghafla akaingia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na ikajiainisha sindano kwa miyale ya nuru ya uso wa Mtume, nikacheka, akasema: 'Ewe Humayrau, kwanini unacheka?' Nikasema: Ilikuwa kadha wakadha. Akanadi kwa sauti yake ya juu: 'Ewe Aisha, ole wake, kisha ole wake, mtu ambaye atanyimwa kutizama uso huu, hakuna muumini yeyote wala kafiri isipokuwa anatamani kuutizama uso wangu."' - Amesema: Ameiandika Ad-Daylamiy na Ibn Asakir.

**Al-Haythamiy katika Majmau yake Juz. 8, uk. 279:**[44]

Amesema: Kutoka kwa Abu Qarswafah amesema: "Tulipompa kiapo cha utii Mtume wa Mwenyezi Mungu, mimi, mama yangu na mama yangu mdogo, na tukarejea kutoka kwake, mama yangu mzazi na mama mdogo waliniambia: 'Ewe mwanetu, hatujawahi kumuona mtu mwenye uso mzuri kushinda huyu, wala mwenye nguo safi kushinda huyu, na wala mwenye maneno laini kushinda huyu, na tumeona nuru ikitoka kinywani mwake."'

**— Amesema: Kaipokea Tabaraniy.**

**Nasema:** al-Munawi ametaja ndani ya *Kunuzul-Haqaiqu*uk. 155,[45] hadithi isiyo na njia yake yote, kutoka kwa Mtume (saww) ambayo inafaa kutajwa mwishoni mwa mlango huu, tamko lake ni: "Kunitizama ni ibada." Yaani Mtume. - Amesema: Kaiandika Tabaraniy na al-Hakim.

---

[40] *Sunan ad-Daramiy*: Mlango unaohusu uzuri wa Mtume, hadithi ya 60.
[41] *Sunan ad-Daramiy*: Mlango unaohusu uzuri wa Mtume, hadithi ya 58.
[42] *Tarikh Baghdad*: Wasifu wa Muhammad bin Abdullah, Abu Bakr al-Ashnaniy, namba 2963.
[43] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha fadhila, mlango wa fadhila za Mtume, katika fadhila zake mbalimbali, hadithi ya 35492.
[44] *Majmauz-Zawa'id*: Kitabu cha alama za unabii, mlango wa sifa zake (saww).
[45] *Kunuzul-Haqaiq*: Herufi Nun, hadithi ya 8247.

# MLANGO UNAOZUNGUMZIA UZURI WA HARUFU YA MTUKUFU MTUME (SAWW), ULAINI WA NGOZI YAKE, TEMBEA YAKE YA KUYUMBA, UZURI WA JASHO LAKE, NA ARDHI KUFICHA UCHAFU UTOKAO KWAKE

**Sahih Bukhari: Kitabu cha mwanzo wa uumbaji, mlango wa sifa ya Mtume (saww):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Jahifah, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alitoka wakati wa joto kali kuelekea Bat'hau, akachukua wudhu kisha akasali Swala ya Adhuhuri rakaa mbili na Laasiri rakaa mbili huku mbele yake kukiwa na fimbo." -Aliendelea kusimulia mpaka akasema-: "Watu wakasimama wakawa wanachukua unyevunyevu toka kwenye mikono yake na wanazipaka nyuso zao, nami nikauchukua mkono wake nikauweka juu ya uso wangu, nikaukuta ni baridi kushinda hata barafu na una harufu nzuri kushinda harufu ya miski."

**Sahih Muslim: Kitabu cha fadhila, mlango wa uzuri wa harufu ya Mtume (saww):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas amesema: "Kamwe sijawahi kunusa ambari wala miski wala kitu chochote chenye harufu nzuri kushinda harufu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, na wala kamwe sijawahi kugusa kitu wala hariri iliyo laini kushinda mwili wa Mtume wa Mwenyezi Mungu."

**Sahih Muslim: Kitabu cha fadhila, mlango wa uzuri wa harufu ya Mtume (saww):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alikuwa na rangi ya kung'aa, jasho lake lilikuwa kama lulu, anapotembea huyumba, sijawahi kugusa hariri laini kushinda kitanga cha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), na wala sijawahi kunusa miski au ambari yenye harufu nzuri kushinda harufu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu."

**Sahih Tirmidhiy Juz. 1, uk. 363:[46]**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas, amesema: "Nilimtumikia Mtume miaka kumi, hakuwahi kamwe kunifokea, na wala hakuwahi kuniambia kwa nini umefanya hivi katika lolote nililofanya, wala kuniambia kwa nini umeacha katika lolote nililoacha. Na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa mzuri wa umbile kushinda watu wote, na sikuwahi kugusa hariri laini wala kitu kilicho laini kushinda kitanga cha Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na wala kamwe sijawahi kunusa miski wala uturi wenye harufu nzuri kushinda jasho la Mtume (saww).

**Musnad Ahmad bin Hanbal Juz. 3, uk. 136:[47]**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik, amesema: "Mtume alifika kwetu na akalala kwetu, na akatokwa na jasho, mama yangu alikuja na chupa na kukinga jasho lake, Mtume alipoamka alisema: 'Ewe Ummu Salim, ni kitu gani hichi ulichofanya?' Akasema: 'Hili ni jasho lako, tunaliweka katika manukato yetu, nalo lina harufu nzuri kushinda manukato."'

[46] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha wema, mlango wa yaliyokuja kuhusu umbile la Mtume, hadithi ya 2015.
[47] *Musnad Ahmad bin Hanbal:* Musnad Anas bin Malik, hadithi ya 11988.

**Musnad Ahmad bin Hanbal Juz. 3, uk. 136:**[48]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir bin Yazid bin al-As'wad as-Sawaiy, kutoka kwa baba yake, kuwa yeye aliswali pamoja na Mtume Swala ya Subhi.-Aliendelea kusimulia mpaka aliposema: "Kisha watu walisimama na kuanza kuuchukua mkono wake na kuzipaka nyuso zao, nami nikauchukua na kuupaka uso wangu, nikaukuta ni wa baridi kushinda barafu na una harufu nzuri kushinda miski."

**Sunan ad-Daramiy Juz. 1, uk. 31:**[49]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa mtu kutoka kabila la Harish, amesema: "Nilikuwa pamoja na baba yangu wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu alipompopoa mawe Maizi bin Malik, nilipochukua jiwe nilitetemeka, ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu akanikumbatia na nikapatwa na jasho lake toka katika kwapa lake, lilikuwa na harufu nzuri kama harufu ya miski."

**Sunan ad-Daramiy Juz. 1, uk. 31:**[50]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir kwamba Mtume (saww) hakuwahi kupita njia au alikuwa hapiti njia kisha akafuatiwa na mtu isipokuwa mtu huyo atajua kutokana na harufu nzuri ya jasho lake kuwa ni Mtume ndiye aliyepita kabla yake."

**Tarikh Baghdad Juz. 6, uk. 23:**[51]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kuwa alisema: "Mtu mmoja alisema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu hakika mimi nimemuoza binti yangu, napenda unisaidie.' Mtume akasema: 'Sina kitu, lakini nivumilie mpaka kesho wakati utakapokuja kwangu nikiwa nimefunga mlango, uje na chupa yenye mdomo mkubwa na kijiti cha mti.' Alikuja nayo na akawa anakinga jasho kutoka kwenye dhiraa zake mpaka chupa ikajaa, Mtume akamwambia: 'Ichukue na umwamuru mkeo atakapo kujipaka manukato basi achovye kijiti hiki ndani ya chupa na ajipake." Basi alikuwa anapojipaka manukato hayo Madina yote husikia harufu nzuri, hivyo wakaitwa 'wanukisha manukato."

**Tarikh Baghdad Juz. 8, uk. 62:**[52]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha, amesema: "Mtume alipokuwa akiingia chooni nilikuwa nikiingia baada yake, na sikuwa naona kitu, nikamwambia hilo, akasema: 'Ewe Aisha hivi hujui kuwa miili yetu imetokana na roho za watu wa peponi, hakuna kitu kinachotoka kwetu isipokuwa ardhi hukimeza."'

**Nasema:** Katika riwaya aliyoitaja al-Qanduziy katika kitabu chake *Yanabiul-Mawaddah* ni kuwa alisema: "Miili yetu imejengeka kutokana na roho za peponi."[53]

**Mustadrakus-Sahihayni Juz. 4, uk. 72:**[54]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu aliingia kujisaidia, nami nikaingia baada yake, sikuona chochote bali nilikuta harufu nzuri ya miski, nikamwambia:

[48] *Musnad Ahmad bin Hanbal*: Hadithi ya Yazid bin al-As'wad al-Amiriy, hadithi ya 17024.
[49] *Sunan ad-Daramiy:* Mlango wa uzuri wa Mtume, hadithi ya 63.
[50] *Sunan ad-Daramiy*: Mlango wa uzuri wa Mtume, hadithi ya 66.
[51] *Tarikh Baghdad:* Wasifu wa Ibrahim bin Ismail as-Sawtiy, namba 3055.
[52] *Tarikh Baghdad*: Wasifu wa Husain bin Alawani bin Qadamah, namba 4138.
[53] *Yanabiul-Mawaddah* Juz. 2 Uk. 263.
[54] *Mustadrakus-Sahihayni*: Kitabu cha kuwajua Masahaba, mlango wa kumtaja Laila mtumwa wa Aisha.

Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hakika sijaona kitu, akasema: 'Hakika ardhi imeamrishwa kumeza uchafu utokao kwetu sisi Manabii."

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA WATU KUTABARUKU KWA WUDHU WA MTUKUFU MTUME (SAWW), KWA MATE YAKE NA KWA NYWELE ZA KICHWA CHAKE

**Sahihi Bukhari: Kitabu cha mavazi, mlango wa kuba jekundu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Jahifah kutoka kwa baba yake, amesema: "Nilikuja kwa Mtume naye akiwa katika kuba jekundu, nikamuona Bilal akichukua maji yanayotoka kwenye wudhu wa Mtume na watu wakigombania maji ya wudhu huo, anayepata chochote toka katika wudhu huo anajipaka, na ambaye hajapata chochote anachukua kutoka kwenye unyevunyevu wa mkono wa rafiki yake."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 4, uk. 323:**[55]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa al-Masuri bin Mukhrimah na Mar'wan bin al-Hakam, wamesema: "Katika mwaka wa Hudaybiya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alitoka akikusudia kuizuru Nyumba Tukufu." -Waliendelea kusimulia mpaka waliposema-: "Kisha akawaambia watu: 'Teremkeni.' Wakasema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ni bonde lisilo na maji watakayoyatumia watu.' Mtume wa Mwenyezi Mungu akatoa mshale kutoka kwenye mfuko wake na akampa mmoja wa Masahaba wake, naye akateremka hadi kwenye kisima miongoni mwa visima, akauchomeka humo, maji yakatoka kwa wingi watu wakanywa hadi wakatosheka." -Aliendelea kusimulia hadi akasema-:

"Mushrikina wakampeleka mjumbe wao Ur'watu bin Mas'ud at-Thaqafiy, naye alitoka kwa Mtume hali akiwa tayari kaona yanayofanywa na Masahaba zake, Mtume hachukui wudhu isipokuwa hugombania maji yatokanayo na wudhu wake, na wala hatemi mate isipokuwa huyagombania, na wala haudondoki unywele wake isipokuwa huuchukua. Aliporejea kwa Makuraishi aliwaambia: 'Enyi kundi la Makuraishi, hakika mimi nilifika kwa Kisra wakati wa ufalme wake, nilifika kwa Kaisari na Najashi wakati wa ufalme wao, wallahi sijawahi kuona ufalme mfano wa ufalme wa Muhammad kwa Masahaba zake. Hakika nimewaona watu ambao kamwe hawawezi kumsalimisha kwa lolote lile."'

**Nasema:** Ameipokea kwa njia nyingine ndani ya Juz. 4, uk. 328:[56]Humo amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu hakutema kikohozi chochote isipokuwa kilitua ndani ya kiganja cha mmoja wao, naye alijipaka kikohozi hicho uso wake na ngozi yake. Na anapowaamuru jambo hutekeleza amri yake, na wanapotawadha hukaribia kuuwana kwa sababu ya kugombania maji yatokanayo na wudhu wake, wanapozungumza huzungumza kwa sauti ya chini mbele yake, na wala hawamkodolei macho kwa sababu ya kumuheshimu."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 3, uk.133:**[57]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas, amesema: "Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa ananyolewa na kinyozi, huku Masahaba zake wakiwa wamemzunguka na hawataki unywele udondoke isipokuwa ndani ya mkono wa mmoja wao."

[55] *Musnad Ahmad bin Hanbal*: Hadithi ya al-Masuri bin Mukhrimah, hadithi ya 18431.
[56] *Musnad Ahmad bin Hanbal*: Hadithi ya al-Masuri bin Mukhrimah, hadithi ya 18449.
[57] *Musnad Ahmad bin Hanbal*: Musnad Anas bin Malik, hadithi ya 11955.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 3, uk.146:[58]**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alitaka kunyoa kichwa chake kwa ajili ya kuumika, Abu Talha alichukua nywele kwa mkono wake na akaja nazo mpaka kwa Ummu Salim, na Ummu Salim alikuwa akiziweka ndani ya manukato yake."

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA KUWA MTUKUFU MTUME NDIYE ALIYEWEKA JIWE JEUSI SEHEMU YAKE KABLA YA KUKABIDHIWA UNABII

**Tabaqat Ibn Saad Juz. 1, sehemu ya kwanza, Uk. 93:[59]:**

Amepokea hadithi ndefu kuhusu Makuraishi kubomoa Kaaba na kuijenga tena kabla ya Mtume kukabidhiwa unabii, amesema: "Walipokubaliana kuibomoa, baadhi yao walisema: 'Katika gharama za kuijenga msiingize chumo lenu lolote isipokuwa lililo safi, ambalo humo hamjavunja udugu na wala hamjamdhulumu yeyote.' Walid bin al-Mughira ndiye aliyeanza kuibomoa, alichukua sururu, akasimama juu ya Kaaba na kuanza kubomoa mawe huku akisema: 'Ewe Mwenyezi Mungu, hakika tunakusudia kheri.' Akabomoa na Makuraishi wakabomoa pamoja naye. Kisha wakaanza kujenga, wakaainisha Nyumba na kuainisha ramani yake, hivyo eneo la kuanzia nguzo nyeusi mpaka nguzo ya jiwe, eneo ambalo ndio uso wa nyumba, likakabidhiwa kwa Abdu Manafi na Zuhrah. Bani Asad bin Abdul-Uzza na Bani Abdudari bin Qusway wakakabidhiwa eneo la kuanzia nguzo ya jiwe mpaka nguzo nyingine ya jiwe. Taymu na Makhzum wakakabidhiwa kuanzia nguzo ya jiwe mpaka nguzo ya al-Yamaniy. Sahmi, Jum'u, Adi, na Amir bin Luay wakakabidhiwa eneo la kuanzia nguzo ya al-Yamaniy mpaka nguzo nyeusi.

"Wakajenga, walipofikia eneo ambalo jiwe jeusi huwekwa, kila kabila lilisema: 'Sisi ndio wenye haki zaidi ya kuliweka.' Walitofautiana mpaka kukazuka khofu ya kuuwana, na ndipo wakakubaliana kuwa wakwanza kuingia kupitia mlango wa Bani Shayba ndiye atakayeliweka.Wote wakasema tumeridhia na tumekubali. Basi Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ndiye aliyekuwa wa kwanza kuingia kupitia mlango wa Bani Shayba, walipomuona walisema: 'Huyu ni mwaminifu tumeridhia atakachohukumu baina yetu.' Kisha wakamsimulia habari ilivyo, Mtume wa Mwenyezi Mungu akachukua joho lake akalitandika aridhini, kisha akachukua jiwe na kuliweka ndani ya joho, kisha akawaambia: 'Kila kundi miongoni mwa makundi ya Kikuraishi limtoe mtu mmoja aje hapa.' Katika kundi la Bani Abdi Manafi alijitokeza Utbah bin Rabiah, katika kundi la pili alijitokeza Abu Zam'ah, katika kundi la tatu alijitokeza Abu Hudhayfa bin al-Mughira, na katika kundi la nne alijitokeza Qaysu bin Adiy.

"Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Kila mmoja wenu ashike pembe moja kati ya pembe za nguo, kisha linyanyueni ninyi nyote." Wakalinyanyua juu kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaliweka katika sehemu yake, pale lilipo sasa. Mtu mmoja kutoka katika watu wa Najdi alikwenda na kutaka kumpa Mtume waMwenyezi Mungu (saww) jiwe jingine kwa ajili ya kuamirishia jiwe jeusi, Abbas bin Abdul-Muttalib akasema: 'Hapana,' na akamuondoa, kisha yeye Abbas bin Abdul-Muttalib akampa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) jiwe hilo ambalo aliamirishia jiwe jeusi, lakini mtu yule kutoka Najdi alikasirika kwa kuzuiliwa na Abbas, ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Hapasi kujenga Nyumba pamoja nasi isipokuwa mtu kutoka kwetu." Mtu yule wa kutoka Najdi akasema: "Nawashangaa watu wenye heshima, akili, umri mkubwa na mali, imekuwaje wamemuachia

[58] *Musnad Ahmad bin Hanbal*: Musnad Anas bin Malik, hadithi ya 18431.
[59] *Tabaqat Ibn Saad:* Kutaja kuhudhuria kwa Mtume katika kubomoa Kaaba na kuijenga.

kazi hii mtoto mdogo mno kwao, na asiye na mali zaidi yao, wamempa uraisi juu yao katika jambo la heshima kwao, na amewamiliki kana kwamba wao ni watumishi wake, wallahi naapa atawashinda wote na atagawa hadhi na heshima baina yao." Inasemekana mtu huyo kutoka Najdi alikuwa ni Ibilisi.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA DALILI ZA UNABII WA MTUKUFU NABII (SAWW)

**Sahih Muslim: Kitabu cha fadhila, mlango wa ubora wa nasaba ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir bin Samrah, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amesema: 'Hakika mimi nalijua jiwe ambalo lilikuwa likinitolea salamu huko Makka hata kabla sijakabidhiwa unabii. Hakika mpaka sasa nalijua."'

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 284:**[60]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ali bin Abu Talib (as) kuwa amesema: "Nilikuwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) huko Makka, tukatoka tukizunguka katika baadhi ya viunga vyake, basi hakuna jabali wala jiwe isipokuwa lilimpokea kwa kumtolea salamu: Asalam Alayka ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 4, uk. 75:**[61]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Mujahid, amesema: "Alitusimulia mzee mmoja aliyewahi kuishi zama za ujahiliya anaitwa Ibn Absu, tulikuwa katika vita vya Rawdasi, alisema: 'Nilikuwa naswaga ngo'mbe wa jamaa yangu, ghafla nikasikia sauti kutoka ndani ya tumbo lake ikisema: 'Ewe Aali Dharihu kuna mtu ananadi kauli fasaha akisema: Hakuna mungu isipokuwa Allah.' Tulipofika Makka tukamkuta Nabii (saww) akiwa amedhihiri huko Makka."'

**Tabaqat Ibn Saad Juz. 1, sehemu ya kwanza, Uk. 114:**[62]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Said al-Hadhramiy amesema: "Mtu mmoja kutoka Bani Aslam akiwa anachunga mbuzi wake katika mbuga ya Dhul-Halifa ghafla mbwa mwitu alishambulia kundi la mbuzi wake na kumchukua mbuzi mmoja, mtu yule alianza kumkimbiza mbwa mwitu yule na kumpiga kwa mawe mpaka akamnyang'anya mbuzi wake. Basi mbwa mwitu yule alikuja mpaka mbele ya mtu yule na kuanza kulalamika kwa kuchezesha mkia wake, na kusema: 'Hivi humuogopi Mwenyezi Mungu mpaka unaninyang'anya mbuzi ambaye Mwenyezi Mungu kaniruzuku.' Mwanaume yule akasema: 'Wallahi katu sijawahi kusikia niliyosikia leo hii.' Mbwa mwitu akasema: 'Unashangaa kitu gani?' Mwanaume yule mchungaji akasema: 'Nashangaa mbwa mwitu kunisemesha.' Mbwa mwitu akasema: 'Nimeacha maajabu zaidi ya hayo huko Haramaini, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa kwenye mitende anawasimulia watu mambo yaliyopita, anawasimulia mambo yatakayokuja, lakini nakushangaa wewe ungali hapa wachunga mbuzi wako.'

---

[60] *Sahih Tirmidhiy*, Kitabu cha fadhila, Mlango wa 6, Hadithi ya 3626.
[61] *Musnad Ahmad bin Hanbal:* Hadithi ya Ibn Absu, mzee aliyeishi zama za ujahiliyah. Namba 16254.
[62] *Tabaqat Ibn Saad*: Kutaja alama za unabii baada ya kuteremka wahyi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

"Mwanaume yule baada tu ya kusikia kauli ya mbwa mwitu alianza kuwaswaga mbuzi wake mpaka akafika nao Quba – Katika kijiji cha Maanswari - akaulizia kuhusu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na ghafla akamkuta katika nyumba ya Abu Ayub al-Ansariy, akamweleza habari za mbwa mwitu, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Umesema kweli, njoo jioni, ukiona watu wamekusanyika wasimulie habari hiyo.' Naye alifanya hivyo, baada ya kuswali na watu kukusanyika mtu yule kutoka Banni Aslam aliwaeleza na kuwasimulia kisa cha mbwa mwitu. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema mara tatu: 'Amesema kweli, amesema kweli, amesema kweli, maajabu hayo yamenifikia si muda mrefu. Naapa kwa yule ambaye nafsi ya Muhammad imo mikononi Mwake si muda mrefu mtu ataanza kuwa mbali na mke wake kutwa nzima au siku nzima kisha mjeledi wake au fimbo yake au kiatu chake kitamueleza yote aliyotenda mke wake baada yake."'

**Usudul-Ghabah Juz. 4, uk. 153:**[63]

Ametaja hadithi kutoka kwa Hisham bin al-Kalbiy amesema: "al-Awamu bin Jahil al-Musamiy kutoka Hamadani alikuwa ni mlinzi wa sanamu la Yaghuth, alisimulia baada ya kusilimu kwake kuwa:'Ilikuwa ni usiku nikiongea na jamaa zangu na ghafla jamaa zangu walikwenda katika nyumba zao kulala, nami nikalala katika hekalu la masanamu, nililala katika usiku ambao ulikuwa na upepo mkali, radi na ngurumo, kulipoanza kupambazuka nilisikia sauti ikitoka kwenye sanamu ikisema: 'Ewe mtoto wa Jahil masanamu yamepata hasara, hii hapa nuru imechomoza toka ardhi takatifu, hivyo liage sanamu la Yaghuthu.'Kabla ya hapo hatukuwahi kusikia masanamu yakitamka, wallahi kauli hiyo ikaweka hali ya kuyakana masanamu moyoni mwangu, lakini niliwaficha jamaa zangu yale niliyoyasikia. Nikasikia sauti ikisema: 'Je umesikia kauli ewe al-Awam au umekusudia kuyapuuza maneno. Sitara za giza zimeshaondolewa na watu wanakusanyika katika Uislamu.'

"Nikasema:'Ewe mwenye kuwaamsha waliolala mimi si mwenye kuyapuuza maneno, nakusihi nieleze Uislamu ni nini.' Na wallahi kabla ya hapo sikuwa najua Uislamu ni nini, akanijibu kwa kusema: 'Nenda kwa jina la Allah na taufiki Yake, bila kuchelewa wala taabu, hadi katika kundi bora kushinda makundi yote, kwa Mtume mkweli mwenye kusadikika.' Nikatupa sanamu na nikatoka nikimkusudia Mtukufu Mtume (saww), nikakutana na ujumbe kutoka Hamdani wakimkusudia Mtukufu Mtume (saww), nikawaelezea habari yangu wakafurahishwa na kauli yangu, wakaniambia waambie Waislamu, na Mtukufu Mtume (saww) akaniamuru kuvunja masanamu, na tukarejea Yamani huku Mwenyezi Mungu akiwa tayari kishazitahini nyoyo zetu kwa Uislamu.'"

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 285:**[64]

Amesema: Kutoka kwa Zumal bin Amru al-Adhriy amesema: "Bani Adhra walikuwa na sanamu lao lililokuwa linaitwa Hamam na mlinzi wake alikuwa ni mwanaume mmoja aliyekuwa anaitwa Tariqu. Alipodhihiri Mtukufu Mtume (saww) tulisikia sauti ikisema: 'Enyi kizazi cha Hindi bin Haram, haki imedhihiri na Hamam ameangamia. Uislamu umeondoa shirki.' Kwa sauti hiyo tukaingiwa na woga sisi na familia zetu. Tukakaa na baada ya siku kadhaa tukasikia sauti ikisema: 'Ewe Tariqu, ewe Tariqu, ameletwa Nabii mkweli kwa wahyi utamkao, imedhihiri haki katika ardhi ya Tuhama, watakaomnusuru watasalimika na watakao mtelekeza watajuta, hii ni kauli ya kuaga kutoka kwangu mpaka Siku ya Kiyama.' Hapo sanamu likaangukia uso. Zumal anasema:'Nikatafuta usafiri nikasafiri mpaka kwa Mtukufu Mtume (saww) nikiwa na kundi kati ya jamaa zangu, nikamsomea shairi.'"

[63] *Usudul-Ghabah*, Mlango wa Ain na Waw, al-Awam bin Jahil al-Musamiy.
[64] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha fadhila, mlango wa fadhila za Mtume, Miujiza na dalili za unabii, Hadithi ya 35405.

**Nasema:** Alitaja beti za shairi husika, miongoni mwa beti hizo ni: "Na nashahidia kwamba Allah hana chochote kilicho mshirika wake, namtii Yeye maadamu nyayo zangu zingali juu ya kiatu changu." Kisha alisema: "Nikasilimu na kumpa kiapo cha utii na nikampa habari na kumhadithia yale tuliyosikia." Ameiandika Ibn Asakir.

**Kanzul-Ummal Juz. 6 Uk. 308:**[65]

Amesema: Kutoka kwa Ibn Abbas bin Mirdasi as-Salmiy amesema kuwa alikuwa katika kazi ya kupandikiza dume katika mitende jike, ilikuwa ni katikati ya mchana, ghafla akachomoza mbuni mweupe, juu ya mgongo wake kuna mpandaji aliyevaa nguo nyeupe mfano wa maziwa, mpandaji yule akasema: 'Ewe Abbas bin Mirdasi hivi huoni kuwa mbingu imezuia ukali wake (joto lake), na vita vinavuta pumzi yake na farasi wametua mizigo yao? Na kwamba dini imeteremka na wema na uchamungu siku ya Jumatatu usiku wa Jumanne ikiwa pamoja na mtu wa ngamia al-Qas'wa?'

Anasema: Nikatoka huku nikitetemeka, nikitetemeshwa na yale niliyoyaona na kuyasikia, nilitoka mpaka katika sanamu langu lililokuwa likiitwa Dhamari na tulikuwa tukiliabudu, nilifagia uchafu uliokuwa umelizunguka, nikalipangusa kasha nikalibusu. Ghafla nikasikia msemaji akisema kutoka ndani ya tumbo lake: "Yaambie makabila yote ya Salim, Dhamari ameangamia na wamefaulu watu wa msikitini. Dhamari ameangamia naye alikuwa anaabudiwa mara moja kabla ya Swala iliyokuja pamoja na Nabii Muhammad. Hakika huyu tuliyemtaja ametumwa na uwongofu baada ya mwana wa Mariam, naye ni kutoka kwa Kuraishi na ni mwenye kuongoa."

Anasema: Nikatoka nikitetemeka mpaka kwa jamaa zangu, nikawasimulia kisa na nikawaambia habari ilivyokuwa, nikatoka nikiwa na watu mia tatu kati ya jamaa zangu wa Bani Haritha, tulikwenda mpaka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), naye alikuwa huko Madina, tukaingia msikitini. Mtukufu Mtume (saww) aliponiona alinifurahia na kusema: "Ewe Abbas, ilikuwaje hadi ukasilimu?" Nikamsimulia kisa na kwa kweli alifurahi sana na kuserma: "Umesema kweli." Nikasilimu mimi na jamaa zangu.

— Ameiandika al-Kharaitiy ndani ya kitabu *al-Hawatif*, na pia kaiandika Ibn Asakir.

**Kanzul-Ummal Juz. 7, uk. 64:**[66]

Amesema: Kutoka kwa Amru bin Marrah al-Jahniy, amesema: "Tulitoka tukiwa mahujaji katika zama za ujahiliyah, nikiwa na kundi kati ya jamaa zangu, nikiwa Makka niliona usingizini nuru iliyochomoza kutoka ndani ya Kaaba, nuru hiyo iliangaza mpaka Yathriba (Madina), nikasikia sauti ikitoka ndani ya nuru ile ikisema: 'Giza limetoweka, na nuru imechomoza, na Nabii wa mwisho ameletwa.' Kisha nuru ile iliangaza mara ya pili mpaka nikayaona makasri ya Hira na majumba meupe ya Madain, na nikasikia sauti ikitoka ndani ya nuru ikisema: 'Uislamu umedhihiri, masanamu yamevunjika, na vizazi vimeunganishwa.' Nikashtuka kutoka usingizini, nikapatwa na khofu na hivyo nikawaambia jamaa zangu: Wallahi katika mtaa huu wa Makuraishi kutatokea jambo kubwa. Nikawasimulia kile nilichokiona.

Tulipofika katika mji wetu ilitufikia habari kuwa mtu mmoja anayeitwa Ahmadi ametumwa kuwa Nabii, basi nilitoka mpaka kwake na nikamsimulia kile nilichoona, akasema: "Ewe Amru bin Marrah, mimi ni Nabii niliyetumwa kwa waja wote, nawalingania katika Uislamu, nawaamrisha kuheshimu damu na kuunga udugu, na kumwabudu Allah peke yake na kuyakataa masanamu, kuhiji Nyumba tukufu, na kufunga mwezi wa Ramadhani kati ya miezi kumi na mbili. Hivyo atakayeniitikia atapata pepo na yule atakayeniasi atapata moto. Amini ewe Amru Mwenyezi Mungu atakusalimisha na misukosuko ya Jahannamu."

[65] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha fadhila, mlango wa fadhila za Mtume, Dalili kuu na alama za unabii, Hadithi ya 35561.

[66] *Kanzul-Ummal:* Kitabu cha fadhila, mlango wa fadhila za Masahaba, kumhusu Amru bin Marah al-Jahniy, Hadithi ya 37292.

Nikasema: Nashahidia kwamba hakuna mungu isipokuwa Allah, na hakika wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Nimeamini yote uliyoleta miongoni mwa halali na haramu, hata kama wengi kati ya watu watachukia hilo. Kisha nikasoma baadhi ya beti za shairi, beti ambazo nilizisoma pale niliposikia kutumwa kwake. Na tulikuwa na sanamu letu ambalo msimamizi wake alikuwa ni baba yangu mzazi, nikasimama na kulivunja, kisha nilikwenda kumkumbatia Mtume huku nikisema: "Nashahidia kwamba Allah ni haki, na hahika mimi ni wa mwanzo kuiacha miungu ya mawe. Nakunja shati langu na kuhama kwa kuyaacha masanamu na kukimbilia kwako, ili niandamane na mtu ambaye ndio nafsi bora na atokanaye na mzazi bora, Mtume Mfalme wa watu aliye juu zaidi." Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Karibu ewe Amru. – Amesema: Ameiandika ar-Rawiyyaniy na Ibn Asakir.

**Kanzul-Ummal Juz. 6 Uk. 96:**[67]

Amesema: Kutoka kwa Abbas bin Abdul-Muttalib amesema: "Nilisema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), lililonifanya kuingia katika dini yako ni nguvu ya unabii wako, nilikuona usingizini ukiwa sawa na mwezi, unauashiria kwa kidole chako na unakwenda kule unakoashiria." Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Hakika mimi nilikuwa nauongelesha nao unaniongelesha na unanizuia nisilie, kwani nilikuwa nasikia wajibu ulio nao pindi unaposujudu chini ya Arshi."'

Amesema: Ameiandika al-Bayhaqiy, Abu Uthman, al-Khatibu na Ibn Asakiri.

**Al-Haythamiy ndani ya al-Majmau, Juz. 8, uk. 250:**

Amesema: Kutoka kwa Hasan bin Zubairi al-Asadiy, amesema: "Umar bin al-Khattab alisema siku moja kumwambia Ibn Abbasi: 'Nisimulie hadithi itakayonivutia.' Akasema: Alinisimulia Kharim bin Fatik al-Asadiy, alisema: Ngamia wangu alikimbia, nikatoka kumtafuta nikamkuta katika ardhi ngumu yenye mawe, nikamfunga naye akalalia dhiraa yake, nikasema: 'Najikinga kwa mkubwa wa bonde hili, najikinga kwa adhimu wa bonde hili.' Na ndivyo walivyokuwa wakifanya katika zama za ujahiliyah, ghafla nikasikia sauti ikinadi:

"'Ole wako, jikinge kwa Allah Mwenye utukufu aliyeteremsha haramu na halali. Mpwekeshe Allah wala usijali vitisho vyovyote vya majini, kwani Allah anatajwa juu ya majabali, katika ardhi tambarale na milimani, na hakika vitimbi vya majini vimeanguka chini isipokuwa uchamungu na matendo mema.'

"Alisema: Nikasema: 'Ewe mwenye kunadi, umebeba nini, je ni uongofu au upotovu?' Akasema: 'Huyu hapa Mtume wa Mwenyezi Mungu mwenye kheri nyingi, amekuja na Yasin na Haamim, na Sura nyingi baada ya zile zenye kufafanua, zenye kuharamisha na kuhalalisha. Anaamuru Saumu na Swala na anawakanya watu mambo duni, ambayo hivi sasa ni mambo maovu.'

"Alisema: Nikasema: 'Mwenyezi Mungu akurehemu, wewe ni nani?' Akasema: 'Mimi ni Malaika ambaye nimetumwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa watu wa Najdi.' Nikasema: 'Laiti ningepata mtu wa kuniangalizia ngamia wangu huyu basi ningemfuata ili nimwamini.' Akasema: 'Mimi nitakuangalizia mpaka nimfikishe nyumbani kwako salama Inshaallah.' Basi nikamfungua ngamia wangu na kisha nikaja Madina, nikawakuta watu ikiwa ni siku ya Ijumaa, nao walikuwa katika Swala, nikasema ngoja kwanza wamalize Swala yao ndio na mimi niingie. Basi ghafla nikiwa nampigisha magoti mnyama wangu wa safari ghafla alikuja Abu Dhari (r.a) na kuniambia: 'Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) anasema ingia.' Nikaingia, aliponiona alisema: 'Mzee aliyechukua dhamana ya kukufikishia nyumbani ngamia wako amefanya nini? Tayari amemfikisha akiwa salama.' Nikasema: 'Mwenyezi Mungu amrehemu.' Mtume

[67] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha fadhila, mlango wa fadhila za Masahaba, kumhusu Amru bin Marah al-Jahniy, Hadithi ya 37292.

wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Ndiyo, Mwenyezi Mungu amrehemu.' Nikasema: 'Nashahidia kwamba hapana mungu isipokuwa Allah.'"

al-Haythamiy amesema: Ameipokea Tabaraniyy.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA USHUHUDA WA MAPADRI NA MAKASISI NA WENGINEO JUU YA UNABII WA MTUME WA MWENYEZI MUNGU (SAWW), KABLA YA KUKABIDHIWA UNABII WAKE NA BAADA YA KUKABIDHIWA

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 2, uk. 601:**[68]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas kutoka kwa baba yake kuwa alisema: Alisema Abdul-Muttalib: "Tulifika Yemen katika safari ya kiangazi, tukafikia kwa kasisi mmoja wa Kiyahudi, ndipo mtu mmoja miongoni mwa wasomi wa Zaburi akaniambia: 'Ewe Abdul-Muttalib, je waniruhusu niutizame mwili wako katika sehemu zile zisizokuwa utupu?' Basi akafunua pua yangu na kutizama, kisha akafunua pua ya pili kadhalika, kisha akasema: 'Nashahidia hakika katika mkono wako mmoja kuna ufalme na katika mkono mwingine kuna unabii, na ninayaona hayo kwa wana wa Zuhra, inakuwaje?' Nikamwambia sijui. Akaniambia: 'Je una Shaa?' Nikamwambia nini maana ya Shaa? Akasema: 'Mke.' Nikamwambia hivi sasa sina. Akasema: 'Basi ukirudi ukaoe kwao.' Abdul-Muttalib alirejea Makka na kumuoa Halah binti Wahbi IbnAbdimanafi, na ndipo akamzalia Hamza na Swafiyyah. Na Abdullah bin Abdul-Muttalib alimuoa Amina binti Wahbi na wakamzaa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Abdullah alipomuoa Amina Makuraishi walisema: "Abdullah amemshinda baba yake."

**Tabaqat Ibn Saad, Juz. 1, Sehemu ya kwanza, Uk. 104[69]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Sufiyan bwana wa Ibn Abi Ahmad kuwa kusilimu kwa Thaalabah bin Saayah, Asid bin Saayah na Asadu bin Ubaydu mtoto wa ami yao, kulitokana na hadithi ya Ibn al-Hayban ambaye ni Abu Umayru. Ibn al-Hayban akiwa ni Yahudi miongoni mwa Mayahudi wa Sham alikuja miaka kadhaa kabla ya Uislamu, (Thaalabah bin Saayah, Asid bin Saayah na Asadu bin Ubaydu) wanasema: "Hatujapata kumuona mtu asiyeswali Swala tano aliye bora kushinda yeye. Na ilikuwa ikitokea mvua imegoma sisi hukimbilia kwake, huwa tunamwambia: 'Ewe Ibn al-Hayban toka na utuombee mvua.' Lakini yeye husema: Sintafanya mpaka kwanza mtoe sadaka kabla sijatoka. Huwa tunamuuliza tutoe nini? Naye husema: Pishi moja la tende au vibaba viwili vya shairi kwa kila nafsi.

Baada ya kufanya hivyo hutoka pamoja nasi wakati wa adhuhuri na kufanya maombi, wallahi hautapita muda mrefu isipokuwa mawingu huanza kutembea na hatimaye mvua kutunyeshea. Alishafanya hivyo mara nyingi na kila mara mvua ilinyesha, na wakati mmoja akiwa pamoja nasi katika maombi hayo ndipo mauti yalipomfika, akasema: "Enyi Mayahudi, hivi mnadhani ni kitu gani kilichonitoa kwenye ardhi ya pombe na utajiri mpaka kwenye ardhi ya ufakiri na njaa?" Watu wakasema: Wewe wajua zaidi ewe Abu Umayru. Akasema: "Hakika nimekuja hapa nikitaraji kumpokea Nabii ambaye mmezingirwa na zama zake, na huu ndio mji atakaohamia, na mimi nilikuwa nataraji kumdiriki ili nimfuate, hivyo mkimsikia msiache wengine wakawatangulia kumwamini, hakika yeye atamwaga damu na atawateka watoto na wanawake, lakini hilo lisiwazuie kumwamini." Kisha akawa amefariki.

[68] *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha historia, Mayahudi wazungumzia kuzaliwa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).
[69] *Tabaqat Ibn Saad*: Alama za unabii zaonekana kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hata kabla ya kukabidhiwa wahyi.

Ulipofika usiku ambao asubuhi yake ilifunguliwa ngome ya Bani Quraydha, Thaalabah na Asidu watoto wa Saayah na Asadu bin Ubaydu wakiwa ni vijana, waliwaambia wenzao: "Enyi Mayahudi, wallahi huyu ndiye yule mtu ambaye alitupa wasifu wake Abu Umayru Ibn al-Hayban, hivyo mwogopeni Mwenyezi Mungu na mfuateni." Wakasema: "Si huyu." Akawaambia: "Wallahi ni huyu, ndiye mwenyewe." Wao walikwenda na wakasilimu lakini jamaa zao walikataa kusilimu.

**Tabaqat Ibn Saad, Juz. 1, Sehemu ya kwanza, Uk. 106[70]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdurahman bin Zaydu bin al-Khattab, amesema kuwa Zaydu bin Amru bin Nafil amesema: "Niliunusa uyahudi na unasara na sikuupenda, siku moja nilikuwa Sham ndipo nikamfuata padri katika jumba la utawa, nikasimama mbele yake na kuanza kumweleza kujitenga kwangu mbali na jamaa zangu na jinsi ninavyochukia kuabudu masanamu, uyahudi na unasara, akaniambia: "Nakuona unaitaka dini ya Ibrahim ewe ndugu wa watu wa Makka, hakika wewe unatafuta dini ambayo ndio inayofaa kwa sasa, nayo ni dini ya baba yako Ibrahim, alikuwa ni mwenye kujinyenyekeza kwa Allah, hakuwa Yahudi wala Nasara, alikuwa akiswali na kusujudu kwa kuelekea Nyumba hii ambayo ipo katika nchi yako, hivyo haki ipo katika nchi yako, hakika atatumwa Nabii kutoka katika jamaa zako ndani ya nchi yako, yeye atakuja na dini ya Ibrahim ambayo ni unyenyekevu, na huyo ndio kiumbe bora kushinda vyote mbele ya Mwenyezi Mungu."

**Tabaqat Ibn Saad, Juz. 1, Sehemu ya kwanza[71]:**

Kabla ya hadithi iliyotangulia, tena bila kitenganishi amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aamir bin Rabiah kuwa amesema: "Nilimsikia Zaidu bin Amru bin Nafil akisema: 'Mimi namngojea Nabii kutoka katika kizazi cha Isma'il, kisha ni kutoka kizazi cha Abdul-Muttalib, natamani niweze kumdiriki, nimwamini na nimsadikishe na nishahidilie kuwa hakika yeye ni Nabii. Ikiwa utaishi muda mrefu na ukabahatika kumuona basi mfikishie salamu zangu, na nitakueleza ni zipi sifa zake ili ziwe bayana kwako." Nikasema haya nieleze, akasema:

"Yeye si mrefu wala si mfupi, si mwenye nywele nyingi wala chache na macho yake hayaachi kuwa na wekundu. Muhuri wa unabii wake upo baina ya mabega yake, jina lake ni Ahmad na katika nchi hii ndipo atakapozaliwa na ndipo atakapokabidhiwa unabii, kisha watu wake watamfukuza na watachukia kile atakachokuja nacho mpaka atalazimika kuhamia Yathrib (Madina), na huko jambo lake litashinda, hivyo usidanganyike kwa kujitenga naye, kwani mimi nimezunguka nchi zote nikitafuta dini ya Ibrahim, na kila ninayemuuliza miongoni mwa Mayahudi, Manasara na Majusi ananiambia dini hiyo umeiacha nyuma huko, na hunieleza sifa zake kama hizi nilizokueleza na anasema hakuna Nabii aliyebakia zaidi yake." Aamir bin Rabiah amesema: Niliposilimu nilimueleza Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kauli ya Zaid bin Amru na nikamfikishia salamu zake, naye akamjibu salamu na kumuombea rehema, na akasema: "Hakika nimemuona peponi akitembea kwa fahari."

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 301:[72]**

Amesema: Kutoka kwa Hasan bin Thabit, amesema: "Wallahi hakika mimi nilikuwa mtoto wa miaka saba mwenye akili, mwenye kuelewa kila ninachosikia, ndipo nilipomsikia Yahudi mmoja akipiga kelele juu ya minara ya Yathrib: 'Enyi Mayahudi, katika usiku huu imechomoza nyota ya Ahmadi ambayo ni dalili ya kuzaliwa kwake." - Amesema: Ameiandika Ibn Asakir.

[70] *Tabaqat Ibn Saad*: Alama za unabbi zaonekana kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hata kabla ya kukabidhiwa wahyi.
[71] *Tabaqat Ibn Saad*: Alama za unabbi zaonekana kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hata kabla ya kukabidhiwa wahyi.
[72] *Kanzul-Ummal*, Kitabu cha fadhila, Mlango wa fadhila za Mtukufu Mtume (saww), kuzaliwa kwake, Hadithi ya 35518.

**Tabaqat Ibn Saad, Juz. 1, Sehemu ya kwanza, Uk. 106[73]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha kuwa amesema: "Kuna Yahudi mmoja aliishi Makka akiuza biashara zake, ulipoingia usiku ambao humo alizaliwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema katika moja ya mabaraza ya Makuraishi: 'Je kuna mtoto yeyote kazaliwa kwenu katika usiku huu?' Wakasema hatujui, basi akasema: 'Wallahi nimekosea kuuliza pale nilipokuwa napachukia, sikieni ninyi Makuraishi na hifadhini yale nitakayowaambia: Katika usiku huu kazaliwa Nabii wa mwisho wa ummah huu Ahmad, kama si kwenu basi ni Palestina, baina ya mabega yake ana baka lenye rangi nyeusi na njano lenye nywele zenye kufuatana.'

"Watu wakanyanyuka kutoka walipoketi huku wakiwa wamestaajabishwa na mazungumzo yake, walipofika majumbani mwao waliwaeleza wake zao, baadhi yao wakaambiwa: 'Katika usiku huu Abdullah bin Abdul-Muttalib kapata mtoto na kumpa jina Muhammad.' Baada ya siku hiyo walikutana na kwenda nyumbani kwa Yahudi, wakasema: 'Je ulitambua kuwa kuna mtoto kazaliwa miongoni mwetu?' Akasema: 'Alizaliwa baada ya habari yangu au kabla?' Wakasema ni kabla na jina lake ni Ahmadi. Akasema: 'Nipelekeni alipo.' Wakatoka pamoja naye mpaka wakaingia kwa mama yake, naye akatoka naye kwao, Yahudi akaona baka mgongoni kwake akazimia kisha akazinduka, wakasema: 'Una nini?' Akasema: 'Unabii umeondoka kutoka kizazi cha Israil na Kitabu kimeondoka toka mikononi mwao, imeandikwa kuwa atawauwa na atazishinda habari zao, wamefaulu Waarabu kwa unabii, je mmefurahi enyi Makuraishi? Wallahi atapata nguvu kupitia ninyi, nguvu ambayo habari zake zitaenea Mashariki hadi Magharibi.'"

**Tabaqat Ibn Saad, Juz. 1, Sehemu ya kwanza, Uk. 97[74]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Zaid bin Aslam, kutoka kwa baba yake, amesema: "Halima alipofika, alikuja yeye pamoja na mume wake na mtoto mdogo aliyekuwa akimnyonyesha, aliyekuwa akiitwa Abdullah wakiwa na punda na ngamia wao mzee mkondefu ambaye miundi yake imekonda kwa sababu ya njaa, katika chuchu za mama yake (Abdullah) hakukuwa na hata tone la maziwa, wakasema: 'Je tutapata kweli mtoto wa kunyonyesha.' Alikuwa pamoja na wanawake wengine wa kabila lake, walipofika walikaa siku kadhaa na wakapata watoto lakini Halima hakuweza kupata, na kila alipokuwa akimletewa Nabii (saww), yeye alisema: 'Ni yatima asiye na baba.' Mpaka mwisho akawa amemchukua na tayari marafiki zake walikuwa wametoka hapo siku moja kabla, Amina akasema: "Ewe Halima, tambua kuwa hakika wewe umemchukua mtoto mwenye jambo adhimu, Wallahi nimebeba mimba yake na wala sikuwa napata uzito ambao wanawake huupata kutokana na mimba, nilipouliza niliambiwa: 'Hakika wewe utamzaa mtoto na mwite mtoto huyo Ahmad, naye ni Bwana wa walimwengu wote.' Na nilipomzaa alitoka akiwa ameweka mikono yake juu ya ardhi huku kainua kichwa chake mbinguni."'

"Halima alitoka na kwenda kumweleza mumewe, naye alifurahishwa sana na hilo, na wakatoka wakiwa wamempanda punda wao na ngamia wao huku akiwa amejaa maziwa, na walikuwa wakimkamua asubuhi na jioni. Na mara akawa amewakuta marafiki zake na walipomuona walisema: 'Umemchukua nani?' Akawaeleza, wakasema: 'Wallahi hakika tunataraji atakuwa mbarikiwa.' Halima akasema: 'Tumeshaona baraka zake, nilikuwa siwezi kumnyonyesha mwanangu Abdullah wala tulikuwa hatulali kwa kilio, lakini sasa yeye na kaka yake wananyonya watakavyo na wanalala na hata kama ningekuwa nina mtoto wa tatu ningeweza kumtosheleza. Mama yake ameniamuru nifanye utafiti kuhusu yeye.'

"Halima alirejea mpaka katika mji wake, aliishi naye mpaka ulipowadia msimu wa soko la Ikadhi, akatoka na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mpaka wakafika kwa mpiga bao wa kabila la Hudhailu ili aweze kuwaonesha watu maajabu ya mtoto wao, alipomtizama alinadi kwa sauti: 'Enyi watu wa

[73] *Tabaqat Ibn Saad*: Alama za unabbi zaonekana kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hata kabla ya kukabidhiwa wahyi.

[74] *Tabaqat Ibn Saad*: Alama za unabbi zaonekana kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hata kabla ya kukabidhiwa wahyi.

kabila la Hudhailu, enyi Waarabu!' wakakusanyika kwake watu waliokuwa wamefika katika msimu huo, akasema: 'Muuweni mtoto huyu.' Halima akampokonya, watu wakawa wanauliza mtoto gani? Mpiga bao akawa anawajibu: 'Mtoto huyu' lakini wao hawaoni kitu, kwani mama yake alikuwa ameshaondoka naye. Akaulizwa ni nani? Akasema: 'Nimemuona mtoto, yeye na Mungu wake atawauwa watu wa dini yenu na ataivunja vunja miungu yenu na jambo lake litakuwa juu zaidi yenu.' Wakamtafuta Ikadhi yote bila kumpata, na Halima alikuwa amerudi naye nyumbani kwake, na tangu hapo hakumpeleka tena kwa mpiga bao wala kwa mtu yeyote.

**Tabaqat Ibn Saad, Juz. 3, Sehemu ya kwanza, Uk. 153[75]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibrahim bin Muhammad bin Talha, amesema:"Talha bin Muhammad amesema: Nilihudhuria katika soko la Basra, mara nikamsikia padri akisema ndani ya jumba lake la utawa: 'Waulizeni watu wa msimu huu je kati yao kuna mtu yeyote miongoni mwa wakazi wa Eneo Takatifu (Makka)?' Talha anasema: Nikasema ndio, mimi hapa. Padri akasema: 'Je bado Ahmad hajadhihiri?' Nikasema ni nani huyo Ahmad? Akasema: 'Ni mtoto wa Abdullah bin Abdul-Muttalib, huu ndio mwezi wake ambao atadhihiri naye ndio mwisho wa Manabii, kuzaliwa kwake ni huko Eneo Takatifu na kuhamia kwake ni huko katika mji wa mitende, joto na chumvi, jihadhari usiweze kumkimbilia.' Yakanikaa moyoni yale aliyosema hivyo nikatoka haraka mpaka nikafika Makka, nikauliza je kuna tukio lolote? Wakasema: Ndio, Muhammad bin Abdullah mwaminifu ametangaza unabii…"'

**Tabaqat Ibn Saad, Juz. 1, Sehemu ya kwanza, Uk. 99[76]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Daud bin al-Haswin, amesema: "Abu Talib alipokwenda Sham, kwa mara ya kwanza alikwenda pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa ni mtoto wa miaka kumi na miwili. Msafara ulipofika Basra ukitokea Sham, hapo alikuwepo padri aliyekuwa akiitwa Buhayra alikuwa ndani ya jumba lake la utawa. Ulamaa wa Kikristo walikuwa wanapatikana ndani ya jumba hilo la utawa huku wakirithishana sinagogi hilo kutokana na habari walizokuwa wakizisoma ndani ya Kitabu. Ni mara nyingi tu walikuwa wakipita kwa Buhayra lakini hakuwa anawasemesha mpaka katika mwaka huu, ndipo alipowasemesha walipofika kwake, kwani walifikia eneo lililo karibu na sinagogi lake, eneo ambalo walikuwa wakifikia kabla ya mara hii kila walipopita hapo.

"Padri aliwatengenezea chakula kisha akawaalika. Hakika kilichomfanya awaalike ni kwamba, walipochomoza aliwaona wakiwa na wingu ambalo lilikuwa likimfunika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) baina ya watu wote mpaka walipopumzika chini ya mti. Kisha akaliona wingu likiwa limeufunika mti huo, na alipoketi chini ya mti huo matawi ya mti huo yalijikusanya juu ya Mtume. Buhayra alipoona hayo alishuka kutoka katika jumba lake la utawa na akaamuru kiandaliwe chakula hicho. Kilipoletwa akatuma mjumbe akisema: 'Hakika nimewaaandalia chakula enyi Makuraishi, na mimi napenda muhudhurie ninyi nyote wala msimuache yeyote kati yenu, si mdogo wala mkubwa, muungwana wala mtumwa, hakika mtakuwa mmenikirimu kwa kuitikia wito huu.'

"Mtu mmoja akasema: 'Hakika wewe una jambo fulani ewe Buhyra usingeweza kututengenezea chakula hiki hivi hivi tu, una jambo gani leo?' Akasema: 'Hakika mimi nimetamani kuwakirimu na ninyi mna haki.' Ndipo wakakusanyika kwake na wakamuacha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) chini ya mti kati ya watu wote kutokana na udogo wake, kwani baina ya watu wote hakukuwa na mdogo kuliko yeye. Buhayra alipowaona jamaa hakuweza kuiona sifa anayoijua na iliyopo kwake. Akawa anawatazama jamaa bila kuona mawingu yakimfunika yeyote kati ya jamaa bali aliyaona yakiwa yamebaki juu ya

[75] *Tabaqat Ibn Saad*: Kutaja habari za Talha bin Abdullah.
[76] *Tabaqat Ibn Saad:* Alama za unabbi zaonekana kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hata kabla ya kukabidhiwa wahyi.

kichwa cha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Buhayra akasema: 'Enyi Makuraishi! Asibaki yeyote miongoni mwenu bila kuja kula chakula changu.' Wakasema: 'Hakuna aliyebaki isipokuwa kijana mdogo ambaye ni mdogo zaidi katika msafara wao.' Akasema: 'Mwacheni aje kula chakula changu, ni ubaya ulioje ninyi kuhudhuria katika chakula changu huku mkiwa mmemwacha mtu ilhali naye namuona ni miongoni mwenu.'

"Jamaa wakasema: 'Wallahi yeye ni mwenye nasaba adilifu kuliko sote, na yeye ni mtoto wa kaka yake na huyu – Yaani Abu Talib – na yeye anatokana na kizazi cha Abdul-Muttalib.' Harith bin Abdul-Muttalib bin Abdu Manaf akasema: 'Wallahi itakuwa ni mkosi kwetu kumuacha mtoto wa Abdul-Muttalib peke yake.' Kisha akasimama akamfuata na kumkumbatia, alikwenda naye na akaketi naye mbele ya chakula huku mawingu yakitembea juu ya kichwa chake. Buhyra akawa anamchunguza kwa makini huku akichunguza vitu kadhaa ndani ya mwili wake akitaraji kuwa anaweza kupata baadhi ya sifa zake.

"Walipoondoka toka kwenye chakula, padri alisimama na kumfuata na kumwambia: 'Ewe Kijana, nakuomba kwa haki ya Lata na Uzza unipe habari za yale nitakayokuuliza.' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Usiniulize kwa Lata na Uzza, Wallahi hakuna kitu ninachokichukia kushinda masanamu hayo mawili.' Padri akasema: 'Basi kwa haki ya Mwenyezi Mungu nieleze habari ya yale nitakayokuuliza.' Mtume akamwambia niulize ulilonalo. Basi akaanza kumuuliza kuhusu vitu kadhaa, kuanzia hali yake mpaka kulala kwake. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa akimweleza na vikiafikiana na taarifa alizonazo. Kisha alianza kuchunguza macho yake, kisha akafunua mgongo wake na kuiona alama ya unabii baina ya mabega yake katika sifa ile ile aliyokuwa na taarifa nayo, hivyo akabusu eneo la alama. Makuraishi wakasema: 'Hakika Muhammad ana hadhi mbele ya padri huyu.'

"Abu Talib akaingiwa na khofu juu ya mtoto wa kaka yake kutokana na yale aliyoyaona kwa padri, ndipo padri akamwambia Abu Talib:'Mtoto huyu si wako.'Abu Talib akasema ni mwanangu. Padri akasema: 'Si mtoto wako, kwani baba wa mtoto huyu hafai kuwa hai mpaka sasa.'Abu Talib akasema ni mtoto wa kaka yangu. Padri akamuuliza: 'Baba yake amefanya nini?' Akasema: 'Amefariki akiwa angali mimba tumboni mwa mama yake.' Padri akamuuliza: 'Amefanya nini mama yake?' Akasema:'Amefariki hivi karibuni.' Padri akasema: 'Umesema kweli, rejea na mtoto wa kaka yako katika nchi yake na chukua tahadhari kwa kumlinda dhidi ya Mayahudi, Wallahi laiti wakimuona na kutambua toka kwake yale niliyoyatambua watakula njama za kumuuwa, kwani hakika litakalokuwa kwa mtoto huyu wa kaka yako ni jambo kubwa ambalo limo ndani ya vitabu vyetu na tumelipokea kutoka kwa wazazi wetu. Na tambua kuwa hakika mimi nimeshatekeleza wajibu wangu wa kukunasihi.'

"Walipomaliza biashara zao aliondoka pamoja naye haraka, na tayari baadhi ya Mayahudi walikuwa wameshamuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na wametambua sifa zake na wakataka kumvamia na kumuuwa. Hivyo walikwenda kwa Nuhayra na wakamueleza nia yao lakini yeye aliwakataza na kuwaambia: 'Je mmepata sifa yake kwake?' Wakasema ndiyo, akasema: 'Basi hamna njia ya kumkana bali ni juu yenu kumsadikisha na kumuacha.'Abu Talib alirejea pamoja naye na hakuwahi tena kutoka naye katika safari yoyote kwa kukhofia wasije kumdhuru."

**Nasema:** Pia al-Khatib amepokea kwa muhtasari ndani ya *Tarikh Baghdad* Juz. 1, uk. 252, na amesema humo: "Akaushika (Yaani Buhayra – mkono wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kusema: 'Huyu ni Bwana wa walimwengu wote. Huyu ni Mtume wa Mola Mlezi wa walimwengu wote. Huyu katumwa na Mwenyezi Mungu kuwa rehema kwa walimwengu wote."

**Tabaqat Ibn Saad, Juz. 1, Sehemu ya kwanza, Uk. 82[77]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Nafsiyyah binti Muniyyah – Dada wa Ya'ala bin Muniyyah – amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alipofikisha umri wa miaka ishirini na tano, Abu Talib alimwambia: 'Mimi ni mtu nisiyekuwa na mali na bila shaka hali imekuwa ngumu juu yetu, na huu ni msafara wa kibiashara wa jamaa zako na umewadia wakati wa kutoka kwenda Sham, na Khadija binti Khuwaylid huwatuma wanaume kutoka katika jamaa zako ili waende kumuuzia biashara yake, hivyo kama utakwenda kwake na kumtaka akukabidhi atafanya haraka kukukabidhi. Khadija akafikiwa na habari za mazungumzo ya ami yake kwake, hivyo akamtumia mjumbe kuhusu hilo na kumwambia: 'Mimi nitakulipa mara mbili ya ninavyowalipa watu wengine kutoka katika jamaa zako.'"

Baada ya hadithi hii, katika hadithi aliyofuata baada ya hadithi moja, Ibn Saad anasema:"Alitoka pamoja na mtumishi wa Khadija aliyeitwa Maysara, na ami zake wakawa wanawausia watu wa msafara juu ya mtoto wao. Mpaka wao wawili walipofika Basra wakitokea Sham, wakafikia chini ya kivuli cha mti, ndipo padri Nestori akasema: 'Katu hawezi kufikia katika mti huu isipokuwa Nabii.' Kisha akamwambia Maysara: 'Je ana wekundu machoni mwake?' Akasema, ndio na hauachani naye. Padri akasema: 'Yeye ni Nabii na ndio Nabii wa mwisho.' Kisha aliuza bidhaa zake na ikatokea sintofahamu baina yake na mtu mmoja, ndipo mtu yule akamwambia: 'Apa kwa Lata na Uzza.' Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: 'Katu siwezi kuapa kwa majina hayo, hakika mimi naapa kwa jina lingine na si kwa hayo.' Mtu yule akasema fanya utakavyo, kisha akamwambia Maysara: 'Wallahi huyu ni Nabii ambaye mapadri wetu wamekuta sifa zake zimeandikwa ndani ya vitabu vyao.'

Kila hali ya hewa ilipokuwa ni joto kali, Maysara aliona Malaika wawili wakimkinga Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) dhidi ya jua kwa kumuwekea kivuli, nayote hayo Maysara aliyahifadhi, kana kwamba Mwenyezi Mungu aliweka upendo moyoni mwa Maysara wa kumpenda Mtume, hivyo alikuwa kama mtumwa wake. Waliuza bidhaa zao na wakapata faida mara mbili ya ile waliyokuwa wakipata. Waliporejea na kufika Dhaharani, Maysara alimwambia Mtume: "Ewe Muhammad, nenda kwa Khadija na mweleze lile ambalo Mwenyezi Mungu amemfanyia kupitia wewe, hakika yeye atalitambua hilo kwa ajili yako." Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikwenda mpaka akaingia Makka mchana adhuhuri huku Khadija akiwa katika kasri lake. Khadija akamuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa juu ya ngamia wake huku malaika wawili wakimkinga jua, akawaonesha wanawake wenzake nao wakastaajabu.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliingia kwake na kumueleza faida waliyopata kupitia yeye, Khadija akafurahi, na Maysara alipoingia alimweleza yale aliyoyaona, Maysara akasema: "Niliyaona haya tangu tulipotoka Sham." Na akamweleza yale aliyosema padriNestori, na yale aliyoyasema mtu mwingine walipopishana katika mauziano. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuja na biashara yake na Khadija akapata faida mara mbili ya ile aliyokuwa akipata, hivyo naye akamlipa mara mbili ya makubaliano yao.

**al-Isabah, Juz. 1, Sehemu ya tatu, Uk. 181[78]:**

Amesema: al-Haythamiy bin Adiy amesema katika habari zake kutoka kwa Said bin al-Aas, amesema: Alipouwawa Abul-Aswi bin Said bin al-Aas siku ya Badri nilikuwa nikilelewa na ami yangu Aban bin Said bin al-Aas. Alitoka na kwenda Sham kibiashara na alikaa huko mwaka mzima kisha akarejea. Na yeye alikuwa mara nyingi akimtusi Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), hivyo jambo la kwanza alil-

[77] *Tabaqat Ibn Saad*: Alama za unabbi zaonekana kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hata kabla ya kukabidhiwa wahyi.

[78] *al-Isabah*: Herufi Bau, Kulia kwa padri, namba 783.

ouliza kuhusu Mtume ilikuwa ni: “Muhammad kafanya nini?” Ami yangu Abdullah alimjibu: “Wallahi sasa ana nguvu kushinda alivyokuwa na amekuwa juu zaidi.” Aban akakaa kimya bila kumtusi kama alivyokuwa akimtusi, kisha alitengeneza chakula na kuwaalika matajiri wa Bani Umaiyyah na kuwaambia:

“Mimi nilikuwa katika kijiji kimoja, nikamuona humo Padri mmoja anayeitwa Bukau. Ana miaka arubaini hajateremka aridhini, siku hiyo aliteremka na ndipo watu wakawa wanamtazama. Nikamwambia mimi nina haja binafsi, akanichukua faragha, nikamwambia: ‘Hakika mimi ni Mkuraishi, na hakika kuna mtu mmoja kati yetu anadai kuwa eti Allah kamtuma kuwa Mtume.’ Akaniambia jina lake anaitwa nani? Nikamwambia anaitwa Muhammad. Akaniuliza ana muda gani tangu ameanza kudai utume? Nikamwambia ni tangu miaka ishirini iliyopita. Akasema je nikutajie sifa zake? Nikasema ndiyo, basi alianza kutoa sifa zake na hakukosea chochote katika sifa zake, kisha akaniambia: ‘Wallahi yeye ndio Nabii wa ummah huu, Wallahi lazima atashinda.’ Kisha akaingia hekaluni kwake na kuniambia: “Mfikishie salamu zangu.” Na hiyo ilikuwa zama za Hudaibiyah.

**Maj’mauz-Zawa’id ya al-Haythamiy, Juz. 8, Uk. 231[79]:**

Amesema: Imepokewa kutoka kwa Abu Sufiyan bin Harbu kuwa Umaiyyah bin Abus-Swalti alikuwa pamoja naye huko Ghaza, amesema: Tulipofunga mlango alisema: “Ewe Abu Sufiyan..” -Aliendelea kueleza mpaka akasema: “Akasema: Hakika mimi nilikuwa naona ndani ya vitabu vyangu kuwa kuna Nabii atatumwa kutoka katika Eneo letu Takatifu, hivyo nilikuwa nadhani bali nilikuwa sina shaka kuwa Nabii huyo ni mimi. Lakini nilipowadadisi wenye elimu niligundua kuwa atatokana na watoto wa Abdu Manaf, nilipochunguza kwa watoto wa Abdu Manaf sikupata hata mmoja anayefaa kwa jambo hili isipokuwa Ut’bah bin Rabiah. Lakini aliponitajia nasaba yake niligundua kuwa Nabii huyo si yeye kwani ameshavuka miaka arubaini bila kupewa wahyi.”

Abu Sufiyan anasema: “Dahari ikapiga pigo lake na hatimaye wahyi ukafunuliwa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, ndipo nikatoka na msafara wa Makuraishi kuelekea Yemen kibiashara, nikapita kwa Umaiyyah bin Abus-Swalti, nikamwambia kama mwenye kumdhihaki: ‘Ewe Umaiyyah amedhihiri Nabii ambaye ulikuwa ukimsubiri.’ Akasema: ‘Ndio yeye ni haki tupu mfuate.’ Nikamwambia: Ni kitu gani chakuzuia wewe kumfuata? Akasema: ‘Nawaonea aibu watu wa Thaqifu, mimi nilikuwa nawasimulia kuwa Nabii huyo ni mimi, kisha leo wanione namfuata kijana kutoka kizazi cha Abdu Manaf.’ Kisha Umaiyyah akasema: Ee Abu Sufiyan, ukithubutu kumpinga nitakuona umefungwa kama anavyofungwa ndama kisha utapelekwa kwake na yeye atakuhukumu atakavyo.”’

Al-Haythamiy amesema: Kaipokea Tabaraniy.

**Maj’mauz-Zawa’id ya al-Haythamiy, Juz. 8, Uk. 232[80]:**

Amesema: Imepokea kutoka kwa Jubairi bin Muti’imu amesema: Nilikuwa nachukizwa na maudhi ya Makuraishi waliyokuwa wanamfanyia Mtukufu Mtume (saww). Nilipodhani kuwa watamuuwa, nilitoka na kwenda hadi katika moja ya hekalu, na wanahekalu lile walitoka na kwenda kumwambia kiongozi wao, akawaambia: “Mtimizieni haki yake anayostahiki ambayo ni kukaa hapo siku tatu.” Walipomuona hajaondoka walikwenda tena kwa kiongozi wao na kumweleza, akasema: “Mwambieni: Tumeshakutimizia haki yako uliyostahiki, hivyo kama ulikuwa na uchovu tayari uchovu wako umekwisha, na kama ulikuwa ni mwenye kuendelea na safari basi umeshawadia muda wa kuendea unakokwenda, na kama ni mfanyabiashara basi umeshawadia muda wa kutoka na kwenda katika biashara yako.”

[79] *Maj’mauz-Zawa’id Waman’baul-Fawaid*: Taarifa walizokuwa nazo Mayahudi kuhusu unabii wake (saww).
[80] *Maj’mauz-Zawaid Waman’baul-Fawaid*: Taarifa walizokuwa nazo Mayahudi kuhusu unabii wake (saww).

Akasema: “Mimi si mwenye kuendelea na safari wala si mfanyabiashara wala si mwenye uchovu.” Basi wakatoka na kwenda kumwambia kiongozi wao, akasema: “Basi yeye ana jambo hebu muulizeni ni jambo gani alilonalo?” Basi wakamfuata na kumuuliza, akasema: “Wallahi sina lolote isipokuwa ni kwamba katika mji wa Ibrahim mtoto wa ami yangu anadai eti yeye ni Nabii, na jamaa zake wanamtendea maudhi hivyo nimetoka ili nisiweze kushuhudia maudhi hayo.” Wakatoka na kwenda kumweleza kiongozi wao kauli niliyosema, akasema: “Mleteni,” nilikwenda kwake na nikamsimulia kisa changu.

Akasema: “Je unaogopa kwamba wataweza kumuuwa?” Nikasema ndio, akasema: “Je unaweza kulitambua umbile lake kama utaona picha yake ya kuchorwa?” Nikasema ni hivi karibuni tu tangu nimuone kwa mara ya mwisho. Ndipo akanionyesha picha kadhaa za kuchora zilizokuwa zimefunikwa, akawa ananifunulia picha moja baada ya nyingine huku akiniuuliza je unamjua huyu? Na mimi namjibu simjui, mpaka alipofunua picha fulani iliyokuwa imefunikwa, nikasema: Sijaona kitu chenye kushabihiana na kitu kingine kushinda picha hii ilivyoshabihiana na yeye, urefu huu na mwili huu nikama wa kwake na pia upana uliyopo baina ya mabega yake.

Akasema: “Je unaogopa wasije kumuuwa?” Nikasema: Nadhani watakuwa tayari wameshamaliza kumuuwa. Akasema: “Wallahi hawawezi kumuuwa na hakika atamuuwa kila atakayethubutu kutaka kumuuwa, na hakika yeye ni Nabii na Mwenyezi Mungu atampa ushindi, tangu sasa umekuwa na haki ya wajibu kutoka kwetu, hivyo ishi hapa kadiri utakavyo na lingania utakalo.” – Al-Haythamiy amesema: Kaipokea Tabaraniyy.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA KUWA MTUKUFU MTUME (SAWW) ALITEULIWA KUWA MTUME KATIKA KARNE BORA KUSHINDA ZOTE, NA ALIPOTEULIWA MAJINI WALIFUKUZWA

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 2, Uk. 373[81]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kwamba Mtukufu Mtume (saww) alisema: “Niliteuliwa kuwa Mtume katika karne bora kushinda karne zote za wana wa Adam, ilipita karne moja baada ya nyingine mpaka nilipoteuliwa kuwa Mtume katika karne niliyokuwemo.”

**Tabaqat Ibn Saad, Juz. 1, Sehemu ya kwanza, Uk. 110[82]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: “Alipopewa utume Muhammad (saww) majini walifukuzwa na wakatupiwa vimondo, na kabla ya hapo walikuwa wakisikiliza, kila kabila kati ya makabila ya majini lilikuwa na makao wanayoketi kusikiliza. Watu wa kwanza walioshtushwa na hali hiyo ni watu wa Twaifu, hivyo wakaanza kuchinja wanyama wa sadaka kwa ajili ya miungu yao. Aliyekuwa na kondoo au ngamia alichinja kila siku, mpaka mali zao zikakaribia kutoweka. Ndipo wakakatazana na kuambizana: ‘Hivi hamuoni kuwa hali ya mbingu ingali kama ilivyokuwa hakuna chochote kilichobadilika?’ Ibilisi akasema: ‘Hili ni jambo lililotokea aridhini, hivyo nileteeni udongo kutoka kila pande ya ardhi.’ Basi alikuwa akiletewa udongo anaunusa na kuutupa, mpaka alipoletewa udongo wa Tuhamah, aliunusa na kusema: Ni hapa..

[81] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*, Musnad ya Abuhuraira, Hadithi ya 8640.
[82] *Tabaqat Ibn Saad*: Alama za unabbi zaonekana kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hata kabla ya kukabidhiwa wahyi.

# MLANGO UNAOZUNGUMZIA KUAMINI KWA AN-NAJASHI PINDI MTUKUFU MTUME (SAWW) ALIPOWAPELEKA BAADHI YA WAISLAMU KWAKE

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 1, Uk. 461[83]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Mas'ud kuwa amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alitupeleka kwa an-Najashi tukiwa ni wanaume themanini."Walikuwemo Abdullah bin Mas'ud, Ja'far, Abdullah bin Arfatwah, Uthman bin Madh'un na Abu Musa. Walipofika kwa an-Najashi Makuraishi walimtuma Amru bin al-Aas na Ammarah bin Walidi wakiwa na zawadi. Walipoingia kwa an-Najashi walisujudu mbele yake kisha wakafanya haraka kusimama kuliani na kushotoni kwake, kisha wakamwambia: 'Hakika kuna kundi la watoto wa ami yetu wamekimbilia katika ardhi yako, hawatutaki sisi na mila yetu.' Akawauliza wako wapi? Wakasema: 'Wapo katika ardhi yako, tuma mtu akawalete.'

"An-Najashi akamtuma mtu kwao, Ja'far akasema: 'Mimi nitakuwa ndiye msemaji wenu leo.' Basi wakamfuata na alipoingia alitoa salamu bila kusujudu, wakamwambia: 'Kwa nini humsujudii Mfalme?' Akasema: "Hakika sisi hatusujudu isipokuwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.' Akasema: 'Kwa nini?' Akajibu: 'Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ametuletea Mtume Wake, na yeye ametuamuru tusimsujudie yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu, na ametuamuru kuswali na kutoa Zaka.'

"Amru bin al-Aas akasema: 'Hakika wao wanakukhalifu kuhusu Isa bin Mariyam.' Akasema: 'Mnasema nini kuhusu Isa bin Mariyam na mama yake?' Wakasema: 'Tunasema kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu: Yeye ni neno la Mwenyezi Mungu na roho yake, aliliweka neno hilo kwa bikira mtawa ambaye hakuguswa na mtu.' An-Najashi alinyanyua fimbo yake kutoka aridhini na kusema: 'Enyi watu wa Habasha (Ethiopia), makasisi na mapadri! Wallahi hawajaongeza chochote katika yale tunayoyaamini, bali yanalingana na haya. Karibuni sana, ninyi na wale mliokuja nao kutoka kwake (kwa Mtume), nashahidia hakika yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, hakika yeye anapatikana katika Injili na yeye ndiye Mtume ambaye alibashiriwa na Isa bin Mariyam. Ishini mtakavyo, wallahi kama si ufalme nilionao ningekwenda kwake ili niwe mbebaji wa viatu vyake na msafishaji wa nyayo zake.'

"Kisha aliamuru ziletwe zile zawadi na akazirudisha kwao (kwa Amru bin al-Aas na jamaa yake), kisha Abdullah bin Mas'udi aliharakisha kurudi Makka kiasi kwamba aliweza kuidiriki vita ya Badri. Na alidai kuwa Mtukufu Mtume (saww) alimuombea maghufira an-Najashi pindi alipopata habari za kufariki kwake."

[83] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*, Musnad ya Abdullah bin Mas'ud, Hadithi ya 4386.

# MLANGO UNAOZUNGUMZIA KUWA MTUKUFU MTUME (SAWW) NDIYE BWANA WA WANA WA ADAM, HABABI WA MWENYEZI MUNGU KUSHINDA WOTE, KHALILI WA MWENYEZI MUNGU NA APENDWAYE ZAIDI NA MWENYEZI MUNGU NA NDIYE MBORA ZAIDI KULIKO WAO MBELE YA MWENYEZI MUNGU

**Sahih Muslim, Kitabu cha fadhila, Mlango wa ubora wa Nabii wetu juu ya viumbe wote:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Mimi ni bwana wa watoto wa Adam Siku ya Kiyama, na ndiye mtu wa kwanza atakayefufuliwa toka kaburini, wa kwanza atakayepewa nafasi ya uombezi na wa kwanza atakayekubaliwa uombezi."'

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 195[84]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Said, amesema: "Mimi ni bwana wa watoto wa Adam Siku ya Kiyama na si fakhari, na mikononi mwangu kutakuwa na bendera ya himidi na si fakhari. Na hakutakuwa na Nabii yeyote siku hiyo, kuanzia Adam na wengineo, isipokuwa atakuwa chini ya bendera yangu, na mimi ndiye mtu wa kwanza atakayefufuliwa toka kaburini, nasi fahari."'

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 283[85]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas amesema: "Baadhi ya watu miongoni mwa Masahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) walikaa wakimsubiri yeye. Punde akatoka mpaka akawa karibu nao, akawasikia wakikumbushana, akasikia mazungumzo yao, mmoja wao alisema: 'Ajabu iliyoje! Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu alijichagulia khalili kutoka kwa viumbe wake, akamchagua Ibrahim kuwa khalili.' Mwingine akasema: 'La ajabu zaidi ni jinsi alivyozungumza na Musa.' Mwingine akasema: 'Issa ni neno la Mwenyezi Mungu na roho yake.' Mwingine akasema: 'Adam aliteuliwa na Mwenyezi Mungu.' Ndipo Mtume akatoka na kuwatolea salamu na kuwaambia:

"'Nimesikia maneno yenu na kustaajabishwa kwenu, kwamba Ibrahim ni khalili wa Mwenyezi Mungu, na ndivyo ilivyo. Na Musa ni mtu aliyeongea na Mwenyezi Mungu, na ndivyo ilivyo. Na Isa ni roho wa Mwenyezi Mungu na neno lake, na ndivyo ilivyo. Na Adam ni mteule wa Mwenyezi Mungu, na ndivyo ilivyo. Fahamuni kuwa na mimi ni hababi wa Mwenyezi Mungu na si fakhari, na mimi ndiye mbebaji wa bendera ya himidi Siku ya Kiyama na si fakhari, na mimi ndiye mtu wa kwanza atakayepewa nafasi ya uombezi na wa kwanza atakayekubaliwa uombezi Siku ya Kiyama na si fakhari, na mimi ndiye mtu wa kwanza atakayetikisa kengele ya mlango wa pepo, Mwenyezi Mungu atanifungulia na nitaingia nikiwa pamoja na waumini mafakiri, na si fakhari. Na mimi ndiye mbora kushinda watu wote wa kwanza na wa mwisho na si fakhari."

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 104[86]:**

Kwa mujibu wa lafudhi yake Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Alimchagua Ibrahim kuwa khalili wake, na Musa kuwa mtu aliyeongea naye, na mimi amenichagua kuwa hababi wake, kisha alise-

[84] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha fadhila, Mlango wa fadhila za Mtukufu Mtume (saww), Hadithi ya 3615.
[85] *Sahih Tirmidhiy:* Kitabu cha fadhila, Mlango wa fadhila za Mtukufu Mtume (saww), Hadithi ya 3616.
[86] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha fadhila, fadhila mbalimbali na nasaba yake (saww), Hadithi ya 31893.

ma: 'Naapa kwa nguvu na utukufu Wangu, hakika nitamchagua hababi Wangu kabla ya khalili Wangu na kabla ya aliyeongea na Mimi.'"

Amesema: Ameiandika al-Bayhaqiy katika matawi ya imani kutoka kwa Abu Huraira.

**Faydhul-Qadir Juz. 4, Uk. 499[87]:**

Kwa mujibu wa lafudhi yake Jibril alisema: "Nimezunguka Magharibi na Mashariki na sijampata mtu aliye mbora kushinda Muhammad (saww). Na nimezunguka Magharibi na Mashariki na sijapata kizazi cha mwanaume kilicho bora kushinda kizazi cha Hashim."Amesema: Ameiandika al-Hakim katika*al-Kuna*, na ameiandika Ibn Asakir kutoka kwa Aisha.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 1, Uk.395[88]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Muammar kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: **"Na akamfanya Ibrahim kuwa khalili."** Amesema: Abdullah bin Umayr alinipa habari kutoka kwa Khalid bin Rabi'y, kutoka kwa IbnMas'ud, kuwa alisema: "Hakika Mwenyezi Mungu alimteua rafiki yenu kuwa khalili, yaani Muhammad (saww)."

**Taarikh Baghdad Juz. 12, Uk. 301[89]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah kuwa alisema: "Hakika Mwenyezi Mungu alimchagua Ibrahim kuwa khalili Wake, na hakika rafiki yenu ni khalili wa Mwenyezi Mungu, na hakika Muhammad (saww) ndiye bwana wa wana wa Adam Siku ya Kiyama." Kisha alisoma Aya: **"Na amka usiku kwa ibada; ni ziada ya sunnah khasa kwako wewe. Huenda Mola Wako Mlezi akakunyanyua cheo kinachosifika."**

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 104[90]:**

Kwa mujibu wa lafudhi yake ni: "Hakika Mwenyezi Mungu amenichagua kuwa khalili." – Amesema: Ameiandika al-Hakim ndani ya *al-Mustadrak* kutoka kwa Jundubi.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 114[91]:**

Kwa mujibu wa lafudhi yake ni: Adam alipotenda kosa alisema: "Ewe Mola! Nakuomba kwa haki ya Muhammad uweze kunisamehe." Mwenyezi Mungu akamwambia: "Umemjuaje Muhammad wakati bado sijamuumba?" Akasema: "Ewe Mola! Kwa sababu uliponiumba kwa mikono yako na kunipulizia roho yako ulinyanyua kichwa changu, nikaziona nguzo za Arshi yako zikiwa zimeandikwa: 'Hapana mungu isipokuwa Allah, na Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Nikatambua kuwa hakika wewe hujaunga jina lako isipokuwa katika jina la kiumbe umpendaye zaidi kushinda wote." Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema: "Umesema kweli ewe Adam, hakika yeye ndio kiumbe nimpendaye zaidi kushinda vyote, na kwakuwa umeniomba kwa haki yake basi nimeshakusamehe na laiti kama si Muhammad nisingekuumba." – Amesema: Ameiandika Abu Daud at-Twayalasiy, Said bin Mansuri, Abu Na'im, al-Hakim, al-Bayhaqiy na Ibn Asakir, kutoka kwa Ibn Umar.

[87] *Faydhul-Qadir*: Herufi Qaf, Hadithi ya 6074.

[88]

[89] *Taarikh Baghdad*: Wasifu wa Aqil bin as-Swamit Abul-Qasim, Namba 6746.

[90] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*, Musnad ya Abdullah bin Mas'ud, Hadithi ya 3741.

[91] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha fadhila, fadhila mbalimbali na nasaba yake (saww), Hadithi ya 31952.

**Faydhul-Qadir Juz. 4, Uk. 107[92]:**

Kwa mujibu wa lafudhi yake ni: Malaika alinitolea salamu kisha akaniambia: "Nimeendelea kumuomba Mola Wangu Mtukufu anipe ruhusa ya kukutana na wewe, mpaka muda huu ndio kanipa idhini, na hakika mimi nakubashiria kuwa hakuna mtu aliye mbora mbele ya Mwenyezi Mungu kushinda wewe." – Amesema: Ameiandika Ibn Asakir.

**Sunanud-Daramiy Juz. 1, Uk. 26[93]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Mimi ndiye nitakuwa mtu wa kwanza kufufuliwa, na mimi ndiye nitakuwa kiongozi wao watakapokusanywa, na mimi ndiye nitakuwa msemaji wao watakaponyamaza, na mimi ndiye nitakuwa muombezi wao atakapohesabiwa, na mimi ndiye nitakayewabashiria watakapokata tamaa. Hakika heshima na ufunguo siku hiyo vitakuwa mikononi mwangu, na mimi ndiye mbora mbele ya Mola Wangu kushinda wana wote wa Adam, nitazungukwa na watumishi elfu moja kana kwamba yai lililofichwa au lulu iliyohifadhiwa."

**Nasema:** Na hili limetangulia katika mlango wa pili katika yale aliyoyataja As-Suyutiy katika *ad-Darul-Manthur* kutoka katika hadithi ya Ibn Abbas, katika hadithi hii kuna maelezo: "Na mimi ndiye mchamungu zaidi kushinda wana wote wa Adam na mbora wao mbele ya Mwenyezi Mungu kushinda wote, na si fahari." Rejea huko.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA KUWA MTUKUFU MTUME ALIPEWA VITU VITANO AMBAVYO HAKUNA YEYOTE ALIYEPEWA KABLA YAKE, NA KWA VITU SITA AKAWASHINDA MANABII WOTE KWA UBORA

**Sahih Bukhari: Kitabu cha Tayamamu, Hadithi ya pili:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir bin Abdullah kwamba Mtukufu Mtume (saww) alisema: "Nimepewa vitu vitano ambavyo hajapewa yeyote kabla yangu: Nilisalimishwa na woga mwendo wa mwezi mzima, nimefanyiwa ardhi kuwa ni sehemu ya kusujudia na kujitoharishia, hivyo mtu yeyote kutoka katika ummah wangu akifikiwa na wakati wa Swala aswali, nimehalalishiwa ngawira na hakuna yeyote aliyehalalishiwa kabla yangu, nimepewa uombezi, na Nabii alikuwa akitumwa kwa jamaa zake tu, lakini mimi nimetumwa kwa watu wote."

**Sahih Muslim: Kitabu kinachozungumzia sehemu ya kusujudia, Hadithi ya saba:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kuwa Mtukufu Mtume (saww) alisema: "Nimefanywa bora kushinda Manabii wote kwa mambo sita: Nimepewa jumuisho la maneno, nilisalimishwa na woga, nimehalalishiwa ngawira, nimefanyiwa ardhi kuwa ni sehemu ya kusujudia na kujitoharishia, nimetumwa kwa viumbe wote na mimi ndio mwisho wa Manabii."

[92] *Faydhul-Qadir*: Herufi Sin, Hadithi ya 4698.
[93] *Sunanud-Daramiy*: Mlango wa fadhila alizopewa Mtukufu Mtume (saww), Hadithi ya 48.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 1, Uk. 98:**[94]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ali bin Abu Talib (as) kuwa alisema: Mtukufu Mtume (saww) alisema: "Nimepewa mambo ambayo hakuna Nabii yeyote aliyepewa zaidi yangu." Tukasema: Ewe Mtukufu Mtume (saww) ni mambo gani hayo? Akasema: "Nimesalimishwa na woga, nimepewa funguo za ardhi, nimepewa jina Ahmad, nimefanyiwa ardhi kuwa ni sehemu ya kusujudia na kujitoharishia, na umma wangu umefanywa umma bora kushinda zote."

**Mushkilatul-Athar Juz. 2, Uk. 263**[95]**:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Mujahidul-Makkiy, kutoka kwa Abu Huraira, amesema: "Tulikuwa tukimlinda Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika vita moja. Usiku mmoja nilikwenda sehemu ambayoMtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa amelala, lakini sikumkuta Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) sehemu yake ya kulala, nikadhania kuwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ameamka kuswali, nikatazama kulia na kushoto na ndipo nikamuona Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amesimama katika mti akiswali. Nilipokimbilia upande wake nikamkuta mtu mwingine naye katoka akimtafuta kama mimi, ndipo tukasimama mimi na mtu huyo nyuma ya Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na tukaswali Swala ya Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

"Aliswali kadiri Mwenyezi Mungu alivyotaka aswali, na alipofika katikati ya Swala yake alisujudu sijda ambayo tulidhani kuwa amefariki, tukamkimbilia na tukaketi mbele yake nikiwa mimi na rafiki yangu, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akatuuliza nasi tukamuuliza, kisha akasema: 'Je kuna chochote ambacho hamjakifuata katika Swala yangu hii ya usiku?' Tukasema: Ndiyo ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), kwani umesujudu katikati ya Swala yako sijda ndefu hadi tukadhani kuwa umefishwa.

"Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Hakika mimi nimepewa vitu vitano ambavyo hakuna yeyote aliyepewa kabla yangu: Hakika mimi nimetumwa kwa watu wote, wekundu na weusi, ilihali kila Nabii wa kabla yangu alikuwa akitumwa kwa watu wa nyumbani kwake au kwa watu wa kijiji chake. Na nimesalimishwa na woga wa kumuogopa adui yangu mwendo wa mwezi mzima ujao na wa mwezi mzima uliopita. Nimehalalishiwa ngawira na khumsi na hakuhalalishiwa Nabii yeyote kabla yangu, bali ilikuwa inachukuliwa na kuwekwa sehemu na kisha inateremkiwa na moto kutoka mbingu mchana kweupe na kuteketezwa na moto huo. Na nimefanyiwa ardhi kuwa ni sehemu ya kusujudia na kujitoharishia, naswali popote Swala inaponikuta. Na nimepewa nafasi ya maombi lakini nimeyaweka akiba ili yawe uombezi kwa ummah wangu Siku ya Kiyama.'"

Mujahidu amesema: Abu Huraira alisema: "Rafiki yangualikuwa mbora kunishinda mimi, na nimesahau mwisho wakauli yaMtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): "Nataraji uombezi wangu utampata yule asiyemshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote katika ummah wangu."

[94] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*, Musnad ya Ali bin Abu Talib, Hadithi ya 865

[95] *Mushkilatul-Athar*: Mlango unaozungumziwa matatizo yaliyopokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwa mujibu wa kauli yake.

# MLANGO UNAOZUNGUMZIA KUWA HAKIKA MTUKUFU MTUME (SAWW) NI BWANA WA MANABII NA IMAMU WAO, NA WAO WANAMWAMINI

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 2, Uk. 546[96]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira, amesema: "Mabwana wa Manabii ni watano, na Muhammad (saww) ndio bwana wa hao watano: Nuhu, Ibrahim, Musa, Isa na Muhammad (saww).

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 108[97]:**

Kwa mujibu wa lafudhi yake ni: "Mimi ni bwana wa Mitume watakapofufuliwa, ni kinara wao watakapokusanywa, ni mbashiri wao watakapokata tamaa, ni imamu wao watakaposujudu, na mimi ndiye atakayeketi karibu zaidi na Mwenyezi Mungu watakapokusanyika, nitaongea na atanisadikisha, nitauombea ummah wangu na atanikubalia, nitamuomba na atanipa."Amesema: Ameiandika Ibn an-Najari.

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 2, Uk. 614[98]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Mwenyezi Mungu alimfunulia Nabii Isa (as): 'Ewe Isa mwamini Muhammad, na mwamuru yeyote atakayemdiriki kati ya watu wa ummah wako amwamini, kwani kama si Muhammad nisingemuumba Adam, na kama si Muhammad nisingeumba pepo na moto. Na hakika niliumba Arshi juu ya maji ikawa inachezacheza, ikaandikwa: 'Hapana mungu isipokuwa Allah na Muhammad ni Mtume wa Allah' ikatulia."

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 2, Uk. 617[99]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik, amesema: "Tulikuwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika safari, tukashuka sehemu na ghafla tukamsikia mtu bondeni akisema: 'Ewe Mwenyezi Mungu nijaalie miongoni mwa ummah wa Muhammad uliorehemiwa, uliosamehewa na wenye thawabu.' Nilipochungulia bondeni nikamuona mtu ambaye urefu wake ni zaidi ya dhiraa mia tatu, akaniambia: 'Wewe ni nani?' Nikamwambia: 'Mimi ni Anas bin Malik mtumishi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).' Akaniambia: 'Yeye yuko wapi?' Nikamwambia: Anasikia maneno yako. Akasema: 'Nenda kamfikishie salamu kutoka kwangu na mwambie: Ndugu yako Ilyasa anakutolea salamu.'

"Nilikwenda kwa Mtukufu Mtume na nikamweleza habari husika, na yeye alikuja akakutana naye na wakakumbatiana na kumtolea salamu, kisha walikaa na wakazungumza, Ilyasa akamwambia: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hakika mimi nakula mara moja kwa mwaka, na leo ndio siku ya kula kwangu hivyo tule mimi na wewe.' Ikawateremkia meza ya chakula kutoka mbinguni ikiwa na mikate na chewa, wakala na wakanipa nami na tukaswali Laasiri, kisha alimuaga na kisha nikamuona akipita mawinguni mbinguni."

---

[96] *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha historia, Mlango unaosema mabwana wa Manabii ni watano na Muhammad ndio bwana wa hao watano.

[97] Kitabu cha fadhila, fadhila mbalimbali, Hadithi ya 32043.

[98] *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha historia, Mlango unaosema kuwa Mtukufu Mtume (saww) alikuwa mkarimu kushinda upepo.

[99] *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha historia, Mlango unaozungumzia Ilyasa alivyokutana na Mtukufu Mtume.

**Sunanud-Daramiy Juz. 1, Uk. 115[100]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir kwamba Umar bin al-Khattab alimpelekea Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) nakala ya Taurati, akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hii ni nakala ya Taurati." Lakini Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikaa kimya, na akaanza kuisoma huku uso wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ukibadilika. Abu Bakr akasema: "Wakulilie wanawake, unaona jinsi uso wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ulivyobadilika?" Umar akautazama uso wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kusema: "Najikinga kwa Mwenyezi Mungu kutokana na ghadhabu ya Mtume Wake, tumeridhia kuwa Allah ndio Mola Wetu, Uislamu ndio dini yetu na Muhammad ndio Nabii wetu." Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Naapa kwa yule ambaye nafsi ya Muhammad imo mikononi Mwake, Wallahi kama atawadhihirikia Musa na ninyi mkamfuata na kuniacha mtakuwa mmepotea mbali na njia ya sawa, kama angekuwa hai na akaudiriki unabii wangu angenifuata."

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA KUWA MTUKUFU MTUME (SAWW) NDIYE NABII MWENYE WAFUASI WENGI KUSHINDA MANABII WOTE

**Sahih Muslim: Kitabu cha imani, Mlango wa kauli ya Mtukufu Mtume (saww): Mimi ndiye mtu wa kwanza atakayewaombea watu peponi:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amesema: 'Mimi ndiye Nabii mwenye wafuasi wengi Siku ya Kiyama, na ndiye mtu wa kwanza atakayegonga mlango wa pepo.'"

**Sahih Muslim:**

Amepokea hadithi katika mlango uliotangulia, kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Mimi ndiye mtu wa kwanza atakayewaombea watu peponi, na mimi ndiye Nabii mwenye wafuasi wengi.'"

**Sahih Muslim:**

Amepokea hadithi katika mlango uliotangulia, kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Mimi ndiye mtu wa kwanza atakayewaombea watu peponi, hakuna Nabii aliyesadikishwa kama nilivyosadikishwa, kwani katika Manabii yupo ambaye hakusadikishwa isipokuwa na mtu mmoja.'"

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA KUWA MTUKUFU MTUME (SAWW) NDIYE MWISHO WA MANABII

**Sahih Bukhari: Kitabu kinachozungumzia mwanzo wa uumbaji, Mlango wa mwisho wa Manabii:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kuwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Hakika mfano wangu na mfano wa Manabii waliopita kabla yangu ni mfano wa mtu aliyejenga

[100] *Sunanud-Daramiy*:

nyumba, akaipamba na kuipendezesha isipokuwa sehemu ya tofali moja pembeni, watu wanapoizunguka nyumba hiyo huwavutia na husema: 'Kama ungeweka tofali hili ingependeza zaidi.' Mimi ndiye tofali hilo, mimi ndio mwisho wa Manabii."

**Sahih Muslim: Kitabu cha fadhila, Mlango unaozungumiza kuwa yeye (saww) ndiye mwisho wa Manabii:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir, kutoka kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amesema: "Mfano wangu na mfano wa Manabii ni mfano wa mtu aliyejenga nyumba akaikamilisha na kuitimiza isipokuwa sehemu ya tofali moja, watu wakawa wanaingia ndani ya nyumba hiyo na inawavutia huku wakisema: 'Kama si sehemu hii ya tofali ingependeza zaidi.' Mimi ndiye sehemu hiyo ya tofali nimekuja na nimehitimisha idadi ya Manabii."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 5, Uk. 396[101]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Hudhayfa kwamba Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Katika ummah wangu kuna waongo madajali ishirini na saba, wane kati yao ni wanawake, na hakika mimi ndiye Nabii wa mwisho hakuna Nabii baada yangu."

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA KUWA MTUKUFU MTUME (SAWW) HUONA HADI

**Sahih Bukhari: Kitabu cha Swala, Mlango unaosema adhama ya Imamu wa watu ni katika kutimiza Swala:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kuwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Je mnaona kibla changu hapa? Wallahi haufichikani kwangu unyenyekevu wenu wala rukuu zenu, hakika mimi nawaona ninyi kwa nyuma ya mgongo wangu."

**Sahih Bukhari: Mlango uliotangulia:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik, amesema: "Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alituswalisha Swala kisha akapanda mimbarini na akasema kuhusu – Swala na rukuu: 'Hakika mimi nawaona kwa nyuma ya mgongo wangu kama ninavyowaona kwa mbele.'"

**Sahih Bukhari: Mlango unaozungumzia kunyoosha safu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas, amesema: "Ilisimamishwa Swala na ndipo Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akatugeukia kwa uso wake na kusema: 'Pangeni safu zenu na zinyoosheni, hakika mimi nawaoneni kwa nyuma ya mgongo wangu."'

**Sahih Muslim: Kitabu cha Swala, Mlango unaoamrisha kuisali vizuriSwala:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kuwa amesema: "Siku moja Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alituswalisha kisha akageuka na kusema: 'Ewe fulani kwa nini huiswali vizuri Swala yako? Kwa nini mwenye kuswali asichunguze jinsi gani anavyoswali? Hakika anajiswalia mwenyewe, na hakika mimi Wallahi namuona aliye nyuma yangu kama ninavyomuona aliye mbele yangu."'

**Sahih Muslim: Mlango unaokataza kumtangulia imamu:**

[101] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*, Hadithi ya Hudhayfah bin al-Yaman, Hadithi ya 22849.

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas, amesema: "Siku moja Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alituswalisha, alipomaliza Swala alitugeukia kwa uso wake na kusema: 'Enyi watu! Hakika mimi ni Imamu wenu hivyo msinitangulie katika rukuu wala sijda wala kisimamo wala kuondoka, hakika mimi nawaoneni kwa mbele na kwa nyuma.' Kisha akasema: 'Naapa kwa ambaye nafsi ya Muhammad imo mikononi Mwake, lau mngekuwa mna uwezo wa kuona yale ninayoyaona basi mngecheka kidogo na kulia sana.' Wakasema ni kitu gani ulichokiona ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)? Akasema: 'Nimeona pepo na moto.'"

**Taarikh Baghdad Juz. 4, Uk.272[102]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha kuwa alisema: "Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa akiona katika giza kama anavyoona katika mwanga."

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA KUWA SHETANI HAJIFANANISHI NA SURA YA MTUKUFU MTUME (SAWW)

**Sahih Bukhari: Kitabu cha elimu, Mlango wa madhambi ayapatayo mwenye kumzushia uwongo Mtukufu Mtume (saww):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira, kutoka kwa Mtukufu Mtume (saww) kuwa alisema: "Jiiteni jina langu na wala msijiite kwa kuniya yangu. Na yeyote atakayeniona usingizini ajue kweli kaniona, kwani hakika shetani hajifananishi katika sura yangu. Na yeyote atakayenizushia uwongo makusudi basi ayaandae makalio yake kwa ajili ya moto."

**Sahih Bukhari: Mlango wa mtu atakayemuona Mtukufu Mtume ndotoni:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas, amesema: "Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Yeyote atakayeniona usingizini ajue kweli kaniona, kwani hakika shetani hajifananishi na mimi, na ndoto ya muumini ni moja ya sehemu arubaini na sita za unabii.'"

**Sahih Muslim: Kitabu cha ndoto, Mlango unaozungumzia kauli ya Mtukufu Mtume: Yeyote atakayeniona usingizini ajue kweli kaniona:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira, amesema: "Nilimsikia Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Yeyote atakayeniona usingizini ataniona kwa macho, au ni sawa na mtu aliyenionakwa macho yake, kwani hakika shetani hajifananishi na mimi.'"

[102] *Taarikh Baghdad*: Wasifu wa Ahmadi bin Abdul-Aala al-Baghdadiy, Namba 2019.

# MLANGO UNAOZUNGUMZIA KUWA MTUKUFU MTUME (SAWW) HULISHWA NA KUNYWESHWA NA MOLA WAKE

**Sahih Bukhari: Kitabu cha swaumu, Mlango wa kuunganisha Swaumu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kutoka kwa Mtukufu Mtume (saww) kuwa alisema: "Msiunganishe." Wakasema mbona wewe waunganisha? Akasema: "Mimi si kama yeyote kati yenu, hakika mimi nalishwa na kunyweshwa. Au hakika mimi nakesha na ninalishwa na kunyweshwa."

**Sahih Bukhari: Kitabu cha swaumu, Mlango wa kuunganisha Swaumu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Said kuwa alimsikia Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: "Msiunganishe swaumu, yeyote atakayekuunganisha basi aunganishe mpaka usiku wa manane." Wakasema: "Hakika wewe unaunganisha ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)." Akasema: "Hakika mimi si kama ninyi, hakika mimi nakesha na ninaye mlishaji anayenilisha na mnyweshaji anayeninywesha."

**Sahih Bukhari: Mlango wa kutoa funzo kwa yule mwenye kuunganisha Swaumu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira, amesema: "Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikataza kuunganisha swaumu, mtu mmoja katika Waislamu akamwambia: 'Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mbona wewe unaunganisha?' Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Na ni nani mfano wangu kati yenu? Hakika mimi nakesha, na Mola Wangu hunilisha nakuninywesha.' Alipoona wamekataa kuacha kuunganisha swaumu aliwaunganishia siku ya kwanza na siku yapili na ndipo mwezi ukaandama, akasema: 'Lau ungechelewa kuandama ningewaongezea.' Kama kutoa funzo kwao pindi walipokataa kuacha kuunganisha."

**Sahih Bukhari: Mlango wa kutoa funzo kwa yule mwenye kuunganisha swaumu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kutoka kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuwa alisema: "Acheni kuunganisha swaumu siku mbili." Pakasemwa: Hakika wewe unaunganisha. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Hakika mimi nakesha, na Mola Wangu hunilisha na kuninywesha, katika amali toshekeni na ile muiwezayo."

**Sahih Muslim: Kitabu cha swaumu, Mlango wa kukataza kuunganisha Swaumu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas, amesema: "Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliunganisha Swaumu mwanzoni mwa mfungo wa Ramadhani, na Waislamu wengine nao wakaunganisha, zilipomfikia habari hizo alisema: 'Lau mwezi ungeendelea basi tungeendelea kuunganisha kiasi kwamba wenye kung'ang'ania kuendelea kuunganisha wangeacha ung'ang'anizi wao, hakika ninyi si kama mimi –Au alisema: Hakika mimi si kama ninyi – hakika mimi nakesha, na Mola Wangu hunilisha na kuninywesha."'

# MLANGO UNAOZUNGUMZIA MUUJIZA WA MTUKUFU MTUME (SAWW) KATIKA MAJI YA WUDHU

**Sahih Bukhari: Kitabu cha vinywaji, Mlango wa kinywaji chenye baraka na maji yenye baraka:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir bin Abdullah, amesema: "Nilikuwa pamoja na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), ukawadia wakati Swala ya Laasiri huku tukiwa hatuna maji isipokuwa kidogo, basi yakawekwa ndani ya chombo kisha akapelekewa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), akaingiza mkono wake ndani ya maji hayo na kutanua vidole vyake, kisha akasema: 'Haya njooni wenye kuchukua udhu, imekufikieni baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu.'Hakika niliona maji yakibubujika kutoka baina ya vidole vyake, watu walichukua udhu na kunywa, nikawa sihisi uzito wa yale maji niliyoweka ndani ya tumbo langu, nikajua kuwa maji hayo ni baraka." Nikamwambia Jabir: Mlikuwa watu wangapi siku hiyo? Akasema: "Elfu moja mia nne."

**Sahih Bukhari: Kitabu cha kuanza uumbaji, Mlango wa alama za Unabii katika Uislamu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir bin Abdullah, amesema:"Watu walipatwa na kiu siku ya Hudaibiyah huku Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa kashika ndoo ndogo ya ngozi, alitawadha na ghafla watu wakamzunguka, akasema: 'Mna nini?' Wakasema: 'Hatuna maji ya kutawadha wala kunywa isipokuwa yaliyopo kwako.' BasiMtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaweka mkono wake ndani ya ndoo na hapo maji yakaanza kububujika baina ya vidole vyake kama maji ya mto, tukanywa na kutawadha."Nikamwambia: Mlikuwa wangapi? Akasema: Hata tungekuwa laki moja yangetutosha, tulikuwa elfu moja mia tano."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 3, Uk. 357:**[103]

Amepokea kwa njia yake kutoka Jabir bin Abdullah, amesema: "Tulisafiri pamoja na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Ukawadia wakati wa Swala, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Je jamaa wana maji?' Mtu mmoja akaja na maji machache aliyokusanya toka kwenye vyombo, akayamiminia ndani ya bilauri, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akatawadha. Kisha jamaa wakaleta maji mengine, akasema: 'Jipakeni, jipakeni.' Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawasikia, ndipo Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaweka mkono wake ndani ya maji yale, kisha akawaambia: 'Chukuweni udhu kwa maji safi.'"

Jabir bin Abdullah alisema: "Naapa kwa yule aliyenifanya kipofu –wakati huo alikuwa tayari ameshakuwa kipofu – niliyaona maji yakitoka baina ya vidole vya Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), hakuondoa mkono wake mpaka walipotawadha watu wote." - Al-As'wad amesema: "Tulikuwa mia mbili au zaidi."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 3, Uk. 169:**[104]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik, amesema: "Nilimwambia, katika maajabu haya tusimulie jambo ambalo hatatusimulia mtu mwingine, akasema: 'Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliswali Dhuhri kisha akaketi sehemu ambayo alikuwa akiketi anapofikiwa na Jibril (as). Bilali

[103] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*, Musnad Jabir bin Abdullah, Hadithi ya 14446.
[104] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*, Musnad Anas bin Malik, Hadithi ya 12316

alipokuja akamruhusu kutoa adhana kwa ajili ya Swala ya Laasiri, kisha akasema: 'Yeyote mwenye mke mbali na Madina akidhi haja yake (aende msalani kujisafi) kisha atawadhe.' Hivyo walibakia Muhajirina wasiokuwa na wake Madina, kisha Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliletewa bilauri ambayoilikuwa na maji kidogo, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliweka kitanga chake ndani ya bilauri lakini kitanga chake hakikuweza kutosha, ndipo akaweka vidole vyake hivi vine, kisha akasema: 'Sogeeni mje mtawadhe.' Wakatawadha kiasi kwamba hakuna aliyebaki bila kutawadha.'" Tukasema: Ewe Abu Hamza! Unadhani walikuwa wangapi? Akasema: Kati ya sabini mpaka themanini.

**Nasema:** Mlango huu una habari nyingi, tumetaja hizi tu kwa ufupi kwa kuhofia kurefusha mambo.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA MIUJIZA YA MTUKUFU MTUME (SAWW) KATIKA KUNYWESHA MAJI

**Sahih Bukhari: Kitabu cha kuanza uumbaji, Mlango wa alama za Unabii katika Uislamu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa al-Barau, amesema: "Siku ya Hudaibiyah tulikuwa watu elfu moja mia nne, basi tulitumia maji ya kisima cha Hudaibiyah kiasi kwamba hatukubakisha hata tone, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasimama ukingoni mwa kisima akaomba apewe maji, akasukutua na kuyatemea ndani ya kisima, hatukukaa muda mrefu tukaanza tena kunywa hadi tukatosheka na wakatosheka wanyama wetu."

**Sahih Bukhari: Kitabu cha kuanza uumbaji, Mlango wa alama za Unabii katika Uislamu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Amran bin Haswin kuwa wao walikuwa pamoja na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika safari moja. – Aliendelea kusimulia mpaka akasema: Tulipatwa na kiu kali sana, na wakati tukiwa bado tunaendelea na safari yetu tulimkuta mwanamke aliyenyoosha miguu yake baina ya viriba viwili, tukamwambia: "Maji yako wapi?" Akasema: "Hakika hakuna maji." Tukamwambia: "Kuna urefu kiasi gani baina ya sehemu waliyopo jamaa zako na palipo na maji?" Akasema: "Ni mchana na usiku." Tukamwambia: "Nenda kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)." Akasema: "Ni nani Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu?" Kabla hatujamaliza kumjibu swali lake Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akafika, na mwanamke yule akamsimulia kama alivyotusimulia.

Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliamuru viletwe viriba vyake, kisha akapitisha kiganja chake katika mdomo mdogo wa kiriba, basi tulikunywa maji watu arobaini tuliokuwa na kiu mpaka tukatosheka, na tukajaza maji kila kiriba na chombo tulichokuwa nacho, isipokuwa hatukuwanywesha ngamia, na kiriba kilikaribia kutoboka kutokana na ujazo, kisha Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Leteni chakula mlichonacho." Zikakusanywa tende na kupewa mwanamke yule, na yeye akarejea kwa jamaa zake, alipofika aliwaambia: "Nimekutana na mtu mchawi kushinda watu wote au yeye ni Nabii kama walivyodai jamaa zake." Mwenyezi Mungu akaliongoa kundi lile kupitia mwanamke yule, alisilimu yeye pamoja na jamaa zake.

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 78[105]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira, amesema: "Watu wa Swafah walikuwa ni wageni wa Waislamu, hawana ndugu wala mali.Wallahi naapa kwa yule ambaye hapana mungu isipokuwa Yeye,

[105] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha sifa za Siku ya Kiyama, Mlango wa 36, Hadithi ya 2477.

nilikuwa nalalia tumbo langu kwa sababu ya njaa, na ninafunga jiwe tumboni kwa sababu ya njaa. Na kuna siku moja niliketi katika njia yao ya kutokea msikitini na akapita Abu Bakr na nikamuuliza kuhusu Aya fulani kutoka ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Na sikumuuliza isipokuwa ni ili anipe chakula, lakini alipita na hakunipa chakula. Kisha alipita Umar na nikamuuliza kuhusu Aya fulani kutoka ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Na sikumuuliza isipokuwa ni ili anipe chakula, lakini alipita na hakunipa chakula. Kisha alipita Abul-Qaism (saww) na alitabasamu pindi aliponiona, kisha akasema: 'Ewe Abu Huraira!' Nikasema: 'Labaika ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).' Akasema: 'Nifuate.'

"Aliondoka na mimi nikamfuata. Aliingia nyumbani kwake, nikamuomba idhini ya kuingia akaniruhusu. Nikakuta bilauri la maziwa, akasema: 'Yametoka wapi maziwa haya?' Pakasemwa: 'Ameletewa kamazawadi na fulani.'Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Ewe Abu Huraira!' Nikasema: 'Labaika ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).' Akasema: 'Nenda kawaite watu wa Swafah.' - Nao walikuwa ni wageni wa Uislamu hawana ndugu wala mali, ilikuwa anapoletewa sadaka huwapelekea na alikuwa hali kitu katika sadaka hiyo hata kidogo. Na akiletewa zawadi huwaita nyumbani kwake na kushirikiana nao katika zawadi hiyo – hivyo jambo hilo la kwenda kuwaita halikunipendeza, nikasema: Itafaa nini bilauri hii mbele ya watu wote wa Swafah? Na mimi ndiye mjumbe wake kwao hivyo ataniamuru niwazungushie bilaurihilo na hivyo huenda nisiambulie kitu, wakati ambapo nilikuwa nataraji kuwa nitapata kiasi cha kunitosha katika maziwa hayo, na nilikuwa sijaanza kumtii Mwenyezi Mungu na kumtii Mtume wake.

"Nilikwenda nikawaita na walipoingia kwake kila mmoja aliketi sehemu yake. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Ewe Abu Huraira chukua bilauri na uwazungushie.'Nikachukua bilauri na kuanza kumpa mtu mmoja mmoja, naye anakunywa mpaka anatosheka kisha ananirudishia nami nampa mwingine, hivyo hivyo mpaka nikafika kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) huku watu wote wakiwa wametosheka. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akachukua bilauri akaiweka mikononi mwake kisha akanyanyua kichwa chake na kutabasamu, kisha akasema: 'Ewe Abu Huraira kunywa,' nikanywa. Kisha akasema: 'Kunywa,' nikaendelea kunywa huku akiniambia: Kunywa. Mpaka nikasema: Naapa kwa yule ambaye kakutuma kwa haki sina uwezo tena wa kuendelea. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akachukua bilauri akamuhimidi Mwenyezi Mungu akataja jina la Mwenyezi Mungu na kisha akanywa.'"

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 5, Uk. 298:[106]**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Qatadah, amesema: Tulikuwa pamoja na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika safari, akasema: "Msipopata maji mtateswa na kiu kesho." Watu wakatoka haraka kwenda kutafuta maji – Aliendelea kusimulia mpaka akasema: Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipanda mnyama wake na kuondoka na tuliondoka pamoja naye kwa urefu wa muda mchache, kisha aliteremka na kusema: "Je mna maji?" Nikasema: "Ndiyo, nina chombo cha kutawadhia ambacho kina maji kidogo." Akasema: "Kilete." Nikakileta, akasema: "Tawadheni toka humo, tawadheni toka humo." Watu wakatawadha na yakabakia maji kiasi cha funda moja. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Yahifadhi ewe Abu Qatadah, hakika yatakuwa na habari nzito."

Aliendelea kusimulia mpaka akasema: Joto lilipozidi Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliongea nao, wakasema: "Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) tunaangamia kwa kiu, makoo yamekauka." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Sina chochote cha kuwapeni." Kisha akasema: "Ewe Abu Qatadah! Leta chombo cha kutawadhia." Nikampelekea. Akasema: "Ng'oa bilauri yake." Nikang'oa na kumpa bilauri hiyo. Akaanza kumiminia maji ndani ya bilauri na kuwanywesha

[106] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*, Hadithi ya Abu Qatadah al-Ansariy, Namba 22040.

watu, hivyo watu wakajazana kwake. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: “Enyi watu! Jazeni vizuri vyombo vyenu, kwani hakika ninyi nyote mtajikuta mko mbali na chanzo cha maji.” Watu wakanywa maji kiasi kwamba hakubaki yeyote bila kunywa maji zaidi yangu mimi na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Akanimiminia na kuniambia: “Kunywa ewe Abu Qatadah.” Nikamwambia: “Kunywa wewe ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).” Akasema: “Hakika mwenye kutoa huduma ya maji kwa watu hunywa mwisho.” Nikanywa na yeye akanywa baada yangu na chombo cha kutawadhia kikabaki kama kilivyokuwa, na wakati huo kiliwahudumia watu mia tatu.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 5, Uk. 237:**[107]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Maadhi kuwa wao walitoka pamoja na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mwaka wa vita vya Tabuk. – Aliendelea kusimulia mpaka akasema: Kisha Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: “Hakika ninyi mtafika kesho Inshaallah katika chemchemu ya Tabuk, na hamtafika hapo isipokuwa wakati wa dhuha, hivyo atakayefika asiguse maji yake mpaka nitakapofika.” Tulikwenda, na watu wawili walitutangulia kufika hapo na wakakuta chemchemu ikiwa kama kishimo kidogo chenye maji kidogo. – Aliendelea kusimulia mpaka akasema: Kisha waliyachota maji yale kwa mikono yao kidogo kidogo kutoka katika chemchemu mpaka yakakusanyika katika kitu, kisha Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaosha uso wake na mikono yake ndani ya kitu hicho. Kisha akayarudisha maji yale machache ndani ya chemchemu. Basi chemchemu ikabubujika maji mengi na watu wote wakaweza kunywa maji. Kisha Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: “Si mbali ewe Maadhi – Kama utaishi muda mrefu - utayaona maji hapa hapa yakiwa yamejaa ndani ya mioyo.”

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 3, Uk. 343:**[108]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir bin Abdullah, amesema: Masahaba walimlalamikia Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuhusu kiu, basi akaomba aletewe bilauri na ilikuwa ina maji kidogo. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaweka mkono wake ndani ya bilauri hiyo, na kuwaambia: “Kunyweni.” Watu wakanywa. Nilikuwa naona chemchemu ikibubujika toka baina ya vidole vya Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

**Tabaqat Ibn Saad, Juz. 1, Sehemu ya kwanza, Uk. 98[109]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Amru bin Said kuwa Abu Talib alisema: “Nilikuwa huko Dhul-Majazi pamoja na mtoto wa ndugu yangu – yaani Mtukufu Mtume (saww)- na ghafla nikapatwa na kiu, nikamlalamikia kwa kumwambia: ‘Ewe mtoto wa ndugu yangu nimepatwa na kiu.’ Na si kwakuwa niliona ana kitu ndio nikamwambia hivyo, hapana hakuwa na kitu. Hivyo alikusanya mapaja yake na kuteremka kutoka katika kipando chake, akasema: ‘Ewe ami yangu umepatwa na kiu?’ Nikasema ndiyo. Basi akagandamiza kisigino chake aridhini, ghafla maji yakaanza kutoka, akasema: ‘Ami kunywa.’ Nikanywa.”

**Taarikh Baghdad Juz. 12, Uk. 287[110]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Nafiu. – Alikuwa ni sahaba wa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) – amesema: “Nilikuwa pamoja na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu

[107] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*, Hadithi ya Maadh bin Jabal, Namba 21565.
[108] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*, Musnad Jabir bin Abdullah, Hadithi ya 14287.
[109] *Tabaqat Ibn Saad*: Alama za unabbi zaonekana kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hata kabla ya kukabidhiwa wahyi.
[110] *Taarikh Baghdad*: Wasifu wa Usmat bin Sulayman al-Khazaz al-Kufiy, Namba 6727.

(saww) safarini. Tulikuwa karibuni watu mia nne, tukateremka sehemu ambayo haina maji, hali hiyo ikawa nzito juu ya Masahaba zake, wakasema: 'Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ndiye ajuaye zaidi.' Akaja mbuzi mwenye pembe mbili na kusimama mbele ya Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), akamkamua maziwa akanywa mpaka akatosheka, na akawanywesha Masahaba zake mpaka wakatosheka, kisha akasema: 'Ewe Nafiu mmiliki mbuzi huyu usiku huu japokuwa huwezi kummiliki.' Nikamchukua mbuzi yule nikamuwekea nguzo kisha nikamfunga kwa kamba. Nilipoamka usiku sikumuona mbuzi na nikaiona kamba ikiwa imetupwa. Nilikwenda kwaMtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) nikampa habari kabla hajaniuliza, akaniambia: 'Ewe Nafiu, amemchukua aliyemleta.'"

**Al-Athar cha as-Shaybaniy Uk. 53: Mlango wa fadhila za Saumu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ali bin al-Aqmar kwamba Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa anashinda na Swaumu na anakesha akifanya ibada na kuswali, kisha anakwenda kunywa maziwa kidogo ambayo huwa amewekewa, na hiyo ndio inakuwa futari yake na daku yake mpaka kesho wakati kama huo. Siku moja alikwenda kunywa kinywaji chake akamkuta mmoja wa Masahaba zake kazidiwa, hivyo sahaba huyo akayanywa maziwa yale. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akatafutiwa chakula au kinywaji kutoka katika nyumba za wakeze lakini hakikupatikana.Wakatafuta katika nyumba za Masahaba zake lakini hawakupata kitu. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Yeyote atakayenipa chakula Mwenyezi Mungu atampa chakula mara mbili." Lakini hawakupata chakula cha kuweza kumpa ale, ghafla wakamuona mbuzi, wakamkuta kajazia maziwa, wakamkamua maziwa sawa na kiasi cha maziwa ya Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA MIUJIZA YA MTUKUFU MTUME KATIKA KULISHA CHAKULA

**Sahih Bukhari: Kitabu kinachozungumzia mali ya kuokota, Mlango unaopendekeza kuchanga chakula pindi kinapopungua:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Iyas bin Salmah kutoka kwa baba yake, amesema: Tulitoka pamoja na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika vita moja, tukashikwa na njaa kiasi kwamba tulikusudia kuwachinja baadhi ya wanyama waliobeba mizigo yetu. Ndipo Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akatoa amri ya kukusanya vyakula vyetu. Tukamtandikia mrago wa ngozi, na vikakusanywa vyakula vya jamaa juu ya mrago huo. Nikachungulia ili niweze kukadiria ni vingi kiasi gani, nikakuta vyote kwa ujamla ni sawa na utumbo wa mbuzi, na kipindi hicho tulikuwa watu elfu moja mia nne. Lakini tulikula mpaka tukashiba wote, kisha tukajaza chakula ndani ya mifuko yetu ya kubebea chakula. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Je kuna maji ya kuchukulia udhu?" Mtu mmoja akaleta chombo chake kikiwa na maji kidogo, akayamimina ndani ya bilauri. Basi tulitawadha maji hayo sisi sote watu elfu moja mia nne tena kwa kujimwagia maji mengi. Kisha baada ya hapo walikuja watu nane, wakasema: "Je mna maji?"Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Udhu umeyamaliza."

**Sahih Bukhari: Kitabu cha vinywaji, Mlango unaoruhusu kufuatana na mtu mwingine katika nyumba ya mtu ambaye ana uhakika kuwa ataridhia:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir bin Abdullah kuwa alisema: Handaki lilipochimbwa niliona alama ya njaa kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), nikakimbilia kwa mke wangu na kumwambia: Je, kuna chochote? Hakika nimemuona Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa katika njaa kali. Basi mke wangu akanitolea mfuko uliokuwa na pishi moja la shairi, na tulikuwa na kuku, basi nikamchinja na nikasaga shairi, nilipomaliza kusaga nikakanda unga na nikamkatakata kuku na kumuweka ndani ya chungu. Kisha nikakusudia kwenda kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), ndipo mke wangu akasema: "Usinifedheheshe mbele ya Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) pamoja na wale walio pamoja naye." Nilipofika kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) niliongea naye kwa siri, nikasema: Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) tumemchinja mnyama wetu na nimetwanga pishi moja la shairi tuliyokuwa nayo, hivyo karibu wewe na watu kadhaa wakiwa pamoja na wewe.

Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akanadi na kusema: "Enyi wachimbaji wa handaki, hakika Jabir ametengeneza chakula hivyo anawakaribisheni." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaniambia: "Msiopoe chungu chenu na wala msioke unga wenu mpaka nitakapofika." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuja nao akiwa mbele, mpaka mke wangu akanifuata na kuniambia: "Tunafedheheka kwa sababu yako." Nikamwambia: Nimefanya kama ulivyoniambia, mke wangu akamletea Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) unga wetu, naye Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akatemea mate ndani ya unga huo na kuubariki. Kisha alikwenda kwenye chungu chetu akatemea mate ndani yake na kukibariki, kisha akasema: "Sasa mwache muokaji aoke mikate pamoja na wewe, na mpakue chungu chenu kikiwa jikoni msikiopoe." Walikuwa ni watu elfu moja.Wallahi naapa kwa Mwenyezi Mungu, walikula mpaka wakaacha na kuondoka, na hakika chungu chetu kikiwa bado kimejaa kama kilivyokuwa, na hakika unga wetu uliendelea kuokwa na kubaki vile vile ulivyo.

**Sahih Muslim: Kitabu cha ndoa, Mlango wa ndoa ya Zainabu binti Jahshi:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik amesema: Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alioa na akaingia na mkewe. Mama yangu Ummu Salim alitengeneza chakula aina ya *Hiysu* na kukiweka ndani ya chombo kidogo, akasema: "Nenda na chakula hiki kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na mwambie: Nimetumwa na mama yangu nilete chakula hiki kwako, naye anakutolea salamu, na anasema: Hiki ni kutoka kwetu ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ijapokuwa kichache." Nilimpelekea Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na nikamwambia: Hakika mama yangu anakutolea salamu, na anasema: Hakika hiki ni chakula chako kutoka kwetu ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ijapokuwa ni kichache. Akaniambia kiweke hapo, kisha akasema: "Nenda kaniitie fulani na fulani na fulani na utakayekutana naye." Aliwataja majina, hivyo nikawaita aliowataja na niliokutana nao.

Mpokezi anasema: Nilimuuliza Anas walikuwa wangapi? Akasema: Karibuni mia tatu, na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliniambia: "Ewe Anas! Lete chombo." Na watu waliingia mpaka wakajaa chumba na Swafah. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Waingie watu kumi kumi na kila mmoja ale sehemu ya mbele yake." Walikula mpaka wakashiba, likawa linatoka kundi hili na kuingia kundi jingine mpaka wakala wote, kisha Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaniambia: "Ewe Anas! Ondoa, nikaondoa, kwa kweli sijui ni wakati gani chakula hicho kilikuwa kingi zaidi, ni wakati nilipokiweka au ni wakati nilipokiondoa.

**Sahih Muslim: Kitabu cha vinywaji, Mlango unaozungumzia kumkirimu mgeni:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdurahman bin Abu Bakr kuwa alisema: Tulikuwa watu mia moja na thelathini pamoja na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Mtukufu Mtume (saww) akasema: "Je kati yenu kuna yeyote mwenye chakula?" Akajitokeza mtu mmoja akiwa na pishi moja la chakula au mfano wake, unga ukakandwa, kisha alikuja mushriku mmoja mrefu huku akimswaga kondoo, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamuuliza: "Ni biashara au ni zawadi?" Akasema: "Hapana ni biashara." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akanunua kondoo kutoka kwake, akapikwa na akaamuru kuwanyama ya tumbo ichomwe. Wallahi hakuna mtu kati ya watu wote mia moja na thelathini isipokuwa alipewa hisa yake na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Aliyekuwepo alipewa na ambaye hakuwepo aliwekewa. Yakawekwa mabakuli mawili tukala wote katika mabakuli hayo hadi tukashiba.

**Sahih Muslim: Kitabu cha vinywaji, Mlango unaoruhusu kufuatana na mtu mwingine katika nyumba ya mtu ambaye ana uhakika kuwa ataridhia:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik amesema: Abu Talha alimwambia Ummu Salim: Nimesikia sauti ya Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ikiwa dhaifu, iliyoenesha kuwa ana njaa, je una kitu chochote? Akasema: Ndiyo, akatoa vipande vya mkate wa shairi, kisha akachukua sehemu ya kitambaa chake akafunga mkate ndani ya kitambaa hicho, kisha akakiweka ndani ya nguo yangu na akanifunika na sehemu iliyo baki ya kitambaa chake, kisha alinituma kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Nilikwenda na nikamkuta Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ameketi msikitini pamoja na watu, nikasimama mbele yao. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Je umetumwa na Abu Talha?" Nikasema ndiyo. Akasema: "Chakula?" Nikasema ndiyo.

Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawaambia waliokuwa pamoja naye: "Simameni." Basi wakasimama na kuondoka na niliondoka mbele yao mpaka nilipofika kwa Abu Talha na kumpa habari. Abu Talha akasema: "Ewe Ummu Salim!Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amekuja pamoja na watu ilihali hatuna chakula cha kuweza kuwapa." Akasema: "Mwenyezi Mungu na Mtume wake ndio wajuao zaidi." Abu Talha akatoka mpaka akamlaki Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuja pamoja naye mpaka wakaingia wao wawili ndani, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Ewe Ummu Salim leta ulicho nacho." Akaleta mkate, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaamuru ukatwe vipande vipande, kisha Ummu Salim akaukamulia samli hivyo akawa ameulainisha. Kisha Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akausomea dua aliyotaka Mwenyezi Mungu ausomee, kisha akasema: "Waruhusu waingie watu kumi." Akawaruhusu wakala wakashiba kisha wakatoka, kisha akasema: "Waruhusu waingie wengine kumi." Akawaruhusu wakala wakashiba kisha wakatoka, kisha akasema: "Waruhusu waingie wengine kumi." Mpaka wakala na kushiba jamaa wote, na walikuwa ni watu sabini au thamanini."

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2 Uk. 284[111]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Samrah bin Jundub, amesema: "Tulikuwa pamoja na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) tukipokezana bakuli kuanzia chakula cha mchana mpaka cha usiku, wanasimama watu kumi na kuketi watu kumi." Nikamuuliza: Halikuwa linamiminiwa (linaongezwa chakula)? Akasema: "Unashangaa nini? Halikuwa linamiminiwa isipokuwa kutoka hapa." Akaashiria kwa mkono wake mbinguni.

[111] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha fadhila, Mlango wa dalili ziinazothibitisha unabii wa Mtukufu Mtume (saww), Hadithi ya 3625.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 3 Uk. 337[112]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir, amesema: "Mtu mmoja alikuja kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuomba chakula, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akampa chakula ambacho ni pishi sitini za shairi, basi mtu yule aliendelea yeye na mke wake na mtoto wao kula chakula kile mpaka wakaamua kukipima, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawaambia: "Kama msingekipima basi mngeendelea kula na kingeendelea kuwepo."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 3 Uk. 340[113]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir kwamba Ummu Malik al-Bahziyyah alikuwa akimpelekea Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) zawadi ya samli kwa kuibeba ndani ya mfuko wake wa ngozi. Siku moja watoto wake walimuomba kilainishia mkate –hakuwa na kitu – hivyo alikwenda kwenye mfuko wake ambao alikuwa akibebea samli anayompelekea Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), akakuta samli kidogo ndani ya mfuko huo, basi aliendelea kuwa anatumia samli hiyo kidogo kwa kuwalainishia watoto wake mikate mpaka alipoamua siku moja kuukamua mfuko. Alipokwenda kwaMtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Mtume alimuuliza: "Umeukamua?" Akasema ndiyo, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Laiti ungeuacha bila kuukamua basi samli hiyo ingeendelea kuwepo."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 3, uk. 484[114]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Ubaydah kuwa kilipikwa chungu cha nyama kwa ajili ya Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Nipe mkono wake." Nikampa, akasema tena: "Nipe mkono wake." Nikampa, akasema tena: "Nipe mkono wake." Nikasema: EweMtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwani mbuzi ana mikono mingapi? Akasema: "Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu imo mikononi mwake, laiti ungekaa kimya basi ningekupa mkono niliokuomba."

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 3, Uk. 246[115]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Nawfal bin al-Harith bin Abdul-Muttalib kuwa alimuomba Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amsaidie katika suala la kuoa, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamuoza mwanamke, alipomuomba kitu hakupata cha kumpa, ndipo Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamtuma Abu Rafiu na Abu Ayubu waende kuiweka deraya yake rehani, wakaiweka rehani kwa Yahudi mmoja kwa thamani ya pishi thelathini za shairi. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alinikabidhi shairi hiyo, nasi tulikula shairi hiyo nusu ya mwaka mzima, kisha tukaipima tukaikuta iko vilevile kama tulivyopewa. Nikamweleza habari hizo Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), akasema: "Laiti kama usingeipima basi ungeendelea kula shairi hiyo maisha yako yote."

---

[112] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal:* Musnad Jabir bin Abdillah, Hadithi ya 14211.

[113] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Musnad Jabir bin Abdillah, Hadithi ya 14254.

[114] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Hadithi ya Abu Ubaydah, Hadithi namba 15537.

[115] *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha kuatambua Masahaba, kutaja habari za Mtukufu Mtume (saww) kumuozesha Nawfal bin al-Harith kwa rehani ya deraya yake.

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 4, Uk. 116[116]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Wathilah bin al-Asqau – yeye alikuwa ni mmoja kati ya watu wa Swafah - amesema: Tulikaa siku tatu bila chakula, na kila aliyekuwa akitoka kwenda msikitini alikuwa akiwachukua watu wawili au watatu, kila mmoja kadiri ya uwezo wake, na kwenda kuwapa chakula. Mimi nilikuwa mmoja kati ya wale ambao walikaa siku hizo tatu bila chakula, ndipo nikamuona Abu Bakr usiku, nikamfuata na kumuomba anisomee Sura Sabai, alisoma mpaka akafika nyumbani kwake, na nilitaraji kwamba ataniita kwenye chakula. Alinisomea mpaka akafika kwenye mlango wa nyumba, kisha alisimama mlangoni na kunimalizia kipande kilichokuwa kimebaki, kisha aliingia ndani na kuniacha nje.

Nilipomuona Umar nilimfanyia hivyo hivyo kama nilivyomfanyia Abu Bakr. Ilipofika asubuhi nilikwenda mapema kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kumpa habari, akamwambia mtumishi wake: "Je kuna chochote?" Akasema: "Kuna kipande cha mkate na samli kidogo." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaomba viletwe. Kisha aliukatakata mkate kwa mkono wake, kisha alichukua samli hiyo chache na kuimimina katika mikate ile, kisha aliikusanya kwa mkono wake na kuifanya mseto uliotandazwa, kisha alisema: "Nenda ukaniitie watu kumi, wewe uwe wa kumi wao." Nikawaita watu kumi mimi nikiwa wa kumi wao, kisha alisema: "Kaeni," tulipokaa liliwekwa bakuli, kisha akasema: "Kuleni kwa jina la Mwenyezi Mungu, kuleni pembeni wala msile kwa juu, kwani hakika baraka huteremkia kwa juu." Tulikula mpaka tukatoboa kana kwamba tumechora mistari ndani ya chakula hivyo kwa vidole vyetu. Kisha alichukua chakula akakitengeneza na kukirudisha kama mwanzo. Halafu alisema: "Niitieni kumi wengine." Kisha aliwaita kumi wengine mara mbili, na wote walikula na kukiacha.

**Tabaqat Ibn Saad Juz. 8, Uk. 234[117]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ummu Aamir Asmau binti Yazid bin as-Saknu, amesema: Nilimuona Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiswali Maghrib ndani ya msikiti wetu. Nilikwenda nyumbani kwangu na kumletea mfupa wenye nyama na kipande cha mkate, nikamwambia: "Naapa kwa haki ya baba yangu na mama yangu, kula chakula hiki cha jioni." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawaambia Masahaba zake: "Kuleni kwa jina la Mwenyezi Mungu." Basi akala yeye na Masahaba zake waliokuja pamoja naye na waliokuwepo miongoni mwa watu wa nyumbani kwangu. Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu imo mikononi Mwake, niliuona mfupa ukiwa vilevile haujaliwa nyama yake, na mkate ulikuwa vile vile, na hakika siku hiyo walikuwa watu arubaini. Kisha alikunywa maji nyumbani kwangu kwa kiriba kibichi kisha aliondoka. Nikachukua kiriba kile nikakipaka mafuta na kukikunja, basi tulikuwa tukimnyweshea mgonjwa na wakati mwingine tukinywea kwa lengo la kupata baraka zake.

**Tabaqat Ibn Saad, Sehemu ya kwanza, Uk. 114[118]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka ka Salim bin Abu al-Jaad, amesema: Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliwatuma watu wawili katika moja ya amri zake, watu wale wakasema: "Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hatuna chakula cha kubeba." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Nitafutieni kiriba cha kubebea maji." Wakamletea kiriba, kisha alituamuru tukijaze maji nasi tukakijaza, akasema: "Nendeni mpaka mtakapofika sehemu fulani hakika Mwenyezi Mungu atawaruzuku." Basi waliondoka mpaka wakafika sehemu hiyo, na ghafla kiriba kilifunguka na wakaona maziwa ya kondoo, wakanywa na kula mpaka wakashiba.

---

[116] *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha vyakula, Baraka huteremshwa katikati ya chakula.

[117] *Tabaqat Ibn Saad*: Wake wa Ansari waitwa Waislamu wenye kutoa kiapo, Ummu Aamiru al-Ash'haliyyah.

[118] *Tabaqat Ibn Saad*: Alama za unabbi zaonekana kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hata kabla ya kukabidhiwa wahyi.

**Usudul-Ghabah Juz. 5, Uk. 629[119]:**

Amesema: Amepokea Muhammad bin Is'haqa kutoka kwa Said bin Mina, amesema: Hakika binti ya Bashiri dada yake na Nu'man bin Bashiri alisema: Mama yangu Umrat binti Rawaha aliniita na kunipa baadhi ya tende ndani ya nguo yangu, kisha aliniambia: "Nenda nazo kwa baba yako na mjomba wako Abdullah bin Rawaha kwa ajili ya chakula chao cha mchana." Nilipita kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) nikimtafuta baba yangu na mjomba wangu. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Umebeba nini?" Nikasema: "Hizi ni tende mama yangu amenituma nimletee baba na mjomba kwa ajili ya chakula chao cha mchana." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Zilete." Nikazimimina kwenye viganja vya Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) lakini hazikujaa viganja vyake.

Kisha aliamuru iletwe nguo, ikaletwa na kutandikwa, kisha alimwagia tende juu ya nguo na zikatawanyika juu ya nguo. Kisha akamwambia aliyekuwepo pale: "Waite ndani ya handaki kuwa njooni kwenye chakula cha mchana." Wakakusanyika watu wa handaki, wakaanza kula na zikaendelea kuongezeka mpaka zikawatosha watu wote wa handaki, na hakika zilikuwa zikidondoka toka kwenye pembe za nguo, na wao walikuwa watu elfu tatu.

**al-Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 8 Uk. 309[120]:**

Amesema: Imepokewa kutoka kwa mama yake na Anas bin Malik kuwa alisema: Tulikuwa na mbuzi wetu, nikakusanya samli yake ndani ya mfuko wa ngozi, nilipojaza mfuko nilimtuma Rabiba aupeleke, nilimwambia: "Ewe Rabiba, mfikishie mfuko huu Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ili awe anatumia kulainishia mkate." Rabiba aliondoka mpaka kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kumwambia: "Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), huu ni mfuko wa samli amekuletea Ummu Salim." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Mimina samli na umrudishie mfuko wake." Nikamimina na kumrudishia mfuko wake.

Nilipoondoka Ummu Salim alikuja na kuona samli ikidondoka, naye akasema: "Ewe Rabiba hivi sikukuamuru upeleke samli hii kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)?" Nikamwambia nimeshafanya, na kama huniamini nenda kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na umuulize. Basi Ummu Salim alikwenda kwaMtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa pamoja na Rabiba, akasema: "Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), mimi nilimtuma akuletee samli ikiwa ndani ya mfuko." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Amefanya hivyo, ameniletea." Ummu Salim akasema: "Naapa kwa yule ambaye amekuleta na uongofu na dini ya haki, hakika mfuko ungali umejaa na wadondoka samli." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Unashangaa Mwenyezi Mungu kukupa chakula kama ulivyompa chakula Nabii Wake? Kula na lisha chakula." Ummu Salim anasema: Nilikuja nyumbani na kuigawa samli ile kwa majirani zetu na nikaacha kiasi kidogo tulichodumu nacho mwezi au miezi miwili.

— Amesema: "Kaipokea Abu Ya'ala na Tabaraniy, isipokuwa yeye amesema ni Zainabu badala ya Rabiba."

[119] *Usudul-Ghabah*: Kitabu cha anaake, kutaja habarri za aliyemjua dada wa Fulani, dada wa Nuuman.

[120] *Majmauz-Zawa'id Wamanbaul-Fawaid*: Kitabu cha alama za unabii, Mlango wa miujiza ya Mtukufu Mtume (saww) katika chakula na baraka zake katika chakula.

**al-Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 8, uk. 309[121]:**

Amesema: Imepokewa kutoka kwa mama yake na Malik al-Ansariyah kuwa alimpelekea Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mfuko wa samli, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwamuru Bilali kumimina samli kisha akamrudishia mfuko. Aliporudi nyumbani, ghafla akauona umejaa, akarudi kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kumwambia: "Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuna chochote kimeteremka kuhusu mimi?" Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Kwa nini ewe mama Malik?" Akasema: "Kwa nini umerudisha zawadi yangu?" Wakamwita Bilal na kumuuliza kuhusu hilo, akasema: "Naapa kwa yule ambaye amekuleta kwa haki, hakika nilimimina na kukamua mpaka nikaona aibu." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Hongera ewe mama Malik, Mwenyezi Mungu amekulipa thawabu zake." Kisha alimfundisha kusoma kila baada ya Swala "Subhanallah" mara kumi, "Alhamdulilah" mara kumi na "Allahu Akbaru" mara kumi. – Amesema: Kaipokea Tabrani.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA MIUJIZA YA MTUKUFU MTUME (SAWW) KATIKA SHINA LA MTI AMBAO ALIKUWA AKITOLEA HOTUBA HAPO

**Sahih Bukhari: Kitabu cha kuanza uumbaji, Mlango wa alama za Unabii katika Uislamu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir bin Abdullah kuwa alisema: Msikiti ulikuwa umeezekwa juu ya nguzo za mashina ya mitende, hivyo ilikuwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) anapotoa hotuba husimama mbele ya shina miongoni mwa mashina hayo. Basi alipotengenezewa mimbari – tena akiwa juu ya mimbari - tulisikia sauti ikitoka katika shina hilo, mpaka alipokuja Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kuweka mkono juu yake ndipo ilipotulia.

**Sahih Bukhari: Kitabu cha mauzo, Mlango wa fundi seremala:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir bin Abdullah, amesema kuwa: Kuna mwanamke mmoja wa Kiansari alimwambia Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): "Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) je nikuwekee kitu ambacho utakuwa unaketi juu yake? Hakika mimi nina mtoto ambaye ni fundi seremala." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Ukipenda." Basi akamtengenezea mimbari, ilipofika siku ya Ijumaa, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikaa juu ya mimbari aliyotengenezewa, na ghafla ule mtende ambao alikuwa akihutubu mbele yake ukapiga kelele kiasi cha kukaribia kupasuka. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akateremka na kuukumbatia, ukaanza kutonga kama atongavyo mtoto mdogo anayebembelezwa, mpaka ulipotulia, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Ulikuwa unalia kutokana na dhikri uliokuwa ukisikia."

**Sahih an-Nasaiy Juz. 1 Uk. 207[122]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir bin Abdullah kuwa amesema: Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa anapohutubu huegemea shina la mtende ambao ni moja kati ya nguzo za msikiti,

[121] *Majmauz-Zawa'id Wamanbaul-Fawaid*: Kitabu cha alama za unabii, Mlango wa miujiza ya Mtukufu Mtume (saww) katika chakula na baraka zake katika chakula.

[122] *Sahih an-Nasaiy:* Kitabu cha Ijumaa, Mlango unaozungumzia sehemu anayopasa kusimama imamu wakati a hotuba.

alipotengenezewa mimbari na kukaa juu yake, shina lile lilitoa sauti kama sauti ya ngamia mwenye kulia kiasi kwamba waliweza kuisikia sauti yake watu waliokuwemo msikitini. Mpaka akateremka Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kwenda kulikumbatia, ndipo likatulia.

**Nasema:** Katika mlango huu kuna habari nyingi lakini tunakomea katika zile tulizozitaja kutokana na kukaribiana maudhui ya hadithi zote na kutotafautiana kwake isipokuwa kidogo sana katika baadhi ya lafudhi.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA MIUJIZA YA MTUKUFU MTUME (SAWW) KATIKA KUPASUKA KWA MWEZI

**Sahih Bukhari: Kitabu cha kuanza uumbaji, Mlango unaozungumzia kupasuka kwa mwezi:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik kuwa watu wa Makka walimuomba Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) awaoneshe muujiza, akawaonesha mwezi ukiwa vipande viwili kiasi kwamba waliweza kuona uwazi baina ya vipande viwili.

**Sahih Bukhari: Kitabu cha kuanza uumbaji, Mlango unaozungumzia kupasuka kwa mwezi:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah amesema: Mwezi ulipasuka tukiwa pamoja na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) huko Mina, akasema: "Shuhudieni." Kipande kimoja kikaelekea upande wa milimani. Abu Dhuha amesema kwa kupokea kutoka kwa Masruqu kutoka kwa Abdullah kuwa ulipasuka huko Makka.

**Sahih Bukhari: Kitabu cha tafsiri, Mlango wa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: Na mwezi ukapasuka:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa IbnMas'ud kuwa alisema: Mwezi ulipasuka vipande viwili zama za Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), huku kipande kikiwa juu ya mlima na kingine kikiwa chini yake, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Kuweni mashahidi."

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, uk. 211[123]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa alisema: "Watu wa Makka waliomba dalili, ndipo ukapasuka mwezi huko Makka mara mbili, ikateremka: **"Saa imekaribia, na mwezi umepasuka!"** mpaka: **"Na kila jambo ni lenye kuthibiti." (Sura al-Qamar: 1 – 7).**

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2 Uk. 211[124]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jubair bin Muti'imu kuwa alisema: Mwezi ulipasuka zama za Mtukufu Mtume (saww) kiasi kwamba ukawa sehemu mbili, juu ya mlima huu na juu ya mlima ule. Watu wakasema: Muhammad katuroga. Wengine wakasema: Ingekuwa katuroga asingeweza kuwaroga watu wote.

[123] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha tafsiri, Mlango wa 54 wa Sura al-Qamar, Hadithi ya 3286 na 3289.
[124] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha tafsiri, Mlango wa 54 wa Sura al-Qamar, Hadithi ya 3286 na 3289.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 1 Uk. 413[125]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah kuwa amesema: Mwezi ulipasuka zama za Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kiasi kwamba niliuona mlima baina ya mpasuko wa mwezi.

**Nasema:** Katika mlango huu kuna habari nyingi lakini sisi tumefupisha kwa kutaja hizi tulizozitaja, hiyo ni kwa sababu madhumuni ya hadithi zote yanakaribiana, na kwakuwa kisa hiki ni mashuhuri.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA MIUJIZA YA MTUKUFU MTUME (SAWW) KATIKA MAMBO MBALIMBALI

**Sahih Bukhari: Kitabu cha kuanza uumbaji, Mlango wa alama za unabii katika Uislamu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah kuwa amesema: Tulikuwa tukiichukulia miujiza kuwa ni baraka lakini ninyi mnaichukulia kuwa ni hofisho. Tulikuwa pamoja na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) safarini, tulipopungukiwa maji alisema: "Tafuteni mabaki ya maji." Basi mtu akamletea chombo kikiwa na maji machache, akaingiza mkono wake ndani ya chombo, kisha akasema: "Njooni kwenye maji masafi yaliyobarikiwa ambayo ni baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu." Hakika niliona maji yakibubujika kutoka baina ya vidole vya Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Na pia tulikuwa tukisikia tasbihi inayotolewa na chakula pindi anapokula.

**Sahih Bukhari: Kitabu cha kuanza uumbaji, Mlango wa alama za Unabii katika Uislamu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas, amesema: Kuna mtu mmoja alikuwa ni mkiristo kisha alisilimu na kusoma Sura al-Baqarah na Aali Imran, na alikuwa mwandishi wa Mtume, kisha aliritadi nakuwa mkiristo. Alikuwa akisema: "Muhammad hajui chochote ila yale niliyomwandikia." Ndipo Mwenyezi Mungu akamfisha, walipomzika walimkuta asubuhi juu ya ardhi, amekataliwa na ardhi. Wakasema: "Hiki ni kitendo cha Muhammad na Masahaba zake kwakuwa aliwakimbia. Hivyo wamemfukua jamaa yetu na kumtupa." Hivyo wakamchimbia kaburi la kina kirefu, lakini walipoamka asubuhi walimkuta kakataliwa na ardhi. Wakasema: "Hiki ni kitendo cha Muhammad na Masahaba zake kwakuwa aliwakimbia, hivyo wamemfukua jamaa yetu na kumtupa nje ya kaburi." Hivyo wakamchimbia kaburi la kina kirefu kadiri walivyoweza, lakini walipoamka asubuhi walimkuta kakataliwa na ardhi, hapo wakatambua kitendo hiki hakifanywi na watu, hivyo wakamtupa.

**Sahih Bukhari: Kitabu cha mauzo, Mlango unaozungumzia wajibu wa muuzaji na mnunuaji kupima bidhaa:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir, amesema: Abdullah bin Amru bin Haram alifariki huku akiwa na deni, nikamuomba msaada Mtukufu Mtume (saww) awaombe wadai wake wasamehedeni lake. Mtukufu Mtume (saww) akawaomba lakini hawakufanya hivyo. Ndipo Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaniambia: "Nenda kachambue tende zako na kuziweka katika anuai zake, al-Aj'wa peke yake na Idhquzaydu peke yake, kisha uzilete kwangu." Nilifanya hivyo kisha nilizipeleka kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Basi aliketi juu ya mfuko uliokuwa juu au katikati, kisha alisema: "Wapimie jamaa." Niliwapimia mpaka zikawatosha kadiri ya haki yao, na tende zangu zikabakia vile vile kana kwamba sijapunguza kitu.

[125] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal:* Musnad Abdullah bin Mas'ud, Hadithi ya 3914.

**Al-Adab al-Mufradu cha Bukhari Uk. 56[126]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah kwamba Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliteremka sehemu. Mmoja kati ya Masahaba zake akachukua yai la ndege jamii ya mbayuwayu, ndege yule alikwenda na kuanza kurukaruka juu ya kichwa cha Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Mtume akasema: "Nani kamuumiza ndege huyu kwa kuchukua yai lake?" Yule mtu akasema: "Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ni mimi ndiye niliyechukua yai lake." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Mrudishie kwa kumhurumia."

**Sahih Muslim: Kitabu cha jihadi na safari, Mlango unaozungumzia vita vya Hunayni:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Iyas bin Salmah kutoka kwa baba yake, amesema: Tulipigana vita vya Hunayni tukiwa pamoja na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Adui alipotushambulia nilitangulia kupanda mlima, na ghafla akanipokea mtu mmoja kutoka kwa maadui. Nilipotaka kumrushia mshale wangu alijificha, nikabaki sijui la kufanya. Nilipowatazama jamaa nikawaona wamechomoza kutokea upande wa pili wa njia ya mlimani, hivyo wakakutana uso kwa uso na Masahaba wa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), lakini Masahaba wa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) walikimbia. Hivyo nilirudi nikiwa ni mwenye kuishiwa nguvu huku nikiwa na shuka mbili, moja nimejifunga msuli na nyingine nimejitanda, msuli wangu ulipofunguka nilizikusanya shuka zote mbili.

Nilipita kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) nikiwa ni mwenye kuishiwa nguvu huku-Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa juu ya nyumbu wake as-Shah'bau. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Ibn al-Ak'wau ameingiwa na woga." Walipomfuata Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliteremka toka kwenye nyumbu wake kisha akachota kufi moja la udongo toka aridhini, kisha akazielekea nyuso zao na kusema: "Nyuso zimeharibika." Basi hakuna mtu aliyeumbwa na Mwenyezi Mungu kati yao isipokuwa macho yake yalijjaa udongo huo, wakakimbia na kurudi nyuma, Mwenyezi Mungu akawasambaratisha na kuwashinda, na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akagawa ngawira zao baina ya Waislamu.

**Sahih Muslim: Kitabu kinachozungumzia kuipa nyongo dunia, Mlango wa hadithi ndefu ya Jabir:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abadah bin Walid, amesema: Nilitoka mimi na baba yangu tukitafuta elimu katika mtaa huu wa Ansari kabla hawajafariki. Na mtu wa kwanza tuliyekutana naye ni Abul-Yasri, sahaba wa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). – Aliendelea kusimulia mpaka aliposema: Kisha tulikwenda mpaka kwa Jabir bin Abdullah tukamkuta msikitini kwake akisali. – Aliendelea kusimulia mpaka Jabir aliposema:

Tulikwenda pamoja na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mpaka tuliposhuka katika bonde la Af'yahu, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikwenda kukidhi haja yake, na mimi nikamfuata nikiwa nimebeba chombo cha maji. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipotazama hakuona kitu cha kuweza kukitumia kama sitara. Ghafla akaona miti miwili ikiwa pembezoni mwa bonde. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikwenda na kuchukua tawi moja na kusema: "Nifuate kwa idhini ya Mwenyezi Mungu." Basi likamfuata na kwenda pamoja naye kama ngamia mwenye kuchezeshwa chezeshwa na muongozaji wake. Kisha alikwenda katika mti wa pili na kuchukuwa tawi lake na kusema: "Nifuate kwa idhini ya Mwenyezi Mungu." Nalo likamfuata na kwenda pamoja naye mpaka alipofika sehemu ambayo ni katikati ya miti yote miwili. Akaikusanya na kusema: "Shika-

[126] *Al-Adab al-Mufradu cha Bukhari*: Mlango unaozungumzia uchukuaji wa yai kutoka kwa ndege jamii ya mbayuwayu, Hadithi ya 382.

maneni kwa kunikinga mimi kwa idhini ya Mwenyezi Mungu." Na kweli ikashikamana. – Aliendelea kusimulia mpaka Jabir aliposema:

Ulipofika muda wa kugeuka kumtazama Mtume, nilijikuta nikionana uso kwa uso na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) huku miti miwili ikiwa imeachana, kila mmoja ukiwa umejisimamia wenyewe kwa shina lake.

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 285[127]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: Kuna bedui alikuja kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kusema: "Kwa kitu gani nitatambua kuwa hakika wewe ni Nabii?" Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Je nikiita tende hii kutoka katika mtende huu je utashahidia kuwa hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu?" Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaiita, nayo ikaanza kuteremka kutoka katika mtende mpaka ikaanguka kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), kisha akaiambia: "Rudi." Ikarudi, na hapo bedui akasilimu.

**Sahih an-Nasaiy Juz. 2, Uk.64[128]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa mmoja wa Masahaba wa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuwa alisema: Pindi Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipoamuru kuchimba handaki lilijitokeza jiwe kubwa ambalo lilituzuia kuendelea kuchimba, ndipo aliposimama Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kuchukua sururu, akavua joho lake na kuliweka pembeni mwa handaki, kisha alisema: **"Na yametimia maneno ya Mola Mlezi Wako kwa kweli na uadilifu. Hapana awezaye kuyabadilisha maneno yake. Na Yeye ndiye Mwenye kusikia na Mwenye kujua."** Theluthi ya jiwe ikang'oka, wakati huo Salman alikuwa amesimama akitazama, na aliona mwanga ukiwaka pindi Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipopiga sururu.

Kisha Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipiga sururu kwa mara ya pili na kusema: **"Na yametimia maneno ya Mola Mlezi Wako kwa kweli na uadilifu. Hapana awezaye kuyabadilisha maneno yake. Na Yeye ndiye Mwenye kusikia na Mwenye kujua."** Theluthi nyingine ikang'oka na uliwaka mwanga ambao Salman aliuona. Kisha Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipiga sururu kwa mara ya tatu na kusema: **"Na yametimia maneno ya Mola Mlezi Wako kwa kweli na uadilifu. Hapana awezaye kuyabadilisha maneno yake. Na Yeye ndiye Mwenye kusikia na Mwenye kujua."** Theluthi iliyobaki ikang'oka, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akatoka akachukua joho lake na kukaa.

Salman akasema: "Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) nimekuona pindi ulipokuwa ukipiga sururu, hukupiga pigo isipokuwa liliambatana na mwanga uliowaka." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Ewe Salman! Uliuona kweli?" Akasema: "Ndiyo naapa kwa yule aliyekuleta kwa haki ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu." Mtume akasema: "Hakika nilipopiga pigo la kwanza nililetewa miji ya Kisra na ile inayoizunguka na miji mingine mingi, nikaiona yote kwa macho yangu." Mmoja kati ya Masahaba aliokuwepo pale akasema: 'Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) muombe Mwenyezi Mungu aifungue kupitia sisi, atupe ngawira za majumba yao na kwa mikono yetu aharibu nchi yao.' Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaomba hayo.

"Kisha nilipiga pigo la pili, nikaletewa miji ya Kaysari na miji mingine inayoizunguka, nikaiona yote kwa macho yangu." Wakasema: 'Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) muombe Mwe-

[127] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha fadhila, dalili za kuthibitisha unabii wa Mtukufu Mtume (saww), Hadithi ya 3628.
[128] *Sahih an-Nasaiy*: Kitabu cha jihadi, Vita vya Uturuki na Uhabeshi.

nyezi Mungu aifungue kupitia sisi, atupe ngawira za majumba yao na kwa mikono yetu aharibu nchi yao.' Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaomba hayo.

"Kisha nilipiga pigo la tatu, nikaletewa miji ya Uhabeshi na miji mingine inayoizunguka, nikaiona yote kwa macho yangu." HapoMtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Waacheni wahabeshi kama walivyokuacheni, na waacheni waturuki kama walivyokuacheni."

**Sahih Abi Daud Juz. 16, Uk. 254[129]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Ja'far kuwa alisema: Siku moja Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alinipandisha nyuma ya mnyama wake na akaongea nami baadhi ya mazungumzo ya siri ambayo alinitaka nisimweleze mtu yeyote. Kitu ambacho Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipendelea sana kujisitiri kwacho pindi aendapo katika haja yake ni ukuta au makuti ya mtende, hivyo aliingia katika bustani ya mtu mmoja miongoni mwa Ansari, na ghafla Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamuona ngamia, na ngamia alipomuona Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alianza kulia na macho yake kutoka machozi. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimfuata na kumfuta machozi yake naye akanyamaza. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Ni nani bwana wa ngamia huyu, ngamia huyu ni wa nani?" Ghafla alikuja kijana wa Kiansari na kusema: "Ni wa kwangu ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Hivi humuogopi Mwenyezi Mungu kuhusu mnyama huyu ambaye Mwenyezi Mungu amekumilikisha? Hakika amenishtakia kuwa hakika wewe unamuacha na njaa na unamchosha."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 2, Uk. 303[130]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: Hakika kundi la Makuraishi lilikusanyika katika jiwe na kukubaliana kwa kuapa kwa Lata, Uzza, Manat, Nailah na Asaf, kuwa kama tutamuona Muhammad tutamshambulia shambulio la mtu mmoja, na hatutamuacha mpaka tumuuwe. Ghafla akatokeza binti yake Fatimah (as) huku akilia, akaingia kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kusema: "Kundi hili la Makuraishi limekubaliana dhidi yako kuwa kama watakuona watakushambulia mpaka wakuuwe, hakuna mtu miongoni mwao isipokuwa ameshajua fungu lake kutoka katika damu yako."

Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Ewe binti yangu, niletee maji." Akachukua udhu kisha akawafuata msikitini, walipomuona walisema: "Huyu hapa." Wakainamisha macho yao na videvu vyao vikafika kwernye vifua vyao na wakanata pale walipokuwa wameketi. Hakuna aliyenyanyua jicho kumtizama wala hakuweza kusimama hata mtu mmoja. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikwenda mpaka akasimama juu ya vichwa vyao, akachukua kufi la udongo na kusema: "Nyuso zimeharibika." Kisha akawarushia mchanga huo, hakuna mtu kati yao aliyepatwa na mchanga huo isipokuwa aliuwawa siku ya Badri akiwa kafiri.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 2, Uk. 303[131]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik, amesema: Kuna watu wa nyumba moja ya Ansari walikuwa na ngamia ambaye walikuwa wakimtumia katika kumwagilia mazao yao. Siku moja aliwago-

[129] *Sahih Abi Daud*: Kitabu cha jihadi, Mlango wa mambo yanayofaa kutendewa wanyama, Hadithi ya 2549.
[130] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Musnad Abdullah bin Abbas, Hadithi ya 2757.
[131] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Musnad Anas bin Malik, Hadithi ya 12203.

mea na kuwakatalia mgongo wake. Ansari wale walikuja kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kumwambia: "Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), hakika tulikuwa na ngamia ambaye tulikuwa tukimtumia katika umwagiliaji, lakini amegoma na kutuzuia kupanda mgongo wake, na sasa mimea na mitende imezidi kuhitajia maji." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawaambia Masahaba zake:"Simameni." Wakasimama na kuingia ndani ya bustani, wakamkuta ngamia kasimama pembeni ya bustani.

Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimfuata ngamia upande aliokuwepo, yule Ansari akasema: "Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu, hakika amekuwa mfano wa mbwa hivyo tunahofia asije akakushambulia." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Hakuna ubaya utakaonisibu kutoka kwake." Ngamia alipomtazama Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimfuata na kusujudu mbele yake, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamshika utosini. Ngamia alionekana mtiifu kushinda hata alivyokuwa, kisha Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwingiza kazini. Masahaba zake wakasema: "Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ngamia huyu asiyekuwa na akili anakusujudia, na sisi tuna akili, hivyo sisi ndio twastahiki zaidi kukusujudia." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Haifai binadamu kumsujudia binadamu mwenzake, na kama ingefaa basi ningemwamuru mwanamke kumsujudia mumewe kutokana na haki kubwa aliyo nayo kwake."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 2, Uk. 303[132]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Uthman bin Hunayfu kuwa hakika mtu mmoja aliyekuwa kipofu alikuja kwaMtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kumwambia: "Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu, niombee kwa Mwenyezi Mungu aniafu." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Ukitaka nitakuakhirishia hilo kwani ndio bora kwa ajili ya Akhera yako, na ukitaka nitakuombea sasa hivi." Akasema: "Hapana, bali niombee kwa Mwenyezi Mungu." Basi akamwamuru achukue udhu na asali rakaa mbili na aombe dua hii: "Ewe Mwenyezi Mungu nakuomba na naelekea kwako kupitia Nabii wako Muhammad Nabii wa rehema. Ewe Muhammad, hakika mimi naelekea kwa Mola wangu kupitia kwako ili haja yangu hii iweze kukidhiwa. Niombeena kuomba kwa ajili yangu." Kipofu yule alikuwa akisoma hivyo mara kwa mara.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 4, Uk. 170[133]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ya'ala bin Marah kuwa amesema: Niliona mambo matatu kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), mambo ambayo hakupata kuyaona yeyote kabla yangu, na wala hatayaona yeyote baada yangu. Nilitoka pamoja naye katika safari moja, mpaka tulipofika sehemu fulani ya njia, tukamkuta mwanamke ameketi pamoja na mwanaye mdogo, mwanamke yule akasema: "Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mtoto wangu huyu kapatwa na balaa, nami nimepatwa na balaa kutoka kwake, sijui ni mara ngapi kwa siku anapatwa na mashetani." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Nipe huyo mtoto." Mwanamke yule akampa, Mtume akamuweka baina yake yeye na mnyama wa safari, kisha alimfunua kinywa na kumtemea mate mara tatu, na kusema: "Bismillahi mimi ni mja wa Mwenyezi Mungu, ondoka ewe adui wa Mwenyezi Mungu." Kisha akamrudishia mtoto wake na kumwambia: "Tukutane hapa wakati wa kurudi na ili utueleze amefanya nini."

Tulikwenda na tukarejea na kumkuta mwanamke yule sehemu ile akiwa na mbuzi watatu. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamuuliza: "Amefanya nini mwanao?" Akasema: "Naapa kwa yule aliyekuleta kwa haki, hatukuhisi chochote kutoka kwake mpaka muda huu, ndipo wakaja mbuzi

[132] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Musnad Anas bin Malik, Hadithi ya 12203.
[133] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Hadithi ya Ya'la bin Marah at-Thaqafiy, Namba 17097.

hawa." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaniambia: "Teremka na mchukue mmoja na waache wengine."

Na nilitoka siku moja kuelekea jangwani nikiwa pamoja na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), tulipofika jangwani alisema: "Tazama je unaona kitu cha kuweza kunisitiri?" Nikamwambia: "Sioni kinachoweza kukusitiri isipokuwa mti ambao nao naona hauna uwezo wa kukusitiri." Akasema: "Ni kitu gani kile karibu ya mti ule?" Nikasema: "Ni mti mfano wake au ulio karibu na mwenzie." Akasema: "Nenda kaiambie kuwa: Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) anakuamrisheni kukusanyika pamoja kwa ajili ya Mwenyezi Mungu." Kweli miti ile ikakusanyika pamoja, alikwenda katika haja yake kisha alirejea. Kisha Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaniambia: "Nenda kaiambie kuwa: Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) anakuamrisheni kila mmoja urudi sehemu yake." Ikarudi.

Siku moja nilikuwa nimeketi kwake na ghafla alikuja ngamia akitembea kwa kurukaruka mpaka akawa ameweka shingo yake mbele ya Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Kisha macho yake yakaanza kububujika machozi. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Chunguza ni wa nani ngamia huyu, kwani hakika ana jambo." Nikatoka kwenda kumtafuta mmiliki wake, nikamkuta ni mwanaume mmoja wa Kiansari. Nikamwita kwenda kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), akamwambia: "Ana habari gani huyu ngamia wako?" Akasema: "Wallahi sijui ana jambo gani, tulikuwa tunafanya kazi na kumtumia katika umwagiliaji na ghafla tu akashindwa kuendelea na umwagiliaji, hivyo tukaazimia kumchinja na kugawana nyama yake." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Msifanye hivyo, nipeni zawadi ngamia huyu au niuzienmi." Akasema: "Kuanzia sasa ni wa kwako ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu." Akamwekea alama ya sadaka kisha akatuma ipelekwe sadaka hiyo.

**Tabaqat Ibn Saad, Sehemu ya kwanza, Uk. 125[134]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Zaid bin Aslam na mwingine, kuwa jicho la Qatadah bin Nu'man lilipigwa, likang'oka na kuanza kuteremka hadi mashavuni, ndipo Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akalirudisha kwa mkono wake, kuanzia hapo macho yake yalikuwa mazuri zaidi na yenye afya zaidi.

**Tabaqat Ibn Saad, Sehemu ya kwanza, Uk. 125[135]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Zaid bin Aslam na Yazid bin Rawman na Is'haqa bin Abdullah bin Abu Farah na wengineo kuwa upanga wa Akashah bin Muhsin ulikatika siku ya Badri, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akampa gongo la mti, likarudi mikononi mwake likiwa limegeuka na kuwa upanga mkali uliyo imara.

**Sunanud-Daramiy Juz. 1, uk. 29[136]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Salmah as-Sukuniy, amesema: Tulikuwa kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na ghafla akasema mwenye kusema: "Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu, je umeleta chakula kutoka mbinguni?" Akasema: "Ndiyo nimeleta." Akasema: "Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu je, kulikuwa na mabaki yoyote?" Akasema: "Ndiyo." Akasema: "Yamefanywa nini?" Akasema (saww): "Yamerudishwa mbinguni."

---

[134] *Tabaqat Ibn Saad*: Kutaja alama za unabii baada ya kuteremka wahyi kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).
[135] *Tabaqat Ibn Saad*: Kutaja alama za unabii baada ya kuteremka wahyi kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).
[136] *Sunanud-Daramiy*: Mlango wa karamu aliyofanyiwa Mtukufu Mtume kwa kuteremshiwa chakula kutoka mbinguni, Hadithi ya 55.

**Sunanud-Daramiy Juz. 1, uk. 29[137]:**

Amepokea ka njia yake kutoka kwa Ibn Umar amesema: Tulikuwa safarini pamoja na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), ghafla alikuja bedui, aliposogea karibu, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia: "Unataka kwenda wapi?" Akasema: "Kwa ndugu zangu."Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamuuliza: "Je unahitaji kheri?" Akasema: "Ni ipi?" Akamwambia: "Ushahidilie kuwa hapana mungu isipokuwa Allah mmoja wa Pekee asiye na mshirika, na kwamba hakika Muhammad ni mja na Mtume Wake." Akasema: "Na ni nani atakayeshahidia hayo usemayo?"Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Mti huu." Kisha Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akauita, nao ulikuwa ukingoni mwa bonde, ukaja huku ukijiburuza aridhini mpaka ukasimama mbele yake, naye akauomba ushahidilie mara tatu, nao ukashahidia mara tatu kama alivyosema, kisha ukarejea sehemu yake. Bedui alirejea kwa jamaa zake na alimwambia Mtume: "Wakinifuata nitawaleta kwako, la sivyo nitarejea kwako na kuishi pamoja na wewe."

**Sunanud-Daramiy Juz. 1, uk. 29[138]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Kuna mtu mmoja kutoka kwa Bani Aamir alikuja kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Je nikuonesha muujiza?" Akasema: "Ndiyo." Akasema: "Nenda kauite mtende ule." Alikwenda na kuuita na ukaja huku ukirukaruka hadi mbele yake. Kisha akamwambia Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): "Uambie urudi mahala pake."Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akauambia: "Rudi mahala pako." Ukarudi mahala pake, mtu yule akasema: "Ewe Bani Aamir sijapata kumuona mtu kama niliyemuona leo, mtu mchawi kushinda yeye."

**Taarikh Baghdad Juz. 13, Uk. 128[139]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Maklabah bin Malakani amesema: Nilipigana vita pamoja na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), mushrikina wakamshambulia shambulio kali mpaka wakaweka kizuizi baina yake na maji. Na ni wao walioteremka sehemu yenye maji, nikamuona Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa na kiu kali amevua nguo yake na kujifunika joho lake na amelalia mgongo wake. Nilichukua chombo changu na kwenda kutafuta maji mpaka nilipofika katika ardhi yenye mchanga, ghafla nikamuona ndege mfano wa kwale nikasogea karibu yake, aliponiona aliruka, nikatizama sehemu aliyokuwepo nikaona unyevunyevu ukitoka, basi nikachimba hapo kwa mkono wangu kwa kina, maji yakatoka, nikanywa hadi nikatosheka, nikatawadha na kujaza chombo na nikarudi hadi kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

Aliponiona aliniambia: "Ewe Maklabah je umekuja na maji?" Nikasema ndiyo ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), akasema: "Nipe haraka." Nikasogea karibu yake nikampa chombo akanywa mpaka akatosheka, akatawadha kwa ajili ya swala, kisha akaniambia: "Ewe Maklabah weka mkono wako juu ya kifua changu mpaka kipoe." Nikaweka mkono wangu juu ya kifua chake mpaka kikapoa. Kisha aliniambia: "Ewe MaklabahMwenyezi Mungu amejua nia yako katika hili." Nikaondoa mkono wangu toka kwenye kifua chake, nikauona mkono wangu ukitoa nuru. Hivyo Maklabah alikuwa akificha mkono wake mchana kwa kuogopa watu wasikusanyike kwake na hatimaye kumuudhi, na hivyo yule asiyemjua anapomuona hudhani kuwa ni mlemavu aliyekatika mkono.

[137] *Sunanud-Daramiy*: Mlango unaoelezea karama ambayo Mwenyezi Mungu alimfanyia Mtukufu Mtume wake, kwa kuaminiwa na miti, wanyama na majini, Hadithi ya 16.

[138] *Sunanud-Daramiy:* Mlango unaoelezea karama ambayo Mwenyezi Mungu alimfanyia Mtukufu Mtume wake, kwa kuaminiwa na miti, wanyama na majini, Hadithi ya 16.

[139] *Taarikh Baghdad*: Wasifu wa al-Mudhaffar bin Asim al-Ajaliy, Namba 7112.

— Al-Mudhaffar anasema: Nilikutana na Maklabah usiku, nikampa mkono nikaona mkono wake ukitoa nuru.

**Taarikh Baghdad Juz. 3, Uk. 442[140]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Maaradh bin Abdullah bin Maaradh, kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake kuwa alisema: Nilihiji Hijja ya kuaga, nikaingia nyumba moja huko Makka, nikamuona humo Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aking'ara uso wake mfano wa mbaramwezi, na nilisikia jambo la ajabu kutoka kwake, kwani kuna mtu mmoja miongoni mwa watu wa al-Yamamah alimleta mtoto siku ileile aliyozaliwa akiwa amemfunika ndani ya kitambaa. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Ewe mtoto mimi ni nani?" Akasema: "Wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Umesema kweli, Mwenyezi Mungu akubariki." Kisha mtoto baada ya hapo hakuwahi tena kutamka mpaka alipokuwa kijana. Baba yangu anasema: Tulikuwa tukimwita mbarikiwa wa al-Yamamah.

**Al-Isabah Juz. 6, Sehemu ya kwanza, Uk. 292[141]:**

Ametaja hadithi kwa njia ya Hamam bin Nafil kuwa alisema: Nilikwenda kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kumwambia: "Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) tumechimba kisima na yametoka maji chumvi." Akanipa chombo ambacho ndani yake kilikuwa na maji kidogo, akaniambia: "Kamwagie maji haya ndani ya kisima." Nikafanya hivyo maji yakawa matamu.

**Al-Istiaab Juz. 2, uk. 556[142]:**

Ametaja hadithi kwa njia ya Abdullah bin Buraydah kutoka kwa Salman al-Farsiy kuwa alisema: Alipeleka sadaka kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), akamwambia: "Hii ni sadaka yako na ya Masahaba zako." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Ewe Salman hakika sisi watu wa nyumba ya Mtume si halali kwetu sadaka." Akaichukua na alikuja nayo tena siku iliyofuata, akasema: "Hii ni zawadi." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawaambia Masahaba zake: "Kuleni." Ndipo Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamnunua kutoka kwa Mayahudi kwa thamani kadhaa ya dirhamu, kwa sharti kwamba awalimie mitende kiasi kadhaa, Salman afanye kazi katika mitende hiyo mpaka tende zitakapoiva. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akapanda mitende yote isipokuwa mtende mmoja ambao ulipandwa na Umar, mitende yote ikapamba isipokuwa mtende mmoja, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akauliza: "Ni nani aliyeupanda?" Wakasema ni Umar, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaung'oa na kuupanda kwa mkono wake, basi ukapamba mwaka huo huo uliyopandwa.

**Usudul-Ghabah Juz. 2, uk. 278[143]:**

Ametaja hadithi kwa njia itokayo kwa binti ya al-Hakam bin Abil-Asi, kuwa alimwambia al-Hakam: Sijapata kuwaona watu waliokuwa na rai mbaya na dhaifu katika jambo la Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kushinda ninyi enyi Bani Umaiyyah. Al-Hakam akasema: "Usitulaumu ewe binti yangu, hakika mimi sintakusimulia isipokuwa yale niliyoyaona kwa macho yangu haya mawili. Wallahi

---

[140] *Taarikh Baghdad*: Wasifu wa Muhammad bin Yunus Abul-Abbas al-Kadimiy, Namba 1574.
[141] *Al-Isabah*: Herufi Hau, Hamamu bin Nafil as-Saadiy, Namba 9002.
[142] *Al-Istiaab*: Herufi Siin, Mlango a Salman al-Farsiy.
[143] *Usudul-Ghabah:* Mlango wa herufi Hau, wasifu a al-Hakam bin Abil-Aasi.

tuliendelea kuwasikia Makuraishi wakisema: 'Huyu Msabai anaswalia ndani ya msikiti wetu.' Hivyo wakakubaliana kumuuwa, tukakubaliana kumshambulia, tulipomuona tulisikia sauti ambayo tulidhani hakuna mlima uliobaki eneo la Tahamah isipokuwa ulitudondokea sisi. Hatukukumbuka mpaka alipomaliza Swala yake na kurejea kwa watu wake. Kisha tulikubaliana kumshambulia katika usiku mwingine. Tulipokwenda kwake, mimi niliona mlima wa Swafa na Mar'wa ikiwa imeshikana na kutuzuia tusiweze kumfikia, wallahi hatukufanikiwa.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 278[144]:**

Amesema: Imepokewa kutoka kwa Umar kuwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa katika kundi la Masahaba zake, ghafla alikuja bedui kutoka kwa Bani Salim akiwa keshamuwinda kenge na amemuweka ndani ya mfuko wake ili ambebe na kwenda kumchoma na kumla. Alipoona kundi la watu alisema: "Kuna nini?" Wakamwambia: "Huyu ndiye anayesemekana kuwa ni Nabii." Basi alikuja akawasukuma watu na kupita, akasema: "Naapa kwa Lata na Uzza wanawake hawajabeba kiumbe chenye ulimi ninachokichukia kukushinda wewe, na laiti si kuogopa watu wangu kuniita 'Mpupiaji' basi ningefanya haraka kukushambulia na kukuuwa, ili kwa kukuuwa wewe niwafurahishe wekundu, weusi, weupe na wengineo." Nikasema: "Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu, niache niende kumuuwa." Akasema: "Ewe Umar hivi hujui kuwa mvumilivu alikaribia kuwa Nabii?" Kisha alimgeukia bedui na kumwambia: "Kitu gani kimekupelekea kusema uliyoyasema, umesema yasiyo haki na wala hujaheshimu baraza langu?"

Akasema: "Hivi bado tena unanisemesha," - akionesha dharau kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). – "Naapa kwa Lata na Uzza sikuamini labda akuamini huyu kenge." Akamtoa kenge kutoka ndani ya mfuko wake na kumtupa mbele ya Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), na kusema: "Akikuamini kenge huyu nami nitakuamini." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Ewe kenge." Kenge akamjibu – kwa lugha ya Kiarabu fasahaambacho alikisikia kila aliyekuwepo: "Labaika Wasaadayka ewe pambo la atakayehudhuria Siku ya Kiyama." Akasema: "Unamwabudu nani ewe kenge?" Akasema: "Ambaye Arshi yake iko mbinguni na ardhini kuna mamlaka Yake, baharini kuna njia Yake, peponi kuna rehema Zake na motoni kuna adhabu Yake." Akasema: "Mimi ni nani ewe kenge?" Akasema: "Wewe ni Mtume wa Mola wa walimwengu na mwisho wa Manabii, na amefaulu yule mwenye kukusadikisha na amepata hasara yule mwenye kukukadhibisha."

Bedui akasema: "Sifuati athari baada ya kuona uhalisia wenyewe.Wallahi nilikuja kwako nikiwa sina mtu ninayemchukia juu ya mgongo wa ardhi kushinda wewe, na hakika leo hii wewe ni mtu nikupendaye sana kushinda mtoto wangu na nafsi yangu. Na hakika mimi nakupenda kwa moyo wangu na mwili wangu, kwa siri na kwa dhahiri. Nashahidia kuwa hapana mungu isipokuwa Allah na hakika wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu."Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Kila himidi njema ni ya Mwenyezi Mungu ambaye amekuongoza katika dini ambayo iko juu na hakuna iliyo juu zaidi yake, na Mwenyezi Mungu haikubali isipokuwa kwa Swala, na Swala haikubaliwi isipokuwa kwa Qur'ani."

Bedui akasema: "Nifundishe Qur'ani." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamfundisha Alhamdu na Surat Ikhlaswi. Akasema: "Niongezee ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), kwani sijapata kusikia maneno mazuri kushinda haya, si katika nathariwala katika mashairi." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Ewe bedui, hakika maneno ya Mwenyezi Mungu si mashairi, na hakika iwapo wewe utasoma: **"Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni wa pekee,"**mara moja utapata malipo ya mtu aliyesoma theluthi ya Qur'ani. Na ukisoma: **"Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni wa pekee,"**mara mbili utapata malipo ya mtu aliyesoma theluthi mbili ya Qur'ani. Na ukisoma **"Sema:**

[144] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha fadhila, Mlango wa fadhila za Mtukufu Mtume (saww), Miujiza na dalili za Unabii, Hadithi ya 3564.

**Yeye Mwenyezi Mungu ni wa pekee,"**mara tatu utapata malipo ya mtu aliyeisoma Qur'ani yote." Bedui akasema: "Ndiyo, Mungu ni Mungu wetu anapokea kichache na kulipa kingi."Mwandishi anasema: Ameiandika Tabaraniy, Ibn Adiy, al-Hakim, Abu Naiim, al-Bayhaqiy na Ibn Asakir.

**Kanzul-Ummal Juz. 6 Uk. 278[145]:**

Amesema: Jarhadi alikwenda kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), na chakula kilikuwa mbele ya Mtume. Jarhad akasogeza mkono wake wa kushoto ili ale – mkono wake wa kulia ulikuwa na maumivu- Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Kula kwa mkono wa kulia." Akasema: "Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hakika wenyewe una maumivu." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akautemea mate, hakulalamika tena kuuma mkono mpaka anafariki. Amesema: - Ameiandika Tabaraniy kutoka kwa Jarhadi.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9 Uk. 10[146]:**

Amesema: Imepokewa kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: Mtu mmoja kutoka kwa Bani Aamir ambaye alikuwa akitibu na kutoa dawa alikuja kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kumwambia Mtume: "Ewe Muhammad, hakika wewe unasema mengi (kama mwendawazimu), je upo tayari nikupe dawa?" Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwita na kumwambia: "Na wewe upo tayari nikupe dawa?" Akasema: "Ndiyo." Na hapo palikuwa na mtende na mti mwingine. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akauita mtende wenye makole, nao ulikuja kwake huku ukisujudu na kuinuka, ukisujudu na kuinuka mpaka ulipofika kwake, ukasimama mbele yake, kisha Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Rejea sehemu yako." Ukarejea sehemu yake, mtu yule akasema: "Wallahi kamwe kuanzia sasa sintakukadhibisha katika chochote usemacho." – Amesema: Ameipokea Abu Ya'ala.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9, uk.21[147]:**

Amesema: Imepokewa kutoka kwa Abu Amamah kuwa alisema: Kuna mwanamke mwenye maneno machafu alikuwa akimtamkia mwanaume maneno machafu. Siku moja alipita kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kumkuta anakula juu ya jiwe kubwa. Mwanamke yule akasema: "Tazama, anakaa kama mtumwa, na anakula kama mtumwa." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Na ni mtumwa yupi ni mtumwa zaidi kushinda mimi?" Akasema: "Anakula hata bila kunikaribisha." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Kula." Akasema: "Nipe kwa mkono wako." Mtume akampa kwa mkono wake, akasema: "Nilishe kile kilichomo kinywani mwako." Mtume akampa naye akala na hapo haya ikamshinda nguvu na kuanzia hapo hakuwahi kumtamkia mtu maneno machafu mpaka kufa kwake.

[145] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha fadhila, Mlango wa fadhila za Mtukufu Mtume (saww), Miujiza na dalili za Unabii, Hadithi ya 35381.
[146] *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid:* Mlango wa miujiza yake (saww) katika wanyama, miti na vinginevyo.
[147] *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid:* Mlango wa unaozungumzia unyenyekevu wake (saww) .

# MLANGO UNAOZUNGUMZIA USHUHUDA WA UT'BAH BIN RABIA'H KWAMBA QUR'ANI SI MASHAIRI WALA SI UCHAWI WALA SI UKUHANI

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 289[148]:**

Amesema: Imepokewa kutoka kwa Muhammad bin Ka'bi al-Qardhiy, amesema: Nilisimuliwa kuwa Ut'bah bin Rabia'h – alikuwa ni bwana mpole – alisema siku moja akiwa ameketi katika nadi ya Makuraishi huku Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa kaketi peke yake msikitini: "Enyi kundi la Makuraishi kwa nini mimi nisiende kwa mtu huyu kuzungumza naye na kupendekeza kwake baadhi ya mambo ambayo huenda atayakubali baadhi nasi tutampa atakalo na hatimaye atatuacha?" Na hiyo ilitokea wakati aliposilimu Hamza bin Abdul-Muttalib, na Makuraishi wakaona kuwa Masahaba wa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) wanazidi kuongezeka na kukithiri. Wakasema: "Nenda, simama ewe Abul-Walid kaongee naye." Ut'bah alisimama na kwenda na kuketi kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kumwambia:

"Ewe mtoto wa ndugu yangu, hakika wewe ni miongoni mwetu na unajua ukubwa wa ukoo wetu na nafasi ya nasaba yetu. Na hakika umewaletea jamaa zako jambo adhimu ambalo kwalo umefarakisha umoja wao, umepuuza ndoto zao, umeitia dosari miungu yao na dini yao na umewakufurisha wahenga wako waliotangulia. Hivyo nakusihi uweze kunisikia nisemacho. Napendekeza kwako mambo fulani ambayo tunataka uyachunguze huenda ukakubali baadhi yake." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Sema ewe Abul-Walid."

Akasema: "Ewe mtoto wa ndugu yangu, hakika ikiwa unachotaka kupitia hii kauli uliyokuja nayo ni mali, basi tutakukusanyia mali zetu mpaka wewe uwe ndiye mwenye mali kutushinda sote. Na ikiwa unachotaka ni heshima basi sisi tutakufanya mtu mwenye heshima juu yetu kiasi kwamba hatutafanya maamuzi yoyote bila uamuzi wako. Na ikiwa unachotaka ni ufalme basi tutakupa ufalme juu yetu, na ikiwa huyo anayekuja kwako ni jini unayemuona lakini huna uwezo wa kumzuia basi tutakutafutia tabibu na tutatoa mali zetu katika matibabu hayo mpaka akusalimishe naye, kwani kuna wakati jini linaweza kumshinda mtu mpaka akahitaji kutibiwa ili limwepuke. Na huenda haya anayokuja nayo ni mashairi anayoyaweka kifuani mwako usiku, na hakika ninyi wana wa Abdul-Muttalib mna uwezo wa kumwepuka katika kiwango ambacho hakuna yeyote awezaye zaidi yenu."

Aliendelea kusema hukuMtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akimsikiliza mpaka aliponyamaza, ndipo Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamuuliza: "Je umemaliza ewe Abul-Walid?" Akasema: "Ndiyo." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Nisikilize." Akasema: "Endelea." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: **"Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi a rehema Mwenye kurehemu. H'a Mim. Uteremsho huu umetoka kwa Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu."**Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliendelea kumsomea Sura hiyo, Ut'bah alipoisikia alikaa kimya na kusikiliza huku akiwa ameegemea mikono yake kwa kuiweka nyuma ya mgongo wake, mpaka Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipofika katika sijda akasujudu kisha akasema:

"Ewe Abul-Walid umeshasikia uliyosikia, jipime wewe na hayo." Ut'bah akasimama na kwenda kwa jamaa zake, wakaanza kuambizana: "Tunaapa kwa Mwenyezi Mungu hakika Abul-Walid amekuja na uso ambao si ule aliokwenda nao." Alipoketi kwao walisema: "Umekuja na nini ewe Abul-Walid?" Akasema:

[148] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha fadhila, Mlango wa fadhila za Mtukufu Mtume (saww), Miujiza na dalili za Unabii, Hadithi ya 35428.

"Wallahi nilichokuja nacho ni kwamba mimi nimesikia kauli ambayo katu sijapata kusikia mfano wake. Wallahi si mashairi wala si uchawi wala si ukuhani. Enyi kundi la Makuraishi, nitiini na yaacheni kwangu, mwacheni mtu huyu na imani yake na jitengeni mbali naye.Wallahi naapa atakuwa habari nzito kutokana na kauli yake niliyoisikia, hivyo kama Waarabu watamdhuru mtakuwa mmejiepusha naye kwa msaada wa watu wengine. Na kama atawashinda Waarabu basi ufalme wake ndio ufalme wenu na nguvu yake ndio nguvu yenu na mtakuwa watu wenye heshima zaidi kupitia yeye." Wakasema: "Wallahi amekuroga ewe Abul-alid kwa ulimi wake." Akasema: "Hii ndio rai yangu kwenu, fanyeni mtakavyo." – Amesema: "Ameiandika al-Bayhaqiy ndani ya kitabu *ad-Dalailu* na pia kaiandika Ibn Asakir."

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA KITENDO CHA MTUKUFU MTUME (SAWW) KUOMBA MVUA

**Sahih Bukhari: Kitabu cha kuanza uumbaji, Mlango wa alama za Unabii katika Uislamu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa amesema: Watu wa Madina walipatwa na ukame zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Akiwa anatoa hotuba siku ya Ijumaa, ghafla alisimama mtu mmoja na kusema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mazao yameangamia na mbuzi wameangamia, muombe Mwenyezi Mungu atuletee mvua." Akanyoosha mikono yake na kuomba.

Anas anasema: Mbingu ilikuwa kama kioo, ghafla ukavuma upepo na kukusanya mawingu kisha mbingu iliteremsha mvua kubwa. Tukatoka huku tukitembea ndani ya maji mpaka majumbani mwetu. Iliendelea kunyesha mpaka Ijumaa iliyofuata, ndipo akasimama mtu yule yule au mwingine na kusema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Nyumba zimebomoka muombe Mwenyezi Mungu aizuie." Mtume akatabasamu kisha alisema: "Iwe pembezoni mwetu na si juu yetu." Nilipotazama mawinguni niliyaona yakiwa yametawanyika pembezoni mwa Madina.

**Sahih Abi Daud Juz. 7, Uk. 115[149]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha kuwa alisema: Watu walimlalamikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ukame wa mvua. Akaamuru itengenezwe mimbari, ikawekwa sehemu ya kuswalia na akawatajia watu siku ya kutoka. Akatoka Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) baada tu ya jua kuchomoza, akaketi juu ya mimbari, akatoa takbira, akamuhimidi Mwenyezi Mungu, kisha alisema: "Hakika ninyi mmenilalamikia ukame uliopo katika majumba yenu na jinsi mvua ilivyochelewa na muda wake kupita. Mwenyezi Mungu amekuamuruni kumuomba na amekuwahidini kukujibuni." Kisha alisema:

"Kila himidi njema ni ya Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu wote. Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Mfalme wa siku ya malipo, hapana mungu isipokuwa Allah ambaye hufanya atakalo. Ewe Mungu Wangu, wewe ni Mwenyezi Mungu ambaye hapana mungu isipokuwa Wewe. Wewe ni tajiri na sisi ni mafukara, tushushie mvua, na jaalia yale utakayoteremsha kwetu yawe ni nguvu na uwezo mpaka muda maalumu."Kisha alinyanyua mikono yake na iliendelea kuwa juu mpaka ukaonekana weupe wa makwapa yake. Kisha aliwageukia watu na kuteremka toka mimbarini. Akaswali rakaa mbili na hapo Mwenyezi Mungu akaanzisha mawingu, radi ikapiga na kutoa mwanga, kisha mvua ikanyesha kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.

[149] *Sahih Abu Daud*: Kitabu cha Swala, Mlango unaozungumzia kunyanyua mikono juu wakati wa kuomba mvua, Hadithi ya 1173.

Kabla hajafika msikitini kwake maji yalianza kutembea kwa wingi, alipoona jinsi wanavyoharakisha kwenda majumbani alicheka mpaka magego yake yakaonekana, akasema: "Nashahidia kuwa hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu, na hakika mimi ni mja wa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 4, Uk. 235 – 236[150]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Sharhabil bin Samtu, amesema: Ka'b bin Marrah aliambiwa: "Ewe Ka'b bin Marrah, tusimulie kuhusu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). - Alisimulia mpaka aliposerma: Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema baada ya mtu mmoja kuja kwake na kusema: Muombe Mwenyezi Mungu awashushie mvua watu wa Mudhari, alisema: "Hakika wewe ni jasiri wa watu wa Mudhari." Mtu yule akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ulimuomba nusra Mwenyezi Mungu akakunusuru na ukamuomba Mwenyezi Mungu akakujibu." Ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akanyanyua mikono yake juu na kusema: Ewe Mungu Wangu, tuteremshie mvua yenye msaada, yenye kuotesha mazao, yenye kulainisha, yenye kuifunika ardhi, nyingi, sasa hivi bila kuchelewa, yenye manufaa isiyo na madhara." Mara wakarudishiwa uhai, na haukupita muda mrefu walikuja kwake na kumlalamikia wingi wa mvua, wakasema: "Nyumba zimebomoka." Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliinua mikono yake mbinguni na kusema: "Ewe Mungu Wangu, iwe pembezoni mwetu na si juu yetu." Mawingu yakaanza kutawanyika kulia na kushoto.

**Sunan ad-Daramiy Juz. 1, Uk. 43[151]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Awsi bin Abdullah kuwa alisema: Watu wa Madina walipatwa na ukame mkali, wakamlalamikia Aisha, naye akasema: "Litazameni kaburi la Mtukufu Mtume (saww) na lifanyeni sehemu ya kutazamia mbingu kiasi kwamba kusiwe na dari baina yake na mbingu (Ondoeni dari na kizuizi)." Walipofanya hivyo ilinyesha mvua kubwa kiasi kwamba majani yaliota na ngamia wakanenepa mpaka wakapasuka kwa mafuta, na mwaka huo ukaitwa 'Mwaka wa kupasuka ngamia'.

## MLANG O UNAOZUNGUMZIA BAADHI YA DUA ALIZOOMBA MTUKUFU MTUME NA ZIKAJIBIWA

**Mustadrakus-Sahihayni Juz. 2, uk. 621[152]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdurahman bin Abu Bakr kuwa alisema: Fulani alikuwa akiketi mbele ya Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Mtume akizungumza kitu yeye hugeuza uso wake. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Kuwa hivyo hivyo." Basi aliendelea kuwa na uso uliogeuka nyuma mpaka kufa kwake.

**Tabaqat Ibn Saad Juz. 1, Sehemu ya kwanza, Uk. 157[153]:**

Kutoka kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) pangoni, ilikuwa ni usiku wa kuamkia Jumatatu, mwezi nne Rabiul-Awal, akapumzika Qadid. Siku ya Jumanne, alipoondoka hapo ndipo alipojitokeza Suraqah bin Jaasham akiwa juu ya farasi wake. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)

[150] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Hadith ya Ka'b bin Marrah au Marrah bin Ka'b, Namba 1760.
[151] *Sunan ad-Daramiy:* Mlango unaozungumzia yale ambayo Mwenyezi Mungu alimkirimu Nabii wake baada ya kufa kwake, Hadithi ya 92.
[152] *Mustadrakus-Sahihayni*: Kitabu cha historia, kusilimu kwa mama yake na Abu Huraira kwa dua ya Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).
[153] *Tabaqat Ibn Saad:* Kutaja kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa na Abu Bakr kwa ajili ya kuhama.

alimuombea dua baya miguu ya farasi wake ikakwama, akasema: “Ewe Muhammad, muombe Mwenyezi Mungu amkwamue farasi wangu na niweze kurejea toka kwako na niwarudishe wale walio nyuma yangu.” Mtume akafanya hivyo. Alikwamuliwa na akarejea na kuwakuta watu wakimtafuta Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), akasema: “Rejeeni nimeshamtafuta hayupo hapa na ninyi mnajua ujuzi wangu wa kutambua nyayo.” Wakarejea bila kumfuata.

**Usudul-Ghabah Juz. 4, Uk. 363[154]:**

Ametaja hadithi kwa njia itokayo kwa Abu Nafawl bin Abu ‘Aqrab kutoka kwa baba yake, amesema: Lahabi bin Abulahabi alikuwa akimtukana Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Mtume (saww) akasema: “Ewe Mungu Wangu mtumie mbwa miongoni mwa majibwa yako.” Basi alipoondoka kuelekea Sham akiwa katika msafara pamoja na rafiki zake walipumzika sehemu, akasema: “Wallahi mimi naogopa dua ya Muhammad.”Hivyo walimzungushia mizigo na wakaketi wakimlinda, lakini alikuja mbwa akamnyakua na kuondoka naye.

**Majmauz-Zawa’id ya al-Haythamiy Juz. 6 Uk. 183[155]:**

Amesema: Imepokewa kutoka kwa Mas’ab bin Shaybah kutoka kwa baba yake, amesema: Nilitoka pamoja na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) siku ya Hunayni, wallahi sikutoka kwa ajili ya Uislamu wala si kwa ajili ya kuutambua, lakini nilikhofu kwamba isije Hawazin ikawashinda Makuraishi, hivyo nilimwambia huku nikiwa pamoja naye: “Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu hakika mimi namuona farasi mwenye mabaka meusi na meupe.” Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: “Ewe Shaybah, hakika hamuoni farasi huyo isipokuwa kafiri.” Akapiga mkono wake juu ya kifua changu, kisha alisema: “Ewe Mungu Wangu muongoe Shaybah.” Kisha aliupiga mara ya pili, kisha akasema tena: “Ewe Mungu wangu muongoe Shaybah.” Wallahi naapa hakuondoa mkono wake mara ya tatu kutoka juu ya kifua changu isipokuwa na mimi nilikuwa tayari sina kiumbe wa Mwenyezi Mungu nimpendaye zaidi kushinda yeye. - Amesema: Kaipokea Tabaraniy.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA ELIMU YA MTUKUFU MTUME (SAWW)

**Sahih Muslim: Kitabu cha fadhila, Mlango unaozungumzia jinsi anavyomjua Mwenyezi Mungu na kumhofu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha, amesema: Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alifanya kitu na kuruhusu jambo hilo kupitia kitendo chake. Habari hizo zikawafikia watu miongoni mwa Masahaba zake, na ni kama walichukia tendo hilo na wakajitakasa nalo. Habari hizo zikamfikia Mtume, ndipo akasimama na kutoa hotuba, alisema: “Wana nini watu ambao wamefikiwa na habari za jambo nililolitenda na kuruhusu jambo hilo lakini wao wamelichukia na kujitakasa nalo? Wallahi naapa hakika mimi namjua zaidi Mwenyezi Mungu kuwashinda wao na ninamhofu zaidi Mwenyezi Mungu kuwashinda wao.”

**Nasema:** Ameipokea pia Bukhari ndani ya *Sahih* yake[156] kwa tofauti kidogo katika baadhi ya maneno.

[154] *Usudul-Ghabah*: Herufi Mim, Wasifu wa Muslim bin Amru.
[155] *Maj’mauz-Zawa’id Waman’baul-Fawaid*: Mlango wa vita vya Hunayni.
[156] *Sahih Bukhari*, Juz. 5, Kitabu cha adabu, Mlango wa 72, Hadithi ya 575, Chapa ya Daru Ibn Kathir na al-Yamamah Beirut.

**Tabaqat Ibn Saad Juz. 1, Sehemu ya kwanza, Uk. 115[157]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas amesema: Kundi la Mayahudi siku moja lilifika kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kumwambia: "Ewe Abul-Qasim! Tusimulie kuhusu mambo ambayo tutakuuliza, hayajui mambo hayo isipokuwa Nabii." Akawaambia: "Niulizeni mtakalo, lakini kwa sharti kwamba mchukue dhima kwa Mwenyezi Mungu na ahadi aliyoichukua Ya'qub juu ya watoto wake, kuwa nikiwasimulia chochote kile na mkakitambua basi mtanipa kiapo cha utii kwa kuingia ndani ya Uislamu." Wakasema umekubaliwa sharti lako. Akasema: "Niulizeni mtakalo." Wakasema: "Tueleze kuhusu mambo manne tutakayokuuliza: Tueleze ni chakula gani ambacho Wana wa Israeli walijizuia kula kabla Taurat haijateremka? Na tueleze namna ya kutofautisha kati ya maji ya mwanamke na maji ya mwanaume? Na ni vipi mwanamume anapatikana kutokana na maji hayo na ni vipi mwanamke anapatikana kutokana na maji hayo? Na tueleze Nabii huyu asiyesoma anakuwaje usingizini? Na ni Malaika gani anayemsimamia?"

Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Kumbukeni mmechukua ahadi kwa Mwenyezi Mungu kuwa nikiwaeleza mtanipa kiapo cha utii." Basi wakaendelea kumpa ahadi kadiri walivyoweza. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Nawaapiza kwa ambaye aliteremsha Taurat kwa Musa. Je mnajua kwamba Israel Ya'qub aliugua ugonjwa mkali kwa muda mrefu ndipo akaweka nadhiri kwa Mwenyezi Mungu kuwa Mwenyezi Mungu akimponya atajizuia kunywa kinywaji akipendacho zaidi na kula chakula akipendacho zaidi, na chakula alichokuwa akikipenda zaidi ni nyama ya ngamia, na kinywaji alichokuwa akikipenda zaidi ni maziwa ya ngamia?" Wakasema: "Ndiyo ewe Mungu wetu." Mtume akasema: "Ewe Mungu Wangu kuwa shahidi juu yao."

Akasema: "Nawaapiza kwa ambaye hapana mungu isipokuwa Yeye ambaye aliteremsha Taurat kwa Musa. Je, mnajua kwamba maji ya mtoto mwanamume ni meupe mazito na maji ya mtoto mwanamke ni ya njano mepesi, na yale yanayokuwa juu (yanayoanza kutoka) kati ya maji hayo ndio hutengeneza mtoto na kutoa jinsia kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Ikiwa yataanza kutoka maji ya mtoto mwanamume kabla ya maji ya mtoto mwanamke, mtoto atakuwa wa kiume kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na ikiwa yataanza kutoka maji ya mtoto mwanamke kabla ya maji ya mtoto mwanamume, basi mtoto atakuwa wa kike kwa idhini ya Mwenyezi Mungu." Wakasema: "Ndiyo ewe Mungu wetu." Mtume akasema: "Ewe Mungu Wangu kuwa shahidi juu yao."

Akasema: "Nawaapiza kwa Mwenyezi Mungu ambaye aliteremsha Taurat kwa Musa. Je, mnajua kwamba Nabii huyu asiyesoma macho yake hulala lakini moyo wake huwa macho?" Wakasema: "Ndiyo ewe Mungu wetu." Mtume akasema: "Ewe Mungu Wangu kuwa shahidi juu yao." Wakasema: "Sasa hivi uko macho, hebu tueleze ni nani msimamizi wako miongoni mwa Malaika? Utakapotujibu ndipo tutajua je tukufuate au tusikufuate." Akasema: "Hakika msimamizi wangu ni Jibril, na hajaletwa Nabii yeyote kamwe isipokuwa Jibril ndiye msimamizi wake." Wakasema: "Kwa jibu hilo hatutakufuata, lau msimamizi wako angekuwa ni malaika mwingine tungekusadikisha." Akawauliza: "Ni kitu gani kinawazuia msimsadikishe?" Wakasema: "Yeye ni adui yetu." Ndipo Mwenyezi Mungu akateremsha: **"Sema: Aliyekuwa ni adui wa Jibril, basi huyo ndiye aliyeiteremsha Qur'ani moyoni mwako kwa idhini ya Mwenyezi Mungu inayo thibitisha yaliyokuwa kabla yake, na ni uwongofu na bishara njema kwa Waumini."** Mpaka: **"kama kwamba hawajui."** Waliposikia hivyo wakajiongezea ghadhabu juu ya ghadhabu.

[157] *Tabaqat Ibn Saad*: Kutaja alama za unabii baada ya wahyi kumteremkia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 8, uk. 263[158]:**

Amesema: Imepokewa kutoka kwa Ibn Umar kutoka kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuwa alisema: "Nimepewa funguo za kila kitu isipokuwa za mambo matano: **"Hakika kuijua Saa (ya Kiyama) kuko kwa Mwenyezi Mungu. Na Yeye ndiye anayeiteremsha mvua. Na anavijua viliomo ndani ya matumbo ya uzazi. Na haijui nafsi yoyote itachuma nini kesho. Wala nafsi yoyote haijui itafia nchi gani. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujua, Mwenye khabari."**[159]

Amesema: Ameipokea Ahmad na Tabaraniyy. Na wapokezi wa Ahmad ni wapokezi sahihi.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA BAADHI YA HABARI ZA GHAIB ZILIZOELEZWA NA MTUKUFU MTUME (SAWW)

Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: **"Yeye ndiye Mwenye kujua ya siri, wala hamdhihirishii yeyote siri yake. Isipo kuwa Mtume wake aliye mridhia. Naye huyo humwekea walinzi mbele yake na nyuma yake."**[160]

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 1, Uk. 353[161]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: Aliyemteka Abbas bin Abdul-MutTalib ni Abul-Yasri bin Amru naye ni Ka'b bin Amru ambaye ni mmoja kati ya watu wa Bani Salmah. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia: "Uliwezaje kumteka ewe Abul-Yasri?" Akasema: "Alinisaidia mtu mmoja ambaye sijapata kumuona mtu mwenye umbile kama yeye baada wala kabla yake." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Aliyekusaidia ni Malaika mwema." Kisha akamwambia Abbas: "Ewe Abbas jikomboe na mkomboe mtoto wa kaka yako Aqil bin Abu Talib na Nawfal bin al-Harith na rafiki yako wa yamini Ut'bah bin Jahdam mmoja kati ya watoto wa al-Harith bin Fahri." Abbas akakataa na kusema: "Hakika mimi nilikuwa mwislamu kabla ya hapo lakini walinilazimisha kutoka." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Mwenyezi Mungu ndiye mjuzi zaidi wa jambo lako, ikiwa unalodai ni haki basi Mwenyezi Mungu atakulipa kwalo, ama dhahiri ya mambo ni kuwa ulikuwa dhidi yetu, hivyo jikomboe."

Huko kabla Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa ameshachukua gramu ishirini za dhahabu kutoka kwake, hivyo Abbas akamwambia: "Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu! Zihesabu miongoni mwa fidia yangu." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Hapana, hicho ni kitu ambacho alitupa Mwenyezi Mungu kutoka kwako." Abbas akasema: "Hakika sina mali."Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Iko wapi mali uliyoiweka Makka kwa Ummul-Fadhli ulipokuwa unatoka tena mkiwa ninyi wawili tu, ukamwambia: 'Nikifa katika safari hii basi al-Fadhlu atapata kadha, Qutham atapata kadha na Abdullah atapata kadha?" Abbas akasema: "Naapa kwa yule aliyekuleta kwa haki hakuna mtu yeyote aliyejua hili isipokuwa mimi na yeye, na hakika mimi nimejua hakika wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu."

[158] *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid:* Mlango wa elimu aliyopewa (saww).
[159] Sura Luqman: 34
[160] Sura Jinni: 26 – 27.
[161] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Musnad Abdullah bin Abbas, Hadithi ya 3300.

**Mustadrakus-Sahihayni Juz. 3, uk. 246[162]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ali bin Isa an-Nawfal, amesema: Alipotekwa Nawfaliy bin al-Harith siku ya Badri, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia: "Jikomboe ewe Nawfal." Akasema: "Sina kitu cha kujikombolea ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu." Mtume akasema: "Jikomboe kwa mikuki yako iliyopo Jiddah." Akasema: "Wallahi baada ya Mwenyezi Mungu hakuna mwingine zaidi yangu aliyekuwa anajua kuwa nina mikuki huko Jiddah. Nashahidia hakika wewe niMtume wa Mwenyezi Mungu." Na hapo akajikomboa kupitia mikuki yake, na idadi yake ilikuwa ni mikuki elfu moja.

**Tabaqat Ibn Saad Juz. 1, Sehemu ya kwanza, Uk. 125[163]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa mzee mmoja wa Kikuraishi kwamba wakati Makuraishi walipoandikiana mkataba dhidi ya Bani Hashim pindi walipokataa kuwakabidhi Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), na walikuwa wameandikiana kuwa wasiowe kwao wala kuwaoza, wala wasinunue kwao wala kuwauzia, wala wasichanganyikane nao katika chochote wala wasiwasemeshe. Walikaa miaka mitatu wakiwa katika shamba lao wakiwa wote kwenye vikwazo isipokuwa wale watokanao na Abulahabi, wenyewe hawakuingia pamoja nao katika vikwazo. Miongoni mwa walioingia pamoja nao katika vikwazo ni watoto wa Abdul-Muttalib bin Abdi Manaf, hivyo ilipopita miaka mitatu, Mwenyezi Mungu alimjulisha Nabii wake kuhusu jambo lililotokea katika waraka wa mkataba wao, kwamba mchwa wamekula eneo lenye maneno ya dhulma na ujeuri na limebakia lile lenye kutaja jina la Mwenyezi Mungu. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimjulisha hilo Abu Talib, na Abu Talib akasema: "Ni kweli unayoniambia ewe mtoto wa ndugu yangu?" Akasema: Ndiyo Wallahi."

Abu Talib aliwajulisha hilo ndugu zake, nao wakamwambia: "Ni ipi dhana yako kwake? Akasema: "Kamwe hajawahi kunidanganya." Akasema: "Unaonaje kuhusu hilo?" Akasema: "Naona mvae nguo nzuri zaidi kati ya zile mlizonazo, kisha mtoke na kwenda kwa Makuraishi, tuwajulishe hilo kabla habari hazijawafikia." Wakatoka mpaka wakaingia msikitini na kupanda kwenye jiwe, walipomuona walinyanyuka na kumtazama atasema nini, Abu Talib akasema: "Hakika sisi tumekuja na jambo hivyo tunaomba jibu kwa lile tutakalowajulisha." Wakasema: "Karibuni sana, na sisi tunayo yenye kukufurahisha, una ombi gani?" Akasema: "Hakika mtoto wa kaka yangu amenipa habari –na kamwe hajawahi kunidanganya – kuwa Mwenyezi Mungu amewapeleka mchwa kwenye waraka wenu mlioandika, na umekula kila eneo lililokuwa na maelezo ya dhulma au ujeuri au ya kuvunja udugu, na limebakia lile lenye kutaja jina la Mwenyezi Mungu. Hivyo ikiwa mtoto wa kaka yangu ni mkweli itawapasa kuachana na rai yenu mbaya, na kama yeye ni muongo nitamkabidhi kwenu mumuuwe au mumsamehe mkitaka."

Wakasema: "Umetufanyia uungwana." Wakatuma waraka uletwe. Ulipoletwa Abu Talib akawataka wausome.Walipoufungua waliukuta ukiwa kama alivyosema Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), umeliwa wote isipokuwa lile eneo lenye kutaja jina la Mwenyezi Mungu. Watu wakapigwa na butwaa na kuinamisha vichwa vyao chini, Abu Talib akasema: "Je imewabainikia sasa kuwa ninyi ndio mnafaa zaidi kudhulumu, kuvunja udugu na kutenda ubaya?" Hakuna yeyote aliyemjibu bali Makuraishi wakaanza kulaumiana kwa yale waliyowatendea Bani Hashim. Hawakukaa muda mrefu, hivyo Abu Talib akarejea shambani huku akisema: "Enyi Makuraishi! Kwa sababu gani tutaendelea kuwekewa vikwazo na kubanwa wakati jambo limeshabainika?" Kisha aliingia yeye na jamaa zake katika shuka la Ka'ba na kusema: "Ewe Mungu Wangu tunusuru dhidi ya yule aliyetudhulumu, aliyevunja udugu wetu na kuhalalisha kutendewa yale yaliyo haramu sisi kutendewa." Kisha waliondoka.

[162] *Mustadrakus-Sahihayni*: Kitabu cha kuwatambua Masahaba, Kutaja fadhila za Nawfal bin al-Harith.
[163] *Tabaqat Ibn Saad*: Kutaja alama za unabii baada ya wahyi kumteremkia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

**Taarikh Baghdad Juz. 3, Uk. 167[164]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Zayd bin Arqam kuwa amesema: Kuna bedui alikuja kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa kafunga mifuko ya joho lake, akasema: “Muhammad ni yupi kati yenu?” Wakasema: “Mwenye uso wa kung’ara.” Akasema: “Kama kweli yeye ni Nabii, nimebeba nini?”Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: “Nikikueleza je utatoa shahada?” Akasema ndio, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: “Ulipita katika bonde la Aali fulani – au alisema: Shamba la Aali fulani – na uliona kiota cha njiwa pori kikiwa na vifaranga vyake viwili, ukachukua vifaranga vyake. Njiwa pori aliporudi katika kiota chake hakuviona vifaranga, hivyo aliruka porini kuchunguza na hakumuona yeyote zaidi yako, alirukaruka juu ya kichwa chako na wewe ukamfungulia mfuko wa joho lako naye akawa ameingia, hivyo huyo hapo amevikumbatia vifaranga vyake kwa mabawa yake.”

Bedui akafungua mfuko wa joho na kukuta kama alivyosema Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Masahaba wa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) walishangazwa sana na njiwa huyo na jinsi alivyovikumbatia vifaranga vyake. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: “Mnashangazwa na njiwa pori na jinsi alivyovikumbatia vifaranga vyake? Wallahi Mwenyezi Mungu ni mwenye furaha sana na ni mwenye kumwelekea mja wake muumini kushinda njiwa huyu anavyovikumbatia vifaranga vyake.

**Mirqatul-Mafatihi Juz. 5, Uk. 481[165]:**

Amesema: Imepokewa kutoka kwa Anas kuwa amesema: Tulikuwa pamoja na Umar baina ya Makka na Madina –Aliendelea kusimulia mpaka aliposema: Kisha Umar akaanza kutusimulia kuhusu watu wa Badri, alisema: “Hakika Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa akituonesha sehemu watakayofia watu wa Badri siku moja kabla, anasema: ‘Hapa atafia fulani kesho inshaallah, na hapa atafia fulani kesho inshaallah.’” Umar alisema: “Naapa kwa yule aliyemleta kwa haki, Wallahi hawakuvuka mipaka aliyoiainisha Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Na waliwekwa ndani ya kisima (kaburi) cha pamoja, kisha Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliwafuata na kuwaambia: “Ewe fulani mtoto wa fulani, ewe fulani mtoto wa fulani, je mmeyakuta ni kweli yale aliyokuahidini Mwenyezi Mungu na Mtume wake? Hakika mimi nimekuta ni kweli yale aliyoniahidi Mwenyezi Mungu.” Umar akasema: “Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu! Inakuwaje unaisemesha miili isiyokuwa na roho?” Akasema: “Ninyi si wenye kusikia zaidi kushinda wao yale ninayowaambia, isipokuwa tu ni kwamba wao hawawezi kunijibu kitu.” - Amesema: Kaipokea Muslim.

**Majmauz-Zawa’id ya al-Haythamiy Juz. 8 Uk. 284[166]:**

Amesema: Imepokewa kutoka kwa Muhammad bin Ja’far bin Zubair, amesema: Umair bin Wahbi al-Jamhiy na Swaf’wan bin Umaiyyah waliwekwa kizuizini kwa siku chache baada ya Makuraishi kuuwawa katika vita vya Badri. Umair bin Wahbi alikuwa ni shetani miongoni mwa mashetani wa Kikuraishi, kwani alikuwa ni mmoja kati ya watu waliokuwa wakimuudhi sanaMtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu na Masahaba zake, wote walipata shida za maudhi yake huko Makka. Wahbi bin Umair bin Wahbi alikuwa ni mmoja kati ya mateka wa vita vya Badri, hivyo siku moja walikumbushana vifo vya watu wa kisima cha Qalib (mushrikina waliouwawa katika vita vya Badri na kuzikwa katika kisima hicho), Swaf”wan akasema: “Wallahi hakuna kheri katika maisha baada yao.” Umair bin Wahbi akasema: “Wal-

[164] *Taarikh Baghdad*: Wasifu wa Muhammad bin al-Farkhan Abu Tayyib ad-Dawriy, Namba 1213.
[165] *Mir’qatul-Mafatihi*: Juz. 5, Uk. 481.
[166] *Maj’mauz-Zawaid Waman’baul-Fawaid*: Mlango unaozungumzia habari za ghaibu zilizotolewa na Mtukufu Mtume (saww)

lahi umesema ukweli, laiti ingekuwa si deni ninalodaiwa ambalo sina uwezo wa kulilipa, na si familia yangu ambayo nahofia itateseka baada yangu, ningepanda mnyama na kwenda kwa Muhammad mpaka nimuuwe kwani nina sababu kati yao, mwanangu yupo kwao mateka mikononi mwao."

Swaf'wan akachukua dhima ya kumtekelezea mahitaji yake, akasema: "Deni lako nitalibeba, nitakulipia mimi, na familia yako nitaitunza sawa na familia yangu muda wote wa maisha yao, sintawatunza wangu bila wa kwako." Umair akasema: "Nifichie siri hii, iwe ni mimi na wewe tu." Swaf'wan akamwambia: "Nitafanya hivyo." Kisha aliamrisha aletewe upanga wake akaunoa na kuupaka sumu kisha aliondoka kwenda Madina.Wakati Umar akiwa Madina katikati ya kundi la Waislamu wakikumbushana na kuhadithiana habari za siku ya Badri na jinsi Mwenyezi Mungu alivyowakirimu na alivyowatendea maadui zao, ghafla alimuona Umair bin Wahbi ameketi katika mlango wa msikiti huku kabeba upanga wake, Umar akasema: "Wallahi huyu ni yule mbwa Umair bin Wahbi na hakuja huku isipokuwa kwa shari, huyu ndiye aliyetuvuruga na kutuzuia tusiweze kuwamaliza jamaa siku ya Badri."

Umar aliingia kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kumwambia: "Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu! Huyu hapa Umair bin Wahbi amekuja akiwa kabeba upanga." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): "Nenda kamlete." Umar alikwenda akashika mkanda wa kubebea upanga aliokuwa ameuvaa shingoni, akamvuta na kumburuza kwa mkanda huo. Na aliwaambia baadhi ya watu miongoni mwa Ansari waliokuwa pamoja naye: "Nendeni kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mketi kwake na mchukue tahadhari kwa kumlinda dhidi ya mbwa huyu kwani haaminiki."

Kisha Umar alikwenda naye mpaka kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) huku akiwa kamkaba kwa mkanda wa kubebea upanga wake. Mtume akasema: "Mwachie ewe Umar. Sogea karibu na mimi ewe Umair." Aliposogea alimsalimu Mtume kwa maamkizi ya zama za kijahiliyya. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema:"Mwenyezi Mungu ametukirimu kwa kutupa maamkizi mazuri kushinda maamkizi yako ewe Umair, as-Salam ni maamkizi ya watu wa peponi."Umair akasema: "Wallahi kama kweli wewe Muhammad ni hadithi aliyoahidi."

Mtume akamuuliza: "Ni kitu gani kilichokuleta?" Akasema: "Nimekuja kwa ajili ya mateka huyu ambaye yumo mikononi mwenu, ili nijuwe thamani yake." Mtume akamwambia: "Vipi kuhusu upanga uliyopo shingoni mwako?" Akasema: "Mwenyezi Mungu auharibu kati ya panga zote, je umetusaidia kutenda chochote." Mtume akasema: "Niambie kweli umekuja kufanya nini?" Akasema: "Sikuja isipokuwa kwa ajili ya huyu." Mtume akasema: "Hapana, ulikaa wewe na Swaf'wan bin Umaiyyah kizuizini mkaanza kukumbushana vifo vya Makuraishi wa kisima cha Qalib, ukasema: 'Laiti isingekuwa ni deni ninalodaiwa na si kuhofia familia yangu kuteseka, ningetoka na kwenda kumuuwa Muhammad.' Ndipo Swaf'wan akabeba gharama za deni lako na za matumizi ya familia yako ili uje kuniuwa, lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyezuia baina yako na azma yako."

Umair akasema: "Nashahadia hakika wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Tulikuwa ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu tukikukadhibisha kwa zile habari za mbinguni unazotuletea na wahyi unaoteremshiwa, na hakika hakuwepo katika jambo hili yeyote isipokuwa mimi na Saf'wan.Wallahi natambua kwa yakini hakuna aliyekueleza haya isipokuwa Mwenyezi Mungu. Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu aliyeniongoa kwa kuniingiza katika Uislamu na akanipitisha katika njia hii." Kisha alitoa shahada ya kweli, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Mfundisheni ndugu yenu dini yake, msomesheni Qur'ani na mwacheni huru mateka wake." Kisha alisema: "Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), hakika mimi nilikuwa mwenye juhudi kubwa katika kuzuia nuru ya Mwenyezi Mungu, mwenye maudhi mengi kwa yule aliyekuwa katika dini ya Mwenyezi Mungu, na hakika napenda unipe ruhusa niende Makka nikawalinganie kwa Mwenyezi Mungu na kuwaita katika Uislamu huenda Mwenyezi Mungu atawaongoa, na niwaudhi kama nilivyokuwa nikiwaudhi Masahaba zako katika dini yao."

Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimruhusu akarudi Makka. wakati Umair bin Wahbi alipotoka kwenda Madina Swaf'wan aliwaambia Makuraishi: "Nawabashirieni tukio ambalo litakusahaulishieni machungu ya tukio la Badri." Na alikuwa akiulizia habari zake kupitia wasafiri, mpaka alipokuja msafiri mmoja ambaye alimpa habari za kusilimu kwake, hivyo Swaf'wan akaapa kwamba kamwe hatamsemesha na wala hatamsaidia chochote. Umair alipofika Makka aliishi humo na kuwaita watu katika Uislamu huku akiwaudhi sana wale wenye kumpinga, wakasilimu mikononi mwake watu wengi. - Amesema: Kaipokea Tabaraniy kwa kuvusha, na njia (sanadi) yake ni nzuri.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 8, uk. 287[167]:**

Amesema: Imepokewa kutoka kwa Abu Bakrah kuwa amesema: Alipoletwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Kisra alimtumia barua aliyekuwa Gavana wake katika nchi ya Yemen na miji ya Kiarabu inayoizunguka Yemen – alikuwa anaitwa Badam – kuwa: Zimenifikia habari kuwa amejitokeza mtu upande wako ambaye anadai kuwa yeye ni Nabii, mwambie aache kabisa jambo hilo la sivyo nitamtumia mtu atakayemuuwa au kuwauwa jamaa zake. Alifika mjumbe wa Badam kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), na kumweleza hayo. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Ingekuwa ni kitu nilichokifanya mwenyewe basi ningeacha, lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu amenituma." Mtume akampokea mjumbe kwake, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Hakika Mola Wangu amemuua Kisra na hakuna tena Kisra baada ya leo. Na amemuuwa Kaisari na hakuna Kaisari baada ya leo." Mjumbe yule aliandika saa, siku na mwezi ambao Mtume alimpa habari hizo, kisha alirejea kwa Badam na kumkuta Kisra amefariki na Kaisar ameuawa. - Amesema: Ameipokea Tabaraniy, na wapokezi wake ni wapokezi sahihi.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 8 Uk. 288[168]:**

Amesema: Kutoka kwa Kharim bin Awsi amesema: Nilimsikia Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: Hii hapa Hira nyeupe nimepewa, na huyu hapa Shamau binti Baqilah al-Azdiyyah akiwa juu ya nyumbu wa kijivu amejifunika mtandio mweusi." Nikasema: "Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu! Tutakapoingia Hira na kumkuta akiwa katika sifa hii basi atakuwa wangu." Mtume akasema: "Ni wa kwako." Kisha Waarabu waliritadi lakini hakuna yeyote wa kutoka Tway'u aliyeritadi, hivyo tulikuwa tukiwapiga vita watu wa kabila la Qaysu ili waingie katika Uislamu, na miongoni mwao ni Ut'bah bin Haswinu. –Aliendelea kusimulia hadi aliposema: Kisha Khalid bin Walid alikwenda Musaylamah, tulikwenda pamoja naye, tulipomalizana na Musaylamah na jamaa zake tulikwenda upande wa Basra tukakutana na Harmuzu huko Kadhimah akiwa na kundi kubwa – na hakuna mtu aliyekuwa na uadui na Waarabu kumshinda Harmuzu -

IbnWalid alibarizi kupambana naye na akamtaka wapambane, Harmuzu alipambana na mwishowe Khalid akamuuwa. Yalipothaminishwa mavazi yake, kofia yake ilifikia thamani ya dirhamu elfu moja. Kisha tulikwenda kwa kufuata njia ya Twaf (Karbala) mpaka tukaingia Hira, mtu wa kwanza kabisa kukutana naye humo ni Shamau binti Baqilah al-Azdiyyah akiwa juu ya nyumbu wa kijivu amejifunika mtandio mweusi. Nikamng'ang'ania na kusema: "Huyu ni zawadi yangu ambayo Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alinizawadia." Khalid akanitaka nitoe ushahidi kisharia, nikatoa ushahidi, na yeye akamsalimisha kwangu. Alikuja kaka yake Abdul-Masihi na kuniambia: "Niuzie mateka huyu." Nikamwambia: "Wallahi si chini ya dirhamu elfu moja." Akanipa dirhamu elfu moja. Nikaambiwa: Hata

[167] *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid*: Mlango unaozungumzia habari za ghaibu zilizotolewa na Mtukufu Mtume (saww)
[168] *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid*: Mlango unaozungumzia habari za ghaibu zilizotolewa na Mtukufu Mtume (saww)

kama ungesema dirhamu laki moja angekupa, nikasema: Sina uwezo wa kuhisabu mali iliyo zaidi ya elfu moja. – Amesema: Ameipokea Tabaraniy.

**Sunanud-Daramiy Juz. 1, Uk. 33[169]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir bin Abdullah kwamba Yahudi mmoja wa kike miongoni mwa Mayahudi wa Khaibari aliweka sumu ndani ya nyama ya mbuzi kisha akampa Mtume zawadi nyama hiyo, Mtume akachukua sehemu ya mkono, akala kidogo na wakala kidogo wote waliokuwa pamoja naye, kisha Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawaambia: "Acheni kula." Kisha Mtume akatuma wamwite mwanamke yule wa Kiyahudi, alipokuja akamwambia: "Je uliweka sumu ndani ya mbuzi huyu?" Akasema: "Ndiyo, nani kakwambia?" Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Mkono huu wa mbuzi uliyomo mikononi mwangu ndio ulioniambia." Akasema: "Ndiyo." Mtume akamuuliza: "Ulikusudia nini kwa kitendo hicho?" Akasema: "Nilisema ikiwa kweli ni Nabii haitamdhuru, na kama si Nabii tutakuwa tumepumzika na yeye." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamsamehe bila kumwadhibu.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA UPASUAJI WA KIFUA CHA MTUKUFU MTUME (SAWW)

**Musnad Ahmad bin Hanbal Juz. 5, Uk. 139:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ubaiyyah bin Ka'b kuwa alisema: Hakika Abu Huraira alikuwa na ujasiri wa kuweza kumuuliza Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mambo ambayo mtu mwingine hawezi, hivyo alisema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ni jambo gani la kwanza kabisa uliloliona katika suala la unabii?" Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alijiweka sawa akiwa ameketi chini kisha akasema: "Umeuliza ewe Abu Huraira, hakika mimi nilikuwa jangwani nikiwa mtoto wa miaka kumi na miezi kadhaa, ghafla nikasikia maneno yakitoka juu ya kichwa changu, nikamsikia mtu akimwambia mtu mwingine: 'Ndiyo mwenyewe?' Yule mwingine akajibu: 'Ndiyo.'

"Walinielekea kwa nyuso ambazo sijapata kamwe kuziona kwa viumbe na kwa roho ambazo kamwe sijawahi kuziona kwa viumbe, na kwa nguo ambazo kamwe sijawahi kuziona kwa yeyote. Walikuja kwangu huku wakitembea mpaka kila mmoja akanishika sehemu ya juu ya mkono bila kuhisi mguso wa yeyote kati yao, mmoja akamwambia mwenzake: 'Mlaze.' Akanilaza bila mkeka wala mrago, mmoja akamwambia mwenzake: 'Pasua kifua chake.' Mmoja akaja sehemu ya kifua changu akakipasua huku naona, bila damu wala maumivu. Akamwambia: 'Toa chuki na hasadi.' Akatoa kitu kama kipande cha damu kisha akakitupa. Akamwambia: 'Ingiza mapenzi na huruma.' Akaingiza kitu kama alichotoa kikiwa kama madini ya fedha. Kisha alitikisa kidole gumba cha mguu wangu wa kulia na kusema: 'Nenda salama.' Nikarejea nikiwa ni mwenye upendo kwa mdogo na mwenye huruma kwa mkubwa."

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 305[170]:**

Amesema: Kutoka kwa Shadad bin Awsi, amesema: Wakati tukiwa tumeketi kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ghafla alikuja mtu kutoka kwa Bani Aamir – Naye alikuwa ndio bwana wao,

[169] *Sunanud-Daeamiy:* Mlango unaozungumzia yale ambayo Mtukufu Mtume amekirimiwa ikiwa ni pamoja na kuongea na wafu, Hadithi ya 68.
[170] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha fadhila za Mtukufu Mtume (saww), Jumuisho la dalili na alama za unabii, Hadithi ya 35559.

mkubwa wao na kiongozi wao - alikuja huku akitembelea mkongojo wake, akasimama mbele ya Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kumnasibisha Mtume mpaka kwa babu yake, kisha akasema: "Ewe mtoto wa Abdul-Muttalib, hakika nimeambiwa kuwa wewe wadai ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa watu. Amekutuma na yale aliyowatuma nayo Ibrahim, Musa, Isa na Manabii wengine, na hakika wewe umetamka mambo makubwa, kwani hakika Manabii na wafalme walikuwa wakitokana na nyumba mbili za Bani Israil, nyumba ya unabii na nyumba ya ufalme, na wewe hautokani na nyumba yoyote kati ya hizo mbili, si katika hii wala si katika ile, bali wewe ni Mwaarabu, wapi wewe na unabii? Lakini kila kitu kina ukweli wake, hivyo niambie ukweli wa kauli yako na jambo lako."

Mtume alistaajabishwa sana na swali lake, kisha alisema: "Ewe ndugu wa watoto wa Aamir! Hakika jambo ulilouliza lina habari na baraza hivyo kwanza keti chini." Akakunja miguu yake na kupiga magoti kama ngamia. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Ewe ndugu wa watoto wa Aamir! Hakika ukweli wa kauli yangu na mwanzo wa jambo langu ni maombi ya baba yangu Ibrahim na ubashiri wa ndugu yangu Isa bin Mariam."

**Nasema:** Ameitaja hadithi hii kwa njia nyingine. Katika njia hiyo amesema: Mtu yule wa Bani Aamir alikaa mbele ya Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Hakika mzazi wangu alipomuoa mama yangu alishika mimba; mama akaona usingizini kuwa nuru imetoka tumboni mwake, akawa anafuata kwa kuitazama mpaka eneo lote la baina ya mbingu na ardhi likajaa nuru. Alimsimulia hayo mzee mmoja mwenye busara kati ya watu wa familia yake, mzee yule akamwambia: 'Wallahi kama ndoto yako ni kweli basi atatoka tumboni mwako kijana ambaye utajo wake utaenea baina ya mbingu na ardhi.' Na walikuwa watu wa mtaa huu wa Bani Saad bin Hawzaniwana ada ya kuwachukua wanawake wa Makka ili wawanyonyeshe watoto wao na wao wanufaike na kheri zao, na hakika mama yangu alinizaa katika mwaka ambao wanawake hawa walikuja katika mtaa huo, na tayari mzazi wangu alikuwa keshakufa nimebaki yatima chini ya ulezi wa ami yangu Abu Talib, hivyo wanawake walikuwa wakinikataa wakisema: 'Mtoto mdogo asiye na baba nadhani hatutaweza kupata kheri yoyote kupitia kwake.

"Kati yao alikuwemo mwanamke aliyekuwa akiitwa mama Kabshah binti ya Harith, akasema: 'Wallahi mwaka huu kamwe siondoki mikono mitupu, akanichukua na kuniweka juu ya kifua chake, maziwa yakajaa na akaninyonyesha. Alipopata habari hizo, ami yangu Abu Talib alimpa ngamia na nguo na mavazi, na hakubakia ami yangu yeyote isipokuwa alimpa nguo na mavazi. Zilipowafikia habari hizo wale wanawake walimfuata na kumwambia: 'Wallahi mama Kabshah lau tungejua baraka za mtoto huyu zitakuwa hivi basi usingemchukua kabla yetu.' Kisha nililelewa na kukua ili hali nimefunzwa kuyachukia masanamu ya Makuraishi na ya Waarabu, siyakaribii wala kuyasogelea."

**Nasema:** Katika njia ya kwanza ambayo tumeitaja mwanzo, amesimulia hilo kwa lafudhi hii:"Nilipokua nilifunzwa kuyachukia masanamu na kuyachukia mashairi. Nilinyonyeshwa kwa Bani Jashmi bin Bakri, hivyo wakati mmoja nikiwa katikati ya bonde pamoja na watoto wa rika langu, ghafla niliona kundi la watu watatu likiwa na bakuli la dhahabu lililojaa maji, wakanichukua baina ya marafiki zangu, na rafiki zangu wakakimbia mpaka wakafika ukingoni mwa bonde. Kisha wakalielekea lile kundi la watu watatu na kuwaambia: 'Mnataka nini kwa kijana huyu? Huyu kijana ni mgeni, ni mtoto wa bwana mmoja wa Kikuraishi, amekuja kunyonyeshwa tu baina yetu ni kijana yatima asiye na baba, basi ni kwa nini mnataka kumuuwa? Na kama ni lazima kuuwa basi mchagueni yeyote mumtakaye kati yetu atakuja na mtamuuwa badala yake, mwacheni kijana huyu.' Lakini hawakuwajibu kitu.Watoto wale walipoona kuwa jamaa hawawajibu waliondoka haraka wakikimbia kwenda katika mtaa ule huku wakitangaza na kupiga kelele.

"Mmoja alinikamata na kunilaza ardhini taratibu, kisha alipasua eneo la baina ya kifua na maoteo ya nywele za chini ya kitofu, huku nikimtazama bila kuhisi mguso. Kisha alitoa vitu vya tumboni mwangu

akaviosha kwa maji yale taratibu kisha alipomaliza akavirudisha sehemu yake. Kisha alisimama wa pili akamwambia rafiki yake: 'Sogea.' Kisha aliingiza mkono wake tumboni mwangu na kutoa moyo wangu huku nikitizama. Akaugonga na kutoa kijinyama cheusi na akakitupa, kisha alinyoosha mkono wake kama vile anakula chakula. Nikaona pete mkononi mwake ikitoa nuru kali yenye kuumiza macho ya wengine wasiokuwa yeye. Akaipiga kama muhuri juu ya moyo wangu, ndipo moyo wangu ukajaa nuru na hekima, kisha aliurudisha sehemu yake. Daima wakati wote naupata ubaridi wa pete ile.

"Kisha alisimama wa tatu akamuondoa rafiki yake, akapitisha mkono wake baina ya chuchu zangu na mwisho wa shingo langu, kisha kwa idhini ya Mwenyezi Mungu mpasuo ule ukajiunga. Kisha alinishika mkono akaninyanyua polepole kutoka nilipokuwa, akasema yule wa kwanza aliyepasua tumbo langu: 'Mpimeni na watu kumi wa ummah wake.' Wakanipima nikawashinda. Kisha akasema:'Mpimeni na watu mia moja wa ummah wake.' Wakanipima nikawashinda. Kisha akasema: 'Mpimeni na watu elfu moja wa ummah wake.' Wakanipima nikawashinda. Kisha akasema: 'Mwacheni hata mkimpima na ummah wake wote atawashinda.' Kisha walisimama na kunikumbatia vifuani mwao, wakabusu kichwa changu na baina ya macho yangu, kisha wakasema: 'Ewe hababi lau ungejua kheri inayokusudiwa kwako macho yako yangefurahi.' Wakati tukiwa hivyo ghafla walitokeza watu wa mtaani wakiwa wamejiandaa kwa vita huku mlezi wangu akiwa mbele ya kundi la watu wa mtaani akinadi kwa sauti ya juu kabisa: 'Ewe dhaifu.' Ndipo wakanikumbatia."

**Nasema:** Yaani Malaika ambao walipasua baina ya kifua chake na maoteo ya nywele za chini ya kitofu chake: "Walinikumbatia na kunibusu huku wakisema: 'Wewe si dhaifu.' Mlezi wangu aliposema: 'Ewe mpweke!' walinishika na kunikumbatia katika vifua vyao na kusema: 'Wewe si mpweke, hujaachwa peke yako, Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wewe na pia Malaika wake na waumini miongoni mwa wakazi wa ardhini wako pamoja na wewe.' Mzazi wangu aliposema: 'Ewe yatima ambaye umekuwa mnyonge baina ya marafiki zako na hivyo umeuwawa kwa sababu ya unyonge wako.' Walinikumbatia katika vifua vyao na wakabusu kichwa changu na kusema: 'Wewe si yatima una heshima kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu laiti ungekuwa unajua kheri iliyokusudiwa kwako.' Na mara wakawa wamefika pembezoni mwa bonde, mlezi wangu aliponiona alisema: 'Ewe mwanangu! Ungali hai?' Alikuja akanishika na kunikumbatia kifuani kwake. Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu imo mikono Mwake mimi nilikuwa mapajani mwake amenikumbatia huku mkono wangu ukiwa mkononi mwa mmoja wao (kati ya watu wale watatu). Nilidhani kuwa jamaa wanawaona kumbe walikuwa hawawaoni.

"Alikuja mtu mmoja kati ya watu wa mtaani akasema: 'Kijana huyu kapatwa na majini, hivyo twende naye kwa kuhani amtazamie na kumpa dawa.' Nikamwambia: Mimi sina chochote kati ya hayo uliyosema, hakika mimi nina nafsi salama na kifua salama na wala sina wendawazimu.' Baba yangu mume wa mlezi wangu akasema: 'Hivi hamuoni maneno yake yangali sahihi? Nadhani mwanangu hana tatizo lolote.' Lakini mwisho jamaa wakaafikiana kuwa wanipeleke kwa kuhani, wakanibeba na kunipeleka kwake, walipomsimulia kisa changu alisema: 'Nyamazeni nimsikie kijana mwenyewe kwani yeye ajua zaidi jambo lake.' Nikamsimulia jambo langu mwanzo wake mpaka mwisho wake, aliposikia niliyosema alinikumbatia kifuani kwake na kunadi kwa sauti yake ya juu kabisa: 'Enyi Waarabu! Muuweni kijana huyu na niuweni pamoja naye. Naapa kwa Lata na Uzza kama mtamuacha atakuja kubadili dini yenu, atadharau mawazo yenu na mawazo ya wahenga wenu, atapinga jambo lenu na atawaletea dini ambayo hamjawahi kusikia mfano wake.'

"Ndipo mzazi wangu akanichukua toka mikononi mwake na kumwambia: 'Wewe ni mwendawazimu zaidi na umepandwa na jini zaidi kuliko yeye, na laiti ningejua kuwa utasema hivi nisingemleta kwako.' Kisha alinibeba na kunirudisha kwa ndugu zangu, nikapatwa na huzuni kutokana na yaliyonipata, na

athari ya mpasuko uliyopo baina ya kifua changu na mwisho wa nywele za chini ya kitofu ukawa kama kamba za mtego, huu ndio ukweli wa kauli yangu na mwanzo wa jambo langu."

Mzee yule akasema: "Nashahidia kwamba hapana mungu isipokuwa Allah, na kwamba hakika Muhammad ni Mtume wa Allah, na kwamba hakika jambo lako ni haki. Naomba unipe habari za mambo ambayo nitakuuliza." Mtume akamwambia: "Uliza kuhusu wewe." Na alikuwa anapenda kuwaambia waulizaji kabla hawajauliza: "Uliza utakalo." Lakini siku hiyo alimwambia mzee wa Bani Aamir: "Uliza kuhusu wewe." Ni kwakuwa ndio lugha iliyokuwa ikitumika kwa Bani Aamir hivyo akamsemesha kwa lugha aijuayo. Mzee akasema: "Nieleze ewe mtoto wa Abdul-Muttalib, ni kitu gani huongeza shari?" Akasema: "Ni ujeuri." Akauliza: "Je kutenda wema kuna manufaa yoyote baada ya kufanya maovu." Akasema: "Ndiyo, hakika toba hufuta madhambi na hakika mazuri hufuta mabaya, mja akimtaja Mola Wake wakati wa raha na Yeye humsaidia wakati wa balaa."

Mzee yule wa Bani Aamir akasema: "Ni vipi linatokea hilo ewe mtoto wa Abdul-Muttalib?" Akasema: "Hiyo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu anasema: 'Kamwe simkusanyii mja amani mbili pamoja, wala kamwe simkusanyii hofu mbili pamoja. Ikiwa atasalimika Nami duniani basi atanihofu siku ambayo nitawakusanya pamoja viumbe Wangu, na kama atanihofu duniani basi nitamsalimisha siku ambayo nitawakusanya pamoja viumbe wangu katika hadhara tukufu. Amani yake itadumu na wala sintamuweka pamoja na nitakaowaadhibu.'"

Mzee wa Bani Aamir akasema: "Ewe mtoto wa Abdul-Muttalib! Unatuita katika jambo gani?" Akasema: "Nawaita katika ibada ya kumwabudu Mwenyezi MunguMmoja asiye na mshirika, na kuyatupilia mbali masanamu na kuyakufuru masanamu ya Lata na Uzza, na kuamini yale yaliyokuja kutoka kwa Mwenyezi Mungu kupitia Kitabu na Mtume wake, kusali Swala tano kama zilivyo, kufunga mwezi mmoja katika mwaka mzima, kutoa Zaka ya mali yako ili Mwenyezi Mungu akutakase kwayo na akuhalalishie mali yako, kuhiji Nyumba ya Allah utakapopata uwezo, kuoga janaba, kuamini kuwa kuna ufufuo baada ya kifo, na kuna pepo na moto." Akasema: "Ewe mtoto wa Abdul-Muttalib: Nikifanya haya nitapata nini?" Mtume akasema: **"Bustani za milele zipitazo mito kati yake, wadumu humo. Na hayo ni malipo ya mwenye kujitakasa."** Akasema: "Ewe mtoto wa Abdul-Muttalib pamoja na haya je kuna kitu kingine naweza kupata duniani kwani tunapenda wepesi katika maisha?" Mtume akasema: "Ndiyo, ushindi na nguvu katika nchi." Mzee yule wa Kibani Aamir akamkubalia na akatubu. – Amesema: Ameiandika Abu Ya'ala, Abu Naiim na Ibn Asakir.

**Nasema:** Katika mlango wa Mtume kwenda miraji itakuja hadithi kutoka katika *Sahih Muslim* ambayo nayo ina maelezo ya Jibril kumpasua kifua Mtukufu Mtume, ngojea.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA MWANZO WA KUSHUKA WAHYI KWA MTUKUFU MTUME (SAWW) NA JINSI ULIVYOSHUKA

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 8, uk. 255[171]:**

Amesema: Kutoka kwa Ibn Abbas, amesema kwamba Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Khadija:"Hakika mimi naona mwanga na ninasikia sauti, na ninahofu kuwa nisiwe nina jini." Khadija akasema: "Mwenyezi Mungu hawezi kukufanyia hivyo ewe mtoto wa Abdullah." Kisha alikwenda kwa Waraqah bin Nawfal na kumwelezea hayo, akasema: "Ikiwa ni mkweli basi huyu ni

[171] *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid:* Mlango unaozungumzia kutumwa kwake Mtukufu Mtume (saww) na kuteremshiwa kwake wahyi.

Malaika wa wahyi mfano wa Malaika wa wahyi wa Musa (as), na kama atakabidhiwa unabii ningali hai basi nitamuunga mkono, nitamnusuru na nitamwamini.

- Amesema: Ameipokea Ahmad kwa njia ya sanadi ya kuungana na ya kuvusha, na pia Tabaraniy kapokea kama hivyo lakini ameongeza: "Na nitamsaidia." Na wapokezi wa Ahmad ni wapokezi sahihi.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 8, uk. 256[172]:**

Amesema: Kutoka kwa Khadija amesema: Nilimwambia: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ewe mtoto wa ami yangu, je unaweza kunipa habari ya kuja kwake pindi atakapokujia yule anayekujia? Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Ndio ewe Khadija.' Siku moja Jibril akamjia na mimi nikiwa pamoja naye, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Ewe Khadija, huyu hapa rafiki yangu ambaye hunijia, amekuja.' Nikamwambia: Simama na uketi kwenye paja langu la kulia, je unamuona? Akasema: 'Ndiyo.' Nikamwambia: Hama na keti kwenye paja langu la kushoto, akahama na kuketi, nikamuuliza je unamuona? Akasema: 'Ndiyo.' Nikamwambia hama na uketi mapajani mwangu, akaketi, nikamwambia: Je unamuona? Akasema: 'Ndiyo.' Basi nikavuamtandio wangu na kuutupa, nikamuuliza je unamuona? akasema: 'Hapana.' Nikamwambia Wallahi huyu ni Malaika mtakatifu, Wallahi huyu si shetani. Nikamwambia Waraqah bin Nawfal bin Asad bin Abdul-Uzza bin Quswayy yale aliyonieleza Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Waraqah akasema: 'Ni kweli kakuhadithia ewe Khadija?'"
- Amesema: Ameipokea Tabaraniy ndani ya kitabu al-Awsat, na njia yake ni nzuri.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 8, uk. 256[173]:**

Amesema: Kutoka kwa Waraqah al-Ansariy amesema: Nilimwambia: Ewe Muhammad nieleze jinsi anavyokujia huyo mwenye kukujia – yaani Jibril - Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Hunijia kutoka mbinguni, mbawa zake zang'ara kama lulu na chini ya nyayo zake kuna rangi ya kijani." - Amesema: Ameipokea Tabaraniy ndani ya kitabu *al-Kabir* na *al-Awsat.*

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 8, uk. 256[174]:**

Amesema: Kutoka kwa Abdullah bin Umar amesema: "Nilimuuliza Mtukufu Mtume (saww), nikamwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Je unahisi wahyi?" Akasema: "Ndiyo, nasikia sauti kisha huwa ninakaa kimya. Kila mara anaponijia hudhani kuwa roho yangu inatolewa." - Amesema: Kaipokea Ahmad na Tabaraniy, na njia yake ni nzuri.

**Nasema:** Pia Bukhari kapokea ndani ya *Sahih* yake riwaya inayokaribiana na hiyo. Ameipokea katika mlango wa kwanza wa kitabu chake, nao ni mlango wa jinsi gani wahyi ulianza kuteremka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

[172] *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid*: Mlango unaozungumzia kutumwa kwake Mtukufu Mtume (saww) na kuteremshiwa kwake wahyi.

[173] *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid:* Mlango unaozungumzia kutumwa kwake Mtukufu Mtume (saww) na kuteremshiwa kwake wahyi.

[174] *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid*: Mlango unaozungumzia kutumwa kwake Mtukufu Mtume (saww) na kuteremshiwa kwake wahyi.

# MLANGO UNAOZUNGUMZIA MIRAJI YA MTUME (SAWW)

**Sahih Muslim: Kitabu cha imani, Mlango unaozungumzia Mtume wa Mwenyezi Mungu kupelekwa Palestina:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik, amesema: Abu Dhari alikuwa akisimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Dari la nyumba yangu lilipasuliwa nami nikiwa huko Makka, akateremka Jibril na kupasua kifua changu, kisha alikiosha kwa maji ya zamzam, kisha alikuja na bakuli la dhahabu likiwa limejaa hekima na imani na kumiminia lote ndani ya kifua changu, kisha alikishona na kunishika mkono na kupaa na mimi mpaka mbingu ya dunia. Tulipofika mbingu ya dunia Jibril alimwambia mlinzi wa mbingu ya dunia: 'Fungua.' Akauliza wewe ni nani? Akasema: 'Mimi ni Jibril.' Akauliza je uko pamoja na yeyote? Akasema: 'Ndiyo, niko pamoja na Muhammad (saww).' Akasema je amepewa utume? Akasema: 'Ndiyo.' Akafungua.

"Tulipofika juu kabisa ya mbingu ya dunia ghafla nilimuona mtu, kushotoni kwake kuna watu na kuliani kwake kuna watu, akitazama upande wa kuliani kwake anacheka, akitazama upande wa kushotoni kwake analia, akaniambia: 'Karibu ewe Nabii mwema na mtoto mwema.' Nikamwambia Jibril: Ewe Jibril, huyu ni nani? Akasema: 'Huyu ni Adam na hawa waliyopo kuliani kwake na kushotoni kwake ni roho za watoto wake, waliopo kuliani ndio watu wa peponi na waliopo kushotoni ndio watu wa motoni. Hivyo anapotazama upande wa kuliani kwake anacheka, na akitazama upande wa kushotoni kwake analia.' Kisha Jibril alipaa na mimi mpaka tukafika mbingu ya mbali, akamwambia mlinzi wake: 'Fungua.' Mlinzi akamjibu kama alivyojibu yule wa mbingu ya dunia, kisha alifungua."

Anas bin Malik amesema: Akaeleza kuwa huko mbinguni alimkuta Adam, Idirisa, Isa, Musa na Ibrahim, swala za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao wote. Haijathibiti vyeo vyao viko vipi lakini alichoeleza ni kuwa alimkuta Adam katika mbingu ya dunia, na Ibrahim katika mbingu ya sita. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na Jibril walipofika kwa Idirisa (as) alisema: "Karibu ewe Nabii mwema na ndugu mwema." Mtume alisema: Tukapita, nikamwambia: Huyu ni nani? Akasema: 'Huyu ni Idirisa.' Kisha tulipita kwa Musa, akasema: 'Karibu ewe Nabii mwema na ndugu mwema.' Nikamwambia: Huyu ni nani? Akasema: 'Huyu ni Musa.' Kisha tulipita kwa Isa, akasema: ''Karibu ewe Nabii mwema na ndugu mwema.' Nikamwambia: Huyu ni nani? Akasema: 'Huyu ni Isa bin Mariam.' Kisha tulipita kwa Ibrahim, akasema: ''Karibu ewe Nabii mwema na mtoto mwema.' Nikamwambia: Huyu ni nani? Akasema: 'Huyu ni Ibrahim.'"

Ibn Shihab amesema: Amenipa habari Ibn Hazmi kuwa Ibn Abbas na Abu Hubbah al-Ansariy walikuwa wakisema kuwa: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Kisha alipaa na mimi mpaka katika usawa ambao niliweza kusikia sauti za kalamu."

Ibn Hazmi na Anas bin Malik wamesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Mwenyezi Mungu akafaradhisha juu ya ummah wangu Swala hamsini, nikarejea nikiwa na faradhi hiyo mpaka nilipofika kwa Musa (as), Musa akaniambia: 'Amekufaradhishia nini juu ya ummah wako?' Nikamwambia amewafaradhishia Swala hamsini, Musa akaniambia: 'Rudi kwa Mola Wako ukaombe takhfifu, kwani hakika ummah wako hautaweza hilo.' Nikarejea kwa Mola Wangu na ndipo akanifaradhishia nusu yake. Nikarudi tena kwa Musa na kumweleza, akaniambia: Rudi kwa Mola Wako ukaombe takhfifu, kwani hakika ummah wako hautaweza hilo.' Nikarejea kwa Mola Wangu na ndipo akaniambia ni:"Swala tano na haibadilishwi kauli Yangu." Nikarudi tena kwa Musa na kumweleza, akaniambia: 'Rudi kwa Mola

Wako ukaombe takhfifu.' Nikamwambia: Namuonea haya Mola Wangu. Kisha Jibril alinichukua mpaka tukafika penye mkunazi wa mwisho ukiwa umefunikwa na rangi ambazo sizijui. Kisha niliingizwa peponi na kukuta dari ya lulu na udongo wa miski."

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, uk. 192[175]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alitetewa buraku katika usiku ambao alipelekwa Miraji. Buraku huyo aliyekuwa kafungwa lijamu na kitanda, aligoma kupandwa na Mtume, Jibril akamwambia: "Hivi unamfanyia haya Muhammad? Hajakupanda yeyote aliye mbora mbele ya Mwenyezi Mungu kumshinda yeye."

**Sahih an-Nasaiy Juz. 1, uk. 77:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Nililetewa mnyama ambaye umbo lake ni kubwa zaidi ya punda na ni dogo kuliko nyumbu, hatua yake ni mwisho wa upeo wa macho yake, nikampanda nikiwa pamoja na Jibril. Tulikwenda mpaka aliponiambia teremka uswali. Nikateremka na kuswali, akaniambia: 'Unajua umeswalia wapi? Umeswalia Twiba (Madina), na utahamia hapo.' Kisha akaniambia tena teremka na uswali, nikaswali, akaniambia: 'Unajua umesalia wapi? Umeswalia katika mlima Sinai sehemu ambapo Mwenyezi Mungu aliongea na Musa (as).' Kisha akaniambia tena teremka na uswali, nikaswali, akaniambia: 'Unajua umeswalia wapi? Umeswalia Bethlehemu sehemu ambapo alizaliwa Isa (as).'

"Kisha niliingia Baytul-Maqdas akanikusanyia Manabii (as) na kunitanguliza niwe Imamu wao. Kisha alinipaisha mpaka mbingu ya dunia na hapo nikamkuta Adam (as), kisha alinipandisha mpaka mbingu ya pili, hapo nikawakuta watoto wa mama yangu mdogo Isa na Yahya (as), kisha alinipandisha hadi mbingu ya tatu, hapo nikamkuta Yusuf (as), kisha alinipandisha hadi mbingu ya nne, hapo nikamkuta Harun (as), kisha alinipandisha hadi mbingu ya tano, hapo nikamkuta Idirisa (as), kisha alinipandisha hadi mbingu ya sita, hapo nikamkuta Musa (as), kisha alinipandisha hadi mbingu ya saba, hapo nikamkuta Ibrahim (as), kisha alinipandisha juu zaidi ya mbingu saba mpaka tukafika penye mkunazi wa mwisho, hapo nikashikwa na baridi, nikaporomoka na kusujudu. Nikaambiwa: 'Hakika siku nilipoumba mbingu na ardhi nilifaradhisha juu yako na juu ya ummah wako Swala hamsini, hivyo zitekeleze wewe na ummah wako.'

"Nikarejea, nilipofika kwa Ibrahim hakuniuliza kitu, nilipofika kwa Musa akasema: 'Umefaradhishiwa Swala ngapi wewe na ummah wako?' Nikamwambia hamsini, akasema: 'Hakika hutaweza kuzitekeleza, si wewe wala si ummah wako. Rejea kwa Mola Wako na umuombe akupunguzie.' Nikarejea hadi kwa Mola Wangu akanipunguzia Swala kumi.' Kisha nikaja kwa Musa, akaniamuru nirejee tena, nikarejea na kupunguziwa tena kumi. Kisha mwishoni zilipunguzwa hadi kufika Swala tano, Musa akasema: 'Rejea kwa Mola wako umuombe akapunguzie kwani hakika alifaradhisha juu ya Wana wa Israil Swala mbili tu lakini hawakuweza kuzitekeleza.' Nikarejea kwa Mola Wangu nikamuomba apunguze, akasema: 'Hakika siku niliyoumba mbingu na ardhi nilifaradhisha juu yako na juu ya ummah wako Swala hamsini, hivyo sasa zimekuwa tano badala ya hamsini, zitekeleze wewe na ummah wako.' Nikafahamu huo ndio uamuzi wa mwisho wa Mwenyezi Mungu, nikarejea kwa Musa, akaniambia: 'Rejea,' lakini kwakuwa nilikuwa nimejua kuwa huo ndio uamuzi wa mwisho wa Mwenyezi Mungu sikurejea.

[175] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha tafsiri ya Qur'an, Mlango wa Sura Bani Israil, Hadithi ya 3131.

**Taarikh Baghdad Juz. 5, Uk. 13[176]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kuwa alimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: "Nilipopelekwa mbinguni Jibril alinifikisha penye mkunazi wa mwisho, akanizamisha ndani ya nuru kisha akaniacha peke yangu, nikasema: Habibi Jibril, ni sehemu hii nakuhitajia zaidi, mbona waniacha na kujitenga na mimi? Akasema: 'Ewe Muhamad! Wewe umesimama sehemu ambayo hasimami hapo yeyote, si Nabii aliyetumwa wala Malaika aliyewekwa karibu na Mwenyezi Mungu, wewe uko karibu na Mwenyezi Mungu kushinda pinde za mshale.' Akanijia Malaika na kuniambia: 'Hakika Rahman anajisabihi Mwenyewe.' Hapo nikamsikia Rahman akisema: 'Subhanallah! Ni adhimu kiasi gani Mwenyezi Mungu! Hapana mungu isipokuwa Allah!'"

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 1, Uk. 309[177]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Ulipopita usiku niliopelekwa Miraji, asubuhi niliamka nikiwa Makka. Lilinikosesha nguvu jambo langu na nikajua kuwa watu watanipinga. Nikaketi peke yangu huku nikiwa nimejawa na huzuni. Ghafla alipita adui wa Mwenyezi Mungu Abu Jahli. Alikwenda na kuketi kwake, kisha alimwambia kwa kebehi: "Je kuna chochote?" Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Ndiyo." Akasema: "Ni kipi hicho?" Akasema: "Usiku huu nilipelekwa sehemu?" Akasema: "Wapi?" Akasema: "Baytul-Maqdas." Akasema: "Kisha umeamka ukiwa baina yetu ee?" Akasema: "Ndiyo." Akasema: "Je nikiwaita jamaa zako utawasimulia kama ulivyonisimulia?" Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Ndiyo." Akasema: "Enyi kundi la Bani Kaab bin Luay."

Ibn Abbas anasema: Watu wakaacha sehemu zao na kuja na kuketi pamoja nao. Abu Jahli akasema: "Wasimulie jamaa zako yale uliyonisimulia." Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Hakika katika usiku huu nilipelekwa sehemu." Wakasema: "Wapi?" Akasema: "Baytul-Maqdas." Wakasema: "Kisha umeamka ukiwa baina yetu?" Akasema: "Ndiyo." Kila mmoja akashangaa. Yupo aliyepiga makofi na yupo aliyeweka mkono juu ya kichwa, wote wakishangaa uwongo huo kama walivyodai. Wakasema: "Je waweza kutuelezea msikiti ulivyo?" –Kati yao kulikuwa na watu ambao waliwahi kusafiri kwenda mji ule na kuuona msikiti - Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Niliendelea kuwaelezea msikiti ulivyo mpaka baadhi ya sifa zikanichanganya, ndipo nikaletewa msikiti mbele yangu ukawekwa karibu na nyumba ya Aqil. Nikawa naelezea ulivyo huku nikiutazama. Wakasimama baadhi ya jamaa wakasema: 'Wallahi hizo ndio sifa zake amepatia.'"

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA KUMPENDA MTUKUFU MTUME (SAWW)

**Sahih Bukhari: Kitabu cha iman, Mlango unaosema kuwa kumpenda Mtukufu Mtume ni imani:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas, amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu imo mikononi Mwake, si muumini yeyote miongoni mwenu mpaka mimi niwe ni mtu ampendaye sana kuliko mzazi wake, kizazi chake na watu wote."

[176] *Taarikh Baghdad*: Wasifu wa Ahmad bin Muhammad al-Maruziy, Namba 2364.
[177] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Musnad Abdullah bin Abbas, Hadith ya 2815.

**Sahih Bukhari: Kitabu cha iman, Mlango unaozungumzia utamu wa imani:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas, amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Mambo matatu mtu akiwa nayo ni lazima ataupata utamu wa imani: Iwapo anawapenda zaidi Mwenyezi Mungu na Mtume wake kushinda kitu kingine chochote, iwapo anampenda mtu si kwa jambo lingine isipokuwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na iwapo anachukia kurudi katika ukafiri kama asivyopenda kuingizwa motoni."

**Sahih Muslim: Kitabu cha iman, Mlango unaozungumzia wajibu wa kumpenda Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas, amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Mtu hatakuwa muumini mpaka mimi niwe ndiye mtu ampendaye zaidi kushinda familia yake, mali yake na watu wote."

**Hilyatul-Awliyai Juz. 4, Uk. 42[178]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdul-Mun'im bin Idirisa, kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake Wahbi, amesema: Katika Wana wa Israel kulikuwa na mtu aliyemuasi Mwenyezi Mungu miaka mia mbili, kisha alifariki, wakachukua mwili wake na kuutupa jalalani, Mwenyezi Mungu akampelekea wahyi Musa (as) kuwa uchukue na umswalie. Musa akasema: "Ewe Mola, Wana wa Israel wameshuhudia kuwa alikuasi miaka mia mbili." Mwenyezi Mungu akampelekea wahyi kuwa hivyo ndivyo alivyokuwa, lakini yeye alikuwa kila anapofunua Taurat na kuona jina 'Muhammad' analibusu na kuliweka baina ya macho yake na kumswalia, hivyo nikamshukuru kwa hilo na nikamsamehe dhambi zake na kumuozesha mahurulaini sabini.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA UKARIMU WA MTUKUFU MTUME (SAWW)

**Sahih Muslim: Kitabu cha fadhila, Mlango unaozungumzia ushujaa wa Mtukufu Mtume (saww):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik, amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa mwema kushinda watu wote, alikuwa mkarimu kushinda watu wote na alikuwa shujaa kushinda watu wote….."

**Nasema:** Pia ameipokea Tirmidhiy ndani ya *Sahih* yake,[179] humo amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa jasiri kushinda watu wote, alikuwa mkarimu kushinda watu wote na alikuwa shujaa kushinda watu wote."

**Sahih Muslim: Kitabu cha fadhila, Mlango unaosema kuwa Mtukufu Mtume (saww) alikuwa mkarimu wa kheri kushinda watu wote:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa mkarimu wa kheri kushinda watu wote, na alikuwa mkarimu zaidi ndani ya mwezi wa Ramadhani. Hakika Jibril (as) alikuwa akikutana naye kila mwaka ndani ya mwezi wa Ramadhani mpaka un-

[178] Wasifu wa Wahbi bin Munabihu. Habari zake kutoka katika Taurat na kutoka kwa Manabii wa kizazi cha Israil.
[179] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha jihadi, Mlango unaozungumzia kutoka wakati wa fadhaa, Hadithi ya 1687.

apoisha. Na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa akimsomea Qur'ani. Na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) huwa mkarimu wa kheri anapokutana na Jibril kushinda hata upepo mkali."

**Nasema:** Ameipokea Muslim[180] kwa njia tofauti, kadhalika Bukhari ndani ya *Sahih* yake[181].

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 286[182]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibrahim bin Muhammad ambaye atokana na kizazi cha Ali bin Abu Talib (as), amesema: Ali (as) alikuwa anapotoa sifa za Mtukufu Mtume (saww) husema: "Hakuwa mrefu wa kupindukia, - mpaka aliposema : baina ya mabega yake kulikuwa na muhuri wa unabii, nao ndio muhuri wa Manabii. Alikuwa mkarimu wa kutoa kuliko watu wote, mvumilivu kuliko watu wote, mkweli kuliko watu wote, mwenye tabia njema kuliko watu wote, na mkarimu kwa familia kuliko watu wote. Mwenye kumuona kwa mara ya kwanza ni lazima anyenyekee mbele yake, na mwenye kuamiliana naye na kumtambua ni lazima ampende. Anasema mwenye kumsifu kuwa: Sijapata kumuona mtu mfano wake si kabla yake wala baada yake."

**Muwatau Imam Malik bin Anas: Kitabu cha jihadi, Uk. 195[183]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Amru bin Shuaib kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipotoka Hunayni –akikusudia kwenda al-Jaaranah – watu walimuomba mpaka ngamia wake akasogea karibu na mti na joho lake likakwama kwenye mti na kumvuka toka mgongoni, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Nirudishieni joho langu, hivi mnahofu kuwa nisiwagawie kile alichowapeni Mwenyezi Mungu? Naapa kwa ambaye nafsi yangu imo mikononi Mwake, lauMwenyezi Mungu angewapeni neema mfano wa mti wa Tihamah basi ningewagawieni, na hamtanikuta nikiwa bakhili, wala muoga wala muongo."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 3, Uk. 175[184]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa mtu mmoja alikwenda kumuomba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akampa kondoo aliyekuwa baina ya milima miwili. Mtu yule alikwenda kwa jamaa zake na kuwaambia: "Enyi jamaa zangu ingieni katika Uislamu, wallahi hakika Muhammad anampa mtu kwa kiwango ambacho hatakhofia tena ufukara."

**Sunanud-Daramiy Juz. 1, Uk. 34[185]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir amesema: Kamwe Mtukufu Mtume (saww) hakuwahi kuombwa na akasema hapana."

**Sunanud-Daramiy Juz. 1, Uk. 30[186]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Umar kuwa alisema: "Sikupata kumuona mtu jasiri wala mkarimu wala shujaa wala ang'arae wala msafi kushinda Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

[180] *Sahih Muslim*: Kitabu cha fadhila, Mlango unaosema Mtukufu Mtume (saww) alikuwa mkarimu wa kheri kushinda hata upepo mkali.
[181] *Sahih Bukhari*: Mlango unaozungumzia jinsi wahyi ulivyoanza kuteremka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).
[182] *Sahih Tirmidhiy:* Kitabu cha fadhila, Mlango unaozungumzia sifa za Mtukufu Mtume (saww), Hadithi ya 3738.
[183] *Muwatau Imam Malik bin Anas*: Kitabu cha jihadi, Mlango unaozungumzia upindukiaji mipaka, Hadithi ya 994.
[184] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Musnad Anas bin Malik, Hadithi ya 12379.
[185] *Sunanud-Daramiy:* Mlango unaohusu ukarimu wa Mtukufu Mtume (saww), Hadithi ya 70.
[186] *Sunanud-Daramiy*: Mlango unaohusu uzuri wa Mtukufu Mtume (saww), Hadithi ya 59.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9, uk. 13[187]:**

Amesema: Kutoka kwa Anas amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amesema: "Je niwape habari ni nani aliye mkarimu kushinda wa karimu wote? Mwenyezi Mungu ndiye mkarimu kushinda wakarimu wote, na mimi ni mkarimu kushinda wana wote wa Adam." - Amesema: Ameipokea Abu Ya'ala.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9, uk. 13[188]:**

Amesema: Kutoka kwa Umar, amesema: Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), na siku moja alikwenda kwa muuza duka na kununua toka kwake kanzu kwa dirhamu nne, na akatoka akiwa ameivaa, ghafla alikuja mtu mmoja miongoni mwa Ansari na kusema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Nivishe kanzu Mwenyezi Mungu atakuvisha nguo ya peponi." Akavua kanzu ile na kumvisha. Kisha alirejea kwa muuza duka na kununua kanzu kwa dirhamu nne na kubakiwa na dirhamu mbili, ghafla alikutana na mtumishi wa kike akilia njiani, akamuuliza: "Kitu gani chakuliza?" Akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Jamaa zangu walinipa dirhamu mbili nikawanunulie unga lakini zimepotea." Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akampa zile dirhamu mbili zilizobakia, mtumishi yule aliondoka huku akilia, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwita na kumuuliza: "Kitu gani chakuliza wakati umeshachukua dirhamu mbili?" akasema: "Nahofia kuwa watanipiga."

Mtume akafuatana naye mpaka kwa jamaa zake, alipotoa salamu walitambua sauti yake, kisha akasalimu kwa mara ya pili, kisha mara ya tatu, ndipo wakamwitikia. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Je mliisikia salamu yangu ya awali?" Wakasema: "Ndiyo lakini tulipenda uzidi kutusalimu, kwa haki ya baba yetu na mama yetu ni kitu gani kimekusumbua?" Akasema: "Nimemuonea huruma mtumishi huyu msije mkampiga." Bwana wake akasema: "Yeye yu huru kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kwa kuwa umekuja naye." Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawabashiria kheri na pepo, na akasema: "Mwenyezi Mungu aitie kumi baraka, kwayo kamvisha Mtume wake kanzu, kamvisha mtu miongoni mwa Ansari kanzu, na kwayo kamkomboa mtumwa. Na ninamuhimidi Mwenyezi Mungu kwani Yeye ndiye aliyeturuzuku haya kwa uwezo wake." - Amesema: Kaiandika Tabaraniy.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA USHUJAA WA MTUKUFU MTUME (SAWW), KUPENDA KWAKE KUFA KISHAHIDI, NA KULINDWA KWAKE NA JIBRIL NA MIKAIL KATIKA MAPAMBANO

**Nasema:** Katika mlango uliopita yametangulia maelezo yanayoonesha kuwa alikuwa shujaa kushinda watu wote, na haya ni maelezo mengine yanayohusu hilo:

**Sahih Bukhari: Kitabu cha jihadi na safari, Mlango unaozungumzia mtu mwenye kuongoza mnyama wa mwenzake vitani:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Is'haqa, amesema: Mtu mmoja alimwambia al-Barau bin Azib: "Je mlimkimbia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) siku ya Hunayni?" Akasema: "Lakini Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hakukimbia, hakika watu wa Hawazin walikuwa wanarusha mishale, na tulipokutana nao mimi niliwashambulia mpaka wakakimbia, ndipo Waislamu wakaelekeakwenye ngawira na hapo watu wa Hawazin wakatuelekea kwa mishale. Ama Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) yeye

[187] *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid:* Mlango unaozungumzia ukarimu wa Mtukufu Mtume (saww).
[188] *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid:* Mlango unaozungumzia ukarimu wa Mtukufu Mtume (saww).

hakukimbia. Nilimuona akiwa juu ya nyumbu wake mweupe huku Abu Sufiyan – Yaani Abu Sufiyan bin al-Harith bin Abdul-Muttalib mtoto wa ami yake Mtume – akiwa kashika lijamu yake na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: "Mimi ni Nabii na si uwongo. Mimi ni mtoto wa Abdul-Muttalib."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 1, Uk. 86[189]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ali (as) kuwa amesema: "Bila shaka ulituona siku ya Badri tukikimbilia kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) naye akiwa ndiye mtu aliye karibu zaidi na adui kuliko sisi, na ndiye aliyekuwa mwenye mashambulizi makali siku hiyo kushinda watu wote."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 1, Uk. 156[190]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ali (as) kuwa alisema: "Tulikuwa tunajikinga kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) pindi mashambulizi yanapozidi na watu kukutana uso kwa uso. Hakuna mtu aliyekuwa karibu na adui kuliko yeye."

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 276[191]:**

Amesema: Kutoka kwa al-Barau bin Azib, amesema: "Tulikuwa tunajikinga kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) pindi mashambulizi yanapozidi, na hakika hakuna shujaa anayelingana naye."

**Kanzul-Ummal Juz. 5, Uk. 275[192]:**

Amesema: Kutoka kwa Anas, kutoka kwa Miqdad, amesema: Tulipopanga safu kwa ajili ya kupigana – Yaani siku ya Uhudi - Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliketi chini ya bendera ya Mas'abu bin Umairi, walipouwawa wabeba bendera mushrikina walishindwa mara ya kwanza. Waislamu wakavamia kambi yao na kuchukua mali zao. Kisha waliwazunguka Waislamu na kuwajia kwa nyuma, watu wakakimbia na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawaita wabeba bendera. Akaichukua bendera ya Mas'abu bin Umair, kisha akauwawa – mpaka aliposema: Mushrikina wakanadi kwa mbiu yao: "Enyi wafuasi wa Uzza, enyi wafuasi wa Hubal" Wallahi walitutia maumivu kwa kutuuwa mauwaji ya fedheha, na wakamuumiza Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kadiri walivyomuumiza. Naapa kwa ambaye alimtuma kwa haki, hakika sikumuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa ametetereka walau shibri moja. Mara nilikuwa nikimuona kasimama akirusha mishale kwa upinde wake na mara akirusha mawe mpaka yakawapata. - Amesema: Kaiandika al-Waqidiy.

**Sahih Bukhari: Kitabu kinachozunguzia kutamani, Hadithi ya kwanza:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira, amesema: Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: "Naapa kwa ambaye nafsi yangu imo mikononi Mwake, natamani kwamba watu wangechukia kubaki hai baada yangu, na kama ningepata cha kuniwezesha kuwabeba (vitani) basi nisingebaki hai. Ningependa kuona nauwawa katika njia ya Mwenyezi Mungu kisha narudishiwa uhai, kisha nauwawa kisha narudishiwa uhai, kisha nauwawa kisha narudishiwa uhai, kisha nauwawa."

---

[189] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Musnad Ali bin Abu Talib, Hadithi ya 656.
[190] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal:* Musnad Ali bin Abu Talib, Hadithi ya 1350.
[191] *Kanzul-Ummal:* Kitabu cha fadhila, Mlango unaozungumzia fadhila za Mtukufu Mtume na miujiza yake na utoaji wake wa habari za ghaibu, Hadithi ya 35347.
[192] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha vita na misafara, Mlango unaozungumzia vita vya Mtukufu Mtume, vita vya Uhudi, Hadithi ya 30044.

**Sahih Bukhari: Kitabu kinachozungumzia mwanzo wa uumbaji, Mlango unaosema yalipokusudia makundi mawili:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Saad bin Abu Waqas, amesema: "Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) siku ya Uhudi akiwa pamoja na wanaume wawili wakipigana kwa kumlinda, walikuwa wamevaa nguo nyeupe, wakipigana kwa mashambulizi makali ambayo sijapata kuona mfano wake kabla yao wala baada yao."

**Nasema:** Pia kaipokea Muslim ndani ya *Sahih* yake katika kitabu cha fadhila, katika Mlango unaozungumzia Jibril na Mikail kupigana kwa ajili ya kumhami Mtukufu Mtume siku ya Uhudi.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA TABIA ZA MTUKUFU MTUME (SAWW)

**Al-Fakhru ar-Raziy ndani ya Tafsiri yake: Mwishoni mwa kauli ya Mwenyezi Mungu: "Na hakika wewe una tabia tukufu." Katika Sura al-Qalam:**

Amesema: Amepokea Hisham bin Ur'wah kutoka kwa baba yake kutoka kwa Aisha, amesema: "Hakuna mtu aliyekuwa na tabia njema kumshinda Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Hakuitwa na yeyote miongoni mwa Masahaba zake wala miongoni mwa watu wa nyumba yake isipokuwa aliitikia: Labaika. Na kwa ajili hii Mwenyezi Mungu akasema: **"Na hakika wewe una tabia tukufu."**

**Al-Fakhru ar-Raziy ndani ya tafsiri yake: Mwishoni mwa kauli ya Mwenyezi Mungu: "Hakika kwa Mola Wako Mlezi ndio marejeo." Katika Sura al-Alaq:**

Amesema: Amepokea kwa maana hii, kuwa Myahudi mmoja miongoni mwa mafasihi wa Kiyahudi alikuja kwa Umar zama za ukhalifa wake, akasema: "Nieleze tabia za Mtume wenu." Umar akasema: "Zitafute kutoka kwa Bilal yeye azijua zaidi kuliko mimi." Kisha Bilali alimwelekeza Myahudi yule kwa Fatimah (as), kisha Fatimah (as) alimwelekeza kwa Ali (as), alipomuuliza Ali kuhusu tabia zake (saww), Ali (as) alisema: "Nieleze sifa za starehe za dunia ili nikueleze sifa za tabia zake." Myahudi akasema: "Hili ni jambo gumu kwangu." Ali (as) akamwambia: "Umeshindwa kunieleza sifa za starehe za dunia ilihali Mwenyezi Mungu ameshathibitisha uchache wake aliposema: **'Sema: Starehe za dunia ni chache.'** Vipi mimi nikueleze sifa za Mtukufu Mtume (saww) wakati Mwenyezi Mungu amethibitisha kuwa sifa zake ni tukufu aliposema: **'Na hakika wewe una tabia tukufu."'**

**Sahih Bukhari: Kitabu cha uwakala, Mlango unaozungumzia kulipa madeni:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kuwa mtu mmoja alikwenda kwa Mtukufu Mtume (saww) kudai deni lake, alipofika alitamka maneno machafu. Masahaba zake wakanyanyuka kutaka kumwadabisha, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Mwacheni, hakika mwenye haki ana haki ya kusema." Kisha alisema: "Mpeni majani (chakula cha mnyama) mazuri kama majaniyake." Wakasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Hatuna isipokuwa yaliyo bora kushinda yake." Akasema: "Mpeni hayo kwani hakika aliye mbora kati yenu ni yule mwenye kulipa vizuri."

**Sahih Bukhari: Kitabu cha adabu, Mlango unaozungumzia tabasamu na kucheka:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik kuwa alisema: "Nilikuwa ninatembea pamoja na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa kavaa nguo nzito ya Najrani. Mara akakutana na Bedui ambaye aliikokota nguo ile kwa nguvu." Anas anasema: "Nilipotazama juu ya shingo ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) niliona athari zilizotokana na nguo ile kuvutwa kwa nguvu. Kisha bedui alisema: 'Ewe Muhammad amrisha nipewe sehemu ya mali ya Mwenyezi Mungu iliyopo kwako.' Mtume alimgeukia na kucheka kisha aliamuru apewe."

**Sahih Bukhari: Kitabu cha zawadi, Mlango unaozungumzia zawadi chache:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kutoka kwa Mtukufu Mtume (saww) kuwa alisema: "Hata kama nitaalikwa kwenye mkono au muundi nitaitikia. Na hata kama nitapewa zawadi ya mkono au muundi nitaipokea."

**Sahih Bukhari: Kitabu kinachozungumzia mwanzo wa uumbaji, Mlango wa sifa za Mtukufu Mtume (saww):**

Amepokea kwa sifa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kuwa alisema: "Kamwe Mtume hakuwahi kudharau chakula, akikitamani hukila la sivyo hukiacha."

**Sahih Bukhari: Kitabu kinachozungumzia usia, Mlango unaozungumzia kumtumikisha yatima safarini na nyumbani:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa alisema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alifika Madina akiwa hana mtumishi. Abu Talha alinishika mkono na kwenda na mimi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Nimekuletea kijana mwerevu awe anakuhudumia." Nikawa namhudumia nyumbani na safarini, hakuwahi kunifokea: "Kwa nini umefanya hivi?" kwa lolote nililotekeleza, wala hakuwahi kunifokea: "Kwa nini hujafanya hivi?" kwa lolote ambalo sikutekeleza.

**Sahih Bukhari: Kitabu cha adabu, Mlango unaozungumzia tabia njema na ukarimu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas, amesema: "Nilikuwa mhudumu wa Mtukufu Mtume (saww) muda wa miaka kumi, na kamwe hakuwahi kuniambia: "Ah!" wala "Kwa nini umefanya hivi?" wala "Kwa nini hujafanya?"

**Sahih Bukhari: Kitabu kinachozungumzia mwanzo wa uumbaji, Mlango wa sifa za Mtukufu Mtume (saww):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Umar, amesema: "Mtukufu Mtume (saww) hakuwa mtu mwenye maneno machafu wala tabia mbaya. Na alikuwa akisema: 'Hakika aliye mbora kati yenu ni yule mwenye tabia njema zaidi kati yenu.'"

**Sahih Bukhari: Kitabu cha adabu, Mlango unaozungumzia kiburi:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas, amesema: "Mtumwa miongoni mwa watumwa wa wakazi wa Madina alikuwa anaweza kumshika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mkono na kwenda naye kokote atakako."

**Sahih Bukhari: Kitabu kinachozungumzia kuomba idhini, Mlango unaozungumzia kuwasalimu watoto:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipita kwa watoto na kuwasalimu. Na amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa akifanya hivyo."

**Sahih Bukhari: Kitabu cha adabu, Mlango unaozungumzia jina la ubaba la mtoto:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa na tabia njema kushinda watu wote, na nilikuwa na kaka yangu akiitwa Abu Umair, alikuwa anapokuja kwa Mtume humwambia: 'Ewe Abu Umair kasuku amefanya nini?' Alikuwa na kasuku aliyekuwa akicheza naye."

**Al-Adab al-Mufrad cha BukhariUk. 42[193]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik kuwa alisema: "Mtume alikuwa mwingi wa huruma, na hakufikiwa na mtu isipokuwa alimwahidi na kumtimizia kama anacho. Siku moja palikimiwa Swala na mara alikuja bedui na kuchukua nguo yake, akasema: 'Katika haja yangu nimebakiwa na jambo dogo na ninahofia nisije kulisahau.' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisimama pamoja naye na akamtimizia haja yake kisha alikuja na akaswali."

**Al-Adab al-Mufrad cha BukhariUk. 169[194]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Rifah al-Adawiy, amesema: Nilikwenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) nikamkuta akitoa hotuba, nikasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mtu mgeni amekuja kuuliza kuhusu dini yake hajui ni ipi dini yake." Alinifuata na kusitisha hotuba yake, alikuja na kiti ambacho miguu yake ilibadilika na kuwa ya chuma. Hamid anasema: "Nilikuwa naiona ikiwa ya mbao, mara nikaiona ni ya chuma, alikaa juu ya kiti hicho na kuanza kunifundisha yale aliyofundishwa na Mwenyezi Mungu, kisha alimalizia hotuba yake."

**Sahih Muslim: Kitabu cha fadhila, Mlango unaosema kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa na tabia njema kushinda watu wote:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa mwenye tabia njema kushinda watu wote. Siku moja alinituma katika mahitaji yake, nikamwambia: Wallahi sintakwenda, huku moyoni nikiwa nimekusudia kwenda katika lile aliloniamuru Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Nilitoka na kupita kwa watoto wakiwa wanacheza sokoni, mara nikahisi Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kaishika shingo yangu kwa nyuma. Nikamtazama na kumuona akicheka, akasema: 'Anas umekwenda nilikokutuma?' Nikasema ndiyo ninakwenda sasa, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Wallahi nilikuwa mtumishi wake muda wa miaka tisa lakini sikuwahi kusikia akinifokea: 'Kwa nini umefanya hivi na hivi?' katika lile nililofanya au kunifokea: 'Kwa nini hujafanya hivi na hivi' katika lile nililoacha kufanya."

[193] *Al-Adab al-Mufrad* cha Bukhari: Mlango wa ukarimu wa nafsi, Hadithi ya 278.
[194] *Al-Adab al-Mufrad* cha Bukhari: Mlango unaozungumzia kuketi juu ya kitanda, Hadithi ya 1164.

**Sahih Muslim: Kitabu cha fadhila, Mlango unaozungumzia kujitenga kwake (saww) mbali na madhambi:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha kuwa amesema: "Kamwe Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hakuwahi kukipiga kitu kwa mkono wake, wala kumpiga mwanamke au mfanyakazi, labda awe anapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu. Na kamwe hakuwahi kutendewa ubaya kisha akalipiza kisasi, labda heshima ya Mwenyezi Mungu ivunjwe ndipo atalipiza kisasi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu."

**Sahih Muslim: Kitabu cha fadhila, Mlango unaozungumzia kuwaonea huruma watoto na familia:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik amesema: "Sikupata kumuona mtu mwenye huruma kwa familia yake kumshinda Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)."

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 80[195]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik kuwa alisema: "Alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) anapokutana na mtu humpa mkono na hauondoi mpaka mtu yule aanze yeye kuuondoa wake, wala hauondoi uso wake mbele yake mpaka mtu yule aanze yeye kuuondoa wake, wala hakuwahi kuonekana kanyoosha magoti yake mbele ya mtu aliyeketi naye."

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 255[196]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Umar, amesema: "Alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) anapomuaga mtu humshika mkono na hauachii mpaka mtu yule aanze yeye kuuachia wa Mtume, na alikuwa akisema: 'Mkabidhi Mwenyezi Mungu dini yako, amana yako na matendo yako ya mwisho."'

**Sahih Tirmidhiy Juz. 1, Uk. 363[197]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Abdullah al-Jadliy kuwa alisema: Nilimuuliza Aisha kuhusu tabia za Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), akasema: "Hakuwa mtu mwenye maneno machafu wala tabia mbaya, wala mpiga kelele sokoni wala hakulipa ubaya kwa ubaya aliotendewa, lakini alisamehe."

**Sahih Abi Daud Juz. 3, Uk. 175[198]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kuwa amesema: "Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa akiketi pamoja na sisi katika baraza moja na kutusimulia, na anaposimama nasi husimama mpaka tuhakikishe kuwa ameingia katika nyumba ya mmoja ya wake zake. Siku moja alikuwa anatusimulia na akasimama kutaka kuondoka, nasi tukasimama. Aliposimama, tukamuona bedui kamuwahi na kumvuta nguo yake kiasi kwamba mvuto ule ukabadili rangi ya shingo yake kuwa nyekundu, nguo ilikuwa nzito, alipomgeukia bedui alimwambia: "Nijazie shehena ngamia wangu hawa wawili, kwani hakika hunijazii kutoka kwenye mali yako wala ya baba yako." Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Hapana, na ninamtaka Mwenyezi Mungu msamaha. Hapana, na ninamtaka Mwenyezi Mungu msamaha. Sikujazii mpaka unipe fidia ya kunivuta ulikonivuta." Wakati wote huo

[195] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha wasifu wa Kiyama, watumwa na uchamungu, Mlango wa 46, Hadithi ya 2490.
[196] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha daawa, Mlango wa maneno asemayo anapomuaga mtu, Hadithi ya 2442.
[197] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha daawa, Mlango wa maneno asemayo anapomuaga mtu, Hadithi ya 2442.
[198] *Sahih Abi Daud*: Kitabu cha adabu, Mlango unaozungumzia uvumilivu na tabia za Mtukufu Mtume, Hadithi ya 4775.

bedui alikuwa akimwambia: "Wallahi sikufidii." – Alisimulia mpaka aliposema: Kisha alimwita mtu na kumwambia: "Mjazie shehena ngamia wake hawa wawili, mmoja shairi na mwingine tende." Kisha alitugeukia na kusema: "Nendeni kwa baraka ya Mwenyezi Mungu Mtukufu."

**Sahih Abi Daud Juz. 3, Uk. 187[199]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa alisema: "Sikupata kumuona mtu akimnong'oneza Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) sikioni kisha Mtume akaondoa kichwa chake, ni mpaka pale mtu yule atakapoondoa yeye kichwa chake. Na sikuwahi kumuona kauondoa mkono wa mtu alipopewa mkono, mpaka mtu yule aanze yeye kuuondoa wake."

**Sahih Ibn Majah Uk. 176, Milango ya sadaka[200]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Said al-Khidriy kuwa alisema: Alikuja bedui mmoja kwa Mtukufu Mtume akimtaka amlipe deni lake alilokuwa akimdai. Akawa mkali kwake mpaka akamwambia: "Nitaendelea kukusumbua la sivyo unilipe." Masahaba zake wakamkemea na kumwambia: "Ole wako unajua unamwambia na nani?" Akasema: "Mimi nataka haki yangu." Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Hivi ndivyo mnavyoamiliana na wenye haki?" Kisha alituma ujumbe kwa Khawlah binti ya Qaysu na kumwambia: "Kama una tende tukopeshe, tutakulipa pindi zitakapotujia tende zetu." Akasema: "Sawa ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwa haki ya baba yangu." Akamkopesha, akamlipa bedui na kumpa chakula, bedui akasema: "Umelipa na Mwenyezi Mungu akulipie." Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Hao ndio watu bora, hakika hauna heshima ummah ambao mnyonge hachukui haki yake bila kukwidana."

**Nasema:** Wemesema baadhi yao katika maelezo: Inasemekana mtu huyu –bedui – alikuwa kafiri na alisilimu baada ya kushuhudia tabia hii tukufu, na akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, sijapata kumuona mtu mwenye subira kushinda wewe."

**Sahih Ibn Majah Uk. 318, Milango ya kujinyima dunia[201]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa akiwatembelea wagonjwa, akisindikiza jeneza na akiitikia mwaliko wa mtumwa. Alikuwa akipanda punda na hata siku ya kupambana na Bani Quraydha na Bani Nadhiri alikuwa juu ya punda, na pia siku ya Khaibar alikuwa juu ya punda.."

**Sahih Ibn Majah Uk. 281, Milango ya adabu[202]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa alisema: "Alitujia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) wakati tukiwa watoto, akatusalimu."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 6, Uk. 163[203]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Saad bin Hisham, alisema: "Nilimuuliza Aisha nikamwambia: Nieleze kuhusu tabia za Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Akasema: 'Tabia yake ilikuwa ni Qur'ani.'"

[199] *Sahih Abi Daud*: Kitabu cha adabu, Mlango unaozungumzia kuishi vizuri na watu, Hadithi ya 4794.
[200] *Sahih Ibn Majah*: Kitabu cha sadaka, Mlango unaosema kuwa mwenye haki ana mamlaka, Hadithi ya 2426.
[201] *Sahih Ibn Majah*: Kitabu kinachozungumzia kujinyima dunia, Mlango unaozungumzia kujiepusha na kiburi na kuwa mnyenyekevu, Hadithi ya 4178.
[202] *Sahih Ibn Majah*: Kitabu cha adabu, Mlango unaozungumzia kuwatolea salamu watoto na wanawake, Hadithi ya 3700.
[203] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Hadithi ya Sayyidah Aisha, Hadithi ya 24774.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 6, Uk. 106[204]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Hisham kutoka kwa baba yake, amesema: Aisha aliambiwa: Mtume alikuwa akifanya nini nyumbani kwake? Akasema: “Kama anavyofanya mmoja wenu, alikuwa anashona viatu vyake na nguo yake.”

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 2, Uk. 622[205]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Musa bin Ja’far kutoka kwa baba zake kutoka kwa Ali bin Abu Talib (as) kuwa Myahudi mmoja aliyekuwa akiitwa Jarijirah alikuwa ana dinari kadhaa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Alipokwenda kudai deni lake kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), alimwambia: “Ewe Myahudi, sina cha kukupa.” Myahudi akasema: “Hakika mimi sikuachi ewe Muhammad mpaka unipe.” Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: “Basi nitakaa na wewe.” Akaketi pamoja naye, na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaswali pamoja naye Swala ya Dhuhri, Laasir, Maghrib, Isha na Subhi. Wakati huo Masahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) walikuwa wakimtisha na kumwahidi kumwadhibu, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipogundua hilo alisema: “Jambo gani hili mtendalo?” Wakasema: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kwa nini Myahudi akuweke kizuizini!” Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: “Mola Wangu amenikataza kumdhulumu mwenye ahadi na mimi au mwingineo.”

Mchana ulipoondoka Myahudi alisema: “Nashahidia kwamba hapana mungu isipokuwa Allah. Na nashahidia kwamba hakika Muhammad ni mja wake na Mtume wake.” Na akasema: “Naitoa nusu ya mali yangu katika njia ya Mwenyezi Mungu. Wallahi sikufanya hili nililofanya ila ni ili nipime sifa zako na zile zilizomo ndani ya Taurat: ‘Muhammad bin Abdullah, atazaliwa Makka na atahamia Twibah na ufalme wake utakuwa Sham. Si mkali si mgumu wala si mpiga kelele masokoni, si msema maneno machafu wala kauli mbaya.’ Nashahidia kuwa hapana mungu isipokuwa Allah, na hakika wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Hii hapa mali yangu, itumie kama alivyokutaka Mwenyezi Mungu.” Na Myahudi huyu alikuwa ni mwingi wa mali.

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 2, Uk. 614[206]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Abi Awfa kuwa alisema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa akikithirisha dhikri na haongei upuuzi, alikuwa akirefusha Swala na kufupisha hotuba, wala hakuona vibaya kutembea pamoja na mtumwa na mjane mpaka awatimizie haja zao.”

**Sunanud-Daramiy Juz. 1, Uk. 35[207]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Akrimah kuwa alisema: Abbas alisema: Nilitaka kujua ni muda upi umebakia kabla Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hajaacha kuendelea kuwa na sisi, hivyo nilimwambia: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mimi nimewaona wakikuudhi na hata vumbi lao limekuudhi, natamani kama ungetengeneza kiti cha ufalme na kuwahutubia ukiwa juu yake.” Akasema: “Nitaendelea kuwa baina yao wakikanyaga nyayo zangu na kuninyang’anya joho langu mpaka Mwenyezi Mungu anipumzishe mbali na wao.” Hapo nikajua kuwa muda wa yeye kuendelea kubaki kati yetu ni mchache.

---

[204] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Hadithi ya Sayyidah Aisha, Hadithi ya 24228.
[205] *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha historia, Mlango wa alama za unabii.
[206] *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha historia, Mlango wa alama za unabii.
[207] *Sunanud-Daramiy*: Mlango unaohusu kifo cha Mtukufu Mtume (saww), Hadithi ya 75.

**Hilyatul-Awliyai Juz. 3, Uk. 26:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa ni mpole kushinda watu wote.Wallahi hakuwa anamkataza mtumwa wa kiume wala wa kike wala mtoto mdogo kuja na maji asubuhi yenye baridi ili aoshe uso wake na mikono yake. Na kamwe hakuwahi kuulizwa na muulizaji isipokuwa alimsikiliza na hakuondoka kwake mpaka muulizaji aanze yeye kuondoka. Na kamwe hakuwahi kupewa mkono na mtu isipokuwa aliupokea na hakuuondoa mpaka yule aliyempa aanze kuuondoa wa kwake.

**Sunanul-Bayhaqiy Juz. 2, Uk. 420[208]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Musa kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa akipanda punda, akivaa nguo ya sufi, akifunga mbuzi na akitoka kumpokea mgeni."

**Taarikh Baghdad Juz. 6, Uk. 277[209]:**

Amepokea kwa njia tofauti kutoka kwa IbnMas'ud na mwingineo kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimsemesha mtu, yule mtu akatetemeka, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Hakika mimi si Malaika, isipokuwa mimi ni mtoto wa mwanamke wa Kikuraishi ambaye alikuwa anakula chakula."

**Tabaqat Ibn Saad, Juz. 1, Sehemu ya tatu, Uk. 94[210]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Hamza bin Abdullah bin Ut'bah, alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa na sifa ambazo hazipatikani kwa madikteta: Hakuitwa na mweusi wala mwekundu isipokuwa aliitikia wito wake. Na huenda akakuta tende imetupwa lakini ataiokota na kuipeleka mdomoni kwake, na alikuwa akiogopa isije kuwa ni sadaka. Na alikuwa akipanda punda mtupu asiyekuwa na kitanda juu yake."

**Tabaqat Ibn Saad, Juz. 2, Sehemu ya tatu, Uk. 92[211]**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Yahya bin Abi Kathir kuwa alisema: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Nakula kama anavyokula mtumwa na ninaketi kama anavyoketi mtumwa, hakika mimi ni mtumwa.'Na alikuwa akikaa kwa kukunja miguu yake."

**Tabaqat Ibn Saad, Juz. 1, Sehemu ya pili, Uk. 95[212]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Sufiyan kwamba Hasan alisema: "Mwenyezi Mungu alipompa unabii Muhammad (saww) alisema: 'Huyu ni Nabii, huyu ndiye mbora Kwangu, jiambatanisheni naye na mfuateni katika mwenendo wake na njia yake.' Milango haikuwa inafungwa ili asionane na mtu, wala kizuizi hakikuwa kinawekwa kumzuia mtu kukutana naye. Alikuwa anakaa aridhini na anakula chakula chake aridhini, anavaa nguo hafifu na anapanda punda na anampa lifti mwingine na alikuwa akiramba vidole vyake, alikuwa akisema: 'Yeyote asiyefuata mwenendo wangu si mfuasi wangu."

[208] *Sunanul-Bayhaqiy*: Kitabu cha Swala, Mlango unaozungumzia kitu cha kusalia ikiwemo sufi au nywele, Hadithi ya 4188.
[209] *Taarikh Baghdad*: Wasifu wa Ismail bin Asad Abu Is'haqa, Namba 2307.
[210] *Tabaqat Ibn Saad*: Kutaja sifa za tabia ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).
[211] *Tabaqat Ibn Saad*: Kutaja sifa za tabia ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).
[212] *Tabaqat Ibn Saad*: Kutaja sifa za tabia ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

**Mushkilul-Athar Juz. 1, Uk. 498[213]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa akiwatembelea Maansari, akifika katika majumba ya Maansari watoto wa Maansari walikuwa wakimzunguka, na alikuwa akiwaombea na kupitisha mkono juu ya vichwa vyao na kuwasalimu."

**Al-Isabah Juz. 4, Sehemu ya kwanza, Uk. 4[214]:**

Ametaja hadithi kwa njia ya Hasan kuwa alisema: Tuliingia kwa Aswim bin Hadrad, akasema: "Kamwe Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hakuwa na mlinzi wala hakuwa na meza wala hakuwa anatembea na mto."

**Kanzul-Ummal Juz. 4, Uk. 30[215]:**

Lafudhi yake ni: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa anapokaa siku tatu bila kumuona mtu fulani huulizia habari zake, kama atakuwa amesafiri atamuombea mazuri, na kama atakuwa yupo mjini atakwenda kumtembelea, na kama ni mgonjwa atakwenda kumjulia hali." – Amesema: Kaiandika Abu Ya'ala kutoka kwa Anas.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 107[216]:**

Lafudhi yake ni: Hakika alinishukia Malaika kutoka mbinguni, Malaika ambaye kamwe hajawahi kushuka kwa Nabii yeyote na wala hatashuka kwa yeyote baada yangu, naye ni Israfil. Alishuka wakati nikiwa na Jibril, akasema: "Salamu iwe juu yako ewe Muhammad." Kisha alisema: "Mimi ni Mjumbe wa Mola Wako kwako, ameniamuru nikupe hiyari ya kuchagua, ukitaka kuwa Nabii mtumwa na ukitaka kuwa Nabii mfalme." Nilimtazama Jibril, na Jibril akaniashiria kuwa ninyenyekee, hivyo nikasema: "Nabii mtumwa." Na kama ningesema Nabii mfalme kisha ningetaka hivyo, basi milima ingetembea pamoja na mimi ikiwa ni dhahabu." - Amesema: Ameiandika Tabaraniy kutoka kwa Ibn Umar.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9, uk. 21[217]:**

Amesema: Kutoka kwa Aamir bin Rabia'h, amesema: "Nilitoka pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwenda msikitini, kiatu chake kikakatika mkanda, nikakichukua ili nikishone, akaninyang'anya toka mikononi mwangu, na kusema: "Huko ni kujipendelea, na mimi sipendi kujipendelea."

---

[213] *Mushkilul-Athar:* Mlango unaozungumzia hadithi zilizopokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kuhusu salamu atoayo mtu pindi anaposimama kwenye mlango wa ndugu yake.
[214] *Al-Isabah:* Herufi Ain, Wasifu wa Aswim bin Hadradu al-Ansariy, Namba 4349.
[215] *Kanzul-Ummal*: Mlango unaozungumzia sifa, tabia, matendo na kauli, tabia zinazohusu haki za urafiki, Hadithi ya 18483.
[216] *Kanzul-Ummal*: Mlango unaozungumzia fadhila mbalimbali na kutaja nasaba ya Mtukufu Mtume (saww), Hadithi ya 32027.
[217] *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid:* Mlango unaozungumzia haya.

# MLANGO UNAOZUNGUMZIA STAHA YA MTUKUFU MTUME (SAWW)

**Sahih Bukhari: Kitabu kinachozungumzia mwanzo wa uumbaji, Mlango wa sifa za Mtukufu Mtume (saww):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Said al-Khudriy kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa mwingi wa staha kuliko hata bikira aliye ndani ya utawa wake."

**Nasema:** Ameipokea pia kutoka kwa Shaabah[218], na amesema humo: Na alikuwa asipopendezwa na kitu hali hiyo itaonekana usoni kwake.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 8, uk. 26[219]:**

Amesema: Kutoka kwa Anas, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa mwingi wa staha kuliko hata bikira aliye ndani ya utawa wake. Na alikuwa asipopendezwa na kitu basi tutaijua hali hiyo usoni kwake. Na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Staha ndio kheri yote.'"- Amesema: Ameipokea al-Bazzar.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9, uk. 13[220]:**

Amesema: Kutoka kwa Ali (as) amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa anapoombwa kufanya jambo na akawa anataka kulifanya husema: 'Ndiyo.' Na ikiwa hataki kulifanya hukaa kimya, alikuwa hasemi: Hapana." - Amesema: Ameipokea Tabaraniy ndani ya *al-Awsat* katika hadithi ndefu katika kitabu cha dua.

# MLANGO UNAOZUNGUMZIA USHUHUDA WA ABU SUFIYAN ALIOUTOA KWA MFALME WA URUMI HARQAL WAKATI AKIWA BADO KAFIRI, KUWA HAKIKA MTUKUFU MTUME (SAWW) HASEMI UWONGO

**Sahih Bukhari: Mlango wa kwanza wa kitabu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Abbas, amesema: "Hakika Abu Sufiyan bin Harbi alimwambia kuwa Harqal alimwita kwake alipokuwa na msafara wa Makuraishi walipokuwa Sham kibiashara.Walipokwenda huko Iliyau aliwaita katika baraza lake ambalo lilikuwa limezungukwa na mabwana wa Urumi. Alimwita pia mkalimani wake, akasema: 'Ni nani kati yenu aliye karibu zaidi kinasaba na mtu huyu anayedai kuwa yeye ni Nabii?' Abu Sufiyan anasema: Nikasema: 'Mimi ndiye niliye karibu naye kinasaba kushinda wengine.' Akasema: 'Msogezeni karibu na mimi, na wasogezeni jamaa zake na uwaweke nyuma yake.' Kisha alimwambia mkalimani wake: 'Waambie: Hakika mimi namuuliza huyu kuhusu mtu huyo, hivyo akinidanganya mpingeni.' Wallahi kama si kuona haya kuwa wataniumbua kwa uwongo ningesema uongo dhidi yake. Jambo la kwanza aliloanza kuniuliza ni: 'Vipi nasaba yake kwenu?' Nikasema: 'Yeye kati yetu ni mwenye nasaba yenye heshima.'

[218] *Sahih Bukhari*: Kitabu kinachozungumzia mwanzo wa uumbaji, Mlango wa sifa za Mtukufu Mtume (saww).
[219] *Maj'mauz-Zawaid Waman'baul-Fawaid:* Mlango unaozungumzia haya.
[220] *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid:* Mlango unaozungumzia ukarimu wake (saww).

"Akasema: 'Je kuna yeyote miongoni mwenu aliyewahi kudai hili kabla yake?' Nikasema hapana, akasema: 'Je kati ya wahenga wake kuna yeyote aliyekuwa mfalme?' Nikasema hapana. Akasema: 'Wanaomfuata ni mabwana au wanyonge?' Nikasema ni wanyonge, akasema: 'Wanaongezeka au wanapungua?' Nikasema wanaongezeka. Akasema: 'Je kuna mtu yeyote anaachana na dini yake kwa kuichukia baada ya kuingia katika dini hiyo?' Nikasema hapana. Akasema: 'Je mlikuwa mkimtuhumu kwa uwongo kabla hajasema alilosema?' Nikasema hapana. Akasema: 'Je huhadaa?' Nikasema: 'Hapana, nasi tuna muda kidogo tangu tuachane naye hivyo hatujui amefanya nini ndani ya muda huo.' Abu Sufiyan anasema: 'Mazungumzo hayakunipa fursa ya kuingiza kitu zaidiya neno hili.'

"Akasema: 'Je mmejaribu kumuuwa?' Nikasema ndiyo. Akasema: 'Ilikuwaje mlipojaribu kumuuwa?' Nikasema: 'Vita baina yetu na yeye bado vinaendelea, mara anatushinda na mara tunamshinda.' Akasema: 'Anakuamrisheni nini?' Nikasema: Anasema: 'Mwabuduni Mwenyezi Mungu mmoja peke Yake msimshirikishe na chochote. Acheni wanayoyaamini wahenga wenu.' Anatuamrisha kuswali, kusema ukweli, kuwa na staha na kuunga udugu.

"Akamwambia mkalimani wake: 'Mwambie: Nilipokuuliza kuhusu nasaba yake ulisema kuwa ni mwenye nasaba ya heshima kati yenu, kadhalika Mitume hutumwa kutoka katika nasaba ya watu aliotumwa kwao. Na nilikuuliza je kuna yeyote miongoni mwenu alidai haya kabla yake? Ukasema hapana, kama kungekuwa kuna mtu aliyedai hili kabla yake ningesema kuwa mtu huyu anafuata kauli iliyosemwa kabla yake.

"Na nilikuuliza je kati ya baba zake kuna yeyote aliyekuwa mfalme? Ukasema hapana, kama kati ya baba zake kungekuwa na yeyote aliyekuwa mfalme ningesema kuwa mtu huyu anatafuta ufalme wa baba yake. Na nilikuuliza je mlikuwa mnamtuhumu kwa uwongo kabla hajasema aliyoyasema? Ukasema hapana, hapo nikajua kuwa hawezi kuacha kuwasemea watu uwongo kisha akamsemea Mwenyezi Mungu uwongo. Na nilikuuliza je wafuasi wake ni mabwana au wanyonge? Ukasema ni wanyonge ndio waliomfuata, na hao ndio wafuasi wa Mitume. Na nilikuuliza je wanaongezeka au wanapunguka? Ukasema wanaongezeka, hivyo ndivyo lilivyo jambo la imani mpaka litimie. Na nilikuuliza je kuna mtu yeyote ametoka katika dini yake kwa kuichukia baada ya kuingia katika dini hiyo? Ukasema hapana, hivyo ndivyo ilivyo imani mpaka bashasha yake ichanganyikane na nyoyo.

"Na nilikuuliza je anahadaa? Ukasema hapana, kadhalika Mitume hawahadai. Na nilikuuliza anakuamrisheni nini? Ukasema kuwa anakuamrisheni kumwabudu Mwenyezi MunguMmoja na msimshirikishe na chochote, anakukatazeni kuabudu masanamu na anakuamrisheni kuswali, kutoa sadaka, na kuwa na staha. Hakika ikiwa unayosema ni haki basi atamiliki sehemu ya kukanyagia nyayo zangu mbili hizi, na nilikuwa najua atakuja kutokea lakini sikuwa nadhani kuwa atatokana nanyi, na ningekuwa nina yakini kuwa nitamfikia basi ningejilazimisha kukutana naye, na kama ningekuwa kwake basi ningemuosha nyayo zake.' Kisha aliomba aletewe barua ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliyompa Dahyah aipeleke kwa gavana wa Busra, naye akampelekea Harqal, akaisoma, humo mlikuwa na:

> "Kwa jina Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Kutoka kwa Muhammad mja wa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, kwenda kwa Harqal, mtawala wa Urumi. Salamu ya Mwenyezi Mungu iwe juu ya atakayefuata uwongofu, ama baad. Hakika mimi nakuita kwa wito wa Uislamu, silimu usalimike, Mwenyezi Mungu atakupa malipo mara mbili, na kama utapinga jua kuwa madhambi ya Wairisi yatakuwa juu yako. **'Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Njooni kwenye neno lilio sawa baina yetu na nyinyi: Ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu, wala tusimshirikishe na chochote; wala tusifanyane sisi kwa sisi kuwa Waola Walezi badala ya Mwenyezi Mungu. Na wakigeuka basi semeni: Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu.'"**

"Abu Sufiyan anasema: Baada ya kusema aliyosema na kumaliza kusoma barua, minong'ono iliongezeka na sauti ikaongezeka, hivyo tukatoka. Nikawaambia jamaa zangu tulipotoka: 'Limekua jambo la mtoto wa Abu Kabshah kiasi kwamba hata mfalme wa Bani al-Asfar anamuogopa.'Niliendelea kuwa na yakini kuwa ipo siku atashinda mpaka Mwenyezi Mungu aliponiingiza katika Uislamu. Ibn an-Nadhur gavana wa Iylau na Harqal askofu wa Wakristo wa Sham walikuwa wakisimulia kuwa pindi Harqal alipofika Iylau aliamka siku moja akiwa mnyonge wa nafsi, baadhi ya viongozi wa Urumi wakasema: 'Hatujapendezwa na mwonekano wako.' Ibn an-Nadhur anasema: Harqal alikuwa ni mnajimu, hivyo walipomuuliza kuhusu hali yake aliwaambia: 'Jana usiku nilipotazama katika nyota nilimuona mfalmealiyetahiriwa amedhihiri. Ni nani aliyetahiriwa katika ummah huu?' Wakasema: 'Hakuna wanaotahiriwa isipokuwa Mayahudi, hivyo lisikusumbue jambo lao, wewe waandikie barua magavana wa miji yako wawauwe Mayahudi walioko katika miji hiyo.'

"Wakati wakiwa bado wanashauriana juu ya jambo lao, Harqal alikuja na mjumbe aliyetumwa kwake na gavana wa Ghasan akimpa habari za Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Baada ya Harqal kumuhoji alisema: 'Nendeni mkamchunguze, je katahiriwa au la.' Walipomtazama walikuta katahiriwa, na alipomuuliza kuhusu Waarabu, alisema: Huwa wanatahiriwa. Harqal akasema: 'Huyu ndiye mfalme wa ummah huu, amedhihiri.' Kisha Harqal alimwandikia barua rafiki yake wa huko Rumiyyah, naye alikuwa ni kama yeye katika elimu ya unajimu.

"Kisha Harqal aliondoka na kwenda Hamsu. Kabla hajafika Hamsu akapata barua kutoka kwa rafiki yake akiafiki rai ya Harqal ya kuwa Mtukufu Mtume (saww) amedhihiri na kuwa yeye ni Nabii. Hivyo Harqal akawaita viongozi wa Urumi katika Ikulu yake huko Hamsu kisha akaamuru milango yake ifungwe, alipowatokea alisema: 'Enyi watu wa Urumi je mko tayari kumpa utii wenu Nabii huyu ili mfaulu na kuongokewa na ufalme wenu uendelee kubaki?' Walinyanyuka na kutaka kutoka kwa nguvu kama watu waliotawanywa na mnyama mkali, lakini walikuta milango imefungwa. Harqal alipoona jinsi walivyokataa na alipokata tamaa ya wao kuamini, alisema: 'Warudisheni kwangu.' Na akasema: 'Hakika mimi nimesema kauli hii niliyoisema muda mchache uliopita ili tu niwajaribuni na kujua jinsi gani mlivyo imara katika dini yenu, na tayari nimeshaona.' Basi wakamsujudia na kumridhia, na huo ndio ukawa mwisho wa jambo la Harqal."- Amesema: Ameipokea Salih bin Kaysan na Yunus na Maamar kutoka kwa az-Zahriy.

**Nasema:** Hadithi hii kaipokea pia Bukhari[221] na Muslim[222] kwa njia tofauti tofauti.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA JINSI IBN SALAM ALIVYOTAMBUA KUWA MTUKUFU MTUME HASEMI UWONGO, NA AKATAJA JINSI ANAVYOTEKELEZA AHADI YAKE

**Sahih Ibn Majah Uk. 95[223]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Salam, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipofika Madina watu walimkusanyikia, na pakasemwa: 'Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amekuja.' Nikaja katikati ya watu ili nimuone. Nilipoutazama uso wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) niligundua kuwa uso wake si uso wa mtu muongo, jambo la kwanza aliloongea ni: 'Enyi watu! Toeni salamu, lisheni chakula, swalini Swala za usiku wakati watu wamelala, mtaingia peponi."

[221] *Sahih Bukhari:* Mlango unaozungumzia jinsi wahyi ulivyoanza kuteremka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).
[222] *Sahih Muslim*: Mlango wa barua ya Mtume kwa Harqal akimwita katika Uislamu.
[223] *Sahih Ibn Majah*: Kitabu kunachozungumzia kusimamisha Swala na Sunna yake, Mlango wa maelezo yaliyokuja kuhusu Swala ya usiku, Hadithi ya 13334.

**Usudul-Ghabah Juz. 3, Uk. 146[224]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Abil-Hamsai kuwa alisema: Nilimpa kiapo cha utii Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hata kabla hajawa Nabii. Nilimwahidi kuwa nitakwenda kumpa kiapo cha utii pale pale alipokuwa, lakini siku hiyo na siku iliyofuata nikasahau kwenda. Nilikwenda siku ya tatu akiwa pale pale alipokuwa, akaniambia: "Ewe kijana, bila shaka una shauku na mimi, nami ningali hapa siku ya tatu sasa nakungojea."

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA KUWA HAKIKA MTUKUFU MTUME ANAWAPENDA MASIKINI NA ANACHUKIA KUWAONA WATU WAKIMSIMAMIA, WAKIBUSU MKONO WAKE AU KUTEMBEA NYUMA YAKE

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 56[225]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Ewe Mungu Wangu, Niache hai nikiwa masikini na nifishe nikiwa masikini, na siku ya Kiyama nifufue katika kundi la masikini." Aisha akasema: "Kwa nini ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu!" Akasema: "Hakika wao wataingia peponi miaka arubaini kabla ya matajiri wao, ewe Aisha! Usimfukuze masikini hata kwa kipande cha tende, ewe Aisha! Wapende masikini na kuwa karibu nao, hakika Mwenyezi Mungu atakusogeza karibu Yake Siku ya Kiyama.

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 4, Uk. 322[226]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Said, amesema: Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: "Ewe Mungu Wangu, Niache hai nikiwa masikini na nifishe nikiwa masikini, na Siku ya Kiyama nifufue katika kundi la masikini. Na hakika muovu zaidi ya waovu wote ni yule aliyekusanyikiwa na ufakiri wa dunia na adhabu ya Akhera."

Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 125[227]:

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas, amesema: Hapakuwa na mtu wampendaye zaidi kuliko Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Walikuwa hawasimami wanapomuona kwa kuwa walikuwa wanajua kuwa anachukizwa na hilo (la kusimamiwa).

**Sahih Abi Daud Juz. 32, Uk. 224[228]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Umamah, amesema: "Alitutokea Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa anachechemea kwa fimbo yake, nasi tukasimama, akasema: 'Msisimame kama wanavyosimama wasiokuwa Waarabu kwa kutukuzana wao kwa wao.'"

---

224 *Usudul-Ghabah*: Herufi Ain, Wasifu wa Abdullah bin Abil-Hamsai.

225 *Sahih Tirmidhiy:* Kitabu kinachozungumzia kujinyima dunia, Mlango unaosema mafakiri waliohama wataingia peponi kabla ya matajiri wao, Hadithi ya 2352.

226 *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha watumwa, Mlango usemao kuwa muovu zaidi ya waovu wote ni yule aliyekusanyikiwa na ufakiri wa dunia na adhabu ya Akhera.

227 *Sahih Tirmidhiy:* Kitabu cha adabu, Mlango unaozungumzia karaha ya mtu kumsimamia mtu mwingine, Hadithi ya 2754.

228 *Sahih Abi Daud*: Kitabu cha adabu, Mlango unaozungumzia mtu kumsimamia mtu mwingine, Hadithi ya 5230.

**Mizanul-Iitidal Juz. 2, Uk. 105[229]:**

Ametaja hadithi kwa njia ya Abu Huraira kuwa alisema: "Niliingia sokoni pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), akaketi kwa wauza nguo na akanunua suruwali kwa dirhamu nne.Watu wa sokoni walikuwa na kipimo wanachopimia dirhamu, ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia muuzaji: 'Ukipima nitashinda.' Mpimaji akasema: 'Sijawahi kusikia neno hili kutoka kwa yeyote.'"

Abu Huraira anasema: "Nikamwambia mpimaji: Hebu acha udhaifu na kuficha dini yako, hivi humjui Nabii wako? Akatupa kipimo na kuirukia mikono ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kuanza kuibusu. Mtume akaiondoa kwake na kusema: 'Haya hufanywa na wasiokuwa Waarabu kuwafanyia wafalme wao na mimi si mfalme, mimi ni mtu miongoni mwenu.' Akapima na akashinda na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akachukua suruwali."

Abu Huraira anasema: "Nilikwenda ili nimbebee lakini akasema: 'Mwenye mali ana haki zaidi ya kubeba mali yake isipokuwa kama ni dhaifu au hana uwezo wa kuibeba hapo ndipo anasaidiwa na nduguye mwislamu.' Nikamwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Hivi na wewe unavaa suruwali? Akasema: 'Ndiyo, safarini na nyumbani, usiku na mchana, hakika mimi nimeamrishwa kujisitiri na sijapata kitu chenye kusitiri zaidi kushinda yenyewe."' - Amesema: Ameipokea Ibn Haban kutoka kwa Abu Ya'ala kutoka kwake (Abu Huraira).

**Taarikh Baghdad Juz. 12, Uk. 91[230]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Nilitembea nyuma ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ili nimjaribu na kuona je anachukia mimi kutembea nyuma yake au anapenda hilo? Basi alinishika mkono na kuniweka sawa na yeye na nikatembea pembeni yake. Kisha nilibaki nyuma tena na kuanza kutembea nyuma yake, akanishika mkono na kuniweka usawa na yeye, nikagundua kuwa anachukizwa na hilo.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA MIZAHA YA MTUKUFU MTUME (SAWW) NA TABASAMU LAKE

**Sahih Tirmidhiy Juz. 1, Uk. 359[231]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kuwa alisema: "Walisema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Hakika wewe unatufanyia mzaha.' Akasema: 'Hakika mimi sisemi isipokuwa haki.'"

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk.287[232]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin al-Harith bin Hazmi, amesema: "Sijapata kumuona mtu mwenye tabasamu nyingi kumshinda Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)."

---

[229] *Mizanul-Iitidal*: Heruf Ain, Wasifu wa Abdurahman bin Ziyad al-Ifriqiy, Namba 4866.

[230] *Taarikh Baghdad*: Wasifu wa Ali bin Muhammad as-Siybiy al-Qasriy, Namba 6508.

[231] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha kufanya wema na kuunga udugu, Mlango unaozungumzia yaliyosemwa kuhusu mizaha, Hadithi ya 1990.

[232] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha fadhila, Mlango unaozungumzia bashasha ya Mtukufu Mtume (saww), Hadithi ya 3641.

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 287[233]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin al-Harith bin Hazmi, amesema: "Uchekaji wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) haukua zaidi ya tabasamu."

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 287[234]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir bin Samrah kuwa alisema: "Katika muundi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kulikuwa na wembamba, na alikuwa hacheki zaidi ya tabasamu, na kila nilipokuwa nikimtazama nilikuwa nikijisemea moyoni: 'Kapaka wanja macho yake,' wakati hajapaka.'"

**Sunanul-Bayhaqiy Juz. 7, Uk. 52[235]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Samak bin Harb kuwa amesema: "Nilimwambia Jabir bin Samrah: Je ulikuwa unakaa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu! Akasema: 'Ndiyo, alikuwa mwingi wa ukimya, mchache wa kucheka, na kuna wakati Masahaba zake walikuwa wakisoma mashairi mbele yake au mambo yao, wao wanacheka lakini yeye huenda akatabasamu tu.'"

**Taarikh Baghdad Juz. 8, Uk. 308[236]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Akrimah kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: "Kulikuwa na mizaha kwa Mtume (saww)."

**Mirqatul-Mafatih Juz. 4, Uk. 650: Katika matini[237]:**

Amesema: Kutoka kwa Anas kutoka kwa Mtukufu Mtume (saww), alimwambia mwanamke ajuza: "Ajuza hataingia peponi." Mwanamke yule alikuwa akisoma Qur'ani, hivyo akasema: "Wao watapata nini?" Akamwambia: "Hujasoma Qur'ani: **'Hakika Sisi tutawaumba upya. Na tutawafanya vijana.'"**

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9, uk. 17[238]:**

Amesema: Kutoka kwa Jabir, amesema: "Ilikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) anapofikiwa na wahyi au anapotoa waadhi, mimi husema: 'Ni mwenye kuwaonya watu waliofikiwa na adhabu.' Hali hiyo ikimuondoka, namuona akiwa na uso mkunjufu kushinda watu wote, mwenye kucheka zaidi yao na mwenye furaha kushinda wao."

**Nasema:** Si rahisi Mtume (saww) kuwa mwenye kucheka zaidi yao kama ilivyo katika riwaya ya mwisho. Lakini ni rahisi baada ya kutambua kuwa kutabasamu ndio kucheka kwake kama ilivyo katika riwaya ya tatu na ya nne, hivyo maana yake itakuwa: Alikuwa mwingi wa tabasamu kushinda wao, na hapo riwaya hii itaafikiana na riwaya ya pili. Ndiyo, imebaki riwaya ya al-Bayhaqiy isemayo: 'Ndiyo, alikuwa mwingi wa ukimya, mchache wa kucheka' hapo ni kucheka kwa maana yake halisi, na hivyo baada ya kukusanya riwaya zote za mlango huu tunapata kuwa yeye (saww) alikuwa mchache wa kucheka, mwingi wa tabasamu kuliko wao na mwenye uso mkunjufu kuliko wao na mwenye furaha kushinda wao.

---

[233] *Sahih Tirmidhiy:* Kitabu cha fadhila, Mlango unaozungumzia bashasha ya Mtukufu Mtume (saww), Hadithi ya 3642.
[234] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha fadhila, Mlango unaozungumzia sifa za Mtukufu Mtume (saww), Hadithi ya 3645.
[235] *Sunanul-Bayhaqiy*: Kitabu cha ndoa, Mlango usemao: Mtu hakuwa akitaka kuiona haki na kuishi vizuri na watu, Hadithi ya 13339.
[236] *Taarikh Baghdad*: Wasifu wa Khalid bin Ziyad az-Zayat, Namba 4407.
[237] *Mirqatul-Mafatihi* Juz. 4, Uk. 650.
[238] *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid*: Mlango unaozungumzia uzuri wa tabia zake (saww) na kuishi kwake vizuri na watu.

## MLANGO UNAOSEMA KUWA MTUKUFU MTUME (SAWW) ALIKUWA MBALI NA MADHAMBI KULIKO WATU WOTE, NA ALIKUWA AKIHARAKISHA KUGAWA MALI YA MWENYEZI MUNGU

**Sahih Bukhari: Kitabu kinachozungumzia mwanzo wa uumbaji, Mlango wa sifa za Mtukufu Mtume (saww):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hakupewa khiyari ya kuchagua moja kati ya mambo mawili isipokuwa alichagua lililo jepesi maadamu tu jambo hilo si dhambi, kama ni dhambi basi yeye atakuwa mbali nalo kushinda watu wote. Na wala Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hakuwahi kulipiza kisasi kwa ajili yake mwenyewe, isipokuwa ikivunjwa heshima ya Mwenyezi Mungu, hapo hulipiza kwa ajili ya Mwenyezi Mungu."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 4, Uk. 384[239]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aqabah bin al-Harith kuwa alisema: "Niliswali Laasiri pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), alipotoa salamu alisimama haraka na kuingia katika nyumba ya mmoja kati ya wakeze, kisha alitoka, akaona alama ya mshangao katika nyuso za jamaa kutokana na yeye kufanya haraka, akasema: 'Wakati nikiwa katika Swala nilikumbuka tunadhahabu mbichi iliyopo kwetu, hivyo sikupenda ishinde na ilale kwetu, hivyo nimeamrisha igaiwe.''

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 6, Uk. 104[240]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Musa bin Jubair, kutoka kwa Abu Umamah bin Sahli, amesema: "Niliingia siku moja mimi na Ur'wah bin Zubair kwa Aisha, akasema: 'Natamani mngemuona Mtume (saww) siku alipotokewa na ugonjwa, alikuwa na dinari zake kwangu, hivyo akaniamuru nizigawe, lakini maumivu ya Mtume (saww) yalinisahaulisha mpaka Mwenyezi Mungu alipomuafu (na hivyo sikuweza kuzigawa). Kisha aliniuliza kuhusu dinari hizo, akasema: 'Umezifanya nini zile dinari sita au saba?' Nikasema Wallahi maumivu yako yalinisahaulisha. Akaomba nimpe, nikampa akazimwaga katika kitanga chake na kusema: 'Hivi angefanywa nini Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kama angekutana na Mwenyezi Mungu na hali hizi zikiwa kwake.'"

**Hilyatul-Awliyai Juz. 8, Uk. 127[241]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: "Siku moja Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alitoka huku akiwa na kipande cha dhahabu mkononi, akamwambia Abdullah bin Umar: 'Muhammad atamwambia nini Mola Wake ikiwa atakutana naye huku akiwa na hiki?' akakigawa kabla hajasimama…"

Tutaikamilisha hadithi hii inshaallah katika Mlango unaozungumzia maisha ya Mtume (saww) na kujinyima kwake.

[239] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Hadithi ya Aqabah bin al-Harith, Hadithi ya 18933.
[240] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Hadithi ya Sayyidah Aisha, Hadithi ya 24212.
[241] *Hilyatul-Awliyai:* Wasifu wa al-Fadhil bin Iyadh, Hadithi alizopokea al-Fadhil kutoka kwa Maimamu wa Tabiina kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

**Usudul-Ghabah Juz. 1, Uk. 28[242]:**

Aisha amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa na dinari sita, akatoa nne zikabaki mbili, akashindwa kulala, Aisha alipomuuliza alimweleza sababu, Aisha akamwambia: Utakapoamka utaziweka mahala pake, Mtume akasema: 'Ni nani aliyenihakikishia kuwa nitafika asubuhi?'"

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 10 Uk. 238[243]:**

Amesema: Kutoka kwa Ummu Salmah amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliingia kwangu akiwa kakunja uso, nikahofia kuwa huenda ni kutokana na maumivu, nikamwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kwa nini umekunja uso? Akasema: 'Ni kwa ajili ya dinari saba ambazo zilitufikia jana, na leo tumeshinda zikiwa chini ya tandiko."' Na katika riwaya nyingine alisema: "Zilitufikia lakini hatujazitoa."

— Amesema: Kaipokea Ahmad na Abu Ya'ala, na wapokezi wao ni wapokezi sahihi.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA KUKETI KWA MTUKUFU MTUME (SAWW) NA MALAIKA KUTEMBEA NYUMA YAKE

**Sahihi Abi Daud Juz. 3, Uk. 190[244]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Salam, kutoka kwa baba yake, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa anapoketi kuzungumza, anakithirisha kutazama mbinguni."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 2, Uk. 21[245]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Umar, amesema: "Hakika tulikuwa tukimhesabia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), katika baraza moja alikuwa akisema: 'Ewe Mola! Nisamehe na nikubalie toba, hakika wewe ni Mwingi wa kukubali toba na Mwingi wa kusamehe.' Mara mia moja."

**Nasema:** Ameipokea pia Ibn Majah katika *Sahih*[246] yake kutoka kwa Ibn Umar, na amesema: Wewe ni Mwingi wa kukubali toba Mwingi wa kurehemu.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 3, Uk. 332[247]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir kuwa amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa anapotoka nyumbani kwake, sisi hutumbea mbele yake na kuuwacha mgongo wake kwa ajili ya Malaika."'

[242] *Usudul-Ghabah:* Kutaja sehemu ya tabia zake na miujiza yake (saww).
[243] *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid*: Mlango wa kutoa na kubana.
[244] *Sahih Abi Daud*: Kitabu cha adabu, Mlango wa maneno yenye uongofu, Hadithi ya 4837.
[245] *Musnad Abdullah bin Umar*, Hadithi ya 4712.
[246] *Sunan Ibn Majah*: Kitabu cha adabu, Mlango wa kuomba msamaha, Hadithi ya 3814.
[247] *Musnad Jabir bin Abdullah*, Hadithi ya 14146.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 3, Uk. 398[248]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir bin Abdullah –katika hadithi ndefu – amesema katika hadithi hiyo: "Alipomaliza – yaani Mtume – alisimama yeye na wakasimama Masahaba zake mbele yake, na alikuwa akisema: 'Uacheni mgongo wangu kwa ajili ya Malaika.'"

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA FADHILA ZA KUMSWALIA MTUKUFU MTUME (SAWW)

**Sunanud-Daramiy Juz. 2, Uk. 317[249]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Abu Talha kutoka kwa baba yake, amesema: "Siku moja Mtukufu Mtume (saww) alikuja huku furaha ikionekana katika uso wake. Pakasemwa: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Hakika sisi tunaona furaha usoni kwako, furaha ambayo hatukuwa tunaiona. Akasema: 'Ndio, hakika Malaika amenijia na kuniambia: Ewe Muhammad hakika Mola Wako anakuambia: Hivi huridhiki kuwa hakuswalii mtu yeyote kutoka katika ummah wako isipokuwa nami humswalia mara kumi, na wala hakutolei salamu yeyote isipokuwa na mimi humtolea salamu mara kumi? Nikasema ndio nimeridhia."'

**Taarikh Baghdad Juz. 8, Uk. 41[250]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Talha, amesema: "Siku moja niliingia kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na siku hiyo sikumuona mtu aliyekuwa na furaha zaidi na mwenye nafsi safi kushinda yeye, nikamwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kwa haki ya baba yangu na mama yangu, Wallahi sijawahi kukuona ukiwa na furaha na mwenye nafsi safi kushinda leo hii, akasema: 'Ewe Abu Talha! Kitu gani kitanizuia nisiwe hivyo? Wakati ni punde tu Jibril kaachana na mimi na ameniambia: Ewe Muhammad! Hakika Mola Wako kanituma kwako akisema: Hakika hakuna mtu katika ummah wako atakayekuswalia isipokuwa Mwenyezi Mungu atamswalia kama alivyokuswalia, la sivyo atamwandikia mema kumi kwa swala hiyo, atamfutia madhambi kumi na atamnyanyua kwayo daraja kumi. Na haitaishia swala hiyo isipokuwa karibu na Arshi, na haitapita kwa Malaika yeyote isipokuwa atasema: Mswalieni mwenyewe kama alivyomswalia Muhammad."'

**Taarikh Baghdad Juz. 8, Uk. 381[251]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Atakayeniswalia mara moja Mwenyezi Mungu atamswalia mara kumi, na atamfutia madhambi kumi."'

**Taarikh Baghdad Juz. 2, Uk. 250[252]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah, kutoka kwa Mtukufu Mtume (saww) kutoka kwa Jibril, kutoka kwa Mikail, kutoka kwa Israfil, kutoka kwa Rafiu, kutoka kwenye ubao uliohifadhiwa, kutoka

---

[248] *Musnad Jabir bin Abdullah,* Hadithi ya 14857.
[249] *Sunanud-Daramiy*: Mlango unaozungumzia fadhila za kumswalia Mtukufu Mtume (saww).
[250] *Taarikh Baghdad*: Wasifu wa Husain bin Khalid Abi al-Junaydi kipofu, Namba 4097.
[251] *Taarikh Baghdad*: Wasifu wa Daud bin Sulayman Abul-Hasan al-Bazaz, Hadithi ya 4487..
[252] *Taarikh Baghdad*: Wasifu wa Muhammad bin Husain bin al-Khaffaf, Hadithi ya 719.

kwa Mwenyezi Mungu kuwa aliandika katika ubao kuwa ubao umwambie Rafiu, na Rafiu amwambie Israfil, na Israfil amwambie Mikail, na Mikail amwambie Jibril, na Jibril amwambie Muhammad (saww) kuwa: Atakayekuswalia mara mia moja mchana na usiku nitamswalia mara elfu mbili, nitamkidhia haja elfu moja, na ndogo kabisa ni kumwepusha na moto.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA SWALA YA MTUKUFU MTUME (SAWW)

**Sahih Bukhari: Kitabu kinachozungumzia tahajudi, Mlango unaozungumzia Swala za usiku za Mtukufu Mtume (saww):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa al-Mughirah amesema: "Hakika Mtukufu Mtume (saww) alikuwa akisimama na kuswali mpaka nyayo zake zinavuja jasho au miundi yake, anapoambiwa husema: 'Hivi hamtaki niwe mja mwenye kushukuru.'"

**Sahih Bukhari: Kitabu cha tafsiri, Mlango unaozungumzia kauli ya Mwenyezi Mungu: Ili Mwenyezi Mungu akughufuri:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa akisimama usiku mpaka nyayo zake zinavuja jasho, Aisha akamwambia: "Kwa nini unafanya hivi ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Wakati Mwenyezi Mungu ameshakusamehe dhambi zilizotangulia na zijazo?" Akasema: "Kwa nini nisiwe mja mwenye kushukuru?.."

**Sahih Bukhari: Kitabu cha tahajudi, Mlango unaozungumzia kurefusha kisimamo cha usiku:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah kuwa alisema: "Niliswali pamoja na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika usiku mmoja, aliendelea kusimama mpaka nikakusudia kutenda jambo baya." Tukamuuliza ni jambo gani ulilokusudia? Akasema: "Nilikusudia kukaa na kumsukuma Mtume."

**Sahih Bukhari: Kitabu cha tahajudi, Mlango unaozungumzia kusimama kwa Mtukufu Mtume kwa ajili ya Swala ya usiku katika mwezi wa Ramadhani na miezi mingine:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Salmah bin Abdurahman kuwa alimuuliza Aisha: "Ilikuwaje Swala ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ndani ya mwezi wa Ramadhani?" Akasema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hakuwa anazidisha rakaa kumi na moja, si katika mwezi wa Ramadhani au mwezi mwingine. Alikuwa akiswali rakaa nne ambazo usiseme kuhusu uzuri wake na urefu wake, kisha husali nyingine nne ambazo nazo usiseme kuhusu uzuri wake na urefu wake, kisha husali tatu. Siku moja nikamwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Utalala kabla ya kuswali witiri? Akasema: 'Ewe Aisha! Hakika macho yangu yanalala lakini moyo wangu haulali.'"

**Sahih Bukhari: Kitabu cha Swaumu, Mlango unaosema: Je alikuwa akichagua siku maalumu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Alqamah, alisema: Nilimwambia Aisha: "Je Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa akichagua siku maalumu? Akasema: 'Hapana, amali yake ilikuwa ya kudumu, na ni nani miongoni mwenu anaweza kufanya aliyokuwa anayaweza Mtume wa Mwenyezi Mungu!?'"

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 152[253]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ya'ala bin Mamlak kuwa alimuuliza Ummu Salama mke wa Mtukufu Mtume (saww) kuhusu kiraa cha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na Swala yake, akasema: "Mna jambo gani na Swala yake? Alikuwa akiswali kisha analala kadiri alivyoswali, kisha anaswali kadiri alivyolala, kisha analala kadiri alivyoswali mpaka asubuhi inaingia, nilifuatilia kiraa chake nikakikuta ni kiraa cha herufi kwa herufi."

**Sahih Tirmidhiy Juz. 1, Uk. 90[254]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha kuwa alisema: "Alisimama Mtume (saww) kuswali usiku kwa kusoma Aya ya Qur'ani usiku mzima."

**Sahih an-Nasaiy Juz. 1, Uk. 140[255]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aswim bin Dhamarah amesema: "Nilimuuliza Ali bin Abu Talib (as) kuhusu Swala ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mchana kabla ya Swala ya faradhi, akasema: 'Ni nani anaweza hilo?'"

**Sahih an-Nasaiy Juz. 1, Uk. 156[256]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Dhari kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisimama usiku kuswali kwa kusoma Aya moja mpaka asubuhi ikaingia, na Aya yenyewe ni: **Ukiwaadhibu basi hao ni waja wako. Na ukiwasamehe basi Wewe ndiye Mwenye nguvu na Mwenye hikima**."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 5, Uk. 400[257]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Hudhayfa kuwa alisema: "Nilikuja kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika usiku wa Ramadhan, akasimama kuswali, alipotoa takbira alisema: 'Mungu mkuu mwenye ufalme, ujabari kiburi na adhama.' Kisha alisoma Sura al-Baqarah, kisha an-Nisaa, kisha Aali Imran. Hakuwa anapita katika Aya ya kuhofisha isipokuwa alisimama hapo, kisha alirukuu na kusema: 'Utakatifu ni wa Mola Wangu Adhimu.' Kadiri ileile ya muda alioutumia katika kusimama, kisha aliinua kichwa chake na kusema: 'Mwenyezi amemsikia aliye muhimidi, Mola Wetu himidi njema ni zako.' Kadiri ileile ya muda alioutumia katika kusimama, kisha alisujudu na kusema: 'Utakatifu ni wa Mola Wangu aliye juu.' Kadiri ileile ya muda alioutumia katika kusimama, kisha alinyanyua kichwa chake na kusema: 'Mola nisamehe.' Kadiri ileile ya muda alioutumia katika kusimama, kisha alisujudu na kusema: 'Utakatifu ni wa Mola wangu aliye juu.' Kadiri ileile ya muda alioutumia katika kusimama, kisha alinyanyua kichwa chake na kusimama. Hakuswali isipokuwa rakaa mbili na Bilal akawa amefika na kumwadhinia kwa ajili ya Swala."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 3, Uk. 101[258]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa akifupisha Swala na kuikamilisha."

[253] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha fadhila za Qur'ani, Mlango unaozungumzia jinsi Mtume alivyokuwa akisoma, Hadithi ya 2923.
[254] *Sahih Tirmidhiy*: Milango ya Swala, Mlango unaozungumzia kiraa cha usiku, Hadithi ya 448.
[255] *Sahih an-Nasaiy*: Kitabu cha uimamu, kuswali kabla ya Laasiri, Hadithi ya 874.
[256] *Sahih an-Nasaiy*: Kitabu cha ufunguzi, Mlango wa kurudia Aya, Hadithi ya 1009.
[257] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Hadithi ya Hudhayfa bin al-Yaman, Hadithi namba 22890.
[258] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Musnad Anas bin Malik, Hadithi ya 11579.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 3, Uk. 173[259]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa akifupisha Swala kushinda watu wote na akiikamilisha."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 3, Uk. 233[260]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik kuwa alisema: "Sijapata kuswali nyuma ya Imamu mwenye kufupisha Swala na kuikamilisha kumshinda Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) anaposikia mtoto akilia hufupisha Swala akihofia ummah wake usije ukaingia majaribuni."

**Nasema:** Riwaya hii ndio yenye hitimisho lenye kukusanya riwaya zenye kuonesha kuwa alikuwa akirefusha Swala yake na zile zenye kuonesha kuwa alikuwa akifupisha Swala yake. Alikuwa anafupisha katika jamaa na alikuwa anarefusha nje ya jamaa.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 4, Uk. 302[261]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa al-Barau kuwa alisema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisoma: **'Naapa kwa tini na Zaituni.'** Sijapata kumsikia mtu mwenye kusoma vizuri kushinda yeye anaposoma.

**Kanzul-Ummal Juz. 1, Uk. 273[262]:**

Amesema: Kutoka kwa Ali (as) amesema: "Ilipoteremka: **'Ewe uliye jifunika! Kesha usiku kucha, ila kidogo tu!'** alisimama usiku wote mpaka nyayo zake zikavimba, akawa anainua mguu mmoja na kusimamia mmoja, Jibril akateremka na kumwambia: **Twaha!** ikanyage ardhi kwa nyayo zako ewe Muhammad, **Hatukukuteremshia Qur'ani ili upate mashaka.**'"

Amesema: Kaiandika Ibn Mardawayhi.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA KULIA KWA MTUKUFU MTUME KATIKA SWALA NA PINDI ANAPOSOMA QUR'ANI TUKUFU

**Sahih Abi Daudi Juz. 5, Uk. 91[263]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Mutrif kutoka kwa baba yake kuwa alisema: "Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiswali na kifuani kwake kukitoka mngurumo kutokana na kulia kama mngurumo wa jiwe la kusagia."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 1, Uk. 374[264]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa IbnMas'ud kuwa alisema: "Nilisoma kuanzia Sura an-Nisaa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), nilipofika Aya hii: **'Basi itakuwaje pindi tukiwaletea ku-**

[259] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal:* Musnad Anas bin Malik, Hadithi ya 12362.
[260] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Musnad Anas bin Malik, Hadithi ya 13033.
[261] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Hadithi ya al-Barau bin Azib, Hadithi ya 18206.
[262] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha nyuradi, sehemu ya vitendo, Mlango unaozungumzia fadhila za sura za Qur'ani, Sura Muzammil.
[263] *Sahih Abi Daud*: Kitabu cha Swala, Mlango unaozungumzia kulia ndani ya Swala, Hadithi ya 904.
[264] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Musnad Abdullah bin Mas'ud, Hadithi ya 3541.

**toka kila ummah shahidi, na tukakuleta wewe kuwa shahidi wa hawa?’** macho yake yakabubujika machozi.”

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 1, Uk. 380[265]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah, amesema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: “Nisomee.’ Nikamwambia: Nikusomee ilihali imeteremka kwako? Akasema: ‘Hakika mimi napenda niisikie ikisomwa na mwingine asiye kuwa mimi.’ Nikamsomea na nilipofika: **‘Basi itakuwaje pindi tukiwaletea kutoka kila ummah shahidi, na tukakuleta wewe kuwa shahidi wa hawa?’** Nikaona macho yake yakibubujika machozi.”

## MLANGO UNAOSEMA KUWA MTUKUFU MTUME (SAWW) ALIBEBA TOFALI LA KUJENGEA MSIKITI NA ALIBEBA UDONGO SIKU YA HANDAKI. NA UNABAINISHA SEHEMU YA MASHAIRI YAKE

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 2, Uk. 381[266]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kuwa alisema: “Walikuwa wakibeba matofali ya kujengea msikiti na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa pamoja nao.” Abu Huraira anasema: “Nikakutana na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa amebeba tofali sawa na tumbo lake, nikadhani kuwa limemshinda, nikamwambia: Nipe nilibebe ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Akasema: ‘Chukua jingine ewe Abu Huraira, hakika hakuna maisha mazuri isipokuwa maisha ya Akhera.”’

**Mushkilatul-Athar Juz. 4, Uk. 299[267]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa al-Barau bin Azib kuwa alisema: “Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akibeba udongo siku ya handaki mpaka udongo ukajaa kwenye nywele za kifuani kwake huku akisoma shairi la Abdullah bin Rawaha, akisema: ‘Ewe Mungu Wangu, bila Wewe tusingeongokewa, tusingetoa sadaka wala kuswali. Tuteremshie utulivu na imarisha nyayo zetu siku tutakayokutana. Hakika hawa wametudhulumu na walipotaka fitina tulikataa.’ Alisoma haya kwa sauti yake ya juu.

**Mushkilatul-Athar Juz. 4, Uk. 298[268]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa alisema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alitoka siku moja katika asubuhi yenye baridi kali huku Muhajirina na Ansari wakichimba handaki kwa mikono yao. Akasema: ‘Ewe Mungu Wangu. Maisha hasa ni maisha ya Akhera, wasamehe Muhajirina na Ansari.’ Wakamjibu: ‘Sisi ndio tuliompa kiapo cha utii Muhammad, kuwa tutapigana jihadi maadamu tungali hai.’”

[265] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal:* Musnad Abdullah bin Mas’ud, Hadithi ya 3595.
[266] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Musnad Abuhuraira, Hadithi ya 8728.
[267] *Mushkilul-Athar:* Mlango unaozungumzia maneno yaliyopokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ambayo jamaa zake walidai kuwa ni sehemu ya mashairi, huku wengine wakikanusha.
[268] *Mushkilul-Athar*: Mlango unaozungumzia maneno yaliyopokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ambayo jamaa zake walidai kuwa ni sehemu ya mashairi, huku wengine wakikanusha.

**Mushkilatul-Athar Juz. 4, Uk. 299[269]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jundub kuwa alisema: "Tulikuwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) vitani, kidole chake kikaumia, akasema: 'Wewe si chochote bali ni kidole kilichovuja damu, na haya nimeyapata katika njia ya Mwenyezi Mungu."'

**Sunanul-Bayhaqiy Juz. 7, Uk. 43[270]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hakuwahi kukusanya shairi kamwe isipokuwa ubeti mmoja."

**Nasema:** Imetangulia katika Mlango unaozungumzia ushujaa wake kauli yake ya siku ya Hunayni: "Mimi ni Nabii sisemi uwongo, mimi ni mtoto wa Abdul-Muttalib." Nayo ni maneno yanayoshabihiana na shairi.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA TAWAKALI YA MTUKUFU MTUME (SAWW) KWA MWENYEZI MUNGU

**Sahih Muslim: Kitabu cha fadhila, Mlango unaozungumzia tawakali yake kwa Mwenyezi Mungu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir bin Abdullah, amesema: "Nilipigana vita moja pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kabla ya Najdi, tukamkuta Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika bonde lenye miti mingi yenye miba. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliteremka na kukaa chini ya mti na akautungika upanga wake katika moja ya matawi ya mti ule.Watu walitawanyika katika bonde kutafuta kivuli katika miti. Baadaye Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Hakika kuna mtu mmoja kanijia nikiwa nimelala, alipochukua upanga wangu niliamka na kumkuta amesimama juu ya kichwa changu. Sikuhisi kitu isipokuwa akiwa na upanga unaong'aa mikononi mwake, akaniambia: Ni nani atakuzuia dhidi yangu? Nikamwambia ni Mwenyezi Mungu, akasema mara ya pili ni nani atakuzuia dhidi yangu? Nikamwambia ni Mwenyezi Mungu, akaingiza upanga ndani ya ala yake, na ni huyu hapa ameketi."'

**Nasema:** Katika kitabu *Riyadhus-Salihin* cha an-Nawawi katika mlango wa yakini na tawakali, amesema: "Na katika riwaya nyingine Jabir amesema: 'Tulikuwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika ardhi yenye miti mingi, tulipofika katika mti wenye kivuli kikubwa tulimwacha hapo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), ndipo alikuja mtu mmoja miongoni mwa mushrikina huku upanga wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ukiwa umetungikwa juu ya mti, akauchopoa na kusema: Je wanihofu? Mtume akasema hapana, akasema: Ni nani atakuzuia dhidi yangu? Mtume akasema ni Mwenyezi Mungu.

An-Nawawi anasema: Na katika riwaya ya Abu Bakr al-Ismailiy ndani ya *Sahih* yake amesema: Akasema: 'Ni nani atakuzuia dhidi yangu?' Mtume akasema ni Mwenyezi Mungu, hapo upanga ukadondoka toka mikononi mwake, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akauchukua upanga na kumwambia: 'Ni nani atakuzuia dhidi yangu?' Akasema: 'Kuwa mchukuaji bora.' Mtume akamwambia: 'Je utashahidia kuwa hapana mungu isipokuwa Allah na kwamba hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu?' Akas-

[269] *Mushkilul-Athar*: Mlango unaozungumzia maneno yaliyopokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ambayo jamaa zake walidai kuwa ni sehemu ya mashairi, huku wengine wakikanusha.

[270] *Sunanul-Bayhaqiy*: Kitabu cha ndoa, Mlango unaosema kuwa haikumfaa yeye kujifunza mashairi wala kuandika, Hadithi ya 13291.

ema: 'Hapana, lakini nakuahidi kuwa sintakupiga vita wala sintakuwa pamoja na watu wenye kukupiga vita.' Mtume akamwacha aende zake, alipofika kwa jamaa zake aliwaambia: 'Nimekuja kutoka kwa mtu bora kushinda watu wote."'

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA JINSI MTUKUFU MTUME (SAWW) ALIVYOWATAKA USHAURI MASAHABA ZAKE LICHA YA KUWA YEYE NDIYE MWENYE AKILI ZAIDI KUSHINDA WATU WOTE

Mwenyezi Mungu amesema katika theluthi ya mwisho ya Sura Aali Imran: **"Na shauriana nao katika mambo. Na ukishakata shauri basi mtegemee Mwenyezi Mungu. HakikaMwenyezi Mungu huwapenda wanaomtegemea."**[271]

**Sunanul-Bayhaqiy Juz. 7, Uk. 45[272]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kuwa alisema: "Sikupata kumuona mtu mwenye kupenda kuwashauri masahaba zake kumshinda Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)."

**Hilyatul-Awliyai Juz. 4, Uk. 26[273]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Wahbi bin Munabihu, amesema: "Nilisoma vitabu sabini na moja na nikakuta ndani ya vitabu vyote: Hakika akili ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu kawapa watu wote tangu kuanza kwa dunia mpaka kuisha kwake si chochote ikipimwa na akili ya Muhammad, isipokuwa ni sawa na punje ya mchanga kati ya mchanga wa dunia nzima, na hakika Muhammad ndiye mtu mwenye akili kuwashinda watu wote na ndiye mwenye rai bora kushinda watu wote."

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA MAISHA YA MTUKUFU MTUME (SAWW) NA KUJINYIMA KWAKE

**Sahih Bukhari: Kitabu cha mauzo, Mlango unaozungumzia jinsi Mtume alivyonunua kwa mali kauli:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa alikwenda kwa Mtukufu Mtume (saww) na mkate wa shairi na kilainishi chenye kubadilika harufu. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa keshaweka rehani deraya yake huko Madina kwa Myahudi kwa thamani ya shairi aliyoichukua na kuipa familia yake, na nilimsikia akisema: "Katika familia ya Muhammad hakushindi pishi la ngano, wala hakushindi pishi la matunda, na hakika kwake kuna wanawake tisa."

**Sahih Bukhari: Kitabu cha zawadi, Hadithi ya pili:**

---

[271] **Sura Aaali Imran: 159**.

[272] *Sunanul-Bayhaqiy*: Kitabu cha ndoa, Mlango unaozungumzia ushauri alioamrishwa na Mwenyezi Mungu, Hadithi ya 1330.

[273] *Hilyatul-Awliyai*: Wasifu wa Wahbi bin Munabihu, Neno lake lisemalo kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ndiye mwenye akili kushinda watu wote.

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha kuwa alimwambia Ur'wah mtoto wa dada yake: "Sisi tulikuwa tukitizama mbalamwezi, kisha mbalamwezi kisha mbalamwezi, mbalamwezi tatu katika miezi miwili bila moto kuwashwa ndani ya nyumba yoyote ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)." Nikasema: Ewe mama mdogo mlikuwa mnaishi kwa kitu gani? Akasema: Kwa vyeusi viwili, tende na maji, isipokuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa na jirani ambaye ni Ansari, na alikuwa na wanyama hivyo walikuwa wakimzawadia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) maziwa yao naye anatupa tunakunywa."

**Sahih Bukhari: Kitabu cha jihadi na safari, Mlango unaozungumzia deraya ya Mtukufu Mtume (saww):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alifariki huku deraya yake ikiwa rehani kwa Myahudi kwa thamani ya pishi thelathini za shairi."

**Sahih Bukhari: Kitabu cha vyakula, Hadithi ya pili:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira, amesema: "Mpaka anafariki dunia, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hakuwahi kushiba chakula siku tatu mfululizo."

**Sahih Bukhari: Kitabu cha vyakula, Mlango wa mkate uliolainishwa:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Qatadah kuwa alisema: "Tulikuwa kwa Anas akiwa na mikate yake, akasema: 'Kamwe Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hakuwahi kula mkate uliolainishwa, wala mbuzi choma mpaka anakutana na Mwenyezi Mungu."'

**Sahih Bukhari: Kitabu cha vyakula, Mlango wa mkate uliolainishwa:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Qatadah kuwa alisema: "Kamwe sikuwahi kumuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akilia chakula ndani ya sahani wala akila mkate laini, na kamwe hakuwahikula juu ya meza." Akaulizwa Qatadah: "Walikuwa wanalia juu ya nini?" Akasema: "Juu ya meza."

**Sahih Bukhari: Kitabu cha vyakula, Mlango unaozungumzia chakula alichokuwa akila Mtume (saww) na Masahaba zake:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Hazim, amesema: "Nilimuuliza Sahli bin Saad, nikamwambia: Je Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliwahi kula shairi nyeupe? Akasema: 'Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hakuwahi kuona shairi nyeupe tangu amepewa unabii hadi anachukuliwa na Mwenyezi Mungu.' Nikamwambia: Je mlikuwa na zana za kukobolea katika zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)? Akasema: 'Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hakuwahi kuona zana yoyote ya kukobolea tangu amepewa unabii hadi anachukuliwa na Mwenyezi Mungu.' Nikamwambia: Mliwezaje kula shairi isiyokobolewa? Akasema: 'Tulikuwa tunaisaga na kupuliza, pumba zinaruka kadiri zitakavyoruka na zinazobaki tunatengeneza mikate na tunakula."'

**Sahih Bukhari: Kitabu cha vyakula, Mlango unaozungumzia chakula alichokuwa akila Mtume (saww) na Masahaba zake:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kuwa yeye Abu Huraira alipita sehemu na kuwakuta watu wakiwa na mbuzi choma, wakamkaribisha akakataa kula, kisha akasema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alitoka katika dunia hii bila kushiba mkate washairi."

**Sahih Bukhari: Kitabu cha watuwa, Mlango unaozungumzia jinsi yalivyokuwa maisha ya Mtukufu Mtume (saww) na Masahaba zake, na jinsi walivyojiepusha na dunia:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha kuwa alisema: "Hakika familia ya Muhammad haikuwahi kula milo miwili katika siku moja isipokuwa mmoja utakuwa ni tende."

**Sahih Bukhari: Kitabu cha watuwa, Mlango unaozungumzia jinsi yalivyokuwa maisha ya Mtukufu Mtume (saww) na Masahaba zake, na jinsi walivyojiepusha na dunia:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Ewe Mungu Wangu! Iruzuku familia ya Muhammad chakula." Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha kuwa alisema: "Tandiko la Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) lilikuwa la ngozi na maganda ya mitende."

**Sahih Muslim: Kitabu kinachozungumzia kujinyima, Mlango ulio kabla na mlango usemao: Msiingie katika makazi ya wale waliodhulumu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha mke wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alifariki huku akiwa hajawahi kushiba kwa mkate na mafuta mara mbili katika siku moja."

**Sahih Muslim: Kitabu kinachozungumzia kujinyima, Mlango kabla ya mlango uliotangulia:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha mke wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alifariki huku tukiwa hatujawahi kushiba vyeusi viwili, tende na maji."

**Sahih Muslim: Kitabu kinachozungumzia kujinyima, Mlango kabla ya mlango uliotangulia:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Samak kuwa alisema: "Nilimsikia Nu'man bin Bashir akisema: 'Nyinyi si mnakula na kunywa kadiri mtakavyo? Hakika mimi nilimuona Mtume wenu akiwa hana hata tende ya kujaza tumbo lake."'

**Sahih Muslim: Kitabu cha mavazi na mapambo, Mlango unaozungumzia kuvaa mavazi ya hali ya chini:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha, amesema: "Hakika mto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliokuwa akiegemea ulikuwa umetengenezwa kwa ngozi na maganda ya mitende."

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 57[274]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa akilala siku zenye kufuatana bila kula, huku wakeze wakiwa hawana chakula cha usiku, na mara nyingi mkate wao ulikuwa ni mkate wa shairi."

[274] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu kinachozungumzia kujinyima, Mlango unaozungumzia maisha ya Masahaba wa Mtume (saww) na wakeze, Hadithi ya 2360.

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 59[275]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Talha, amesema: "Tulimshitakia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) njaa, na kila mmoja wetu akaondoa jiwe kutoka tumboni, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaondoa mawe mawili."

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 77[276]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Nimetishwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu katika kadiri ambayo hakuna mwingine atakayetishwa zaidi yangu. Na nimeudhiwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu katika kadiri ambayo hakuna mwingine kaye udhiwa zaidi yangu. Nilikaa siku thelathini mchana na usiku, nikiwa sina mimi wala Bilali chakula cha kuweza mtu mzima kula isipokuwa kidogo sana cha kuweza kufunikwa na kwapa la Bilali.

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk.60[277]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alilala juu ya mkeka, akaamka ukiwa umeathiri mbavu zake, tukasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu!Tukutengenezee cha kutandika. Akasema: 'Wapi na wapi mimi na dunia? Mimi si chochote katika dunia hii isipokuwa ni sawa na mtu aliyepumzika chini ya mti kisha ataondoka na kuuwacha."' - Kisha Amesema: Hadithi hii ni nzuri na sahihi.

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 56[278]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Amamah, kutoka kwa Mtukufu Mtume (saww) kuwa alisema: "Mola Wangu alinipa pendekezo la kutaka kunibadilishia ardhi yote ya Makka iwe dhahabu, nikamwambia: Hapana ewe Mola, lakini mimi nitashiba siku moja na kukaa na njaa siku moja." Alisema tatu au kama idadi hii, "Nitakapokuwa na njaa nitanyenyekea kwako na kukukumbuka, na nitakapokuwa na shibe nitakushukuru na kukuhimidi."

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 57[279]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa haweki kitu akiba kwa ajili ya kesho."

**Sahih Ibn Majah: Milango inayozungumzia kujinyima Uk. 316[280]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kuwa alisema: "Siku moja Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliletewa chakula cha moto, alipomaliza kula alisema: 'Kila himidi njema ni ya Mwenyezi Mungu, tangu siku kadhaa hakijaingia chakula cha moto tumboni mwangu."'

---

275 *Sahih Tirmidhiy:* Kitabu kinachozungumzia kujinyima, Mlango unaozungumzia maisha ya Masahaba wa Mtume (saww), Hadithi ya 2371.

276 *Sahih Tirmidhiy:* Kitabu kinachozungumzia sifa za Kiyama, watumwa na uchamungu, Mlango wa 34, Hadithi ya 2472.

277 *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu kinachozungumzia kujinyima, Mlango wa 44,, Hadithi ya 2377.

278 *Sahih Tirmidhiy:* Kitabu kinachozungumzia kujinyima, watumwa na uchamungu, Mlango unaozungumzia kujizuia na kufanya subira, Hadithi ya 2347.

279 *Sahih Tirmidhiy:* Kitabu kinachozungumzia kujinyima, Mlango unaozungumzia maisha ya Masahaba wa Mtume (saww) na wakeze, Hadithi ya 2362.

280 *Sahih Ibn Majah:* Kitabu kinachozungumzia kujinyima, Mlango unaozungumzia maisha ya familia ya Muhammad (saww), Hadithi ya 4150.

**Sahih Ibn Majah: Milango inayozungumzia kujinyima Uk. 316[281]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Khalid bin Umair kuwa alisema: "Ut'bah bin Ghazawan alituhutubia akiwa juu ya mimbari, akasema: 'Hakika niliiona siku ya saba tukiwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) huku tukiwa hatuna chakula cha kuweza kula isipokuwa majani ya mti, mpaka mashavu yetu ya ndani yakatoa vidonda."

**Sahih Ibn Majah: Milango inayozungumzia vyakula Uk. 247[282]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ummu Ayman kuwa: Nilikoboa unga na kumtengenezea Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kipande cha mkate, akasema: "Kitu gani hiki?" Akasema: "Ni chakula cha nyumbani kwetu, hivyo nimependa nikutengenezee mkate kutokana na unga huu." Akasema: "Rudisha kisha ukande upya."

**Sahih Ibn Majah: Milango inayozungumzia vyakula Uk. 247[283]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alivaa nguo za sufi na viatu vya kushona." Na amesema pia: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikula chakula kisichokuwa kizuri na alivaa nguo hafifu, siku moja Husain aliambiwa: Ni kipi hicho chakula kisichokuwa kizuri? Akasema: Ni shairi ngumu, hakuwa anaweza kuimeza isipokuwa kwa funda la maji."

**Sahih Ibn Majah: Milango inayozungumzia kujinyimaUk. 316[284]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Umar kuwa alisema: "Siku moja Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipita kwetu akatukuta tunafumua nyumba yetu ya miti, akasema: 'Jambo gani hili (mfanyalo)?' Nikasema: 'Ni nyumba yetu ya miti tunaitengeneza.' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Naona jambo (la kujenga nyumba ya Akhera) ni la haraka zaidi kuliko hilo."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 3, Uk. 300[285]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na masahaba zake walikaa siku tatu wakichimba handaki bila kuonja chakula. Wakasema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Hapa kuna jabali gumu. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Linyunyizieni maji.' Wakanyunyizia maji, kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akachukua sururu na kusema: '*Bismillahi*.' Akalipiga mara tatu likapasuka pasuka na kuwa vipande vinyowezekana." Jabir anasema: "Nilipomtazama Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) nikamuona kafunga jiwe kwenye tumbo lake.'"

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 3, Uk. 300[286]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na masahaba zake walipatwa na mchoko mkubwa pindi walipokuwa wakichimba handaki, mpaka Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akafunga jiwe kwenye tumbo lake kutokana na njaa."

281 *Sahih Ibn Majah:* Kitabu kinachozungumzia kujinyima, Mlango unaozungumzia maisha ya masahaba wa Mtukufu Mtume (saww), Hadithi ya 4156.
282 *Sahih Ibn Majah*: Kitabu kinachozungumzia vyakula, Mlango unaozungumzia unga mweupe, Hadithi ya 3336.
283 *Sahih Ibn Majah*: Kitabu kinachozungumzia vyakula, Mlango unaozungumzia mkate wa shairi, Hadithi ya 3347.
284 *Sahih Ibn Majah*: Kitabu kinachozungumzia kujinyima, Mlango unaozungumzia kujenga na kubomoa, Hadithi ya 4160.
285 *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Musnad Jabir bin Abdullah, Hadithi ya 13799.
286 *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Musnad Jabir bin Abdullah, Hadithi ya 13808.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 1, Uk. 300[287]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimgeukia mmoja wao na kusema: 'Naapa kwa yule ambaye nafsi ya Muhammad imo mikononi Mwake, nitafurahi sana kama mtu ataipa familia ya Muhammad dhahabu na niitoe katika njia ya Mwenyezi Mungu, nife siku nitakayokufa na hali sina katika dhahabu hiyo isipokuwa dinari mbili ambazo nitaziacha kwa ajili ya kulipa deni kama lipo.' Na alikufa bila kuacha dinari wala dirhamu wala mtumwa wa kiume wala wa kike. Na aliacha deraya yake ikiwa rehani kwa Myahudi kwa thamani ya pishi thelathini za shairi."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 4, Uk. 150[288]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aqabah bin Aamir al-Jahniy kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipewa zawadi ya kanzu ya hariri, akaivaa na kuwasalishia watu Swala ya Maghrib, alipotoa salamu ya kumaliza Swala yake, aliivua kwa nguvu na kuitupa. Tukamwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Umeivaa na kuswalia. Akasema: 'Hakika hili halifai kwa wachamungu."'

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 6, Uk. 104[289]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Musa bin Jubair, kutoka kwa Abu Umamah bin Sahli, amesema: "Niliingia siku moja mimi na Ur'wah bin Zubair kwa Aisha, akasema: 'Natamani mngemuona Mtume (saww) siku alipotokewa na ugonjwa, alikuwa na dinari zake kwangu, hivyo akaniamuru nizigawe, lakini maumivu ya Mtume (saww) yalinisahaulisha mpaka Mwenyezi Mungu alipomuafu (na hivyo sikuweza kuzigawa). Kisha aliniuliza kuhusu dinari hizo, akasema: 'Umezifanya nini zile dinari sita au saba?' Nikasema Wallahi maumivu yako yalinisahaulisha. Akaomba nimpe, nikampa akazimwaga katika kitanga chake na kusema: 'Hivi angefanywa nini Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kama angekutana na Mwenyezi Mungu na hali hizi zikiwa kwake.'"

**Nasema:** Hadithi hii tumeshaitaja katika mlango usemao kuwa Mtukufu Mtume (saww) alikuwa ni mtu aliye mbali zaidi na madhambi na aharakishaye kugawa mali ya Mwenyezi Mungu kushinda watuwote. Rejea huko.

**Hilyatul-Awliyai Juz. 8, Uk. 127[290]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: "Siku moja Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alitoka huku akiwa na kipande cha dhahabu mkononi, akamwambia Abdullah bin Umar: 'Muhammad atamwambia nini Mola Wake ikiwa atakutana naye huku akiwa na hiki?' akakigawa kabla hajasimama, kisha akasema: 'Nitafurahi sana kama nitaona Sahaba wa Muhammad amepata dhahabu mfano wa mlima huu – akaashiria mlima wa uhudi – kisha aitoe katika njia ya Mwenyezi Mungu na kuacha dinari tu katika dhahabu yote hiyo.'" Ibn Abbas anasema: "Na alikufa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) bila kuacha dinari wala dirhamu wala mtumwa wa kiume wala wa kike, na aliacha deraya yake ikiwa rehani kwa Myahudi kwa thamani ya pishi thelathini za shairi ambazo alikuwa akizitumia kwa chakula chake na cha familia yake."

---

287 *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Musnad Abdullah bin Abbas, Hadithi ya 2719.

288 *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Hadithi ya Aqabah bin Aamir al-Jahniy, Namba 16901.

289 *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Hadithi ya Sayyidah Aisha, Namba 24212.

290 *Hilyatul-Awliyai:* Wasifu wa al-Fadhil bin Iyadh, Hadithi alizopokea al-Fadhil kutoka kwa Maimamu wa Tabiina kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

**Hilyatul-Awliyai Juz. 7, Uk. 262[291]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Zaid bin Thabit kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alilala juu ya mkeka na ukaacha athari katika mbavu zake, Aisha akamwambia: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kisra na Kaysari wako katika ufalme adhimu lakini wewe Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hauna kitu, unalala juu ya mkeka na unavaa nguo mbaya.' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: 'Ewe Aisha! Laiti nikitaka mlima utembee na mimi huku ukiwa ni dhahabu tupu utatembea. Jibril alinipa funguo za hazina ya dunia nasijamrudishia, hembu funua mkeka.' Alipofunua akakuta chini ya kila kona ya mkeka kuna ubao wa dhahabu ambao mtu mzima ndio awezaye kuubeba. Akamwambia: 'Itizame ewe Aisha, hakika dunia haizifikiikheri za Mwenyezi Mungu (siku ya Kiyama) hata kwa kadiri ya ubawa wa mbu.' Kisha mbao zile zilitoweka."

**Tabaqat Ibn Saad Juz. 1, Sehemu ya pili, Uk. 114[292]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik kuwa alisema: "Hakika Fatimah (as) alikuja na kipande cha mkate kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), akasema: 'Ni kipande cha nini hiki ewe Fatimah?' Akasema: 'Ni vipande vya mkate nilivyooka, nafsi yangu haikuridhika mpaka nimekuletea kipande hiki.' Mtume akasema: 'Hakika hiki ndio chakula cha kwanza kinachoingia katika kinywa cha baba yako tangia siku tatu.'"

**Tabaqat Ibn Saad Juz. 1, Sehemu ya pili, Uk. 114[293]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha kuwa alisema: "Mpaka Muhammad anafariki, haikuwahi hata siku moja familia yake kushiba mara tatu kwa mkate wa ngano. Na mpaka anafariki, hayakuwahi kunyanyuliwa hata siku moja mabaki ya mkate kutoka katika meza yake ya chakula. "

**Tabaqat Ibn Saad Juz. 1, Sehemu ya pili, Uk. 115[294]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Hasan (as) kuwa alisema: "Siku moja Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alitoa hotuba akasema: 'Wallahi hakuna siku pishi la chakula limeshinda katika nyumba ya familia ya Muhammad, na ni familia ya nyumba tisa.' Wallahi hakusema hayo kulalamika uchache wa riziki ya Mwenyezi Mungu kwao, bali alitaka uma wake umuige katika hilo."

**Taarikh Baghdad Juz. 11, Uk. 102[295]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha kuwa alisema: "Aliingia kwangu mwanamke mmoja wa Kiansari, akaliona tandiko la Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) likiwa ni joho lililokunjwa kunjwa, alitoka na kwenda kumletea tandiko la sufi. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipoingia kwangu alisema: 'Kitu gani hiki ewe Aisha?' Nikasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mwanamke fulani wa Kiansari aliingia kwangu na kuona tandiko lako, ndipo alikwenda na kuleta tandiko hili. Akasema: 'Lirudishe."' Aisha anasema: "Sikulirudisha na nilipenda liwe ndani ya nyumba yangu, mpaka aliponiambia mara tatu nilirudishe, alisema: 'Lirudishe ewe Aisha, Wallahi kama nikitaka Mwenyezi Mungu atanipa mlima wa dhahabu na fedha wenye kutembea pamoja na mimi."'

[291] *Hilyatul-Awliyai:* Wasifu wa Mas'aru bin Kidam, Hadithi za Mtume zilizopokewa kuhusu nasaha, unyenyekevu, kujinyima na uchamungu.
[292] *Tabaqat Ibn Saad:* Kuzungumzia maisha magumu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).
[293] *Tabaqat Ibn Saad:* Kuzungumzia maisha magumu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).
[294] *Tabaqat Ibn Saad:* Kuzungumzia maisha magumu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).
[295] *Taarikh Baghdad:* Wasifu wa Ibadu bin Ibadu, Abu Muawiya al-Mahlabiy, Hadithi namba 5798.

**Taarikh Baghdad Juz. 11, Uk. 102[296]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipewa zawadi ya ndege watatu, akala ndege mmoja, mfanyakazi wake akawa amewahifadhi akiba ndege wawili, ilipofika asubuhi mfanyakazi alimpelekea Mtume ndege wawili, Mtume akamwambia: 'Nini hiki?' Akasema: 'Ni ndege wawili ambao nilikuhifadhia akiba ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Mtume akasema: 'Hivi sijakukataza kuweka akiba kitu mpaka kesho, hakika Mwenyezi Mungu huipa kilasiku riziki yake."'

**Ad-Durul-Manthur ya as-As-Suyutiy: Mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: Basi subiri, kama walivyosubiri Mitume wenye stahmala kubwa:**

Amesema: Kaandika Ibn Abu Hatim na ad-Daylamiy kutoka kwa Aisha kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alishinda amefunga kisha akakesha bila kula, kisha akashinda amefunga na akakesha bila kula, kisha akashinda amefunga, akasema: 'Ewe Aisha hakika dunia haifai kwa Muhammad na familia ya Muhammad. Ewe Aisha hakika Mwenyezi Mungu hajaridhia toka kwa Mitume wenye stahamala kubwa isipokuwa subira juu ya mambo yenye kukarahisha na subira ya kuwa mbali na yale wanayoyapenda. Kisha hajaridhia kutoka kwangu isipokuwa kwa kuniamrisha yale aliyowaamrisha wao, akasema: **'Basi subiri, kama walivyosubiri Mitume wenye stahmala kubwa.'**Na hakika Wallahi mimi nitaendelea kufanya subira kama walivyosubiri juhudi zangu, na hakuna nguvu isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu.

## MLANGO UNAOSEMA KUWA MTUKUFU MTUME (SAWW) ALIONGEZEWA MAJARIBU KAMA ALIVYOONGEZEWA MALIPO

**Sahih Ibn Majah Juz. 2, Milango ya mitihani, Uk. 1334[297]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Said al-Khudriy alisema: "Niliingia kwa Mtukufu Mtumewa Mwenyezi Mungu (saww) nikamkuta ameshikwa na homa kali. Nikaweka mkono wangu juu yake, nikahisi joto kali juu ya shuka, nikasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mbona una joto kali? Akasema: 'Hivyo ndivyo tunavyoongezewa majaribu na kuongezewa malipo.' Nikamwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ni watu gani wenye majaribu zaidi? Akasema: 'Manabii.' Nikamwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kisha kina nani? Akasema: 'Watu wema, kwani utamkuta mmoja wao kajaribiwa kwa ufukara kiasi kwamba hana kitu isipokuwa joho tu analovaa, na utamkuta mmoja wao anafurahia majaribu kama anavyofurahia mmoja wao raha."'

**Mushkilatul-Athar Juz. 3, Uk. 63[298]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Mas'ud kuwa alisema: "Niliingia kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kumkuta akiwa na homa kali. Nikamgusa kwa mkono wangu na kusema: Ewe Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu! Hakika wewe una homa kali sana, akasema: 'Ndio, hakika mimi napatwa na joto kali ambalo ni sawa na joto la homa ya watu wawili miongoni mwenu.'

[296] *Taarikh Baghdad*: Wasifu wa Yusuf bin Husain ar-Raziy, Hadithi namba 7638.

[297] *Sahih Ibn Majah*: Kitabu cha mitihini, Mlango unaozungumzia kufanya subira wakati wa majaribu, Hadithi ya 4023.

[298] *Mushkilul-Athar:* Mlango unaozungumzia maneno yaliyopokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) pindi homa kali ilipokuwa ikimpata.

Nikasema: Basi una malipo mardufu. Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Hakuna Mwislamu atakayepatwa na adha ya maradhi au mfano wake isipokuwa ni lazima Mwenyezi Mungu atamfutia makosa yake kama mti unavyopukutisha majani yake."'

**Mushkilatul-Athar Juz. 3, Uk. 64[299]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha kuwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipatwa na maradhi hivyo akaanza kujigeuza geuza juu ya tandiko lake. Aisha akamwambia: 'Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu, laiti mmoja wetu angefanya hivi ungemghadhibikia.' Akasema: 'Hakika Waumini majaribu yao huongezeka, na hakika muumini hapatwi na msiba au maradhi isipokuwa Mwenyezi Mungu humuinua daraja kwa balaa hilo na humfutia makosa yake."'

**Al-Athar cha as-Shaybaniy Uk. 145[300]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibrahim kuwa alisema: "Hakika Umar alimgusa Nabii wa Mwenyezi Mungu wakati alipokuwa na homa, Umar akasema: 'Hivi inakufanya hivi wakati wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu?' Akasema: 'Hakika inaponipata inanizidia, hakika mwenye majaribu makubwa zaidi katika ummah huu ni Nabii wake, kisha watenda kheri kisha wanaofuatia katika kutenda kheri, na hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa Manabii na mataifa ya kabla yenu.

## MLANGO UNAOSEMA KUWA MALAIKA WA MAUTI ALIOMBA IDHINI KWA MTUKUFU MTUME (SAWW) NA HAKUWAHI KUOMBA IDHINI KWA YEYOTE KABLA YAKE

**Kanzul-Ummal Juz. 4, Uk. 54[301]:**

Amesema: Kutoka kwa Ali (as) alisema: "Siku tatu kabla ya kufariki Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Mwenyezi Mungu alimteremsha Jibril kwake, akasema: 'Ewe Ahmad, hakika Mwenyezi Mungu amenituma kwako na jambo ambalo ni heshima kwako, ni fadhila kwako na ni makhususi kwako, anakuuliza jambo ambalo yeye analijua zaidi kuliko wewe, anasema: Unahali gani?' – Aliendelea kusimulia mpaka aliposema: Jibril akamwambia: 'Ewe Ahmad huyu hapa Malaika wa mauti anaomba idhini ya kuingia, na kamwe hajawahi kumuomba idhini mwana yeyote wa Adam kabla yako, na kamwe hatamuomba idhini mwana yeyote wa Adam baada yako.' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Mpe idhini.' Akampa idhini

— Aliendelea kusimulia paka akasema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipofariki tulianza kupokea tanzia. Alikuja aliyekuja ambaye sauti yake watu waliisikia lakini yeye mwenye hawakuweza kumuona, akasema: 'Asalam Alaykum enyi watu wa Nyumba ya Mtume na rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yenu. Kwa Mwenyezi Mungu kuna tanzia ya kila msiba, na badala ya kila kilichotoweka, na hudirikiwa kila kilichopita. Kuweni na imani na Mwenyezi Mungu na mfanyeni tumaini lenu. Hakika aliyenyimwa hasa ni yule aliyenyimwa thawabu, na hakika aliyepatwa na msiba hasa ni yule aliyenyimwa thawabu.Wasalamu alaykum.' Ali (as) akasema: 'Mnamjua ni nani huyu?' Wakasema hapana, akasema: 'Huyu ni Khidhri.'" – Mwandishi anasema: Ameiandika al-Adiy na Ibn Saad na al-Bayhaqiy ndani ya *ad-Dalail*.

---

[299] *Mushkilul-Athar*: Mlango unaozungumzia maneno yaliyopokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuhusu yale yanayowapata wasiokuwa Manabii na je wanalipwa kwa hayo?.

[300] *Al-Athar* cha as-Shaybaniy Uk. 145.

[301] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha tabia, Hadithi mbalimbali zinazohusu kifo chake, Hadithi ya 18785.

**Tabaqat Ibn Saad Juz. 2, Sehemu ya pili, Uk. 48[302]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ja'far bin Muhammad kutoka kwa baba yake, kuwa alisema: "Zilipobakia siku tatu kabla ya kifo cha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) Jibril alishuka kwake na kumwambia: 'Ewe Ahmad, hakika Mwenyezi Mungu amenituma kwako na jambo ambalo ni heshima kwako, ni fadhila kwako na ni makhususi kwako, anakuuliza jambo ambalo yeye analijua zaidi kuliko wewe, anasema: Una hali gani?' Akasema: 'Ewe Jibril ni mwenye huzuni, ewe Jibril ni mwenye mashaka.' Ilipofika siku ya pili Jibril aliteremka na kusema: 'Ewe Ahmad, hakika Mwenyezi Mungu amenituma kwako na jambo ambalo ni heshima kwako, ni fadhila kwako na ni makhususi kwako, anakuuliza jambo ambalo yeye alijua zaidi kuliko wewe, anasema: Una hali gani?' Akasema: 'Ewe Jibril ni mwenye huzuni, ewe Jibril nimwenye mashaka.'

"Ilipofika siku ya tatu Jibril aliteremka akiwa pamoja na Malaika wa mauti, naye aliteremka pamoja na Malaika anayeitwa Ismail, ambaye huishi hewani, kamwe hajawahi kupanda mbinguni na kamwe hajawahi kuteremka aridhini tangu ardhi iumbwe, naye alikuwa na Malaika elfu sabini na kila Malaika alikuwa na Malaika elfu sabini wengine. Jibril aliwatangulia kufika, alipofika akasema: 'Ewe Ahmad, hakika Mwenyezi Mungu amenituma kwako na jambo ambalo ni heshima kwako, ni fadhila kwako na ni makhususi kwako, anakuuliza jambo ambalo yeye alijua zaidi kuliko wewe, anasema: Unahali gani?' Akasema: 'Ewe Jibril nimwenye huzuni, ewe Jibril nimwenye mashaka.'

"Kisha Malaika wa mauti aliomba idhini, Jibril akasema: 'Ewe Ahmad, huyu hapa Malaika wa mauti anaomba idhini ya kuingia, na kamwe hajawahi kumuomba idhini mwana yeyote wa Adam kabla yako, na kamwe hatamuomba idhini mwana yeyote wa Adam baada yako.' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Mpe idhini.' Akampa idhini, Malaika wa mauti akaingia na kusimama mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), akasema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ewe Ahmad! Hakika Mwenyezi Mungu amenituma kwako na ameniamuru nikutii katika kila utakachoniamuru. Ukiniamuru nichukue roho yako nitaichukua, na ukiniamuru niiache nitaiacha.' Mtume akasema: 'Utafanya hivyo kweli ewe Malaika wa mauti?' Akasema: 'Nimeamrishwa hivyo nikutii katika kila utakaloniamuru.' Jibril akasema: 'Ewe Ahmad! Hakika Mwenyezi Mungu ana shauku kubwa na wewe.' Mtume akasema: 'Tekeleza ewe Malaika wa mauti kile ulichoamrishwa.' Jibril akasema: 'Asalam alayka ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Hii ndio mara yangu ya mwisho kukanyaga aridhini, kwani hakika wewe ndio uliyekuwa haja yangu duniani.'

"Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akafariki na ikaja tanzia ambayo mwenye kuitoa alikuwa anasikika sauti lakini yeye mwenyewe haonekani, alisema: 'Asalam Alaykum enyi watu wa Nyumba ya Mtume na rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yenu, kila nafsi itaonja mauti, na hakika mtalipwa kwa ukamilifu malipo yenu Siku ya Kiyama. Hakika kwa Mwenyezi Mungu kuna tanzia ya kila msiba, na badala ya kila kilichotoweka, na hudirikiwa kila kilichopita. Kuweni na imani na Mwenyezi Mungu na mfanyeni tumaini lenu. Hakika aliyenyimwa hasa ni yule aliyenyimwa thawabu, wasalamu alaykum warahmatiullahi wabarakatuhu."

[302] *Tabaqat Ibn Saad*: Kutaja kifo cha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

# MLANGO UNAOSEMA KUWA MOLA MLEZI NDIYE ALIYEKUWA WA KWANZA KUMSWALIA MTUKUFU MTUME –BAADA YA KUFARIKI- JUU YA ARSHI YAKE

**Hilyatul-Awliyai Juz. 4, Uk. 73 – 79[303]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir bin Abdullah na kutoka kwa Ibn Abbas kuwa hao wawili walisema: "Ilipoteremka: **'Itakapo kuja nusura ya Mwenyezi Mungu na ushindi.'** Mpaka mwisho wa Sura –Aliendelea kusimulia hadithi mpaka aliposema: Ali (as) alisema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Utakapofariki ni nani atakuosha? Utakafiniwa kwa kitu gani? Ni nani atakayekuswalia? Na ni nani atakayekuingiza kaburini?' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Ewe Ali! Kuhusu kuniosha utaniosha wewe huku Ibn Abbas atakuwa akimwagilia maji, na wa tatu wenu atakuwa ni Jibril. Mkimaliza kuniosha mnivishe kafani ya vipande vitatu vya nguo mpya, na Jibril ataniletea manukato (karafuu maiti na mkunazi- kutoka peponi, mkishaniweka juu ya kitanda mniweke msikitini na mtoke na kuniacha peke yangu, kwani hakika wa kwanza kabisa atakayenisalia mimi ni Mola Mtukufu juu ya Arshi yake, kisha ni Jibril, kisha ni Mikail, kisha ni Israfil, kisha ni Malaika makundi kwa makundi. Kisha muingie na msimame safu baada ya safu bila yeyote kutangulia mbele.

"Aliendelea kusimulia mpaka aliposema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipofariki Ali bin Abu Talib (as) alimuosha hukuIbn Abbas akimwagilia maji, na Jibril akiwa pamoja nao. Akavishwa kafani ya vipande vitatu vya nguo mpya, akabebwa juu ya kitanda na wakamuungiza msikitini.Walipomuweka msikitini walitoka wote na kumwacha peke yake. Wa kwanza aliyemswalia alikuwa ni Mola Mtukufu juu ya Arshi yake, kisha Jibril, kisha Mikail, kisha Israfil, kisha Malaika makundi kwa makundi. Ali (as) alisema: 'Na tulisikia sauti msikitini bila kuwaona watu, kisha tukasikia mwenye kunadi akinadi: Ingieni Mwenyezi Mungu awarehemu, msalieni Nabii wenu. Tukaingia na kusimama safu baada ya safu kama alivyotuamuru Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Tukatoa takbira ya Jibril na tukamsalia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) Swala ya Jibril na hakutangulia yeyote mbele yetu katika kumswalia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).' Na Ali bin Abu Talib akaingia kaburini…"

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 3, Uk. 60[304]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Mas'ud kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipozidiwa tulisema: Ni nani atakayekuswalia ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu!? Akalia nasi tukalia, kisha alisema: 'Vuteni subira, Mwenyezi Mungu akusameheni na akulipeni kheri kwa ajili ya Nabii wenu. Mtakaponiosha na kunitia manukato (karafuu maiti na mkunazi) na kunivisha kafani, mniweke kwenye mdomo wa kaburi langu kisha mtoke na kuniacha peke yangu muda kidogo. Hakika wa kwanza atakayeniswalia ni vipenzi vyangu na marafiki zangu Jibril na Mikail, kisha ni Malaika wa kifo akiwa pamoja na jeshi la Malaika, kisha ndipo waanze kuniswalia wanaume kutoka katika Nyumba yangu, kisha wanawake wao, kisha ndipo muingie makundi kwa makundi.."

[303] *Hilyatul-Awliyai*: Wasifu wa Wahbi bin Munabihu, Habari yake ndefu kuhusu kisa cha kufariki kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).
[304] *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha vita, Wasia wa Mtukufu Mtume kuhusu mtu atakayemswalia kwa utaratibu.

# MLANGO UNAOSEMA KUWA MTUKUFU MTUME (SAWW) NI MZURI WA HARUFU KUANZIA ALIPOKUWA HAI HADI ALIPOKUWA MAITI

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 1, Uk. 260[305]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: "Walipokusanyika jamaa ili wamuoshe Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), nyumbani kwake hakukuwa na mtu isipokuwa ndugu zake, ami yake Abbas bin Abdul-Muttalib, Ali bin Abu Talib (as), al-Fadhlu bin Abbas, Qutham bin Abbas, Usama bin Zaid bin Harith na mfanyakazi wakeSalih. Walipokusanyika ili wamuoshe, Awsi bin Khula al-Ansariy ambaye ni mmoja kutoka Bani Awfi Ibn Khazraj alimwita Ali bin Abu Talib (as) huku akiwa nyuma ya mlango, alimwambia: 'Ewe Ali! Nakuapiza kwa Mwenyezi Munguhembu kumbuka fungu letu kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).' Ali (as) akamwambia: 'Ingia.' Akaingia na kuhudhuria katika zoezi la kuoshwa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), lakini hakujishughulisha na chochote katika kumuosha."

Ibn Abbas amesema: "Akamwegemeza kifuani kwake huku akiwa na kanzu yake, Abbas, al-Fadhl, Qutham pamoja na Ali bin Abu Talib (as) walikuwa wakimgeuza, na Usamah bin Zayd na mfanyakazi wao Salih walikuwa wakimwagia maji, Ali (as) akawa anamuosha na hakuona chochote ambacho muoshaji hukiona toka kwa maiti, alikuwa akisema: "Naapa kwa haki ya baba yangu na mama yangu, una harufu nzuri ilioje kuanzia ulipokuwa hai hadi maiti yako." Hadi walipomaliza kumuoshaMtume wa Mwenyezi Mungu (saww), na walikuwa wakimuosha kwa maji na mkunazi uliokaushwa. Kisha walimfanyia yale ambayo maiti hufanyiwa, kisha aliingizwa ndani ya vipande vitatu vya nguo, viwili vyeupe na shuka jipya, kisha Abbas aliwaita watu wawili na kuwaambia: 'Mmoja wenu aende kwa Abu Ubaydah al-Jarah – huyu alikuwa ndiye mchimba kaburi wa watu Makka – na mwingine aende kwa Abu Talha bin Sahli al-Ansariy – huyu alikuwa ndiye mchimba mwanandani wa watu wa Madina.' Kisha Abbas akasema: 'Ewe Mungu Wangu mpumzishe Mtume Wako.' Wakaondoka, aliyekwenda kwa Abu Ubaydah hakumkuta, na aliyekwenda kwa Abu Talha alimkuta yupo, alikuja naye na ndiye aliyechimba mwanandani wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)."

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 1, Uk. 362[306]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ali bin Abu Talib (as) kuwa alisema: "Nilimuosha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), nikawa nachunguza yale ambayo huonekana kwa maiti lakini sikupata kitu, na alikuwa na harufu nzuri kuanzia alipokuwa hai hadi maiti."

**Tabaqat Ibn Saad Juz. 2, Sehemu ya pili, Uk. 62:**

Amepokea kwa njia tofauti kutoka kwa Said bin al-Musayyab, amesema: "Ali (as) alitafuta kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) yale ambayo hutoka kwa maiti wakati wa kumuosha lakini hakupata kitu, akasema: 'Naapa kwa haki ya baba yangu na mama yangu, una harufu nzuri ilioje kuanzia ulipokuwa hai hadi maiti yako.'"

**Nasema:** Katika mlango huu kuna habari nyingi zenye maana hii, nasi tumetosheka na hizo tulizozitaja.

[305] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Musnad Abdullah bin Abbas, Hadithi ya 2353.
[306] *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu kinachozungumzia jeneza, Fadhila za safu tatu katika Swala ya jeneza.

# MLANGO UNAOSEMA KUWA MALAIKA HUSHUKA KATIKA KABURI LA MTUKUFU MTUME KILA SIKU. NA UNABAINISHA FADHILA ZA KUMZURU

**Sunanud-Daramiy Juz. 1, Uk. 44[307]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Nabiyyuhu bin Wahbi, amesema: “Kaab aliingia kwa Aisha, wakamtaja Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika mazungumzo yao, Kaab akasema: ‘Hakuna siku inayochomoza isipokuwa huteremka Malaika sabini elfu na kulizunguka kaburi la Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), hulipepea kwa mbawa zao na kumswalia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), inapofika usiku hupaa na kuteremka wengine mfano wao na kufanya kama waliotangulia, na hata siku ambayo ardhi itapasuka atatoka huku akisindikizwa na Malaika sabini elfu.”’

**Kanzul-Ummal Juz. 8, Uk. 99[308]:**

Lafudhi yake ni: “Yeyote atakayehiji na kulizuru kaburi langu baada ya kufa kwangu atakuwa sawa na mtu aliyenizuru wakati wa uhai wangu.” - Amesema: Ameiandika Tabaraniy na al-Bayhaqiy kutoka kwa Ibn Umar.

**Kanzul-Ummal Juz. 8, Uk. 99[309]:**

Lafudhi yake ni: “Yeyote atakayezuru kaburi langu atapata shafaa yangu.”Amesema: Ameiandika Ibn Adiy na al-Bayhaqiy kutoka kwa Ibn Umar.

**Kanzul-Ummal Juz. 8, Uk. 99[310]:**

Lafudhi yake ni: “Yeyote atakayenizuru huko Madina kwa kutaraji thawabu nitakuwa shahidi yake – au muombezi wake – Siku ya Kiyama.”

— Amesema: Kaiandika al-Bayhaqiy kutoka kwa Anas.

**Majmauz-Zawa’id ya al-Haythamiy Juz. 3 Uk. 2[311]:**

Amesema: Kutoka kwa Ibn Umar, amesema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: ‘Atakayekuja kunizuru huku akiwa hana haja yoyote isipokuwa kunizuru tu mimi, itakuwa ni wajibu juu yangu kuwa muombezi wake Siku ya Kiyama.”’ - Amesema: Kaipokea Tabaraniy ndani ya *al-Awsat* na *al-Kabir*.

[307] *Sunanud-Daramiy:* Mlango unaozungumzia yale ambayo Mwenyezi Mungu kamkirimu Nabii Wake baada ya kifo chake, Hadithi ya 94.
[308] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha mauti, Kulizuru kaburi la Mtukufu Mtume, Hadithi ya 42582.
[309] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha mauti, Kulizuru kaburi la Mtukufu Mtume, Hadithi ya 42583.
[310] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha mauti, Kulizuru kaburi la Mtukufu Mtume, Hadithi ya 42584.
[311] *Maj’mauz-Zawa’id Waman’baul-Fawaid*: Mlango unaozungumzia kumzuru Bwana wetu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

# MLANGO UNAOZUNGUMZIA KAUTHARI YA MTUKUFU MTUME NA CHEO KINACHO SIFIKA, NA KWAMBA HUKO PEPONI ATAMUOA KADHIJA, MARIAM BINTI IMRAN, MKE WA FIRAUNI NA DADA YAKE MUSA

**Sahih Muslim: Kitabu cha Swala, Mlango unaozungumzia hoja ya yule asemaye kuwa Bismillahi ni Aya:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik kuwa alisema: "Siku moja Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa miongoni mwetu alisinzia kidogo, kisha aliinua kichwa chake huku akitabasamu, tukamuuliza: Ni kitu gani chakuchekesha ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: 'Punde tu imenishukia Sura.' Akaisoma: **"Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Hakika tumekupa kheri nyingi. Basi swali na uchinje kwa ajili ya Mola Wako Mlezi. Hakika anayekuchukia ndiye aliye mpungufu."** Kisha akasema: 'Mnajua kheri nyingi ni nini?' Tukasema: Mwenyezi Mungu na Mtume wake ndio wajuao zaidi. Akasema: 'Ni mto ambao Mola Wangu kaniahidi ukiwa na kheri nyingi, nao ni Hodhi ambalo hapo utafika ummah wangu. Vyombo vyake (vya kunywea) ni sawa na idadi ya Nyota. Miongoni mwao kuna ambaye atazuiliwa, nami nitasema huyo ni katika ummah wangu, nitaambiwa: Hujui yale aliyozusha baada yako."'

**Sahih Muslim: Kitabu cha fadhila, Mlango unaothibitisha Hodhi la Nabii wetu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Amru bin Al-Aas, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Hodhi langu ni mwendo wa mwezi mzima, na pande zake zinalingana, na maji yake ni meupe kushinda karatasi, na harufu yake ni nzuri kushinda miski, na vyombo vyake ni kama nyota za mbinguni, atakayekunywa toka humo hatapata kiu tena.'"

Anasema: Asmau binti Abu Bakr alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Hakika mimi nitakuwa katika Hodhi mpaka nimjue ni nani atakayezuiwa miongoni mwenu, kwani kuna watu watazuiliwa wasifike kwangu, nitasema: Ewe Mola, hao ni kutoka katika ummah wangu, patasemwa: Hivi unajua ni kitu gani walichotenda baada yako? Wallahi baada yako hawakuacha kurudi nyuma kwa visigino vyao.'"

Anasema: Hivyo Ibn Abu Malikah alikuwa akisema: "Ewe Mungu Wangu, hakika sisi tunajilinda kwako tusiweze kurejea kwa visigino vyetu au kupatwa na mtihani wa kujitenga na dini yetu."

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 240[312]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas kuhusu: **Hakika tumekupa kheri nyingi,** kuwa alisema: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Ni mto uliopo peponi, kingo zake ni za lulu. Nikasema: Ni kitu gani hiki ewe Jibril? Akasema: 'Hii ni Kauthari –kheri nyingi- ambayo Mwenyezi Mungu amekupa.'"

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 240[313]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas, amesema: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Nilipokuwa nikitembea peponi mara niliona mto ambao kingo zake ni za lulu. Nikasema kum-

[312] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha tafsiri ya Qur'ani, Mlango unaozungumzia Sura al-Kauthar, Hadithi ya 3359.
[313] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha tafsiri ya Qur'an, Mlango unaozungumzia Sura al-Kautharii, Hadithi ya 3360.

wambia Malaika: Ni kitu gani hiki? Akasema: 'Hii ni Kauthari –kheri nyingi- ambayo Mwenyezi Mungu amekupa.' Kisha alipiga kwa mkono wake katika udongo na kutoa miski, kisha alinionesha eneo la mkunazi wa mwisho, nikapaona pakiwa na nuru adhimu."'

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 240[314]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Umar kuwa alisema: Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Kauthari ni mto uliomo peponi, kingo zake ni za dhahabu, na unatembea juu ya yakuti, udongo wake una harufu nzuri kushinda miski, na maji yake ni matamu kushinda asali na ni meupe kushinda theluji."'

**Musnad Imam Abi Hanifa Uk. 272[315]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Said al-Khudriy kuwa alisema: "Nilimisikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: '**Huenda Mola Wako Mlezi akakunyanyua cheo kinacho sifika.** Kupitia uombezi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Mwenyezi Mungu atawatoa motoni jamaa miongoni mwa wale walioamini na kufuata Kibla, na hiyo ndio maana ya cheo kinachosifika. Wataletewa mto ambao unaitwa '*Hayawani*', watatupiwa humo, wataota nyama na kukua kama vinavyokua vifaranga. Kisha watatolewa na kuingizwa peponi na watajulikana kwa jina la 'Wanajahannam'. Kisha watamuomba Mwenyezi Mungu awaondolee jina hilo naye atawaondolea.'"

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9, uk. 218[316]:**

Amesema: Kutoka kwa Abu Rawwad, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliingia kwa Khadijah wakati wa maradhi yake yaliyomfisha, akamwambia: 'Si kwa kupenda kwangu hili nilionalo kwako ewe Khadijah, na Mwenyezi Munguhuenda akaweka kheri nyingi katika lile asilopenda mtu. Hivi hujui kuwa Mwenyezi Mungu pamoja na kunioza wewe peponi pia amenioza Mariam binti Imran na mke wa Firaun na Kultham dada yake na Musa?' Khadijah akasema: 'Je Mwenyezi Mungu ameshafanya hilo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu!' Akasema: 'Ndiyo.' Khadijah akasema: 'Kwa raha na watoto.' - Amesema: Kaipokea Tabaraniy.

**Faydhul-Qadir Juz. 3, Uk. 237, katika matini[317]:**

Lafudhi yake ni: "Hakika Mwenyezi Mungu alinioza peponi Mariam binti Imran, mke wa Firauni na dada yake na Musa." - Amesema: Kaiandika Tabaraniy kutoka kwa Saad bin Junadah.

**Kanzul-Ummal Juz. 8, Uk. 99[318]:**

Lafudhi yake ni: "Hivi hujui kuwa Mwenyezi Mungu amenioza Mariam binti Imran, Kultham dada yake na Musa na mke wa Firauni, huko peponi?" - Amesema: Kaiandika Tabaraniy kutoka kwa Abu Umamah.

314 *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha tafsiri ya Qur'an, Mlango unaozungumzia Sura al-Kauthar, Hadithi ya 3360.
315 *Musnad* Imam Abi Hanifa pamoja na Sharhu yake ya Imam Mula Ali al-Qariy, Uk. 553, Chapa ya Darul-Kutubi al-Ilmiyah, Beirut.
316 Maj'mauz-Zawaid Waman'baul-Fawaid: Mlango unaozungumziafadhila za Mariam, Asia na wengineo.
317 Faydhul-Qadir: Mlango wa herufi Alif, Hadithi ya 1744.
318 Kanzul-Ummal: Kitabu cha fadhila, Mlango wa fadhila balimbali, Hadithi ya 31943.

# KUSUDIO LA PILI: LINAHUSU FADHILA ZA ALI BIN ABU TALIB (AS) MLANGO UNAOZUNGUMZIA WINGI WA FADHILA ZA ALI (AS)

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, Uk. 214[319]:**

Amesema: Kutoka kwa Umar bin Khattab, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Hakuna mchumaji aliyechuma fadhila mfano wa Ali, yeye humuongoza rafiki yake kwenye uongofu na kumzuia dhidi ya upotofu."

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 3, Uk. 107[320]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Muhammad bin Mansuri at-Tusiy kuwa alisema: "Nilimsikia Ahmad bin Hanbal akisema: 'Hakuna sahaba yeyote wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliyepatikana na fadhila kushinda fadhila zilizopatikana kumhusu Ali bin Abu Talib (as).''

**Al-Istiaab Juz. 2, Uk. 466[321]:**

Amesema: Ahmad bin Hanbal na Ismail bin Is'haqa al-Qadhiy wamesema: "Hakuna sahaba yeyote ambaye fadhila zake zimepokewa kwa njia nzuri kama zilivyopokewa fadhila za Ali bin Abu Talib." Kadhalika amesema hayo Ahmad bin Shuaib bin Ali bin an-Nasaiy.

**Nasema:** Kalisema hilo Ibn Hajar ndani ya *as-Sawa'iqul-Muhriqah*Uk. 72, na al-Asqalaniy ndani ya *Fat'hul-Bariy* Juz. 8, Uk. 71, na as-Shablanjiy ndani ya *Nurul-Absari*Uk. 73, yeye katika kuwataja waliosema kamwongeza Abu Ali an-Nisaburi.

**Al-Imamah Was-Siyasah Uk. 93[322]:**

Amesema: Wametaja kuwa mtu mmoja kutoka Hamadani anayeitwa Barad alikwenda kwa Muawiya, akamsikia Amru akimkashifu Ali (as), akamwambia: "Ewe Amru! Hakika mashekhe zetu wamesikia kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Yeyote ambaye mimi ni kiongozi wake huyu Ali ndiye kiongozi wake.' Je hilo ni haki au batili?" Amru akasema: "Ni haki, na mimi nakuongezea kuwa hakika kati ya Masahaba wote wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hakuna mwenye fadhila kama Ali." Kijana yule akashtuka.

**Taarikh Baghdad Juz. 6, Uk. 221[323]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: "Ziliteremka Aya mia tatu zikizungumzia fadhila za Ali bin Abu Talib (as)."

---

319 *Ar-Riyadh an-Nadhrah*: Fadhila za Amirul-Muuminina Ali bin Abu Talib, Ametaja humo kuwa hakuna mchumaji aliyechuma fadhila mfano wake.

320 *Mustadrakus-Sahihayni*: Kitabu cha kuwatambua Masahaba. Miongoni mwa fadhila za Amirul-Muuminina Ali bin Abu Talib (as).

321 *Al-Istiaab Bihamishil-Iswabah*: Harfu Ain, Wasifu wa Ali bin Abu Talib (as).

322 *Al-Imamah Was-Siyasah*: Amru bin Al-Aasi amkashifu Ali (as).

323 *Taarikh Baghdad*: Wasifu wa Ismail bin Muhammad al-Madainiy, Namba 3275.

**As-Sawa'iqul-MuhriqahUk. 76;[324] Na Nurul-Abswar ya as-Shablanjiy Uk. 73[325]:**

Wamesema: "Ameandika Ibn Asakir kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: 'Hakuna mtu ambaye Kitabu cha Mwenyezi Mungu kimeteremka na fadhila zake kama kilivyoteremka na fadhila za Ali (as).'" Kisha wamesema: "Ameandika Ibn Asakir kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: 'Ziliteremka Aya mia tatu zikizungumzia fadhila za Ali bin Abu Talib (as).'"

## MLANGO UNAOSEMA KUWA NURU YA MTUKUFU MTUME (SAWW) NA YA ALI (AS) ZILIUMBWA KABLA YA ADAM (AS), NA WALIUMBWA KUTOKANA NA UDONGO MMOJA

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, Uk. 164[326]:**

Amesema: Kutoka kwa Salman, amesema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Mimi na Ali tulikuwa nuru moja mbele ya Mwenyezi Mungu miaka elfu moja mia nne kabla Adam (as) hajaumbwa, Mwenyezi Mungu alipomuumba Adam (as) aliigawa nuru hiyo vipande viwili, kipande kimoja ndio mimi na kipande kingine ni Ali.'"

— Amesema: Ameiandika Ahmad ndani ya *al-Manaqib*.

**Nasema:** Ameitaja ad-Dhahabiy ndani ya *Mizanul-Iitidal* Juz. 1, uk. 235, akinukuu kutoka kwa Ibn Asakir kutoka ndani ya *Taarikh* yake kwa njia ya Salman.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9, uk. 128[327]:**

Amesema: Kutoka kwa Buraydah amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimtuma Ali (as) kuwa Amiri wa watu wa Yemeni, na akamtuma Khalid bin Walid kuwa Amiri wa watu wa mlimani, akasema: 'Mtakapokutana Ali ndio atakuwa Amiri wa watu wote.' Wakakutana na wakapata ghanima ambazo walikuwa hawajawahi kupata mfano wake. Ali (as) akachukua suria kutoka katika khumsi, Khalid bin Walid akamwita Buraydah na kumwambia: 'Tumia fursa hiyo, mwambie Mtume alichofanya.' Basi nilikwenda Madina na nikaingia msikitini hukuMtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa nyumbani kwake na masahaba zake wakiwa mlangoni kwake. Wakasema: 'Kuna habari gani ewe Buraydah?' Nikasema: Mwenyezi Mungu amewapa ushindi Waislamu. Wakasema: Kitu gani kilichokuleta?' Nikasema: Suria ambaye Ali kamchukua kutoka kwenye khumsi, nimekuja ili nimpe habari Mtukufu Mtume (saww). Wakasema: 'Mwambie Mtume hakika yeye atashuka thamani mbele ya Mtukufu Mtume.'

"Walisema hayo huku Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisikia maneno yao. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akatoka akiwa ameghadhibika, akasema: 'Wana nini watu ambao wanamtia doa Ali? Mwenye kumtia doa Ali amenitia doa mimi, na yeyote mwenye kujitenga na Ali amenitenga mimi. Hakika Ali ni sehemu yangu na mimi ni sehemu ya Ali, ameumbwa kutokana na udongo wangu, nami nimeumbwa kutokana na udongo wa Ibrahim, na mimi ni bora kuliko Ibrahim. **Ni wazao wao kwa wao;**

---

[324] *As-Sawa'iqul-Muhriqah*: Masahaba na watangulizi wamsifu Ali (as).

[325] *Nurul-Abswar* ya as-Shablanjiy: Kutaja fadhila za Bwana wetu Ali bin Abu Talib (as), zimepatikana aya na hadithi nyingi kuhusu fadhila zake.

[326] *Ar-Riyadh an-Nadhrah:* Fadhila za Amirul-Muuminina Ali bin Abu Talib. Ametaja khususia za Ali kuwa yeye aligawana nuru na Mtukufu Mtume, nuru ambayo iliumbwa kabla ya Adam.

[327] *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid*: Mlango unaozungumzia fadhila za Ali bin Abu Talib (as). Mlango unaokusanya habari za wanaompenda na wanaomchukia.

**na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia na Mwenye kujua.** Ewe Buraydah! Hivi hujui kuwa Ali ana suria wengi kuliko huyo aliyemchukua, na kuwa yeye ndiye Walii wenu baada yangu.' Nikasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kwa haki ya uswahaba naomba ukunjue mkono wako ili nikupe kiapo cha utii katika Uislamu upya." Buraydah anasema: "Sikuondoka ila baada ya kuwa nimempa kiapo cha utii katika Uislamu."

— Amesema: Ameipokea Tabaraniy ndani ya *al-Awsat*.

**Taarikh Baghdad Juz. 6, Uk. 58[328]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Musa bin Ja'far bin Muhammad kutoka baba yake kutoka babu yake, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Mimi, Harun bin Imran, Yahya bin Zakaria na Ali bin Abu Talib tuliumbwa kutokana na udongo mmoja."'

**Hilyatul-Awliyau Juz. 1, uk. 84[329]:**

Amepokea kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Apendaye kuishi maisha yangu na afe kifo changu na aishi katika bustani ya kudumu aliyoipanda Mola Wangu, basi na amfanye Ali kuwa kiongozi wake baada yangu. Ampende ampendaye na awafuate Maimamu baada yangu, kwani hakika wao ndio kizazi changu wameumbwa kutokana na udongo wangu na wameruzukiwa ufahamu na elimu. Ole wao wale wenye kupinga fadhila zao kutoka katika ummah wangu, wenye kukata udugu wangu, Mwenyezi Mungu hatawapa uombezi wangu."

## MLANGO UNAOSEMA KUWA ADAM (AS) ALIMUOMBA MWENYEZI MUNGU KWA HAKI YA MUHAMMAD, ALI, FATIMAH, HASAN NA HUSEIN (AS), TOBA YAKE IKAKUBALIKA

**Ad-Durul-Manthur ya As-As-Suyutiyiy: Mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: Kisha Adam akapokea maneno kwa Mola Wake Mlezi, na Mola Wake Mlezi alimkubalia toba yake; hakika Yeye ndiye Mwingi wa kukubali toba na Mwenye kurehemu:**

Amesema: Ibn an-Najar ameandika kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Nilimuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuhusu maneno ambayo Adam aliyapokea kutoka kwa Mola Wake na akamkubalia kwayo toba yake? Akasema: 'Aliomba kwa haki ya Muhammad, Ali, Fatimah, Hasan na Husain, nikubalie toba yangu. Mwenyezi Mungu akamkubalia toba."'

**Kanzul-Ummal Juz. 1, Uk. 234[330]:**

Amesema: Kutoka kwa Ali (as) amesema: "Nilimuuliza Mtukufu Mtume (saww) kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: **Kisha Adam akapokea maneno kwa Mola Wake Mlezi.** Akasema: Hakika Mwenyezi Mungu alimteremsha Adam huko India, na akamteremsha Hawa huko Jidah, na akamteremsha Ibilisi huko Maisan, na akamteremsha nyoka huko Isfihan, na nyoka huyo alikuwa na miguu kama ya ngamia. Adam aliishi India miaka mia moja huku akilia juu ya kosa lake, ndipo Mwenyezi Mungu akamtuma Jibril na kwenda kumwambia: 'Ewe Adam! Hivi sikukuumba kwa mkono wangu? Hivi sikukupulizia roho

[328] *Taarikh Baghdad:* Wasifu wa Ibrahim bin Husain bin Daud: Abu Is'haqa al-Qatan, Namba 3088.
[329] *Hilyatul-Awliyai*: Wasifu wa Ali bin Abu Talib, Wasifu wa wafuasi wake na masahaba zake.
[330] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha fadhila, Faslu ya tafsiri

yangu? Hivi sikuwaamuru Malaika wangu wakusujudie? Hivi sikukuozesha Hawa mja wangu?' Akasema ndiyo ulifanya hivyo.

Akasema: 'Basi ni kwa nini unalia hivi?' Akasema: 'Ni kitu gani kitanizuia kulia wakati umeshanitoa pembezoni mwa Rahman?' Akasema: Basi shikamana na maneno haya, hakika Mwenyezi Mungu atakubali toba yako na kukusamehe dhambi zako, sema: 'Ewe Mungu Wangu hakika mimi nakuomba kwa haki ya Muhammad na Aali Muhammad. Utakatifu ni wako hapana mungu isipokuwa Wewe, nimetenda maovu na nimeidhulumu nafsi yangu, nikubalie toba yangu hakika Wewe ndiye Mwingi wa kukubali toba na ni Mwingi wa kurehemu. Ewe Mungu Wangu hakika mimi nakuomba kwa haki ya Muhammad na Aali Muhammad. Nimetenda maovu na nimeidhulumu nafsi yangu, nikubalie toba yangu hakika Wewe ndiye Mwingi wa kukubali toba na ni Mwingi wa kurehemu.' Haya ndio maneno aliyapokea Adam (as)." – Amesema: Ameiandika ad-Daylamiy.

**Nasema:** Na ameitaja as-As-Suyutiy ndani ya *ad-Durul-Manthur* mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: **Kisha Adam akapokea maneno kwa Mola Wake Mlezi.** Amesema: Ameiandika ad-Daylamiy katika musnad ya Firdawsi kwa njia aliyoipokea kutoka kwa Ali (as). Na akaitaja hadithi kama ilivyotangulia lakini kwa tofauti kidogo.

## MLANGO UNAOSEMA KUWA MTUKUFU MTUME (SAWW) NA ALI (AS) WANATOKANA NA MTI MMOJA

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 2, Uk. 241[331]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir bin Abdullah kuwa alisema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akimwambia Ali (as): 'Ewe Ali hakika watu wanatokana na miti tofauti, lakini mimi na wewe tunatokana na mti mmoja.' Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasoma: **Na zipo bustani za mizabibu, na mimea mingine, na mitende yenye kuchipua kwenye shina moja na isiochipua kwenye shina moja, nayo inatiliwa maji yale yale.**[332]"' – Al-Hakim amesema: Hii ni hadithi yenye njia sahihi.

**Nasema:** Ameitaja pia as-As-Suyutiyiy ndani ya *ad-Durul-Manthur* mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: **"Na katika ardhi vimo vipande vilivyo karibiana, na zipo bustani za mizabibu, na mimea mingine, na mitende yenye kuchipua kwenye shina moja na isiochipua kwenye shina moja, nayo inatiliwa maji yale yale."**Mwanzoni mwa Sura Raad, na amesema: Kaiandika Ibn Mardawayhi.

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 3, Uk. 160[333]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa mtumishi wa Abdurahman bin Awfi kuwa alisema: "Chukueni kutoka kwangu kabla hadithi hazijachanganyika na batili (uwongo), nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Mimi ni mti na Fatimah ni tawi lake, na Ali ni mpandishiaji wake na Hasan na Husain ni matunda yake, na wafuasi wetu ni majani yake. Shina la mti liko katika pepo ya Aden, na sehemu nyingine za mti huo ziko ndani ya pepo nyingine.'"

331 *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha tafsiri, Mlango wa unyenyekevu wake (saww).

332 **Sura Raad: 4**.

333 *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha kuwajua masahaba, Mlango unaozungumzia fadhila za Fatimah (as).

**Kunuzul-Haqaiq Uk. 155[334]:**

Amesema: "Alisema: 'Watu wote wanatokana na miti tofauti, lakini mimi na Ali tunatokana na mti mmoja."' – Amesema: Kaiandika Tabaraniy.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 154[335]:**

Amesema: Alisema: "Mimi na Ali tunatokana na mti mmoja, na watu wengine wanatokana na miti tofauti."

— Amesema: Ameiandika ad-Daylamiy kutoka kwa Jabir.

**Dhakhairul-Uqba Uk. 16[336]:**

Amesema: Kutoka kwa Abdul-Aziz kwa njia ifikayo kwa Mtukufu Mtume (saww) kuwa alisema: "Mimi na Ahlul-Baiti wangu ni mti uliopo peponi, na matawi yake yapo duniani, yeyote atakayeshikamana nasi atakuwa amejitengenezea njia ya kumfikisha kwa Mola Wake."

— Amesema: Kaiandika Abu Saad ndani ya *Sharafun-Nubuwah*.

## MLANGO UNAOSEMA KUWA MWENYEZI MUNGU ALIMTEUA MTUKUFU MTUME (SAWW) NA ALI (AS)

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 3, Uk. 129[337]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kuwa alisema: "Fatimah (as) alisema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Umenioza kwa Ali bin Abu Talib (as) naye ni mtu fakiri asiyekuwa na mali.' Mtume akamwambia: 'Ewe Fatimah! Hivi huridhii kuwa hakika Mwenyezi Mungu aliwatazama watu wa aridhini na kuwachagua watu wawili kati yao, wa kwanza ni baba yako na mwingine ni mume wako?'"

**Nasema:** Ameipokea al-Khatibu al-Baghdadiy kwa njia tofauti ndani ya *Taarikh* yake Juz. 4, uk. 195[338], na amesema humo: Mtume (saww) alipomuoza Fatimah (as) kwa Ali (as), Fatimah (as) alisema… (akasimulia hadithi).

**Usudul-Ghabah Juz. 4, Uk. 42[339]:**

Ametaja hadithi kwa njia itokayo kwa Ali bin Ali al-Hilaliy kuwa alisema: "Niliingia kwa Mtukufu Mtume (saww) wakati wa maradhi yake yaliyomfisha, nikamkuta Fatimah akiwa kichwani kwake. Fatimah alilia mpaka sauti ikasikika, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akafunua upande wake na kumtazama, akasema: 'Kipenzi changu Fatimah, ni kipi chakuliza?' Akasema: 'Nahofia kupuuzwa baada yako.' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Kipenzi changu, hivi hujui kuwa Mwenyezi Mungu aliwatazama wakazi wa ardhini mara ya kwanza akamteua baba yako kutoka humo, kisha akatazama mara ya pili akamteua mume wako kutoka humo, na akaniletea wahyi kuwa nikuozeshe kwake?'"

[334] *Kunuzul-Haqaiq*: Herufi Nun, Hadithi ya 8211.
[335] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha fadhila za Makhalifa wanne, Fadhila za Ali (as), Hadithi ya 32943.
[336] *Dhakhairul-Uqba*: Mlango unaotaja fadhila za Ahlul-Bait (as).
[337] *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha kuwajua masahaba, Mlango unaozungumzia fadhila za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (as), Ali alikuwa kiongozi wa watu wema.
[338] *Taarikh Baghdadi:* Wasifu wa Ahmad bin Salih, Abu Ja'far al-Muqriu, Namba 1886.
[339] *Usudul-Ghabah:* Herufi Ain, Wasifu wa Ali al-Hilaliy, Namba 3790.

— Amesema: Kaiandika Abu Na'im na Abu Musa.

**Nasema:** Ameitaja pia al-Haythamiy ndani ya *Majmauz-Zawa'id* Juz. 9, uk. 165. Na al-Muhibu Tabari ndani ya *Dahakhairul-Uqba*Uk. 135, kila mmoja kaitaja kwa urefu. Itakuja katika mlango unaosema kuwa Ali ni wasii wa Mtume. Wa kwanza amesema: Kaipokea Tabaraniy ndani ya *al-Kabir* na ndani ya *al-Awsat*. Na wa pili amesema: Kaiandika al-Hafidh Abul-Alai al-Hamadaniy.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 153[340]:**

Amesema: Alisema: "Hivi hujui kuwa Mwenyezi Mungu aliwatazama wakazi wa aridhini akamchagua baba yako kuwa Nabii toka miongoni mwao. Kisha akatazama mara ya pili na kumchagua mume wako, akaniletea wahyi kuwa nikuoze kwake na nikamfanya Wasii?" - Amesema: "Kaisema Fatimah." Kisha akasema: "Kaiandika Tabaraniy kutoka kwa Abu Ayub."

**Nasema:** Ameitaja pia al-Haythamiy ndani ya *Majmauz-Zawa'id* Juz. 8, uk. 253.

**Kanzul-Ummal Juz. 7, Uk. 103[341]:**

Amesema: Alisema: "Hivi huridhii kuwa hakika mimi nimekuoza kwa mtu wa kwanza kusilimu kabla ya Waislamu wote na mwenye elimu kushinda wote. Hakika wewe ndiye bibi mbora kushinda wanawake wote wa ummah wangu kama Mariam alivyokuwa bora kwa jamaa zake. Hivi huridhii ewe Fatimah kwamba Mwenyezi Mungu aliwatazama wakazi wa ardhi na kuchagua watu wawili kutoka miongoni mwao, akamfanya mmoja kuwa baba yako na mwingine kuwa mume wako?" **-** Amesema: Kaiandika al-Hakim na Tabaraniy na al-Khatibu.

**Kanzul-Ummal Juz. 7, Uk. 103[342]:**

Amesema: Kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Hakika Mungu Wangu aliniteua pamoja na watu watatu kutoka katika Ahlul-Baiti wangu, na mimi ndiye bwana wa hao watatu na ndiye bwana wa wana wa Adam Siku ya Kiyama na wala si kujifakharisha. Aliniteua na Ali bin Abu Talib, na Hamza bin Abdul-Muttalib na Ja'far bin Abu Talib. Tulikuwa tumelala huko Abtahi kila mmoja akiwa kalala kwa nguo yake, Ali alikuwa kuliani kwangu, Ja'far kushotoni kwangu na Hamza miguuni kwangu, na hakuna aliyeniamsha kutoka usingizini isipokuwa mbawa za Malaika na ubaridi wa dhiraa ya Ali uliokuwa chini ya shavu langu. Nilipoamka nikamkuta Jibril akiwa na Malaika watatu, mmoja kati ya wale Malaika watatu akasema: 'Ewe Jibril umetumwa kwa nani kati ya hawa wanne?' Akanipiga kwa mguu wake na kusema: 'Kwa huyu, naye ndiye bwana wa wana wote wa Adam.' Akasema: 'Ni nani huyu ewe Jibril?' Akasema: 'Muhammad bin Abdullah bwana wa Manabii, na huyu hapa ni Ali bin Abu Talib na huyu ni Hamza bin Abdul-Muttalib bwana wa Mashahidi, na huyu ni Ja'far, yeye ana mbawa mbili ambazo kwazo ataruka peponi atakavyo."' - Amesema: Kaiandika Ya'qub bin Sufiyan na al-Khatib na Ibn Asakir.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 192[343]:**

Amesema: Alisema: "Hakika Mwenyezi Mugu amewachagua Waarabu kutoka katika watu wote, na amewachagua Kuraishi kutoka katika Waarabu, na amewachagua watoto wa Hashim kutoka kwa Makuraishi,

[340] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha fadhila za Makhalifa wane, Fadhila za Ali (as), Hadithi ya 32923.

[341] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha fadhila za Makhalifa wane, Fadhila za Ali (as), Hadithi ya 32925.

[342] *Kanzul-Ummal*: Kitabu cha fadhila za Ahlul-Baiti na wasiokuwa Masahaba, Faslu inayozungumzia fadhila zao kwa ujumla, Hadithi ya 3726.

[343] *Kanzul-Ummal*: Fadhila za Masahaba zimejikusanya toka kwa watu watatu mpaka kumi na kuendelea, Hadithi ya 3368.

na amenichagua na kuniteua pamoja na kundi kutoka katika Ahlul-Baiti wangu, Ali, Hamza, Ja'far, Hasan na Husain."

## MLANGO UNAOSEMA KUWA MWENYEZI MUNGU ALIMTIA NGUVU MTUKUFU MTUME KUPITIA ALI (AS)

**Taarikh Baghdad Juz. 11, Uk. 173[344]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Nilipopelekwa mbinguni niliona mguu wa Arshi ukiwa umeandikwa: Hapana mungu isipokuwa Allah, Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, nimemtia nguvu kupitia Ali, na nimemnusuru kupitia Ali."'

**Ad-Durul-Manthur ya As-As-Suyutiyiy: Mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: Ametakasika aliyemchukua mja wake usiku mmoja kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali:**

Amesema: Ibn Adiy na Ibn Asakir wameandika kutoka kwa Anas kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Nilipopelekwa mbinguni niliona mguu wa Arshi ukiwa umeandikwa: Hapana mungu isipokuwa Allah, Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, nimemtia nguvu kupitia Ali."'

**Dhakhairul-Uqba Uk. 69[345]:**

Amesema: Kutoka kwa Abu Khamis amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Nilipopelekwa mbinguni niliutazama mguu wa kulia wa Arshi, nikauona umeandikwa maandishi niliyoyafahamu: Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, nimemtia nguvu kupitia Ali na nimemnusuru kupitia yeye."' - Amesema: Ameiandika Mula ndani ya Sira yake.

**Nasema:** Ameitaja pia Ali al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 6, uk. 158[346], kwa tofauti kidogo, ameitaja kutoka kwa Tabaraniy toka ndani ya *al-Kabir* kutoka kwa al-Abu Hamrau.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 158[347]:**

Amesema: Alisema: "Katika usiku niliopelekwa mbinguni niliona mguu wa Arshi ukiwa umeandikwa: Hakika mimi ni Allah ambaye hapana mungu isipokuwa Mimi, nimeiumba pepo ya Aden kwa mkono Wangu. Muhammad ni chaguoLangu kati ya viumbe Wangu, nimemtia nguvu kupitia Ali na nimemnusuru kupitia Ali." – Amesema: Ameiandika Ibn Asakir na Ibn al-Jawziy kwa njia mbili kutoka kwa Abu Hamrau.

**Nasema:** Ameipokea Abu Na'im ndani ya *Hilyatul-Awliyai* Juz. 3, uk. 26[348] kwa njia itokayo kwa Abu Hamrau kwa tofauti kidogo.

---

[344] *Taarikh Baghdad*: Wasifu wa Issa bin Muhammad bin Ubaydullah Abu Musa, Hadithi namba 5876.
[345] *Dhakairul-Uqba*: Kutaja habari ya Mwenyezi Mungu kumtia nguvu Mtume (saww) kupitia Ali (as).
[346] *Kanzul-Ummal*: Fadhila za Ali (as), Hadithi ya 33041.
[347] *Kanzul-Ummal*: Fadhila za Ali (as), Hadithi ya 33040.
[348] *Hilyatul-Awliyai*: Wasifu wa Yunus bin Ubayd ambaye ni sheikh wake katika hadithi.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 158[349]:**

Amesema: Alisema: "Imeandikwa katika mlango wa pepo miaka elfu mbili kabla ya kuumbwa mbingu na ardhi: Hapana mungu isipokuwa Allah, Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, nimemtia nguvu kupitia Ali." - Amesema: Ameiandika al-Uqayliy kutoka kwa Jabir.

## MLANGO UNAOSEMA KUWA HAKIKA ALI (AS) ALIZALIWA NDANI YA KA'ABA NA YEYE ANA CHEO SAWA NA KA'ABA

**Mustadrakus-Sahihayni Juz. 3, Uk. 483[350]:**

Amesema: "Ni habari mutawatiri kuwa Fatimah binti Asad alimzaa Amirul-Muuminina Ali bin Abu Talib akiwa ndani ya Ka'aba.

**Nurul-Abswari Uk. 69[351]:**

Amesema: Amezaliwa r.a. huko Makka ndani ya Nyumba Tukufu, siku ya Ijumaa mwezi kumi na tatu Rajab, mwaka wa thelathini tangu kutokea tukio la tembo, miaka ishirini na tatu kabla ya Mtume kuhamia Madina. Na imesemekana kuwa ni mwaka wa ishirini na tano tangu kutokea tukio la tembo na miaka kumi na mbili kabla ya Mtume kuhamia Madina. Na imesemekana ni kabla ya miaka kumi. Na hakupata kuzaliwa ndani ya Ka'aba mtu yeyote kabla yake. - Amesema: Amesema hilo Ibn as-Swabaghu.

**Kunuzul-Haqaiq Uk. 188[352]:**

Amesema: Alisema: "Ewe Ali! Wewe una cheo sawa na Ka'aba."

— Amesema: Kaiandika ad-Daylamiy.

**Usudul-Ghabah Juz. 4 Uk. 31[353]**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa as-Swanabajiy kutoka kwa Ali (as) kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Wewe una cheo sawa na Ka'aba, unafuatwa wala hupasi kumfuata mtu…"'

[349] *Kanzul-Ummal*: Fadhila za Ali (as), Hadithi ya 33040.
[350] *Mustadrakus-Sahihayn*: Kutaja fadhila za Hakim bin Huzam al-Qarashiy.
[351] *Nurul-Abswar*: Kutaja fadhila za Bwana wetu Ali bin Abu Talib binamu yake Mtukufu Mtume (saww) ambaye ni upanga wa Mwenyezi Mungu wenye sumu.
[352] *Kunuzul-Haqaiq:* Herufi Yau, Hadithi ya 10027.
[353] *Usudul-Ghabah*: Wasifu wa Ali bin Abu Talib (as), Ukhalifa wake.

## MLANGO UNAOSEMA KUWA MTUKUFU MTUME (SAWW) ALIMCHUKUA ALI (AS) KUTOKA KWA ABU TALIB

**Mustadrakus-Sahihayni Juz. 3, Uk. 576[354]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Mujahidu bin Jabri Abu al-Hajjaj, amesema: "Ilikuwa ni miongoni mwa neema za Mwenyezi Mungu juu ya Ali bin Abu Talib (as) kile ambacho Mwenyezi Mungu alimfanyia Ali (as) na ile kheri aliyomtakia. Hakika Makuraishi walipatwa na baa la njaa kali, na Abu Talib alikuwa na watoto wengi, hivyo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia ami yake Abbas, naye alikuwa ndiye mwenye wepesi wa maisha kati ya Bani Hashim: 'Ewe Abul-Fadhli! Hakika kaka yako Abu Talib ana watoto wengi, na watu wamepatwa na baa hili la njaa kali, twende tukampunguzie mzigo kwa kuwachukua baadhi ya watoto wake, mimi nitamchukua mwanaume mmoja kati ya watoto wake na wewe umchukue mmoja.' Abbas akasema: 'Sawa.'

"Walikwenda hadi kwa Abu Talib na kumwambia: Hakika sisi tunataka kukupunguzia mzigo kwa kuwachukua baadhi wa watoto wako mpaka pale watu watakapoondokewa na baa walilonalo. Abu Talib akawaambia: 'Kama mtaniachia Aqil basi fanyeni mtakavyo.' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamchukua Ali (as) na kumkumbatia, na Abbas akamchukua Ja'far na kumkumbatia. Ali (as) aliendelea kuishi na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mpaka alipokabidhiwa utume na yeye akamsadiki. Na Abbas alimchukua Ja'far na aliendelea Ja'far kuishi na Abbas mpaka aliposilimu na kuanza kujitegemea."

**Mustadrakus-Sahihayni Juz. 3, Uk. 576[355]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Zaid bin Ali bin Husain kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake (as), amesema: Alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alitoka nyumbani akiwa na ami zake Abbas na Hamza, wakawakuta Ali, Ja'far na Aqil wakiwa shambani wanafanya kazi, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawaambia ami zake: "Chagueni kutoka katika hawa.' Mmoja wao akasema: 'Nimemchagua Ja'far.' Na mwingine akasema: 'Nimemchagua Aqil.' Mtume akasema: 'Nimekupeni hiyari nanyi mkachagua, nami Mwenyezi Mungu amenichagulia Ali."'

## MLANGO USEMAO KUWA ALI NDIYE WA KWANZA KUUKUBALI UISLAMU

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 301[356]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Hamza, amesema: "Nilimsikia Zayd bin Arqam akisema: "Wa kwanza kuukubali Uislamu ni Ali (as)."

**Nasema:** Kaipokea al-Hakim ndani ya *Mustadrakus-Sahihayn* Juz. 3, Uk. 136, na amesema ni riwaya sahihi. Na ameipokea an-Nasaiy ndani ya *Khasa'is* yake Uk. 2. Na ameipokea Ibn Saad ndani ya *Tabaqat* yake Juz. 3, Sehemu ya kwanza, Uk. 12. Na ameipokea Ibn al-Athir ndani ya *Usudul-Ghabah*, Juz. 4

[354] *Mustadrakus-Sahihayni*: Kitabu cha kuwatambua Masahaba, Kutaja habari za Aqil bin Abu Talib, Mtukufu Mtume awalea watoto wa Abu Talib.

[355] *Mustadrakus-Sahihayni*: Kitabu cha kuwatambua Masahaba, Kutaja habari za Aqil bin Abu Talib, Mtukufu Mtume awalea watoto wa Abu Talib.

[356] *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha fadhila, Fadhila za Ali bin Abu Talib (as), Mlango wa 21, Hadithi ya 3735.

Uk. 17. Na ameitaja al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 6 Uk. 400, amesema: Ameiandika Ibn Abu Shaybah. Na ameipokea Ahmad bin Hanbal ndani ya *Musnad* yake Juz. 4, kwa njia mbili, moja wapo katika Uk. 368 na nyingine katika Uk. 371. Na ameipokea Ibn Jarir Tabari ndani ya *Taarikh* yake Juz. 2 Uk. 55 kwa njia mbili.

**Taarikh Ibn Jarir Tabariy Juz. 2, uk. 57[357]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Muhammad bin al-Munkadir na kutoka kwa Rabiah bin Abu Abdurahman na kutoka kwa Abu Hazim al-Madaniy na kutoka kwa al-Kalbiy kuwa wamesema: "Ali ndiye mtu wa kwanza kuukubali Uislamu." - Amesema: Al-Kalbiy alisema: "Aliukubali Uislamu akiwa ni mtoto wa miaka tisa."

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 3, Uk. 465[358]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: "Abu Musa al-Ash'ariy alisema: 'Hakika Ali ndiye mtu wa kwanza aliyeingia katika Uislamu pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).'" Kisha mwandishi akasema: Hadithi hii ni yenye njia (sanadi) sahihi.

**Mustadrakus-Sahihayni Juz. 3, Uk. 136[359]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Salman, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Mtu wa kwanza kukutana nami katika hodhi kati yenu ni yule aliyekuwa wa kwanza kuukubali Uislamu, Ali bin Abu Talib.'"

**Nasema:** Ameipokea al-Khatib al-Baghdadiy ndani ya *Taarikh* yake Juz. 2, uk. 18. Na ameipokea Ibn Abdul-Barri ndani ya *Istiaab* yake Juz. 2, uk. 457. Na ameipokea Ibn Al-Athiir ndani ya *Usudul-Ghabah* Juz. 4, uk. 17. Na ameitaja al-Munawi ndani ya *Kunuzul-Haqaiq* na amesema: 'Ameiandika ad-Daylamiy.' Na ameitaja al-Mutaqi ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 6, uk. 400, amesema: 'Ameiandika Ibn Abu Shaybah.' Na ameitaja al-Haythamiy ndani *Maj'mauz-Zawa'id* yake Juz. 9, uk. 102, amesema: 'Ameiandika Tabaraniy.'

**Mustadrakus-Sahihayni Juz. 3, Uk. 499[360]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Qays bin Abi Hazim kuwa alisema: "Nilikuwa Madina, wakati nikiwa nazunguka sokoni mara nilifika katika mawe ya kuuzia mafuta, nikawaona watu wamekusanyika hapo wakimshangaa mpanda farasi ambaye alikuwa yuko juu ya mnyama huku akimkashifu Ali bin Abu Talib (as) na watu wamesimama pembeni yake. Mara alikuja Saad bin Abi Waqas, akasimama mbele yao na kusema: 'Kitu gani hiki?' Wakasema: Ni mtu anamkashifu Ali bin Abu Talib. Saad akasogea, walipomuona walimfungulia njia mpaka akasimama mbele ya mtu yule, akasema: "Wewe kwa nini unamkashifu Ali bin Abu Talib? Hivi si yeye aliyekuwa mtu wa kwanza kuukubali Uislamu?Si yeye aliyekuwa mtu wa kwanza kuswali pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu!? Si yeye aliyekuwa mwenye kujinyima kushinda watu wote? Si yeye aliyekuwa na elimu kushinda watu wote?'

"Aliendelea kutaja mpaka akasema: 'Si yeye aliyekuwa mkwe wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)

[357] *Taarikh Tabari*: Kutaja habari za Mtukufu Mtume, kumtaja mtu aliyesema kuwa mwanaume wa kwanza kumwamini Mtukufu Mtume (saww) ni Ali bin Abu Talib (as).

[358] *Mustadrakus-Sahihayni*: Kitabu cha kuwatambua Masahaba, Kutaja fadhila za Abu Musa al-Ash'ariy.

[359] *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha kuwatambua Masahaba, Fadhila za Amirul-Muuminina Ali (as). Mtu wa kwanza kukutana nami katika hodhi ni yule aliyekuwa wa kwanza kuukubali Uislamu.

[360] *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha kuwatambua Masahaba, Mlango wa kutaja fadhila za Abu Is'haqa Saad bin Abi Waqas.

kwa binti yake? Si yeye aliyekuwa mbeba bendera ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika vita vyake?' Kisha alielekea kibla akainua mikono yake na kusema: 'Ewe Mungu Wangu, hakika huyu anamkashifu walii miongoni mwa mawalii wako, usiache mkusanyiko huu utawanyike bila kumuonesha uwezo wako.'"

— Qays anasema: "Wallahi hatukutawanyika isipokuwa tayari mnyama wake alikuwa ameshamwangusha chini na kumbamiza kwenye yale mawe na ubongo wake kupasuka."

— Al-Hakim anasema: Hii ni hadithi sahihi kwa mujibu wa masharti ya Masheikh wawili (Bukhari na Muslim).

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 5, Uk. 26[361]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Maaqal bin Yasar, amesema: "Nilimsafisha Mtume (saww) siku moja, akaniambia: 'Je tunaweza kwenda kwa Fatimah kumtembelea?' Nikasema ndiyo, akasimama akiwa kaniegemea, akasema: 'Hakika uzito wake ataubeba mtu mwingine na malipo yake yatakuwa kwako.' Niliondoka naye na sikupata uzito wowote kana kwamba sijabeba chochote, mpaka tukaingia kwa Fatimah (as), akamwambia: 'Una hali gani?' Fatimah akasema: 'Wallahi huzuni yangu ni kubwa na ufukara wangu ni mkubwa na maradhi yangu yanaendelea?'"

Abu Abdurahman anasema: "Nilikuta hadithi hii ndani ya kitabu cha baba yangu ambacho alikiandika kwa hati yake mwenyewe: Alisema: "Hivi huridhii kuwa mimi nimekuoza kwa mtu wa kwanza kuukubali Uislamu kabla ya watu wote wa umma wangu, na ndiye mwenye elimu kuliko wote na ndiye mwenye busara kuliko wote?"

**Nasema:** Ameitaja al-Mutaqi ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 6, uk. 153, na al-Haythamiy ndani *Maj'mauz-Zawaid* yake Juz. 9, uk. 101, na Uk. 114, na amesema: 'Ameiandika Tabaraniy.' Wa kwanza amesema: 'Kaiandika ndani ya *al-Kabir*.' Na wa pili kasema: 'Kwa wapokezi waaminifu.'

**Musnad Imam Abi Hanifa Uk. 247[362]:**

Kapokea kwa njia yake kutoka kwa Habah, amesema: "Nilimsikia Ali (as) akisema: 'Mimi ndiye mtu wa kwanza kuingia katika Uislamu, na aliswali pamoja nami Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).'"

**Nasema:** Ameipokea al-Khatib al-Baghdadiy ndani ya *Taarikh* yake Juz. 4 Uk. 233.

**Al-Isabah Juz. 4, Sehemu ya kwanza, Uk. 118[363]:**

Amesema: Ameipokea Ibn Shahin kwa njia ya Ibrahim bin Ja'far, kutoka kwa baba yake Ja'far bin Abdullah bin Salamah, kutoka kwa Amru bin Murrah al-Jahniy na Abdullah bin Nadhalah al-Mazniy, kutoka kwa Jabir, amesema: "Hakika wao walikuwa wakisema: Ali bin Abu Talib ndiye mtu wa kwanza kuingia katika Uislamu."

**Al-Isabah Juz. 8, Sehemu ya kwanza, Uk. 183[364]:**

Amesema: Ameandika Ibn Mundah kutoka katika riwaya ya Ali bin Hashim bin al-Baridu, amesema: Alinisimulia Layla al-Ghafariyyah, alisema: "Nilikuwa napigana vita pamoja na Mtukufu Mtume (saww). Nilikuwa nikiwapa huduma ya matibabu majeruhi, na kuwauguza wagonjwa. Alipotoka Ali (as) kwenda Basra (kwenda kwenye vita vya Ngamia) nilikwenda pamoja naye. Nilipomuona Aisha nilimfuata na

[361] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Hadithi ya Maaqal bin Yasar, Hadithi namba 19796.

[362] Musnad Imam Abi Hanifa pamoja na Sharhu yake ya Imam Mula Ali al-Qariy, Uk. 498 - 499 Chapa ya Darul-Kutubi al-Ilmiyah, Beirut.

[363] *Al-Isabah*: Herufi Ain, Wasifu wa Abdullah bin Fadhalah al-Mazniy, Namba 974.

[364] *Al-Isabah*: Kitabu cha wanawake, Herufi Laam, Wasifu wa Layla al-Ghafariyyah, Namba 974.

kumwambia: 'Je ulisikia fadhila yoyote ya Ali (as) kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)?' Akasema: 'Ndio, siku moja aliingia kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) wakati Mtume akiwa pamoja nami huku akiwa kajifunika nguo nzito. Alipoingia alikuja na kuketi baina yetu, nikasema: Hivi nafasi yote hii hujapata sehemu ya kuketi isipokuwa hii? Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: Ewe Aisha! Niachie ndugu yangu, hakika yeye ndiye mtu wa kwanza kuukubali Uslamu kabla ya watu wote, na ndiye mtu wa mwisho ambaye nitaagana naye, na ndiye mtu wa kwanza ambaye atakutana na mimi Siku ya Kiyama."'

**Usudul-Ghabah Juz. 5, Uk. 520[365]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa al-Harith kutoka kwa Ali (as) kuwa alisema: "Abu Bakr na Umar walikwenda kuchumbia – yaani kumchumbia Fatimah – kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawakatalia, Umar akasema: 'Ni wa kwako ewe Ali.' Nikasema: 'Sina chochote isipokuwa deraya yangu nitakayoiweka rehani.' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akanioza Fatimah, alipopata habari hiyo Fatimah, alilia. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaingia kwake na kumwambia: 'Una nini ewe Fatimah mbona unalia? Wallahi nimekuoza kwa mtu ambaye ndiye mwenye elimu kushinda watu wote na ndiye mpole kuwashinda wote na ndiye wa kwanza kuukubali Uislamu kabla yao wote."'

**Nasema:** Ameitaja al-Mutaqy ndani ya *Kanzul-Ummal*, Juz. 6, Uk. 392, humo amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akanioza Fatimah (as)…."Na Amesema: Ameiandika Ibn Jarir na kusema kuwa ni sahihi, na ad-Dawlabiy ndani ya *ad-Dhuriyyah at-Twahirah*.

**Ar-Riyadhu an-Nadhrah Juz. 2, uk. 182[366]:**

Amesema: Kutoka kwa Anas, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipomuoza Fatimah (as) kwa Ali, alisema: 'Ewe Ummu Ayman! Mpeleke binti yangu kwa Ali na mwamrishe asianze kujamiiana naye mpaka nije.' Aliposwali Isha alikwenda na chombo kilichokuwa na maji, akayasomea dua maji hayo kadiri Mwenyezi Mungu alivyotaka, kisha akasema: 'Kunywa ewe Ali na uchukue udhuu, na kunywa ewe Fatimah na uchukue udhuu.' Kisha aliwafungia mlango, Fatimah akalia. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Kitu gani chakuliza wakati nimekuoza kwa mtu ambaye ndiye wa kwanza kuukubali Uislamu kabla yao wote na ndiye mwenye tabia nzuri kuliko wote."' - Amesema: Ameiandika Abul-Khair al-Hakimiy.

**Al-Istiaab Juz. 2, Uk. 456[367]:**

Amesema: Amepokea kutoka kwa Salman, Abu Dhari, Miqdad, Abu Said al-Khudriy na Zayd bin Arqam, kuwa Ali bin Abu Talib (as) ndiye mtu wa kwanza kuingia katika Uislamu, na hawa wanamuona ndiye bora kumshinda mwingine yeyote.

**Al-Istiaab Juz. 2, Uk. 457[368]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Umar na kutoka kwa mtumishi wa Afrah, kuwa amesema: "Muhammad bin Kaab al-Qaradhiy aliulizwa kuhusu mtu wa kwanza kuingia katika Uislamu ni Ali (as) au ni

[365] *Usudul-Ghabah*: Kitabu cha wanawake, Hefuri Fau, Wasifu wa Fatimah binti ya Rasuli wa Mwenyezi Mungu (saww).

[366] *Ar-Riyadh an-Nadhrah*: Mlango wa fadhila za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (as), alimpa upendeleo makhususi kwa kumuoza Fatimah (as).

[367] *Al-Istiaab*: Herufi Ain, Mlango unaozungumzia wasifu wa Ali bin Abu Talib (as).

[368] *Al-Istiaab*: Herufi Ain, Mlango unaozungumzia wasifu wa Ali bin Abu Talib (as).

Abu Bakr? Akasema: Subhanallah! Ali ndiye wa kwanza wao kuingia katika Uislamu, na hakika jambo hili limewachanganya watu kwakuwa Ali alificha Uislamu wake kwa kumuogopa Abu Talib, lakini Abu Bakr aliposilimu alidhihirisha Uislamu wake, na hapana shaka kuwa kwetu sisi Ali (as) ndiye wa kwanza kuukubali Uislamu kabla yao wote."

**Al-Istiaab Juz. 2, Uk. 458[369]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Qatadah, kutoka kwa Hasan, amesema: "Ali aliukubali Uislamu akiwa mtu wa kwanza kuukubali Uislamu, naye alikuwa ni mtoto wa miaka kumi na tano au kumi na sita."

**Al-Istiaab Juz. 2, Uk. 458[370]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Mtu wa kwanza kuukubali Uislamu ni Ali." - Kisha Amesema: Imepokewa kutoka kwa Ibn Umar kwa njia mbili nzuri.

**Nasema:** Na ameipokea Ibn al-Athiir katika *Usudul-Ghabah* Juz. 4, uk. 17. Na ameitaja al-Haythamiy ndani ya *Maj'mauz-Zawa'id* yake Juz. 9, uk. 12, ameitaka kwa kunukuu toka kwa Tabaraniy.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 395[371]:**

Amesema: Kutoka kwa Umar, amesema: "Msimtukane Ali, hakika mimi nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema mambo matatu kuhusu Ali. Mimi kuwa na jambo moja kati ya mambo matatu ni jambo nilipendalo sana kuliko kuwa na vitu vyote vilivyochomozewa na jua. Nilikuwa kwa Mtukufu Mtume (saww) pamoja na Abu Bakr, Abu Ubaydah bin Jarah na Masahaba kadhaa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Mtume akapiga mkono wake begani kwa Ali (as) na kusema: 'Wewe ndiye mtu wa kwanza kuukubali Uislamu kabla ya watu wote, na ndiye mtu wa kwanza kuamini kabla ya watu wote na wewe kwangu mimi ni sawa na Harun kwa Musa."

— Amesema: Kaiandika Ibn an-Najar.

**Nasema:** Ameitaja pia kwa njia nyingine isemayo: Kutoka kwa Ibn Abbas, alisema: "Umar bin Khattab alisema: 'Acheni kumtaja vibaya Ali bin Abu Talib (as). Hakika mimi nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema mambo matatu kuhusu Ali, mimi kuwa na moja …..Alisimulia hadithi kama ilivyotangulia, mwishoni akasema: 'Ni muongo yule anayedai kuwa ananipenda wakati anakuchukia wewe.'

Amesema: Ameiandika Hasan bin Badru katika hadithi walizozipokea Makhalifa, na al-Hakim ndani ya *al-Kuna*, na as-Shiraziy ndani ya *al-Alqab* na Ibn an-Najari.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 153[372]:**

Amesema: Kutoka kwa Abi Is'haqa, amesema: "Hakika Ali (as) alipomuoa Fatimah (as), Mtume alimwambia Fatimah: 'Nimekuoza kwake, hakika yeye ndiye sahaba wangu wa kwanza kuukubali Uislamu, na ndiye mwenye ilimu kuwashinda wote na ndiye mpole kuwashinda wote."' - Amesema: Kaiandika Tabaraniy.

[369] *Al-Istiaab*: Herufi Ain, Mlango unaozungumzia wasifu wa Ali bin Abu Talib (as).
[370] *Al-Istiaab:* Herufi Ain, Mlango unaozungumzia wasifu wa Ali bin Abu Talib (as).
[371] *Kanzul-Ummal*: Fadhila za Ali (as), Hadithi ya 36395.
[372] Kanzul-Ummal: Fadhila za Ali (as), Hadithi ya 32937.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 153 na Uk. 397[373]:**

Amesema: Alisema: "Nimekuoza kwa mtu bora kushinda watuwangu wote, ni mwenye elimu kuwashinda wote, ni mpole kuwashinda wote na ndio wa kwanza wao kuingia katika Uislamu kabla yao wote."

Amesema: Alisema hayo kumwambia Fatimah (as). Kisha akasema: Ameiandika al-Khatibu ndani ya *al-Mutaffaq* na ndani ya *al-Muftaraq* kutoka kwa Buraydah.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 153[374]:**

Amesema: Alisema: "Hivi huridhii kuwa hakika mimi nimekuoza kwa mtu ambaye ndiye Mwislamu wa kwanza na mwenye elimu kushinda wote. Hakika wewe ni bibi mbora wa wanawake wote wa ummah wangu kama ambavyo Mariam alikuwa bibi mbora kwa jamaa zake.."

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 156[375]:**

Amesema: Alisema: "Hakika Malaika waliniswalia mimi na Ali miaka saba kabla binadamu yeyote hajaukubali Uislamu." - Amesema: Ameiandika Ibn Asakiri.

**Hilyatul-Awliyai Juz. 4, Uk. 294[376]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Hasan, amesema: "al-Hajjaj alikwenda kwa Said bin Jubair na kumwambia: 'Wewe ni Shaqiyu (muovu) bin Kasiri.' Akasema: 'Mimi ni Said (mwema) bin Jubair.' Akasema: 'Wewe ni Shaqiyu (muovu) bin Kasiri.' Akasema: 'Mama yangu alikuwa alijua jina langu vizuri kuliko wewe.' Akasema: 'Unasemaje kuhusu Muhammad?' Akasema: 'Unamaanisha Mtume (saww)?' Akasema: 'Ndiyo.' Akasema: 'Yeye ni bwana wa wana wote wa Adam, Nabii Mteule, ndiye mbora kushinda wote waliobaki hai na kushinda wote waliopita.'"

Aliendelea kusimulia mpaka aliposema: "Akasema: Unasemaje kuhusu Ali? Akasema: 'Yeye ni binamu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, ni wa kwanza kuukubali Uislamu, ni mume wa Fatimah na ni baba wa Hasan na Husain (as)."

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9, uk. 220[377]:**

Amesema: Kutoka kwa Malik bin al-Huwayrith, amesema: "Mtu wa kwanza kuukubali Uislamu miongoni mwa wanaume ni Ali (as), na miongoni mwa wanawake ni Khadija (as)." - Amesema: Kaipokea Tabaraniy.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9, uk. 220[378]:**

Amesema: Kutoka kwa Buraydah, amesema: "Khadija ni mtu wa kwanza kuukubali Uislamu pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na Ali bin Abu Talib (as)." - Amesema: Kaipokea Tabaraniy.

---

[373] *Kanzul-Ummal*: Fadhila za Ali (as), Hadithi ya 32926. Na Fadhila za Ali, Hadithi ya 36423.

[374] *Kanzul-Ummal*: Fadhila za Ali (as), Hadithi ya 32925.

[375] *Kanzul-Ummal*: Fadhila za Ali (as), Hadithi ya 32989.

[376] *Hilyatul-Awliyai*: Wasifu wa Said bin Jubair, Habari zilizopokewa kutoka kwake kuhusu kumhofisha kwake al-Hajjaj, na hadithi inayohusu kuuwawa kwake.

[377] *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid*: Mlango unaozungumzia fadhila za Khadija binti Khuwaylid mke wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

[378] *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid:* Mlango unaozungumzia fadhila za Khadija binti Khuwaylid mke wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9, uk. 220[379]:**

Amesema: Kutoka kwa Abu Rafiu, amesema: "Wa kwanza kuukubali Uislamu miongoni mwa wanaume ni Ali (as), na wa kwanza kuukubali Uislamu miongoni mwa wanawake ni Khadija." - Amesema: Kaipokea al-Bazar, na wapokezi wake ni wapokezi sahihi.

**Ad-Durul-Manthur ya As-As-Suyutiyiy: Mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: Na nyinyi mtakuwa namna tatu:**

Amesema: Ibn Mardawayhi ameandika kutoka kwa Ibn Abbas kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: **"Na wa mbele watakuwa mbele."** Amesema: "Iliteremka ikimuhusu Ezekiel muumini wa familia ya Firaun, na Habibu an-Najar ambaye katajwa katika Sura Yasin, na Ali bin Abu Talib (as), na kila mmoja kati ya hao watatu atakua mbele ya ummah wake, na Ali ndiye atakuwa mbele yao wote."

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 152[380]:**

Amesema: "Waliotangulia ni watatu: Aliyetangulia kwa Musa ni Yoshua bin Nun, aliyetangulia kwa Isa ni aliyezungumziwa katika Sura Yasin, na aliyetangulia kwa Muhammad ni Ali bin Abu Talib (as). - Amesema: Ameiandika Tabaraniy na Ibn Mardawayhi kutoka kwa Ibn Abbas.

**Nasema:** Ameitaja pia al-Munawi ndani ya *Faydhul-Qadir al-Mutni* Juz. 4, uk. 135. Na ameitaja Ibn Hajar ndani ya *Sawaiqul-Muhriqah*Uk. 72, na amesema: 'Ameiandika ad-Daylamiy kutoka kwa Aisha.' Na ameitaja al-Muhibu Tabari ndani ya Dhakhairu yake Uk. 58, na ndani ya *ar-Riyadh an-Nadhrah*, Juz. 2, uk. 158, na amesema: 'Ameiandika Ibn ad-Dhahak ndani ya *al-Ahad* na al-*Mathaniy*.' Na ameitaja as-As-Suyutiyiy ndani ya *ad-Durul-Manthur* mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: Na ninyi mtakuwa aina tatu, na amesema: 'Ameiandika Ibn Abi Hatim kutoka kwa Ibn Abbas.'

**Al-Quswas cha at-Thaalabiy Uk. 238[381]:**

Amesema: Imepokewa kutoka kwa Mtukufu Mtume (saww) kuwa alisema: "Walio mbele katika ummah ni watatu, hawajawahi kumkufuru Mwenyezi Mungu hata kidogo: Ezekiel muumini wa familia ya Firaun, Habibu an-Najari aliyezungumziwa ndani ya Sura Yasin, na Ali bin Abu Talib (as) na ndiye mbora wao."

**Nasema:** Na ameitaja katika Uk. 257, na amesema: "Ali ndiye muumini wa Aaali Muhammad, naye ndiye mbora wao." Na ameitaja katika Uk. 558 na kutaja sanad yake, na amesema: "Ametupa habari al-Khamashawi kwa njia yake itokayo kwa Ibn Abi Layla kutoka kwa baba yake, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema." Akaitaja hadithi kama ilivyotangulia. Na ameitaja Zamakhshari ndani *al-Kashaf* katika tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: **"Na akaja mtu mbio kutokea upande wa mbali wa mjini, akasema: Enyi watu wangu! Wafuateni hawa waliotumwa."** Katika Sura Yasin.

**Ad-Durul-Manthur ya As-As-Suyutiyiy: Mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: "Na wapigie mfano wa wakaazi wa mji walipo wafikia walio tumwa":**

Amesema: Ibn Adiy na Ibn Asakir wameandika: "Watu watatu kamwe hawakuwahi kumkufuru Mwenyezi Mungu: Muumini wa Aali Yasin, Ali bin Abu Talib (as) na Asia mke wa Firauni."

[379] *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid*: Mlango unaozungumzia fadhila za Khadija binti Khuwaylid mke wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

[380] *Kanzul-Ummal*: Fadhila za Ali (as), Hadithi ya 32896.

[381] *Quswasul-Anbiyai (as) al-Musamma Araisul-Majalis*: Mlango unaozungumzia kisa cha Musa kumuuwa Mkibti na kutoka kwake Misri hadi katika maji ya Madyan.

**Taarikh Baghdad Juz. 14, Uk. 155[382]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Watu watatu hawakuwahi kuukufuru wahyi hata kidogo: Muumini wa Aali Yasin, Ali bin Abu Talib (as) na Asia mke wa Firauni."'

**Tahdhibut-Tahdhib Juz. 7, Uk. 236: Katika wasifu wa Afifu al-Kindiy[383]:**

Amesema: Aliposilimu al-Askariy – yaani Afif- alisema: "Natamani Mwenyezi Mugu angekuwa ameniruzuku Uislamu tangu zamani ili niwe wa pili pamoja na Ali (as)."

**Nasema:** Hadithi hii inaonesha kuwa Ali ndiye aliyekuwa wa kwanza kuukubali Uislamu, na kitafuata kisa cha Afif kwa njia tofauti katika mlango usemao: "Ali (as) ndiye mtu wa kwanza kuswali." Ngojea kitakufikia.

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 3, Uk. 125[384]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Is'haqa, amesema: "Nilimuuliza Qutham bin Abbas: Ilikuwaje Ali (as) akamrithi Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) badala ya ninyi? Akasema: 'Kwa sababu yeye alikuwa wa kwanza wetu kuungana naye na mwenye kushikamana naye zaidi kuliko sisi."'–Amesema: Hadithi hii ni yenye sanad sahihi.

**Nasema:** Kaitaja al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 6, Uk. 400 kutoka kwa Ibn Abi Shaybah.

**Nurul-Abswari Uk. 69[385]:**

Amesema: "Imenukuliwa kutoka kwake –yaani kutoka Fatimah binti Asad – kuwa yeye alikuwa kila anapotaka kulisujudia sanamu –wakati Ali (as) akiwa ndani ya tumbo lake – Ali huweka miguu yake juu ya tumbo lake na kukutanisha mgongo wake na mgongo wa Fatimah na hivyo kumzuia kusujudu, na kwa ajili hiyo anapotajwa husemwa: 'Mwenyezi Mungu autukuze uso wake.' Usiweze kulisujudia sanamu."

**Nasema:** Kinachodhihiri kutoka katika hadithi hii ni kuwa Ali (as) aliukubali Uislamu kabla hata hajazaliwa, bali alikuwa ni mwanatauhidi hata kabla Mtume hajakabidhiwa unabii.

## MLANGO USEMEAO KUWA ALI (AS) NDIYE MTU WA KWANZA KUMWAMINI MTUKUFU MTUME (SAWW)

**Taarikh Ibn Jarir Tabari Juz. 2, uk. 75[386]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Is'haqa, amesema: "Mwanaume wa kwanza kumwamini Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), kuswali pamoja naye na kusadiki yale aliyokuja nayo kutoka kwa Mwenyezi Mungu alikuwa ni Ali bin Abu Talib (as), wakati huo alikuwa ni mtoto wa miaka kumi. Na

382 *Taarikh Baghdad*: Wasifu wa Yahya bin Husain al-Madainiy, Hadithi namba 7468.
383 *Tahdhibut-Tahdhib:* Herufi Ain, Katika wasifu wa Afif al-Kindiy, Namba 426.
384 *Mustadrakus-Sahihayni*: Kitabu cha kuwatambua Masahaba, Mlango wa kutaja fadhila za Amirul-Muuminin Ali (as).
385 *Nurul-Abswari*: Katika kutaja fadhila za Bwana wetu Ali bin Abu Talib (as).
386 *Taarikh Tabari*: Kuwataja baadhi ya wale waliosema kuwa mwanaume wa kwanza kumwamini Mtume wa Mwenyezi Mungu na kuswali pamoja naye ni Ali bin Abu Talib.

miongoni mwa mambo aliyoneemeshwa Ali bin Abu Talib (as) na Mwenyezi Mungu ni kuwa alikuwa analelewa na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hata kabla ya Uislamu.

**Ad-Durul-Manthur ya As-As-Suyutiyiy: Mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: Basi pelekeni muamuzi kutokana na jamaa za mume, na muamuzi kutokana na jamaa za mke:**

Amesema: Tabaraniy, al-Hakim, Abu Naiim ndani ya *al-Hilyah* na al-Bayhaqiy ndani ya *Sunani* yake, wote wameandika kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: "Mahururiyyah walipojitenga walikuwa bondeni peke yao, nikamwambia Ali (as): Ewe Amirul-Muuminin pumzika kuswali, nataka kwenda kwa jamaa hawa na kuzungumza nao. Nilitoka na kwenda kwao huku nikiwa nimevaa nguo nzuri niliyokuwa nayo, wakasema:' Karibu ewe Ibn Abbas, mbona umependeza hivi?' Nikasema: Ni aibu gani mnayoiona kwangu? Hakika nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa kavaa nguo nzuri kabisa na Mwenyezi Mungu akateremsha: **Sema: Ni nani aliye haramisha pambo la Mwenyezi Mungu alilowatolea waja wake, na vilivyo vizuri katika riziki.**[387] Wakasema: 'Kitu gani kilichokuleta hapa?' Nikasema: Niambieni nijambo gani baya mwaliona kwa binamu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na mkwe wake na mtu wa kwanza kumwamini wakati Masahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu wakiwa pamoja naye.?"Kisha aliendelea kusimulia hadithi ndefu mpaka aliposema: "Wakarejea kutoka kwao watu elfu ishirini, na wakabakia watu elfu nne, hao wakauwawa."

**Nasema:** Ameitaja al-Haythamiy ndani ya *Maj'mauz-Zawa'id* Juz. 6, uk. 239, na amesema: "Ameipokea Tabaraniy na Ahmad amepokea sehemu tu ya riwaya hiyo. Na wapokezi wao ni wapokezi sahihi."

**Ad-Durul-Manthur ya As-As-Suyutiyiy: Mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: "Je, mnafanya kuwanywesha maji Mahujaji na kuamirisha Msikiti Mtakatifu ni sawa na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho:"**

Amesema: Ameandika Abu Na'im katika *Fadhailus-Sahabah*, na Ibn Asakir, kutoka kwa Anas kuwa alisema: "Abbas na Shayba mtunza Nyumba walikaa na kuanza kujigamba, Abbas akamwambia Shayba: 'Mimi ni adhimu kuliko wewe, mimi ni ami ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), ni wasii wa baba yake na mtoa huduma ya maji kwa mahujaji.' Shayba akasema: 'Mimi ni adhimu kuliko wewe, mimi ndiyo mtunzaji wa Nyumba ya Mwenyezi Mungu na muweka hazina wake, kwa nini basi asikuamini kama alivyoniamini?' Mara akatokeza Ali mbele yao, wakamweleza waliyoyasema, Ali (as) akasema: 'Mimi ni adhimu kuliko ninyi, mimi ndiye wa kwanza kuamini na kuhama.' Wakatoka wote watatu na kwenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), walipomwambia hakuwajibu kitu, hivyo wakaondoka, ndipo wahyi ukateremka baada ya siku kadhaa. Mtume akawaita na kuwasomea: **"Je, mnafanya kuwanywesha maji Mahujaji na kuamirisha Msikiti Mtakatifu ni sawa na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na akapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhaalimu."**

**Sunanul-Bayhaqiy Juz. 6 Uk. 206[388]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Hasan na mwingineo: "Mtu wa kwanza kumwamini Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa ni Ali bin Abu Talib, wakati huo akiwa ni mtoto wa miaka kumi na mitano au kumi na sita."

**Nasema:** Kaitaja al-Haythamiy ndani ya *Maj'mauz-Zawaid* Juz. 9, uk. 102, akinukuu kutoka kwa Tabaraniy, amesema: 'Wapokezi wake ni wapokezi sahihi.'

[387] Sura Aaraf: 32.

[388] *Sunanul-Bayhaqiy:* Kitabu kinachozungumzia mtoto wa kuokota, Mlango unaosema kuwa atahukumiwa kuwa ni Mwislamu, Hadithi ya 12164.

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 3[389]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Amru bin Ibad bin Abdullah kuwa alisema: "Ali (as) alisema: 'Mimi ni mja wa Mwenyezi Mungu na ndugu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), na mimi ndiye msemakweli bora, hatasema haya baada yangu isipokuwa muongo. Niliamini miaka saba kabla ya watu kuanza kuamini."'

**Usudul-Ghabah Juz. 4 Uk. 19[390]**

Amesema: Ametupa habari Abu Ja'far bin as-Samini kwa njia yake ifikayo kwa Yunus bin Bakiri, kutoka kwa Abu Is'haqa anapotaja majina ya waliohudhuria Badri miongoni mwa Makuraishi, kisha miongoni mwa Bani Hashim, amesema: "Na Ali bin Abu Talib, na yeye ndiye wa kwanza kumwamini Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)."

**Al-Istiaab Juz. 2, Uk. 759[391]:**

Amesema katika wasifu wa Layla al-Ghafariyyah, hadithi yake: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Aisha: "Huyu Ali bin Abu Talib, ndiye mtu wa kwanza kuamini kabla ya watu wote."
— Amesema: Kaipokea kutoka kwake Muhammad bin Qasim at-Taiy.

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2 Uk. 157[392]:**

Amesema: Kutoka kwa Abu Dhari, amesema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akimwambia Ali (as): 'Wewe ndiye mtu wa kwanza aliyeniamini mimi na kunisadiki."'

— Amesema: Kaiandika al-Hakimiy.

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2 Uk. 157[393]:**

Amesema: Kutoka kwa Maadhah al-Adawiyyah, amesema: "Nilimsikia Ali (as) akiwa juu ya mimbari huko Basra akisema: 'Mimi ndiye msema kweli bora. Niliamini kabla hata Abu Bakr hajaamini na niliukubali Uislamu hata kabla Abu Bakr hajasilimu."'

— Mwandishi amesema: Ameiandika Ibn Qutaybah ndani ya *al-Maarif*.

**Nasema:** Ameitaja al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 6, uk. 405, amesema: "Ameiandika Muhammad bin Ayubi ndani ya Juzuu yake na ndani ya *al-Aqiliy*." Na ameitaja ad-Dhahabiy ndani ya *Mizanul-Iitidal* Juz. 1, uk. 417 kwa muhtasari kutoka kwenye kitabu *al-Aqiliy*.

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2 Uk. 198[394]:**

Amesema: Kutoka kwa Mu'adh bin Jabal, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Ali (as): 'Utawasimamishia watu hoja kwa mambo saba na hakuna yeyote miongoni mwa Maquraishi

[389] *Khasa'isun-Nasaiy*: Mlango wa Swala ya Amirul-Muuminina Ali bin Abu Talib, Tofauti ya lafudhi za walionukuu.
[390] *Usudul-Ghabah*: Herufi Ain, Wasifu wa Ali bin Abu Talib (as), Kuhudhuria kwake Badri na katika vita vingine.
[391] *Al-Istiaab*: Herufi Ain, Kitabu cha wanawake, Wasifu wa Layla al-Ghafariyyah.
[392] *Ar-Riyadh an-Nadhrah*: Mlango wa fadhila za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib, Kutaja kuwa yeye ndiye wa kwanza kuukubali Uislamu.
[393] *Ar-Riyadh an-Nadhrah*: Mlango wa fadhila za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib, Kutaja kuwa yeye *ndiye wa kwanza kuukubali Uislamu.*
[394] *Ar-Riyadh an-Nadhrah*: Mlango wa fadhila za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib, Kutaja kuwa yeye ndiye ajuaye hukumu kuliko ummah wote.

atakayeweza kujibu hoja yako: Wewe ndiye wa kwanza wao kumwamini Mwenyezi Mungu, ndiye mwenye kutekeleza ahadi ya Mwenyezi Mungu kushinda wao, ndiye mwenye kusimamia ipasavyo amri ya Mwenyezi Mungu kuliko wao, ndiye mwenye kugawa kwa usawa kuliko wao, ndiye mwadilifu zaidi kwa raia kuliko wao, ndiye mjuzi zaidi wa hukumu kuliko wao na ndiye mwenye fadhila adhimu zaidi kuliko wao."' – Amesema: Ameiandika al-Hakimiy.

**Nasema:** Na pia ameipokea Abu Na'im ndani ya *Hilyatul-Awliyai* Juz. 1, Uk. 66.

**Al-Isabah Juz. 7, Sehemu ya kwanza, Uk. 167[395]:**

Amesema: Ameandika Abu Ahmad na Ibn Mundah na wengineo kwa njia ya Is'hqa bin Bashari al-Asadiy, kutoka kwa Khalid bin al-Harith, kutoka kwa Awfi, kutoka kwa Hasan, kutoka kwa Abu Layla al-Ghafariy, amesema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Kutakuwa na machafuko baada yangu, hilo likitokea basi shikamaneni na Ali bin Abu Talib, kwani hakika yeye ndiye mtu wa kwanza aliyeniamini, na ndiye mtu wa kwanza atakayenipa mkono Siku ya Kiyama, naye ndiye msema kweli bora, naye ndiye mtenganishi wa batili na haki katika ummah huu, naye ndiye kiongozi wa Waumini na mali ndio kiongozi wa wanafiki."'

**Faydhul-Qadir Juz. 4, uk. 358[396]:**

Amesema: Amepokea Tabaraniy na al-Bazar kwa urefu kutoka kwa Abu Dharr na Salman, wamesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimshika Ali (as) mkono na kusema: 'Huyu ndiye wa kwanza kuniamini mimi, huyu ndiye wa kwanza atakayenipa mkono Siku ya Kiyama, na huyu ndiye msema kweli bora, na huyu ndiye mtenganishi wa batili na haki katika ummah huu, na huyu ndiye kiongozi wa Waumini na mali ndio kiongozi wa madhalimu."'

**Nasema:** Ameitaja al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 6, uk. 156 kwa kunukuu kutoka kwa Tabaraniy toka ndani ya *al-Kabir*, kutoka kwa wote wawili Salman na Abu Dharr. Na kwa kunukuu kutoka kwa al-Bayhaqiy toka ndani ya *as-Sunanul-Kubra*, na kutoka kwa Ibn Adiy toka ndani ya *al-Kamil* kutoka kwa Hudhayfa.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 393[397]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Maamun, kutoka kwa Rashid, kutoka kwa Mahdi, kutoka kwa Mansuri, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Abdullah bin Abbas, alisema: "Nilimsikia Umar bin Khattab akisema: 'Acheni kumtaja vibaya Ali bin Abu Talib, hakika nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akithibitisha kwake sifa ambazo familia ya Khattab kuwa na sifa moja kati ya hizo ni jambo nilipendalo zaidi kuliko vyote vilivyochomozewa na jua. Nilikuwa mimi na Abu Bakr na Abu Ubaydah pamoja na kundi la Masahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Tulikwenda mpaka katika mlango wa Ummu Salamah, tukamkuta Ali (as) akiwa kasimama mlangoni, tukasema: Tunamtaka Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), akasema: 'Karibu atatoka.' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipotoka alimwegemea Ali bin Abu Talib kisha alipiga mkono wake juu ya bega lake na kusema: Hakika wewe ni mtoa hoja na utatoa hoja, wewe ndiye muumini wa kwanza kabla ya waumini wote, ndiye mjuzi zaidi wa masiku ya Mwenyezi Mungu kuliko wao, ndiye mtekelezaji zaidi wa ahadi Yake kuliko wao, ndiye mgawaji kwa usawa zaidi kuliko wao, ndiye mwenye huruma zaidi na raia kuliko wao, na ndiye mwenye

395 *Al-Isabah*: Herufi Laam, Wasifu wa Ali bin Abu Talib. Sifa zake kwa mujibu wa ulimi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).
396 *Faydhul-Qadir*: Herufi Ain, Fadhila za Ali (as).
397 *Kanzul-Ummal*: Fadhila za Ali (as), Hadithi ya 36378.

fadhila adhimu zaidi kuliko wao. Wewe ndiye nguvu yangu, ndiye utakayeniosha, ndiye utakayenizika na ndiye utakayesonga mbele kuelekea katika kila zito na la hatari, na kamwe baada yangu hutakuwa kafiri, wewe utakuwa mbele yangu na bendera ya himidi, na utaihami familia yangu.'"

Kisha Ibn Abbas akasema toka ndani ya nafsi yake mwenyewe: "Ali (as) amefuzu kwa kuwa na ukwe na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), kwa kuwa na nguvu katika familia, kwa kutoa misaada, kwa kuwa na elimu ya uteremsho (Aya za Qur'ani), kwa kuielewa tafsiri, na kwa kupata marafiki."

**Nasema:** Imetangulia katika mlango uliotangulia riwaya kutoka ndani ya *Kanzul-Ummal* kutoka kwa Umar, aliposema: "Akapiga –Yaani Mtume - kwa mkono wake juu ya bega la Ali (as) na kusema: 'Wewe ndiye wa kwanza kuukubali Uislami kabla ya watu wote, na wewe ndiye wa kwanza kuamini kabla ya watu wote…"'

## MLANGO USEMAO KUWA IMANI YA ALI (AS) ITASHINDA

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 156[398]:**

Amesema: "Laiti kama mbingu na ardhi zitawekwa katika mkono mmoja na imani ya Ali (as) ikawekwa mkono mwingine basi imani ya Ali itashinda."

— Amesema: Ameiandika kutoka kwa Ibn Umari.

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 6, uk. 226[399]:**

Amesema: Kutoka kwa Umar bin Khattab, alisema: "Nashahidia mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuwa nilimsikia akisema: 'Laiti kama mbingu na ardhi zitawekwa katika mkono mmoja na imani ya Ali (as) ikawekwa mkono mwingine basi imani ya Ali itashinda."'

— Amesema: Ameiandika Ibn as-Saman, na al-Hafidh as-Salafiy ndani ya *al-Mashikhatul-Baghdadiyyah,* na al-Fadhailiy.

## MLANGO USEMAO KUWA ALI (AS) NDIYE MTU WA KWANZA KUSWALI

**Sahih Ibn Majah Uk. 12[400]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka Ubadi bin Abdullah, amesema: "Ali (as) alisema: 'Mimi ni mja wa Mwenyezi Mungu na ndugu wa Mtume wake (saww), na mimi ni msema kweli bora, hatasema hayo baada yangu isipokuwa muongo. Nilianza kuswali miaka saba kabla watu hawajaanza kuswali."'

**Nasema:** Pia ameipokea al-Hakim ndani ya *Mustadrakus-Sahihayn* Juz. 3, uk. 111, na amesema mwishoni: "Kabla yeyote katika ummah huu hajaanza kumwabudu (Mwenyezi Mungu)." Na ameipokea Ibn Jariri Tabari ndani ya *Taarikh* yake Juz. 2, uk. 56.

[398] *Kanzul-Ummal*: Fadhila za makhalifa wanne. Fadhila za Ali (as), Hadithi ya 32993.
[399] *Ar-Riyadh an-Nadhrah*: Mlango wa fadhila za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib, Kutaja uimara wa nyayo zake katika imani.
[400] *Sahih Ibn Majah,* Utangulizi, Mlango wa 11, Fadhila za Ali bin Abu Talib (as), Hadithi ya 120.

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 3 Uk. 112[401]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Habah bin Juwayni kutoka kwa Ali (as) kuwa alisema: "Nilimwabudu Mwenyezi Mungu nikiwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) miaka saba kabla yeyote katika ummah huu hajaanza kumwabudu."

**Nasema:** Na pia ameitaja al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 6, uk. 394, kwa kunukuu kutoka kwa al-Hakim na kwa Ibn Mardawayhi.

**Usudul-Ghabah Juz. 4, uk. 18[402]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Ayubu al-Ansariy kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Malaika waliniswalia mimi na Ali miaka saba, hiyo ni wakati ambapo hakukuwa na mwanaume anayeswali pamoja nami zaidi yake.'"

**Nasema:** Pia ameitaja al-Muhibu Tabari ndani ya *ar-Riyadh an-Nadhrah* Juz. 2, uk. 165, kwa kunukuu kutoka kwa Abul-Hasan al-Khalmiy, na amesema: "Kwa kuwa tulikuwa tukiswali hali hakuna mwingine zaidi yetu anayeswali pamoja nasi." Lakini hajataja miaka saba.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 1, Uk. 99[403]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Habah al-Araniy, amesema: "Nilimuona Ali (as) akiwa amecheka juu ya mimbari, na sikuwahi kumuona akicheka zaidi kama siku ile kwani hadi magego yake yalionekana, kisha alisema: 'Nimekumbuka kauli ya Abu Talib, siku moja alikuja Abu Talib na kutukuta mimi na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) tukiswali huko Batnun-Nakhlah, akasema: Mnafanya nini ewe mtoto wa ndugu yangu? Mtume wa Mwenyezi Mungu akamlingania katika Uislamu, akasema: Si baya hili mfanyalo – au hili msemalo' - kisha alisema (as): 'Ewe Mungu Wangu, sijui kama kuna mja Wako kutoka katika ummah huu alikuabudu kabla yangu zaidi ya Nabii wako.' Alisema hayo mara tatu, kisha akasema: 'Nilianza kuswali miaka saba kabla watu hawajaanza kuswali."

**Nasema:** Pia ameitaja al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 6, uk. 395, kwa kunukuu kutoka kwa Abu Daud at-Twayalasiy na kwa Ahmad bin Hanbal na kwa Abu Ya'ala na kwa al-Hakim toka ndani ya *Mustadrakus-Sahihayn*. Na ameitaja al-Haythamiy ndani ya *Maj'mauz-Zawa'id* Juz. 9, uk. 102, na amesema: "Ameipokea Ahmad, Abu Ya'ala, al-Bazar na Tabaraniy ndani ya *al-Awsat*.

Na ameipokea Ibn Abdul-Bari ndani ya *Istiaab* yake Juz. 2, uk. 58, na lafudhi yake ni: "Nilianza kumwabudu Mwenyezi Mungu miaka mitano kabla ya yeyote katika ummah huu hajaanza kumwabudu." Na ameipokea Ibn al-Athir ndani ya *Usudul-Ghabah* Juz. 4, uk. 17, humo amesema: "Miaka mitano au miaka saba."

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 395[404]:**

Amesema: Kutoka kwa Habah, amesema: "Hakika Ali (as) alisema: 'Ewe Mungu Wangu! Hakika wewe wajua kuwa hakuna mja Wako yeyote kutoka katika ummah huu aliyeanza kukuabudu kabla yangu mimi. Nilianza kukuabudu miaka sita kabla mtu mwingine yeyote kutoka katika ummah huu hajaanza kukuabudu.'" - Amesema: Ameiandika Tabaraniy ndani ya *al-Awsat.*

---

[401] *Mustadrakus-Sahihayni*: Kitabu cha kuwatambua Masahaba, Mlango wa kutaja Uislamu wa Amirul-Muuminin Ali (as).
[402] *Usudul-Ghabah*: Mlango wa Ain na Laam, Wasifu wa Ali bin Abu Talib (as).
[403] *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*: Musnad Ali bin Abu Talib (as), Hadithi ya 778.
[404] *Kanzul-Ummal*: Fadhila za Ali (as), Hadithi ya 36391.

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 3[405]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ali (as) kuwa alisema: "Simjui mtu yeyote kutoka katika ummah huu zaidi yangu mimi, ambaye alimwabudu Mwenyezi Mungu baada ya Mtume wetu. Nilianza kumwabudu Mwenyezi Mungu miaka tisa kabla mtu yeyote mwinginge kutoka katika ummh huu hajaanza kumwabudu.

**Asbabun-Nuzuli cha Al-Wahidiy, Uk. 182[406]:**

Amesema: Hasan, as-Shaabiy na al-Qardhiy wamesema: "Iliteremka Aya kuwahusu Ali (as), Abbas na Talha Ibn Shaybah, hiyo ni baada ya kila mmoja kujigamba, Talha alisema: 'Mimi ndiye mtunza Nyumba na ufunguo umo mikononi mwangu na kwangu ndio kuna nguo ya Nyumba yake.' Abbas akasema: 'Mimi ndiye mtoa huduma ya maji kwa mahujaji na msimamizi wake.' Ali (as) akasema: 'Sijui mtasema nini. Nimeswali miezi sita kabla ya watu wote, na mimi ndiye mwanajihadi.' Ndipo Mwenyezi Mungu akateremsha Aya hii, yaani kauli ya Mwenyezi Mungu: **'Je, mnafanya kuwanywesha maji Mahujaji na kuamirisha Msikiti Mtakatifu ni sawa na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na akapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhaalimu. Wale walioamini, na wakahama, na wakapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao, hao wana cheo kikubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu. Na hao ndio wenye kufuzu.'**"

**Nasema:** Na ameipokea Ibn Jarir Tabari ndani ya *Tafsiir*yake Juz. 10, uk. 68, kwa njia itokayo kwa Muhammad bin Kaab al-Qaradhiy. Na ameitaja Razi ndani ya *Tafsiir* yake mwishoni mwa tafsiri ya Aya hii katika Surat-Tawba.

**Al-Istiaab Juz. 2, Uk. 459[407]:**

Amesema: Ali (as) alisema: "Niliswali pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) muda kadha wakadha, wakati ambapo ukiniacha mimi hakuwepo mwingine yeyote aliyekuwa anaswali pamoja naye isipokuwa Khadija."

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 301[408]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Aliyekuwa mtu wa kwanza kuswali ni Ali (as)."

**Nasema:** Ameipokea Ibn Jarir ndani ya *Taarikh* yake Juz. 2, uk. 55. Na ameitaja al-Muhibu Tabari ndani ya *ar-Riyadh an-Nadhrah* Juz. 2, uk. 158, na amesema: "Ameiandika Abul-Qasim ndani ya *al-Muwafaqat*.

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 3, uk. 111[409]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Ali ana sifa nne ambazo hakuna mwingine mwenye sifa hizo: Yeye ndiye wa kwanza kuswali pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kabla

405 *Khasa'isun-Nasaiy*: Ibada ya Ali (as).
406 *Asbabun-Nuzul:* Sura al-Baraah.
407 *Al-Istiaab*: Herufi Ain, Kitabu cha wanawake, Wasifu wa Layla al-Ghafariyyah.
408 *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha fadhila. Fadhila za Ali bin Abu Talib (as), Mlango wa 21, Hadithi ya 3734.
409 *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha kuwatambua Masahaba, Mlango wa kutaja Uislamu wa Amirul-Muuminin Ali (as).

ya mtu mwingine yeyote mwaarabu na asiyekuwa mwaarabu, na yeye ndiye aliyekuwa mbeba bendera yake katika kila vita, na yeye ndiye aliyesubiri pamoja naye siku ya maji ya Uhudi, na yeye ndiye aliyemuosha na kumwingiza kaburini."

**Nasema:** Na ameipokea Ibn Abdul-Bari ndani ya *Istiaab* yake Juz. 2, uk. 457.

Ibn al-Athiri al-Jazriy amesema ndani *an-Nihayah*: "Mtume (saww) alipatwa na kiu siku ya Uhudi, Ali akamletea maji kutoka kwenye jiwe na kumuosha uso uliokuwa na damu.."

Imetangulia pia katika mlango wa tisa kutoka kwa al-Hakim kwa njia itokayo kwa Qaysu kuwa alisema: "Akasema – yaani Saad: Wewe kwa nini unamkashifu Ali bin Abu Talib? Hivi si yeye aliyekuwa mtu wa kwanza kuukubali Uislamu? Hivi si yeye aliyekuwa mtu wa kwanza kuswali…"

Imetangulia pia katika mlango wa tisa riwaya kutoka kwa Abu Hanifa ndani ya *Musnad* yake kutoka kwa Habah, kuwa alisema: "Nilimsikia Ali (as) akisema: 'Mimi ndiye mtu wa kwanza aliyeukubali Uislamu na kuswali pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).'" Rejea huko.

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 2[410]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Habah al-Arniy, amesema: "Nilimsikia Ali (as) akisema: 'Mimi ndiye mtu wa kwanza aliyesali pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).'"

**Nasema:** Ameipokea pia Ahmad bin Hanbal ndani ya *Musnad* yake Juz. 1 uk. 141, na ameipokea Ibn Saad ndani ya *Tabaqat* yake Juz. 3, Sehemu ya kwanza uk. 13. Na ameipokea Ibn al-Athir ndani ya *Usudul-Ghabah* Juz. 4, uk. 17, na humo amesema: "Pamoja na Nabii (saww)".

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 2[411]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Amrah, kutoka kwa Zayd bin Arqam, amesema: "Mtu wa kwanza aliyesali pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ni Ali bin Abu Talib (as)."

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 2[412]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Hamza mtumishi wa Ansari, amesema: Nilimsikia Zayd bin Arqam akisema: "Mtu wa kwanza aliyeswali pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ni Ali bin Abu Talib (as)."

**Nasema:** Na ameipokea pia Ahmad bin Hanbal ndani ya *Musnad* yake Juz. 4, uk. 368, na uk. 370. Na ameipokea Abu Daud at-Twayalasiy ndani ya *Musnad* yake Juz. 3, uk. 93. Na ameipokea al-Bayhaqiy ndani ya *Sunan* yake Juz. 6, uk. 206. Na ameipokea Ibn Abdul-Barri ndani ya *Istiaab* Juz. 2, uk. 458. Na ameipokea Ibn Jarir Tabari ndani ya *Taarikh* yake Juz. 2, uk. 56, na amesema: "Mwanaume wa kwanza aliyeswali pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ni Ali bin Abu Talib (as)."

**Tabaqat Ibn Saad Juz. 3, Sehemu ya kwanza, Uk. 13[413]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Mujahid, amesema: "Mtu wa kwanza kuswali ni Ali (as), akiwa mtoto wa miaka kumi."

410 *Khasa'isun-Nasaiy*: Swala ya Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (as).
411 *Khasa'isun-Nasaiy*: Swala ya Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (as).
412 *Khasa'isun-Nasaiy*: Tofauti ya lafudhi za walionukuu.
413 *Tabaqat al-Kubra:* Kutaja Uislamu wa Ali (as) na Swala yake.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 156[414]:**

Lafudhi yake ni: “Mtu wa kwanza aliyesali pamoja nami ni Ali (as).” Amesema: “Ameiandika al-Hakim ndani ya *Taarikh* yake na ad-Daylamiy kutoka kwa Ibn Abbas.”

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 395[415]:**

Amesema: Kutoka kwa Ali (as), amesema: “Mimi ndiye mtu wa kwanza aliyeswali pamoja na Mtume (saww). – Amesema: Ameiandika Abu Daud at-Twayalasiy, Ibn Abi Shaybah, Ahmad bin Hanbal na Ibn Saad.

**Taarikh Ibn Jariri Tabari Juz. 2, uk. 57[416]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Is’haqa, amesema: “Mwanaume wa kwanza kumwamini Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), aliyeswali pamoja naye na kuamini aliyokuja nayo kutoka kwa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alikuwa ni Ali bin Abu Talib (as), wakati huo alikuwa ni mtoto wa miaka kumi. Na miongoni mwa neema za Mwenyezi Mungu alizomneemesha Ali bin Abu Talib (as) ni kuwa yeye alikuwa akilelewa na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hata kabla ya Uislamu.”

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 300[417]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik, amesema: “Nabii (saww) alikabidhiwa unabii siku ya Jumatatu, na Ali (as) akaswali siku ya Jumanne.” Amesema: “Na katika mlango mwingine imepokewa kutoka kwa Ali (as).” Kisha amesema: “Huyu amepokea kutoka kwa Muslim, kutoka kwa Habah, kutoka kwa Ali mfano wa hii.”

**Taarikh Ibn Jariri Tabari Juz. 2, uk. 55[418]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir, amesema: “Nabii (saww) alikabidhiwa unabii siku ya Jumatatu, na Ali (as) akaswali siku ya Jumanne.”

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 3, uk. 112[419]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Buraydah, amesema: “Abu Dharr alikwenda – Ameendelea kusimulia hadithi mpaka akasema: na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliletewa wahyi siku ya Jumatatu, na Ali (as) akaswali siku ya Jumanne.” – Amesema: Hadithi hii ni yenye njia sahihi.

**Khasa’isun-Nasaiy Uk. 3:[420]**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Afif –yaani al-Kindiy- amesema: “Katika zama za ujahiliya nilikuja Makka nikiwa na lengo la kutaka kuinunulia familia yangu nguo za Makka na uturi zake. Nilikwenda kwa Abbas –alikuwa ni mfanyabiashara - wakati nikiwa nimeketi kwake nikitazama Ka’aba, huku jua

414 *Kanzul-Ummal*: Fadhila za Ali (as), Hadithi ya 32992.
415 *Kanzul-Ummal*: Fadhila za Ali (as), Hadithi ya 36396.
416 *Taarikh Tabari*: Kutaja habari zinazozungumzia amri ya Nabii wa Mwenyezi Mungu (saww).
417 *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha fadhila, Fadhila za Ali bin Abu Talib (as), Mlango wa 21, Hadithi ya 3734.
418 *Taarikh Tabari*: Kutaja habari zinazozungumzia amri ya Nabii wa Mwenyezi Mungu (saww).
419 *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha kuwatambua Masahaba, Mlango wa kutaja Uislamu wa Amirul-Muuminin Ali (as).
420 *Khasa’isun-Nasaiy:* Swala ya Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (as).

likiwa limeshakengeuka huko mbinguni, limepanda na kuondoka, mara alikuja kijana akatupia macho yake mbinguni kisha akasimama na kuielekea Ka'aba. Sikukaa muda mrefu akawa amekuja mtoto na kusimama kuliani kwake, kisha sikukaa muda mrefu akawa amekuja mwanamke na kusimama nyuma yao. Kijana aliporukuu, nao mtoto na mwanamke wakarukuu, kijana alipoinua kichwa, nao mtoto na mwanamke wakainua, kijana aliposujudu, nao mtoto na mwanamke wakasujudu.

"Nikasema: Ewe Abbas jambo adhimu hili. Abbas akasema: 'Ndiyo jambo adhimu, unajua huyu kijana ni nani?' Nikasema: Hapana. Akasema: 'Huyu ni Muhammad bin Abdullah mtoto wa ndugu yangu. Unajua huyu mtoto ni nani? Huyu ni Ali mtoto wa ndugu yangu. Unajua huyu mwanamke ni nani? Huyu ni Khadija binti Khuwaylid. Hakika mtoto huyu wa ndugu yangu amenipa habari kuwa Mola Wake, Mola wa mbingu na ardhi amemwamuru kuja na dini hii anayoifuata, na Wallahi juu ya ardhi yote hakuna hata mtu mmoja mwenye kufuata dini hii zaidi ya hawa watatu."'

**Nasema:** Ameipokea pia Ahmad bin Hanbal ndani ya *Musnad* yake Juz. 1, uk. 209, na amesema mwishoni mwake: "Hakuna ambaye amemfuata katika jambo lake isipokuwa mke wake na mtoto wa ami yake mtoto huyu, na yeye anadai kuwa kwa dini hiyo atazimiliki hazina za Kisra na Kaysari."

Amesema: Afif –ambaye ni binamu wa Ash'ath bin Qaysi- alikuwa akisema baada ya kusilimu: "Natamani Mwenyezi Mungu angeniruzuku Uislamu siku ile nikawa mtu wa tatu pamoja na Ali bin Abu Talib."

Na ameipokea al-Hakim ndani ya *Mustadrakus-Sahihayn* Juz. 3, uk. 183, na amesema mwishoni: Alisema Afif al-Kindiy: "Natamani kwamba ningesilimu siku ile nikapata robo ya Uislamu." Kisha alisema: Hii ni hadithi yenye njia sahihi. Na ameipokea pia Ibn Saad ndani ya *Tabaqat* yake Juz. 8, uk. 10, na amesema mwishoni: Afif amesema: "Baadaye nilitamani kuwa ningekuwa wa nne wao."

Na ameitaja pia Ibn Hajar ndani ya *Al-Isabah* Juz. 4, Sehemu ya kwanza, Uk. 248 katika wasifu wa Afif al-Kindiy, na amenasibisha riwaya yake na al-Baghawi, Abu Ya'ala, an-Nasaiy, al-Aqiliy, Bukhari, Ibn Abi Khaythamah, Ibn Mundah na mwandishi wa *al-Ghaylaniyan*.

Na ameipokea Ibn Abdul-Barri ndani ya *Istiaab* yake Juz. 2, uk. 458 na uk. 511. Na ameitaja al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 6, uk. 391 kwa kunukuu kutoka kwa Ibn Adiy ndani ya *al-Kamil* na Ibn Asakir. Na ameipokea pia Ibn al-Athir ndani ya *Usudul-Ghabah* Juz. 3, uk. 414, na ameitaja al-Haythamiy ndani ya *Maj'ma'uz-Zawaid* Juz. 9, uk. 103, amesema: "Na ameipokea Ahmad, Abu Ya'ala na Tabaraniy kwa sanadi."Na ameipokea Ibn Jarir Tabari ndani ya *Taarikh* yake Juz. 2, uk. 56 na uk. 57 kwa njia tofauti lakini kwa lafudhi zenye kukaribiana.

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2 Uk. 159[421]:**

Amesema: Ibn Is'haqa amesema: "Baadhi ya ulamaa wamesema kuwa, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa akienda kwenye mabonde ya Makka wakati wa Swala unapowadia, na alikuwa akitoka pamoja na Ali bin Abu Talib (as) kwa kujificha kwa kumuogopa ami yake Abu Talib na kwa kuwaogopa ami zake wengine pamoja na jamaa zake wengine. Walikuwa wakiswali Swala zao huko, jioni inapoingia wanarejea. Waliendelea na mtindo huo kadiri Mwenyezi Mungu alivyotaka, kisha ndipo Abu Talib akawagundua pale alipowakuta siku moja wakiswali. Akamwambia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): 'Ewe mtoto wa ndugu yangu, ni dini gani hii ambayo naona waifuata?' Akasema: 'Ewe ami yangu, hii ni dini ya Mwenyezi Mungu na dini ya Malaika Wake na dini ya Mitume Wake na dini ya baba yetu Ibrahim – au kama alivyosema: Mwenyezi Mungu amenituma kuwa Mtume kwa waja wake, na wewe ewe ami yangu una haki zaidi ya kunifuata kati ya wale niliowapa nasaha na kuwaita kwenye uwongofu,

[421] *Ar-Riyadh an-Nadhrah*: Mlango wa fadhila za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib, Kutaja uimara wa nyayo zake katika imani.

na ndiye mwenye haki zaidi ya kuniitikia na kunisaidia katika jambo hili' – au kama alivyosema: Abu Talib akasema: 'Ewe mtoto wa ndugu yangu, hakika mimi Wallahi siwezi kuachana na dini ya wahenga wangu na imani waliyokuwa wakifuata, lakini Wallahi halitakufikia jambo ambalo walichukia maadamu tu ningali hai.'

"Na wametaja kuwa yeye alimwambia Ali (as): 'Ewe mwanangu, ni dini gani hii ambayo wewe waifuata?' Akasema: 'Ewe baba yangu, nimemwamini Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na nimesadikisha aliyokuja nayo na nimeswali pamoja naye na nimemfuata.' Wakadai kuwa alisema: 'Hakika yeye hajakuita isipokuwa kwenye kheri hivyo shikamana naye.'" - Amesema: Ameiandika Ibn Is'haqa.

**Nasema:** Na ameipokea Ibn Jarir Tabari pia ndani ya Taarikh yake Juz. 2 Uk. 58 kutoka kwa Ibn Is'haqa.

**Kanzul-Ummal Juz. 7, Uk. 56:**[422]

Kutoka kwa Abdullah bin Mas'ud, amesema: "Hakika kitu cha kwanza nilichokijua kutoka katika jambo la Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ni kwamba, nilikwenda Makka nikiwa pamoja na ami zangu, tukaongozwa njia ya kwenda kwa Abbas bin Abdul-Muttalib, tukafika kwake na kumkuta kakaa mbele ya Zamzam, nasi tukaketi mbele yake. Wakati tukiwa hapo, mara alitokeza mtu kutokea kwenye mlango wa Swafa, mweupe anaeelekea kwenye wekundu, ana vywele nyingi za kujaa zinazoishia kwenye masikio yake, ana pua ya kusimama na meno yake ya mbele yanang'ara, macho yake ni ya mviringo yenye weusi, ana ndevu za kujaa, ana vitanga na nyayo imara, amevaa nguo mbili nyeupe, anang'ara kama mbalamwezi katika usiku wa nusu ya mwezi, alikuwa akitembea huku kuliani kwake kukiwa na mtoto mwenye uso mzuri, ni kijana ambaye anakaribia kubalehe au ameshabalehe, anafuatiwa na mwanamke ambaye alikuwa kafunika uso wake. Alikwenda mpaka katika jiwe na kuligusa, kisha na kijana aliligusa jiwe lile, kisha na mwanamke akaligusa, kisha alizunguka Nyumba mara saba huku kijana na mwanamke wakizunguka pamoja naye.

"Tukasema: Ewe Abul-Fadhli, hakika hii ni dini ambayo hatujapata kuiona kwenu au ni jambo jipya? Akasema: 'Huyu ni mtoto wa ndugu yangu Muhammad bin Abdullah, na kijana huyu ni Ali bin Abu Talib, na mwanamke huyu ni mkewe Khadija. Wallahi juu ya ardhi yote hakuna hata mtu mmoja tunayemjua kuwa anafuata dini hii zaidi ya hawa watatu."'

— Amesema: Ameiandika Ya'qubu bin Shaybah na Ibn Asakir.

**Nasema:** Ameitaja pia al-Haythamiy ndani ya *Majmauz-Zawa'id* yake Juz. 9, uk. 222 kwa kunukuu kutoka kwa Tabaraniy, na ameongeza: "Amesema baada ya kauli: huku kijana na mwanamke wakizunguka pamoja naye: Kisha aligusa nguzo na akainua mikono yake na kutoa takbira. Kijana akasimama kuliani kwake naye akainua mikono na kutoa takbira, na mwanamke akasimama nyuma yao akainua mikono yake na kutoa takbira. Alirefusha kisimamo kisha akarukuu na kurefusha rukuu, kisha aliinua kichwa chake kutoka kwenye rukuu na akakunuti hali amesimama, kisha alisujudu, huku kijana na mwanamke wakifanya kama anavyofanya yeye, wanamfuata anavyofanya yeye. Tukaona kitu ambacho tulikuwa hatujawahi kukiona Makka. Tukakikataa na hivyo tulimgeukia Abbas na kumwambia: 'Ewe Abul-Fadhli, hakika hii ni dini ambayo hatujapata kuiona kwenu au ni jambo jipya?' Akasema: 'Ndiyo, hivi Wallahi hamumjui huyu?' Tukasema hapana hatumjui. Akasema: 'Huyu ni mtoto wa ndugu yangu Muhammad bin Abdullah, na kijana huyu ni Ali bin Abu Talib, na mwanamke huyu ni Khadija binti Khuwaylid. Wallahi juu ya ardhi yote hakuna hata mtu mmoja anayemwabudu Mwenyezi Mungu kwa kufuata dini hii zaidi ya hawa watatu."'

[422] *Kanzul-Ummal*: Fadhila za Abdullah bin Mas'ud (as), Hadithi ya 37215.

# MLANGO UNAOSEMA KUWA HAKIKA ALI (AS) HUSWALI KAMA MTUME WA MWENYEZI MUNGU (SAWW)

**Sahih Bukhari: Kitabu cha Swala, Mlango unaozungumzia kukamilisha takbira ndani ya rukuu:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Mutrifu kutoka kwa Imran bin Huswayni, amesema: "Aliswali pamoja na Ali (as) huko Basra, akasema: 'Mtu huyu katukumbusha Swala tuliyokuwa tukiswali pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).' Akasema kuwa alikuwa akitoa takbira kila anapoinua na kila anapoweka.

**Sahih Bukhari: Kitabu cha Swala, Mlango unaozungumzia kukamilisha takbira ndani ya sijda:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Mutrifu bin Abdullah, amesema: "Niliswali nyuma ya Ali bin Abu Talib (as) mimi na Imran bin Huswayni. Alikuwa kila anaposujudu hutoa takbira, na anapoinua kichwa chake anatoa takbira, na anaponyanyuka kutoka kwenye rakaa mbili anatoa takbira. Alipomaliza Swala; Imrani bin Huswayni alinishika mikono na kusema: 'Hakika huyu kanikumbusha Swala ya Muhammad (saww).' Au alisema: 'Hakika ametuswalisha Swala ya Muhammad (saww).'"

**Nasema:** Na ameipokea katika mlango mwingine miongoni mwa milango ya Swala, na pia kaipokea Muslimu katika *Sahih* yake katika kitabu cha Swala katika mlango wa kuthibitisha takbira kila wakati wa kuinamisha kichwa na kila wakati wa kuinua. Na ameipokea an-Nasaiy ndani ya *Sahih* yake Juz. I, uk. 164 na uk. 167. Na ameipokea Abu Daudi pia ndani ya *Sahih* yake Juz. 5, uk. 84. Na ameipokea Ahmad bin Hanbal ndani ya *Musnad* yake Juz. 4, uk. 428, na amesema: "Nilikuwa pamoja na Imran bin Huswayni huko Kufa, Ali bin Abu Talib (as) akatuswalisha." Akaendelea kusimulia hadithi, na kaipokea pia katika uk. 429 na uk. 440.

**Sahih Ibn Majah: Kitabu cha Swala, Mlango wa kutoa salamu[423]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Musa, amesema: "Siku ya Ngamia, Ali (as) alituswalisha Swala ambayo ilitukumbusha Swala ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), ima tulikuwa tumeisahau na ima tulikuwa tumeiacha, akatoa salamu kulia na kushoto."

**Nasema:** Na ameipokea pia Ahmad bin Hanbal ndani ya *Musnad* yake Juz. 4, uk. 392 kwa njia mbili, na katika uk. 400 na uk. 415 zikitofautiana kidogo katika lafudhi.

**Fathul-Bariy Fii Sharhil-Bukhari Juz. 2, uk. 413:[424]**

Amesema: Ahmad na At-Twahawi wamepokea kwa njia sahihi kutoka kwa Abu Musa al-Ash'ariy, kuwa alisema: "Ali (as) alitukumbusha Swala ambayo tulikuwa tukiswali pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), ima tulikuwa tumeisahau na ima tulikuwa tumeiacha kwa kusudi."

Na amesema katika uk. 414: "Na katika riwaya ya Qatadah kutoka kwa Mutrif ni kuwa Imran bin Huswayni alisema: 'Ni muda kadhaa wakadhaa sasa sijaswali Swala inayofanana na ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kushinda Swala hii."

---

[423] *Sunan Ibn Majah*: Kitabu cha kusimamisha Swala, 28- Mlango wa kutoa salamu, Hadithi ya 917.
[424] *Fathul-Bariy Fii Sharhil-Bukhari*: Kitabu cha adhana, 115 - Mlango wa kutimiza takbira katika rukuu.

# MLANGO UNAOZUNGUMZIA UZURI WA USO WA ALI (AS) NA NAKSHI ZA PETE ZAKE

**Al-Istiaab Juz. 2. Uk. 469:[425]**

Amesema: "Na kizuri nilichokiona katika sifa za Ali (as) ni kuwa yeye alikuwa miongoni mwa wanaume wenye kimo cha katikati chenye kuelekea kwenye ufupi, mwenye macho ya mviringo yenye weusi, mwenye uso mzuri kama mbalamwezi ya usiku wa nusu mwezi, mwenye tumbo kubwa, mwenye mabega mapana, mwenye vitanga imara, mwili wa kuyumba, shingo yake ni kama birika la fedha. Alikuwa na upara, hakuwa na nywele kichwani ila kwa nyuma. Mwenye ndevu nyingi, bega lake lilikuwa na mfupa kama mfupa wa simba pori, dhiraa yake ilikuwa imemezana na kifupapanya chake kiasi kwamba maungio yake hayaonekani. Anapotembea hunepa, na anaposhika dhiraa ya mtu huizuia pumzi yake na hapo huwa hawezi kupumua. Hakuwa mnene, ni mwenye dhiraa na mkono imara, na anapokwenda vitani hutembea kwa kasi. Ni mwenye moyo thabiti, shujaa mwenye nguvu na mwenye kupata ushindi dhidi ya anayepambana naye.

**Usudul-Ghabah Juz. 4, uk. 39[426]:**

Amesema: Ibn Abi Dun'ya amesema: Alinisimulia Abu Huraira: Alitusimulia Abdullah bin Daud: Alitusimulia Mudrik Abul-Hajjaj, alisema: "Nilimuona Ali (as) akitoa hotuba, na alikuwa mwenye uso mzuri kuliko watu wote."

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, uk. 202:[427]**

Amesema: Mula ameandika ndani ya Sira yake: "Pakasemwa: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Atawezaje Ali kubeba bendera ya Himidi?' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Na kwa nini asiwezi hilo wakati amepewa sifa mbalimbali: Subira kama subira yangu, uzuri kama uzuri wa upanga na nguvu kama nguvu za Jibril."'

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, uk. 218:[428]**

Amesema: Kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Yeyote atakaye kumuona Ibrahim katika upole wake, na kumuona Nuhu katika hekima yake, na kumuona Yusuf katika uzuri wake, basi na amtazame Ali bin Abu Talib (as)."

— Amesema: Kaiandika Mula ndani ya *Sira* yake.

**Kanzul-Ummal Juz. 3, Uk. 336:[429]**

Kutoka kwa Abdi Barri, amesema: "Ali bin Abu Talib (as) alikuwa na pete nne alizokuwa akivaa: Yakuti ya kipato chake, feruzi ya ushindi wake, chuma cha China kwa ajili ya nguvu yake, na rubi kwa ajili

[425] *Al-Istiaab*: Herufi Ain, Mlango wa Ali bin Abu Talib (as).
[426] *Usudul-Ghabah*: 3783, Ali bin Abu Talib (as), kuuwawa kwake na kujua kwake kuwa atauwawa.
[427] *Ar-Riyadh an-Nadhrah*: Mlango wa nne katika fadhila za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib, Kutaja khususia yake ya kubeba bendera ya Himidi Siku ya Kiyama.
[428] *Ar-Riyadh an-Nadhrah*: Mlango wa nne katika fadhila za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib, Kutaja kushabihiana kwake na Manabii watano katika fadhila zao.
[429] *Kanzul-Ummal:* Fadhila za Abdullah bin Mas'ud (as), Hadithi ya 37215.

ya kinga yake. Yakuti ilikuwa imenakishiwa: 'Hapana mungu isipokuwa Allah Mfalme wa haki aliye bayana.' Nakshi ya feruzi ilikuwa ni: 'Allah Mfalme.' Nakshi ya chuma cha China ilikuwa ni: 'Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu.' Na nakshi ya rubi ilikuwa katika mistari mitatu: 'Atakayo Mwenyezi Mungu, hapana nguvu isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu, namuomba msamaha Mwenyezi Mungu.'" – Amesema: Ameiandika al-Hakim ndani ya Taarikh yake, na as-Swabuni ndani ya al-Miatayni, na Abu Abdurahman as-Salmiy ndani ya *Amal* yake.

**Nurul-Absar Uk. 94[430]:**

Amesema: Nakshi ya pete yake (yaani Ali (as) – ilikuwa: "Nimeuegemeza mgongo wangu kwa Mwenyezi Mungu." Na imesemekana: "Mwenyezi Mungu anitosha."

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA MAJINA YA UBABA YA ALI (AS) NA BAADHI YA LAKABU ZAKE TUKUFU

**Sahih Bukhari: Kitabu kinachozungumzia mwanzo wa uumbaji, Mlango unaozungumzia fadhila za Ali bin Abu Talib (as):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Hazim kwamba mtu mmoja alikuja kwa Sahli bin Saad na kumwambia: "Fulani anamwita Ali (as) kwa jina fulani juu ya mimbari." Akamwambia: "Anamwitaje?" Akasema: "Anamwita: Abu Turabi." Sahli akacheka kisha akasema: "Wallahi hakuna aliyempa jina hilo isipokuwa Mtukufu Mtume (saww), na hakuna jina alilokuwa akilipenda yeye mwenyewe kushinda hilo."Nikataka kujua undani wa hadithi ya Sahli, nikamwambia: Ewe Abu Abbas ilikuwaje? Akasema: "Ali (as) aliingia kwa Fatimah kisha akatoka na kwenda kulala msikitini, Mtukufu Mtume (saww) akamuuliza Fatimah (as): 'Yuko wapi mtoto wa ami yako?' Akasema: 'Msikitini.' Mtume akatoka na kumfuata, akakuta shuka lake limedondoka na kuuacha mgongo wake wazi huku udongo ukiwa umetapakaa katika mgongo wake. Mtume akaanza kumfuta udongo kutoka kwenye mgongo wake huku akisema: 'Kaa chini ewe Abu Turabi.' Alisema hivyo mara mbili."

**Nasema:** Ameipokea tena kwa tofauti kidogo katika kitabu cha Swala katika Mlango unaozungumzia wanaume kulala msikitini, na katika kitabu cha adabu katika Mlango unaozungumzia kujipa jina la ubaba la Abu Turabi, na pia katika kitabu kinachozungumzia kuomba idhini, katika Mlango unaozungumzia mwanamke mwenye kuongea msikitini. Na pia Bukhari ameipokea ndani ya *al-Adab al-Mufrad*[431] katika Mlango unaozungumziamtu atakayempa mtu jina la ubaba kulingana na sifa aliyonayo. Na ameipokea pia Muslim ndani ya *Sahih* yake katika kitabu cha fadhila za Masahaba katika mlango wa fadhila za Ali bin Abu Talib (as). Na ameipokea pia Ibn Jariri Tabari ndani ya *Taarikh* yake Juz. 2, uk. 124.

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 39[432]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ammar bin Yasir, amesema: "Mimi na Ali bin Abu Talib (as) tulikuwa marafiki wawili katika vita vya Ashira katika bonde la Yanbui. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipofika hapo alikaa hapo mwezi mzima, na hatimaye akafanya sulhu na Bani Mudliju na wa-

[430] *Nurul-Absar*: Faslu inayozungumzia fadhila za Ali bin Abu Talib (as), kutaja watoto wake, kuuwawa kwake, muuwaji wake, lakabu zake na majina yake ya ubaba.

[431] *al-Adab al-Mufrad*: Mlango wa 387, Mlango unaozungumzia mtu atakayempa mtu jina la ubaba kulingana na sifa aliyonayo, Hadithi ya 852.

[432] *Khasa'isun-Nasaiy*: Kumtaja aliye muovu kuliko watu wote.

shirika wao kutoka katika Bani Mudhmira, kisha akawaaga. Ali (as) akaniambia: 'Je upo tayari ewe Abu Yaqdhan tulifuate kundi hili la Bani Mudliju linalofanya kazi katika chemchemu yao ili tuone ni jinsi gani wanavyofanya?' Nikamwambia ukitaka. Tulikwenda na tukatazama kazi zao muda kadhaa kisha usingizi ukatushika. Nikaondoka mimi na Ali (as) na kwenda kulala chini ya kivuli cha mtende kwenye udongo. Tulilala hapo kiasi kwamba Wallahi hakuna aliyetuamsha isipokuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwa kututikisa kwa mguu wake, huku tukiwa tumetapakaa udongo huo tuliolalila. Siku hiyo ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Ali (as): 'Vipi Abu Turabi (baba wa udongo)?' Kutokana na udongo uliokuwa unaonekana kwake.

"Kisha Mtume akasema: 'Je niwaambieni ni nani na nani walio waovu kuliko watu wote?' Tukasema ndiyo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Akasema: 'Ni Uhaymar wa kabila la Thamud ambaye alimchinja ngamia, na mwingine ni yule ambaye ataipiga shingo yako hii. - Akaweka mkono wake juu ya shingo ya Ali (as)- mpaka hizi zilowane kutokana na pigo hilo.' Hapo akashika ndevu zake."

**Nasema:** Ameipokea Ahmad bin Hanbal ndani ya *Musnad* yake Juz. 4, uk. 263, al-Hakim ndani ya *Mustadrakus-Sahihayn* Juz. 3, uk. 140, Na at-Twahawi ndani ya *Mushkilul-Athar* Juz. 1, uk. 351. Na ameitaja al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 6, uk. 399, amesema: "Ameiandika al-Baghawi na Tabaraniy na Ibn Mardawayhi na Abu Nai'im na Ibn Asakir na Ibn an-Najar.

**Kanzul-Ummal Juz. 4, Uk. 390[433]:**

Amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikwenda msikitini na kumkuta Ali (as) akiwa amelala huku nguo yake ikiwa imedondoka toka kwenye mgongo wake na udongo umetapakaa katika mgongo wake. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaanza kumfuta udongo kwa mkono wake huku akisema: 'Kaa chini ewe Abu Turabi.' Hakuna jina alilokuwa akilipenda kuliko hili. Na hakuna aliyempa jina hilo isipokuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)." – Amesema: Ameiandika Abu Na'im ndani ya *al-Maarifah* kutoka kwa Sahli bin Saad as-Saidiy.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9, uk. 111:[434]**

Kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Mtukufu Mtume (saww) alipounga udugu baina ya Masahaba zake baina ya Muhajirina na Ansari, hakuunga udugu baina ya Ali bin Abu Talib na yeyote miongoni mwao. Ali akatoka akiwa ameghadhibika na kwenda kulala ardhini kwa kuegemea dhiraa yake. Upepo ukammwagia udongo. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamtafuta mpaka akampata, akamwamsha kwa mguu wake na kumwambia: 'Haifai zaidi ya wewe kuwa Abu Turabi, je umenighadhibikia pindi nilipounga udugu baina ya Muhajirina na Ansari bila kuunga udugu baina yako na yeyote kati yao? Hivi huridhii kuwa wewe kwangu mimi una cheo cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu? Fahamu atakayekupenda ataishi kwa amani na imani, na atakayekuchukia Mwenyezi Mungu atamfisha kifo cha kijahiliyah na atahesabiwa kwa amali zake sawa na aliyemo katika Uislamu.'" – Amesema: Ameipokea Tabaraniy ndani ya *al-Kabir* na *al-Awsat*.

**Nasema:** Ameitaja al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 6, uk. 154.

433 *Kanzul-Ummal*: Fadhila za Abdullah bin Mas'ud (as), Hadithi ya 37215.

434 *Maj'mauz-Zawa'id Waman'baul-Fawaid:* Mlango unaozungumzia fadhila za Khadija binti Khuwaylid mke wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

**Hilyatul-Awliyai Juz. 3, uk. 201:**[435]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir kuwa alisema: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Ali bin Abu Talib (as): 'Amani iwe juu yako ewe baba wa maua mawili, nakuusia kuyatendea kheri maua yangu ya duniani, karibu nguzo zako mbili zitaporomoka, na Mwenyezi Mungu ndiye mrithi wangu kwako.' Alipofariki Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) Ali (as) alisema: 'Hii ni moja kati ya nguzo mbili ambazo Mtukufu Mtume (saww) aliniambia.' Na alipofariki Fatimah (as) Ali (as) alisema: 'Hii ndio nguzo ya pili ambayo Mtukufu Mtume (saww) aliniambia."'

**Nasema:** Ameitaja al-Muhibu Tabari ndani ya *ar-Riyadh an-Nadhrah* Juz. 2, uk. 154, na pia kaitaja Ali bin Sultan ndani ya *Mirqatihi* katika ufafanuzi, uk. 597, wote wameitaja kutoka kwa Ahmad toka ndani ya *al-Manaqib*, amesema humo: "Alipofariki Fatimah (as) alisema: Hii ni nguzo nyingine."

Na ameitaja al-Munawi ndani ya *Kunuzul-Haqaiq* kwa muhtasari, kwa kunukuu kutoka kwa ad-Daylamiy, Na ameitaja al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 1, uk. 159, kwa kunukuu kutoka kwa Abu Na'im na Ibn Asakir, na katika Juz. 7, uk. 107 kwa kunukuu kutoka kwa Abu Na'im toka ndani ya *al-Maarifah*, na kutoka kwa ad-Daylamiy na Ibn Asakir.

**Nurul-Absar Uk. 94:**[436]

Amesema: Ama lakabu za Imam Ali (as) ni Murtadha, Haidar, Amirul-Muuminina, na al-Anza'ul-Batwin. Ama majina yake ya ubaba ni Abul-Hasan, Abus-Sibtwayni na Abu Turabi, na hilo alipewa na Mtukufu Mtume (saww).

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, uk. 155:**[437]

Amesema: Pia lakabu yake ni Baydhatul-Balad, Amin, Sharif, Hadi, Muhtada, na Dhil-Udhunil-Waia. Na imekuja katika hadithi sahihi shairi lake lisemalo: "Mimi ndiye niliyepewa jina Haidari na mama yangu." Aliendelea kusimulia mpaka aliposema: Haidari ni jina lenye maana ya Simba, Fatimah alipojifungua alimpa jina la baba yake, alipokuja Abu Talib akampa jina la Ali.

**Nasema:** Pia ana lakabu nyingine ambazo Inshaallah tutazitaja katika milango ifuatayo, kwa mfano yeye kuwa Malikia wa dini, Imamu wa wachamungu na kiongozi wa kundi mashuhuri, na nyinginezo.

## MLANGO UNAOSEMA KUWA DUA HUZUILIWA MPAKA ATAKAPOSALIWA MUHAMMAD NA AALI MUHAMMAD

**Kanzul-Ummal Juz. 1, uk. 173:**[438]

Hakuna dua isipokuwa ina kizuizi baina yake na Mwenyezi Mungu mpaka atakaposwaliwa Mtume (saww), kizuizi huondoka pindi anapofanya hivyo, na asipofanya hivyo dua hurejea. – Amesema: Ameiandika ad-Daylamiy kutoka kwa Ali (as).

[435] *Hilyatul-Awliyai*: Hadithi zake sahihi.

[436] *Nurul-Absar*: Faslu inayozungumzia fadhila za Ali bin Abu Talib (as), kutaja watoto wake, kuuwawa kwake, muuwaji wake, lakabu zake na majina yake ya ubaba.

[437] *Ar-Riyadh an-Nadhrah*: Mlango wa nne katika fadhila za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib. Kutaja kushabihiana kwake na Manabii watano katika fadhila zao.

[438] *Kanzul-Ummal*: Faslu ya pili katika adabu za dua, Hadithi ya 3270.

**Nasema:** Ameitaja pia Ibn Hajar ndani ya *Sawa'iqu* yake uk. 88, lakini kwa lafudhi isemayo: "Amesema: ameiandika ad-Daylamiy kuwa yeye (saww) alisema: 'Dua huzuiliwa mpaka atakaposwaliwa Muhammad na watu wa nyumbani kwake: Ewe Mungu wangu mswalie Muhammad na Aali zake.''

**Faydhul-Qadir Juz. 5, uk. 19:**[439]

Amesema: Amepokea Tabaraniy ndani ya *al-Awsat* kutoka kwa Ali (as), alisema: "Dua huzuiliwa mpaka atakaposwaliwa Muhammad na Aali Muhammad." - Amesema: al-Haythamiy amesema: Wapokezi wake ni waaminifu.

**Nasema:** Ameitaja pia al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 1, uk. 314 kwa kunukuu kutoka kwa Ubaydullah bin Abi Hafsu al-Ayshiy ndani ya Hadithi yake, na Abdul-Qadir ar-Rahawiy ndani ya *al-Arbaun*, na Tabaraniy ndani ya *al-Kabir*, na al-Bayhaqiy ndani ya *Shuabul-Iman*.

**Faydhul-Qadir Juz. 3, uk. 543:**[440]

Matini yake: "Dua huzuiliwa isimfikie Mwenyezi Mungu hadi atakaposwaliwa Muhammad na watu wa nyumbani kwake." - Amesema: Kaiandika Abu Shaykh kutoka kwa Ali (as.). - Na amesema kwenye ufafanuzi: al-Bayhaqiy ameiandika kwa lafudhi iliyoandikwa kutoka kwa Ali (as) bila kutaja mnyororo wa wapokezi, bali pia kaipokea Tirmidhiy kutoka kwa Ibn Umar kwa tofauti kidogo.

**Nasema:** Riwaya mbili zifuatazo zinaziunga mkono riwaya zilizotangulia: Moja ni ile aliyoitaja al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal*Juz. 1, uk. 181:[441]

Amesema: Alisema: "Ewe Ali iwapo utahuzunishwa na kitu sema: Ewe Mungu Wangu nilinde kwa jicho lako lisilo lala na niweke katika ngome yako isiyoshindwa- Aliendelea kusimulia dua hiyo mpaka aliposema: Nakuomba mswalie Muhammad na Aali Muhammad, na kupitia wewe najihami na shingo za maadui na wakandamizaji." - Amesema: Ameiandika ad-Daylamiy ndani ya *Musnadul-Firdawsi* kutoka kwa Ali (as).

Na nyingine ni ile aliyoitaja at-Thaalabiy ndani ya*Quswaswul-An'biyai*, katika kisa cha Yusuf uk. 157[442]:

— Amesema: "Ilipofika siku ya nne Jibril (as) alimjia na kumwambia: 'Ewe kijana ni nani aliyekutupia ndani ya kisima hiki?' Akasema: 'Ndugu zangu wa baba mmoja.' Akasema: 'Kwa nini?' Akasema: 'Wananionea husuda kutokana na cheo changu kwa baba yangu.' Akasema: 'Je unapenda kutoka kwenye kisima hiki?' Akasema: 'Ndio.' Akasema: 'Sema: Ewe Mtengenezaji wa kila kilichotengenezwa, ewe Mwenye kuganga kila kilichovunjika, ewe uliye hadhiri katika kila mkusanyiko, ewe Mwenye kushuhudia kila siri, ewe Uliye karibu usiye mbali, ewe Mwenye kumfariji kila aliye mpweke, ewe Mshindi usiyeshindwa, ewe Mjuzi wa mambo ya ghaibu, ewe Mzima wa milele usiyekufa, ewe Mwenye kuhuisha maiti. Hapana mungu isipokuwa Wewe uliyetakasika. Nakuomba ewe ambaye himidi njema ni Yake, ewe Muumba wa mbingu na ardhi, ewe Mmiliki wa ufalme, ewe Mwenye utukufu na ukarimu, nakuomba mswalie Muhammad na Aali Muhammad na nipe faraja na njia ya kutokea katika jambo langu hili na katika dhiki yangu hii. Na niruzuku katika hali ninayoitegemea na katika hali nisiyoitegemea.' Yusuf alisema maneno hayo na Mwenyezi Mungu akampa njia ya kutokea kisimani na akampa faraja dhidi ya vitimbi vya ndugu zake na akampa ufalme wa Misri bila ya kutegemea.

[439] *Faydhul-Qadir*: Herufi Kaf, mwishoni mwa hadithi ya 6303.
[440] *Faydhul-Qadir*: Herufi Dal, Hadithi ya 4266.
[441] *Kanzul-Ummal*: Faslu ya tano, katika dua za muda, Hadithi ya 3441.
[442] *Quswasul-An'biyai*: Kikao cha kisa cha Yusuf.

# MLANGO UNAOSEMA: SWALA HAIKUBALIKI MPAKA ATAKAPOSALIWA HUMO MUHAMMAD NA AALI MUHAMMAD (AS)

**Sunanul-Bayhaqiy Juz. 2, uk. 379:**[443]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Mas'ud, amesema: "Laiti ningeswali Swala ambayo humo sijawaswalia Aali Muhammad, ningeona kuwa Swala yangu haijatimia."

**Nasema:** Na ameipokea kwa njia nyingine baada ya hii, humo amesema: "Laiti ningeswali Swala ambayo humo sijamswalia Muhammad na Aaali Muhammad, nisingeona kuwa imetimia." Na pia kaipokea ad-Daru Qutuniy ndani ya *Sunan* yake uk. 136.

**Sunanud-Daru Qutuniy Uk. 136:**[444]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Mas'ud al-Ansariy, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Atakayeswali Swala ambayo humo hajaniswalia mimi wala watu wa nyumba yangu, haitakubaliwa Swala yake."'

**Dhakhairul-Uqba Uk. 19**[445]**:**

Amesema: Imepokewa kutoka kwa Jabir kuwa alikuwa akisema: "Laiti ningeswali Swala ambayo humo sijamswalia Muhammad na Aaali Muhammad, nisingeona kuwa itakubaliwa."

**As-Sawa'iqul-MuhriqahUk. 88:**[446]

Amesema: Shafiy ana beti zisemazo: "Enyi watu wa nyumba ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, kuwapenda ninyi ni faradhi kutoka kwa Mwenyezi Mungu aliyoiteremsha ndani ya Qur'ani. Inatosha kuwa heshima kubwa kwenu ninyi kuwa asiyewaswalia ninyi hana Swala."

**Nasema:** Beti hizi mbili kazitaja pia Shabalanjiy ndani ya *Nurul-Absari*uk. 104, na katika mlango ufuatao zitakuja habari zinazoamrisha kumswalia Mtukufu Mtume (saww) na Aali zake katika tashahudi ndani ya Swala, mfano kauli yake (saww) isemayo: "Mmoja wenu atakapotoa tashahudi ndani ya Swala basi na aseme: Ewe Mungu wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad."

Inajulikana wazi kuwa kitendo cha kuamrisha humaanisha wajibu, na kwamba yeyote atakayeacha makusudi wajibu miongoni mwa wajibu za Swala, Swala yake hubatilika, bali kwa mujibu wa kanuni hubatilika hata kama ataacha kwa kusahau, isipokuwa kama kuna dalili ya kipekee inayoonesha usahihi wake, mfano hadithi isemayo: Swala hairudiwi isipokuwa kutokana na mambo matano…

Kisha hakika Razi amesema ndani ya tafsiri yake mwishoni mwa tafsiri ya Aya ya Mapenzi katika Sura Shura: "Kuwaombea dua Aali ni cheo adhimu, na kwa ajili hiyo ndio maana amefanya dua hii kuwa hitimisho la tashahudi katika Swala, nayo ni kauli yake: Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad."

---

443 *Sunanul-Kubra*: Kitabu cha Swala, Mlango wa 471, Wajibu wa kumswalia Mtukufu Mtume (saww), Hadithi ya 3968.

444 *Sunanud-Dari Qutuniy*: Kitabu cha Swala, Mlango unaozungumzia wajibu wa kumswalia Mtukufu Mtume (saww), Tashahudi, Hadithi ya 6.

445 *Dhakhairul-Uqba*: Sehemu ya kwanza, Mlango unaozungumzia ubora wa Ahlul-Baiti.

446 *As-Sawa'iqul-Muhriqah*: Faslu ya kwanza, Aya zinazowazungumzia wao, Aya ya tatu.

# MLANGO UNAOZUNGUMZIA NAMNA YA KUMSALIA MUHAMMAD NA AALI MUHAMMAD

**Nasema:** Zimepokewa habari nyingi kuhusu namna ya kumswalia Muhammad na Aali Muhammad kiasi kwamba haziwezi kuhesabika, kama linavyodhihiri jambo hilo unaporejea katika kitabu *ad-Durul-Manthur* cha as-As-Suyutiyiy mwishoni mwa tafsiri ya Aya tukufu katika Sura Ahzab: **"Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake humswalia Nabii"**, ametaja hadithi mutawatiri zinazoonesha maana hii kutoka kwa Kaab bin Ajarah, Yunus bin Khabab, Ibrahim na Abdurahman bin Abi Kathir. Na kutoka kwa mtu mmoja miongoni mwa Masahaba wa Mtume (saww), na kutoka kwa Talha bin Ubaydullah, Abu Said al-Khidriy, Abu Huraira, Abu Mas'ud, Aqabah bin Amru, Ali (as), Zaidu bin Abi Kharijah, Buraydah, na IbnMas'ud.

Nasi katika mlango huu tutataja riwaya kadhaa kutoka katika kundi hilo kubwa la riwaya, tunasema:

**Sahih Bukhari: Kitabu cha dua, Mlango unaozungumzia kumswalia Mtukufu Mtume (saww):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdurahman bin Layla, amesema: "Nilikutana na Kaab bin Ajarah, akasema: 'Je nikupe zawadi? Hakika siku moja Mtukufu Mtume alitutokea, tukasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Tumeshajua namna ya kukutolea salamu, tutakuswaliaje? Akasema: Semeni: Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyowaswalia Aali Ibrahim, hakika wewe ni Muhimidiwa Msifiwa. Ewe Mungu wangu mbariki Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahim, hakika wewe ni Muhimidiwa Msifiwa."'

**Nasema:** Ameipokea pia ndani ya kitabu kinachozungumzia mwanzo wa uumbaji, na katika kitabu cha tafsiri. Na pia ameipokea Muslim ndani ya *Sahih* yake katika kitabu cha Swala. Na katika Mlango unaozungumzia kumswalia Mtukufu Mtume (saww) baada ya tashahudi, ameipokea kwa njia mbalimbali. Na ameipokea pia an-Nasaiy ndani ya *Sahih* yake, na Ibn Maja ndani ya *Sahih* yake, na Abu Daud ndani ya *Sahih* yake, na al-Hakim ndani ya *Mustadrakus-Sahihayn*, na Ahmad bin Hanbal ndani ya *Musnad* yake, na Abu Daud at-Twayalasiy ndani ya *Musnad* yake, na ad-Daramiy ndani ya *Sunan* yake, na al-Bayhaqiy ndani ya *Sunan* yake, na Abu Na'im ndani ya *Hilyatul-Awliyai*, na at-Twahawi ndani ya *Mushkilul-Athar*, na al-Khatibu al-Baghdadiy ndani ya *Taarikh* yake. Na hawa wa mwisho miongoni mwa maimamu wa hadithi wameikusanya kila mmoja kwa njia mbalimbali kutoka kwa Kaab bin Ajarah.

**Sahih Bukhari: Kitabu cha tafsiri, Mlango wa kauli ya Mwenyezi Mungu: "Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake humsalia Nabii…":**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Said al-Khidriy amesema: "Tulimwambia: Hii ni namna ya kukutolea salamu, tutakuswaliaje? Akasema: 'Semeni: Ewe Mungu wangu mswalie Muhammad mja wako na Mtume wako, kama ulivyowaswalia Aali Ibrahim, na mbariki Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahim."'

**Nasema:** Pia kaipokea kwa tofauti kidogo ndani ya kitabu cha dua katika Mlango unaozungumzia namna ya kumswalia Mtukufu Matume (saww). Na ameipokea an-Nasaiy ndani ya *Sahih* yake Juz. 1, uk. 190, na ameipokea Ahmad bin Hanbal ndani ya *Musnadi* yake Juz. 3, uk. 47, na ameipokea at-Twahawi ndani ya *Mushkilul-Athar* Juz. 3, uk. 73.

**Al-Adab al-Mufrad cha Bukhari Uk. 93:**[447]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Mtukufu Mtume (saww) kuwa alisema: “Atakayesema: Ewe Mungu wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyomswalia Ibrahim na Aali Ibrahim, na mbariki Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahim na Aali Ibrahim. Na mrehemu Muhammad na Aali Muhammad kama ulivyomrehemu Ibrahim na Aali Ibrahim. Nitamtolea ushahidi Siku ya Kiyama na nitamuombea.”

**Sahih Bukhari: Kitabu cha Swala, Mlango unaozungumzia kumswalia Mtukufu Mtume (saww) baada ya tashahudi:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Mas’ud al-Ansariy, amesema: “Siku moja Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alitujia tukiwa tumeketi kwa Saad bin Ubadah, Bashir bin Saad akamwambia: ‘Mwenyezi MunguMtukufu ametuamuru tukuswalie wewe, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, tutakuswaliaje?’ Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikaa kimya hadi tukatamani kwamba tusingemuuliza, kisha akasema: ‘Semeni: Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyomswalia Ibrahim, na mbariki Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahim katika walimwengu wote, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa. Ama salamu ni kama mlivyojua.’”

**Nasema:** Ameipokea Tirmidhiy ndani ya *Sahih* yake Juz. 2, uk. 212, amesema: “Na katika mlango huu kuna riwaya kutoka kwa Ali (as), na kutoka kwa Abu Hamid, Kaab bin Ajarah, Talha bin Ubaydullah, Abu Said, Zayd bin Kharijah –jina lake lingine ni Harithah- na Buraydah.“Kisha akasema: “Hadithi hii ni nzuri na sahihi.” Na ameipokea pia an-Nasaiy ndani ya *Sahih* yake, na Abu Daud ndani ya *Sahih* yake, na Malik bin Anas ndani ya *Muwatwau* yake, na Ahmad bin Hanbal ndani ya *Musnad* yake, na al-Hakim ndani ya *Mustadrakus-Sahihayn*, na ad-Daramiy ndani ya *Sunan* yake, na al-Bayhaqiy ndani ya *Sunan* yake, na at-Twahawi ndani ya *Mushkilul-Athar*, baadhi yao wameipokea kwa njia tofauti tofauti.

**Sahih an-Nasaiy Juz. 1, uk. 190:**[448]

Ameipokea kwa njia yake kutoka kwa Musa bin Talha, kutoka kwa baba yake, amesema: “Tulimwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! tutakuswaliaje? Akasema: ‘Semeni: Ewe Mungu wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyomswalia Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa. Na mbariki Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa.”’

**Nasema:** Pia ameipokea kwa njia nyingine kutoka kwa Musa bin Talha, na ameipokea Ibn Jariri Tabari ndani ya *Tafsiri* yake, na Ahmad bin Hanbal ndani ya *Musnad* yake, na Abu Na’im ndani ya *Hilyatul-Awliyai*, na at-Twahawi ndani ya *Mushkilul-Athar*, na Ibn Abdul-Barri ndani ya *al-Istiaab*, baadhi yao wameipokea kwa njia mbili.

**Sahih an-Nasaiy Juz. 1, uk. 190:**[449]

Ameipokea kwa njia yake kutoka kwa Musa bin Talha, amesema: “Nilimuuliza Zayd bin Kharijah, akasema: ‘Mimi nilimuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: Niswalieni na jitahidini katika dua, na semeni: Ewe Mungu wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad.”’

[447] *Al-Adab al-Mufrad* cha Bukhari, Mlango wa 280, Swala ya kumsalia Mtukufu Mtume (saww), Hadithi ya 641.
[448] *Sunanu an-Nasaiy*: Kitabu cha sahau, Mlango wa 52, Hadithi ya 1289.
[449] *Sunanu an-Nasaiy*: Kitabu cha sahau, Mlango wa 52, Hadithi ya 1291.

**Nasema:** Ameipokea pia Ahmad bin Hanbal ndani ya *Musnad* yake, Abu Na'im ndani ya *Hilyatul-Awliyai*, at-Twahawi ndani ya *Mushkilul-Athar*, na al-Munawi ndani ya *Faydhul-Qadir* katika matini na katika ufafanuzi, ameipokea kutoka katika kundi la wanahadithi. Na ameipokea Ibn al-Athir ndani ya *Usudul-Ghabah*.

**Sahih Ibn Majah Uk.65: Kitabu cha Swala[450]:**

Ameipokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Mas'ud, amesema: "Mnapomswalia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mswalieni vizuri, kwani hakika ninyi hamjui huenda akaoneshwa swala hiyo. Walimwambia: Tufundishe namna ya kukuswalia, akasema: 'Semeni: Ewe Mungu Wangu wekaswala zako, rehema zako na baraka zako juu ya bwana wa Mitume – Aliendelea kusimulia mpaka aliposema: Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyomswalia Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa. Ewe Mungu wangu mbariki Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa."'

**Nasema:** Ameipokea pia Abu Na'im ndani ya *Hilyatul-Awliyai* Juz. 4 Uk. 271.

**Fat'hul-Bariy Fii Sharhil-Bukhari Juz. 13, uk. 411[451]:**

Amesema: Tabari ameandika ndani ya *Tahdhib* yake kwa njia itokayo kwa Handhalah bin Ali, kutoka kwa Abu Huraira, kwa kuivusha, amesema: "Yeyote atakayesema: Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyomswalia Ibrahim na Aali Ibrahim, na mbariki Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahim na Aali Ibrahim. Na mrehemu Muhammad na Aali Muhammad kama ulivyomrehemu Ibrahim na Aali Ibrahim. Nitamtolea ushahidi Siku ya Kiyama na nitamuombea."

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 1, uk. 269[452]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa IbnMas'ud, kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuwa alisema: "Mtu atakapo kutoa tashahudi katika Swala basi na aseme: Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad, na mbariki Muhammad na Aali Muhammad, na mrehemu Muhammad na Aali Muhammad kama ulivyomswalia, ulivyombariki na ulivyomrehemu Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa."

**Nasema:** Na ameipokea al-Bayhaqiy ndani ya Sunan yake Juz. 2, uk. 279.

**Tafsiri Ibn Jarir at-Tabari Juz. 22, uk. 31[453]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Israil, kutoka kwa Yunus bin Khabab, amesema: "Alituhutubia huko Faris, akasema: **'Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake…'** akasema: Aliniambia yule aliyemsikia Ibn Abbas akisema: Hivyo ndivyo ilivyoshuka, tukasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Tumeshajua namna ya kukutolea salamu, tutakuswaliaje? Akasema: 'Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyomswalia Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa. Ewe Mungu Wangu mbariki Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa."'

---

[450] *Sahih Ibn Majah*: Kitabu kinachozungumzia kusimamisha Swala.
[451] *Fat'hul-Bariy Fii Sharhil-Bukhari*: Kitabu cha dua, Mlango wa 32, Kumswalia Mtukufu Mtume (saww), mwishoni mwa Hadithi ya 6358.
[452] *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha Swala, Mlango unaozungumzia matendo ya Swala baada ya tashahudi.
[453] *Tafsiri Tabari*: Sura Ahzab, Aya 56, Hadithi ya 28635.

**Tafsiri Ibn Jarir at-Tabari Juz. 22, uk. 31[454]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibrahim kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: **'Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake…'** wakasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Salamu tumeshaijua, tutakuswaliaje? Akasema: 'Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad mja wako na Mtume wako, na watu wa nyumbani kwake, kama ulivyomswalia Ibrahim hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 5, uk. 353[455]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Buraydah al-Khuzaiy, amesema: "Tulisema: Tumeshajua namna ya kukutolea salamu, tutakuswaliaje? Akasema: 'Semeni: Ewe Mungu Wangu weka swala zako, rehema zako na baraka zako juu ya Muhammad na Aali Muhammad kama ulivyoziweka juu ya Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa."

— **Nasema:** Na ameipokea pia al-Khatib al-Baghdadiy ndani ya *Taarikh* yake Juz. 8, uk. 142.

**Sunanul-Bayhaqiy Juz. 2 Uk. 147[456]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdurahman bin Abi Layla, kutoka kwa Kaab bin Ajarah, kutoka kwa Mtukufu Mtume (saww) kuwa alikuwa akisema ndani ya Swala: "Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyomswalia Ibrahim na Aali Ibrahim, na mbariki Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa."

**Nasema:** Ameipokea pia Shafi'i ndani ya *Musnad* yake uk. 23.

**Sunanud-Daru Qutuniy Uk. 135[457]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abi Layla- au Abu Maamar- amesema: "IbnMas'ud alinifundisha tashahudi na kuniambia kuwa: Alinifundisha tashahudi hii Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kama alivyokuwa akitufundisha Sura ya Qur'ani: Maamkizi, Swala na mazuri ni ya Mwenyezi Mungu. Amani iwe juu yako ewe Nabii, pia rehema zake na baraka zake. Amani iwe juu yetu na juu ya waja wema wa Mwenyezi Mungu. Nashahidia kwamba hapana mungu isipokuwa Allah, na nashahidia kwamba hakika Muhammad ni mja wake na Mtume wake. Ewe Mungu wangu mswalie Muhammad na watu wa nyumbani kwake kama ulivyomswalia Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa. Ewe Mungu wangu mbariki Muhammad na watu wa nyumbani kwake kama ulivyombariki Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa."

**Sunanud-Daru Qutuniy Uk. 135[458]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Mas'ud al-Ansariy Aqabah bin Amru, alisema: "Alikuja mtu mmoja na kuketi mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), nasi tukiwa kwa Mtume, akasema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ama namna ya kukutolea salamu tumeshajua, tutakuswaliaje tunapotaka kukuswalia ndani ya Swala zetu?' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikaa kimya hadi tukatamani kuwa mtu yule asingemuuliza, kisha akasema: 'Mnapotaka kuniswalia mimi semeni: Ewe Mungu

[454] *Tafsiri Tabari*: Sura Ahzab, Aya 56, Hadithi ya 28636.
[455] *Musnad Ahmad bin Hanbal:* Hadithi ya Burayda al-Aslamiy, Hadithi ya 22479.
[456] *Sunanul-Kubra*: Kitabu cha Swala, Mlango wa 253, Kumswalia Mtukufu Mtume (saw) ni sehemu ya tashahudi, Hadithi ya 2852.
[457] *Sunanud-Daru Qutuniy*: Kitabu cha Swala, Mlango unaozungumzia wajibu wa kumswalia Mtukufu Mtume (saww), Hadithi ya 1.
[458] *Sunanud-Daru Qutuniy*: Kitabu cha Swala, Mlango unaozungumzia wajibu wa kumswalia Mtukufu Mtume (saww), Hadithi ya 2.

Wangu mswalie Muhammad Nabii ambaye hakuwahi kusoma wala kuandika, na Aali Muhammad, kama ulivyomswalia Ibrahim na Aali Ibrahim. Nambariki Muhammad Nabii ambaye hakuwahi kusoma wala kuandika, na Aali Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa.

**Musnad Imam as-Shafiy Uk. 23[459]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira kuwa alisema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Tutakusaliaje – yaani ndani ya Swala- akasema: 'Mtasema: Ewe Mungu wangu msalie Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyomsalia Ibrahim. Na mbariki Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahim. Kisha mtanitolea salamu."'

**Nasema:** Ameitaja pia al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 4, uk. 103, kwa kunukuu kutoka kwa Shafi, na al-Bayhaqiy ndani ya *al-Maarifah* kutoka kwa Abu Huraira. Na ameipokea at-Twahawi ndani ya *Mushkilul-Athar* Juz. 3, uk. 75 kutoka kwa Abu Huraira.

**Taarikh Baghdad Juz. 14 Uk. 303[460]:**

Ameipokea kwa njia yake kutoka wa Ali (as) kuwa alisema: "Walisema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Tutakuswaliaje? Akasema: 'Semeni: Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyomswalia Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa. Na mbariki Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahim na Aali Ibrahim.'"

**Kanzul-Ummal Juz. 1, uk. 124[461]:**

Lafudhi yake ni: "Alizikabidhi Jibril mikononi mwangu na akasema kuwa hivyo ndivyo zilivyoteremka kutoka kwa Mola Mtukufu: Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyomswalia Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa. Ewe Mungu Wangu mbariki Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa. Ewe Mungu Wangu mrehemu Muhammad na Aali Muhammad kama ulivyomrehemu Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa. Ewe Mungu Wangu na mfikishie salamu Muhammad na Aali Muhammad kama ulivyomfikishia salamu Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa."

— Amesema: Ameiandika al-Bayhaqiy ndani ya *Shuabul-Iman* na ad-Daylamiy kutoka kwa Umar.

**Kanzul-Ummal Juz. 1, uk. 214[462]:**

Amesema: al-Hakim amesema ndani ya *Ulumul-Hadithi*: "AlizikabidhiAbu Bakr bin Abi Hazim mikononi mwangu. –Akaendelea kutaja sanad mpaka akasema: Alizikabidhi Ali bin Abu Talib (as) mikononi mwangu na akasema: Alizikabidhi Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mikononi mwangu na akasema: Alizikabidhi Jibril mikononi mwangu na akasema kuwa hivyo ndivyo zilivyoteremka kutoka kwa Mola Mtukufu: Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyomswalia Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa. Ewe Mungu Wangu mbariki Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa. Ewe

[459] *Musnad Imam as-Shafiy*: Kitabu cha kinachozungumzia kuelekea Kibla ndani ya Swala, Hadithi ya 90.
[460] *Taarikh Baghdad*: Wasifu wa Yusuf bin Nafisi al-Baghdadiy, Hadithi ya 7614.
[461] *Kanzul-Ummal*: Mlango wa sita, katika kumswalia (saww), Hadithi ya 2183.
[462] *Kanzul-Ummal:* Mlango wa sita, katika kumswalia (saww), Hadithi ya 3991.

Mungu Wangu mrehemu Muhammad na Aali Muhammad kama ulivyomrehemu Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa. Ewe Mungu Wangu mhurumie Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyomhurumia Ibrahim n Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa. Ewe Mungu Wangu na mfikishie salamu Muhammad na Aali Muhammad kama ulivyomfikishia salamu Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa."

— Amesema: Ameiandika al-Bayhaqiy ndani ya *Shuabul-Iman* kutoka kwa al-Hakim. Na ameiandika at-Tamimiy na Ibn al-Mufadhal, na Ibn Musaddiy, wote wameiandika ndani ya *Musalsalah* zao. Na ameiandika al-Qadhi Iyadh ndani ya *as-Shifau*, na pia ad-Daylamiy.

**Kanzul-Ummal Juz. 1 Uk. 215[463]:**

Amesema: Musnad ya Anas, Ibn Asakir: Alitueleza Abul-Maaliy al-Fadhlu bin Sahli, alizikabidhi mikononi mwangu. - Akaendelea kutaja sanadi mpaka akasema: "Ametusimulia Anas bin Malik, alizikabidhi mikononi mwangu, akasema: Alizikabidhi Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mikononi mwangu na akasema: Alizikabidhi Jibril mikononi mwangu na akasema: Alizikabidhi Mikail mikononi mwangu na akasema: Alizikabidhi Israfil mikononi mwangu na akasema: Alizikabidhi Mola wa walimwengu mikononi mwangu. Kisha aliniambia: Sema: 'Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyomswalia Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa. Ewe Mungu Wangu mrehemu Muhammad na Aali Muhammad kama ulivyomrehemu Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa. Ewe Mungu Wangu mhurumie Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyomhurumia Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa."

— Amesema: Ameiandika Ibn Asakiri.

**Kanzul-Ummal Juz. 4, uk. 104[464]:**

Kutoka kwa Aisha, alisema: "Masahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) walisema: Umetuamuru tukithirishe kukuswalia wewe katika usiku wa kwanza wa mwezi na katika mchana wa kwanza wa mwezi, na tunapenda tukuswalie kama upendavyo. Akasema: 'Semeni: Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyomswalia Ibrahim na Aali Ibrahim. Na mrehemu Muhammad na Aali Muhammad kama ulivyomrehemu Ibrahim na Aali Ibrahim. Na mbariki Muhammad na Aali Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa. Ama kunitolea salamu tayari mmeshajua namna yake.

— Amesema: Ameiandika Ibn Asakir.

**Kanzul-Ummal Juz. 4, uk. 104[465]:**

Lafudhi yake ni: "Mtakapotaka kuniswalia semeni: Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad Nabii ambaye hakuwahi kusoma wala kuandika, na Aali Muhammad, kama ulivyomswalia Ibrahim na Aali Ibrahim. Na mbariki Muhammad Nabii ambaye hakuwahi kusoma wala kuandika, na Aali Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa."

— Amesema: Ameiandika Ibn Haban kutoka kwa IbnMas'ud.

---

463 *Kanzul-Ummal*: Mlango wa sita, katika kumswalia (saww), Hadithi ya 3998.

464 *Kanzul-Ummal*: Mlango wa sita, katika kumswalia (saww), Hadithi ya 2178. *Kanzul-Ummal*: Kumswalia (saww) katika tashahudi, Hadithi ya 19888.

465 *Kanzul-Ummal*: Kumswalia (saww) katika tashahudi, Hadithi ya 19888.

**Kanzul-Ummal Juz. 3, uk. 15[466]:**

Lafudhi yake ni: "Hakuna Mwislamu atakayesimama usiku wa Arafa sehemu anayopasa kusimama, kisha akaelekea kibla na kusema mara mia moja: 'Hapana mungu isipokuwa Allah, Mmoja wa pekee asiye na mshirika, ufalme ni Wake na himidi njema ni Zake, kheri imo mikononi Mwake naYeye ni Muweza wa kila kitu.' Kisha akasoma Sura al-Fat'hah mara mia moja, kisha akasema mara mia moja: 'Nashahidia kuwa hapana mungu isipokuwa Allah, Mmoja wa pekee asiye na mshirika, na hakika Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake.' Kisha akamsabihi Mwenyezi Mungu mara mia moja kwa kusema: 'Utakasifu ni wa Mwenyezi Mungu, kila himidi njema ni ya Mwenyezi Mungu, na hapana mungu isipokuwa Allah, Mwenyezi Mungu ni Mkubwa, na hakuna uweza wala nguvu isipokuwa kwa msaada wa Mwenyezi Mungu.' Kisha akasoma Sura al-Ikhalsi mara mia moja, kisha akasema mara mia moja: 'Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad kama ulivyomswalia Ibrahim na Aali Ibrahim, hakika wewe ni Mhimidiwa Msifiwa, na ziwe juu yenu pamoja nao.' Isipokuwa ni lazima Mwenyezi Mungu atasema: 'Enyi Malaika Wangu, ni yapi malipo ya mja Wangu huyu? Amenisabihi na kunihalili, amenitukuza na kuniadhimu, amenitakasa, ameninasabisha, amenitambua, amenisifia na amemswalia Nabii Wangu, kuweni mashahidi enyi Malaika Wangu kuwa hakika Mimi nimemsamehe na nimemuombea, na laiti akitaka kuwaombea watu waliosimama hapa nitamkubalia ombi lake."'-Amesema: Ameiandika al-Bayhaqiy ndani ya *Shuabul-Iman*, na Ibn an-Najar na ad-Daylamiy kutoka kwa Jabir.

**Nasema:** Inadhihiri kutokana na aliyoyasema Ibn Hajar ndani ya *as-Sawa'iq*kwamba hakika kumuuliza kwao Mtukufu Mtume (saw) kuhusu namna ya kumswalia, ilikuwa ni baada ya kuteremka kauli ya Mwenyezi Mungu: **"Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamswalia Nabii. Enyi mlio amini! Mswalieni na mumsalimu kwa salamu."** Na kwamba kuuliza kwao baada tu ya kuteremka Aya hii na jibu lake kuwa: "Semeni: Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad." Ni dalili ya kwamba Swala ya kuwaswalia Aali ndio iliyokusudiwa katika Aya hii tukufu. Nasi hapa tunataja maneno yake kama yalivyo:

Amesema ndani ya *as-Sawa'iq*uk. 87: Aya ya pili- yaani miongoni mwa Aya zilizopatikana kuhusu Ahlul-Baiti- ni kauli ya Mwenyezi Mungu: "**'Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamswalia Nabii. Enyi mlioamini! Mswalieni na mumsalimu kwa salamu.'** Imesihi kutoka kwa Kaab bin Ajarah kuwa alisema: 'Ilipoteremka Aya hii tulisema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Tumeshajua namna ya kukutolea salamu, je, tutakuswaliaje? Akasema: Semeni: Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad- mpaka mwisho wake." – Amesema: "Na katika riwaya ya al-Hakim: Tulisema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, tutawaswaliaje ninyi Ahlul-Baiti? Akasema: Semeni Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad- mpaka mwisho wake."

— Amesema: Kuuliza kwao baada ya kuteremka Aya hii na yeye kuwajibu kuwa semeni: Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad mpaka mwisho wake, ni dalili ya dhahiri kuwa amri ya kuwaswalia Ahlul-Baiti wake ndio muradi wa Aya hii, la sivyo basi wasingemuuliza kuhusu kuwaswalia Ahlul-Baiti wake na Aali zake baada tu ya kuteremka kwake, na wala asingewajibu kama alivyowajibu, hivyo alipowajibu kwa jibu hilo ikaonesha kuwa kuwaswalia wao ni sehemu ya amri ya Aya hiyo, na kwamba yeye amewaweka nafasi yake, kwasababu makusudio ya kumswalia yeye ni kumtukuza yeye na kuwatukuza wao. Kisha alipoingia katika kishamiya alisema: "Ewe Mungu Wangu, hakika wao ni sehemu yangu na mimi ni sehemu yao, hivyo weka swala Zako, rehema Zako msamaha Wako na radhi Zako juu yangu na juu yao." Na katika kujibu dua hii Mwenyezi Mungu aliwaswalia wao pamoja naye, na wakati huo akawataka Waumini nao wawaswalie pamoja naye.

---

466 *Kanzul-Ummal*: Dua za siku ya Arafa, Hadithi ya 12110.

**Nasema:** Kwa uadilifu kabisa amepatia dalili katika kuthibitisha kuwa kuwaswalia wao Aali ndio muradi uliokusudiwa katika Aya hii tukufu kwa mujibu wa aliyoyataja, hivyo hakika Mwenyezi Mungu amewaamuru Waumini kumswalia Nabii, nao wakamuuliza Nabii ni jinsi gani wataweza kumswalia yeye? Akasema: Semeni: Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad. Hivyo nabii yuko katika kubainisha muradi alioukusudia Mwenyezi Mungu katika Aya hii tukufu, na hivyo laiti muradi wa Mwenyezi Mungu katika kumswalia Nabii usingekuwa ni kumswalia yeye na Aali zake basi Mtukufu Mtume asingeamuru kuswaliwa yeye na Aali zake katika jibu lake.

Kisha hakika kauli ya Ibn Hajar kuwa: "Na katika kujibu dua hii Mwenyezi Mungu aliwaswalia wao pamoja naye, na wakati huo akawataka Waumini nao wawaswalie pamoja naye." Maana yake ni kwamba Mtukufu Mtume (saww) alipowaingiza Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as) chini ya kishamiya, aliwaombea, na akamtaka Mwenyezi Mungu aweke swala Zake na baraka Zake juu yao, na katika kujibu dua yake Mwenyezi Mungu alimswalia yeye na wao, na hapo Mwenyezi Mungu akawataka Waumini wamswalie Nabii (saww) yeye na Aali zake kama alivyomswalia yeye na kuwaswalia wao.

Na Razi ana maelezo yake kama alivyosema Ibn Hajar ndani ya *as-Sawa'iq* yake uk. 89, na inafaa kuyaeleza hapa, amesema: "Na Fakhru Razi amesema kuwa hakika Ahlul-Baiti wake wako sawa na yeye katika mambo matano: Katika salamu, amesema: Salamu iwe juu yako ewe Nabii, na akasema: **'Salamu iwe juu ya Aali Yasin.'**Na katika kumswalia yeye na wao ndani ya tashahudi. Na katika utakaso, Mwenyezi Mungu amesema: **'Taha'**, yaani Msafi, na amesema: **'Na kuwatakaseni kabisa.'** Na katika kuharamishiwa sadaka na katika kuwapenda, Mwenyezi Mungu amesema: **'Nifuateni, Mwenyezi Mungu atawapenda.'** Na akasema: **'Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa karaba wangu.'**"

## MLANGO UNAOSEMA KUWA HAKIKA ALI, FATIMAH, HASAN NA HUSAIN (AS) NDIO AALI MUHAMMAD

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 6, Uk. 323[467]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Shahru bin Hawshab, kutoka kwa Ummu Salamah kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Fatimah (as): "Niitie mumeo na wanao, akawaita, akawafunika kishamiya cha Fadak, akaweka mkono juu yao na kusema: Ewe Mungu, hakika hawa ndio Aali Muhammad, weka swala Zako na baraka Zako juu ya Muhammad na juu ya Aali Muhammad, hakika Wewe ni Mhimidiwa Msifiwa." Ummu Salama anasema: "Nikafunua kishamiya ili niingie pamoja nao, lakini Mtume akakivuta toka mikononi mwangu na kusema: 'Hakika wewe upo katika kheri."'

**Nasema:** Ameipokea at-Twahawi ndani ya *Mushkilul-Athar* Juz. 1, uk. 334. Na ameipokea al-Mutaqiy al-Hindiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 7, uk. 103. Na ameitaja as-As-Suyutiy ndani ya *ad-Durul-Manthur* mwishoni mwa tafsiri ya Aya ya utakaso katika Sura Ahzab, na amesema: Ameiandika Tabaraniy.

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 3, uk. 108[468]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aamir bin Saad, amesema: Muawiya alimwambia Saad bin Abi Waqas: "Ni kitu gani chakuzuia kumtukana mtoto wa Abu Talib?" Akasema: "Siwezi kumtukana ninapo-

[467] *Musnad Ahmad bin Hanbal*: Hadithi ya Ummu Salamah mke wa Mtume, Hadithi ya 26206.
[468] *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha kuwatambia Masahaba, Kutaja baadhi ya fadhila za Ali (as).

kumbuka mambo matatu aliyoyasema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuhusu yeye, kwani kuwa na moja kati ya hayo ni jambo ninalotamani sana kuliko ngamia mwekundu." Muawiya akamwambia: "Na yapi hayo ewe Abu Is'haqa?" Akasema: "Siwezi kumtukana ninapokumbuka aliposhushiwa wahyi, akamchukua Ali na watoto wake na Fatimah na kuwaingiza chini ya nguo yake, kisha akasema: Ewe Mungu hakika hawa ndio Ahlul-Baiti wangu. Siwezi kumtukana ninapokumbuka alipomwacha mjini pamoja na watoto na wanawake, akasema: Hivi huridhii kuwa cheo chako kwangu ni sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu? Na wala siwezi kumtukana ninapokumbuka siku ya Khaibari, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: Kesho nitampa bendera mtu ambaye anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na Mwenyezi Mungu ataleta ushindi mikononi mwake. Tukamtazama Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa hamu, akasema: Ali yuko wapi? Wakasema: Anaumwa macho. Akasema: Mwiteni. Alipoitwa alimtemea mate machoni kisha akamkabidhi bendera na Mwenyezi Mungu akampa ushindi."

— Amesema: Hadithi hii ni sahihi kwa mujibu wa masharti ya masheikh wawili (Bukhari na Muslim).

**Nasema:** Pia ameipokea kwa muhtasari katika Juz. 3, uk. 147, na ameitaja al-Mutaqiy ndani *Kanzul-Ummal* Juz. 6, uk. 405 kwa kunukuu toka kwa Ibn an-Najar. Na ameipokea an-Nasaiy ndani ya *Khasa'isu* yake uk. 16.

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 3, uk. 148[469]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Ja'far bin Abu Talib, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipoona rehema ikishuka, alisema: 'Niitieni, niitieni.' Swafiyyah akasema: 'Nani ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu!' Akasema: 'Ahlul-Baiti wangu: Ali, Fatimah, Hasan na Husain.' Wakaitwa, Mtume akawafunika kishamiya, kisha akanyanyua mikono yake na kusema: 'Ewe Mungu Wangu, hawa ndio Aali wangu, basi mswalie Muhammad na Aali Muhammad.' Hapo Mwenyezi Mungu akateremsha: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**"

— Amesema: Hadithi hii ina sanadi sahihi.

**Ad-Durul-Manthur ya as-As-Suyutiyiy: Mwishoni mwa tafsiri ya Aya ya utakaso katika Sura Ahzab:**

Amesema: Ameandika Ibn Jarir, al-Hakim na Ibn Mardawayhi kutoka kwa Saad, amesema: "Wahyi ulimteremkia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), akawaingiza Ali, Fatimah na watoto wao chini ya nguo, kisha akasema: Ewe Mungu Wangu, hawa ndio familia yangu na watu wa nyumba yangu."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 6, Uk. 296[470]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ummu Salamah, amesema: "Siku moja Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa nyumbani kwangu, mara mtumishi wa kike alimwambia Mtume: 'Hakika Ali na Fatimah wako mlangoni.' Akaniambia: 'Simama na unipishe mimi na Ahlul-Baiti wangu.' Nikasimama na kwenda pembeni humo humo ndani ya nyumba. Mara akaingia Ali na Fatimah wakiwa pamoja na watoto wao Hasan na Husain wakiwa wangali watoto wadogo. Akawachukua watoto na kuwaweka mapajani mwake na kuwabusu, akamkumbatia Ali kwa mkono wake mmoja na Fatimah kwa mkono mwingine. Akambusu Ali na kumbusu Fatimah, kisha akawafunika kishamiya cheusi, akasema: 'Ewe Mungu Wangu

[469] *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha kuwatambia Masahaba, Hadithi zinazoeleza baadhi ya sifa makhususi za Ahlul-Baiti (as).
[470] *Musnad Ahmad bin Hanbal*: Hadithi ya Ummu Salamah mke wa Mtume, Hadithi ya 26206.

tuelekeze kwako na si kwenye moto, mimi na Ahlul-Baiti wangu.' Nikasema: Na mimi ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: 'Na wewe.'"

**Nasema:** Ameitaja Tabari ndani ya *Dhakhairul-Uqba*uk. 21, na amesema: "Ameiandika Ahmad na ad-Dawlabiy ameandika maana yake kwa muhtasari." Na ameitaja al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 7, uk. 103, na amesema: "Ameiandika Ibn Abi Shayba." Na ameiandika kwa mara ya pili kwa muhtasari katika uk. 103, na amesema: "Ameiandika Tabaraniy.

**Kanzul-Ummal Juz. 6 Uk. 217[471]:**

Lafudhi yake ni: "Ewe Mungu Wangu hakika Wewe uliweka sala Zako, rehema Zako, msamaha wako na radhi Zako juu ya Ibrahim na Aali Ibrahim. Ewe Mungu Wangu hakika wao ni sehemu yangu na mimi ni sehemu yao, hivyo weka swala Zako, rehema Zako, msamaha Wako na radhi Zako, juu yangu na juu yao, yaani Ali, Fatimah, Hasan na Husain."

— Amesema: Ameiandika Tabaraniy kutoka kwa Wathilah.

**Kanzul-Ummal Juz. 7, uk. 92[472]:**

Amesema: Kutoka kwa Wathilah, amesema: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliwakusanya Fatimah, Ali, Hasan na Husain chini ya nguo yake, akasema: 'Ewe Mungu Wangu hakika Wewe uliweka swala Zako, rehema Zako, msamaha Wako na radhi Zako juu ya Ibrahim na Aali Ibrahim. Ewe Mungu Wangu hakika hawa ni sehemu yangu na mimi ni sehemu yao, hivyo weka swala Zako, rehema Zako, msamaha Wako na radhi Zako, juu yangu na juu yao.'" Wathilah anasema: "Nilikuwa mlangoni, nikasema: Na juu yangu ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwa haki ya baba yangu na mama yangu? Akasema: 'Ewe Mungu Wangu, juu yangu na juu ya Wathilah."'

— Amesema: Ameiandika ad-Daylamiy.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9 Uk. 167[473]:**

Amesema: Kutoka kwa Wathilah bin al-Asqau, amesema: "Nilitoka nikiwa namtaka Ali, nikaambiwa: 'Yeye yuko kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).' Nilipokwenda nikawakuta kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) huku akiwa kawaweka Ali, Fatimah, Hasan na Husain chini ya nguo, akasema: 'Ewe Mungu Wangu hakika Wewe umeweka swala Zako, rehema Zako, msamaha Wako na radhi Zako, juu yangu na juu yao.'"

— Amesema: Ameipokea Tabaraniy.

**Nasema:** Habari zinazoeleza kuwa Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as) ndio Aali Muhammad hazikomei katika hizi tu tulizozitaja katika mlango huu, bali zitafuata tena habari nyingi katika mlango unaosema kuwa Aya ya utakaso ilitereka kuhusu Mtukufu Mtume, Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as).

---

[471] *Kanzul-Ummal*: Mlango wa tano kuhusu fadhila za Ahlul-Bait, Hadithi ya 2486.
[472] *Kanzul-Ummal*: Herufi Waw, Wathilah bin al-Asqau, Herufi 37544.
[473] *Maj'mauz-Zawaid Waman'baul-Fawaid*: Mlango unaozungumzia fadhila za Ahlul-Baiti wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

## MLANGO UNAOKATAZA KUMSWALIA MTUKUFU MTUME (SAWW) SALA KIGUTU

**As-Sawa'iqul-MuhriqahUk. 87:**

Amesema: Imepokewa: "Msinisalie swala kigutu." Wakasema ni ipi hiyo swala kigutu? Akasema: "Ni kusema: 'Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad,'na muishie hapo, bali semeni: 'Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad.'"

**Nasema:** Na la ajabu na kustaajabisha zaidi ni kuhusu hawa ulamaa, maimamu wa hadithi, watunzi na waandishi wa Kisunni, ambao wamepokea habari ambazo tayari umeshazijua ambazo zinaonesha kuwa dua huzuiliwa mpaka aswaliwe Muhammad na Aaali Muhammad, na kwamba Swala haikubaliwi mpaka aswaliwe humo Muhammad na Aali Muhammad, na wao wenyewe wameonesha namna ya kumswaliaMuhammad na Aali Muhammad, na kwamba Mtukufu Mtume (saww) alikataza kuswaliwa swala kigutu, yaani kumswalia Mtume bila kuwataja Aali zake, na dhahiri ni kwamba katazo hili ni la kuharamisha, lakini cha ajabu pamoja na hayo bado utawakuta wanang'ang'ania kumswalia Mtume bila kuwataja Aali zake wakati wa kumswalia, hivyo watakapo kumswalia Mtukufu Mtume (saww) husema: "Mwenyezi Mungu amswalie na kumfikishia salamu yeye." Bila kuwataja Aali zake, na kama una shaka na haya tuliyoeleza basi rejea vitabu vyao vya hadithi, tafsiri, fadhila, wapokezi, sira na mfano wake, utakuta ni kweli tupu yale tuliyosema.

Na la ajabu zaidi ni kuwa wakati ambapo wanataja habari za kumswalia Mtume, na wakati ambapo wanapokea hadithi za namna ya kumswalia, na kwamba Mtukufu Mtume alisema: "Mtakapo kuniswalia semeni: Ewe Mungu Wangu, mswalie Muhammad na Aali Muhammad;" ni wakati huo huo ikiwa watataja jina la Mtume utawaona wakisema: "Mwenyezi Mungu amswalie na kumfikishia salamu yeye." Wanaacha kuwataja Aali Muhammad. Naapa kwa umri wangu hakika si chochote isipokuwa ni chuki binafsi na kumkhalifu Mtukufu Mtume ambaye hatamki kwa matamanio yake.

## MLANGO UNAOSEMA KUWA AYA YA UTAKASO ILITEREMKA KWA AJILI YA MTUKUFU MTUME (SAWW), ALI, FATIMAH, HASAN NA HUSAIN (AS)

Sahih Muslim: Kitabu kinachozungumzia fadhila za Masahaba, Mlango unaozungumzia fadhila za Ahlul-Baiti (as):

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Swafiyyah binti Shaybah, amesema: "Aisha alisema: Siku moja asubuhi Mtukufu Mtume (saww) alitoka huku akiwa kajifunika shuka jeusi, mara alikuja Hasan bin Ali akamwingiza ndani ya shuka hilo, kisha akaja Husain naye akamwingiza, kisha akaja Fatimah naye akamwingiza, kisha akaja Ali naye akamwingiza, kisha akasema: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**"

**Nasema:** Pia ameipokea al-Hakim ndani ya *Mustadrakus-Sahihayni* Juz. 3, uk. 147, na amesema humo: "Hadithi hii ni sahihi kwa mujibu wa sharti za Mashekhe wawili." Na ameipokea al-Bayhaqiy ndani ya *Sunan* yake Juz. 2 uk. 149. Na ameipokea Ibn Jarir ndani ya *Tafsiri* yake Juz. 2, uk. 5, kutoka kwa Aisha. Na ameitaja as-As-Suyutiy ndani ya *ad-Durul-Manthur* katika tafsiri ya Aya ya utakaso katika Sura Ahzab, na amesema humo: "Ameiandika Ibnu Abi Shaybah, Ahmad na Ibn Abi Hatim." Na ameitaja

Zamakhshariy ndani ya *al-Kashaf* katika tafsiri ya Aya ya maapizano, na pia Fakhru Razi kaitaja katika tafsiri ya Aya hiyo, na amesema: "Na tambua kuwa hakika riwaya hii ni kama wameafikiana juu ya usahihi wake watu wote wa tafsiri na hadithi.

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, uk. 209:**[474]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Umar bin Abi Salamah mtoto wa kulea wa Mtukufu Mtume (saww), amesema: "Ilipoteremka Aya hii juu ya Mtukufu Mtume (saww): **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara,'**ndani ya nyumba ya Ummu Salamah, Mtume alimwita Fatimah, Hasan na Husain na kuwafunika kishamiya huku Ali (as) akiwa nyuma ya mgongo wake, aliwafunika kishamiya kisha akasema: 'Ewe Mungu Wangu hawa ndio Ahlul-Baiti wangu, waondolee uchafu na wasafisheni barabara.' Ummu Salama akasema: 'Je na mimi niko pamoja nao ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu?' Akasema: 'Wewe una sehemu yako, wewe uko katika kheri.'"

**Nasema:** Ameipokea pia ndani ya Juz. 2, uk. 308, kisha akasema: "Na katika mlango huu kuna riwaya kutoka kwa Ummu Salamah na Maaqal bin Yasar, Abil-Hamrai na Anas." Na ameipokea at-Twahawi ndani ya *Mushkilul-Athar* Juz. 1, uk. 335, na ameipokea Ibn al-Athir al-Jazriy ndani ya *Usudul-Ghabah* Juz. 2, uk. 12. Na ameipokea Ibn Jarir Tabari ndani ya *Tafsiri* yake Juz. 22, uk. 6 na ndani ya uk. 7, amesema: "Kutoka kwa Ummu Salamah."

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2 Uk. 319:**[475]

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Shahri bin Hawshab, kutoka kwa Ummu Salamah, alisema: "Hakika Mtukufu Mtume (saww) alimfunika kishamiya Hasan, Husain, Ali na Fatimah, kisha akasema: 'Ewe Mungu Wangu, hawa ndio Ahlul-Baiti wangu na watu makhususi kwangu, waondolee uchafu na wasafishe barabara.' Ummu Salamah akasema: 'Na mimi niko pamoja nao ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu!' Akasema: 'Hakika wewe uko katika kheri."'

Amesema: Nayo ndio hadithi nzuri zaidi (kimapokezi) kati ya zile zilizopokewa katika mlango huu. Kisha akasema: Na katika mlango huu kuna hadithi kutoka kwa Amru bin Abi Salamah, Anas bin Malik, Abil-Hamrau, Maaqal bin Yasari na Aisha.

**Nasema:** Ameipokea Ibn Jarir Tabari ndani ya *Tafsir* yake Juz. 22, uk. 6, amesema humo: "Nikawawekea chakula wakala na kulala, -Mtume- akawafunika shuka, kisha akasema: Ewe Mungu Wangu, hawa ndio Ahlul-Baiti wangu…"

Na ameipokea Ahmad bin Hanbal ndani ya *Musnad* yake Juz. 6, uk. 306. Na ameipokea Ibn al-Athir al-Jazriy ndani ya *Usudul-Ghabah* Juz. 4, uk. 29. Na ameitaja Ibn Hajar al-Asqalaniy ndani ya *Tahdhibut-Tahdhib* Juz. 2, uk. 297, na ameitaja al-Muhibu Tabari ndani ya *Dhakhairu* yake uk. 21, kwa tofauti kidogo.

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2 Uk. 209:**[476]

Ameipokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa akipita kwenye mlango wa Fatimah, muda wa miezi sita kila siku aendapo kwenye Swala ya Alfajiri, na kusema: "Swala enyi Ahlul-Baiti **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu,**

[474] *Sunanit-Tirmidhiy*: Kitabu cha tafsiri ya Qur'ani, Mlango wa 34 wa Sura Ahzab, Hadithi ya 3205.
[475] *Sunanit-Tirmidhiy*: Kitabu cha tafsiri ya Qur'ani, Mlango wa 61, Fasli ya Fatimah binti Muhammad (saww), Hadithi ya 3871.
[476] *Sunanit-Tirmidhiy*: Kitabu cha tafsiri ya Qur'ani, Mlango wa 34 wa Sura Ahzab, Hadithi ya 3206.

**enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**"

— Amesema: Na katika mlango huu kuna riwaya kutoka kwa Abil-Hamrau, Maaqal bin Yasari na Ummu Salamah.

**Nasema:** Ameipokea pia Ibn Jarir Tabari ndani ya *Tafsiri* yake Juz. 22, uk. 5, na ameipokea al-Hakim ndani ya *Mustadrakus-Sahihayn* Juz. 3, uk. 158, na amesema: "Hadithi hii ni sahihi kwa mujibu wa sharti za mashekhe wawili." Na ameipokea Ahmad bin Hanbal ndani ya *Musnad* yake Juz. 3, uk. 252, na ameipokea Ibn al-Athir al-Jazriy ndani ya *Usudul-Ghabah* Juz. 5, uk. 521. Na ameitaja al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 7, uk. 103 kwa kunukuu kutoka kwa Ibn Abi Shayba. Na ameitaja As-Suyutiy ndani ya *ad-Durul-Manthur* katika tafsiri ya Aya ya utakaso katika Sura Ahzab, amesema: "Ameiandika Ibn al-Mundhir na Tabaraniy kutoka kwa Ibn Mardawayhi.

**Ad-Durul-Manthur ya As-Suyutiy katika tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: "Na waamrishe watu wako kuswali"[477]:**

Amesema: Ameandika Ibn Mardawayhi na Ibn Asakir kutoka kwa Abi Said al-Khudriy kuwa alisema: "Ilipoteremka: **"Na waamrishe watu wako kuswali"**Mtukufu Mtume (saww) alikuwa akija kwenye mlango wa Ali (as) kila wakati wa Swala ya Alfajri, muda wa miezi nane, na kusema: 'Swala, Mwenyezi Mungu akurehemuni. **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**"

**Tafsiri Ibn Jarir Tabari Juz. 22, uk. 7[478]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Hakim bin Saad, amesema: "Tulimtaja Ali bin Abu Talib (as) mbele ya Ummu Salamah, akasema: 'Ni kwa ajili yake iliteremka: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**"

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 2, uk. 416[479]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ummu Salamah kuwa alisema: "Aya hii: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'** Iliteremkia ndani ya nyumba yangu, na ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akatuma aitwe Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as), akasema: 'Ewe Mungu Wangu hakika hawa ndio Ahlul-Baiti wangu.' Ummu Salamah akasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Je mimi sio miongoni mwa Ahlul-Baiti? Akasema: 'Hakika wewe uko katika kheri, na hawa ndio Ahlul-Baiti wangu, ewe Mungu Wangu Ahlul-Baiti wangu ndio wenye haki zaidi.'"

— Amesema: Hadithi hii ni sahihi kwa mujibu wa sharti za Bukhari.

**Nasema:** Na ameipokea pia katika Juz. 3, uk. 147. Na ameipokea al-Bayhaqiy ndani ya *Sunan* yake Juz. 2, uk. 150. Na ameipokea at-Twahawi ndani ya *Mushkilul-Athar* Juz. 1, uk. 334. Na ameipokea al-Khatib al-Baghdadiy ndani ya *Taarikh Baghdad* Juz. 9, uk. 126. Na ameipokea Ibn Jarir Tabari ndani ya *Tafsiri* yake Juz. 22, uk. 7. Na ameipokea Ibn al-Athir al-Jazriy ndani ya *Usudul-Ghabah* Juz. 5, uk. 521 na uk. 589. Na ameitaja al-Muhibu Tabari ndani ya *Dhakhairu* yake uk. 23, amesema: "Ameiandika Abul-Khairi al-Qazuwiniy."

---

477 *Tafsiru ad-Durul-Manthur*: Sura Taha, Mwishoni mwa Aya ya 132.

478 *Tafsiru Tabariy*: Sura Ahzab, Aya ya 33, Hadithi ya 28502.

479 *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha tafsiri, tafsiri ya Sura Ahzab, Mlango unaozungumzia jinsi Mtume alivyowakusanya Ahlul-Baiti wake na kusema: Ewe Mungu Wangu, hawa ndio Ahlul-Baiti wangu.

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 3, uk. 147[480]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Ja'far bin Abu Talib kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipoona rehema ikishuka, alisema: 'Niitieni, niitieni.' Swafiyyah akasema: 'Nani ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu!' Akasema: 'Ahlul-Baiti wangu: Ali, Fatimah, Hasan na Husain.' Wakaitwa, Mtume akawafunika kishamiya, kisha akanyanyua mikono yake na kusema: 'Ewe Mungu Wangu, hawa ndio Aali wangu, basi mswalie Muhammad na Aali Muhammad.' Hapo Mwenyezi Mungu akateremsha: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**"

— Amesema: Hadithi hii ina sanadi sahihi.

**Ad-Durul-Manthur ya As-Suyutiy, Juz. 5 Uk. 198 na 199: Katika tafsiri ya Aya ya utakaso katika Sura Ahzab:**

Amesema: Ibn Mardawayhi ameandika kutoka kwa Ummu Salamah kuwa alisema: "Aya hii: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara'**iliteremkia ndani ya nyumba yangu, na ndani ya nyumba tulikuwa saba: Jibril, Mikail, Ali, Fatimah, Hasan, Husain na mimi nikiwa mlangoni. Nikasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Je mimi sio miongoni mwa Ahlul-Baiti? Akasema: 'Hakika wewe uko katika kheri, hakika wewe ni miongoni mwa wake wa Nabii.'"

Na amesema pia: Ibn Mardawayhi na al-Khatib wameandika kutoka kwa Abi Said, amesema: "Ilikuwa ni siku ya Ummu Salamah mama wa Waumini (r.a.), ndipo Jibril akateremka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa na Aya hii: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'** Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwita Hasan, Husain, Fatimah na Ali (as) na kuwakumbatia, kisha akawafunika nguo huku kukiwa na kizuizi mbele ya Ummu Salamah, kisha akasema: 'Ewe Mungu Wangu, hawa ndio Ahlul-Baiti wangu. Ewe Mungu Wangu, waondolee uchafu na watakase barabara.' Ummu Salamah akasema: 'Je mimi niko pamoja nao ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu?' Akasema: 'Wewe una sehemu yako, hakika wewe uko katika kheri.'"

Na amesema pia: Ameandika Tirmidhiy ndani ya *Sahih* yake, na Ibn Jarir na Ibn al-Mundhir na al-Hakim ambaye amesema ni riwaya sahihi, na Ibn Mardawayhi na al-Bayhaqiy ndani ya *Sunan* yake, wameandika kwa njia mbalimbali kutoka kwa Ummu Salamah kuwa amesema: "Aya hii: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara'**iliteremkia ndani ya nyumba yangu, na ndani ya nyumba alikuwemo Fatimah, Ali, Hasan na Husain (as), Mtume wa Mwenyezi Mungu akawafunika kwa kishamiya alichokuwa kajifunika, kisha akasema: 'Hawa ndio Ahlul-Baiti wangu, waondolee uchafu na watakase barabara."'

Na amesema pia: Ameiandika Ibn Jarir na Ibn Abi Hatim na Tabaraniy kutoka kwa Abi Said al-Khudriy (r.a.) kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Aya hii: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara'** iliteremka kwa ajili yangu mimi, Ali, Fatimah, Hasan na Husain."'

Amesema pia: Na ameandika Ibn Abi Shayba na Ahmad na Ibn Jariri na Ibn al-Mun'dhir na Ibn Abi Hatim na Tabaraniy na al-Hakim ambaye amesema kuwa ni hadithi sahihi, na al-Bayhaqiy ndani ya *Sunan* yake, wameandika kutoka kwa Wathilah bin al-Asqau kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikwenda kwa Fatimah (as) akiwa pamoja na Hasan, Husain na Ali (as), alipoingia aliwasogeza karibu Ali na Fatimah na kuwakalisha mbele yake, na akamkalisha Hasan na Husain kila mmoja katika

[480] *Mustadrakus-Sahihayn*: Kitabu cha kuwatambua Masahaba, Mlango wa hadithi zinazozungumzia khususia za Ahlul-Baiti.

paja lake, kisha aliwafunika nguo yake huku mimi nikiwa nyuma yao, kisha akasoma Aya hii: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**"

Na pia amesema: Ameandika Tirmidhiy na Tabaraniy na Ibn Mardawayhi na Ibn Na'im na al-Bayhaqiy, hawa wawili kwa pamoja wameandika ndani ya *ad-Dalailu* kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Hakika Mwenyezi Mungu aliwagawa viumbe mafungu mawili, akaniweka mimi katika fungu bora kati ya hayo mawili- aliendelea kusimulia mpaka aliposema: Kisha akayawekea makabila nyumba, akaniweka mimi katika nyumba bora kati ya nyumba za makabila hayo, na hiyo ndio kauli ya Mwenyezi Mungu: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'** Hivyo mimi na Ahlul-Baiti wangu tumetakaswa dhidi ya madhambi."

Amesema pia: Ameandika Ibn Jarir na Ibn Abi Hatim kutoka kwa Qatadah kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'** Amesema: "Hao ni Ahlul-Baiti, Mwenyezi Mungu amewatakasa dhidi ya maovu na kuwachagua kwa rehema zake."

Amesema: "Na amesimulia ad-Dhahak bin Muzahim kwamba Mtukufu Mtume (saww) alikuwa akisema: "Sisi ndio Ahlul-Baiti ambao Mwenyezi Mungu amewatakasa, sisi twatokana na mti wa unabii, sisi ndio maweko ya utume, mapishano ya Malaika, nyumba ya rehema na chimbuko la elimu."

Na amesema pia: Na ameandika Ibn Mardawayhi kutoka kwa Abi Said al-Khidri kwamba alisema: "Ali (as) alipomuoa Fatimah (as), Mtukufu Mtume (saww) alikwenda kwenye mlango wao muda wa siku arubaini kila asubuhi, na kusema: 'Amani iwe juu yenu enyi watu wa nyumba ya Mtume, na pia rehema za Mwenyezi Mungu na baraka zake ziwe juu yenu. **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'** Hakika mimi ni mwenye kumpiga vita yule mwenye kuwapigeni ninyi vita na ni mwenye kuishi kwa amani na yule mwenye kuishi kwa amani na ninyi."'

Na amesema pia: Ameandika Ibn Jarir na Ibn Mardawayhi kutoka kwa Abul-Hamrai, amesema: "Nilihifadhi kutoka kwaMtume wa Mwenyezi Mungu (saww) matukio ya miezi nane akiwa huko Madina, hakuwahi hata mara moja kwenda kwenye Swala ya Subhi bila kwenda kwenye mlango wa Fatimah (as) na kuweka mikono yake miwili katika pande mbili za mlango na kusema: 'Swala, swala, **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'"**

Na pia amesema: Ameandika Ibn Mardawayhi kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: "Nilimshuhudia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) muda wa miezi tisa kila siku wakati wa kila Swala akienda kwenye mlango wa Ali bin Abu Talib (as) na kusema: 'Amani iwe juu yenu na pia rehema za Mwenyezi Mungu na baraka zake enyi watu wa nyumba ya Mtume. **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'** Swala Mwenyezi Mungu akurehemuni.' Alikuwa akisema hayo kila siku mara tano."

Na pia amesema: Ameandika Tabaraniy kutoka kwa Abul-Hamrau kuwa amesema: "Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) muda wa miezi sita akija kwenye mlango wa Fatimah na Ali na kusema: '**'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'"**

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 1, uk. 330[481]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Amru bin Maimuna kuwa alisema: "Wakati nikiwa nimeketi kwa Ibn Abbas mara alijiwa na watu tisa, wakasema: 'Ewe mtoto wa Abbas ima unyanyuke pamoja nasi na ima hawa ulionao watupishe.' Ibn Abbas akasema: 'Bali nanyanyuka pamoja nanyi.' Wakati huo alikuwa bado mzima hajapofuka. Walikwenda pembeni na kuanza kuzungumza, na hatujui walizungumza nini. Mara alirudi huku akipukuta nguo yake na kusema: 'Ole wao, ole wao, wanawezaje kumtuhumu mtu mwenye mambo kumi. Wanamtuhumu mtu ambaye Mtukufu Mtume (saww) alimwambia: 'Nitamtuma mtu ambaye kamwe Mwenyezi Mungu hatamdhalilisha, anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake.' Akatamani hilo mwenye kutamani, akasema (saww): 'Yuko wapi Ali?' Wakasema: Yuko kwenye mizigo anatwanga. Akasema: 'Kwa nini asitwange mmoja wenu?' Ndipo akaja akiwa anaumwa macho kiasi kwamba hawezi kuona, akamtemea mate machoni kisha akatikisa bendera mara tatu na kumkabidhi, na hatimaye akaja na Swafiyyah binti Hayu.

"'Kisha alimtuma fulani aende na Sura Tawba, akamtuma Ali nyuma yake kwenda kuichukua toka kwake (toka kwa huyo fulani), akasema (saww): 'Haendi nayo isipokuwa mtu ambaye ni sehemu yangu na mimi ni sehemu yake.' Na aliwaambia watoto wa ami yake: 'Kati yenu ni nani atanisaidia duniani na Akhera?' Aliyasema hayo akiwa ameketi pamoja na Ali, lakini wote walikataa, Ali (as) akasema: 'Mimi nitakusaidia duniani na Akhera.' Mtume akasema: 'Wewe ndio msaidizi wangu duniani na Akhera.' Akamwacha kisha akamwelekea mtu mmoja kati yao, akasema: 'Kati yenu ni nani atanisaidia duniani na Akhera?' wote wakakataa, Ali (as) akasema: 'Mimi nitakusaidia duniani na Akhera.' Mtume akasema: 'Wewe ndio msaidizi wangu duniani na Akhera.' Na yeye ndiye mtu wa kwanza kuukubali Uislamu baada ya Khadija. Na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alichukua nguo yake na kuwafunika Ali, Fatimah, Hasan na Husain, kisha akasema: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**'

"Ibn Abbas aliendelea kusema: 'Ali (as) aliuza nafsi yake akavaa nguo ya Mtukufu Mtume na kulala sehemu yake, na wakati huo Mushrikina walikuwa wakimkusudia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), alipokuja Abu Bakr alimkuta Ali (as) kalala huku Abu Bakr akidhani kuwa ndiye Nabii wa Mwenyezi Mungu, akamwambia: 'Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu!' Ali (as) akamwambia: 'Hakika Nabii wa Mwenyezi Mungu ametoka na kuelekea upande wa kisima cha Maymuna hivyo mdiriki. Abu Bakr alikwenda na kuingia pamoja naye pangoni. Ali (as) alikuwa akitupiwa mawe kama anavyotupiwa Nabii wa Mwenyezi Mungu (saww) – Aliendelea kusimulia mpaka aliposema: Mtume akatoka na watu kwenye vita vya Tabuk, Ali (as) akamwambia: 'Je nitoke pamoja nawe?' Nabii wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia hapana, Ali (as) akalia, ndipo Mtume akamwambia: 'Hivi huridhii kuwa cheo chako kwangu ni sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa wewe si Nabii? Hakika haifai mimi kwenda bila ya wewekuwa khalifa wangu."

"Ibn Abbas aliendelea kusema: 'Na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Wewe ni mrithi wangu kwa kila muumini baada yangu.' Na alisema: 'Zibeni milango ya msikiti isipokuwa mlango wa Ali.' Alikuwa akiingia msikitini na janaba kwani ilikuwa ndio njia yake hakuwa na njia nyingine. Na akasema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi huyu Ali ndiye mtawala wake.' Na Mwenyezi Mungu ametupa habari ndani ya Qur'ani kuwa amewaridhia watu wa chini ya mti, na amejua yaliyomo ndani ya nyoyo zao, je kuna yeyote aliyetusimulia kuwa baada ya hapo aliwaghadhibikia."'

**Nasema:** Pia ameipokea an-Nasaiy ndani ya *Khasa'is* yake uk. 8, na amesema: "Alimtuma Abu Bakr aende na Sura Tawba, na akamtuma Ali nyuma yake…" Na ameitaja al-Muhibu Tabari ndani ya *ar-Riyadh an-Nadhrah* Juz. 2, uk. 203, na amesema: "Ameiandika kwa ukamilifu wake Ahmad na al-Hafidh

[481] *Musnad Ahmad bin Hanbal*: Musnad Abdullah bin Abbas, Hadithi ya 3052.

Abul-Qasim ad-Damashqiy ndani ya *al-Muwafaqat* na ndani ya *al-Ar'bauna at-Twawali*."Na amesema tena: "Na Ameiandika an-Nasaiy kwa ufupi."Na ameitaja al-Haythamiy ndani ya *Maj'mau* yake Juz. 9, uk. 119, na amesema: "Ameipokea Ahmad na Tabaraniy ndani ya *al-Kabir* na ndani ya *al-Awsat* kwa muhtasari."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 4 Uk. 107[482]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Shadad Abi Ammar, amesema: "Niliingia kwa Wathilah bin al-Asqau, nikamkuta akiwa ameketi na jamaa, wakamtaja Ali (as), walipoondoka akaniambia: 'Je nikueleze yale niliyoyaona toka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu?' Nikasema ndio, akasema: 'Nilikwenda kwa Fatimah kumuulizia Ali (as), akasema: Ameelekea kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Nikaketi nikimsubiri, mpaka alipokuja Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa pamoja na Ali, Hasan na Husain (as) huku kamshika mkono kila mmoja kati ya hao wawili. Alipoingia aliwasogeza karibu Ali na Fatimah na kuwakalisha mbele yake, na akamkalisha Hasan na Husain kila mmoja juu ya paja lake, kisha aliwafunika nguo yake na kusoma Aya hii: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'** Na akasema: 'Ewe Mungu Wangu hawa ndio watu wa nyumba yangu, na watu wa nyumba yangu ndio wenye haki zaidi.'"

**Nasema:** Ameipokea pia Ibn Jarir Tabari kwa njia mbili ndani ya *Tafsiir* yake Juz. 22, uk. 6, na ameipokea al-Hakim ndani ya *Mustadrakus-Sahihayn* Juz. 2, uk. 416, na amesema: "Hii ni hadithi sahihi kwa mujibu wa masharti ya Muslim." Na pia kaipokea katika Juz. 3 uk. 147, na amesema: "Hadithi hii ni sahihi kwa mujibu wa masharti ya mashekhe wawili." Na ameipokea al-Bayhaqiy ndani ya *Sunan* yake kwa njia mbili katika Juz. 2, uk. 152, na ameipokea at-Twahawi ndani ya *Mushkilul-Athar* Juz. 1, uk. 336, na ameitaja al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 7, uk. 92 kwa kunukuu kutoka kwa Ibn Abi Shayba na Ibn Asakir. Na ameitaja al-Haythamiy ndani ya *Maj'mau* yake Juz. 9, uk. 167, na amesema: "Ameipokea Ahmad na Abu Ya'ala kwa muhtasari na Tabaraniy." Na ameipokea tena katika uk. 167 kwa lafudhi nyingine na kusema: "Ameipokea Tabaraniy kwa sanadi mbili.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 6 Uk. 292[483]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ummu Salamah, amesema kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa ndani ya nyumba yake, mara alikuja Fatimah na chungu kilichokuwa na chakula, akaingia nacho mpaka kwake, Mtume akamwambia: 'Niitie mumeo na watoto wako.' Akaja Ali, Hasan na Husain (as), wakaingia kwake na kuketi pamoja na wakaanza kula chakula hicho huku Mtume akiwa juu ya kitanda chake ambacho kilikuwa kimetandikwa kishamiya cha Khaibari. Nami nilikuwa ninaswali katika chumba kingine, ndipo Mwenyezi Mungu akateremsha Aya hii: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'** Mtume akachukua sehemu ya shuka iliyozidi (baada ya kutandika) akawafunika nayo, kisha akatoa mkono wake na kuunyoosha mbinguni na kusema: 'Ewe Mungu Wangu hawa ndio Ahlul-Baiti wangu na watu makhususi kwangu, waondolee uchafu na wasafishe barabara.' Nikaingiza kichwa changu katika chumba walichokuwemo na nikasema: Je na mimi niko pamoja nanyi ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?' Akasema: 'Hakika wewe uko katika kheri."'

**Nasema:** Ameipokea pia al-Wahidiy ndani ya *Asbabun-Nuzul,* uk. 267, na ameipokea at-Twahawi ndani ya *Mushkilul-Athar*, Juz. 1, kwa njia mbili, katika uk. 332 na katika uk. 334. Na ameitaja al-Muhibu Tabari ndani ya *Dhakhairu* yake uk. 23, na mwishoni mwake kuna: "Hakika mimi ni mwenye kumpiga

[482] *Musnad Ahmad bin Hanbal*: Hadith ya Wathilah bin al-Asqau, Hadithi ya 16540.
[483] *Musnad Ahmad bin Hanbal*: Hadith ya Ummu Salamah mke wa Mtume, Hadithi ya 25969.

vita yule mwenye kuwapigeni ninyi vita na ni mwenye kuishi na amani na yule mwenye kuishi na amani na ninyi, na ni mwenye uadui na yule mwenye uadui na ninyi." Na amesema: "Ameiandika Ibn al-Qababiy ndani ya *Mu'jamu* yake." Na ameitaja As-Suyutiy ndani ya *ad-Durul-Manthur* katika tafsiri ya Aya ya utakaso katika Sura Ahzab, na amesema: "Ameiandika Ibn Jarir na Ibn al-Mun'dhir na Ibn Abi Hatim na Tabaraniy na Ibn Mardawayhi kutoka kwa Ummu Salamah.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 6 Uk. 292[484]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Shahri bin Hawshab, amesema: "Nilimsikia Ummu Salamah mke wa Mtume (saww) –zilipofika habari za kifo cha Husain (as) – akiwalaani watu wa Iraki, alisema: 'Wamemuuwa kweli! Mwenyezi Mungu awauwe, wamemhadaa na kumtelekeza, Mwenyezi Mungu awalaani. Hakika mimi nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), siku hiyoFatimah alikuja kwake mchana akiwa kabeba chungu ambacho ndani mlikuwa na chakula alichopika, alikibeba chakula ndani ya mfuniko wa chungu na kukiweka mbele yake, Mtume akamwambia: 'Yuko wapi mtoto wa ami yako?' Akasema: 'Yuko nyumbani.' Akasema: 'Nenda kamwite na uniletee watoto wako.' Fatimah akaja huku akiwa kaongozana na watoto wake kamshika kila mmoja kwa mkono wake, huku Ali akiwa nyuma yao. Walipoingia kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliwakalisha Hasan na Husain mapajani mwake na Ali akaketi kuliani kwake huku Fatimah akiketi kushotoni kwake.'

"Ummu Salamah anasema: 'Mtume alivuta kishamiya cha Khaibari ambacho kilikuwa kimetandikwa juu ya kitanda chetu huko Madina akawafunika, akashikilia pande za kishamiya kwa mkono wake wa kushoto, na akanyoosha mkono wake wa kulia kwa Mola Wake na kusema: 'Ewe Mungu Wangu, hawa ndio Ahlul-Baiti wangu na watu makhususi kwangu, waondolee uchafu na wasafishe barabara. Ewe Mungu Wangu hawa ndio Ahlul-Baiti wangu na watu makhususi kwangu, waondolee uchafu na wasafishe barabara.' Nikasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, je mimi sio katika watu wako? Akasema: 'Ndio wewe ni katika watu wangu, ingia ndani ya kishamiya.' Nikaingia ndani ya kishamiya baada ya kuwa tayari ameshamaliza kumuombea dua binamu yake Ali, watoto wake na binti yake Fatimah (as).'"

**Nasema:** Na ameipokea Ibn Jarir Tabari ndani ya *Tafsiir* yake Juz. 22, uk. 6. Na ameipokea at-Twahawi ndani ya *Mushkilul-Athar*, Juz. 1, uk. 335. Na ameitaja al-Muhibu Tabari ndani ya *Dhakhairu* yake uk. 22.

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 4[485]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aamir bin Saad bin Abi Waqas, amesema: "Muawiya alimwamuru Saad na kumwambia: 'Kitu gani chakuzuia kumtukana Abu Turabi?' Akasema: 'Kamwe siwezi kumtukana kila ninapokumbuka mambo matatu aliyoyasema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), kwani mimi kuwa na moja kati ya hayo ni jambo ninalotamani sana kushinda hata farasi mwekundu. Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akimwambia: 'Hivi huridhii kuwa cheo chako kwangu mimi ni sawa na cheo cha Harun kwa Musa isipokuwa ni kuwa hakuna unabii baada yangu.' Hiyo ni baada ya Ali (as) kumwambia: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Je waniacha pamoja na wanawake na watoto?' Baada ya kumwacha katika moja ya vita vyake. Na nilimsikia akisema siku ya Khaibar: 'Nitampa bendera kesho mtu ambaye anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanampenda yeye.' Kila mmoja wetu akatamani hilo, Mtume

[484] *Musnad Ahmad bin Hanbal*: Hadith ya Ummu Salamah mke wa Mtume, Hadithi ya 26010.
[485] *Khasa'isun-Nasaiy*: Swala ya Amirul-Muuminina Ali bin Abi Talib (as), mlango wa ibada zake.

akasema: 'Niitieni Ali.' Akaja huku akiwa anaumwa macho, akamtemea mate machoni na kumkabidhi bendera. Na ilipoteremka:**'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'** Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwita Ali, Fatimah, Hasan na Husain na kusema: 'Ewe Mungu Wangu, hawa ndio watu wa nyumba yangu."'

**Taarikh Baghdad Juz. 10, uk. 287[486]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Said al-Khudriy kutoka kwa Mtukufu Mtume (saww) kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**Amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliwakusanya Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as) kisha akawafunika kishamiya na kusema: 'Ewe Mungu Wangu, hawa ndio watu wa nyumba yangu. Ewe Mungu Wangu waondolee uchafu na watakase barabara.' Wakati huo Ummu Salamah alikuwa mlangoni, akasema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Je mimi sio miongoni mwao?' Akasema: 'Hakika wewe uko katika kheri.'"

**Nasema:** Na ameipokea pia Ibn Jarir Tabari ndani ya *Tafsiir* yake Juz. 22, uk. 7 kutoka kwa Ummu Salamah.

**Tafsiri Ibn Jarir Tabari Juz. 22, uk. 5[487]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Said al-Khudriy, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Aya hii: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'** iliteremka kwa ajili ya watu watano: Kwa ajili yangu mimi, Ali, Hasan, Husain na Fatimah."

**Nasema:** Na pia kaitaja al-Muhibu Tabari ndani ya *Dhakhairu* yake uk. 24, na amesema: "Kaiandika Ahmad ndani ya *al-Manaqib*." Na ameiandika Tabaraniy na ameitaja al-Haythamiy ndani ya *Maj'mauz-Zawaid* Juz. 9, uk. 167 na amesema: "Ameipokea al-Bazzar." Kisha ameipokea kwa njia nyingine, amesema: "Kutoka kwa Abu Said al-Khudri, amesema: 'Ahlul-Baiti ni wale ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na kuwatakasa barabara.' Akahesabu idadi yao katika mkono wake, akasema ni watano: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as) –Aliendelea kueleza mpaka aliposema: Ameipokea Tabaraniy ndani ya *al-Awsat*, na ameitaja Ali bin Sultan ndani ya *Mirqat* yake Juz. 5, uk. 590 katika ufafanuzi."

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, uk. 188[488]:**

Amesema:"Ilipoteremka kauli ya Mwenyezi Mungu: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'** Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwita Ali, Fatimah, Hasan na Husain katika nyumba ya Ummu Salamah na kusema: 'Ewe Mungu Wangu, hawa ndio watu wa nyumba yangu, waondolee uchafu na watakase barabara."' – Amesema: Ameiandika al-Qal'iy.

**Al-Istiaab Juz. 2, uk. 598[489]:**

---

[486] *Taarikh Baghdad:* Wasifu wa Abdurahan bin Ali al-Maruziy 5396.
[487] *Tafsirut-Tabari*: Sura Ahzab, Aya ya 33, Hadithi ya 28478.
[488] *Ar-Riyadh an-Nadhrahh:* Fadhila za Ali bin Abu Talib.
[489] *Al-Istiaab:* Herufi Hau, Mlango wa Hilal bin Hamrau.

Kutoka kwa Abul-Hamrau amesema: "Niliishi Madina mwezi mzima, na kila asubuhi Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa anakwenda kwenye nyumba ya Fatimah na Ali (as) na kusema: 'Swala, Swala, **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**"

**Nasema:** Ameitaja Ibn al-Athir al-Jazriy ndani ya *Usudul-Ghabah* Juz. 5, uk. 66 na katika uk. 174.

**Tafsiri Ibn Jarir Tabari Juz. 22 Uk. 6[490]:**

Amepokea kwa njia mbili kutoka kwa Abul-Hamrau, amesema: "Niliishi Madina miezi saba zama za Mtukufu Mtume (saww). Nilimuona Mtukufu Mtume (saww) kila alfajiri ilipochomoza akienda kwenye mlango wa Ali na Fatimah na kusema: 'Swala, Swala, **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**"

**Musnad Abi Daud at-Twayalasiy Juz. 8, uk. 274[491]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Mtukufu Mtume (saww) kuwa alikuwa akipita katika mlango wa Fatimah (as) muda wa mwezi mzima kila siku kabla ya Swala ya Subhi na kusema: "Swala enyi watu wa nyumba ya Mtume. **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**"

**Kanzul-Ummal Juz. 7, uk. 92[492]:**

Amesema: Nilikwenda kwa Fatimah kumuulizia Ali (as), akasema: "Ameelekea kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)." Nikaketi nikimsubiri, mpaka alipokuja Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa pamoja na Ali, Hasan na Husain (as) huku akiwa kamshika mkono kila mmoja kati ya hao wawili. Alipoingia aliwasogeza karibu Ali na Fatimah na kuwakalisha mbele yake, na akamkalisha Hasan na Husain kila mmoja juu ya paja lake, kisha aliwafunika nguo yake na kusoma Aya hii: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'** Na akasema: 'Ewe Mungu Wangu hawa ndio watu wa nyumba yangu, na watu wa nyumba yangu ndio wenye haki zaidi.' Nikasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, je na mimi ni miongoni mwa watu wa nyumba yako? Akasema: 'Ndio wewe ni katika watu wa nyumba yangu.'" - Amesema: Ameiandika Ibn Abi Shaiba na Ibn Asakir.

**Usudul-Ghabah Juz. 2, uk. 20[493]:**

Amesema: Amepokea al-Awzaiy kutoka kwa Shadad bin Abdullah, amesema: Wakati kilipoletwa kichwa cha Husain (as) baada ya mtu mmoja kutoka Sham kuwataja vibaya Husein na baba yake (as), Wathilah bin Asqau alisimama na nikamsikia akisema: "Wallahi nitaendelea kumpenda Ali, Hasan, Husain na Fatimah (as) baada ya kumsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema kuhusu wao yale aliyosema. Niliona siku moja pindi nilipokwenda kwa Mtukufu Mtume (saww) katika nyumba ya Ummu Salamah, mara alikuja Hasan (as) na kumkalisha juu ya paja lake la kulia na kumbusu, kisha alikuja Husain (as) akamkalisha juu ya paja lake la kushoto na kumbusu, kisha alikuja Fatimah akamkalisha mbele yake, kisha alimwita Ali (as) kisha akasema: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi**

[490] *Tafsirut-Tabari:* Sura Ahzab, Aya ya 33, Hadithi ya 28491.
[491] *Musnad Abi Daud*: Ali bin Zayd bin Jad'an kutoka kwa Anas, Hadithi ya 2059.
[492] *Kanzul-Ummal*: Herufi Waw, Wathilah bin Asqau, Hadithi ya 37543.
[493] *Usudul-Ghabah*: Wasifu wa Imam Husain bin Ali (as), Hadithi ya 1173.

**Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'"** Nikamwambia Wathilah: Nini makusudio ya uchafu? Akasema: "Shaka kuhusu Mwenyezi Mungu."

**Usudul-Ghabah Juz. 3, uk. 413[494]:**

Amesema: Ameipokea al-Ismailiy katika *as-Swahabah*. Na ameipokea kwa njia yake kutoka kwa Umair Abi Arfajah kutoka kwa Atwiyah, amesema: "Mtukufu Mtume (saww) aliingia kwa Fatimah (as) akamkuta akitengeneza chakula, alikaa mpaka alipoleta chakula. Wakati huo alikuwepo Hasan na Husain, Mtukufu Mtume (saww) akasema: 'Kaniitieni Ali.' Alipokuja walikula pamoja, kisha akachukua shuka walilokuwa wamekalia akawafunika kwalo, kisha akasema: 'Ewe Mungu Wangu hawa ndio watu wa nyumba yangu, waondolee uchafu na watakase barabara.' Nikamsikia Ummu Salamah akisema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, je na mimi niko pamoja nao?' Akasema: 'Hakika wewe uko katika kheri."'

**Nasema:** Ameitaja Ibn Hajar ndani ya *Al-Isabah* yake Juz. 4, uk. 247.

**Mushkilul-Athar Juz. 1, uk. 332[495]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ummu Salamah kuwa alisema: "Aya hii: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'** iliteremka kwa ajili yangu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as)."

**Mushkilul-Athar Juz. 1, uk. 333[496]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ummu Salamah, amesema: "Aya hii: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'** Iliteremkia ndani ya nyumba yangu wakiwa watu saba: Jibril, Mikail, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as). Na hakusema: 'Hakika wewe ni miongoni mwa watu wa nyumba yangu."'

**Mushkilul-Athar Juz. 1, uk. 332[497]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aamir bin Saad kutoka kwa baba yake, amesema: "Ilipoteremka Aya hii, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwita Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as), na kusema: 'Ewe Mungu Wangu, hawa ndio watu wa nyumba yangu."'

**Nasema:** Na ameipokea Ibn Jarir Tabari ndani ya *Tafsiir* yake Juz. 22, uk. 7.

**Mushkilul-Athar Juz. 1, uk. 336[498]:**

---

494 *Usudul-Ghabah*: Mlango wa Ain na Twau, Wasifu wa Atwiyah, Hadithi ya 3691.

495 *Mushkilul-Athar*: Kubainisha mushkilu wa yale yaliyopokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kuhusu muradi wa kauli ya Mwenyezi Mungu: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**

496 *Mushkilul-Athar*: Kubainisha mushkilu wa yale yaliyopokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kuhusu muradi wa kauli ya Mwenyezi Mungu: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**

497 *Mushkilul-Athar*: Kubainisha mushkilu wa yale yaliyopokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kuhusu muradi wa kauli ya Mwenyezi Mungu: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**

498 *Mushkilul-Athar*: Kubainisha mushkilu wa yale yaliyopokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kuhusu muradi wa kauli ya Mwenyezi Mungu: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Umratul-Hamdaniyah, amesema: "Nilikwenda kwa Ummu Salamah kumsalimu, akasema: 'Wewe ni nani?' Nikasema mimi ni Umratul-Hamdaniyah. Nikamwambia ewe Mama wa Waumini nieleze kuhusu mtu huyu aliyeuwawa baina ya migongo yetu ni mtu anayepasa kupendwa au kuchukiwa? –Anamkusudia Ali bin Abu Talib (as). – Ummu Salamah akasema: 'Je unampenda au unamchukia?' Nikamwambia simpendi wala simchukii, Akasema:……Mwenyezi Mungu akateremsha Aya hii: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'** Wakati huo chumbani hakukuwa na mtu zaidi ya Jibril, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as). Nikasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Je mimi ni miongoni mwa watu wa nyumba yako? Akasema: 'Hakika wewe una kheri mbele ya Mwenyezi Mungu.' Kwakweli nilitamani aseme ndiyo, hilo ni jambo nililokuwa nalipenda zaidi kuliko vyote vilivyochomozewa na jua na kuzamiwa na jua."'

**Mushkilul-Athar Juz. 1, uk. 338[499]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abul-Hamrau, amesema: "Nilisuhubiana na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwa muda wa miezi tisa. Alikuwa kila inapoingia asubuhi huenda kwenye mlango wa Fatimah (as) na kusema: 'Amani iwe juu yenu enyi watu wa nyumba ya Mtume, **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**"

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9, uk. 169[500]:**

Amesema: Kutoka kwa Abu Said al-Khudriy amesema kwamba Mtukufu Mtume (saww) alikwenda kwenye mlango wa Ali (as) siku arobaini kila asubuhi baada ya Ali kumuoa Fatimah (as), na alikuwa akisema: "Amani iwe juu yenu enyi watu wa nyumba ya Mtume, pia rehema zake na baraka zake. **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'"**

— Amesema: Ameipokea Tabaraniy ndani ya al-Awsat.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9, uk. 121[501]:**

Amesema: Kutoka kwa Abul-Hamrau, amesema: "Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akija kwenye mlango wa Ali na Fatimah (as) kila siku muda wa miezi sita, na kusema: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'"** – Amesema: Ameipokea Tabaraniy.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9, uk. 169[502]:**

Amesema: Kutoka kwa Abu Barzah, amesema: "Niliswali pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) miezi kumi na saba. Alikuwa kila anapotoka nyumbani kwake huenda moja kwa moja kwenye nyumba ya Fatimah (as) na kusema: 'Swala iwe juu yenu. **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'"** – Amesema: Ameipokea Tabaraniy.

[499] *Mushkilul-Athar*: Kubainisha mushkilu wa yale yaliyopokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kuhusu muradi wa kauli ya Mwenyezi Mungu: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**

[500] *Majmauz-Zawa'id*: Kitabu cha fadhila, Mlango unaohusu fadhila za Ahlul-Baiti (as).

[501] *Majmauz-Zawa'id*: Kitabu cha fadhila, Mlango unaohusu fadhila za Ahlul-Baiti (as).

[502] *Majmauz-Zawa'id*: Kitabu cha fadhila, Mlango unaohusu fadhila za Ahlul-Baiti (as).

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9, uk. 206[503]:**

Amesema: Kutoka kwa Anas, amesema: "Hakika Umar bin al-Khattab alikwenda kwa Abu Bakr na kumuuliza: 'Ewe Abu Bakr, kitu gani kinakuzuia usimuoe Fatimah binti ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)?' Akasema: 'Hawezi kunioza.' –Ameendelea kusimulia habari za Ali (as) kumuoa Fatimah (as) mpaka aliposema: Mtume akasema: 'Ewe Ummu Ayman niletee bilauri ya maji. Nikamletea bilauri kubwa ikiwa na maji, alikunywa kidogo kisha akatemea humo mate kisha akampa Fatimah, naye akanywa, kisha akachukua maji hayo kidogo na kumpiga nayo Fatimah katika mbavu, baina ya mabega yake na katika kifua chake, kisha alimpa bilauri ya maji Ali (as) na kumwambia kunywa. Baada ya kunywa alichukua maji kidogo na kumpiga nayo katika mbavu zake na baina ya mabega yake, kisha akasema: 'Hawa ni watu wa nyumba yangu, waondolee uchafu na watakase barabara."'

— Amesema: Ameipokea al-Bazzar.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9 Uk. 206[504]:**

Amesema: Kutoka kwa Ibn Abbas amesema: "Fatimah (as) alikuwa akiombwa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (akiombwa kuolewa), na hakuna aliyeomba isipokuwa Mtume alimzuia, mpaka watu wakakata tamaa ya kumpata. Ndipo siku moja Sa'ad bin Muadh akakutana na Ali (as) –Ameendelea kusimulia habari za Ali (as) kumuoa Fatimah (as) mpaka aliposema: Mtume akasema: 'Ewe Asmau, niletee beseni la maji.' Asmau alipoleta beseni Mtukufu Mtume (saww) alitemea mate ndani ya maji na kisha akapaka uso wake na nyayo zake, kisha alimwita Fatimah (as) akachukua ukufi wa waji na kumpiga nayo kichwani. Akachukua ukufi wa pili na kumpiga nayo katika matiti yake, kisha alinyunyuzia maji kwenye busati la ngozi na kisha akalitandika na kumkalisha Fatimah hapo. Kisha akasema: 'Ewe Mungu Wangu, hakika yeye ni sehemu yangu na mimi ni sehemu yake. Ewe Mungu Wangu kama ulivyoniondolea uchafu na kunitakasa basi watakase na wao wawili.' Kisha aliomba maji mengine kisha akamwita Ali (as) na kumfanyia kama alivyomfanyia Fatimah, kisha akamuombea kama alivyomuombea Fatimah (as), kisha akawaambia: 'Simameni na muende nyumbani kwenu, Mwenyezi Mungu awaweke pamoja katika siri yenu na awanyooshee mambo yenu."'

— Amesema: Ameipokea Tabaraniy.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9, uk. 146[505]:**

Amesema: Kutoka kwa Abu Tufayl, amesema: "Siku moja Hasan bin Ali bin Abu Talib (as) alitutolea hotuba. Alimhimidi Mwenyezi Mungu na kumsifu –Ameendelea kusimulia mpaka aliposema: Kisha akasema: 'Mimi ni mtoto wa mbashiri, mimi ni mtoto wa mwonyaji, mimi ni mtoto wa Nabii, mimi ni mtoto wa mwenye kulingania kwa Mwenyezi Mungu kwa idhini Yake, mimi ni mtoto wa taa itoayo nuru, mimi ni mtoto wa yule aliyetumwa kuja kuwa rehema kwa walimwengu wote, na mimi ni miongoni mwa watu wa nyumba ya Mtume ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na kuwatakasa barabara."'

Amesema: Ameipokea Tabaraniy ndani ya *al-Awsat* na kwa muhtasari ndani ya *al-Kabir*. Na ameipokea Abu Ya'ala kwa muhtasari na pia al-Bazzar.

[503] *Majmauz-Zawa'id*: Kitabu cha fadhila, Mlango unaohusu fadhila za Fatimah (as) na kuolewa kwake na Ali (as).
[504] *Majmauz-Zawa'id:* Kitabu cha fadhila, Mlango unaohusu fadhila za Fatimah (as) na kuolewa kwake na Ali (as).
[505] *Majmauz-Zawa'id:* Kitabu cha fadhila, Mlango wa hotuba ya Hasan bin Ali (as).

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9, uk. 173[506]:**

Amesema: Kutoka kwa Abu Jamilah, amesema: "Hasan bin Ali (as) alichukua Ukhalifa baada ya kuuwawa Ali (as). Siku moja akiwa anawaswalisha watu, mara alijitokeza mtu mmoja akamrukia Hasan (as) na kuanza kumchoma kwa jambia katika paja lake. Basi akawa ameugua miezi kadhaa kutokana na tukio hilo, kisha alisimama siku moja na kuhutubia juu ya mimbari, akasema: 'Enyi watu wa Iraki, mcheni Mwenyezi Mungu kuhusu sisi, hakika sisi ni viongozi wenu na wageni wenu, na sisi ni watu wa nyumba ya Mtume, watu ambao Mwenyezi Mungu amewazungumzia kwa kusema: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**' Aliendelea kuzungumza siku hiyo kiasi kwamba hakuonekana mtu msikitini isipokuwa alikuwa ni mwenye kulia."

— Amesema: Ameipokea Tabaraniy na wapokezi wake ni watu waaminifu.

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 3, uk. 172[507]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ali bin Husain (as), aesema: "Siku moja Hasan bin Ali (as) aliwahutubia watu baada ya kuuwawa Ali (as). Alimhimidi Mwenyezi Mungu na kumsifu, –Ameendelea kusimulia mpaka aliposema: Kisha akasema: 'Enyi watu! Mwenye kunitambua ananitambua, na asiyenitambua basi ajue mimi ni Mtoto wa Nabii, na mimi ni mtoto wa Wasii, mimi ni mtoto wa mbashiri, mimi ni mtoto wa mwonyaji, mimi ni mtoto wa mwenye kulingania kwa Mwenyezi Mungu kwa idhini Yake, mimi ni mtoto wa taa itoayo nuru, mimi ni mtoto wa watu wa nyumba ambayo Jibril alikuwa akiteremka kwetu na kupanda kutokea kwetu, na mimi ni miongoni mwa watu wa nyumba ya Mtume ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na kuwatakasa barabara."'

**Tafsiri Ibn Jarir Tabari Juz. 22, uk. 7[508]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abud-Daylami, amesema: Ali bin Husain (as) alimwambia mtu mmoja wa Sham: "Hivi hujasoma katika Sura Ahzab: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**?" Mtu yule akasema: "Hivi hao ni ninyi?" Akasema: "Ndiyo."

**Nasema:** Hakika watu wa mtu ni familia yake na ndugu zake, na neno 'Aali' na 'Ahli' yote yana maana moja, kwani katika Kiarabu neno Aali asili yake ni Ahli. Vyovyote iwavyo ni kwamba watu wa nyumba ya mtu licha ya kwamba kilugha ni familia yake na ndugu zake, lakini pia linaweza kutumika neno hilo kumaanisha yeyote yule anayeishi ndani ya nyumba yake, sawa awe huyo anayeishi ni ndugu yake au ni mke wake au mtu baki kabisa. Lakini muradi wa Watu wa Nyumba katika Aya hii tukufu si wengine bali ni watu makhususi ambao ni Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as) na si kila ndugu yake Mtume, achilia mbali wake zake na watu baki. Hiyo ni kwa kuwa Mtukufu Mtume (saww) aliwafunika kishamiya na kuwaashiria kwa tamko makhususi, akasema: "Ewe Mungu Wangu hawa ndio watu wa nyumba yangu, waondolee uchafu na watakase barabara."

Na katika baadhi ya hadithi kuna tamko la wazi linaloelekeza kuwa hakika Aya hii iliteremka kwa ajili ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as). Na katika baadhi ya ya hadithi kuna tamko la wazi kuwa iliteremka kuwahusu watu saba: Jibril, Mikail, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as), na licha ya kwamba katika baadhi ya hadithi

[506] *Majmauz-Zawa'id*: Kitabu cha fadhila, Mlango unaohusu fadhila za Ahlul-Baiti (as).
[507] *Mustadrakus-Sahihayn:* Kitabu cha kuwatambua Masahaba, Hotuba ya Imam Hasan (as) baada ya kuuwawa Imam Ali (as).
[508] *Tafsirut-Tabari*: Sura Ahzab, Aya ya 33, Hadithi ya 28500.

kuna kauli ya Ummu Salamah: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Je mimi sio katika watu wa nyumba yako?’ Akasema: ‘Ndio wewe ni katika watu wa nyumba yangu.’” Au kama ilivyo kauli ya Wathilah: “Je na mimi ni miongoni mwa watu wa nyumba yako?” Akasema: “Ndio na wewe ni miongoni mwa watu wa nyumba yangu.” Lakini hizo:

**Kwanza:** Hazizishindi riwaya nyingine zenye kukanusha hilo, kwani zenyewe idadi yake ni kubwa, sanadi yake ni imara zaidi na madhumuni yake ni mashuhuri zaidi.

**Pili:** Hakika katika habari nyingi za Ummu Salamah utakuta Mtukufu Mtume (saww), alimwambia: “Hakika wewe upo katika kheri.” Au “Wewe una sehemu yako,” au “Akaninyang’anya kishamiya toka mikononi mwangu,” kama ilivyotangulia katika mlango usemao kuwa Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as), ndio Aali Muhammad. Hili nalo linakanusha Ummu Salamah achilia mbali wake wengine wa Mtume, kuwa miongoni mwa watu ambao Aya ya utakaso inawahusu, Aya ambayo iliteremkia nyumbani kwake.

**Tatu:** Hakika Ummu Salamah kama alivyosema katika baadhi ya habari hizo: “Je mimi sio katika watu wa nyumba yako. Akasema: ‘Ndiyo wewe ni katika watu wa nyumba yangu.’” Amesema pia: “Nikaingia ndani ya kishamiya baada ya kuwa tayari ameshamaliza kumuombea binamu yake, watoto wake na binti yake Fatimah (as).” Hili nalo laonesha kuwa Aya hii tukufu haimhusu Ummu Salamah na wala hajumuishwi na hukmu yake, yaani utakaso na kuondolewa uchafu, kama ambavyo linavyoonesha kuwa hata Wathilah naye haimhusu, kwani hakika kauli ya Mtume (saww) kwake: “Ndio na wewe ni miongoni mwa watu wa nyumba yangu.” Ilikuwa ni baada ya kumaliza kumuombea binamu yake, watoto wake na binti yake Fatimah (as).

**Nne:** Hakika tuna dalili nyingine ukiachia mbali hadithi zilizotangulia, ambayo inaonesha kuwa Ummu Salamah na wake wote wa Mtume achilia mbali Wathilah, wote Aya hii tukufu haiwahusu, na kila hadithi yenye neno ‘Watu wa Nyumba ya Mtume.’ Haiwahusu pia. Dalili hiyo ni kauli ya Zayd bin Arqam iliyopokewa ndani ya *Sahih Muslim* katika kitabu cha fadhila za Masahaba, katika mlango wa fadhila za Ali bin Abu Talib (as), amesema humo: “Husayni akamwambia – yaani kumwambia Zayd: ‘Watu wa nyumba yake ni akina nani? Kwani wakeze sio watu wa nyumba yake?’ Akasema: ‘Wake zake ni miongoni mwa watu wa nyumba yake, lakini watu wa nyumba yake (waliokusudiwa katika Aya hii) ni wale ambao wameharamishiwa sadaka baada yake.’ Akasema: ‘Na ni akina nani hao?’ Akasema: ‘Ni Aali Ali, Aali Aqil, Aali Ja’far na Aali Abbas.’ Akasema: ‘Hawa wote wameharamishiwa sadaka?’ Akasema: ‘Ndio.’”

Na katika riwaya nyingine iliyo bayana kuliko hiyo, nayo kaipokea Muslim ndani ya *Sahih* yake katika mlango uliotajwa, amesema humo: “Tukasema –kumwambia Zayd: Je wakeze ni miongoni mwa watu wa nyumba yake? Akasema: ‘Wallahi hapana. Hakika mwanamke huishi na mwanaume muda kadhaa wa maisha yake, kisha hutalikiwa na kurejea kwa jamaa zake. Watu wa nyumba yake (waliokusudiwa katika Aya hii) ni wale ambao ni asili yake na jamaa zake ambao wameharamishiwa sadaka baada yake.’”

Baada ya yote haya hakika madai ya kwamba wakeze wanaingia chini ya Aya hii tukufu na kwamba wao ni miongoni mwa walioondolewa uchafu na kutakaswa barabara, ni madai batili sana na yasiyofaa kusikilizwa.

# MLANGO UNAOSEMA KUWA MTUKUFU MTUME (SAWW) ALIAPIZANA KUPITIA ALI, FATIMAH, HASAN NA HUSAIN (AS)

**Sahih Muslim: Kitabu cha fadhila za Masahaba, Mlango unaozungumzia sehemu ya fadhila za Ali bin Abu Talib (as)[509]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aamir bin Saad bin Abi Waqas, kutoka kwa baba yake, amesema: "Muawiya alimwamuru Saad na kumwambia: 'Kitu gani chakuzuia kumtukana Abu Turabi?' Akasema: 'Kamwe siwezi kumtukana kila ninapokumbuka mambo matatu aliyoyasema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuhusu yeye, kwani mimi kuwa na moja kati ya hayo ni jambo ninalotamani sana kushinda hata farasi mwekundu. Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akimwambia: 'Hivi huridhii kuwa cheo chako kwangu mimi ni sawa na cheo cha Harun kwa Musa isipokuwa ni kuwa hakuna unabii baada yangu.' Hiyo ni baada ya Ali (as) kumwambia: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Je waniacha pamoja na wanawake na watoto?' Baada ya kumwacha katika moja ya vita vyake. Na nilimsikia akisema siku ya Khaibar: 'Nitampa bendera kesho mtu ambaye anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanampenda yeye.' Kila mmoja wetu akatamani hilo. Mtume akasema: 'Niitieni Ali.' Akaja huku akiwa anaumwa macho, akamtemea mate machoni na kumkabidhi bendera na Mwenyezi Mungu akaleta ushindi mikononi mwake. Na ilipoteremka:**'Watakao kuhoji katika haya baada ya kukufikilia ilimu hii waambie: Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wanawake zetu na wanawake zenu, na sisi wenyewe na nyinyi wenyewe, kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo.'** Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwita Ali, Fatimah, Hasan na Husain na kusema: 'Ewe Mungu Wangu, hawa ndio watu wa nyumba yangu."'

**Nasema:** Ameipokea pia Tirmidhiy ndani ya *Sahih* yake Juz. 2, uk.300, na ameipokea Ahmad bin Hanbal ndani ya *Musnad* yake Juz. 1, uk. 185, na ameitaja As-Suyutiy ndani ya *ad-Durul-Manthur* katika tafsiri yake ya Aya ya maapizano katika Sura Aali Imrani, na amesema: "Kaiandika Ibn al-Mun'dhir na al-Hakim na al-Bayhaqiy ndani ya *Sunan* yake kutoka kwa Saad bin Abi Waqas.

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, uk. 166[510]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aamir bin Saad bin Abi Waqas kutoka kwa baba yake, amesema: "Mwenyezi Mungu alipoteremsha Aya hii: **'Watakao kuhoji katika haya baada ya kukufikilia ilimu hii waambie: Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wanawake zetu na wanawake zenu, na sisi wenyewe na nyinyi wenyewe, kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo.'** Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwita Ali, Fatimah, Hasan na Husain na kusema: 'Ewe Mungu wangu, hawa ndio watu wa nyumba yangu."'

**Nasema:** Na ameipokea pia al-Hakim ndani ya *Mustadrakus-Sahihayn*, Juz. 3, uk. 150, na amesema: "Hadithi hii ni sahihi kwa mujibu wa masharti ya masheikh wawili. Na ameipokea al-Bayhaqiy ndani ya *Sunan* yake Juz. 7, uk. 63.

**Tafsirul-Kashaf ya Zaakhshari na Tafsirul-Kabir ya Razi: Mwishoni mwa tafsiri ya Aya ya maapizano katika Sura Aali Imran, na Nurul-Absar ya Shablanjiy, Uk. 100:**

---

509 *Sahih Muslim*: Kitabu cha fadhila za Masahaba, Fadhila za Ali bin Abu Talib (as).

510 *Sahih Tirmidhiy*: Kitabu cha tafsiri ya Qur'ani, Mlango wa 4, Sura Aali Imran, Hadithi ya 2999.

Maelezo haya ni kwa lafudhi ya huyu wa mwisho – yaani Shablanji:

Amesema: Wafasiri wamesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipousomea ujumbe wa Najran Aya hii na kuwaita kwenye Uislamu, walisema: 'Tutarudi kwako kesho tuache twende tukatafakari jambo letu." Walipoachana walimwambia Aqib – ambaye alikuwa kiongozi wao na mkubwa wao: 'Unaonaje ewe mja wa Masihi?' Akasema: 'Bila shaka mmeshajua enyi Wakristo kwamba hakika Muhammad ni Nabii aliyetumwa, na kama mtafanya hivyo basi mtahiliki.' Na katika riwaya nyingine: Aliwaambia: 'Wallahi katu hakuna watu walioapizana na Nabii isipokuwa waliangamia wote, hivyo mkikataa isipokuwa kubakia katika kauli mnayosema kuhusu mtu wenu (kuwa Yesu ni Mungu), basi muageni mtu huyu na muende nchini kwenu.'

"Wakaja kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), naye alikuwa ametoka huku akiwa kamkumbatia Husain (as), kamshika mkono Hasan (as) na Fatimah (as) akitembea nyumba yao, na Ali akiwa nyuma ya Fatimah (as), huku Nabii (saww) akiwaambia: 'Nitakapoomba ninyi muitikie.' Askofu wa Najran alipowaona alisema: 'Enyi Wakristo! Hakika mimi naziona nyuso ambazo kama zitamuomba Mwenyezi Mungu kuondoa mlima toka sehemu yake basi atauondoa. Msiapizane mtakuja kuangamia na hatabakia mkiristo yeyote juu ya ardhi mpaka Siku ya Kiyama.' Wakasema: 'Ewe Abul-Qasim tumeona kuwa tusiapizane na wewe, tukuache katika dini yako na wewe utuache katika dini yetu.' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawaambia: 'Kama hamtaki kuapizana basi silimuni mtapata haki ya kutendewa yale wanayotendewa Waislamu naya kutokutendewa yale wasiyotendewa Waislamu.'

"Lakini waliendelea kukataa, ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawaambia: 'Basi nitakupigeni vita.' Wakasema: 'Hatuna nguvu ya kupigana na Waarabu, lakini sisi tunafanya sulhu na wewe kwa sharti kwamba usituvamie kijeshi, usitutie hofu na wala usituzuie dhidi ya dini yetu, nasi tutakupa kila mwaka nguo elfu mbili, elfu moja katika mwezi wa Safar na elfu moja nyingine katika mwezi wa Rajab." Amesema: Na katika riwaya nyingine ameongeza: 'Na deraya za kawaida thelathini na tatu, ngamia thelathini na tatu na farasi wa kivita thelathini na wanne.'

"Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akafanya nao sulhu kwa masharti hayo, na akasema: 'Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu imo mikononi Mwake, hakika adhabu ilikaribia kuwapata watu wa Najran, na laiti wangeapizana nami basi wangegeuzwa nyani na nguruwe, na bonde lao lingewaka moto, na Mwenyezi Mungu angewamaliza wote mpaka ndege aliye mtini. Usingeisha mwaka isipokuwa tayari Wakristo wote wangekuwa wameangamia.'" – Amesema: Ameiandika al-Khazin na wengineo.

**Nasema:** Baada ya kunukuu kisa hiki Zamakhshari amesema: "Ukisema: 'Kuwataka kwake waje kuapizana ilikuwa ni ili ajulikane ni nani mkadhibishaji na ni nani mpinzani wake, na hilo ni jambo linalomhusu yeye binafsi na yule aliyemkadhibisha, hivyo ina maana gani kuwajumuisha watoto na wanawake?' Nitasema: Hiyo ni dalili ya nguvu inayojulisha jinsi alivyokuwa akiamini hali yake na alivyokuwa na yakini na ukweli wake, kiasi kwamba alithubutu kuwatoa vipenzi vyake na nyama ya ini lake, watu awapendao zaidi kuliko mwingine yeyote. Na alikuwa anaamini kuwa wapinzani wake ni waongo lakini hata hivyo hakukomea tu kujitoa yeye mwenyewe bali ni ili waangamie kabisa wapinzani wake pamoja na vipenzi vyao kama maapizano yatatimu. Na alichagua watoto na wake kwa sababu ndio wapendwa zaidi wa mtu na ndio walio moyoni zaidi, na kuna wakati mtu hujitoa badala yao na hupigana vita hadi kuuawa badala yao. Zaidi ya hapo ni kwamba walikuwa wakienda na wapendwa wao vitani ili wawazuie kukimbia, na wale wenye kuwahami kwa roho zao huitwa walinzi wa kweli. Na ameanza kuwataja kabla ya nafsi ili kuonesha thamani ya nafasi yao na ukaribu wa cheo chao, na ili atangaze kuwa wao hutangulizwa kabla ya nafsi, na nafsi hujitoa fidia kwa ajili yao."

Na Amesema: "Na humo mna dalili juu ya ubora wa watu wa kishamiya, na mna burhani bayana juu ya kusihi unabii wa Mtukufu Mtume (saww), kwasababu hakuna hata mmoja miongoni mwa waungaji hadi wapingaji aliyepokea kuwa wao waliitikia ombi hilo (kuja kuapizana)."

Baada ya kunukuu kisa hiki, Fakhru Razi amesema: "Aya hii yajulisha kuwa Hasan na Husain (as) walikuwa watoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), aliahidi kuwaita watoto wake na akawaita Hasan na Husain (as), hivyo inalazimika wawe watoto wake."

Amesema: "Na linalotilia nguvu kauli hii ni kauli ya Mwenyezi Mungu katika Sura An'am: **Na tukamtunukia (Ibrahim) Is'haq na Yaakub. Kila mmoja wao tulimwongoa. Na Nuhu tulimwongoa kabla. Na katika kizazi chake tulimwongoa Daud na Suleiman na Ayyub na Yusuf na Musa na Harun. Na hivi ndivyo tunavyowalipa wafanyao wema. Na Zakaria na Yahya na Isa na Ilyas. Wote walikuwa miongoni mwa watu wema.** Inajulikana wazi kuwa Isa (as) amenasibishwa na Ibrahim (as) kupitia mama yake na si baba, na hapo imethibiti kuwa mtoto wa binti anaweza kuitwa mtoto wa fulani."

Amesema pia katika tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: **'Na tukamtunukia (Ibrahim) Is'haq na Yaakub. Kila mmoja wao tulimwongoa. Na Nuhu tulimwongoa kabla. Na katika kizazi chake tulimwongoa Daud na Suleiman na Ayyub na Yusuf na Musa na Harun. Na hivi ndivyo tunavyowalipa wafanyao wema. Na Zakaria na Yahya na Isa na Ilyas. Wote walikuwa miongoni mwa watu wema.'**: "Aya inajulisha kwamba Hasan na Husain (as) ni dhuria wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), kwasababu Mwenyezi Mungu amemuweka Isa (as) katika dhuria wa Ibrahim (as) licha ya kwamba hanasibiki na Ibrahim (as) isipokuwa kwa kupitia mama. Kadhalika Hasan na Husain (as) ni dhuria wa Mtume wa Mwenyezi Mungu hata kama wananasibika na Mtume wa Mwenyezi Mungu kupitia mama, na hapo imewajibika wawe dhuria wake.

Amesema: "Inasemekana kuwa: Abu Ja'far al-Baqir (as) alitoa Aya hii kama hoja dhidi ya al-Hajjaj bin Yusuf."Na kabla ya maelezo haya katika tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: **'Na akamfundisha Adam majina yote.'** Katika Sura al-Baqarah, amesema hivi: Kutoka kwa as-Shaabiy, amesema: "Nilikuwa kwa al-Hajjaj na mara akaletwa Yahya bin Ya'mur mwanafiqhi wa Khurasan akiwa kafungwa vyuma, al-Hajjaj akamwambia: 'Wewe umedai kuwa Hasan na Husain ni dhuria wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)?' Akasema ndiyo, al-Hajjaj akasema: 'Niletee hoja bayana kutoka ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu la sivyo nitakukatakata kiungo kimoja baada ya kingine.' Akasema: 'Nitakuletea hoja bayana kutoka ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu ewe Hajjaj.' Kwakweli nilishangaa ujasiri wake wa kusema: Ewe Hajjaj. Akamwambia: 'Usiniletee Aya hii: **Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu**..'

"Akasema: 'Nitakuletea hoja bayana kutoka ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu, nayo ni kauli ya Mwenyezi Mungu: **Na tukamtunukia (Ibrahim) Is'haq na Yaakub. Kila mmoja wao tulimwongoa. Na Nuhu tulimwongoa kabla. Na katika kizazi chake tulimwongoa Daud na Suleiman na Ayyub na Yusuf na Musa na Harun. Na hivi ndivyo tunavyowalipa wafanyao wema. Na Zakaria na Yahya na Isa na Ilyas. Wote walikuwa miongoni mwa watu wema.** Ni nani aliyekuwa baba wa Isa (as), na mbona ameunganishwa na dhuria wa Nuhu? Hajjaj akainamisha kichwa chini kidogo kisha akanyanyua kichwa chake na kusema: 'Kana kwamba sijawahi kusoma Aya hii kutoka katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu, mwacheni huru na mpeni kiasi kadha wa kadha cha mali.'"

**Nasema:** Kisa hiki kakitaja pia Yahya bin Ya'mar as-Suyutiy ndani ya *ad-Durul-Manthur* mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: **'Na tukamtunukia (Ibrahim) Is'haq na Yaakub. Kila mmoja wao tulimwongoa. Na Nuhu tulimwongoa kabla. Na katika kizazi chake tulimwongoa Daud na Suleiman na Ayyub na Yusuf na Musa na Harun. Na hivi ndivyo tunavyowalipa wafanyao wema.'** Katika Sura An'am, amekitaja kwa njia mbili, moja ni kutoka kwa Ibn Abi Hatim kutoka kwa Abi Harbi

bin Abil-As'wad. Na nyingine ni kutoka kwa Abul-Shaikh na al-Hakim na al-Bayhaqiy, kutoka kwa Abdul-Malik bin Umair.

**Tafsiri Ibn Jarir Tabari Juz. 3, uk. 212[511]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Zayd bin Ali (as) kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: **'Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wake zetu na wake zenu, na sisi wenyewe na nyinyi wenyewe, kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo.'** Amesema: "Walikuwa Mtukufu Mtume (saww), Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as)."

**Tafsiri Ibn Jarir Tabari Juz. 3, uk. 212[512]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa as-Sadiy: **'Watakao kuhoji katika haya baada ya kukufikilia ilimu hii waambie: Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wake zetu na wake zenu, na sisi wenyewe na nyinyi wenyewe, kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo.'**Amesema: "Alimshika mkono Hasan na Husain na Fatimah (as) na kumwambia Ali (as) tufuate. Akatoka pamoja nao na siku hiyo hakuna mkiristo aliyetoka, wakasema: 'Hakika sisi tunahofia asije huyu akawa ndiye Nabii, na maombi ya Nabii si sawa na ya mtu mwingine.' hivyo siku hiyo hawakutokea, Mtukufu Mtume (saww) akasema: 'Laiti wangetokea basi wangeungua.'"

**Tafsiri Ibn Jarir Tabari Juz. 3, uk. 213[513]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ulabai bin Ahmar al-Yashkiriy, amesema: "Ilipoteremka Aya hii: **'Watakao kuhoji katika haya baada ya kukufikilia ilimu hii waambie: Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wake zetu na wake zenu, na sisi wenyewe na nyinyi wenyewe, kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo.'** Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwita Ali, Fatimah na watoto wao Hasan na Husain (as), na akawaita Mayahudi ili aapizane nao. Akasema kijana mmoja wa Kiyahudi: 'Ole wenu si aliwaahidini jana kuwa mtakuwa kama ndugu zenu ambao waligeuzwa nyani na nguruwe? Msiapizane naye.' Wakaacha.'"

**Tafsiri Ibn Jarir Tabari Juz. 3 Uk. 213[514]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Zayd, amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliambiwa: "Kama ungeapizana na jamaa ungekuja na nani uliposema: Watoto wetu na watoto wenu?" Akasema: "Hasan na Husain."

**Ad-Durul-Manthur ya As-Suyutiy: Katika tafsiri ya Aya ya maapizano katika Sura Aali Imran:**

Amesema: Ameiandika al-Hakim na kusema kuwa ni hadithi sahihi, na ameiandika Ibn Mardawayhi na Abu Na'im ndani ya *ad-Dalail*, wote wameiandika kutoka kwa Jabir amesema: "Aqib na Sayyid walikwenda kwaMtukufu Mtume (saww), alipowaita katika Uislamu walisema: 'Tumesilimu ewe Muhammad.' Akawaambia: 'Mmeongopa, lakini mkitaka nitawaelezeni ni kitu gani kinawazuia kuukubali Uislamu.' Wakasema haya tueleze, akasema (saww): 'Ni kupenda kwenu msalaba, kunywa pombe na kula nyama ya nguruwe.'"

511 *Tafsirut-Tabari*: Sura Ahzab, Aya ya 63, Hadithi ya 7178
512 *Tafsirut-Tabari*: Sura Ahzab, Aya ya 63, Hadithi ya 7179
513 *Tafsirut-Tabari*: Sura Ahzab, Aya ya 63, Hadithi ya 7186.
514 *Tafsirut-Tabari:* Sura Ahzab, Aya ya 63, Hadithi ya 7186.

Jabir anasema: "Akawaomba waweze kuapizana, nao wakamuahidi kesho yake. Ilipofika kesho, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikwenda akiwa kawashika mkono Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as), kisha akawatumia mjumbe akawaite, lakini walikataa kuja, Mtume akasema: 'Naapa kwa yule ambaye amenituma kwa haki, lau kama wangefanya (wangeingia katika maapizano) basi bonde hili lingenyeshewa na mvua ya moto.'"

Jabir anasema: "Ni kwao iliteremka: **'Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wake zetu na wake zenu, na sisi wenyewe na nyinyi wenyewe, kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo.'Sisi wenyewe** ni Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na Ali (as.). **Watoto wetu** ni Hasan na Husain (as). **Wake zetu** ni Fatimah (as)."

Na pia amesema: Ameandika Abu Na'im ndani ya *ad-Dalail* kwa njia ya al-Kalbiy, kutoka kwa Abu Salih kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Ujumbe wa Wakristo wa Najran ulifika kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), wakiwa ni viongozi wao kumi na nne – ameendelea kusimulia kisa mpaka aliposema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawaambia: 'Hakika Mwenyezi Mungu ameniamuru kuwa iwapo hamtakubali haya basi niapizane nanyi.' Wakasema: 'Ewe Abul-Qasim kwanza tunakwenda kutafakari jambo letu kisha tutakuja - ameendelea kusimulia kisa mpaka aliposema: Na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa ametoka akiwa pamoja na Ali, Hasan, Husain na Fatimah (as). Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Mimi nikiomba ninyi muwe mnaitikia.' Ndipo wakakataa kuombeana laana naye, na wakaamua kufanya sulhu kwa kukubali kulipa kodi."

**Asbabun-Nuzul ya al-Wahidiy Uk. 75[515]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir bin Abdullah, amesema: "Ujumbe wa watu wa Najran ulifika kwa Mtukufu Mtume (saww), walikuwa ni Aqib na Sayyid. Akawaita katika Uislamu, wakasema: 'Tulishasilimu kabla yako.' Akawaambia: 'Mmeongopa, lakini mkitaka nitawaelezeni ni kitu gani kinawazuia kuukubali Uislamu.' Wakasema haya tueleze, akasema (saww): 'Ni kupenda kwenu msalaba, kunywa pombe na kula nyama ya nguruwe.' Akawaomba waweze kuapizana, nao wakamuahidi kesho asubuhi. Ilipofika kesho yake, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikwenda akiwa katika mkono mmoja kawashika Ali na Fatimah, na mkono mwingine Hasan na Husain (as), kisha akawatumia mjumbe akawaite, lakini walikataa kuja na wakakubali kulipa kodi; Mtume akasema: 'Naapa kwa yule ambaye amenituma kwa haki, lau kama wangefanya (wangeingia katika maapizano) basi bonde hili lingenyeshewa na mvua ya moto.'"

Al-Wahidiy anasema: Jabir amesema: "Ni kwao iliteremka: **'Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wake zetu na wake zenu, na sisi wenyewe na nyinyi wenyewe, kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo.'**" Na as-Shaabiy amesema: "**Watoto wetu** ni Hasan na Husain (as). **Wake zetu** ni Fatimah (as). **Sisi wenyewe** ni Ali (as.)."

**Nasema:** Na amepokea tena kisa hicho kama kilivyo katika uk. 74 kwa njia yake kutoka kwa Hasan, na ninadhani ni Hasan al-Basriy.

**As-Sawa'iqul-MuhriqahUk. 93[516]:**

Amesema: Ameandika ad-Daru Qut'niy kwamba Ali (as) alitoa hoja siku ya Shura dhidi ya wanashura, akawaambia: "Nawaapizeni Mwenyezi Mungu, je yupo yeyote miongoni mwenu zaidi yangu mimi aliye

---

[515] *Asbabun-Nuzul*: SUR Imran, kauli ya Mwenyezi Mungu: **'Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wake zetu na wake zenu, na sisi wenyewe na nyinyi wenyewe, kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo.'**

[516] *As-Sawa'iqul-Muhriqah*, Faslu ya kwanza, Aya zilizopokewa kuhusu wao, Aya ya tisa.

karibu zaidi na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika udugu kuliko mimi, na ambaye alimfanya nafsi yake, na kuwafanya watoto wake kuwa watoto wake yeye (saww), na wake zake kuwa wake zake yeye (saww)?" Wakasema: "Wallahi hakuna."

## MLANGO UNAOSEMA KUWA MTUKUFU MTUME (SAWW) ALIMWAMBIA ALI, FATIMAH, HASAN NA HUSAIN (AS): MIMI NI MWENYE KUMPIGA VITA YULE MWENYE KUWAPIGENI VITA NA NI MWENYE KUISHI KWA USALAMA NA YULE MWENYE KUISHI KWA USALAMA NA NINYI:

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, uk. 319[517]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Swabihi mfanyakazi wa Ummu Salamah, kutoka kwa Zayd bin Arqam, amesema: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as):"Mimi ni mwenye kumpiga vita yule mwenye kuwapigeni vita na ni mwenye kuishi kwa usalama na yule mwenye kuishi kwa usalama na ninyi."

**Nasema:** Na ameipokea pia Ibn Majah ndani ya *Sahih* yake uk. 14, na amesema: "Mimi ni mwenye kuishi kwa usalama na yule mwenye kuishi kwa usalama nanyi, na ni mwenye kumpiga vita yule mwenye kuwapigeni vita ninyi." Na ameipokea al-Hakim ndani ya *Mustadrakus-Sahihayn* Juz. 3, uk. 149, na ameipokea Ibn al-Athir al-Jazriy ndani ya *Usudul-Ghabah* Juz. 5, uk. 523, na ameitaja al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 6, uk. 216, kwa kunukuu kutoka kwa Ibn Haban toka ndani ya *Sahih* yake, na katika Juz. 7, uk. 102 kwa kunukuu kutoka kwa Ibn Abi Shayba, Tirmidhiy, Ibn Majah, Ibn Haban, Tabaraniy na ad-Dhiyau al-Muqadasiy. Na ameitaja al-Muhibu Tabari ndani ya *Dhakhairu* yake uk. 25, na amesema: "Ameiandika Abu Hatim na kusema: 'Mimi ni mwenye kumpiga vita yule mwenye kuwapigeni vita na ni mwenye kuishi kwa usalama na yule mwenye kuishi kwa usalama na ninyi.'"

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 2, uk. 442[518]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira amesema: "Mtukufu Mtume (saww) alimtazama Ali, Hasan, Husain na Fatimah (as) na kusema: 'Mimi ni mwenye kumpiga vita yule mwenye kuwapigeni vita na ni mwenye kuishi kwa usalama na yule mwenye kuishi kwa usalama na ninyi."'

**Nasema:** Ameipokea al-Hakim ndani ya *Mustadrakus-Sahihayn*uk. 149, kisha akasema: "Hadithi hii ni nzuri." Na ameipokea al-Khatib al-Baghdadiy ndani ya *Taarikh* yake Juz. 7, uk. 136. Na ameitaja al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 6, uk. 216 kwa kunukuu kutoka kwa Tabaraniy.

**Usudul-Ghabah Juz. 3, uk. 11[519]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Swabih mfanyakazi wa Ummu Salamah, amesema: "Nilikuwa mlangoni kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na mara alikuja Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as) na kuketi pembeni, akatoka Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kusema: 'Hakika ninyi mko katika kheri.' Alikuwa kajifunika kishamiya cha Khaibari, akawafunika na wao, kisha akasema: 'Mimi ni

[517] *Sunan Tirmidhiy:* Kitabu cha fadhila, Mlango wa 61, Fadhila za Fatimah binti Muhammad, Hadithi ya 3780.
[518] *Musnad Ahmad bin Hanbal:* Musnad Abi Huraira, Hadithi ya 9405.
[519] *Usudul-Ghabah*: Mlango wa Swad na Bau na Khau, Wasifu wa Swabih mfanyakazi wa Ummu Salama, 2479.

mwenye kumpiga vita yule mwenye kuwapigeni vita na ni mwenye kuishi kwa usalama na yule mwenye kuishi kwa usalama na ninyi."'

**Nasema:** Na pia kaitaja al-Haythamiy ndani ya *Majmauz-Zawa'id* Juz. 9, uk. 169, na amesema: "Ameipokea Tabaraniy ndani ya *al-Awsat*."

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, uk. 199[520]:**

Amesema: Kutoka kwa Abu Bakr, amesema: "Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa ameweka hema huku akiwa ameegemea upinde wa kiarabu, na ndani ya hema hilo mlikuwa na Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as), akasema: 'Enyi Waislamu, Mimi ni mwenye kuishi kwa usalama na yule mwenye kuishi kwa usalama na wale waliyomo ndani ya hema, na ni mwenye kumpiga vita yule mwenye kuwapiga vita wao, na ni mwenye kumpenda mwenye kuwapenda wao. Hawapendi wao isipokuwa mwema, mtoto wa ndoa, na wala hawachukii wao isipokuwa muovu, mtoto wa nje ya ndoa."'

**Dhakhairul-Uqba Uk. 23[521]:**

Amesema: "Imepokewa kutoka kwake –yaani Ummu Salamah - amesema: "Mtukufu Mtume (saww) alikuwa kwetu huku akiwa kainamisha kichwa chake, Fatimah akamtengenezea chakula na kuja nacho huku akiwa pamoja na Hasan na Husain (as), Mtume akamwambia Fatimah: 'Yuko wapi mumeo? Nenda kamuite.' Alipokuja naye walikula pamoja kisha Mtume akachukua kishamiya na kuwafunika. Akashikilia kishamiya kwa mkono wake wa kushoto na kuinua mkono wake wa kulia mbinguni, na akasema: 'Ewe Mungu Wangu hawa ndio watu wa nyumba yangu, wandani wangu na watu makhususi kwangu. Ewe Mungu Wangu waondolee uchafu na watakase barabara. Mimi ni mwenye kumpiga vita yule mwenye kuwapiga wao vita na ni mwenye kuishi kwa usalama na yule mwenye kuishi nao kwa usalama, na ni adui wa yule mwenye kuwafanyia uadui."'

— Amesema: Ameiandika al-Qababiy ndani ya *Majmau* yake.

**Ad-Durul-Manthur ya As-Suyutiy: Katika tafsiri ya Aya ya utakaso katika Sura Ahzab:**

Amesema: Ameiandika Ibn Mardaayhi kutoka kwa Abu Said al-Khidriy, amesema: "Ali (as) alipomuoa Fatimah (as), Mtukufu Mtume (saww) alikwenda kwenye mlango wa Fatimah muda wa siku arobaini kila siku asubuhi na kusema: "Amani iwe juu yenu enyi watu wa nyumba ya Mtume, na pia rehema Zake na baraka Zake. Swala!Mwenyezi Mungu akurehemuni. **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'** Mimi ni mwenye kumpiga vita yule mnayempiga vita na ni mwenye kuishi kwa usalama na yule mnayeishi naye kwa usalama."'

[520] *Ar-Riyadh an-Nadhrah*: Mlango wa nne katika fadhila za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib. Kutaja khususia zake na watoto wake, na kwamba Mtume aliwaambia: 'Mimi ni mwenye kumpiga vita yule mwenye kuwapigeni vita na ni mwenye kuishi kwa usalama na yule mwenye kuishi kwa usalama na ninyi.

[521] *Dhakhairul-Uqbah*: Mlango wa fadhila za Ahlul-Baiti, Kubainisha kuwa Fatimah, Ali, Hasan na Husain (as) ndio Ahlul-Baiti waliokusudiwa na kauli ya Mwenyezi Mungu: **'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara.'**

### MLANGO UNAOSEMA: ATAKAYEMPENDA MTUKUFU MTUME (SAWW), ALI, FATIMAH, HASAN NA HUSAIN (AS) ATAKUWA PAMOJA NA MTUKUFU MTUME KATIKA DARAJA LAKE

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2 Uk. 301[522]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ali bin Abu Talib (as) kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliwashika Hasan na Husain (as) mkono na kusema: "Yeyote atakayenipenda na kuwapenda hawa wawili, baba yao na mama yao, atakuwa pamoja na mimi katika daraja yangu Siku ya Kiyama."

**Nasema:** Na ameipokea Abdullah bin Ahmad bin Hanbal ndani ya *Musnad* ya baba yake Juz. 1, uk. 77, na ameipokea al-Khatib ndani ya *Taarikh* yake Juz. 3, uk. 187, na ameitaja Ibn Hajar al-Asqalaniy ndani ya *Tahdhibut-Tahdhib* Juz. 10, uk. 430, na amesema: "Amesema Abu Ali bin as-Swawaf kutoka kwa Abdullah bin Ahmad: 'Nasru bin Ali aliposimulia hadithi, Mutawakil aliamuru apigwe mijeledi elfu moja, ndipo Ja'far bin Abdul-Wahid akazungumza naye na akawa anamwambia: Huyu ni miongoni mwa watu wa sunna. Aliendelea kuongea naye mpaka akamwacha."'

Na ameitaja al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 6, uk. 217, na amesema: "Ameiandika Tabaraniy kutoka kwa Ali (as)." Na katika Juz. 7, uk. 102 amesema: "Ameiandika Tirmidhiy na Abdullah bin Ahmad bin Hanbal ndani ya *Ziyadatil-Musnad*, na Nidhamul-Mulki ndani ya *Amali* yake, na Ibn an-Najar na Said bin Mansuri.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 217[523]:**

Lafudhi yake ni: Alisema: "Yeyote atakayewapenda hawa atakuwa amenipenda mimi, na yeyote atakayewachukia hawa atakuwa amenichukia mimi, yaani Hasan, Husain, Fatimah na Ali (as). - Amesema: Kaiandika Ibn Asakir kutoka kwa Zayd bin Arqam.

## MLANG0 UNAOELEZA KUWA SURA AD-DAHRI ILITEREMSHWA KWA HAKI YA ALI, FATIMAH, HASAN NA HUSAIN (AS)

**Usudul-Ghabah cha Ibn Athir al-Jazriy, Juz. 5, Uk. 530,[524] Wasifu wa Bi Fidhah an-Nawbiyah:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Mujahid, naye amepokea kutoka kwa Ibn Abbas, amesema kuhusu kauli yaMwenyezi Mungu: **"Wanatimiza ahadi, na wanaiogopa siku ambayo shari yake inaenea sana. Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa."** Amesema: "Imam Hasan na Husain (as) walikuwa wagonjwa, babu yao Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliwatembelea na akawaahidi atawaletea kijakazi wa kiarabu. Kisha Imam Ali (as) akapewa ushauri ya kuwa: 'Ewe Abal-Hasan laiti ungeweka nadhiri kwa ajili ya watoto wako.' Imam Ali (as) akasema: 'Ikiwa watapona ugonjwa walionao nitafunga siku tatu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kama shukurani yangu Kwake.'Naye Fatimah (as) akasema hivyo hivyo, pia kijakazi wao aliyeitwa Fidhahan-Nawbiyah akasema: 'Ikiwa mabwana zangu hawa watapona nitafunga kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kama shukurani

[522] *Sunan Tirmidhiy*: Kitabu cha fadhila, Mlango wa 21, Hadithi ya 3733.
[523] *Kanzul-Ummal*: Mlango wa tano katika fadhila za Ahlul-Baiti, fadhila ya kwanza katika fadhila zao, Hadithi ya 34194.
[524] *Usudul-Ghabah*: Herufi Fau: Wasifu wa Fidhah at-Tawbiyah, 7202.

yangu Kwake.' Mara wakapona hawa vijana, na wakati huo Aali Muhammad hawakuwa na kitu si kichache wala kingi.

"Ndipo Ali (as) alipokwenda kwa Sham'un Khaybariy na akamkopa pishi tatu za shairi na kumletea Fatimah (as) naye akasaga na kuoka mikate. Baada ya Ali (as) na Mtume wa Mwenyezi Mungu kumaliza kuswali, Ali (as) alirejea nyumbani kwake na mara kikawekwa chakula mbele yake, mara wakajiwa na masikini akiwa amesimama mlangoni na kusema: 'Assalaam Alaykum enyi watu wa nyumba ya Muhammad, mimi ni masikini katika watoto wa Kiislam, nilisheni Mwenyezi Mungu atawalisha chakula katika meza za peponi. Hapo Ali (as) akamsikia na akawaamrisha ahli zake wakampelekea chakula, na wao wakashinda siku nzima na kulala wakiwa hawajaonja chochote zaidi ya maji. Na ilipowadia siku ya pili Fatimah (as) alisaga tena ile shairi na akatengeneza mkate, baada ya Ali (as) na Mtume wa Mwenyezi Mungu kumaliza kuswali, Ali (as) alirejea nyumbani kwake na mara kikawekwa chakula mbele yake, mara wakajiwa na yatima akiwa amesimama mlangoni na kusema: 'Assalaam Alaykum enyi watu wa nyumba ya Muhammad, yatima ambaye baba yake amekufa shahid yupo mlangoni, nilisheni.' Wakampa chakula yule yatima na wakabaki siku mbili bila kuonja chochote zaidi ya maji. Na ilipowadia siku ya tatu Fatimah (as) alisaga tena ile pishi ya shairi iliyobakia na akatengeneza mkate, baada ya Ali (as) na Mtume wa Mwenyezi Mungu kumaliza kuswali, Ali (as) alirejea nyumbani kwake na mara kikawekwa chakula mbele yake, mara wakajiwa na mfungwa, alisimama mlangoni na kusema: 'Assalaam Alaykum enyi watu wa nyumba ya unabii! Hivi kweli tunatekwa na kufungwa na wala hatupewi chakula, nilisheni kwani mimi ni mfungwa.' Wakampa chakula na kubaki siku tatu mchana na usiku bila kuonja chochote zaidi ya maji.

"Baadaye Mtume aliwatembelea na kuiona hali waliyonayo kutokana na njaa, na ndipo Mwenyezi Mungu akateremsha:**"Hakika kilimpitia binaadamu kipindi katika zama ambacho kwamba hakuwa kitu kinacho tajwa. –** mpaka **– Hakika sisi tunakulisheni kwa wajihi wa Mwenyezi Mungu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani."**

— KishaAmesema: Ameiandika Abu Mussa.

**Nasema:** Ameitaja pia Zamakhshariy ndani ya *al-Kashaf* katika tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: **"Na atawajazi Bustani za Peponi na maguo ya hariri kwa vile walivyosubiri."** Katika Sura ad-Dahri. Na ameeleza pia kuwa al-Wahidiy naye kaitaja. Na ameitaja pia Fakhri Raziy katika tafsiri yake *Tafsirul-Kabiir*, amesema:"al-Wahidiy ni katika wafuasi wetu." - akimaanisha ni katika Maashaira. -Ametaja ndani ya kitabu *Al-Basit* kwamba aya hizi ziliteremshwa kwa haki ya Ali (as), amesema:"Mwandishi wa*Tafsiir Al-Kashaf*kakitaja kisa hiki, kapokea kutoka kwa Ibn Abbas, na hapo kaitaja riwaya iliyotangulia.

**Asbabun-Nuzul cha al-Wahidiy Uk. 331: Katika kueleza sababu ya kuteremka kauli yaMwenyezi Mungu: "Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa:"**

Amesema: Amesema Atau kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Ni kwamba Ali (as) aliajiriwa na mtu ili afanye kazi ya kumwagilia mtende kwa malipo ya shairi, na ilipotimia usiku na kulipwa, alichukua theluthi ya ile shairi na kuisaga, akatengeneza chakula kinachoitwa harira, na kilipoiva alikuja masikini nao wakamtolea kile chakula {wao wakabaki na njaa}, kisha siku ya pili wakatengeneza theluthi ya pili na kilipoiva mara akaja yatima akiomba, wakampa kile chakula, na wao wakabaki tena na njaa, siku ya tatu akatengeneza theluthi ya tatu iliyobakia, kilipoiva tu mara akaja mfungwa katika mushirikina akiomba, wakampa, wakalala na njaa tena siku ile, ndipo ikateremshwa hii Aya.

**Nasema:** Na vilevile Tabari amekitaja kisa hiki katika *Riyadh an-Nadhirah*Juz. 2, uk.227, humo ameeleza: "Harira hufahamika kama mkate usiokuwa na mafuta." Na akasema:"Hii ni kauli nzuri." Na

pia kasema Qatadah:“Hakika yule mfungwa alikuwa miongoni mwa mushrikina.” Na amesema Said bin Jubair:“Mfungwa alikuwa miongoni mwa Waislam.”Na ameitaja riwaya hii katika *Dhakhairu*yake uk. 102.

**Ad-Durul-Manthur cha as-Suyutiy, Mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: “Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa:”**

Amesema: Ameandika Ibn Mardaway kutoka kwa Ibn Abbas kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu:**“Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa.”** Amesema: Iliteremkakumhusu Ali binAbu Talib (as) na Fatimahbinti ya wa Mtume waMwenyezi Mungu (as).

**Nurul-Abswar cha as-Shablanjiy Uk. 102:**

Amesema: Na katika maelezo ya Shaykhul-Akbar ni kwamba Abdullah bin Abbas amesema kuhusu kauli yaMwenyezi Mungu:**“Wanatimiza ahadi, na wanaiogopa siku ambayo shari yake inaenea sana:”** “Hasan na Husain wakati wakiwa wadogo walipatwa na maradhi, babu yao Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliwatembelea akiwa amefuatana na Abubakr na Umar, ndipo Umar alipomwambia Ali (as): ‘Ewe Abal-Hasan, laiti ungeweka nadhiri juu ya watoto wako hakika Mwenyezi Mungu atawaponyesha.’ Ali (as) akasema: ‘Nitafunga siku tatu kumshukuru Mwenyezi Mungu.’Fatimah (as) akasema:‘Nami nitafunga siku tatu kumshukuru Mwewnyezi Mungu.’Na watoto wakasema:‘Nasi tutafunga sikutatu.’ Naye kijakazi wao Fidhah akasema: Nitafunga siku tatu.’ Mwenyezi Mungu akawaponyesha na wakaamkia kwenye Swaumu wakiwa hawana chakula. Ndipo Ali alipokwenda kwa jirani yake Myahudi aliyeitwa Sham’un, alikuwa akitengeneza sufi, akamwambia: ‘Je, una chochote cha kunipa katika upande wa sufi ili binti ya Muhammad aweze kukufumia kwa malipo ya pishi tatu za shairi?” Akasema ndio, akampa na akajana zile pishi tatu za shairi na sufi. Alipomueleza Fatimah (as) alikubali na akafuma theluthi ya sufi ile. Akachukua pishi moja ya shairi na kuisaga kisha akatengeneza vipande vitano vya mikate kwa kila mtu kipande kimoja.

“Baada ya Ali (as) kuswali pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu Swala ya Maghrib alirudi nyumbani kwake, alipowekewa chakula na kabla ya kumega tonge la kwanza alifika masikini na kusimama mlangoni, akasema:‘Assalaam Alaykum enyi watu wa nyumba ya Muhammad. Mimi ni masikini wa Kiislam, nilisheni kile mnachokula, Mwenyezi Mungu atakulisheni kutoka katika meza za peponi.’ Ali akatoa tonge mkononi mwake na kumpa yule masikini, kisha akasema: ‘Fatimah mwenye utukufu na yakini! Ewe binti ya aliye mbora kushinda watu wote! Hivi humuoni masikini asiye na kitu, amekuja mlangoni yu mwenye huzuni. Kila mtu ana dhamana kwa kile alichokichuma.’

“Wakati huo huo Fatima akasema: ‘Amri yako ewe mtoto wa ami yangu ni yenye kusikilizwa na kutiiwa, sina la kulaumu wala kukhofu, kwa unyenyekevu wa hali ya juu nimetoa chakula, nataraji kupata radhi kwa kumlisha mwenye njaa, ili niungane na jamaa wema na niingie peponi kwa shifaa.’”

Ibnu Anasema: “Fatimah alichukua kilichokuwa katika sahani na kumpelekea yule masikini, wakalala hali wana njaa na wakaamka wakiwa wenye Swaumu huku wakiwa hawajaonja chochote isipokuwa maji matupu. Kisha alichukua theluthi ya pili ya sufi iliyobaki akaifuma. Kisha alichukua pishi na kuanza kusaga na kutengeneza vipande vitano vya mikate, kila mmoja kipande kimoja. Baada ya Ali (as) kuswali pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu Swala ya Maghrib alirudi nyumbani kwake, alipowekewa chakula na kabla ya kumega tonge la kwanza alifika yatima na kusimama mlangoni, akasema: ‘Assalaam Alaykum enyi watu wa nyumba ya Muhammad. Mimi ni yatima wa Kiislam nilisheni kile mnachokula na Mwenyezi Mungu atakulisheni katika meza za peponi.’ Ali akatoa tonge mkononi mwake na kumpa yule

masikini, kisha akasema: ‘ “Ewe Fatima binti ya Bwana wa wakarimu! Hakika Mwenyezi Mungu ametuletea huyu yatima. Ni nani leo anahitaji radhi ya Rahim? Ahadi yake ni malipo ya pepo yenye neema.’

“Fatimah (as) akajibu kwa kusema: ‘Nitampa wala sitojali, nitamtanguliza Mwenyezi Mungu kabla ya watoto wangu, japo wameshinda na njaa kama mimi, bila shaka mdogo wao atauwawa katika vita.’Kisha alitoa kilichokuwa kwenye sahani na kumpa yule yatima na wakalala na njaa bila kuonja chochote zaidi ya maji matupu, na wakaamka asubuhi hali ya kuwa wamefunga. Kisha alichukua theluthi ya tatu ya sufi iliyobaki akaifuma, kisha alichukua pishi na kuanza kusaga na kutengeneza vipande vitano vya mikate, kila mmoja kipande kimoja. Baada ya Ali (as) kuswali pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu Swala ya Maghrib alirudi nyumbani kwake, alipowekewa chakula na kabla ya kumega tonge la kwanza alifika mfungwa miongoni mwa wafungwa wa Kiislamu na kusimama mlangoni, akasema: ‘Assalaam Alaykum enyi watu wa nyumba ya Muhammad!Hakika makafiri wametuteka, wakatufunga na kututesa wala hawakutupa chakula.’ Ali akatoa lile tonge mkononi mwake na kusema: ‘Eh Fatima binti ya Mtume anayesifiwa, bintiya Mtume Bwana wa heshima. Huyu hapa mfungwa amekuja na hana muongozo, Amefungwa na shingoni mwake pana mnyororo, anatushitakia njaa na mateso. Atakayemlisha leo, kesho (Siku ya Kiyama) atakipata, mbele ya Mtukufu Mmoja wa pekee, kwani kila anachopanda mlimaji (leo) kesho atakivuna.’

“Fatimah (as) akajibu kwa kusema: ‘Haijabaki hata pishi moja uliyoleta, nimekwisha hakiki kwa kutoa. Ewe Mwenyezi Mungu hawa watoto wangu wako kwenye njaa muda wa siku tatu. Ewe Mola Wangu nakuomba usiwahilikishe kwa njaa.’Kisha alitoa kile chakula kilichokuwa kwenye sahani na kumpa yule mfungwa na wakabaki hawana chochote, ndipo Ali na wanawe Hasan na Husain (as) wakaelekea kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) huku watoto wakiwa wamesinyaa kama vifaranga kwa njaa. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipowaona alisema: ‘Ewe Abal-Hasan kinachoniumiza mimi ni yale yaliyokukuteni, haya twendeni kwa binti yangu Fatimah.’ Wakaelekea kwake, walimkuta kwenye mihrab huku tumbo lake likiwa limegusana na mgongo wake, huku macho yake yameingia ndani kwa mateso ya njaa. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipomuona tu alimkumbatia na kusema: ‘Ewe mwenye msaada.’ Basi akateremka Jibril (as) na kusema: ‘Ewe Muhammad, ikirimu familia ya nyumba yako.’ Mtume akamuuliza: ‘Kwa kitu gani ewe Jibril?’ Akasema:**”Hakika kilimpitia binadamu kipindi katika zama ambacho kwamba hakuwa kitu kinacho tajwa, –** mpaka **- Hakika sisi tunakulisheni kwa wajihi wa Mwenyezi Mungu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani.”**

## MLANGO UNAOELEZA KUWA AYA YA MAWADAH IMETEREMSHWA KWA AJILI YA KARABA WA MTUKUFU MTUME (SAWW), NAO NI ALI, FATIMAH, HASAN NA HUSAIN (AS)

Ama kuhusu kuteremka aya ya mawadah, nayo ni kauli yaMwenyezi Mungu Mtukufu katika Sura Ash-Shura: **“Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa karaba,”**kwa ajili yaKaraba waMtume (saww), kuna mapokezi mengi, sisi tunataja sehemu tu ya habari hizokwa haraka haraka, tunasema:

**Tafsir Ibn Jalili Tabari Juz. 25, uk. 16[525]:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Said Ibn Jubair kuhusu kauli yake:**“Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa karaba.”** Amesema: “Ni Karaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).”

**Nasema:** Ameitaja al-Muhibu Tabari katika *Dhakhair* yake, na amesema: “Kaiandika Ibn Sariy.”

[525] *Tafsirut-Tabari:* Sura Shura, Aya ya 33, Hadithi ya 30679.

**Tafsir Ibn Jalili Tabari Juz. 25, uk. 17:**

Amepokea kwa njia yake kutoka Abi Is'haqa amesema: "Nilimuuliza Umrah bin Shua'ib kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu:**"Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa karaba."** Akasema: 'Ni Karaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).'"

**Hilyatul-Awliyai Juz. 3, uk. 201:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir, amesema: "Siku moja alikuja bedui mmoja kwa Mtume (saww) akasema: 'Ewe Muhammad nitangazie Uislamu.'Mtume akamwambia: 'Shuhudia kuwa hakuna mungu isipokuwa Allah pekee, hana mshirika, na hakika Muhammad ni mja na Mtume Wake.' Bedui akauliza: 'Je kwa maelezo haya unahitaji kwangu malipo yoyote?' Mtume akajibu: 'Hapana ila mapenzi kwa karaba.' Bedui akauliza: 'Je nikaraba zangu au zako?' Mtume akajibu: 'Karaba zangu.'Yule bedui akamwambia Mtume:'Basi njoo nikupe kiapo cha utii. Laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu ya yule ambaye hakupendi na wala hawapendi karaba zako basi.'Mtume akaitikia: Amiin."

**ad-Durul-Manthur cha As-Suyutiy katikatafsiri ya kauli yaMwenyezi Mungukatika Sura ash-Shuraa:"Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa karaba."**

Amesema: Ameandika Abdu Ibn Hamid na Ibn Mundhir, wote wameandika kutoka kwa Mujahid kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: **"Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa karaba."** Amesema: "Ikiwa mnanifuata na kuniamini basi ungeni udugu wangu."

Na akasema tena: Ameandika Ibn Mardaway kupitia kwa Ibn Mubaraka kutoka kwa Ibn Abbas kuhusu kauli Yake: **"Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa karaba."** Amesema: "Nilindeni kupitiakaraba zangu."

Na akasema tena: Ameandika Ibn Na'im na ad-Daylamiy kutoka kwa Mujahid kutoka kwa Ibn Abbas, amesema:"Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): **"Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa karaba."** Ni mnilinde mimi kupitia watu wa nyumba yangu na muwapende kwa ajili yangu."

Na akasema tena: Ameandika Said bin Mansur kutoka kwa Said bin Jubair, amesema kuhusu: **"Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa karaba."** Ni karaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

**Mustadrakus-SahihayniJuz. 3, uk. 172:**

Amepokea kwa sanadi yake kutoka kwa Ali bin Husain (as), amesema: "Hasan bin Ali (as) aliwahutubia watu wakati alipouawa Ali (as). Akamhimidi na kumshukuru Mwenyezi Mungu –Aliendelea kusimulia mpaka aliposema: Kisha akasema: 'Enyi watu! Mwenye kunitambua ananitambua, na asiyenitambua basi ajue mimi ni Mtoto wa Nabii na mimi ni mtoto wa Wasii, mimi ni mtoto wa mbashiri, mimi ni mtoto wa mwonyaji, mimi ni mtoto wa mwenye kulingania kwa Mwenyezi Mungu kwa idhini Yake, mimi ni mtoto wa taa itoayo nuru, mimi ni mtoto wa watu wa nyumba ambayo Jibril alikuwa akiteremka kwetu na kupanda kutokea kwetu, na mimi ni miongoni mwa watu wa nyumba ya Mtume ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na kuwatakasa barabara. Na mimi ni katika watu wa Nyumba ya Mtume ambao Mwenyezi Mungu amewajibisha kwa kila Mwislamu kuwapenda, na amesema Yeye aliyetakasika kumwambia Mtume Wake: **"Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa karaba."** Na

anayefanya wema tutamzidishia wema, basi tambueni kuwa kuzidisha wema ni kutupenda sisi watu wa Nyumba ya Mtume."'

**Nasema:** Na pia ameitaja hadithi hii al-Muhibu Tabari katika kitabu chake*Dhakhair*uk. 138, na amesema: "Kutoka kwa Zayd bin Hasan." Kisha akasema: "Ameiandika ad-Dawlaby." Na ameitaja al-Haythamiy katika *Majmau* yake Juz. 9, uk. 146 na amesema: "Imepokewa kutoka kwa Abi Tufayl."Kisha akasema: "Ameipokea Tabaraniy, Abu Ya'ala, al-Bazar na Ahmad."Na pia Ibn Hajar ameitaja katika *as-Sawa'iq* yakeuk. 101, amesema: "Ameiandikaal-Bazar na Tabarani.

**Usudul-Ghabah Juz. 5, uk. 367:**

Amesema: Amepokea Hakim bin Jubair kutoka kwa Habib bin Abi Thabit, amesema: "Nilikuwa nimekaa pamoja na wazee wa Kiansari, mara alipita mbele yetu Ali bin Husain (as), hapo kabla palikuwa palishatokea mabishano kati yake na watu miongoni mwa makuraishi kuhusu mwanamke mmoja aliyeolewa na mmoja wao lakini mume yule hakuridhika na ndoa ya mke huyo, wakasema wazee wa Kiansari: 'Wewe sio uliyetuita jana wakati palitokea mabishano kati yako na watu wa kabila fulani? Wazee wetu wametueleza kwamba siku moja walikwenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na wakamuuliza: Ewe Muhammad hatulazimiki sisi kukupa wewe katika vile ambavyo Mwenyezi Mungu ametujalia kupata katika majumba na mali zetu, kwa kuwa tumetukuzwa na kuheshimiwa kwa ajili yako?hapo ndipo Mwenyezi Mungu alipoteremsha: **"Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa karaba."** Na sisi tunakutambulisheni kwa watu.'" - Kisha mwandishi akasema: "Ameiandika Ibn Mundah.

**Dhakhairul-UqbahUk. 25:**

Amesema: Na imepokewa ya kwamba Mtume (saww) amesema: "Mwenyezi Mungu ameweka malipo yenu kwangu kuwa ni ninyi kuwapenda watu wa nyumba yangu, na mimi nitakuulizeni kesho kuhusu wao." - Amesema: Ameiandika Mula katika kitabu chake cha *sirah*.

**As-Sawa'iqul-MuhriqahUk. 101:**

Amesema: Na amepokea Abu Shaykh na wengine kutoka kwa Ali kuwa alisema: "Kwetu sisi Aali Haa Miim kuna aya inayoelezea kuwa haheshimu mapenzi yetu isipokuwa aliye muumini." Kisha akasoma **"Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa karaba."**

**Nasema:** Pia ameitaja al-Mutaqiy katika *Kanzul-Umal*Juz. 1, uk. 218.

**As-Sawa'iqul-MuhriqahUk. 102:**

Amesema: Na amenuku Tha'alabi na Baghawi kutoka kwa Ibn Abbas, kuwa: "Wakati ilipoteremka kauli ya Mwenyenzi Mungu:**"Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa karaba."** Watu walisema kwa kujiuliza wenyewe: 'Hakuna anachotaka zaidi ya kutusisitiza juu ya ndugu zake baada ya kufa kwake?' Jibril akamueleza Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuwa Masahaba zake wanamtuhumu, na ndipo Mwenyezi Mungu alipoteremsha Aya:**"Ati wanasema: Amemzulia Mwenyezi Mungu uwongo? Mwenyezi Mungu akipenda atapiga muhuri juu ya moyo wako. Na Mwenyezi Mungu anaufuta upotofu na anaithibitisha Haki kwa maneno Yake. Hakika Yeye anayajua yaliomo vifuani."** Watu wakasema: 'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hakika wewe ni mkweli.'Na hapo Mwenyezi akateremsha Aya: **"Naye ndiye anayepokea toba kwa waja Wake, na anasamehe makosa, na anayajua mnayoyatenda."**

**Tafsir Ibn Jalili Tabari Juz. 25, uk. 16:**

Amepokea kwa sanadi yake kutoka kwa Abi ad-Daylami amesema: "Wakati alipoletwa Ali bin Husain (as) akiwa mfungwa, alisimamishwa katika lango la Damascus, na mara alisimama mtu katika watu wa Shamu (Syria) akasema: 'Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu ambaye amekuhilikisheni na amekung'oeni na amekata mizizi ya fitina.' Ali bin Husain (as) akamjibu kwa kumuuliza: 'Je ulishawahi kusoma Qur'ani?' Akaitikia ndio, akamuliza tena:'Je ulisoma Haa Mim?' Akasema: 'Nimesoma Qur'ani na wala sijasoma Haa Mim.' Akamwambia:'Je ulishawahi kusoma: **"Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa karaba.?"**'Akamuuliza je nyie ni katika hao?Ali bin Husain akajibu:'Ndio."'

**Nasema:** Na pia ameitaja Ibn Hajar katika kitabu chake *As-Sawa'iq*uk. 101 na akasema:"Ameipokea Tabaraniy."

Hii ni sehemu tu ya riwaya zinazojulisha kwamba aya ya mapenzi kwa hakika imeshuka kwa ajili ya karaba wa Mtume (saww). Ama kuhusu Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as) kuwa katika ndugu na karaba zake, mapokezi mengine ni yenye kutoa dalili juu ya habari za kundi la mwanzo na kuzitafsiri, nasi kwa haraka haraka tu tunataja sehemu tu ya habari hizo, tunasema:

**Al-Kashaf ya Zamakhshari katika tafsiri ya kauli yaMwenyezi Mungu katika Sura Ash-shura:"Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa karaba:"**

Amesema: Imepokewa ya kwamba ilipoteremshwa Aya hii paliulizwa:Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, ni akina nani hao ndugu zako ambao tumewajibikiwa kuwapenda? Akajibu: "Ni Ali, Fatimah na watoto wao."

**Nasema:** Baada ya Fakhru Razi kunakili katika *Tafsirul-Kabir* mwishoni mwa tafsiri ya Aya ya mawadah katika Sura ash-Shura riwaya iliyotangulia kutoka kwa mwandishi wa *al-Kashaf*, amesema: "Ikathibiti kwamba hawa watu wanne ndio ndugu wa karibu wa Mtume (saww), na inapothibiti hivyo basi ni lazima wawe ni watu maalum na makhususi wenye hadhi ya ziada." Akasema: "Na yanayothibitisha umakhususi wao na adhama yao ya ziada ni mambo yafuatayo:

**Kwanza:** Ni kauli ya Mwenyezi Mungu: **"Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa karaba."** Na jinsi ya kuitolea hoja ni kama ilivyotangulia, yaani alivyosema kabla ya hapo kuwa ndugu wa Muhammad ni wale ambao mambo yao yanarudi kwake, hivyokila ambaye jambo lake linarudi kwake kwa ukaribu na ukamilifu zaidi ndiye ndugu yake wa karibu zaidi, na bila shaka Fatimah, Ali, Hasan na Husain (as) walikuwa na uhusiano wa karibu zaidi na Mtume (saww). Na jambo hili liko wazi zaidi kwa mujibu wa nukuu mutawatiri, hivyoni lazima wao wawe ndio karaba zake.

**Pili:** Hapana shaka kuwa Mtume (saww) alikuwa akimpenda Fatimah (as), amesema (saww): "Fatimah ni pande langu la damu ananiudhi mimi atakayemuudhi yeye." Na imedhihiri kutokana na nukuu zilizoenea kutoka kwa Mtume Muhammad (saww) kuwa alikuwa akiwapenda Ali, Hasan na Husain (as), hivyo likithibiti hilo basi ni lazima kwa ummahkutekeza hilo kwa kauli yake Mtukufu: **"Na mumfuate yeye ili mpate kuongoka."** Na kauli yake Mtukufu:**"Na wajihadhari ambao huenda kinyume na makatazo yake."** N a kauli Yake:**"Sema ikiwa mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni."** Na kauli Yake:**"Amekuwa kwenu Mtume wa Mwenyezi Mungu ni kigezo chema."**

**Tatu:** Hakika du'a kwa Aali ina daraja la juu, kwa sababu hiyo ikawa kuwaombea wao ndio mwisho wa shahada katika Swala, nayo ni kauli yake: 'Ewe Mungu Wangu mswalie Muhammad na Aali Muhammad na mrehemu Muhammad na Aali Muhammad.' Na hajapata haki na heshima hii yeyote isipokuwa

Aali Muhammad, na hiyo inajulisha kuwa kuwapenda Aali Muhammad ni wajibu. Na amesema Shafi'i: 'Ewe msafiri simama katika ardhi ya changarawe ya mina. Na ita (omba Mola) kwa utulivu wa hofu ya dhahiri watakapoondoka mahujaji usiku kuelekea mina, ni kundi kama mafuriko ya Furati. Ikiwa kuwapenda Aali Muhammad ni upinzani basi vishuhudie vizito viwili kuwa mimi ni mpinzani.'"

**Ad-Durrul-Manthur cha As-Suyutiy katika tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu katika Sura ash-Shuraa: "Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa karaba."**

Amesema: Na ameandika Ibn Mundhir na Ibn Abi Hatim na Tabaraniy na Ibn Mardawayhi kutoka katika mapokezi ya Said bin Jubair kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Ilipoteremshwa Aya hii: **"Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa karaba."** Masahaba wakauliza: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ni akina nani hao ndugu zako ambao tumewajibishwa kuwapenda?' Akasema:'Ni Ali, Fatimah na watoto wao wawili.'"

**Dhakhairul-Uqbah, uk. 25:**

Amesema: Ibn Abbas amesema: "Wakati ilipoteremshwa aya: **"Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa karaba."** Masahaba waliuliza: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ni akina nani hao ndugu zako ambao tumewajibishwa kuwapenda?' Akasema: 'Ni Ali na Fatimah na watoto wao wawili.'"

— Mwandishi amesema: Ameipokea Ahmad katika *al-Manaqib*.

**Nasema:** Na ameitaja pia al-Haythamiy katika *Majmau*yake Juz. 7, uk. 103 na katika Juz. 9, uk. 168 na akasema:"Riwaya zote hizo mbili amezipokea Tabaraniy."Na pia Ibn Hajar amezitaja katika *as-Sawa'iq* yake uk. 101 na akasema:"Ameiandika Ahmad na Tabaraniy na Ibn Abi Hatim na Hakim kutoka kwa Ibn Abbas."Na pia Shabalanjiy ameitaja katika *Nurul-Abswar*uk. 101 akinukuu kutoka kwa Baghawi toka katika *Tafsiir* yake.

## MIONGONI MWA AYA ZILIZOTEREMKA ZIKIZUNGUMZIA FADHILA ZA ALI (AS)

Nasema: Imetangulia katika Mlango unaozungumzia wingi wa fadhila za Imam Ali (as), mlango ambao ulikuwa wa kwanza kabisa katika kuelezea fadhila za Ali (as), riwaya ya al-Khatib Baghdadiy katika kitabu chake cha historia Juz. 6, uk. 221, amepokea humo riwaya kwa njia ya Ibn Abbas, amesema: "Aya zilizoteremshwa kwa haki ya Ali ni miatatu." Na Ibn Hajar katika *as-Sawa'iq* yake uk. 76 na Shabalanjiy katika *Nurul-Abswari*uk. 73 wameeleza kutoka kwa Ibn Asakir kuwa yeye ameandika kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema:"Hakuna mtu ambaye Kitabu cha Mwenyezi Mungu kimeteremka na fadhila zake kama kilivyoteremka na fadhila za Ali (as)." Kisha wamesema: "Ameandika Ibn Asakir kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: 'Ziliteremka Aya mia tatu zikizungumzia fadhila za Ali bin Abu Talib (as)."

Na kinachokusudiwa katika mlango huu si kutaja kila aya iliyoteremshwa ikielezea fadhila za Ali (as), kwani zitafuatia Aya mfano wa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **"Ewe Mtume fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola Wako."** Na kauli Yake Mtukufu: **"Leo nimewakamilishia dini yenu."** Na kauli Yake Mtukufu:**"Ameuliza mwenye kuuliza imshukie adhabu."**iliyoteremka katika tukio la Harith bin Numan, wakati alipokataa uteuzi wa Mtume wa Mwenyezi (saww) kwa Ali (as) siku ya Ghadiir, na pia itafuata kauli ya Mwenyezi Mungu: **"Hakika walii wenu ni Mwenyezi**

**Mungu na Mtume Wake na wale ambao wameamini."** Na kauli Yake Mtukufu:**"Na Mwenyezi Mungu amewatoshelezea waumini kupigana."** Na nyinginezo, kila moja itakuja katika mlango wenye kujitegemea.

Kama pia ilivyotangulia kauli yaMwenyezi Mungu: **"Na akapokea Adam kutoka kwa Mola Wake maneno."**Kuwa Aya imeshuka kutokana na maombi ya Adam kwa Mola Wake kwa haki ya Muhammad, Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as). Na pia Aya ya utakaso imeteremka kwa haki ya Mtume, Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as). Na Aya ya maapizano imeteremka katika maapizano kati Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa pamoja na Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as). Na aya ya kulisha chakula imeteremka kwa haki ya Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as). Na aya ya mapenzi imeteremshwa kwa ajili ya karaba wa Mtume (saww), nao ni Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as) kama ulivyotambua katika milango iliyotangulia ambapo tumeitaja kila moja katika mlango wake. Bali makusudio ya kuweka mlango huu ni kukumbushia maelezo ya aya zilizoelezea fadhila za Ali (as) ambazo hatukuziwekea milango yenye kujitegemea, hivyo tunasema: - Kauli yaMwenyezi Mungu:**"Hakika wewe ni Mwonyaji, na kila kaumu ina wa kuwaongoa:"**

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 3, uk. 129:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ubaid bin Abdillahi Al-Asadiy kutoka kwa Ali (as) kuhusu: "**Hakika wewe ni Mwonyaji, na kila kaumu ina wa kuwaongoa."** Ali amesema: "Mtume wa Mwenyezi Munguni mwonyaji na mimi ni mwongozaji." – Amesema: Hadithi hii ni sahihi.

**Nasema:** Piaal-Mutaqiy ameitaji katika *Kanzul-Ummal*Juz. 1, uk. 251, amesema:"Kaiandika Ibn Hatim na pia al-Haythamiy ameitaja katika *Majmau* yake Juz. 1, uk. 41, na akasema kuhusu hilo: "Mwongozaji ni mtu kutoka Bani Hashim." Al-Haythamiy amesema: "Ameipokea Abdullah bin Ahmad na Tabaraniy katika *as-Swaghiru* na *Al-Awsat*, na wapokezi wake ni wakweli."

**Nasema:** Kauli yaImam Ali (as) kuwa: "Mwongozaji ni mtu kutoka kwa Bani Hashim" inamaanisha ni yeye mwenyewe, kama kwamba yeye amekerwa kuliainisha jina lake. Na as-Suyutiy ameitaja katika *ad-Durul-Manthur*mwishoni mwa tafsiri ya aya husikakatika Sura Ra'd, amesema: "Ameiandika Ibn Mardawayhi na Ibn Asakir, amesema: 'Na katika tamko kuna: Mwongozaji ni mtu kutoka katika Bani Hashim.' Inamaanisha kuwa ni yeye mwenyewe.

**Tafsir Ibn Jariri Tabari Juz. 13, uk. 72:**

amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Wakati ilipoteremshwa: "**Hakika wewe ni Mwonyaji, na kila kaumu ina wa kuwaongoa."**Mtume aliweka mkono wake kwenye kifua cha Ali (as) na akasema: 'Mimi ni mwonyaji na kila ummah una kiongozi.'Na akakunja mkono wa kulia kwenye bega la Ali (as) na akasema: 'Wewe ni mwongozaji ewe Ali, kwako wataongoka wenye kutaka kuongoka baada yangu.'"

**Nasema:** Na pia as-Suyutiy ameitaja katika *ad-Durul-Manthur* katika kufasiri aya iliyoko katika Sura Ra'di, amesema: "Ameiandika Ibn Mardawayhi na Ibn Na'im katika *Maarifa* na ad-Daylami na Ibn Najar.

**Tafsirul-Kabir ya Fakhru Razi, mwishoni mwa tafsiri ya Aya katika Sura Ra'ad:**

Amesema: Na jua kuwa watu wa dhahiri ya maneno miongoni mwa wafasiri wameitaja kwa kauli tofauti – aliendelea kueleza mpaka aliposema: Na kauli ya tatu ni kwamba mwonyaji ni Mtume (saww) na kion-

gozi ni Ali (as). Akasema: "Amesema Ibn Abbas: 'Mtume wa Mwenyezi Mungu aliweka mkono wake kwenye kifua chakena akasema:'Mimi ni mwonyaji.'Kisha akakunja mkono wake kwenye bega la Ali (as) na akasema: 'Wewe ni kiongozi, kwako wataongoka wenye kutaka kuongoka baada yangu.'"

**As-Suyutiy katika ad-Durul-Manthur, mwishoni mwa tafsiri ya Aya katika Sura Ra'ad:**

Amesema: Ameandika Ibn Mardawayhi kutoka kwa Abi Barzah Al-Aslamiy amesema:"Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Hakika wewe ni mwonyaji.'Akaweka mkono wake kwenye kifua chake na kisha akauweka mkono wake kwenye kifua cha Ali (as) huku akisema: 'Kila ummah una kiongozi.'"

Amesema pia: Ameandika Ibn Mardawayhi na adh-Dhiyau katika *al-Mukhtarah*, kutoka kwa Ibn Abbas kuwa amesema kuhusu Aya husika: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Mimi nimwonyaji, na kiongozi ni Ali bin Abu Talib (as).'"

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 157:**

Amesema: "Mimi ni mwonyaji na Ali ni kiongozi, na kwako ewe Ali ataongoka mwenye kutaka kuongoka baada yangu."

— Amesema: Kaiandika ad-Daylami kutoka kwa Ibn Abbas.

**Nasema:** Na pia Shablanjiy ameitaja katika *Nurul-Abswar*uk. 70, na al-Munawi pia ameitaja katika *Kunuzul-Haqaiq*uk. 42.

Kauli ya Mwenyezi Mungu:**"Ati aliye Muumini atakuwa sawa na aliye mpotovu? Hawawi sawa:"**

**Tafsiri Ibn Jariri Tabari Juz. 21, uk. 68, mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: "Ati aliye Muumini atakuwa sawa na aliye mpotovu? Hawawi sawa." Katika Sura as-Sajdah:**

Amepokea kutoka kwa Atwau bin Yasar amesema: "Aya hii imeteremshwa Madina ikiwahusu Ali (as) na Walid bin Uqba bin Abi Mu'it. Kulikuwa na mazungumzo kati ya Walid na Ali (as), akasema Walid bin Uqba: 'Mimi ni mfasaha zaidi katika mazungumzo kuliko wewe, ni mshambuliaji hodari kuliko wewe, na ni shujaa kuliko wewe.' Ali (as) akasema: 'Kaa kimya, kwani wewe ni fasiki.'NdipoMwenyezi Mungu akateremsha Aya kwa wawili hao: **"Ati aliye Muumini atakuwa sawa na aliye mpotovu? Hawawi sawa. Ama walioamini na wakatenda mema, watakuwa nazo Bustani za makaazi mazuri. Ndio pa kufikia kwa waliyokuwa wakiyatenda. Na ama wale waliotenda uovu, basi makaazi yao ni Motoni. Kila wakitaka kutoka humo watarudishwa humo humo. Na wataambiwa: Onjeni adhabu ya Moto ambayo mliyokuwa mkiikanusha.'"**

**Nasema:** Na pia Zamakhshari imeitaja katika *al-Kashaf* katika tafsiri ya aya hii katika Sura as-Sajidah, na pia as-Suyutiy ameitaja katika *ad-Durul-Mathur* katika tafsiri ya aya hii, na akasema: "Ameiandika Ibn Is'haqa kutoka kwa Atwai bin Yasar." Kisha akasema: "Na ameiandika kama hivi Ibn Abi Hatim."

**Asbabun-Nuzul cha al-WahidiyUk. 263:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas amesema: "Walid bin Uqba bin Abi Mu'italisema kumwambia Ali bin Abu Talib (as): 'Mimi ni mfasaha zaidi katika mazungumzo kuliko wewe, ni mshambu-

liaji hodari kuliko wewe, na ni shujaa kuliko wewe.' Ali (as) akasema: 'Kaa kimya, kwani wewe ni fasiki.' Ndipo Mwenyezi Mungu akateremsha Aya kwa wawili hao: **"Ati aliye Muumini atakuwa sawa na aliye mpotovu? Hawawi sawa."** Amesema: Muumin inamaanisha ni Ali (as), na fasiki ni Walid bin Uqba."

**As-Suyutiy katika ad-Durul-Manthur, katika tafsiri ya Aya iliyotajwa iliyopo Sura as-Sajdah:**

Amesema: Ameandika Abi Hatim kutoka kwa Abi Rahman kutoka kwa Abi Layla kuhusu kauli yake: **"Ati aliye Muumini atakuwa sawa na aliye mpotovu? Hawawi sawa."** Amesema: "Imeteremshwa kwa ajili ya Ali na Walid bin Uqba."

Amesema tena: Ameandika Ibn Mardawayhi na Khatib na Ibn Asakir, wote wameandika kutoka kwa Ibn Abbas kuhusu kauli yake:**"Ati aliye Muumini atakuwa sawa na aliye mpotovu? Hawawi sawa."** Amesema: "Ama muumin ni Ali (as) na fasiki ni Walid bin Uqba bin Abi Mu'itwi, hiyo ilitokana na sababu iliyokuwepo kati yao, na ndipo Mwenyezi Mungu akateremsha aya kwa tukio hilo."

**Tarikh Baghdad Juz. 13, uk. 321:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Walid bin Uqba alimwambia Ali bin Abu Talib (as): 'Je mimi si ni mfasaha zaidi katika mazungumzo kuliko wewe, ni mshambuliaji hodari kuliko wewe, na ni shujaa kuliko wewe.' Ndipo Mwenyezi Mungu akateremsha Aya kwa wawili hao: **"Ati aliye Muumini atakuwa sawa na aliye mpotovu? Hawawi sawa."**

**Nasema:** Na ameitaja pia as-Suyutiy katika *ad-Durul-Manthur*mwishoni mwa tafsiri yaAya husika katikaSura as-Sajdah, amesema: "Ameiandika Abul-Faraji al-Isbahani katika kitabu *al-Aghani*, na pia ameiandika Ibn Adi na Ibn Mardawayhi na Khatib na Ibn Asakir kwa njia tofauti kutoka kwa Ibn Abbas.

**Ar-Riyadh an-NadhrahJuz. 2, uk. 207:**

Amesema: Na miongoni mwa Aya zilizoteremshwa, zikielezea fadhila za Ali (as) ni kauli Yake Mtukufu:**"Ati aliye Muumini atakuwa sawa na aliye mpotovu? Hawawi sawa."** Amesema: "Amesema Ibn Abbas: 'Imeteremshwa kwa ajili ya Ali (as) na Walid bin Uqba bin Abi Mu'iti, kwa ajili ya mazungumzo yaliyopita kati yao."'

Amesema: Ameiandika Hafidh Salafi. Kisha akasema: "Na imepokewa kutoka kwake (Ibn Abbas) kwamba Walid alimwambia Ali (as): 'Mimi ni mfasaha zaidi katika mazungumzo kuliko wewe, ni mshambuliaji hodari kuliko wewe, na ni shujaa kuliko wewe.' Ali (as) akasema: 'Kaa kimya, kwani wewe ni fasiki.' Na katika riwaya nyingine alimwambia: 'Wee ni fasiki unasema uongo.' Ndipo Mwenyezi Mungu akateremsha Aya hiyo kumsadikisha Ali (as)." Amesema: Qatadah amesema: "Naapa Wallahi hawako sawa si duniani wala mbele ya Mwenyezi Mungu na wala Akhera. Kisha akaeleza mafikio ya makundi mawili, akasema Mtukufu: **Ama wale ambao wameamini**..."'

— Amesema: Ameiandika al-Wahidiy.

Kauli ya Mwenyezi MunguMtukufu:**"Basi je, mtu aliye na dalili wazi itokayo kwa Mola Wake Mlezi, inayofuatwa na shahidi anayetoka kwake:**

**As-Suyutiy katika ad-Durul-Manthur, katika tafsiri ya Aya iliyotajwa iliyopo Sura Hud:**

Amesema: Ameiandika Ibn Abi Hatim na Ibn Mardawayhi na Abu Na'im katika kitabu *al-Maarifah* kutoka kwa Ali bin Abu Talib (as), alisema:"Hakuna mtu yeyote katikaMakuraishi isipokuwa kuna sehemu

ya Qur'ani iliteremka kumuhusu yeye."Mtu mmoja akamuliza: Ni zipi zilizoteremshwa kuhusu wewe? Akasema:"Je hausomi Sura Hud: "**Basi je, mtu aliye na dalili wazi itokayo kwa Mola Wake Mlezi, inayofuatwa na shahidi anayetoka kwake.** Mtume wa Mwenyezi ni dalili iliyo wazi itokayo kwa Mola Wake, na mimi ni shahidi atokaye kwake.'"

**Nasema:** Pia ameitaja ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 1, uk. 251. Na akasema tena: Ameandika Ibn Mardawayhi na Ibn Asakir kutoka kwa Ali (as) kuhusu aya hii, amesema: "Mtume (saww) ni dalili ya wazi itokayo kwa Mola Wake na mimi ni shahidi atokaye kwake."

Na pia akasema: Ameandika Ibn Mardawayhi kutoka katika njia nyingine kutoka kwa Ali (as) kuwa amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungualisema: **Basi je, mtu aliye na dalili wazi itokayo kwa Mola Wake Mlezi,** ni mimi. **Inayofuatwa na shahidi anaye toka kwake.** Amesema: NiAli (as)."

**Tafsirul-Kabir ya Fakhru Razi, katika tafsiri ya Aya iliyotajwa ya Sura Hud:**

Amesema: wameelezea kwa mitazamo mbalimbali katika kutafsiri neno shahidi – Amefafanua mpaka aliposema: Maana ya tatu ni Ali bin Abu Talib (as), maana yake ni kuwa yeye ndiye atakayefuata hiyo dalili, na kauli yake "Anayetoka kwake" yaani huyu shahidi anatokana na Muhammad na ni sehemu yake. Na muradi ni kumtukuza huyu shahidi ya kuwa yeye ni sehemu ya Muhammad (saww).

Kauli ya Mwenyezi Mungu:**"Kama nyinyi wawili hamkutubia kwa Mwenyezi Mungu, basi nyoyo zenu zimekwishaelekea huko. Na mkisaidiana dhidi yake (Mtume), basi hakika Mwenyezi Mungu ndiye kipenzi chake, na Jibril, na Waumini wema, na zaidi ya hayo Malaika pia watasaidia:**

**ad-Durul-Manthur ya as-Suyutiy mwishoni mwa tafsiri ya Aya tukufu iliyopo katika Sura Tahrim:**

Amesema: Na ameandika Ibn Mardawayhi kutoka kwa Asma bint Umais amesema:"Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Waumini wema ni Ali bin Abu Talib (as).'"Na akasema tena: Na ameandika Ibn Mardawayhi na Ibn Asakir kutoka kwa Ibn Abbas kuhusu kauli yake: Waumini wema, amesema: "Ni Ali bin Abu Talib (as)."

**Kanzul-Ummal Juz. 1, uk. 237:**

Amesema: Kutoka kwa Ali (as) amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuhusu kauli yake: Waumini wema: "Ni Ali bin Abu Talib (as)." – Amesema: Ameiandika Ibn Abi Hatim.

**Nasema:** Ibn Hajar amesema katika kitabu chake *as-Sawa'iq*uk. 144 tamko hili: "Isipokuwa imepokewa hadith katika njia ya kuvusha au ya kutotaja sanadi kuwa Waumini wema ni Ali bin Abu Talib (as).

**al-Asqalaniy katika Fat'hilu-BariyJuz. 13, uk. 27:**

Amesema: Ameandika Tabari kutoka kwa Mujahid ya kwamba Waumini wema ni Ali bin Abu Talib (as). Pia akasema: an-Naqashi ameitaja kutoka kwa Ibn Abbas na Muhammad bin Ali al-Baqir na mtoto wake Ja'far as-Sadiq (as) kuwa: Waumini wema ni Ali bin Abu Talib (as).

**Majmauz-Zawa'id ya al-HaythaiyJuz.9, uk. 194:**

Amesema: Kutoka kwa Habib bin Yasar amesema: "Wakati Husain bin Ali (as) alipofikwa na masaibu, Zayd bin Arqam alisimama mbele ya mlango wa msikiti akasema: 'Je mmeyatenda hayo? Nashuhudia

kuwa nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: Ewe Mola Wangu, mimi nawachia hawa wawili na mwema kati ya Waumini.' Akaulizwa Ubaidullah bin Ziyad: Hakika Zayd bin Arqam amesema hivi na hivi. Ubaidullah akasema: 'Yule mzee amechanganyikiwa."' - Amesema: Kaipokea Tabaraniy.

**Nasema:** Na makusudio ya dhamiri ya uwili katika kauli yake: "Ewe Mola Wangu, hakika ya mimi nawaachia hawa wawili."Ni Hasan na Husain (as) na mwema wa Waumini ni Ali bin Abu Talib, hivyo ina maanisha hivi: Ewe Mola nawaachia Hasan, Husain na Ali binAbu Talib. Na hivyo Ubaidullah bin Ziyad alipoambiwa: Hakika Zayd bin Arqam amesema hivi na hivi, alikasirika na akasema: Yule mzee amekwisha changanyikiwa.

Kauli ya Mwenyezi Mungu:**"Ili tuyafanye hayo kuwa ni waadhi kwenu na kila sikio linalosikia liyahifadhi:**

**Tafsiri Ibn Jariri Tabari Juz. 29, uk. 35:**

Amepokea kwa sanadi yake kutoka kwa Mak'huul, anasema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisoma: '**Na kila sikio linalosikia liyahifadhi.'**Kisha akamtazama Ali (as) na akasema: 'Nimemuomba Mwenyezi Mungu alijaalie sikio lakoliwe sikivu.' Ali (as) anasema: 'Sijapata kusikia lolote kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi kisha nikalisahau."'

**Tafsiri Ibn Jariri Tabari Juz. 29, uk. 35:**

Amepokea kwa sanadi yake kutoka Buraydah, amesema: "Nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akimwambia Ali (as): 'Ewe Ali, hakika Mwenyezi Mungu ameniamrisha niwe karibu nawe na wala nisiwe mbali nawe, na nikufundishe na uzingatie, na ni haki kwa Mwenyezi Mungu kukuwezesha kuzingatia.' Na ndipo ikashukaAya hii: '**Na kila sikio linalosikia liyahifadhi.'**"

**Nasema:** Na ameipokea kutoka kwa Buraydah Al-Aslamiy kwa mapokezi mengine kwa tofauti ndogo katika Juz. 29, uk. 36.

**Al-Kashaf ya Zamakhshariy katika tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: 'Na kila sikio linalosikia liyahifadhi.' katika Sura al-Haqah:**

Amesema: Kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Ali (as) wakati ilipoteremshwa Aya hii: "Nilimuomba Mwenyezi Mungu alifanye sikio lako liwe sikivu ewe Ali." Ali (as) anasema: "Sijapata kusahau chochote baada ya hapo na sikuwa mwenye kusahau."

**Nasema:** Na Fakhru Razi ameitaja pia katika *Tafsiiral-Kabiir*yake kama alivyoitaja *al-Kashaf*.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythaiy Juz. 1, uk. 131:**

Amesema: Kutoka kwa Abi Raafii, amesema:"Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema kumwambia Ali (as): 'Hakika Mwenyezi Mungu ameniamrisha nikufundishe na wala nisikukatize, nikuweke karibu na wala nisikuweke mbali, ni haki yangu kwako kukufundisha na ni haki yako kuzingatia."' - Amesema: AmeipokeaBazaar.

**Nasema:** al-Mutaqi ameitaja katika *Kanzul-Ummal*Juz. 6, uk. 398, na akasema kuhusu tukio hilo: "Na ikateremka: **'Na kila sikio linalosikia liyahifadhi.'**" Kisha akasema:"Amepokea Ibn Asakir."

**Hilyatul-AwliyaiJuz. 1, uk. 67:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ali (as) kuwa amesema: "Mtume wa Mwenyezi (saww) alisema: 'Ewe Ali Mwenyezi Mungu ameniamrisha nikuweke karibu na nikufundishe ili uzingatie, ndipo ikateremka Aya hii:**'Na kila sikio linalosikia liyahifadhi.'** basi wewe Ali ni sikio sikivu la elimu yangu.'"

**Ad-Durul-Manthur ya as-Suyutiy katika tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: 'Na kila sikio linalosikia liyahifadhi.' katika Sura al-Haqah:**

Amesema: Ameandika Said bin Mansur na Ibn Jarir na Ibn Mundhir na Ibn Abi Hatim na Ibn Mardawayhi, wote wameandika kutoka kwa Mak'huul kuwa amesema: "Wakati ilipoteremshwa: **'Na kila sikio linalosikia liyahifadhi.'** Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Nilimuomba Mola Wangu alipe usikivu sikio la Ali.'" Mak'huul anasema: "Ali (as) alikuwa akisema: 'Sijapata kusikia lolote kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu na kisha nikalisahau.'"

Na akasema tena: Na ameandika Ibn Jarir na Ibn Abi Hatim na al-Wahidiy na Ibn Mardawayhi na Ibn Asakir na Ibn an-Najar, wote wameandika kutoka kwa Buraydah kuwa amesema: "Alisema Mtume wa Mwenyezi (saww) kumwambia Ali (as):'Hakika Mwenyezi Mungu ameniamrisha nikuweke karibu na wala nisikuweke mbali na nikufundishe na uzingatie, na ni haki yako kuzingatia.' Ndipo ikateremka hii Aya:**'Na kila sikio linalosikia liyahifadhi.'**

**Nasema:** Hadith hii nimeikuta ndani ya *Asbabun-Nuzul* cha al-Wahidiy katika uk. 329, na akasema: "Na ni haki kwa Mwenyezi Mungu kukupa uzingativu."

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 408:**

Amesema: Kutoka kwa Ali (as) kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu:**'Na kila sikio linalosikia liyahifadhi.'** Amesema: "Aliniambia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): 'Ewe Ali, nilimuomba Mwenyezi Mungu alijaalie sikio lako kuwa sikivu.' Na mimi sijapata kusikia lolote kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu na kulisahau."

— Amesema: Ameiandika adh-Dhiyaul-Muqaddas na Ibn Mardawayhi na Abu Na'im katika kitabu *al-Maarifah*.

**Nasema:** Na pia Shabalanjiy ameitaja katika *Nurul-Abswaari*uk. 70, amesema humo: "Sijapata kusikia kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi (saww) isipokuwa nimeyazingatia na kuyahifadhi na sijapata kusahau."

Kauli ya Mwenyezi Mungu:**"Wale wanaotoa mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhaahiri, wana ujira wao kwa Mola Wao Mlezi; wala haitakuwa hofu juu yao, wala hawatahuzunika.**

**Usudul-Ghabah ya Ibn Athir al-Jazriy Juz. 4, uk. 25:**

amepokea katika njia mbili kutoka kwa Mujahid kutoka kwa Ibn Abbas kuhusu kauli ya ya Mwenyezi Mungu: **"Wale wanaotoa mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhaahiri,"**amesema: "Imeteremshwa kwa haki ya Ali bin Abu Talib (as) kwa sababu alikuwa na dirhamu nne akatoa dirhamu moja usiku na moja mchana, na akatoa moja katika siri na moja katika dhahiri."

**Nasema:** Pia Zamakhshariy ameitaja katika *al-Kashaf* katika kutafsiri hii Aya iliyopo mwisho wa Sura ya al-Baqarah, na pia As-Suyutiy ameitaja katika *ad-Durul-Manthur* katika kutafsiriAya hii ya Sura Al-Baqarah, amesema: "Ameiandika Abdulrazaq na Abdi bin Hamid na Ibn Jarir na Ibn Mundhir na Abi Hatim na Taba-

raniy na Ibn Asakir kwa njia ya Wahhab bin Mujahid kutoka kwa baba yake kutoka kwa Ibn Abbas. Na pia al-Haythamiy ameitaja katika *Majmauz-Zawa'id*yake Juz. 6, uk. 324 na akasema:"Ameipokea Tabaraniy."

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, uk. 206:**

Amesema: Kutoka kwa Ibn Abbas kuhusu kauli ya ya Mwenyezi Mungu: **"Wale wanaotoa mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhaahiri,"** amesema: "Imeteremshwa kwa haki ya Ali bin Abu Talib (as) alikuwa na dirhamu nne, akatoa dirhamu moja usiku na moja mchana, na dirhamu moja akaitoa kwa siri na moja kwa dhahiri, ndipo Mtume (s.a.w.w) akamuuliza ni lipi lililokupelekea kutenda hivi? Akajibu: 'Ili niwajibike kupata yale aliyoniahidi Mwenyezi Mungu.' Mtume akamwambia: 'Tambua kuwa una ujira kwa hayo.' Ndipo ikateremshwa hii Aya.'"

— Amesema: Na akafuatia kuelezea Ibn Abbas na Mujahid na as-Saaib na Muqaatil.

**Nasema:** Na pia Fakhru Razi ameitaja kwa tofauti ndogo katika *Tafsirul-Kabiir* katika muendelezo wa kufasiri hii Aya.

**As-Sawa'iqul-MuhriqahUk. 78:**

Amesema: Ameandikaal-Waqidiy kutoka kwa Ibn Abbas kuwa amesema: "Ali (as) alikuwa anamiliki dirhamu nne ambazo alikuwa hamiliki nyingine zaidi ya hizo. Basi akatoa dirhamu moja usiku na moja mchana, na dirhamu moja akatoa kwa siri na moja kwa dhahiri, ndipo ikateremshwa Aya hii kutokana na tukio hilo:**"Wale wanaotoa mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhaahiri, wana ujira wao kwa Mola Wao Mlezi; wala haitakuwa hofu juu yao, wala hawatahuzunika.'**"

**Nasema:** Na pia Shabalanjiy ameitaja katika *Nurul-Abswari*uk. 70 na akasema: "Ameinakili Al-Wahidiy katika *Tafsiir* yake kwa kuivusha kutoka kwa Ibn Abbas."

**Asbabun-Nuzul cha Al-Wahidiy Uk. 64:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Mujahidi, amesema: "Ali (as) alikuwa na dirhamu nne, akatoa dirhamu moja usiku na moja mchana, na dirhamu moja akatoa kwa siri na moja kwa dhahiri, ndipo ikateremka: '**Wale wanaotoa mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhaahiri, wana ujira wao kwa Mola Wao Mlezi; wala haitakuwa hofu juu yao, wala hawatahuzunika.**'"

Amesema: al-Kalbiy amesema: "Imeteremshwa hii Aya kwa ajili ya Ali bin Abu Talib (as), wakati huo hakuwa anamiliki zaidi ya dirhamu nne, akatoa dirhamu moja usiku na moja mchana, na dirhamu moja kwa siri na moja kwa dhahiri, ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamuuliza ni lipi lililokupelekea kutenda hivi? Akajibu: 'Ni Ili niwajibike kupata yale aliyoniahidi Mwenyezi Mungu.' Mtume akamwambia: 'Tambua kuwa una ujira kwa hayo.' Ndipo ikateremshwa hii Aya."

Kauli ya Mwenyezi Mungu: **Hakika walioamini na wakatenda mema Ar-Rahmani Mwingi wa Rehema atawajaalia mapenzi.**

**Al-Kashaf ya Zamakhshariy katika tafsiri yaAya tukufu iliyoko mwishonimwa Sura Maryam:**

Amesema: Imepokewa ya kwambaMtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Ali (as): "Ewe Ali sema: 'Ewe Mola Wangu nijaalie niwe Kwako na ahadi na mapenzi katika nyoyo za waumini.'" Hapo Mwenyezi Mungu akateremsha hii Aya.

**Nasema:** Na pia As-Suyutiy ameitaja katika *ad-Durul-Manthur* kutika kutafsiri hii Aya, amesema: "Nijalie Kwako mapenzi na nifanye katika nyoyo za waumini kipenzi, ndipoMwenyezi Mungu akateremsha: '**Hakika walioamini na wakatenda mema Ar-Rahmani Mwingi wa Rehema atawajaalia mapenzi.** Akasema: "Iliteremshwa kwa ajili ya Ali (as)."

— Amesema: Ameipokea Ibn Mardawayhi na ad-Daylamiy kutoka kwa Bal-Barau.

**Ad-Durul-Manthur ya as-Suyutiy katika kufasiri aya tukufu iliyoko mwisho wa Sura Maryam:**

Amesema: Ameandika Tabaraniy na Ibn Mardawayhi kutoka kwa Ibn Abbas amesema: "Imeteremshwa kwa ajili ya Ali bin Abu Talib (as): '**Hakika walioamini na wakatenda mema Ar-Rahmani Mwingi wa Rehema atawajaalia mapenzi.**'" Akasema:"Mapenzi katika nyoyo za waumini."

**Nasema:** al-Haythamiy pia ameitaja katika *Majmauz-Zawa'id* yake Juz. 9, uk. 205, akasema: "Ameipokea Tabaraniy katika kitabu*al-Awsat*.

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, uk. 207:**

Amesema: Miongoni mwa aya zilizoshukazikieleza fadhila za Ali (as) ni kauli yaMwenyezi Mungu: '**Hakika walioamini na wakatenda mema Ar-Rahmani Mwingi wa Rehema atawajaalia mapenzi.**' Akasema: Amesema Ibn al-Hanafiyah: "Mtu hatobaki kuwa muumini mpaka katika moyo wake awe na mapenzi na Ali na kizazi chake." - Amesema: Ameiandikaal-Hafidh as-Salafiy.

Na pia Ibn Hajar katika *as-Saw'aiq*uk. 102 amesema kama hivyo. Pia Shabalanjiy ameitaja katika *Nurul-Abswari*uk. 101, akasema:"Wamepokea baadhi yao kutoka kwa Muhammad bin al-Hanafiyah." Na akaitaja mpaka akasema: "an-Naqash amesema kuwaAya hii imeteremshwa kwa ajili ya Ali (as).

Kauli ya Mwenyezi Mungu:"**Hakika walioamini na wakatenda mema, hao ndio bora wa viumbe:**

**Tafsiri ya Ibn Jarir Tabari Juz. 30, uk. 171:**

Amepokea kwa sanadi yake kutoka kwa Abi al-Jarud kutoka kwa Muhammad bin Ali, amesema: kuhusu '**Hakika walioamini na wakatenda mema, hao ndio bora wa viumbe:'** Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Ewe Ali! Ni wewe pamoja na wafuasi wako."

**ad-Durul-Manthur ya as-Suyutiy mwishoni mwa tafsiri ya aya tukufu: "Hakika walioamini na wakatenda mema, hao ndio bora wa viumbe" iliyoko katik Sura al-Bayyinah:**

Amesema: Ameandika Ibn Asakir kutoka kwa Jabir bin Abdullah amesema: "Tulikuwa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na mara akafika Ali (as), ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliposema: 'Naaapa kwa yule ambaye nafsi yangu ipo mikononi Mwake, hakika huyu na wafuasi wake hao ndio wenye kufuzu Siku ya Kiyama.' Hapo ikateremshwa: '**Hakika walioamini na wakatenda mema, hao ndio bora wa viumbe'** Maswahaba wa Mtume (saww) wakawa wanasema pindi anapofika Ali (as): 'Amefika mbora wa viumbe."'

Na akasema tena: Ameandika Ibn Adiy na Ibn Asakir kutoka kwa Abi Said kwa njia ya kuvushwa: "Ali ndiye mbora wa viumbe."Na akasema tena: Ameandika Ibn Adiy kutoka kwa Ibn Abbas kuwa amesema:"Wakati ilipoteremshwa:'**Hakika walioamini na wakatenda mema, hao ndio bora wa viumbe'** Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Ali (as): 'Mbora wa viumbe ni wewe na wa-

fuasi wako, mtakujaSiku ya Kiyama hali ya kuwa mmeridhiwa na kuridhia.'"Na akasema tena: Ameandika Ibn Mardawayhi kutoka kwa Ali (as) kuwa amesema: "Mtume wa Mwenyenzi Mungu (saww) aliniambia: 'Je haukusikia kauli ya Mwenyenzi Mungu: '**Hakika walioamini na wakatenda mema, hao ndio bora wa viumbe?'** Ni wewe na wafuasi wako, ahadi yangu mimi na ninyi ni kukutana katika hodhi wakati mataifa yatakaposimama kwa ajili ya hisabu na nyie mtaitwa kundi lililofaulu.'"

**As-Sawa'iqul-MuhriqahUk. 96:**

Amesema: Aya ya kumi na moja ni kauli ya Mwenyezi Mungu: '**Hakika walioamini na wakatenda mema, hao ndio bora wa viumbe.'** Amesema: Ameandika Hafidh Jamalud-Din Zarandiy kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Hakika ilipoteremshwa Aya hii, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Ali (as): "Ni wewe pamoja na wafuasi wako, mtakuja Siku ya Kiyama hali mmeridhia na kuridhiwa, na watakuja maadui zako hali wamekasirika wamehemewa." Akauliza ni kina nani hao maadui zangu? Akajibu: "Ni yule ambaye amejitenga nawe na akakulaani."

**Nasema:** Na pia ameitaja Shabalanjiy katika *Nurul-Abswari*katika uk. 70 na uk. 101.

Kauli ya Mwenyezi Mungu: "**Je, mnafanya kuwanywesha maji Mahujaji na kuamirisha Msikiti Mtakatifu ni sawa na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na akapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhaalimu."**

**Asbabun-Nuzul cha al-Wahidiy Uk. 172:**

Amesema: Hasan na Sha'abiy na Qurtubiy wamesema: Imeteremshwa aya hii kwa ajili ya Ali (as), Abbas na Twalha bin Shayba, walikuwa wakijigamba, akasema Twalha: 'Mimi ndio mlinzi wa nyumba hii (Kaaba) na nina funguo na nguo zake.' Abbas akasema: 'Mimi ni mnyweshaji wa maji na msimamizi wa huduma hiyo.' Na Ali (as) akasema: 'Sijui mnachosema, hakika nimeswali miezi sita kabla ya watu wote na mimi ndio kiongozi wa jihadi.' Hapo ikateremshwaAya hii: "**Je, mnafanya kuwanywesha maji Mahujaji na kuamirisha Msikiti Mtakatifu ni sawa na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na akapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhaalimu. Wale walioamini, na wakahama, na wakapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao, hao wana cheo kikubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu. Na hao ndio wenye kufuzu.**"

**Nasema:** Na pia ameipokea Ibn Jariri Tabari katika *Tafsiir* yake Juz. 10, uk. 68 kwa njia ya Muhammad bin Kaabi al-Qaradhiy, na pia Fakhru Razi ameitaja katika *Tafsiiral-Kabiir*yakemwishoni mwa tafsiri ya Aya hii katika Sura Tawba.

**Tafsiri ya Ibn Jarir Tabari Juz. 10, uk. 68:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa as-Sadiy kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu:**"Je, mnafanya kuwanywesha maji Mahujaji na kuamirisha Msikiti Mtakatifu ni sawa na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na akapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu."**Amesema: Walikuwa wakijigamba Ali (as), Abbas na Shayba bin Uthman, akasema Abbas: 'Mimi ni mbora wenu kwani huwanywesha maji mahujaji wa nyumba ya Mwenyezi Mungu.' Akasema Shayba: 'Mimi huamirisha msikiti wa Mwenyezi Mungu.'Na akasema Ali (as): 'Mimi nimehama pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu na napigana pamoja naye katika njia ya

Mwenyezi Mungu.' NdipoMwenyezi Mungu akateremsha hii Aya:**"Je, mnafanya kuwanywesha maji Mahujaji na kuamirisha Msikiti Mtakatifu ni sawa na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na akapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhaalimu. Wale walioamini, na wakahama, na wakapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao, hao wana cheo kikubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu. Na hao ndio wenye kufuzu. Mola Wao Mlezi anawabashiria rehema zitokazo Kwake, na radhi, na Bustani ambazo humo watapata neema za kudumu. "**

**Fakhru Razi katika Tafsiri yake, katika kufasiri Aya tukufu katika Sura Tawba:**

Amesema: Abbas amesema katika baadhi ya riwaya zake: "Baada ya Ali (as) kumshinda Abbas kwa maneno, Abbas alisema: 'Ikiwa nyinyi mmetutangulia kusilimu na kugura na kupigana jihadi, lakini sisi tulikuwa tunaamirisha msikiti Mtukufu na tunanywesha mahujaji maji.' Ndipo ikashuka Aya hii."

Na akasema tena lafudhi ifuatayo katika kutafsiri Sura Takathur: "Kujigamba na kujifakharisha katika sifa za kweli si jambo baya, na mfano wa kujigamba huko ni kule kulikopokewa kutoka kwa Abbas kuwa alijigamba kuwa unyweshaji wa maji upo mikononi mwake na Shayba akajigamba kuwa ufunguo upo mikononi mwake – Aliendelea kueleza mpaka akasema: Ali (as) akasema:'Na mimi nimekata mkonga wa ukafiri kwa panga langu na hatimaye ukafiri umeshindwa na ninyi mkasilimu.' Akawashinda kwa hilo na hapo ikateremka kauli ya Mwenyezi Mungu:**"Je, mnafanya kuwanywesha maji Mahujaji na kuamirisha Msikiti Mtakatifu ni sawa na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na akapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu.**"

**ad-Durul-Manthur ya as-Suyutiy mwishoni mwa tafsiri ya aya tukufu iliyoko katik Sura Tawba:**

Amesema: AmeandikaAbu Na'imu katika *Fadhailus-Sahabah* na Ibn Asakir, wote wameandika kutoka kwa Anas, amesema: "Walikuwa wamekaa Abbas na Shayba mlinzi wa Nyumba, kila mmoja akajigamba, Abbas akamwambia: 'Mimi ni mbora zaidi kuliko wewe, kwanza mimi ni ami wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), wasii wa baba yake na mnyweshaji maji wa mahujaji.' Shayba akajibu: 'Mimi ni mbora zaidi kuliko wewe kwani mimi ndio mdhamini wa Nyumba ya Mwenyezi Mungu na mwenye ufunguo wa nyumba hiyo, kwa nini basi asikuamini kama alivyoniamini?' Mara akatokeza Ali mbele yao, wakamweleza waliyoyasema, Ali (as) akasema: 'Mimi ni adhimu kuliko ninyi, mimi ndiye wa kwanza kuamini na kuhama.' Wakatoka wote watatu na kwenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), walipomwambia hakuwajibu kitu, hivyo wakaondoka, ndipo wahyi ukateremka baada ya siku kadhaa, Mtume akawaita na kuwasomea: **"Je, mnafanya kuwanywesha maji Mahujaji na kuamirisha Msikiti Mtakatifu ni sawa na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na akapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhaalimu."** Mpaka mwisho wa Sura al-Hashri."

Akasema tena: Ameandika Abdurazak na Ibn Abi Shayba na Ibn Jarir na Ibn Mundhir na Ibn Abi Hatim na Abu Shaykh kutoka kwa Sha'abiy amesema: "Imeteremshwa Aya hii: **"Je, mnafanya kuwanywesha maji Mahujaji na kuamirisha Msikiti Mtakatifu ni sawa na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na akapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhaalimu,"**kwa ajili ya Abbas na Ali (as), kwani walikuwa na mabishano baina yao."

Akasema tena: Ameandika Ibn Mardawayhi kutoka kwa Sha'abiy amesema: "Kulikuwa kati ya Ali (as) na Abbas mabishano, Abbas alimwambia Ali (as): 'Mimi ni mpwa wa Mtume na wewe ni mtoto wa mpwa wake, pia mimi ni mnyweshaji wa maji kwa mahujaji na muamirishaji wa Msikiti mtukufu.' Ndipo Mwenyezi Mungu akateremsha hii Aya:**'Je, mnafanya kuwanywesha maji Mahujaji na kuamirisha Msikiti Mtakatifu ni sawa na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na akapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhaalimu.'**"

Akasema tena: Ameandika Abdul-Razak kutoka kwa Hasan kua amesema: "Imetereshwa Aya hii kwa ajili ya Ali (as), Abbas, Uthman na Shayba, kwani walikuwa kwenye mabishano."

Kauli ya Mwenyezi Mungu: **Na wasimamisheni. Hakika hao watasailiwa:**

**As-Sawa'iqul-MuhriqahUk.89:**

Amesema:Ayayanneni kauli ya Mwenyezi Mungu:**"Na wasimamisheni. Hakika hao watasailiwa."**Amesema: Ameandikaad-Daylamiy kutoka kwa Abi Said Khudiriy kwamba amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alisema: '**Na wasimamisheni. Hakika hao watasailiwa**' kuhusu kumpenda Ali."'

Amesema: Kama kwamba maana hii ndio kusudio la Al-Wahidiy aliposema: "Imepokewa kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: '**Na wasimamisheni. Hakika hao watasailiwa.**' Yaani kuhusu kumpenda Ali na Ahlul-Bait (as), kwa sababu Mwenyezi Mungu amemuamrisha Mtume Wake (saww) awafahamishe watu ya kwamba yeye hawaombi malipo yoyote ya kufikisha ujumbe isipokuwa kuwapenda karaba. Na maana yake ni kuwa: Je waliwapenda ipasavyo? kama walivyousiwa na Mtume (saww) au wamewaacha na kuwapuuza?na hatimaye iwe ni dhambi na makosa?

Kauli ya Mwenyezi Mungu:**"Enyi mlioamini! Atakayeiacha miongoni mwenu Dini yake, basi Mwenyezi Mungu atakuja leta watu anaowapenda nao wanampenda, wanyenyekevu kwa Waumini na wenye nguvu juu ya makafiri, wanapigania Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawaogopi lawama ya anayelaumu. Hiyo ndiyo fadhila ya Mwenyezi Mungu, humpa amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu na Mwenye kujua:**

**Fakhru Razi katika Tafsiri yake al-Kabiir, mwishoni mwa tafsiri ya Aya tukufu iliyoko katika Sura Maidah:**

Amesema: Jamaa wamesema: Hakika Aya hii imeteremshwa kwa ajili ya Ali (as). Amesema tena: Na kinachojulisha hilo ni dalili mbili: Ya kwanza ni kwamba wakati Mtume alipokabidhi bendera kwa Ali (as) siku ya Khaibari alisema: "Nitampa bendera leo mtu ambaye anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanampenda yeye.' Na hii ndio sifa iliyotajwa katika hii aya.

Dalili ya pili: Ni kuwa Yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu ametaja baada ya aya hii kauli yake:**"Hakika walii wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na walioamini, ambao hushika Swala na hutoa Zaka nao wananyenyekea."** Na Aya hii imeteremshwa kwa ajili ya Ali (as), hivyo inafaa hata ya kabla yake iwe ni katika haki zake.

Kauli ya Mwenyezi Mungu: **Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli:**

**ad-Durul-Manthur ya as-Suyutiy mwishoni mwa tafsiri ya aya tukufu iliyoko katika Sura Tawba:**

Amesema: Ameandika Ibn Mardawayhi kutoka kwa Ibn Abbas kuhusu kauli yaMwenyezi Mungu: **"Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli."** Amesema: Ni kuwa pamoja

na Ali (as). Na akasema tena: Ameandika Ibn Asakir kutoka kwa Abi Ja'far (as) kuhusu kauli:**"Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli."** Amesema: "Ni kuwa pamoja na Ali bin Abu Talib (as)."

Kauli ya Mwenyezi Mungu: **"Basi waulizeni wenye ukumbusho kama nyinyi hamjui:"**

**Tafsiri ya Ibn Jarir Tabari Juz. 17, uk. 5:**

Amepokea kwa sanad yake kupitia kwa Jabir al-Ja'afiy, amesema: "Wakati ilipoteremshwa: **"Basi waulizeni wenye ukumbusho kama nyinyi hamjui."** Ali (as) alisema: "Sisi ndio wenye kujua."

Kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **"Na ni tangazo kutokana na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake kwa wote siku ya Hija Kubwa:"**

**ad-Durul-Manthur ya as-Suyutiy mwishoni mwa tafsiri ya aya tukufu iliyoko mwanzoni mwa Sura Tawba:**

Amesema: Ameandika Ibn Abi Hatim kutoka kwa Hakim bin Hamid amesema: "Aliniambia Ali bin Husain (as): 'Hakika katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu kuna jina la Ali (as) lakini hakuna anayejua.' Nikamuuliza ni lipi hilo? Akajibu: 'Je haujasikia kauli ya Mwenyezi Mungu:**"Na ni tangazo kutokana na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake kwa wote siku ya Hija Kubwa?"**Ni yeye na Mwenyezi Mungu ni tangazo.'"

Kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:**"Basi ni kipi baadaye kitacho kukukadhibishia malipo?**

**Taarikh BaghadadJuz. 2, uk. 97:**

Al-Khatib amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas, amesema: "Wakati iliposhushwa Sura Watin kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliifurahia sana mpaka ukabainika kwetu ukubwa wa furaha yake, ndipo tukamuuliza Ibn Abbas baada ya hapo kuhusu tafsiri yake, akasema: 'Ama kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: Watin ni mji wa Sham – Akaendelea kueleza mpaka akasema:**"Basi ni kipi baadaye kitacho kukukadhibishia malipo"**dini ya Ali bin Abu Talib (as).'"

Kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **"Sema: Kwa fadhila ya Mwenyezi Mungu na rehema Yake! Basi nawafurahi kwa hayo. Haya ni bora kuliko hayo wanayoyakusanya."**

**Taarikh Baghadad Juz. 5, uk. 15:**

Al-Khatib amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas, amesema:**"Sema: Kwa fadhila ya Mwenyezi Mungu na rehema yake!"** Fadhila za Mwenyezi Mungu ni Mtume (saw) na rehema zake ni Ali (as)."

Kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:**"Je! Yule tuliyemuahidi ahadi nzuri, tena naye akayapata, ni kama tuliyemstarehesha kwa starehe za maisha ya duniani, na kisha Siku ya Kiyama akawa miongoni mwa wanao hudhurishwa?**

**Tafsiri ya Ibn Jarir Tabari Juz. 20, uk. 62:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Mujahid kuhusu: **'Je! Yule tuliyemuahidi ahadi nzuri, tena naye akayapata, ni kama tuliyemstarehesha kwa starehe za maisha ya duniani, na kisha Siku ya Kiyama**

**akawa miongoni mwa wanaohudhurishwa?'** Amesema: "Iliteremshwa kwa ajili ya Hamza, Ali bin Abu Talib (as) na Abi Jahli."

**Nasema:** Pia Al-Wahidiy ameiandika katika *Asbabun-Nuzul* yakeuk. 255 kwa sanadi itokayo kwa Mujahid, na amesema: "Iliteremshwa kwa ajili ya Hamza, Ali bin Abu Talib (as) na Abi Jahli." Na ameitaja al-Muhibu Tabari katika *Ar-Riyadhun-Nadhrah*Juz. 2, uk. 207 na akasema: "Mujahid amesema: Iliteremshwa kwa ajili ya Hamza, Ali bin Abu Talib (as) na Abi Jahli."

Kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **Je! Yule ambaye Mwenyezi Mungu amemfungulia kifua chake kwa Uislamu, na akawa yuko kwenye nuru itokayo kwa Mola wake Mlezi (ni sawa na mwenye moyo mgumu?) Basi ole wao wenye nyoyo ngumu zisio mkumbuka Mwenyezi Mungu! Hao wamo katika upotofu wa dhaahiri:**

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, uk. 207:**

Amesema: Miongoni mwa Aya zilizoteremshwa ili kuzungumzia fadhila za Ali (as) ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:**"Je! Yule ambaye Mwenyezi Mungu amemfungulia kifua chake kwa Uislamu, na akawa yuko kwenye nuru itokayo kwa Mola Wake Mlezi (ni sawa na mwenye moyo mgumu?) Basi ole wao wenye nyoyo ngumu zisizomkumbuka Mwenyezi Mungu! Hao wamo katika upotofu wa dhaahiri."** Imeteremshwa Aya hii kwa ajili ya Ali (as), Hamza, Abi Lahbi na watoto zake. Ali (as) na Hamza Mwenyezi Mungu amewafungulia vifua vyao kwa Uislamu, ama Abi Lahbi na watoto zake nyoyo zao zimekuwa ngumu.

— Amesema tena: Ameitaja Al-Wahidiy na Abu Faraji.

**Nasema:** Hadithi iliyotajwa nimeikuta ndani ya kitabu *Asbabun-Nuzul* cha Al-Wahidiy ikiwa kwa lafudhi ile ile kama iliyotajwa hapa.

Kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **Na baina ya makundi mawili hayo patakuwapo pazia. Na juu ya Mnyanyuko patakuwa watu watakao wajua wote kwa alama zao, na wao watawaita watu wa Peponi: Assalamu Alaykum, Amani juu yenu! Wao bado hawajaingia humo, lakini wanatumai:**

**As-Sawa'iqul-MuhriqahUk. 101**

Amesema: Aya ya kumi na tatu ni kauli yaMwenyezi Mungu Mtukufu:"**Na juu ya Mnyanyuko patakuwa watu watakao wajua wote kwa alama zao,**"Amesema: Ameandika Tha'alabiy kutoka kwa Ibn Abbas katika tafsiri ya aya hii kuwa hakika yeye alisema:"A'araf ni sehemu iliyonyanyuka katika njia, ambapo watakuwepo hapo Hamza, Ali bin Abu Talib (as) na Ja'far Dhul-Janahayni, na watawatambua wale waliowapenda (duniani) kwa alama ya kuwa na nyuso nyeupe, na watawatambua wale waliowachukia kwa alama ya kuwa na nyuso nyeusi."

Kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **"Miongoni mwa Waumini wapo watu waliotimiza waliyoahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata kidogo."**

**As-Sawa'iqul-MuhriqahUk.80:**

Amesema: Aliulizwa Ali (as) akiwakwenye mimbari ya huko Kufa kuhusu kauli yaMwenyezi Mungu Mtukufu: **"Miongoni mwa Waumini wapo watu waliotimiza waliyoahidiana na Mwenyezi Mun-**

**gu. Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata kidogo."**Akasema: "Ewe Mwenyezi Mungu, umeteremsha hii aya kama msamaha kwangu na ami yangu Hamza na mtoto wa ami yangu Ubayda bin Harith bin Abdul-Muttalib. Ama kuhusu Ubayda yeye amekufa shahid siku ya vita vya Badri, na Hamza amekufa shahid siku ya vita vya Uhudi, ama mimi namngojea muovu kushinda watu wote wa ummah huu ambaye atazilowanisha hizi kwa damu." Akawa ameashiria ndevu zake na kichwa chake kwa mkono wake. Akasema: "Ni ahadi aliyoniahidi Abul-Qasim (saww)."

**Nasema:** Ameitaja Shabalanjiy ndani ya *Nurul-Abswari*uk. 97 kwa kunukuu kutoka kwenye *al-Fusulul-Muhimmah* ya Ibn as-Swabagh.

Kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **"Na aliyeileta Kweli na akaithibitisha - hao ndio wachamngu:"**

**ad-Durul-Manthur ya as-Suyutiy mwishoni mwa tafsiri ya aya tukufu iliyoko katika Sura az-Zumar:**

Amesema: Ameandika Ibn Mardawayhi kutoka kwa Abu Huraira kuhusu:**"Na aliye ileta Kweli,"**amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: **'Na akaithibitisha'**huyo ni Ali bin Abu Talib (as).

Kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **"Anaziendesha bahari mbili zikutane; Baina yao kipo kizuizi, zisiingiliane. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha? Katika hizo bahari mbili zinatoka lulu na marijani:**

**ad-Durul-Manthur ya as-Suyutiy mwishoni mwa tafsiri ya aya tukufu: "Anaziendesha bahari mbili zikutane" iliyoko katika Sura Rahman:**

Amesema: Ameandika Ibn Mardawayhi kutoka kwa Ibn Abbas kuhusu kauli yake Mtukufu:**'Anaziendesha bahari mbili zikutane'**, alisema: "Ni Ali na Fatimah (as), **Baina yao kipo kizuizi, zisiingiliane.** Ni Mtukufu Mtume (saww), **Katika hizo bahari mbili zinatoka lulu na marijani**. Ni Hasan na Husain (as)." - Na akasema tena: Ameandika Ibn Mardawayhi kutoka kwa Anas bin Maliki kuhusu kauli yake Mtukufu:**'Anaziendesha bahari mbili zikutane,'** alisema: "Ni Ali na Fatimah (as), **Katika hizo bahari mbili zinatoka lulu na marijani**. Ni Hasan na Husain (as)."

**Nurul-Abswar ya Shablanjiy Uk. 101:**

Amesema: Imepokewa kutoka kwa Anas bin Maliki kuhusu kauli Yake Mtukufu:**'Anaziendesha bahari mbili zikutane'**, alisema: "Ni Ali na Fatimah (as), **Katika hizo bahari mbili zinatoka lulu na marijani**. Ni Hasan na Husain (as)." – Amesema: Ameipokea mwandishi wa kitabu cha *ad-Duraru*.

Kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **"Ila wale walioamini, na wakatenda mema:"**

**ad-Durul-Manthur ya as-Suyutiy katika tafsiri ya Sura Wal-Asri:**

Amesema: Ameandika Ibn Mardawayhi kutoka kwa Ibn Abbas kuhusu kauli yake Mtukufu: **"Naapa kwa Zama! Hakika binadamu bila ya shaka yumo katika khasara."** Yaani ni Aba Jahli bin Hisham. **"Ila wale walio amini, na wakatenda mema."**Hapa amemtaja Ali (as) na Salman.

Kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **"Je! Wanadhani wanaotenda maovu kuwa tutawafanya kama walioamini, na wakatenda mema, sawa sawa uhai wao na kufa kwao? Ni hukumu mbaya wanayoihukumu:"**

**Tafsirul-Kabiir ya Fakhru Razi mwishoni mwa tafsiri ya aya tukufu iliyoko katika Sura al-Jathiyah:**

Amesema: al-Kalbiy amesema: "Imeteremshwa aya hii kwa ajili ya Ali (as), Hamza, Ubaydah na watu watatu miongoni mwa mushirikina, nao ni: Utbah, Shaybah na Walid bin Utbah. Wao waliwaambia waumini: 'Wallahihakika nyinyi hamna chochote, laiti hicho mnachosema kingekuwa cha kweli basi hali zetu Akhera zingekuwa bora zaidi kuliko nyinyi, kama zilivyo hali bora hapa duniani kuliko ninyi.' Ndipo Mwenyezi Mungu akawakanusha kwa maneno yao hayo, na akabainisha kuwa haiwezekani hali ya muumini mwenye kumtii Mola Wake na daraja la thawabu la mashukio ya watu wema kuwa sawa na hali ya kafiri mwenye kumuasi Mola Wake."

Kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **"Naye ndiye aliyemuumba mwanaadamu kutokana na maji, akamjaalia kuwa na nasaba na ushemeji. Na Mola Wako Mlezi ni Muweza:**

**Nurul-Abswar ya Shablanjiy Uk. 102:**

Amesema: Imepokewa kutoka kwa Muhammad bin Sirin kuhusu kauli yake Mtukufu: **"Naye ndiye aliyemuumba mwanaadamu kutokana na maji, akamjaalia kuwa na nasaba na ukwe."** Amesema: Iliteremshwa kwa ajili ya Mtume (saww) na Ali bin Abu Talib (as), kwani yeye ni mtoto wa ami yake (saww) na ni mume wa binti yake Fatimah (as), hivyo wakawa na mahusiano ya kinasaba na kiukwe.

## MLANGO WENYE KUELEZEA AYA AMBAZO ZIMETEREMSHWA KWA AJILI YA MAADUI WA ALI (AS)

**al-Kashaf ya Zamakhshariy katika tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:"Na wale wanaowaudhi Waumini wanaume na wanawake pasina wao kufanya kosa lolote, bila ya shaka wamebeba dhulma kubwa na dhambi zilizo dhahiri"iliyoko katika SuraAhzab:**

Amesema hivi: Pamesemwa: "Imeteremshwa kwa ajili ya wanafiki ambao walikuwa wakimuudhi na kumsema vibaya Ali (as)."

al-Wahidiy amesema hivi katika *Asbabun-Nuzul*uk. 273: Muqaatil amesema: "Imeteremshwa kwa ajili ya Ali bin Abu Talib (as) kwa sababu kulikuwa na watu katika wanafiki wakimuudhi kwa kumsema vibaya."

**al-Kashaf ya Zamakhshariy katika tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu "Kwa hakika wale waliokuwa wakosefu walikuwa wakiwacheka walioamini.' Iliyoko katika Sura Mutafifina:**

Amesema: Na imesemwa kuwa: "Siku moja Ali bin Abu Talib (as) alipita katika mkusanyiko wa Waislamu, mara wanafiki wakamdhihaki kwa kumcheka na kumsema vibaya na wakarejea kwa jamaa zao huku wakisema: 'Leo tumemuona kipara.' Na wale wakamcheka, hivyo kabla ya Ali (as) hajafika kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ikateremka aya."

**Nasema:** Pia Fakhru Razi amekitaja kisa hiki katika tafsiri yake al-Kabiir.

**ad-Durul-Manthur ya as-Suyutiy katika tafsiri ya Sura Muhammad, na pia huitwa Sura ya mapigano, katika tafsiri ya kauli yake Mtukufu: "Kwa hakika wanaorudi nyuma baada ya kwishawabainikia uwongofu, Shetani huyo amewashawishi na amewaghuri. –mpaka- Je! Wenye maradhi**

**nyoyoni mwao wanadhani kwamba Mwenyezi Mungu hatazidhihirisha chuki zao? Na tungeli penda tungelikuonyesha hao na ungeliwatambua kwa alama zao; lakini bila ya shaka utawajua kwa namna ya msemo wao. Na Mwenyezi Mungu anavijua vitendo vyenu:**

Amesema: Ameandika Ibn Mardawayhi na Ibn Asakir kutoka kwa Abi Said al-Khudriy kuhusu kauli Yake Mtukufu:**“bila ya shaka utawajua kwa namna ya msemo wao.”**Ni kwa kumbughudhi kwao Ali bin Abu Talib (as).

## MLANGO UNAOSEMA: HAKIKA MWENYEZI MUNGU AMEUPUNGUZIA UMMAH HUU KWA KUWAONDOSHEA (WAJIBU) WA SADAKA YA MAZUNGUMZO YA SIRI KUPITIA ALI (AS)

**Sahihi Tirmidhiy Juz. 2, uk. 227, katika milango ya tafsiri ya Qur’ani:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ali bin Abu Talib (as), amesema: “Wakati ilipoteremka: **“Enyi mlioamini! Mnaposema siri na Mtume, basi tangulizeni sadaka kabla ya kusemezana kwenu. Hiyo ni kheri kwenu na usafi zaidi. Na ikiwa hamkupata cha kutoa, basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.”**Mtukufu Mtume (saww) aliniambia: ‘Unaonaje ikiwa ni dinari?’Nikasema hawataweza, akaniuliza: ‘Je ikiwa ni nusu yake?’ Nikajibu hawataweza, akaniuliza tena: ‘Basi unaona ni kiasi gani?’ Nikamjibu *shairi*, akasema: ‘Hakika wewe si mwenye mali.’ Ndipo ikashuka Aya:**“Mnachelea kutanguliza hiyo sadaka kabla ya kusemezana kwenu?”**Hivyo kupitia kwanguMwenyezi Mungu ameupunguzia ummah huu.”

Tirmidhiy amesema: Maana ya kauli yake: *Shairi*ni ujazo wa dhahabu.

**Nasema:** Pia Fakhru Razi ameitaja hadithi hii katika tafsiri yake *al-Kabiir*mwishoni mwa tafsiri ya aya hii iliyoko katika Suraal-Mujadilah, na amesema kuhusu makusudio ya kauli ya Mtume (saww): ‘Hakika wewe si mwenye mali.’ “Maana yake wewe ni mwenye mali chache hivyo umekadiria kulingana na hali yako. Nayo ni hadithi nzuri.”

Na pia amepokea Ibn Jarir Tabari katika *Tafsiir* yake Juz. 28, uk. 15, na pia al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzul-Ummal*Juz. 1, uk.268, na akasema: “Ibn Abi Shaybah, Abdu bin Hamid, Abu Ya’ala, Ibn Jarir, Ibn al-Mundhir, Dawraqiy, Ibn Haban, Ibn Mardawayhi na Said bin Mansuri, wote wameiandika hadithi hii.”

Pia Muhibu Tabari ameitaja katika *Dhakhair*yake uk. 109 na amesema: “Ameiandika Abu Hatim.”Na as-Suyutiy pia ameitaja katika *Durul-Manthur* katika tafsiri ya aya hii ya Suraal-Mujadilah, na wanazuoni wengi wa hadithi wameitaja hadithi hii, miongoni mwao ni al-Mutaqiy ambaye ameitaja katika *Kanzul-Ummal* na majina yao yamekwisha tangulia kutajwa, yao na ya wengineo, na akasema:“Hakika wote hao wamepokea hadithi hiyo.”

**Khasa’isun-NasaiyUk. 39:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ali (as), amesema: “Wakati ilipoteremka:**‘Enyi mlioamini! Mnaposema siri na Mtume, basi tangulizeni sadaka kabla ya kusemezana kwenu. Hiyo ni kheri kwenu na usafi zaidi. Na ikiwa hamkupata cha kutoa, basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.’**Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Ali (as):‘Waamrishe (waumini) watoe sadaka.’ Ali akamuuliza: ‘Ni kiasi gani ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?’ Akajibu ni dinari, akasema (as):

'Hawataweza.' Akasema (saww): 'Basi nusu ya dinari.' Akamjibu tena 'Hawataweza.' Akasema (saww): 'Basi ni kiasi gani?' Akamjibu:'*Shairi*.' Ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia:'Hakika wewe si mwenye mali.' Na ndipoMwenyezi Mungu akateremsha Aya hii:**'Mnachelea kutanguliza hiyo sadaka kabla ya kusemezana kwenu?'**HivyoAli (as) alikuwa akisema: 'Ummah huu umepunguziwa (wajibu) kupitia kwangu.'"

## MLANGO UNAOELEZEA KUWA HAKUNA YEYOTE ALIYEIFANYIA KAZI AYA YA MAZUNGUMZO YA SIRI ISIPOKUWA ALI (AS)

**Tafsir Ibn Jarir Tabari Juz. 28, Uk. 14:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Laith na Mujahid, amesema: "Ali (as) amesema: 'Hakika ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu kuna Aya ambayo hakuna yeyote aliyeifanyia kazi kabla yangu na hakuna atakayeifanyia kazi baada yangu, nayo ni: **'Enyi mlioamini! Mnaposema siri na Mtume, basi tangulizeni sadaka kabla ya kusemezana kwenu.'** Ilifaradhishwa (kutoa sadaka) kisha ikafutwa."

Nasema: Zamakhshariy pia ameitaja katika *al-Kashaf* katika tafsiri ya aya hii iliyoko katikaSura al-Mujadilah, na mwisho akasema: "Nilikuwa na dinari nikaichenji, hivyo nikawa kila ninapozungumza naye kwa siri natoa dirhamu moja." Kisha akasema: "Amesema al-Kalbiy: 'Alitoa sadaka kwa maneno kumi ambayo alimuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).'"

Pia Al-Wahidiy ameitaja katika *Asbabun-Nuzul*uk.308, na amesema humo: "Nilikuwa na dinari nikaiuza, na nikawa kila ninapozungumza kwa siri na Mtume natoa sadaka dirhamu moja mpaka zikaisha, na ndipo ikafutwa kwa Aya: **'Mnachelea kutanguliza hiyo sadaka kabla ya kusemezana kwenu?'**"

Fakhru Razi pia ameitaja katika tafsiri yake na mwisho akasema: "Na amepokea Ibn Jarir na al-Kalbiy na Atwau kutoka kwa Ibn Abbas kuwa amesema: 'Hakika wao (maswahaba) walikatazwa kuongea siri na (Mtume) mpaka watoe sadaka, hakuna aliyeitikia wito huo isipokuwa Ali (as) ambaye alitoa sadaka dinari kisha ikaruhusiwa (kuongea naye siri bila kutoa sadaka).'"

Pia amepokea Ibn Jarir katika Juz. 28, uk.14 kwa njia nyingine kutoka kwa Laith, kutoka kwa Mujahid, amesema: "Nilikuwa na dinari nikaichenji na kupata dirhamu kumi, ikawa kila ninapokwenda kwa Mtume (saww) natoa sadaka dirhamu moja, ndipo ikafutwa. Hakuna yeyote aliyeifanyia kazi kabla yangu: **'Enyi mlioamini! Mnaposema siri na Mtume, basi tangulizeni sadaka kabla ya kusemezana kwenu.'**"

**Tafsir Ibn Jarir Tabari Juz. 28, uk. 14:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abi Najih kutoka kwa Mujahid kuhusu kauli yake:**'Enyi mlioamini! Mnaposema siri na Mtume, basi tangulizeni sadaka kabla ya kusemezana kwenu.'** Amesema: "Walikatazwa kusema siri na Mtume (saww) mpaka watoe sadaka. Hakuna mtu yeyote aliyeitikia wito huo isipokuwa Ali bin Abu Talib (as), yeye alitoa sadaka ya dinari kisha ikateremka rukhsa."

Nasema: Pia ameipokea katika njia nyingine kwa tofauti ndogo ya lafidhi kutoka kwa Ibn Abi Najih.

**ad-Durul-Manthur ya as-Suyutiy mwishoni mwa tafsiri ya aya tukufu: "Enyi mlioamini! Mnaposema siri na Mtume, basi tangulizeni sadaka kabla ya kusemezana kwenu.' iliyoko katika Sura al-Mujadilah:**

Amesema: Said bin Mansur, Ibn Rahawayhi, Ibn Abi Shaybah, Abdu bin Hamid, Ibn Mundhir, Ibn Abi Hatim, Ibn Mardawayhi na al-Hakim ambaye kasema ni hadithi sahihi. Wote wameandika kutoka kwa Ali (as) kuwa alisema: "Hakika katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu kuna Aya ambayo hajaifanyia kazi mtu yeyote kabla yangu wala baada yangu, nayo ni aya ya mazungumzo ya siri: **'Enyi mlioamini! Mnaposema siri na Mtume, basi tangulizeni sadaka kabla ya kusemezana kwenu.'** Nilikuwa na dinari moja nikaiuza kwa dirhamu kumi, na nikawa kila ninapozungumza siri na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) natoa dirhamu moja, kisha ikafutwa amri hii. Hakuifanyia kazi mtu yeyote zaidi yangu, na ndipo ikashuka: "**Mnachelea kutanguliza hiyo sadaka kabla ya kusemezana kwenu?'"**

Nasema: Pia al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzul-Ummal* Juz. 1, uk. 268, na maimamu wengi wa hadithi wameitaja, ambao As-Suyutiy amewataja katika *Durul-Manthur* na majina yao yameshatangulia, na amesema kuwa hakika hao wameipokea. Na pia al-Muhibu Tabari ameipokea katika *Riyadhun-Nadhirah* Juz. 2, uk. 200 na akasema: "Ameiandika Ibn Jawziy katika *Asbabun-Nuzul*. Na akasema tena: Abdul-Razak, Abdu bin Hamid, Ibn Mundhir, Ibn Abi Hatim, Ibn Mardawayhi, wote wameiandika kutoka kwa Ali (as) kuwa: "Hajawahi mtu yeyote kuifanyia kazi isipokuwa mimi mpaka ilipofutwa, na haikudumu isipokuwa saa." Yaani Aya ya mazungumzo ya siri.

Na akasema tena: Abdu bin Hamid, Ibn Mundhir, Ibn Abi Hatim, wote wameiandika kutoka kwa Mujahid, amesema: "Walikatazwa kuongea siri na Mtume (saww) mpaka watoe kwanza sadaka. Hakuna aliyeongea naye kwa siri isipokuwa Ali bin Abu Talib (as), hakika yeye alikuwa na dinari akaitoa sadaka, kisha akaongea siri na Mtume (saww) na akamuuliza mambo kumi, kisha ikateremka rukhsa."

Na akasema tena: Said bin Mansur ameandika kutoka kwa Mujahid, amesema: "Ilikuwa mwenye kutaka kuongea siri na Mtume ni lazima atoe sadaka ya dinari, na wa mwanzo kufanya hivyo alikuwa ni Ali bin Abu Talib (as) kisha ikateremka rukhsa: **'Na ikiwa hamkupata cha kutoa, basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.'"** Na akasema tena: Abdu bin Hamid ameandika kutoka kwa Salma bin Kahil, amesema: **"Aya: 'Enyi mlioamini! Mnaposema siri na Mtume, basi tangulizeni sadaka kabla ya kusemezana kwenu.'** Wa mwanzo aliyetekeleza amri hii alikuwa ni Ali (as) kisha ikafutwa."

**Kanzul-Ummal Juz. 3, Uk. 155:**

Amesema: Kutoka kwa A'mir bin Wathilah amesema: "Nilikuwa nimesimama mlangoni siku ya Shura na mara sauti zikasikika baina yao, ndipo nilipomsikia Ali (as) akisema: 'Watu wametoa kiapo cha utii kwa Abu Bakr, na naapa kwa Mwenyezi Mungu mimi ninastahiki zaidi jambo hili na nina haki kuliko yeye.' - aliendelea mpaka aliposema: kisha akasema: 'Nawaapisheni nyote kwa Mwenyezi Mungu, enyi watu, je kwenu nyinyi mna yeyote mwenye udugu na Mtume (saww) asiyekuwa mimi?' Wakajibu: 'Ewe Mola Wetu hakuna.' Akauliza tena: 'Je kwenu kuna yeyote aliyeongea siri na Mtume (saww) mara kumi na mbili zaidi yangu mpaka Mwenyezi Mungu akasema: **"Enyi mlioamini! Mnaposema siri na Mtume, basi tangulizeni sadaka kabla ya kusemezana kwenu.'** Wakajibu: 'Ewe Mola hakuna.'"

Imebaki hadith moja inayofaa kutajwa mwishoni mwa mlango huu, nayo ni ile aliyoipokea Zamakhshariy katika *al-Kashaf* katika tafsiri ya Aya 'Mazungumzo ya siri' iliyopo katika Sura Al-Mujadilah, amesema: "Imepokewa kutoka kwa Ibn Umar amesema: 'Ali (as) alikuwa na mambo matatu, kuwa na

moja kati ya hayo ni jambo ninalotamani zaidi kuliko neema zote, nayo ni: Kumuoa kwake Fatimah, kukabidhiwa bendera siku ya Khaibari na Aya ya kuongea siri na Mtume."

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA CHEO CHA ALI (AS) KWA MTUME (SAWW)

**Sahihi an-Nasaiy Juz. 1, Uk. 171:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Nujiyyu kutoka kwa baba yake, amesema: "Ali (as) aliniambia: Nilikuwa na cheo mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ambacho hajawahi kuwa nacho yeyote katika viumbe. Nilikuwa nikimwendea kila usiku nikimwambia: 'Asalam Alayka ewe Nabii wa Allah.' Akiguna naondoka na kurudi kwangu, na kama sivyo naingia kwake."

**Nasema:** Pia ameipokea katika *Khasa'is* yake uk. 30, na amepokea tena kwa maana inayokaribiana na hiyo katika uk. 29 na uk. 30, na pia ameipokea Imam Ahmad bin Hanbal katika *Musnad* yake Juz. 1, uk. 85.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 393:**

Amesema: Imepokewa kutoka kwa Sha'abiy, amesema: "Siku moja Abu Bakr alimuona Ali (as) na akasema: 'Yeyote mwenye kupenda kumuangalia mbora wa watu mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na aliye karibu naye zaidi na aliyemshiba sana Nabii wake, basi naamwangalie huyu..." Mpaka mwisho wa hadith. – Amesema: Ameiandika Ibn Abi Dun'ya katika kitabu *Al-Ashraf*, na Ibn Mardawayhi na al-Hakim.

**Nasema:** Pia al-Muhibu Tabari ameitaja katika *Riyadhun-Nadhirah* Juz. 2, uk. 163, amesema: "Ameiandika Ibn as-Saman, pia Ibn Hajar ameitaja katika *Sawa'iq* yake katika uk. 106 na akasema: 'Ameiandika ad-Dar al-Qutniy kutoka kwa Sha'abiy.'"

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, Uk. 213, na Kanzul-Ummal Juz. 6, Uk. 402:**

Wamesema wawili hao: "Kutoka kwa Abdullah bin Harith, amesema: Nilimuuliza Ali bin Abu Talib: Hebu niambie ni kipi cheo bora kabisa ulichonacho kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)? Akajibu: 'Siku moja wakati mimi nikiwa nimelala kwake na yeye akiwa anaswali, alipomaliza Swala yake alisema: Ewe Ali sijamuomba Mwenyezi Mungu kheri yoyote isipokuwa nimekuombea na wewe ile ile, na sijajilinda kwa Mwenyezi Mungu na shari yoyote isipokuwa nimemuomba akulinde na wewe na ile ile.'" – Wao wawili wamesema: "Ameiandika al-Muhamiliy.

**Nasema:** Pia al-Haythamiy ameitaja katika *Majmau* yake Juz. 9, uk. 110, na amesema mwishoni: "Wala sijamuomba Mwenyezi Mungu kitu isipokuwa amenipa, ila Yeye ameniambia kuwa hakuna Nabii baada yangu."

Al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzul-Ummal* Juz. 6, uk. 159, na katika uk. 392, na amesema katika kurasa hizo mbili: "Ameiandika Abu Nai'm katika *Fadhailus-Sahabah*." Na katika uk. 406 ameitaja na kusema: "Ameiandika Ibn Abi A'swim na Ibn Jarir na kusema ni hadithi sahihi, na pia kaiandika Tabaraniy katika *al-Awsat* na Ibn Shahin, na pia ameipokea an-Nasaiy katika *Khasa'is* yake kwa njia mbili, katika uk. 37 na uk. 38."

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, Uk. 164:**

Amesema: Baada ya siku sita tangu kufa kwa Mtume (saww) walikuja Abu Bakr na Ali (as) kulizuru kaburi lake, Ali (as) alimwambia Abu Bakr: 'Tangulia.' Abu Bakr akajibu: "Siwezi kumtangulia mtu ambaye nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema: 'Cheo alichonacho Ali kwangu mimi ni sawa na cheo nilichonacho mbele ya Mola Wangu.'" – Amesema: Ameiandika Ibn as-Samaan katika *al-Muwafaqah*.

**Nasema:** Pia Ibn Hajar ameitaja katika *Sawa'iq* yake, katika uk. 106.

**Taarikh Baghdad Juz. 6, Uk. 12:**

Amesema: Kutoka kwa al-Barau, kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), amesema: "Ali kwangu mimi ni sawa na kichwa changu katika mwili wangu."

**Nasema:** Pia Shablanjiy ameitaja katika *Nurul-Abswar* uk. 72, na amesema: "Ameiandika ad-Daylamiy kutoka kwa Ibn Abbas." Naye Ibn Hajar ameitaja katika *Sawa'iq* yake uk. 75, na pia al-Munawi kaiandika katika *Faydhul-Qadir* Juz. 4, uk. 357, na hao wawili wamesema: "Kutoka kwa al-Khatib kutoka kwa al-Barau kutoka kwa ad-Daylamiy, kutoka kwa Ibn Abbas."

**Mustadrakus-Sahihain Juz. 3, Uk. 130:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ummu Salamah, amesema: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipokuwa na hasira hakuna yeyote miongoni mwetu aliyeweza kumkaribia na kuzungumza naye isipokuwa Ali bin Abu Talib (as)." Kisha akasema: Hii ni hadithi yenye njia (sanadi) sahihi.

**Nasema:** Na pia Abu Nai'im ameipokea katika *Hilyat* Juz. 9, uk. 227, na al-Munawi ameitaja katika *Faydhul-Qadir* katika Juz. 5, uk. 150 katika matni, na akasema pia katika ufafanuzi: "Tabaraniy ameipokea kutoka kwa Ummu Salamah."

**Al-Isabah cha Ibn Hajar Asqalaniy Juz. 1, Sehemu ya nne, uk. 217:**

Ameitaja hadith hii kutoka kwa Khatib katika *al-Muutalaf*, ameipokea kwa njia yake kutoka kwa Anas bin Malik, amesema: "Tulikuwa tunapotaka kumuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) chochote tunamuamrisha Ali (as) au Salman au Thabit bin Muadh, kwani wao walikuwa Maswahaba jasiri zaidi kwake."

**Sahihi Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 299:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdul-Rahman bin Abdullah, amesema: "Ali (as) alisema: 'Nilikuwa ninapomuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hunijibu, na ninapokaa kimya hunianza yeye.'"

**Nasema:** Hiki ni cheo kikubwa alichokuwa nacho Ali (as) mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ambacho hajapata kuwa nacho yeyote katika Sahaba isipokuwa yeye. Na ameipokea hadith hii Tirmidhiy katika mlango huu kwa njia mbili nyingine. Na pia al-Hakim ameipokea katika *Mustadrak* yake Juz. 3, uk. 125, na al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzul-Ummal* Juz. 6, uk. 394 akinukuu kutoka kwa Ibn Abi Shaybah, Tirmidhiy, Shashiy, Abu Na'im katika Hilyat, ad-Dawraqiy, Ibn Asakir, Said bin Mansur, na pia ameipokea an-Nasaiy katika *Khasa'is* yake uk. 30 kwa njia tofauti.

**Tabaqat Ibn Saad Juz. 2, Sehemu ya pili, Uk. 101:**

Amesema: Ali (as) aliambiwa: 'Kwa nini wewe ndiye mwenye hadith nyingi kuliko Maswahaba wote wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)?' Akajibu: "Hakika mimi nilikuwa ninapomuuliza swali hunijibu na nikikaa kimya hunianza."

**Nasema:** Pia ameipokea katika uk. 106 na akasema humo: "Na tukamuuliza: 'Hebu tuambie kuhusu wewe ewe Amirul-Muuminin.' akasema: 'Mnataka hilo tu, nilikuwa ninapouliza hujibiwa na nikikaa kimya huanzwa.'" Na pia amepokea kwa tamko hili Abu Na'im katika *Hilyat* Juz. 1, uk. 68 na katika Juz. 4, uk. 382.

**Tafsirul-Kabir cha Fakhru Razi, mwishoni mwa tafsiri ya kauli tukufu: "Na neema za Mola Wako Mlezi zisimlie.' iliyoko katika Sura adh-Dhuha:"**

Ametaja hadithi, amesema: Wakamwambia - yaani Ali Amirul-Muuminin: "Hebu tuambie kuhusu wewe." Akasema: "Hapana, Mwenyezi Mungu amekwisha kataza mtu kujitakasa." Akaambiwa: "Je Mwenyezi Mungu si anasema: 'Na neema za Mola Wako Mlezi zisimlie.'" Akasema: "Basi mimi nazisimulia, nilikuwa ninapouliza hujibiwa na nikikaa kimya huanzwa, na kifuani nina elimu zote basi niulizeni."

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA KAULI YA MTUKUFU MTUME (SAWW) KWA ALI (AS): CHEO CHAKO KWANGU MIMI NI SAWA NA CHA HARUN KWA MUSA

**Sahihi Bukhari, Kitabu cha mwanzo wa uumbaji, mlango wa fadhila za Ali bin Abu Talib (as):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibrahim bin Said, kutoka kwa baba yake, amesema: Alisema Mtume (saww) kumwambia Ali (as): "Ama huridhii kuwa cheo chako kwangu mimi ni sawa na cha Harun kwa Musa?"

**Nasema:** Pia Muslim ameipokea katika Sahih yake katika kitabu cha fadhila za Maswahaba kwenye mlango wa fadhila za Ali bin Abu Talib (as). Na pia Ibn Majah katika *Sahih* yake uk. 12, na Ahmad bin Hanbal katika *Musnad* yake Juz. 1, uk. 174, na Abu Daud at-Twayalasiy katika *Musnad* yake Juz. 1, uk. 28, na Abu Na'im katika *Hilyat* Juz. 7, uk. 194, na pia an-Nasaiy katika *Khasa'is* yake, yeye ameipokea katika njia mbili, katika uk. 15 na uk. 16.

**Sahihi Bukhari, Kitabu cha mwanzo wa uumbaji, mlango wa vita vya Tabuk:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Mus'ab bin Saad kutoka kwa baba yake, amesema: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipotoka kwenda Tabuk alimuacha Ali (as), ndipo Ali akamuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): 'Unaniacha pamoja na watoto na wanawake?' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: 'Je, huridhii kuwa cheo chako kwangu mimi ni sawa na cha Harun kwa Musa? Isipokuwa hakuna Nabii baada yangu.'"

**Nasema:** Ameipokea pia Muslim katika *Sahih* yake katika kitabu cha fadhila za Maswahaba kwenye mlango wa fadhila za Ali bin Abu Talib (as). Na ameipokea Abu Daud at-Twayalasiy katika *Musnad* yake Juz. 1, uk. 29, na pia ameipokea kwa njia mbali mbali Abu Na'im katika *Hilyat* Juz. 7, uk. 195

na katika uk. 196. Na ameipokea at-Twahawiy katika *Mushkilul-Athaar* Juz. 2, uk. 309, na Ahmad bin Hanbal katika *Musnad* yake Juz. 1, uk. 182, na al-Khatib al-Baghdadiy katika *Taarikh* yake kwa njia mbili katika Juz. 11, uk. 432, na an-Nasaiy katika *Khasa'is* yake uk. 16.

**Sahihi Muslim, kitabu cha fadhila za Maswahaba, mlango wa fadhila za Ali bin Abu Talib (as):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Said bin Musayyab, kutoka kwa Aamir bin Saad bin Abi Waqas, kutoka kwa baba yake, amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Ali (as): "Wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu." Akasema Said: "Nilitamani nimuulize Saad kuhusu riwaya hii, nilipoonana naye nikamwambia yale aliyoniambia Aamir, naye akasema: 'Mimi nimeisikia hivyo.' Nikamuuliza: Uliisikia kweli? Basi akaweka vidole vyake viwili kwenye masikio yake na akasema: 'Ndiyo, kama sivyo basi yazibe.'"

**Nasema:** Na Ibn Athir ameipokea katika *Usudul-Ghabah* Juz. 4, uk. 26, na an-Nasaiy katika *Khasa'is* yake uk. 15, na pia amepokea nyingine mfano wa hiyo kutoka kwa Ibrahim bin Saad kutoka kwa baba yake katika uk. 15.

**Sahihi Muslim, kitabu cha fadhila za Maswahaba, mlango wa fadhila za Ali bin Abu Talib (as):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aamir bin Saad bin Abi Waqas, kutoka kwa baba yake, amesema: "Muawiya bin Abi Sufyan alimwamrisha Saad kwa kumwambia: 'Ni lipi lililokuzuia kumtukana Abu Turab?' Akasema: 'Ninapokumbuka mambo matatu aliyoyasema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuhusu yeye, siwezi kumtukana, kwani kuwa na moja kati ya hayo ni jambo ninalotamani sana kuliko ngamia mwekundu. Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akimwambia: 'Hivi huridhii kuwa cheo chako kwangu mimi ni sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu?' – Hiyo ni baada ya kumwacha mjini katika moja ya vita vyake, na Ali kumwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Unaniacha pamoja na wanawake na watoto-'" Hadithi hii imeshatangulia kwa ukamilifu katika mlango wa maapizano.

**Nasema:** Na pia ameipokea Tirmidhiy katika *Sahih* yake Juz. 2, uk. 300, na Ahmad bin Hanbal katika *Musnad* yake Juz. 1, uk. 185, na an-Nasaiy katika *Khasa'is* yake uk. 4 na uk. 16.

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 301:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Said bin Musayyab, kutoka kwa Saad bin Abi Waqas, kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Ali (as): "Wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu." - Amesema: Imepokewa kwa njia zaidi ya moja kutoka kwa Saad kutoka kwa Mtukufu Mtume (saww).

**Nasema:** Na ameipokea Ahmad bin Hanbal katika *Musnad* yake Juz. 1, uk. 179, na Abu Daud at-Twayalasiy katika *Musnad* yake Juz. 1, uk. 29, na Abu Na'im katika *Hilyat* yake Juz. 7, uk. 195, kwa njia nne, na kaipokea tena katika uk, 196 kwa njia ya tano. Na ameipokea al-Khatib al-Baghdadiy katika *Taarikh* yake Juz. 1, uk. 324, na katika Juz. 4, uk. 204, na katika Juz. 9, uk. 364, na pia kaipokea an-Nasaiy katika *Khasa'is* yake kwa njia mbili katika uk. 14, na kwa njia ya tatu katika uk. 15.

**Nasema:** Asqalaniy katika *Fat'hul-Bariy*Juz. 8, uk. 76, baada ya kuitaja hadithi iliyotangulia kutoka kwa Muslim na Tirmidhiy amesema hivi: "Na kwa Abu Ya'ala kuna riwaya imepokewa kutoka kwa Saad kwawajihi mwingine usio na tatizo lolote, amesema:'Laiti ungewekwa msumeno kwenye maungio yangu ili nimtukane Ali (as) basi nisingemtukana kamwe."

Amesema: "Hadithi hii imepokewa kutoka kwa Mtume (saww) kwa njia isiyokuwa ya Saad, ikiwa ni pamoja na hadithi kutoka kwa Umar, Ali mwenyewe, Abu Hurayra, Ibn Abbas, Jabir bin Abdullah, al-Barau, Zayd bin Arqam, Abu Said, Anas, Jabir bin Samrah, Habashiy bin Junadah, Muawiyah, Asmau bint Umays, na wengineo."Anasema tena: "Ibn Asakir amekusanya njia zake zote katika kueleza wasifu wa Ali (as)."

**Sahihi Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 301:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir bin Abdullah kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Ali (as): "Wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu." – Amesema: Na katika mlango huu kuna hadithi kutoka kwa Saad, Zayd bin Arqam, Abu Huraira na Ummu Salamah.

**Nasema:** Na ameipokea Ahmad bin Hanbal katika *Musnad* yake Juz. 3, uk. 338, na al-Khatib al-Baghdadiy katika *Taarikh* yake Juz. 3, uk. 288, kwa njia mbili, amesema katika njia moja: "Isipokuwa hakuna Nabii baada yangu, na kama angekuwepo basi ungekuwa wewe."

**Sahihi Ibn Majah Uk. 12:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Sabit, naye ni Abdur-Rahman, kutoka kwa Saad bin Abi Waqas, amesema: "Muawiya aliporudi kutoka katika moja ya safari zake, Saad aliingia kwake na wakamtaja Ali (as), Muawiya akamshutumu Ali, ndipo Saad akakasirika na akasema: 'Unasema haya kwa mtu ambaye nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake?' Na nilimsikia akisema: 'Wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu.' Na nilimsikia akisema: 'Nitamkabidhi bendera kesho mtu ambaye Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanampenda.'"

**Mustadrakus-Sahihain Juz. 2, Uk. 337:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Hasan bin Saad mtumishi wa Ali (as) kwamba siku moja Mtume alitaka kwenda vitani, akamwita Ja'far na kumwamrisha Ali abaki Madina (kama kiongozi), akasema: "Kamwe sintobaki tena baada yako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu." Ali anasema: "Ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaniita na kuniambia: 'Najua usingebaki kabla sijaongea.'Ndipo nikaanza kulia, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaniuliza: 'Kipi kinachokuliza ewe Ali?' Nikasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Yanayoniliza mimi ni mengi sio jambo moja, Makuraishi watakuja kusema kesho kuwa amefanya haraka kiasi gani kumkhalifu mtoto wa ami yake na kumsaliti. Na jambo jingine linaloniliza ni kwamba nilikuwa nataka kwenda katika jihadi kwa ajili ya njia ya Mwenyezi Mungu, kwani Mwenyezi Mungu anasema:**"Wala hawaendi mahali panapowaghadhibisha makafiri, wala hakiwapati chochote kutokana na maadui, ila huandikiwa kuwa ni kitendo chema. Hakika Mwenyezi Mungu haupotezi ujira wa wanaofanya mema."**Nilikuwa nataka kupata fadhila za Mwenyezi Mungu."

Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Ama kuhusu kauli yako kuwaMakuraishi watasema: 'Amefanya haraka kiasi gani kumkhalifu mtoto wa ami yake na kumsaliti.' kwa hakika wewe una kiigizo kutoka kwangu, kwani walikwishasema: 'Mimi mchawi, ruhanina muongo.' Hivi huridhii kuwa wewe kwangu mimi una cheo sawa na chaHarun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu? Ama kuhusu kauli yako: 'Nataka kupata fadhila za Mwenyezi Mungu.' Basi chukua hivi viungo vya pilipili tumeletewa kutoka Yemen, uza na tumia wewe na Fatima mpaka Mwenyezi Mungu atakapokupeni katika fadhila zake, kwani Madina haifai kuongozwa na yeyote isipokuwa mimi au wewe."

— Al-Hakim amesema: Hii ni hadithi yenye sanad sahihi.

**Nasema:** Na pia As-Suyutiy ameitaja katika *ad-Durul-Manthur* katika tafsiri ya kauli yake Mtukufu: **"Haiwafalii watu wa Madina na Mabedui walio jirani zao kubakia nyuma wasitoke na Mtume…."** iliyopo katika SuraTawbah. Na akasema: "Ameiandika Ibn Mardawayhi kutoka kwa Ali (as)."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 1, Uk. 170:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Aisha binti Saad kutoka kwa baba yake kwamba hakika Ali (as) alitoka pamoja na Mtume (saww) mpaka alipofika Thaniyatul-Widau, huku Ali akiwa analia na kusema: "Unaniacha pamoja na wenye kubaki nyuma." Akasema:"Hivi huridhii kuwa wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna unabii baada yangu."

**Nasema:** Na pia amepokea al-Khatib al-Baghdadiy katika *Taarikh* yake Juz. 8, uk. 52, na an-Nasaiy katika *Khasa'is* yake kwa njia mbili, katika Uk. 16 na uk. 17, na pia As-Suyutiy ameitaja katika *ad-Durul-Manthur* katika tafsiri ya kauli yake Mtukufu: **"Haiwafalii watu wa Madina na Mabedui walio jirani zao kubakia nyuma wasitoke na Mtume…."** iliyopo katika Sura Tawbah. Na akasema: Ameiandika Ibn Mardawayhi kutoka kwa Sa'd bin Abi Waqas na amesema humo: "Hakika Ali bin Abu Talib (as) alitoka pamoja na Mtukufu Mtume (saww) mpaka akafika Thaniyatul-Widai akikusudia kwenda Tabuk..."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 1, Uk. 173:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Said Ibn Musayyab amesema: "Nilimwambia Saad bin Malik: Hakika nataka kukuuliza kuhusiana na hadithilakini naogopa kukuuliza. Akasema: Usifanye hivyo ewe mtoto wa ami yangu, ukiwa unajua ya kuwa mimi nina elimu basi niulize wala usiniogope. Nikasema ni kuhusu kauli ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kumwambia Ali (as) wakati alipomuacha Madina katika vita vya Tabuk. Saad akasema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwacha Ali (as) Madina katika vita vya Tabuk, Ali akamwambia: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, unaniacha pamoja na wanawake na watoto?' Akasema:"Hivi huridhii kuwa wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa." Akasema:"Ndiyo nimeridhia ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu." Ali akarudi haraka, na ni kana kwamba mimi naangalia vumbi la nyayo zake likipepea."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 1, Uk. 175:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Said bin Musayyab amesema: "Nilimwambia Saad bin Malik: Hakika wewe unaonekana ni mtu mwenye juhudi, nami nataka kukuuliza. Akasema ni lipi? Nikasema ni kuhusu hadithi ya Ali (as), akasema: 'Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Ali (as): Hivi huridhii kuwa wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa. Akasema: Ndiyo nimeridhia.'"

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 1, Uk. 177:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Musayyab kutoka kwa Ibn Saad bin Malik kutoka kwa baba yake, amesema: "Niliingia kwa Saad na nikamwambia: 'Kuna hadithi nimehadithiwa kutoka kwako, inaelezea wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipomwacha Ali (as) Madina.' Basi akaghadhibika na kusema: 'Alikuhadithia nani?' Sikupenda kumwambia kuwa alinihadithia mtoto wake na hatimaye akamkasirikia. Kisha alisema: 'Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipotoka kwenda kwenye vita vya Tabuk alimwacha Ali (as) Madina, Ali (as) akasema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu sipendi wewe

utoke kwenda sehemuyoyoteisipokuwa na mimi niwe pamoja nawe.' Akasema: 'Hivi huridhii kuwa wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu?'"

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 1, Uk. 184:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah kutoka kwa Saad, amesema: "Wakati alipotoka Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwenda katika vita vya Tabuk alimuacha Ali (as), ndipo akamuuliza: 'Unaniacha?' Akamjibu: 'Hivi huridhii kuwa wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu?'"

**Nasema:** Pia ameipokea Ibn Said katika *Tabaqat* Juz. 3, Sehemu ya kwanza, uk. 15, na pia an-Nasaiy ameipokea kwa njia mbili katika uk. 17.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 1, Uk. 330:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Amru bin Maymun, amesema: "Wakati nikiwa nimeketi kwa Ibn Abbas mara alijiwa na watu tisa, wakasema: 'Ewe mtoto wa Abbas ima unyanyuke pamoja nasi na ima hawa ulionao watupishe.' Ibn Abbas akasema: 'Bali nanyanyuka pamoja nanyi.' Wakati huo alikuwa bado mzima hajapofuka, walikwenda pembeni na kuanza kuzungumza, na hatujui walizungumza nini. Mara alirudi huku akipukuta nguo yake na kusema: 'Ole wao, ole wao, wanawezaje kumtuhumu mtu mwenye mambo kumi, -ameendelea kusimulia hadithi mpaka aliposema: Mtume akatoka na watu kwenye vita vya Tabuk, Ali (as) akamwambia: 'Je nitoke pamoja nawe?' Nabii wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia hapana, Ali (as) akalia, ndipo Mtume akamwambia: 'Hivi huridhii kuwa cheo chako kwangu ni sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa wewe si Nabii? Hakika haifai mimi kwenda bila ya wewe kuwa khalifa wangu.'" Imeshatangulia hadithi hii kwa ukamilifu katika Mlango unaozungumzia Aya ya Utakaso.

**Nasema:** Pia ameipokea an-Nasaiy ndani ya Khasa'is yake uk. 8, na ameitaja al-Muhibu Tabari ndani ya *ar-Riyadh an-Nadhrah* Juz. 2, uk. 203, na amesema: "Ameiandika kwa ukamilifu wake Ahmad na al-Hafidh Abul-Qasim ad-Damashqiy ndani ya *al-Muwafaqat* na ndani ya *al-Ar'bauna at-Twawali*. "Na Ameiandika an-Nasaiy kwa ufupi na ameitaja al-Haythamiy ndani ya *Maj'mau* yake Juz. 9, uk. 119, na amesema: "Ameipokea Ahmad na Tabaraniy ndani ya *al-Kabir* na ndani ya *al-Awsat* kwa muhtasari.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 6, Uk. 369:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Musa al-Jahniy, amesema: "Niliingia kwa Fatimah binti Ali (as), rafiki yangu Abu Sahli akamwambia: 'Una umri wa miaka mingapi?' Akanijibu: 'Themanini na sita.' Akamuuliza: 'Hujapata kusikia kutoka kwa baba yako chochote?' Akasema: 'Amenihadithia Asmau bint Umays kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Ali (as): Wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu.'"

**Nasema:** Na ameipokea pia kwa njia nyingine kutoka kwa Musa al-Jahniy katika uk.438, pia ameipokea al-Khatib al-Baghdadiy katika *Taarikh* yake Juz. 10, uk.43, na katika Juz. 12, uk. 323. Na ameipokea Ibn Abdul-Bar katika *al-Isti'ab* Juz. 2, uk. 459, na an-Nasaiy katika *Khasa'is* yake kwa njia ambazo baadhi yake ziko katika uk. 17 na nyingine katika uk.18.

**Khasa'isun-Nasaiy Uk.4:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdur-Rahman bin Sabit kutoka kwa Saad, amesema: "Nilikuwa nimekaa mara wakamshutumu Ali bin Abu Talib (as), nikawaambia: Nimekwishamsikia Mtume wa Mwenyezi

Mungu (saww) akisema kuhusu Ali (as) mambo matatu, kuwa na moja tu kati ya hayo ni jambo ninalotamani zaidi kuliko ngamia mwekundu. Nimemsikia akisema: 'Hakika cheo chake (Ali) kwangu mimi ni sawa na cheo cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu.' Na nikamsikia akisema: 'Nitamkabidhi bendera kesho mtu anayempenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanampenda yeye.' Na nikamsikia akisema: 'Ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.'"

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 14:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Said bin Musayyab kutoka kwa Saad bin Abi Waqas, amesema: "Wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipokwenda kwenye vita ya Tabuk alimuacha Ali (as) Madina, wakasema kuhusu hilo: 'Amemchoka na hakupenda kufuatana naye.' Hapo Ali (as) akamfuata Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mpaka akamkuta njiani, akamwambia: 'Ewe Mtume wa Menyezi Mungu! Umeniacha Madina pamoja na watoto na wanawake, mpaka watu wanasema: 'Amemchoka na hakupenda kufuatana naye.' Mtume (saww) akamjibu: 'Ewe Ali hakika nimekuacha uwe kiongozi kwa watu wangu, hivi huridhii kuwa wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu.'"

**Nasema:** Na pia ameipokea katikauk. 14 kwa njia nyingine kwa tofauti ndogo.

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 17:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Harbu bin Salak, amesema: Saad bin Malik alisema: "HakikaMtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikwenda vitani na ngamia wake al-Jad'au na akamuacha Ali (as), ndipo Ali (as) alikuja na kumvuka ngamia, akasema huku akilia: 'Ewe Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu! Makuraishi wanadai kuwa wewe umeniacha kwa kuwa umenichoka na hupendi kusuhubiana na mimi.' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akanadi katikati ya watu: 'Hakuna mtu kati yenu isipokuwa ana haja kwa mtoto wa Abu Talib. Hivi huridhii kuwa wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu?' Ali (as) akasema: 'Nimemridhia Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume wa Mwenyezi Mungu."

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 19:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Hani kutoka kwa Ali (as), amesema: "Wakati tulipotoka Makka mara alikuja binti ya Hamza huku akiita: 'Ewe ami yangu, ewe ami yangu!' Ali (as) akamchukua na kumbeba, akamwambia mkewe: 'Mtunze mtoto wa ami yako.' Naye akamchukua, na ndipo pakatokea mzozo kati ya Ali (as), Zayd na Ja'far (kila mmoja akitaka amtunze yeye), Ali (as) akasema: 'Mimi nimemchukua kwakuwa yeye ni mtoto wa ami yangu.' Akasema Ja'far: 'Ni binti ya ami yangu na mama yake mdogo yuko chini yangu.'Na Zayd akasema:'Ni bintiya ndugu yangu.' NdipoMtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawasuluhisha kwa kumpeleka kwa mama yake mdogo, na akasema: 'Mama mdogo ana nafasi ya mama mzazi.' Na akamwambia Ali: 'Wewe kwangu mimi una cheo sawa na chaHarun kwa Musa, na wewe ni sehemu yangu na mimi ni sehemu yako.'Na akamwambia Ja'far: 'Umefanana namimi kimaumbile na kitabia.'Na akamwambia Zayd: 'Wewe ni ndugu yetu na mtumishi wetu.'"

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 32:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdullah bin Abi Najih kutoka kwa Muawiya, yeye alimtaja Ali (as) na mara Saad bin Abi Waqas akasema: "Naapa kwa Mwenyezi Mungukuwa na moja kati ya mambo

matatu ni jambo nilipendalo zaidi kuliko vyote vinavyochomozewa na jua: Natamani (Mtume) angeniambia mimi alipomwambia (Ali) wakati alipomzuia kwenda Tabuk: 'Hivi huridhii kuwa wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu?'Hili ni jambo nilipendalo kuliko kuwa na vyote vinavyochomozewa na jua. Na natamani (Mtume) angeniambia mimi wakati alipomwambia (Ali) siku ya Khaibar: 'Nitamkabidhi bendera mtu ambaye anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, Mwenyezi Mungu ataleta ushindi kwa mikono yake, naye si mwenye kukimbia vitani.' Hili ni jambo nilipendalo kuliko kuwa na vyote vinavyochomozewa na jua. Na natamani binti yake angekuwa na mimi na nikapata mtoto kutoka kwake. Hili ni jambo nilipendalo kuliko kuwa na vyote vinavyochomozewa na jua."

**Tabaqat Ibn Saad Juz. 3, Sehemu ya kwanza, Uk. 14:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Said, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipokwenda kwenye vita vya Tabuk nakumuacha nyuma Ali (as) kuwa mwangalizi wa watu wake, baadhi ya watu walisema: 'Hakuna kilichomzuia kutoka naye isipokuwa ni kwa sababu hapendi kufuatana naye.' Maneno hayo yakamfikia Ali (as) naye akamueleza Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), naye akasema: 'Ewe mtoto wa Abu Talib huridhii kupata kwangu cheo sawa na cheo cha Harun kwa Musa?'"

**Nasema:** Ameipokea pia Ibn Na'im kwa ufupi katika *Hilyat*Juz. 8, uk. 307, na kaipokea al-Khatib Al-Baghdadiy pia kwa ufupi katika *Taarikh* yake Juz. 4, uk. 382, na al-Haythamiy ameitaja katika *Majmau* yake Juz. 9, uk. 109, na akasema: "Ameipokea Ahmad. Yaani Ibn Hanbal." Hadithi hii nimeikuta katika *Musnad Ahmad bin Hanbal* kama alivyoitaja katika Juz. 3, uk. 32.

**Tabaqat Ibn Saad Juz. 3, Sehemu ya kwanza, Uk. 15:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwaal-Barau Ibn Azib na Zayd bin Arqam, wote wawili wamesema: "Wakati maandalizi ya jeshi kwa ajili ya vita vya Tabuk yalipotimia, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Ali bin Abu Talib (as): 'Ni lazima mimi nibaki au wewe.' Basi Mtume (saww) akambakisha Ali, na walipokwenda vitani huku nyuma watu wakasema: 'Hakumuacha Ali (as) bure isipokuwa kuna jambo lililomkera kutoka kwake.'Yalipomfikia maneno hayo Ali (as) alimfuata Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mpaka akamkuta, Mtume akamuuliza: 'Lipi lililokuleta hapa ewe Ali?' Akasema: 'Hapana jingine ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, isipokuwa nimesikia watu wakidai kwamba, wewe umeniacha kutokana na jambo lililokukera kutoka kwangu.'Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akatabasamu na kusema: 'Ewe Ali huridhii kuwa wewe kwangu mimi ni sawa na Harun kwa Musa isipokuwa wewe si Mtume?' Akasema:'Nimeridhia ewe Mtume waMwenyezi Mungu.' Akasema: 'Basi hivyo ndivyo ulivyo.'"

**Nasema:** Pia ameitaja al-Haythamiy katika *Majmau* yake Juz. 9, uk. 111 kwa tofauti ndogo katika lafudhi, na amesema:"Ameipokea Tabaraniy kwa sanadi mbili."

**Hilyatul-Awliyai cha Abu Na'im Juz. 4, Uk. 345:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwaHabashiy bin Junadah, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema kumwambia Ali (as): 'Wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu.'"

**Nasema:** Na ameitaja al-Haythamiy katika *Majmau* yake Juz. 9, uk. 109, akiinukuu kutoka kwa Tabaraniy sehemu tatu.

**Hilyatul-Awliyai cha Abu Na'im Juz. 7, Uk. 195:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Saad Ibn Ibrahim, kutoka kwa Aamir bin Saad, kutoka kwa baba yake Saad kwamba Mtume (saww) alimwambia Ali (as): "Je hauridhii kuwa wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu?"

**Hilyatul-Awliyai cha Abu Na'im Juz. 7, Uk. 196:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Said bin al-Musayyab, kutoka kwa Ali (as), amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema katika vita vya Tabuk: 'Nimekuacha ili uwe Khalifa kwa watu wangu.' Nikasema: 'Sintobaki tena baada yako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Akasema: 'Je huridhii kuwa wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu?'"

**Nasema:** Ameitaja al-Mutaqiy katika *Kanzul-Ummal*Juz. 6, uk. 404, na al-Haythamiy katika *Majmau* yake Juz. 9, uk. 110, wote hao wawili wameinukuu kutoka kwa Tabaraniy kutoka katika *al-Awsat*, na al-Haythamiy amesema: "Wapokezi wake ni wapokezi sahihi."

**Taarikh Baghdad Juz. 4, Uk. 71:**

Amepokea kwa njia yake inayoishia kwa Maamun, kutoka kwa ar-Rashid, kutoka kwa Mahdi, amesema: "Aliingia kwangu Sufyani Thawriy, nikamwambia: 'Nielezee fadhila bora zaidi ya Ali (as) iliyopo kwako.' Akaniambia: 'Amenihadithia Salmah bin Kahil kutoka kwa Hajiyah bin Adiy kutoka kwa Ali (as), amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu.'"

**Nasema:** Ameitaja pia al-Mutaqiy katika *Kanzul-Ummal*Juz. 6, uk. 402, akinukuu kutoka kwa Ibn Najar, na ameitaja al-Muhibu Tabari katika *Ar-Riyadh an-Nadhirah*Juz. 2, uk. 162, na akasema: "Ameiandika al-Hafidh as-Salafiy katika chapa ya Baghdadi."

**Taarikh Baghdad Juz. 7, Uk. 452:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Umar bin Khattab kwamba alimuona mtu akimtukana Ali (as), akamwambia: "Hakika nadhani wewe ni mnafiki. Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Hakika Ali kwangu mimi ni sawa na Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu."'

**Nasema:** al-Muhibu Tabari ameitaja katika *Ar-Riyadh an-Nadhirah* Juz. 2, uk. 163, na akasema: "Ameiandika Ibn Saman."

**Taarikh Ibn Jarir Tabari Juz. 2, Uk. 368:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Is'haqa katika hadith ya vita vya Tabuk, amesema humo: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipokwenda vitani, wapo waliobaki miongoni mwa wanafiki akiwemo Abdullah bin Ubay, na huyu Abdullah bin Ubayalikuwa ni ndugu wa Bani Awfi bin Khazraj, na pia alikuwemoAbdullah bin Nabtal ndugu wa Bani Amru Ibn Awfi na Rifaat bin Yazid bin Tabut ndugu wa Bani Qaynaqau, wote hawa walikuwa ni viongozi wa wanafiki, na walikuwa wakiufanyia hila Uislamu na Waislamu –aliendelea kusimulia mpaka aliposema: na kuhusu wao iliteremka:**'Tangu zamani walitaka kukutilieni fitna, na wakakupindulia mambo juu chini, mpaka ikaja Haki na ikadhihirika amri ya Mwenyezi Mungu, na wao wamechukia.'**"

Tabari anasema: Ibn Is'haqa amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamuacha Ali bin Abu Talib (as) na akamwamrisha kuwasimamia –aliendelea kusimulia mpaka aliposema: Kikawatisha wanafiki kitendo cha Ali bin Abu Talib (as) kubaki na hivyo wakasema: 'Hakumuacha bure isipokuwa kwa sababu amechoshwa naye naanataka kujipunguzia mzigo.' Wanafiki waliposema hayo, Ali (as) alichukua silaha yake na kutoka mpaka akafika kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) wakati akiwa Jurfi, Ali (as) akasema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Wanafiki wamedai kuwa umeniacha kwa sababu mimi ni mzigo kwako na unataka kujipunguzia mzigo.' Mtume akamwambia: 'Wamezusha uwongo, hakika mimi nimekuacha kwa sababu ya wale walio nyuma yangu, rudi ukawemsimamizi wa watu wangu na wako, hivi huridhii ewe Ali kuwa wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu?' Ali (as) akarudi Madina na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaendelea na safari yake."

**Usudul-Ghabah cha Ibn Athir Juz. 5, uk. 8:**

Amesema katika wasifu wa Nafiu bin Harith Kaldah: "Na amepokea kutoka kwa Mtume (saww) kuwa yeye alimwambia Ali (as): 'Wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa.'"

**Kanzul-Ummal Juz. 3, uk. 154:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Dhar amesema: "Katika siku ya kwanza tangu Uthman apewe kiapo cha utii, Muhajirina na Ansari walikusanyika msikitini, na mara Ali bin Abu Talib (as) akaja na kuanza kusema:'Hakika jambo wanalopasa kuanza nalo wenye kuanza, na kulitamka wenye kutamka na kulisema wenye kusema, ni kumhimidi Mwenyezi Mungu na kumsifu kwa yale anayostahiki, na kumswalia Mtume (saww) –aliendelea mpaka aliposema: Je mnatambua kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliniambia mimi: 'Wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa?' – aliendelea mpaka aliposema: Je katika viumbe kuna mtu yeyote mwenye cheo hiki zaidi yangu? Sisi ni wenye kusubiri ili Mwenyezi Mungu apitishe hukumu katika jambo ambalo tayari limeshakuwa." – Amesema: Ameiandika Ibn Asakir.

**Kanzul-Ummal Juz. 5, uk. 40:**

Amesema: Wakati Mtume (saww) alipounga udugu kati ya Maswahaba zake, Ali (as) alisema: "Hakika roho yangu imetoweka na uti wa mgongo wangu umekatika pale nilipokuona ukifanya kwa Maswahaba zako namna ambavyo hukunifanyia mimi, ikiwa hili ni kutoa adhabu kwangu basi kwako ni kwenye msamaha na ukarimu." Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Naapa kwa yule aliyenituma kwa haki, sijakucheleweshа isipokuwa kwa ajili yangu mwenyewe, na wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu, na wewe ni ndugu na mrithi wangu." Akasema: "Ni kipi nitakachorithi kutoka kwako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?" Akamsema: "Vile walivyorithiwa Manabii kabla yangu." Akamuuliza:"Ni yapi waliyorithiwa Manabii kabla yako?" Akasema:"Ni Kitabu cha Mola Wao na Sunna za Nabii wao, na wewe utakuwa pamoja nami katika kasri peponi pamoja na binti yangu, na wewe ni ndugu na rafiki yangu."

Amesema: Ameipokea Ahmad bin Hanbal katika kitabu cha fadhila za Ali (as), na pia kaipokea Ibn Asakir.

**Nasema:** Na al-Mutaqiy ameitaja kwa urefu katika *Kanzul-Ummal* katika uk. 40, na Al-Muhibu Tabari ameitaja pia kwa urefu katika *Ar-Riyadh an-Nadhirah*Juz. 1, uk. 13, na wamesema mwashoni mwa hadithi hiyo: "Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasoma: **'wawe ndugu juu ya viti**

**vya enzi wameelekeana.'** Wakipendana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wakitazamana wao kwa wao." Kisha al-Mutaqiy akasema: "Nikasema: Hadithi hii limeiandika kundi la maimamu kama al-Baghawiy na Tabaraniy katika *Muujamu* zao, na al-Bawaridiy katika *al-Maarifah*, na Ibn Adiy." Al-Muhibu Tabari amesema: "Ameiandikaal-Hafidh Abu Qasim ad-Damashqiy katika *Al-Arubain at-Twawaal*.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 154:**

Na tamko lake ni: "Hivi huridhii kuwa wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa." – Amesema: Ameiandika Tabaraniy kutoka kwa Maliki bin Huwayrith.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 154:**

Na tamko lake ni: "Ewe Ali!Wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa kwamba hakuna Nabii baada yangu."

— Amesema: Ameiandika Tabaraniy kutoka kwa Asmau binti Umaysu.

**Nasema:** Na al-Haythamiy ameitaja katika *Majmau* yake Juz. 9, uk. 109 kwa tofauti ndogo katika tamko, na amesema: "Ameipokea Ahmad na Tabaraniy."

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 188:**

Na tamko lake ni: "Ewe Aqil!Wallahi hakika mimi nakupenda kwa mambo mawili: Kwa undugu wako na kumpenda kwako Abu Talib. Ama wewe ewe Ja'far hakika umbile lako linafanana na langu. Ama wewe ewe Ali, wewe kwangu mimi una cheo sawa na cheo chaHarun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu."

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 395:**

Amesema: Kutoka kwa Ibn Abbas amesema: Umar Ibn Khattab alisema: "Acheni kumsema vibaya Ali bin Abu Talib, hakika mimi nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema mambo matatu kuhusu Ali, mimi kuwa na jambo moja kati ya hayo mambo matatu ni jambo nilipendalo sana kuliko kuwa na vitu vyote vilivyochomozewa na jua.' Nilikuwa kwa Mtukufu Mtume (saww) pamoja na Abu Bakr, Abu Ubaydah bin Jarah na Masahaba kadhaa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Mtume alikuwa kamwegamia Ali bin Abu Talib, na mara akapiga mkono wake begani kwa Ali (as) na kusema: 'Wewe ndiye mtu wa kwanza kuukubali Uislamu kabla ya watu wote, na ndiye mtu wa kwanza kuamini kabla ya watu wote – kisha akasema: na wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa. Bila shaka amenizushia uwongo yule mwenye kudai kuwa ananipenda wakati anakuchukia wewe."'

Amesema: Ameiandika Hasan bin Badru katika hadithi walizozipokea Makhalifa, na al-Hakim ndani ya *al-Kuna*, na as-Shiraziy ndani ya *al-Alqab* na Ibn an-Najari.

**Nasema:** Piaal-Mutaqiy ameitaja kwa njia nyingine kwa tofauti ndogo katika *Kanzul-Ummal* katika uk. 395 na wala hakusema mwishoni: "Bila shaka amenizushia uwongo." Na amesema:"Ameiandika Ibn Najar." Na pia al-Muhibu Tabari ameitaja katika *Ar-Riyadh an-Nadhirah*Juz. 2, uk. 163 na katika uk. 175, na pia hakusema mwishoni: "Bila shaka amenizushia uwongo." Na amesema: "Ameiandika Ibn Saman."

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 405:**

Kutoka kwa Saad amesema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akimwambia Ali (as) mambo matatu ambayo mimi kuwa na moja kati ya hayo ni jambo nilipendalo sana kuliko kuwa na dunia yote na vilivyomo. Nilimsikia akisema: 'Wewe kwangu mimi una cheo sawa na cheo cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu.' Na nilimsikia akisema: 'Nitampa bendera kesho mtu ambaye anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanampenda yeye, naye si mwenye kukimbia vitani.' Na nilimsikia akisema: "Yeyote yule ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.'" – Amesema: Ameiandika Ibn Jarir.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 405:**

Kutoka kwa Aamir bin Saad amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema mambo matatu kuhusu Ali, mimi kuwa na moja kati ya hayo ni jambo nilipendalo sana kuliko farasi mwekundu. Uliteremka wahyi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwingiza Ali, Fatimah na watoto wao (as) ndani ya nguo, kisha akasema: 'Ewe Mola Wangu hawa ni kizazi changu na watu wa nyumba yangu.' Na alimwambia wakati alipomuacha katika vita alivyopigana: 'Hivi huridhii kuwa cheo chako kwangu mimi ni sawa na cheo cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna unabii baada yangu?' Hiyo ni baada ya Ali (as) kumwambia: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Je waniacha pamoja na wanawake na watoto?' Na alisema siku ya Khaybar: 'Nitampa bendera kesho mtu ambaye anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanampenda yeye, Mwenyezi Mungu ataleta ushindi mikononi mwake.' Muhajirina wakatamani na kuinua shingo zao ili Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) awaone, Mtume akasema: 'Yuko wapi Ali.' wakasema anaumwa macho, akasema: 'Mwiteni.' Wakamwita akamtemea mate machoni na Mwenyezi Mungu akaleta ushindi mikononi mwake. – Amesema: Kaiandika Ibn an-Najar.

**Kanzul-Ummal Juz. 8, uk. 215:**

Amesema: Kutoka kwa Yahya bin Abdillah bin Hasan kutoka kwa baba yake, amesema: Ali (as) alikuwa akihutubia na mara akasimama mtu na kusema: "Ewe Amirul-Muuminina niambie ni kina nani watu wa umoja, ni kina nani watu wa faraka, ni kina nani watu watu wa Sunna, na ni kina nani watu wa bidaa?" Ali (as) akasema: "Ole wako, utakaponiuliza mimi basi tosheka na utakavyofahamu toka kwangu na wala usimuulize yeyote baada yangu." –Aliendelea kusimulia hadithi mpaka aliposema: Watu wakanadi kutoka kila upande: "Umepatia ewe Amirul-Muuminina, Mwenyezi Mungu akulipe uongofu na unyoofu." Ammari akasimama na kusema: "Enyi watu!Wallahi kama mtamfuata na kumtii yeye hatowapotezeni njia ya Mtume wenu hata kwa kiasi cha uzito wa unywele. Na vipi awapotezeni wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amekwishamuachiakifo, wasia na ufasaha wa maneno katika njia ile ile ya Harun bin Imran? Pale Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliposema: 'Wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu.' Fadhila ambayo Mwenyezi Mungu amempa yeye tu kwa ajili ya kumkirimu Nabii Wake (saww), kwa kumpa kila ambacho hajawahi kumpa yeyote katika viumbe wake." – Hadithi hii itakuja kwa ukamilifu Inshaallah katika Mlango unaozungumzia kupigana na wavunja ahadi, waovu na waasi.

**Majmauz-Zawa'id cha al-Haythamiy Juz. 9, Uk. 109:**

Amesema: Kutoka kwa Ummu Salamah, amesema: "Hakika Mtume (saww) alimwambia Ali (as): 'Huridhii kuwa wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu?'" Ameipokea Abu Ya'ala na Tabaraniy.

**Na pia katika Juz. 9, uk. 109:**

Amesema: Na kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Hakika Mtume (saww) alimwambia Ali (as): 'Hivi huridhii kuwa wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu?'"

— Amesema: Ameipokea al-Bazar na Tabaraniy.

**Na pia katika Juz. 9, uk. 110:**

Amesema: Na kutoka kwa Ibn Umar amesema: "Hakika Mtume (saww) alimwambia Ali (as): 'Hivi huridhii kuwa wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna unabii baada yangu?'"

– Amesema: Ameipokea Tabaraniy katika al-Kabiir na al-Awsat.

**Na pia katika Juz. 9, uk. 109:**

Amesema: Kutoka kwa Abi Said al-Khudriy amesema: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu alisema kumwambia Ali (as) katika vita vya Tabuk: 'Nimekuacha kwa ajili ya watu wangu.' Ali (as) akasema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu!Hakika sipendi Waarabu waje kusema kuwa: Amemsaliti mtoto wa ami yake na amejitenga naye.' Mtume (saww) akasema: 'Hivi huridhii kuwa wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu?'" – Amesema: Ameipokea al-Bazar.

**Na pia katika Juz. 9 Uk. 110:**

Amesema: Na kutoka kwa Jabir –Yaani Ibn Samrah- amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Ali (as): 'Wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu.'" – Amesema: Ameipokea Tabaraniy.

**Na katika Juz. 9, uk. 111:**

Amesema: Kutoka kwa Abu Ayub amesema: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema kumwambia Ali (as): 'Wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu.'" – Amesema: Ameipokea Tabaraniy.

**Na katika Juz. 9, uk. 111:**

Amesema: Na kutoka kwa Ibn Abbas amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Ummu Salamah: 'Huyu Ali bin Abu Talib, nyama yake ni nyama yangu, na damu yake ni damu yangu, na yeye kwangu mimi ana cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu.'" – Amesema: Ameipokea Tabaraniy.

**Nasema:** Na pia al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzul-Ummal*Juz. 6, uk. 154, na akasema humo: "Ewe Ummu Salamah:'Hakika Ali (as) nyama yake imetokana na nyama yangu.'"

**Na katika Juz. 9, uk. 111:**

Amesema: Kutoka kwa Ibn Abbas amesema: "Wakati Mtume (saww) alipounga undugu kati ya Maswahaba zake baina ya Muhajirina na Ansari bila kuunga undugu kati ya Ali bin Abu Talib (as) na yeyote miongoni mwao, Ali (as) alitoka hali ameghadhibika kiasi ambacho misuli ya mkononi ilijitokeza. - Alisimulia mpaka aliposema: Mtume (saww) akamwambi Ali (as): 'Simama! Haifai zaidi ya wewe kuwa Abu Turabi, je umenighadhibikia pindi nilipounga udugu baina ya Muhajirina na Ansari bila kuunga udugu baina yako na yeyote kati yao? Hivi huridhii kuwa wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu? Fahamu atakayekupenda ataishi kwa amani na imani, na atakayekuchukia Mwenyezi Mungu atamfisha kifo cha kijahiliyah na atahesabiwa kwa amali zake sawa na aliyomo katika Uislamu.'" – Amesema: Ameipokea Tabaraniy ndani ya *al-Kabir* na *al-Awsat*.

**Nasema:** Ameitaja al-Mutaqiy ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 6, uk. 154.

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, Uk. 162:**

Amesema: Na kutoka kwake. –Yaani kutoka kwa Saad- amesema: "Wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipofika Jurfi, watu miongoni mwa wanafiki waliukebehi uongozi wa Ali (as) na kusema: 'Hakika amemuacha kwa kuwa amekuwa mzigo kwake.' Ndipo Ali (as) akatoka akabeba silaha yake mpaka akafika kwa Mtume (saww) huko Jurfi, akamwambia: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi, kamwe sijawahi kukuacha wewe katika vita vyovyote kabla ya hivi, kwani wanafiki wanadai kwamba umaniacha kwakuwa nimekuwa mzigo kwako.' Mtume akasema: 'Wamezusha uwongo, lakini nimekuacha kwa sababu ya wale waliokuwa nyuma yangu, rudi ukawe msimamizi wa watu wangu. Hivi huridhii kuwa wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu?'"

Amesema: Ameipokea Ibn Is'haqa, na ameipokea kimaana al-Hafidh ad-Damashqiy katika *Muujamu*yake.

**Nasema:** Na ameitaja pia katika Juz. 1 katika uk. 156.

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, Uk. 164:**

Amesema: Kutoka kwa Asmau bintiUmaysi amesema: "Jibril (as) alishuka kwa Mtume (saww) na kumwambia: 'Ewe Muhammad, hakika Mola Wako anakutolea salamu na anakwambia: Ali kwako wewe ana cheo sawa na cha Harun kwa Musa lakini hakuna Nabii baada yako."' – Amesema: Ameipokea Imam Ali bin Musa.

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, Uk. 195:**

Amesema: Kutoka kwa Abi Hazim amesema: "Alikuja mtu mmoja kwa Muawiya na kumuuliza maswali kadhaa, Muawiya akasema: 'Muulize hayo Ali bin Abu Talib kwani yeye ni mjuzi zaidi.' Mtu yule akasema: 'Ewe Amirul-Muuminin jawabu lako nalipenda zaidi kuliko jawabu la Ali.' Muawiya akasema: 'Ni mabaya kiasi gani hayo uliyosema, umemchukia mtu ambaye Mtume (saww) alikuwa akimhifadhisha elimu yote, na hakika alisema kumwambia yeye: Wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu. Na Umar alipokuwa akipata tatizo lolote la (kielimu) basi ufumbuzi wake alikuwa akiupata kutoka kwake."' – Amesema: AmeiandikaAhmad katika *al-Manaqib*.

**Dhakhairul-Uqba Uk. 120:**

Amesema: Na kutoka kwa Kutoka kwa Asmau binti Umaysi amesema: "Wakati Fatimahalipojifungua Hasan (as) alikuja Mtume (saww) na kusema: 'Ewe Asmau mlete mtoto wangu.'Nikampa huku akiwa kafungwandani ya kitambaa cha njano, Mtume (saww) akamfungua na kukitupa kitambaa hicho, akasema: 'Si nilikukatazeni kwamba msimfunge mtoto mchanga kwenye kitambaa cha njano?' Nikamfunga kwa kitambaa cheupe kisha Mtume akamchukua, akamwadhinia kwenye sikio lake la kulia na kumkimia kwenye sikio la kushoto, kisha akasema kumwambia Ali (as): 'Umempa jina gani mtoto wangu?' Ali akasema: 'Sikuwa mwenye kukutangulia kwa hilo.' Akasema: 'Wala mimi sikuwa mwenye kumtangulia Mola Wangu.' Mara akashuka Jibril (as) na kusema: 'Ewe Muhammad, hakika Mola Wako anakutolea salam na anakwambia: Ali kwako wewe ana cheo sawa na cha Harun kwa Musa lakini hakuna Nabii baada yako, hivyo mwite mtoto wako huyu kwa jina la mtoto wa Harun.' Akamuuliza: Ni lipi lilikuwa jina la mtoto wa Harun ewe Jibril? Akamsema: 'Ni Shibr.' Akasema (saww): 'Hakikalugha yangu ni Kiarabu.' Akasema: 'Mwite Hasan.' Mtume (saww) akafanya hivyo. Baada ya mwaka mmoja akazaliwa Husein (as) na akaja Mtume (saww)." Akataja (Asmau) kama mwanzo na akaendelea kusimulia kisa cha kupewa jinakama mwanzo, na kwamba Jibril (as) alimwamrisha amwite kwa jina la mtoto wa Harun Shubair, na Mtume akamwambia tena kama alivyomwambia mwanzo, akasema: 'Mwite Husein.'" – Amesema: Ameipokea Imam Ali bin Musa Ridha (as).

Kisha hapa kuna hadithi nyingine inafaa zaidi kuitaja mwishoni mwa mlango huu, nayo ni ile aliyoitaja Al-Muhibu Tabari katika *Ar-Riyadh an-Nadhrah* Juz. 2, uk. 164, amesema: Kutoka kwa Anas amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema kumwambia Ali (as) siku ya vita vya Tabuk: 'Hivi huridhii kuwa na ujira mfano wa ujira wangu, na kuwa na mafanikio kama yangu?'" – Tabari amesema: Ameipokea al-Qal'iy.

## MLANGO UNAOSEMA KUWA ALI (AS) NI NDUGU WA MTUKUFU MTUME (SAWW)

**Nasema:** Lengo la kuweka mlango huu si kutaja kila hadithi ambayo inaelezea undugu wa Ali (as) pamoja na Mtume (saww), bali tutaishia kutaja hadithi zilizokusanya udugu tu bila uwaziri. Ama hadithi ambazo zimekusanya viwili hivyo (udugu na uwaziri), tutazitaja Inshaallah katika mlango unaosema kuwa Ali ni waziri wa Mtume (saww), hivyo basi fanya subira.

**Sahihi Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 299:**

Amepokea kwa sanadi yake kutoka kwa Ibn Umar kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyeezi Mungu (saww) aliunga udugu kati ya Maswahaba zake, ndipo akaja Ali (as) huku akiwa anatokwa na machozi, akasema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, umeunga udugu kati ya Maswahaba zako bila kuunga udugu wangu na yeyote.'Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema:'Wewe ni ndugu yangu duniani na Akhera.'" – Amesema: Na katika mlango huu kuna hadithi nyingine kutoka kwa Zaydi bin Awfa.

**Nasema:** Na pia Al-Hakim ameipokea katika Juz 3, uk. 14. Na ameitaja al-Munawikwa muhtasari katika *Kunuzul–Haqaaiq*, na tamko lake ni: "Ali ni ndugu yangu duniani na Akhera."

**Sahihi Ibn Majah, Uk. 12:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ubad bin Abdullah kutoka kwa Ali (as), amesema: Ali (as) alisema: "Mimi ni mja wa Mwenyezi Mungu na ndugu wa Mtume Wake, na mimi ndiye mkweli mkuu, hasemi hilo baada yangu isipokuwa muongo, nimeswali miaka saba kabla ya watu wote."

**Nasema:** Na pia ameipokea al-Hakim katika *Mustadrakus-Sahihayn* Juz. 3, uk. 111, na Ibn Jarir Tabari katika *Taarikh* yake Juz. 2, uk. 56, na an-Nasaiy katika *Khasa'isu* yake uk. 3 na ameitaja kwa muhtasari katika uk. 18. Na pia al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzul–Ummal* Juz. 6, uk. 394, na akasema: "Ameiandika Ibn Abi Shaybah, an-Nasaiy katika *Khasa'isu*, Ibn Abi Aswim katika *as-Sunnah*, Uqayliy, al-Hakim na Abu Na'im katika *al-Ma'rifah*." Pia ameitaja katika uk. 396, na mwisho akasema: "Hatasema hayo baada yangu isipokuwa muongo. Mtu mmoja alipatwa na wendawazimu baada ya kusema hayo."

Amesema: Ameipokea al-Adniy, na pia al-Muhibu Tabari ameitaja katika *ar-Riyadh an-Nadhrah*katika Juz.2, uk.155, na akasema: "Ameipokea al-Qal'iy.

**Mustadrakus-Sahihayn Juz.3, Uk.14:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Umar, amesema: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliunga udugu kati ya Maswahaba zake, akaunga udugu kati ya Abu Bakr na Umar, Talha na Zubair, Uthman bin Affan na Abdur-Rahman bin Awf. Ali (as) akasema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Hakika wewe umeunga udugu kati ya Maswahaba zako basi ni nani ndugu yangu?' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Hivi huridhii ewe Ali mimi kuwa ndugu yako!'" Ibn Umar amesema: "Ali (as) alikuwa shujaa sana, akamjibu: 'Nimeridhia ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.'Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Wewe ni ndugu yangu duniani na Akhera.'"

**Nasema:** Na pia al-Muhibu Tabari ameitaja katika *ar-Riyadh an-Nadhralh* Juz. 2, uk. 167, na akasema: "Ameiandikaal-Qal'iy."

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 3, Uk. 126:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas amesema: "Ali (as) alikuwa akisema zama za uhai wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww):'Hakika Mwenyezi Mungu anasema: **Je akifa au akiuwawa ndiyo mtageuka mrudi nyuma?**Naapa kwa Mwenyezi Mungu haturudi nyuma baada ya Mwenyeezi Mungu kutuongoa, naapa kwa Mwenyezi Mungu ikiwa atakufa au kuuwawa basi ni lazima nipiganie lile ambalo alilokuwa akipigania mpaka nife. Naapa kwa Mwenyezi Mungu hakika mimi ni ndugu yake, ni walii wake, mtoto wa ami yake na mrithi wa elimu yake, basi ni nani mwenye haki naye zaidi kuliko mimi.'"

**Nasema:** Ameipokea an-Nasaiy katika *Khasa'is*yake uk. 18, na al-Muhibu Tabari ameitaja katika *ar-Riyadh an-Nadhrah* Juz. 2. uk. 226, na akasema:"Ameiandika Ahmad *katika al-Manaqib*."Na pia al-Haythamiy ameitaja katika *Majmau* yake Juz. 9, uk. 134, na akasema: "Ameipokea Tabaraniy na wapokezi wake ni wapokezi wa hadithi sahihi."

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 3, Uk. 159:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Asmau binti Umais kuwa amesema: "Nilikuwa kwenye sherehe ya harusi ya Fatimah binti ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), tulipoamka Mtume (saww) alikuja mlangoni na kusema: 'Ewe Ummu Ayman niitie ndugu yangu.' Akasema (Asmau): "Yeye ni ndugu yako mbona sasa umemuozesha (mwanao)?' Akasema: 'Ndio ewe Ummu Ayman.' Ali (as) akaja, na Mtume

(saww) akamrushia maji na akamuombea dua kisha akasema: 'Niitie Fatimah.'" Anasema: "Akaja huku akiona aibu, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: 'Tulia, nimekuozesha kwa mtu ninayempenda zaidi kati ya watu wote wa nyumbayangu.'"Hadithi hii itakuja kwa ukamilifu wake Inshaallah katika milango inayozungumzia ndoa ya Ali na Fatimah (as).

**Nasema:** Na katika *Tabaqat* Juz. 8, uk. 14 Ibn Saad amepokea hadithi inayozungumzia ndoa ya Ali na Fatimah (as), na amesema humo:"Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuja na akapiga hodi, ndipo Ummu Ayman akatoka, Mtume akamuuliza:'Je yupo ndugu yangu!' Ummu Ayman akamjibu: 'Vipi atakuwa ndugu yako wakati umekwisha muozesha binti yako!'Mtume akamjibu: 'Hivyo ndivyo ilivyo.' –Aliendelea kusimulia mpaka akasema: 'Ewe Fatimah sikukosea nilipo kwa aliye bora zaidi kati ya watu wangu.'" Na ameipokea kwa tofauti ndogo katika uk. 15.

Na pia katika *Kanzul–Ummal* Juz. 7, uk. 113 al-Mutaqiy ametaja hadithi inayozungumzia ndoa ya Ali na Fatimah (as), na akasema humo: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuja nakusema: 'Je hapa pana ndugu yangu!' Ummu Ayman akajibu: 'Ndugu yako! Ni yupi ndugu yako na ulikwisha muozesha binti yako!' Mtume akasema: 'Ndiyo."

Na pia katika *Majmauz-Zawa'id* Juz. 9, uk. 205, al-Haythamiy ametaja hadithi inayozungumzia ndoa ya Ali na Fatimah (as), amesema humo: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Je hapa kuna ndugu yangu?-Akimaanisha Ali (as) – 'Ummu Ayman akamjibu: 'Ni ndugu yako wakati umekwisha muozesha binti yako!'"– Amesema: Ameipokea Tabaraniy. Nakatika uk. 209 ametaja hadithi nyingine amesema: "Mtume (saww) alikuja na kuuliza: 'Je kuna ndugu yangu!' Ummu Ayman - naye ni mama Usama bin Zayd na alikuwa mhabeshi, alikuwa mwanamke mwema- akajibu: 'Ewe Mtume wa Mwenyeezi Mungu, huyo ni ndugu yako mbona tena umemuozesha binti yako?' Na Mtume (saww) alikuwa ameshaunga undugu na Maswahaba zake, na yeye aliunga udugu wake na Ali (as), Mtume (saww) akasema: 'Hakika hilo linaweza kuwa ewe Ummu Ayman.'"

Na katika uk. 210 ametaja hadithi ya tatu, amesema humo: "Mtume wa Mwenyezi Munguakamwambia:'Ewe Ummu Ayman niitie ndugu yangu.'Akasema: 'Ndugu yako vipi wakati umemwozesha binti yako?'"

Na an-Nasaiy katika *Khasa'isu* yake uk. 32 amepokea hadithi inayozungumzia ndoa ya Ali na Fatimah (as), amesema humo: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuja akagonga mlango, Ummu Ayman akatoka, Mtume akasema: 'Yupo ndugu yangu?' Ummu Ayman akasema:'Atakuwaje ndugu yako wakati umekwisha muozesha binti yako?' Mtume (saww) akasema: 'Hakika yeye ni ndugu yangu.'"

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 1, Uk. 159:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Rabia bin Najidh kutoka kwa Ali (as) kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliwakusanya -au aliwaita- watoto wa Abdul Muttalib, walikuwemo wanaume wote na kwa pamoja walipaswa kula mnyama mzima na kunywa lita kumi na tatu."Alisema: "Akawatengenezea pishi moja la chakula wakala na kushiba, na kikabaki chakula kama kilivyo kana kwamba hakikuguswa, kisha akawaletea kinywaji wakanywa mpaka wakatosheka na kikabaki kana kwamba hakikuguswa -au hakijanywewa- akasema: 'Enyi watoto wa Abdul Muttalib! mimi nimetumwa makhususi kwenu na kwa watu wote, na mmekwishaona katikadalili hii yale mliyoyaona, hivyo basi ni nani atakayenipa kiapo cha utii ili awe ndugu yangu na rafiki yangu?'" Alisema: "Hakuna yeyote aliyesimama, nikasimama mimi, na nilikuwa mdogo kwao kiumri kushinda wote, akasema (Mtume) mara tatu: 'Kaa chini.'Kila niliposimama aliniambia 'Kaa chini.'Mpaka ilipotimia mara ya tatu, akapiga mkono wake kwenye mkono wangu."

**Nasema:** al-Haythamiy ameitaja katika *Majmau* yake Juz. 8, uk.302, na akasema:“Wapokezi wake ni watu wakweli.”Na pia ameipokea Ibn Jarir Tabari katika *Taarikh* yake Juz. 2, uk. 63, na akasema humo:“Ili awe ndugu yangu, rafiki yangu na mrithi wangu.” Na pia al-Muhibu Tabari ameitaja katika *ar-Riyadh an-Nadhrah*katika Juz. 2, uk.167, na akasema: “Ameiandika Ahmad katika *al-Manaqib*.” Na pia an-Nasaiy ameipokea katika *Khasa'is* yake uk. 18, na mwishoni amesema: “Na ni nani kati yenu atakayenipa kiapo cha utii ili awe ndugu yangu, rafiki yangu na mrithi wangu? – Ameendelea kusimulia mpaka aliposema: Hivyo ndivyo nilivyomrithi mtoto wa ami yangu bila kumrithi ami yangu.” Na al-Mutaqiy pia ameitaja katika *Kanzul-Ummal*katika Juz. 6, uk. 408, na akasema: “Ameiandika Ahmad bin Hanbal, Ibn Jarir na ad-Dhiyau Al–Muqaddasiy.” Na ameitaja pia katika uk. 401, na amesema humo: “Ni nani atakayenipa kiapo cha utii ili awe ndugu yangu na rafikiyangu na walii wenu baada yangu? Nikanyoosha mkono wangu na nikasema: Mimi ninakupa kiapo cha utii.” – Ameendelea kueleza mpaka aliposema: Ameiandika Ibn Mardawayhi.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 1, Uk. 230:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: “Wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipotoka Makka Ali (as) alitoka na binti ya Hamza, na ndipo pakatokea mzozo kati ya Ali (as), Ja'far na Zayd (kila mmoja akitaka amtunze yeye), wakamshitakia hilo Mtukufu Mtume (saww), Ali (as) akasema: ‘Ni mtoto wa ami yangu na mimi ndiye niliyemtoa Makka.’ Akasema Ja'far: ‘Ni binti ya ami yangu na mama yake mdogo yuko chini yangu.’ Na Zayd akasema: ‘Ni binti ya ndugu yangu.’ –kwani Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa ameunga udugu baina yake na Hamza- Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia Zayd: ‘Wewe ni mtumishi wangu na mtumishi wake.’ Na akamwambia Ali (as): ‘Wewe ni ndugu yangu na rafiki yangu.’ Na akamwambia Ja'far: ‘Umefanana na mimi kimaumbile na kitabia. Naye atakwenda kwa mama yake mdogo.”’

**Nasema:** Na pia ameitaja kwa ufupi al-Mutaqiy katika *Kanzul–Ummal* katika Juz. 6, uk. 391, na amesema: “Ameiandika Ibn Najar.”

**Tabaqat Ibn Saad Juz. 8, Uk. 114:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: “Hakika Ammarah binti Hamza bin Abdul Muttalib -ambaye mama yake ni Salma binti Umaysu- alikuwa Makka. Wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipofika Madina, Ali (as) alizungumza naye na akamwambia: ‘Kwa nini unamuacha binti ya ami yetu yatima katika migongo ya Mushirikina?’Kwakuwa Mtume (saww) hakumkataza kutoka naye, yeye alitoka naye. Zayd bin Harithah alikuwa wasii wa Hamza kwani Mtume (saww) alikuwa ameungaudugu kati ya hao wawili wakati alipounga udugu kati ya Muhajirina, hivyo Zayd akasema: ‘Mimi nina haki naye zaidi kwakuwa yeye ni binti ya ndugu yangu.’Ja'far bin Abu Talibaliposikia hayo akasema: ‘Mama mdogo ni sawa na mama mzazi, hivyo mimi nina haki naye zaidi kutokana na nafasi ya mama yake mdogo, Asmau binti Umaysi yupo kwangu. Ali (as) akasema: ‘Nawaona mnagombana kuhusu binti ya ami yangu, mimi ndiye niliyemtoa baina ya migongo yaMushrikina, wala hamna ujamaa naye zaidi yangu, na mimi nina haki naye zaidi kuliko nyinyi.’ Ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: ‘Mimi ninatoa hukumu kati yenu: Ama kuhusu wewe ewe Zayd, wewe ni mtumishi wa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Ama wewe ewe Ali, weweni ndugu yangu na rafiki yangu. Ama wewe ewe Ja'far, wewe unafanana nami kimaumbile na kitabia. Na wewe ewe Ja'far ndiye mwenye haki naye zaidi kwakuwa mama yake mdogo yupo chini yako, mwanamke haolewi pamoja na mama yake mdogo wala pamoja na shangazi yake.’Hivyoakahukumu kuwa ni wa Ja'far.”

**Nasema:** Pia al-Mutaqiyameitaja katika *Kanzul–Ummal* Juz. 3, uk. 124 ikiwa na maelezo ya nyongeza, na amesema:"Ameiandika Ibn Asakir."

**Tabaqat Ibn Saad Juz. 3, Sehemu ya kwanza, Uk. 13:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Muhammad bin Umar bin Ali (as) kuwa alisema: "Wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipofika Madina aliunga udugu kati ya Muhajirina wao kwa wao, na akaunga tena udugu kati ya Muhajirina na Ansari, udugu huu ulikuwa kabla ya vita vya Badri, aliunga udugu kati yao katika haki na kusaidiana, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaungaudugu kati yake na Ali bin Abu Talib (as)."

**Nasema:** Pia katika uk.14 amepokea hadithi nyingine kutoka kwa Muhammad bin Umar bin Ali (as), humo amesema: "Hakika Mtume (saww) - wakati alipounga udugu kati ya Maswahaba zake - aliweka mkono wake kwenye bega la Ali (as) kisha akasema: 'Wewe ni ndugu yangu, utanirithi na mimi nitakurithi.' Iliposhuka Aya ya mirathi, hukumu hii ikakoma."

**ad-Durul-Manthur cha As-Suyutiy mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: "Hakika wale walioamini na wakahama na wakapigania Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao, na wale waliotoa mahala pa kukaa, na wakanusuru, hao ni marafiki na walinzi wao kwa wao." Iliyopo mwishoni mwa Sura al-Anfal:**

Amesema: Ibn Mardawayhi ameandika kutoka kwa Ibn Abbas kuwa amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa ameunga udugu baina ya Waislamu kati ya Muhajirina na Ansari, akaunga udugu kati ya Hamza bin Abdul Muttalib na Zayd bin Harithah, na kati ya Umar bin Khattab na Muadh bin Afrau, na kati ya Zubair bin Awam na Abdullah bin Mas'ud, na kati ya Abubakr na Talha bin Ubaydullah, na kati ya Abdur-Rahman bin Awfi na Saad bin Rabii, na akawaambia baadhi ya Maswahaba zake: 'Ungeni udugu, na huyu ni ndugu yangu –yaani Ali bin Abu Talib (as).'"

**ad-Durul-Manthur cha As-Suyutiy mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: "Akasema: Ewe Mola Wangu Mlezi! Nikunjulie kifua changu." Iliyopo mwanzoni mwa Sura Twaha:**

Amesema: as-Salafiy ameandika katika *at-Tuyuriyat* kutoka kwa Abu Ja'far Muhammad bin Ali (as) kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa juu ya mlima pindi ziliposhuka Aya: **'Na nipe waziri katika watu wangu. Harun, ndugu yangu. Kwake yeye niongeze nguvu zangu.'**Kisha akamwomba Mola Wake kwa kusema: 'Ewe MunguWangu niongeze nguvu kupitia ndugu yangu Ali.'Naye akamjibu hilo."

**Kanzul–Ummal, Juz. 6, Uk. 394:**

Amesema: Kutoka kwa Ali (as) amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliunga udugu kati ya Umar na Abubakr, na kati ya Hamza bin Abdul Muttalib na Zayd bin Harithah, na kati ya Abdullah bin Mas'ud na Zubair bin Awam, na kati ya Abdur–Rahman bin Awfi na Saad bin Malik, na kati yangu mimi na yeye mwenyewe." – Amesema: Ameiandika al-Khala'iy katika *al-Khala'iyat*, na pia ameiandika al-Bayhaqiy, al-Uqayliy, na Said bin Mansur.

**Nasema:** Na pia al-Muhibu Tabari ameitaja katika *ar-Riyadh an-Nadhrah* katika Juz.1, uk. 17, na amesema: "Ameiandikaal-Khala'iy.

**Kanzul–Ummal, Juz. 6, Uk. 400:**

Amesema: Kutoka kwa Abu Rafiu, kutoka kwa Abu Tamamah, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliunga udugu kati ya watu, akaunga udugu kati yake na Ali (as)." – Amesema: Ameiandika Ibn Asakir.

**Nasema:** Na pia al-Haythamiy ameitaja katika *Majmau* yake Juz. 9, uk. 112, na amesema: "Kutoka kwa Abu Umamah." Wala hajasema kutoka kwa Abu Tamamah. Kisha akasema: "Ameipokea Tabaraniy." Pia al-Munawi ameitaja katika *Faydhul–Qadir* katika Juz. 4, uk. 355, na amesema: "Tabaraniy anayo ndani ya *al-Awsat* na pia ad-Daylamiy."

**Kanzul–Ummal, Juz. 3, Uk. 155:**

Amesema: Kutoka kwa Zafir, kutoka kwa mtu mmoja, kutoka kwa Harith bin Muhammad, kutoka kwa Abu Tufayli Amir bin Wathilah, amesema: "Nilikuwa mlangoni siku ya Shura, mara sauti zikanyanyuka kati yao, nikamsikia Ali (as) akisema: 'Watu walimpa Abu Bakr kiapo cha utii, naapa Wallahi mimi ndiye ninayefaa zaidi na jambo hili kuliko yeye, na ndiye mwenye kustahiki zaidi jambo hili kuliko yeye. Lakini nilisikiliza na kutii ili watu wasirejee kwenye ukafiri na kuanza kuuwana kwa mapanga wao kwa wao. Kisha watu wakampa Umar kiapo cha utii, naapa wallahi mimi ndiye ninayefaa zaidi na jambo hili kuliko yeye, na ndiye mwenye kustahiki zaidi jambo hili kuliko yeye. Lakini nilisikiliza na kutii ili watu wasirejee kwenye ukafiri na kuanza kuuwana kwa mapanga wao kwa wao. Kisha nyinyi mnataka kumpa Uthman kiapo cha utii, hivyo niko tayarikusikiliza na kutii, kwani hakika Umar ameniweka katika kundi la watu watano na mimi nikiwa wa sita wao, hatambui ubora wangu juu yaokatika wema wala wao hawautambui kwangu, sisi sote katika sheria tupo sawa. Naapa kwa Mwenyezi Mungu laiti nikitaka kuzungumza kiasi kwambaasiwezekupinga hata sifa moja mtu yeyote kati yao, sawa mtu huyo awe mwarabuau asiyekuwa mwaarabu, au mwenye mkataba na Waislamu au Mushriku, nitafanya.'Kisha akasema: 'Nawaapizeni kwa Mwenyezi Mungunyinyi nyote, je kati yenu kuna yeyote asiyekuwa mimi ambaye ni ndugu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu?' Wakasema: 'Hakuna Wallahi.'"-Kisha aliendelea kusimulia hadithi ndefu - na akataja fadhila nyingi na tukufu ambazo kila moja itakujapeke yake katika mlango wake Inshaallah.

**Kanzul–Ummal, Juz. 3, Uk. 155:**

Ametaja hadithi kwa njia itokayo kwa Abu Dharr kuwa alisema: "Katika siku ya kwanza tangu Uthman apewe kiapo cha utii, Muhajirina na Ansari walikusanyika msikitini, na mara Ali bin Abu Talib (as) akaja na kuanza kusema: 'Hakika jambo wanalopasa kuanza nalo wenye kuanza, na kulitamka wenye kutamka na kulisema wenye kusema, ni kumuhimidi Mwenyezi Mungu na kumsifu kwa yale anayostahiki, na kumswalia Mtume (saww)' –kisha alileta hotuba ndefu mpaka aliposema: 'Nawaapizeni kwa Mwenyezi Mungu, je mnatambua kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: Wakati nilipopandishwa katika mbingu ya saba, kiliondolewa mbele yangu kizuizi kitokanacho na nuru, kisha likaondolewa mbele yangu pazia la nuru, hapo Mwenyezi Mungu akamfunulia Nabii (saww) mambo mbali mbali, aliporejea kutoka kwake, aliita mwenye kuita kutoka nyuma ya pazia, akasema:'Ewe Muhammad! Baba bora ni baba yako Ibrahim, na ndugu bora ni ndugu yako Ali.' Enyi Muhajirina na Ansari! Je mnatambua kuwa yalikuwa haya?' Abdur–Rahman bin Awfi akasema kati yao: 'Niliyasikia haya mawili kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), lasivyo masikio yangu yazibe….."'

**Kanzul–Ummal, Juz. 6, Uk. 122:**

Amesema: "Itakapofika Siku ya Kiyama nitaitwa kutoka ndani ya Arshi: 'Ewe Muhammad! Baba bora ni baba yako Ibrahim, na ndugu bora ni ndugu yako Ali.' Amesema: Ameiandika ar-Rafi'i kutoka kwa Ali (as).

**Kanzul–Ummal, Juz. 6, Uk. 161:**

Amesema: "Wakati nilipopandishwa katika mbingu ya saba, Jibril aliniambia: 'Tangulia ewe Muhammad, Wallahi hakunamalaika wa karibu wala Nabii aliyetumwa aliyewahi kupata heshima hii.' Mola Wangu akanifunulia kitu, na nilipoanza kurejea aliita mwenye kuita kutoka nyuma ya pazia: 'Baba bora ni baba yako Ibrahim, na ndugu bora ni ndugu yako Ali, basi muusie yeye kheri.'"- Na pia ameitaja katika uk.423.

**Kanzul–Ummal, Juz. 6, Uk. 398:**

Kutoka kwa Jabir amesema: "Nilimsikia Ali (as) akisoma shairi huku Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisikiliza:

'Mimi ni ndugu wa Mustafa, hapana shaka katika nasaba yangu.
Nimelelewa na yeye, na wajukuu zake ni wanangu.
Babu yangu na babu wa Mtume ni mmoja.
Na Fatimah ni mke wangu, hajawahi kunikosea.
Nimemwamini yeye huku watu wote wakiwa bado
wamo kwenye giza la upotovu, ushirikina na ukaidi.
Namhimidi na kumshukuru Mwenyezi Mungu,
Ambaye hana mshirika, mwenye kumtendea wema mja
na mwenye kubaki bila kuwa na mwisho.'

Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akatabasamu na akasema: "Umesema kweli ewe Ali."– Amesema: Ameiandika Ibn Asakir.

**Kanzul–Ummal, Juz. 3, Uk. 61:**

Amesema: Kutoka kwa Ibn Umar amesema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika Hija ya kuaga akiongea huku akiwa juu ya ngamia wake, alipiga mkono wake kwenye bega la Ali, akasema: 'Ewe Mungu Wangu mzidishie nguvu, ewe MunguWangu nimekwishafikisha. Huyu ni ndugu yangu na mtoto wa ami yangu, mkwe wangu na baba wa watoto wangu. Ewe MunguWangu mwingize motoni yeyote mwenye kumfanyia uadui.'" – Amesema: Ameiandika Ibn Najar.

**Nasema:** Na pia ameitaja katika Juz.6, uk. 154, na amesema humo: "Ewe Mungu Wangukuwa shahidi kwao, Ewe Mungu Wangu nimekwishafikisha…" Kisha akasema:"Ameiandika Shiraziy katika *al-Alqab*, na Ibn Najar kutoka kwa Ibn Umar."Na huenda neno 'mzidishie nguvu' katika riwaya ya mwanzo usahihi wake ni neno 'kuwa shahidi', na imekuwa hivyo kutokana na makosa ya chapa.

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 1, uk. 13:**

Amesema: Kutoka kwa Zayd bin Abi Awfa, amesema: "Niliingia kwenye msikiti wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), akasema: 'Yupo wapi fulani bin fulani?'akawa anaangalia nyuso za Maswahaba zake na kuwaulizia nakuwatumia ujumbe wa kuwaita kwake, mpaka wakakusanyika mbele yake. Walipojikusanya mbele yake, alimhimidi na kumshukuru Mwenyezi Mungu. Kisha akasema: 'Hakika mimi

ni mwenye kuwahadithia jambo hivyo lihifadhini na lizingatieni na muwahadithie watakao kuja baada yenu. Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ameteua viumbe kadhaa kutoka katika viumbe Wake.'Kisha akasoma: **"Hakika Mwenyezi Mungu huteua Mitume kutoka katika Malaika na miongoni mwa watu."**'Ni viumbe ambao atawaingiza peponi. Na hakika mimi namteua miongoni mwenu yule nipendaye kumteua, na ninaungaudugu kati yenu kama Mwenyezi Mungu alivyounga udugu kati ya Malaika wake" – Aliendelea kusimulia hadithi mpaka aliposema: "Katika kuunga udugu kati ya Maswahaba zake, Mtume (saww) aliwafanya wawili wawili kuwa ndugu – Aliendelea kusimulia hadithi mpaka aliposema: Ali (as) akasema:

'Hakika roho yangu imetoweka na uti wa mgongo wangu umekatika pale nilipokuona ukifanya kwa Maswahaba zako namna ambavyo hukunifanyia mimi, ikiwa hili ni kutoa adhabu kwangu basi kwako ni kwenye msamaha na ukarimu.' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Naapa kwa Yule aliyenituma kwa haki, sijakuchelewesha isipokuwa kwa ajili yangu mwenyewe, na wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu, na wewe ni ndugu yangu na mrithi wangu.' Akasema: 'Ni kipi nitakachorithi kutoka kwako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?' Akasema: 'Vile walivyorithiwa Manabii kabla yangu.' Akasema: 'Ni yapi waliyorithiwa Manabii kabla yako?' Akasema: 'Ni Kitabu cha Mola Wao na Sunnah za Nabii wao, na wewe utakuwa pamoja nami katika kasri peponi pamoja na binti yangu Fatimah.' Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasoma: **'wawe ndugu juu ya viti vya enzi wameelekeana.'** Wakipendana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wakitazamana wao kwa wao.'"

Amesema: Ameiandika al-Hafidh Abu Qasim ad-Damashqiy katika *Al-Arubain at-Twawaal*. Na Imam Ahmad bin Hanbal katika kitabu cha fadhila za Ali bin Abu Talib (as) ameandika kwa muhtasari maana ya hadithi ya undugu.

**Nasema:** Na al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzul-Ummal* katika Juz. 5 uk. 40, na amesema humo: "Kundi la maimamu kama vile al-Baghawi na Tabaraniy limeiandika hadithi hii katika *Muujam* zao, na pia al-Bawaridiy ameiandika katika *al-Maarifah*, na pia Ibn Adiy."

As-Suyutiy katika a*d-Durul-Manthur* mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: **"Hakika Mwenyezi Mungu huteua Mitume kutoka katika Malaika na miongoni mwa watu."** Iliyopo mwishoni mwa Sura al-Hajj, ameongeza idadi ya waliyoiandika, amesema: "Ameiandika Ibn Qaniu na Ibn Asakir, na ameitaja al-Mutaqiy kwa mara ya pili kwa muhtasari katika *Kanzul-Ummal*Juz. 5, uk. 40, na amesema humo: 'Ameiandika Ahmad bin Hanbal katika kitabu cha fadhila za Ali (as), na pia Ibn Asakir, na al-Muhibu Tabari ameitaja pia kwa ufupi sana kwa mara ya pili katika *Ar-Riyadh an-Nadhrah* Juz. 2, uk.209, na amesema humo: Kutoka kwa Zayd bin Abi Awfa, amesema: Hakika Mtume (saww) alimwambia Ali (as): 'Na wewe utakuwa pamoja nami katika kasri peponi pamoja na binti yangu Fatimah, na wewe ni ndugu yangu na rafiki yangu.'Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasoma: **"Wawe ndugu juu ya viti vya enzi wameelekeana.'"** – Amesema: Ameiandika Ahmad katika *al-Manaqib*.

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 1, uk. 15:**

Amesema: Ameandika Ibn Is'haqa alipotaja udugu ulioungwa kati ya Muhajirina na Ansari, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema:'Ungeni udugu wawili wawili kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.' Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaushika mkono wa Ali (as) na akasema: 'Huyu ni ndugu yangu.' HivyoMtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na Ali (as) wakawa ndugu, na Hamza bin Abdul Muttalib na Zayd bin Harithah mtumishi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) wakawa ndugu,

na Ja'far bin Abu Talib na Muadh bin Jabali ndugu wa Bani Salma wakawa ndugu."Akaendelea kuwataja Masahaba wengine wa Mtume waliobaki mpaka mwisho wao.

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 1, uk. 17:**

Amesema: Abu Amru bin Abdul-Bari amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliunga udugu kati ya Muhajirina wao kwa wao, kisha akaunga udugu kati ya Muhajirina na Ansari, na kila alipofanya hivyo alikuwa akisema kumwambia Ali (as): 'Wewe ni ndugu yangu duniani na Akhera.' Na akaunga udugu kati yake (Ali) na yeye mwenyewe."

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, uk. 168:**

Amesema: Kutoka kwa Umar bin Abdullah, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa babu yake kwamba Mtume (saww) aliunga udugu kati ya watu na akamwacha Ali (as), mpaka akawa wa mwisho na haoni nani wa kuwa ndugu yake, Ali (as) akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu!Umeunga udugu kati ya watu lakini umeniacha mimi!" Mtume akasema: "Unaona nimekuachа kwa sababu gani? Hakika nimekuacha kwa ajili yangu mwenyewe, wewe ni ndugu yangu na mimi ni ndugu yako, mtu yeyote akikusema mwambie: Mimi ni mja wa Mwenyezi Mungu na ndugu wa Mtume Wake, hawezi kudai hilo yeyote baada yangu isipokuwa muongo."

— Amesema: Ameiandika Ahmad katika *al-Manaqib*.

**Nasema:** Na pia al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzul–Ummal* Juz.6, uk. 153, na amesema: "Ameiandika Ibn Adiy katika *al-Kamil*uk. 399kwa tofauti kidogo katika tamko, na amesema: Ameiandika Abu Ya'ala."

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, uk. 201:**

Amesema: Kutoka kwa Mukhduju bin Zayd ad-Dhahliy amesema kuwa: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema kumwambia Ali (as): 'Tambua ewe Ali kuwa mtu wa kwanza atakayeitwa Siku ya Kiyama ni mimi -kisha aliendelea kusimulia hadithi kwa urefu mpaka aliposema-bendera ya himidi na akamkabidhi Ali (as)."Na tutaielezea (bendera ya himidi) katika mlango wake huko mbele Insha-Allah.- Aliendelea kusimulia hadithi mpaka aliposema:'Utakwenda na bendera hukuHasan akiwa kuliani kwako na Husain akiwa kushotoni kwako, mpaka utakaposimama kati yangu na Ibrahim (as) kwenye kivuli cha Arshi, kisha utavaa mapambo ya pepo, kisha ataita mwenye kuita kutoka chini ya Arshi: 'Baba bora ni baba yako Ibrahim; na ndugu bora ni ndugu yako Ali.'Furahia eweAli hakika wewe utavishwa nitakapovishwa, utaitwa nitakapoitwa, na utapendwa nitakapopendwa." – Amesema: Ameiandika Ahmad katika *al-Manaqib.*

**Dhakhairul-Uqba Uk. 92:**

Amesema: Kutoka kwa Anas bin Maliki, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipanda mimbari akakumbusha maneno mengi kisha akasema: 'Yupo wapi Ali bin Abu Talib?' Akachupa kwake na kusema: 'Ni mimi hapa ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Akamkumbatia kifuani mwake na akambusu kwenye macho yake na akasema kwa sauti ya juu: 'Enyi Waislamu! Huyu ni ndugu yangu na mtoto wa ami yangu, huyu ni nyama yangu, damu yangu na unywele wangu, huyu ndio baba wa wajukuu zangu wawili Hasan na Husain mabwana wa vijana wa peponi.'"

**Usudul-Ghabah Juz. 3, uk. 317:**

Ametaja hadithi kwa njia itokayo kwa Abdur-Rahman bin Awimu bin Saidah al-Ansariy, huyu alimdiriki Mtume (saww) na hata kabla ya Mtume (saww), amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Ungeni udugu wawili wawili kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.' Na akaushika mkono wa Ali (as) na akasema: 'Huyu ni ndugu yangu.'"

**Al–Istiab, Juz.2, Uk.460:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Tufail, amesema: "Wakati Umar alipokaribia kufariki aliweka Shura kati ya Ali (as), Uthman, Talha, Zubair, Abdur–Rahman bin Awfi na Saad, Ali (as) akawaambia: 'Nakuapizeni kwa Mwenyezi Mungu, je kati yenu nyinyi kuna yeyote asiyekuwa mimi ambaye Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliunga udugu kati yake na yeye Mtume (saww) pale alipounga udugu kati ya Waislamu?' Wakasema: 'Wallahi hakuna.'" – Amesema: Tumepokea kutoka kwa Ali (as) katika sura tofauti kuwa yeye (as) alikuwa akisema: "Mimi ni mja wa Mwenyezi Mungu na ndugu wa Mtume wake, hawezi kusema haya mwingine asiyekuwa mimi isipokuwa muongo."

**Hilyatul–Awliyai, Juz. 7, Uk.256:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Jabir, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Mlango wa pepo umeandikwa tangu miaka elfu moja kabla ya kuumbwa mbingu na ardhi: Hapana Mungu apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, na hakika Muhammad ni Mtume wa Allah, na Ali ni ndugu wa Mtume wa Allah.'"

**Nasema:** Pia al-Khatib al-Baghdadiy ameipokea katika *Taarikh* yake katika Juz.7, uk. 387, na pia al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzul-Ummal*Juz.6, uk. 159 akinukuu kutoka kwa al-Khatib kutoka katika *al-Mutafaq* na *al-Muftaraq*, nakutoka kwa Ibn al-Jawziy, na katika uk. 398 ameinukuu kutoka kwa Ibn Asakir. Na pia al-Munawi ameitaja katika *Faydhul-Qadir*katika Juz.4, uk.355 kwakunukuu kutoka kwa Tabaraniy kutoka katika *al-Awsat*, na ameitaja al-Muhibu Tabari katika *ar-Riyadh an-Nadhrah*katika Juz.2, uk.169 kwa kunukuu kutoka kwa Ahmad kutoka katika *al-Manaqib*.

**Taarikh Baghdad Juz. 12, Uk. 268:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Muhammad bin Ali bn Husain (as), kutoka kwa baba yake kutoka kwa Ali (as), amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Ewe Ali! Wewe ni ndugu yangu, swahiba wangu na rafiki yangu peponi.'"

**Nasema:** Ibn Abdul-Bari ameipokea katika *Isti'ab* yake katika Juz. 2, uk. 460 kutoka kwa Ibn Abbas.

**As-Sawa'iqul-MuhriqahUk. 74:**

Amesema: ad-Daylamiy ameandika kutoka kwa Aisha kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Ndugu yangu bora ni Ali na ami yangu bora ni Hamza, na kumtaja Ali (as) ni ibada."

**Nasema:** al-Munawi ameitaja katika *Faydhul–Qadir* katika Juz. 3, uk. 482 katika maelezo ya asili, na amesema: "Ad-Daylamiy ameiandika katika *Firdawsi* kutoka kwa Ibn Abbas bin Rabiah." Na pia al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzul–Ummal* Juz. 6, uk. 152, na amesema humo: "Katika *Firdawsi* ni kutoka kwa Aisha." Na pia Ibn Hajar ameitaja katika *Al-Isabah* yake katika Juz. 4, Sehemu ya kwanza, uk. 1.

**As-Sawa'iqul-MuhriqahUk. 75:**

Amesema: Ahmad ameandika katika *al-Manaqib* kutoka kwa Ali (as), amesema: "Mtume (saww) alinita bustanini, kisha akanipiga kwa miguu yake na kusema: 'Simama, Wallahi nimekuridhia kuwa wewe ni ndugu yangu na baba wa watoto wangu, pigania Sunnah yangu, yeyote atakayekufa na hali akiwa katika utawala wangu atakuwa katika hazina ya pepo. Na yeyote atakayekufa na hali akiwa katika utawala wako, atakuwa amekwishakufa kishahidi. Na yeyote atakayekufa na hali anakupenda baada ya kufa kwako, Mwenyezi Mungu atampa amani na imani wakati wote kadiri jua litakavyoendelea kuchomoza au kuzama."

**Kunuzul-Haqaiq cha al-Munawi Uk. 27:**

Amesema: Alisema: "Hivi huridhii kuwa wewe ni ndugu yangu na mimi ni ndugu yako!" – Amesema: Ni hadithi ya Tabaraniy.

**Nasema:** al-Haythamiy ameitaja katika *Majmauz-Zawa'id* Juz. 9, uk. 131.

**Majmauz-Zawa'id cha al-Haythamiy Juz. 9, Uk. 121:**

Amesema kutoka kwa Ali (as) alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alinitafuta na akanikuta nikiwa nimelala aridhini, akasema: 'Simama, si wenye kulaumiwa watu wakikuita Abu Turab.'" Ali anasema: "Akaniona kana kwamba nimehuzunishwa na hilo, akaniambia: 'Wallahi nimekuridhia, hakika wewe ni ndugu yangu na baba wa watoto wangu, utapigana kwa ajili ya kutetea Sunnah yangu na utaniondolea dhimma yangu. Yeyote atakayekufa na hali akiwa katika utawala wangu atakuwa katika hazina ya pepo. Na yeyote atakaye kufa na hali akiwa katika utawala wako, atakuwa amekwishakufa kishahidi. Na yeyote atakaye kufa na hali anakupenda baada ya kufa kwako, Mwenyezi Mungu atampa amani na imani wakati wote kadiri jua litakavyoendelea kuchomoza au kuzama. Na yeyote atakayekufa huku akiwa anakuchukia atakuwa amekufa kifo cha kijahiliya, na atahesabiwa kwa yale aliyoyafanya katika Uislamu.'"

— Amesema: Ameipokea Abu Ya'ala.

**Nasema:** al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzul–Ummal* Juz. 6, uk. 404 kutoka kwa Abu Ya'ala, kisha amesema: "al-Buswairiy amesema: Wapokezi wake ni watu waaminifu." Na katika uk.155 amesema:"Je sijakuridhisha ewe Ali! Wewe ni ndugu yangu na waziri wangu, utanilipia deni langu na utatekeleza ahadi yangu na utaondoa dhimma yangu." Na akasema: Ameiandika Tabaraniy kutoka kwa Ibn Umar, na pia Shan'qaytwiy ameitaja katika *Kifayatut-Talib*uk.34, na amesema: Ameiandika Ahmad katika *al-Manaqib.*

**Al-Isabah cha Ibn Hajar Juz. 8, Sehemu ya kwanza, Uk. 183, kwenye wasifu wa Laylah al-Ghafariyyah:**

Amesema: Ibn Mundah ameandika –kutoka kwenye riwaya ya Ali bin Hashim bin al-Baridu- amesema: Alinisimulia Laylah al-Ghafariyyah, amesema: "Nilikuwa napigana vita pamoja na Mtukufu Mtume (saww), nilikuwa nikiwapa huduma ya matibabu majeruhi, na kuwauguza wagonjwa. Alipotoka Ali (as) kwenda Basra (kwenda kwenye vita vya Ngamia) nilikwenda pamoja naye, nilipomuona Aisha nilimfuata na kumwambia: 'Je ulisikia fadhila yoyote ya Ali (as) kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)?' Akasema: 'Ndio, siku moja aliingia kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) wakati Mtume akiwa pamoja nami huku akiwa kajifunika nguo nzito. Alipoingia alikuja na kuketi baina yetu, nikasema: Hivi nafasi yote hii hujapata sehemu ya kuketi isipokuwa hii? Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema:

Ewe Aisha! Niachie ndugu yangu, hakika yeye ndiye mtu wa kwanza kuukubali Uislamu kabla ya watu wote, na ndiye mtu wa mwisho ambaye nitaagana naye, na ndiye mtu wa kwanza ambaye atakutana na mimi Siku ya Kiyama."'

## MLANGO USEMAO KUWA HAKIKA ALI (AS) NI WAZIRI WA MTUKUFU MTUME (SAWW)

**Tabaqat Ibn Saad, Juz. 1, Sehemu ya kwanza, Uk. 124:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ali (as) kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) wakati akiwa Makka alimwamrisha Bibi Khadija amtengenezee chakula, na akamwambia Ali (as): 'Niitie watoto wa Abdul Muttalib.' akawaita watu arobaini, akamwambia Ali: 'Lete chakula chako.'" Ali (as) anasema: "Nikawaletea chakula cha kuweza kula mtu mmoja kati yao, lakini wakala wote mpaka wakatosheka, kisha Mtume (saww) akasema: 'Wanyweshe.' Nikawanywesha kwa kutumia chombo ambacho ni cha ujazo wa kunywa mtu mmoja tu kati yao, wakanywa wote mpaka wakatosheka. Abu Lahbi akasema: 'Muhammad amekurogeni.' Wakatawanyika bila kuwalingania. Baada ya kukaa siku kadhaa aliwatengenezea tena chakula kama kile, kisha akaniamrisha niwakusanye na kisha akawalisha chakula, kisha akawaambia: 'Ni nani atakaye nisaidia katika hili nililonalo na atakaye niitikia ili awe ndugu yangu na malipo yake yawe ni pepo?' Nikasema: 'Mimi ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Wakati huo nilikuwa mdogo kwa umri na kimo kuliko wao wote, watu wote wakanyamaza kisha wakasema: 'Ewe Abu Talib!Je unamwona mtoto wako? Akajibu: 'Mwacheni kwani hatopata kutoka kwa mtoto wa ami yake isipokuwa kheri.'"

**Kanzul-Ummal Juz. 6, UK. 397:**

Amesema: Kutoka kwa Ali (as) amesema: "Ilipoteremka aya hii kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu: **'Waonye jamaa zako wa karibu.'** Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliniita na kuniambia: 'Ewe Ali, hakika Mwenyezi Mungu aliniamrisha niwaonye jamaa zangu wa karibu, hilo likawa gumu kwanguna nikatambua kuwa vyovyote nitakavyowaita katika jambo hili lazima nitashuhudia kutoka kwao yale nisiyoyapenda, hivyo nikajizuia kufanya hivyo mpaka aliponijia Jibril na kuniambia: 'Ewe Muhammad, ikiwa hautafanya unayoamrishwa, Mola Wako atakuadhibu.' Hivyo nitengenezee pishi la chakula, weka mguu wa kondoo na jagi la maziwa, kisha nikusanyie watoto wa Abdul Muttalib ili nizungumze nao na niwafikishie niliyoamrishwa.'

"Nikafanya aliyoniamrisha kisha nikawaita. Siku hiyo walikuwa watu arobaini kama walizidi au kupungua basi ni mtu mmoja, kati yao walikuwemo ami zakeAbu Talib, Hamza, Abbas na Abu Lahab. Walipokusanyika kwake aliniita ili niwaletee chakula nilichowaandalia nami nikawaletea. Nilipokiweka Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alichukua mfupa wa nyamaakauvunja kwa meno yake kisha akautupia kwenye sahani, kisha akasema: 'Kuleni kwa jina la Mwenyezi Mungu.'Wakala wote mpaka wakatosheka, na hatukuona isipokuwa alama za vidole vyao. Naapa kwa Mwenyezi Mungu chakula nilichowapa wote ni cha kutosha kula mtu mmoja miongoni mwao. kisha akasema: 'Wanyweshe watu ewe Ali.'Nikawaletea jagi lile na wakanywa mpaka wote wakatosheka. Naapa kwa Mwenyezi Mungukinywaji nilichowaletea ni cha kutosha kunywa mtu mmoja tu. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipotaka kuzungumza nao Abu Lahab alimtangulia kuzungumza kwa kusema: 'Jamaa yenu amekurogeni.' Hivyo watu wakatawanyika wala Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hakuweza kuzungumza nao.

"Ilipofika kesho yake Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliniambia: 'Ewe Ali! Hakika huyu mtu alinitangulia kwa kusema kauli uliyoisikia, hivyo jamaa wakatawanyika kabla sijazungumza nao, basi tuandalie mfano wa chakula na kinywaji ulichotuandalia jana, kisha wakusanye kwangu.'Nikaandaa kisha nikawakusanya, kisha akaniita niwaletee chakula, nami nikawaletea, naye akafanya kama alivyofanya jana, jamaa wakala na kunywa mpaka wakatosheka. Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akazungumza kwa kusema:

"'Enyi watoto wa Abdul Muttalib, Wallahi hakika mimi simtambui kijana yeyote katika Waarabu ambaye amewaletea watu wake jambo bora kushinda nililowaleteeni nyinyi. Hakika nimekuleteeni kheri ya duniani na Akhera. Hakika Mwenyezi Mungu ameniamrisha nikuiteni katika hilo, hivyo basi ni nani kati yenu atakayenisaidia katika jambo langu hili?' Nikasema – wakati huo nikiwa ndiye mdogo kiumri kushinda wao wote, mwenye macho yenye kung'aa, mwenye tumbo kubwa, na mfupi kuliko wao:'Mimi ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu nitakuwa msaidizi wako.'Akaishika shingo yangu na kusema: 'Hakika huyu ni ndugu yangu, wasii wangu na khalifa wangu kwenu, msikilizeni na mtiini.' Watu wakasimama huku wakicheka, wakimwambia Abu Talib: 'Amekuamrisha umsikilize na kumtii mwanao Ali.'" – Amesema: Ameiandika Ibn Is'haqa, Ibn Jarir, Ibn Abi Hatim, Ibn Mardawayhi, Abu Na'im, na al-Bayhaqiy ambaye kaiandika katika *ad-Dalail.*

**Nasema:** Hadithi hii nimeikuta katika *Taarikh* cha Ibn Jariri Tabari katika Juz. 2, uk. 62. Na pia al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzul–Ummal* kwa tofauti ndogo katika baadhi ya matamshi.

**Kanzul-Ummal, Juz.6, Uk. 392:**

Amesema: Kutoka kwa Ali (as), amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Enyi watoto wa Abdul Muttalib, hakika nimekuleteeni kheri ya duniani na Akhera. Mwenyezi Mungu ameniamrisha nikuiteni katika hilo, hivyo basi ni nani kati yenu atakayenisaidia katika jambo langu hili; ili awe ndugu yangu, wasii wangu na Khalifa wangu kwenu?' Watu wote wakakaa kimya, nikasema: 'Mimi ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu nitakuwa waziri wako katika hilo.' Akaishika shingo yangu na kusema: 'Hakika huyu ni ndugu yangu, wasii wangu na khalifa wangu kwenu, msikilizeni na mtiini.'– Amesema: Ameiandika Ibn Jarir.

**Kanzul-Ummal, Juz. 6, Uk. 155:**

Lafudhi yake ni: "Je sijakuridhisha ewe Ali? Wewe ni ndugu yangu na waziri wangu, utanilipia deni langu na utatekeleza ahadi yangu na utaondoa dhimma yangu. Yeyote atakayekupenda wakati wa uhai wangu atakuwa amekwishakufa kishahidi. Na yeyote atakayekupenda wakati wa uhai wako baada yangu, Mwenyezi Mungu atamhitimishia uhai wake kwa amani na imani. Na yeyote atakayekupenda baada yangu bila kukuona, Mwenyezi Mungu atamhitimishia uhai wake kwa amani na imani na atamsalimisha na mihangaiko ya siku ya fazaa. Na yeyote atakaye kufa huku akiwa anakuchukia atakuwa amekufa kifo cha kijahiliya, na Mwenyezi Munguatamhesabu kwa yale aliyoyafanya katika Uislamu." – Amesema: Ameiandika Tabaraniy kutoka kwa Ibn Umari.

**Al-Isabah Juz. 4, Sehemu ya kwanza, Uk. 217:**

Amesema: al-Khatib ametaja katika *al-Muutalaf* kwa njia ya Qasim bin Khalifa kuwa: Alitusimulia Abu Yahya Tamimiy kutoka kwa Isma'il bin Ibrahim, kutoka kwa Mutwin bin Khalid, kutoka kwa Anas bin Malik, amesema: "Tulikuwa tunapotaka kumuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuhusu

jambo lolote, tunamwamrisha Ali (as) au Salman au Thabit bin Muadh, kwa sababu wao walikuwa-Maswahabawenye ujasiri kwake, hivyo ilipoteremka:**'Itakapokuja nusura ya Mwenyezi Mungu na ushindi.'**Hapo akataja hadithi yenye kuelezea fadhila za Ali (as). Katika hadithi hiyo kuna: "Hakika yeye ni ndugu yangu, waziri wangu na khalifa wangu katika watu wangu na ndiye mbora ninayemuacha baada yangu."

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, uk. 163:**

Amesema: Kutoka kwa Asmau binti Umays, amesema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Ewe Mungu Wangu, hakika mimi nasema kama alivyosema ndugu yangu Musa: Ewe Mungu Wangu! Nipe msaidizi katika ndugu zangu, ndugu yangu Ali, niongezee nguvu kupitia yeye na mshirikishe katika jambo, langu ili tukutakase sana na tukukumbuke sana, hakika Wewe unatuona.'" – Amesema: Ameiandika Ahmad katika *al-Manaqib*.

**Ad-Durul-Manthur ya As-Suyutiy, katika tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: "Akasema: Ewe Mola Wangu Mlezi! Nikunjulie kifua changu." Iliyoko mwanzoni mwa Sura Twaha:**

Amesema: as-Salafiy ameandika katika *at-Tuyuriyat* kutoka kwa Abu Ja'far Muhammad bin Ali (as) kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa juu ya mlima pindi ziliposhuka Aya: **"Na nipe waziri katika watu wangu. Harun, ndugu yangu. Kwake yeye niongeze nguvu zangu.'** Kisha akamwomba Mola Wake kwa kusema: 'Ewe Mungu Wangu, niongeze nguvu kupitia ndugu yangu Ali.' Naye akamjibu hilo."

**Nurul-Absari cha Shablanjiy, na Tafsirul-Kabir cha Razi, mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Hakika walii wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake" iliyopo katika Sura al-Maidah:**

Tamko hapa ni la Shablanjiy, amesema katika uk. 70: Kutoka kwa Abu Dharr al-Ghafariy, amesema: "Siku moja niliswali Swala ya Dhuhri pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), muombaji akaomba msikitini na hakuna mtu yeyote aliyempa kitu. Muombaji akanyanyua mikono yake mbinguni na kusema:'Ewe MunguWangu! Shuhudia kuwa hakika mimi nimeomba katika msikiti wa Nabii Wako Muhammad (saww) na wala hakuna yeyote aliyenipa chochote.' Ali (as) alikuwa kwenye rukuu akiswali, basi akamnyooshea kidole pete chake cha mkono wakulia ambacho kilikuwa na pete, mwombaji yule akaichukua ile pete kutoka katika kidole chake, tena mbele ya macho ya Mtukufu Mtume (saww) ambaye alikuwa msikitini.

"Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akanyanyua macho yake mbinguni na kusema: 'Ewe Mungu Wangu! Hakika ndugu yangu Musa alikuomba kwa kusema: **'Ewe Mola Wangu Mlezi! Nikunjulie kifua changu. Na unifanyie nyepesi kazi yangu. Na ulifungue fundo lililo katika ulimi wangu. Wapate kufahamu maneno yangu. Na nipe waziri katika watu wangu. Harun, ndugu yangu. Kwake yeye niongeze nguvu zangu. Na umshirikishe katika kazi yangu.'** Ukamteremshia: **'Tutautia nguvu mkono wako kwa nduguyo na tutakupeni madaraka hivyo hawatakufikieni.'** Ewe Mungu! Hakika na mimi ni Muhammad Nabii Wako na kipenzi Chako. Ewe Mungu Wangu! Nikunjulie kifua changu. Na unifanyie nyepesi kazi yangu. Na nipe waziri katika watu wangu. Ali, ndugu yangu. Kwake yeye niongeze nguvu zangu." - Abu Dharr anasema: "Hata kabla dua yake haijamalizika, Jibril (as) akawa ameteremka kutoka kwa Allah na kusema: 'Ewe Muhammad, soma: **'Hakika walii wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na walioamini, ambao hushika Swala na hutoa Zaka hali wamerukuu.'"** – Amesema: Ameinukuu Abu Is'haq Ahmad Thaalabiy katika tafsiri yake.

# MLANGO UNAOZUNGUMZIA KAULI YA MTUKUFU MTUME (SAWW): ALI (AS) NI SEHEMU YANGU NA MIMI NI SEHEMU YA ALI (AS)

**Sahih Bukhari, katika sulhu, Mlango unaozungumzia: Hivi ndivyo walivyopatana fulani bin fulani:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa al-Barau bin Azib, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikenda Umrah katika mwezi wa Dhul-Qaada, lakini watu wa Makka wakakataa kumruhusu kuingia mpaka wapatane kwamba atakaa humo muda wa siku tatu. Walipoandikiana mkataba waliandika: 'Haya ndio aliyoafikiana Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Wakasema: 'Hatutambui hilo, lau tungekuwa tunatambua kuwa wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu tusingekuzuia, isipokuwa wewe ni Muhammad bin Abdullah.' Akasema (Mtume): 'Mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na ni Muhammad bin Abdullah.' Kisha akamwambia Ali (as): 'Futa (neno) Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Ali (as) akasema: 'Naapa kwa Mwenyezi Mungu sintokufuta kamwe.' Mtume wa Mwenyezi Mungu akachukua ile karatasi akaandika: 'Haya ndio aliyoafikiana Muhammad bin Abdullah, kuwa asiingie Makka akiwa na silaha isipokuwa katika ala yake, na wala asitoke na yeyote miongoni mwa watu wa Makka ikiwa mtu huyo atataka kumfuata, na wala asimzuie yeyote miongoni mwa Maswahaba zake ikiwa atataka kuishi Makka.'

"Alipoingia Makka na muda waliokubaliana ukaisha, walimfuata Ali (as) na kumwambia: 'Mwambie jamaa yako atoke kwetu kwani muda (tuliokubaliana) umekwisha.' Hapo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akatoka. Binti ya Hamza akawafuata huku akinadi: 'Ewe ami yangu, ewe ami yangu.' Ali (as) akamshika mkono, na akamwambia Fatimah (as): 'Mtunze mtoto wa ami yako.' Naye akamchukua, na ndipo pakatokea mzozo kati ya Ali (as), Zayd na Ja'far (kila mmoja akitaka amtunze yeye), Ali (as) akasema: 'Mimi nina haki naye zaidi kwakuwa yeye ni mtoto wa ami yangu.' Akasema Ja'far: 'Ni binti ya ami yangu na mama yake mdogo yuko chini yangu.' Na Zayd akasema: 'Ni binti ya ndugu yangu.' Ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawasuluhisha kwa kumpeleka kwa mama yake mdogo, na akasema: 'Mama mdogo ana nafasi ya mama mzazi.' Na akamwambia Ali: 'Wewe ni sehemu yangu na mimi ni sehemu yako.' Na akamwambia Ja'far: 'Umefanana na mimi kimaumbile na kitabia.' Na akamwambia Zayd: 'Wewe ni ndugu yetu na mtumishi wetu.'"

**Nasema:** Bukhari ameitaja tena kwa mara ya pili kwa sanad na matini ile ile, katika kitabu kinachozungumzia mwanzo wa uumbaji, katika mlango wa Umrah ya kulipa. Na ameipokea al-Bayhaqiy katika *Sunan* yake kutoka kwa al-Barau, katika Juz. 8, uk. 5. Na pia an-Nasaiy katika *Khasa'is* yake, katikauk.51 kutoka kwa al-Barau. Na pia Ahmad bin Hanbal ameiandika kwa tofauti ndogo katika matamshi, katika *Musnad* yake, katika Juz. 1, uk. 98, kutoka kwa Hani bin Hani, kutoka kwa Ali (as). Pia al-Hakim ameiandika katika *Mustadrakus-Sahihayn*, katikaJuz.3, uk.120, kutoka kwa Hani bin Hani. Na Tabarikaiandika katika *Mushkilul-Athar*, katika Juz.4, uk. 173, kutoka kwa Hani bin Habirah, kutoka kwa Ali. Na al-Khatib al-Baghdadiy ameiandika katika *Taarikh* yake, katika Juz.4, uk. 140, kutoka kwa Hani bin Habirah, kutoka kwa Ali (as).

**Sahihi Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 297:**

Ameipokea kwa njia yake kutoka kwa Imran bin Huswin, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alituma jeshi, na akamteua Ali bin Abu Talib (as) kuwa kiongozi wa kikosi hicho. Alipokwenda Ali (as) alipata suria, lakiniwengine hawakuridhika na jambo hilo, hivyo watu wanne miongoni mwa Maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) wakakubaliana kuwa:'Tutakapokutana na Mtume wa

Mwenyezi Mungu (saww) tutamueleza aliyofanya Ali (as).’Na ilikuwa ni kawaida Waislamu wanaporudi vitani, kwanza hupitia kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kumsalimu kisha ndipo huenda zao, hivyokikosi kiliporudi kilikwenda kumsalimu Mtume, na ndipo akasimama mmoja kati ya wale wanne, akasema: ‘Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu!Hivi humuoni jinsi alivyofanya haya na haya? Ali bin Abi Talib alifanya haya na haya!’Lakini Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akampuuza. Kisha akasimama wa pili na akasema kama alivyosema mwenzake, lakini Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akampuuza. Kisha akasimama wa tatu akasema kama walivyosema wale wawili, lakini Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akampuuza. Kisha akasimama wa nne naye akasema kama walivyosema wenzake, hapo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawaelekea na kusema -huku hasira ikionekana usoni mwake : ‘Mnataka nini kutoka kwa Ali?Mnataka nini kutoka kwa Ali? Mnataka nini kutoka kwa Ali? Hakika Ali ni sehemu yangu, na mimi ni sehemu ya Ali, naye ndiye mtawala wa kila muumini baada yangu.’”

**Nasema:** Na pia Ahmad bin Hanbal ameipokea katika Juz.4, uk.438. Na piaal-Hakim ameipokea katika *Mustadrakus-Sahihayn*, katika Juz.3, uk.110. Na Abu Daud at-Twayalasiy ameiandika katika *Musnad* yake, katika Juz.3, uk.111. Na Abu Na’imameiandika katika *Hilyatul-Awliyai*, katika Juz.6, uk.294. Na al-Mutaqiy ameiandika katika *Kanzul-Ummal*, katika Juz.6, uk.399 kwa kunukuu kutoka kwaIbn Jariri, na kuwa yeye amesema ni hadithi sahihi, na pia kwa kunukuu kutoka kwa Ibn Abi Shayba, katika Juz.6, uk.154 ameinukuu kwa njia mbili fupi kutoka kwa Ibn Abi Shayba. Na pia ameipokea an-Nasaiy katika *Khasa’is*uk.23.

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 299:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa al-Barau bin Azib kwamba Mtukufu Mtume (saww) alimwambia Ali bin Abu Talib (as): “Wewe ni sehemu yangu na mimi ni sehemu yako.”

**Nasema:** Pia ameipokea an-Nasaiy katika *Khasa’isu* yake, katika uk. 19.

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, Uk. 299:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Habashiy bin Junadah, amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: Ali ni sehemu yangu, na mimi ni sehemu ya Ali. Wala hafikishi kwa niaba yangu isipokuwa mimi mwenyewe au Ali.”

**Nasema:** Na Ibn Majah ameitaka katika *Sahih* yake, katika uk.12. Na Ahmad bin Hanbal ameiandika katika njia tano katika *Musnad* yake, katika Juz. 4, njia mbili ni katika uk.164, na zilizobaki ni katika uk.165. Na pia an-Nasaiy ameiandika katika *Khasa’isu* yake kwa njia mbili, moja ni katika uk.19, na nyingine ni katika uk.20. Na pia ameitaja al-Muhibu Tabari katika *ar-Riyadh an-Nadhrah*, katika Juz.2, uk. 174, na amesema: “Ameiandika al-Hafidh as-Salafiy.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 1, Uk. 108:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Hani bin Hani, kutoka kwa Ali (as), amesema: “Nilikuja kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Ja’far na Zayd. Akasema kumwambia Zayd: ‘Wewe ni mtumishi wangu.’ Zayd akaona haya, akasema kumwambia Ja’far: ‘Wewe umefanana nami kimaumbile na kitabia.’Ja’far akaona haya akajifisha nyuma ya Zayd. Na akaniambia mimi: ‘Wewe ni sehemu yangu, na mimi ni sehemu yako.’Nami nikaona hayanikajificha nyuma ya Ja’far.”

**Nasema:** Na ameipokea al-Bayhaqiy katika *Sunan* yake, katika Juz.10, uk. 226, na an-Nasaiyameipokea kwa tofauti ndogo ya tamko katika *Khasa’isu* yake, katika uk. 51.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 5, Uk. 356:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Buraydah, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alituma vikosi viwili vya jeshi kwenda Yemen, cha kwanza kilikuwa chini ya uongozi wa Ali bin Abu Talib (as), na cha pili kilikuwa chini ya uongozi wa Khalid bin Walid, akasema: 'Mtakapokutana Ali ndiye atakuwe Amiri wa watu wote, na mtakapoachana kila mmoja miongoni mwenu nyinyi wawili atakuwa kiongozi wa kikosi chake.'"

Buraydah anasema: "Tukakutana na Bani Zayd katika watu wa Yemen tukapigana nao, Waislamu wakawashinda Mushirikina, tuliwauwa wengi na tukawachukua mateka dhuria wao. Ali (as) akajichagulia mwanamke mmoja kutoka katika mateka wale, ndipo Khalid bin Walid akanipa barua nimpelekeeMtume wa Mwenyezi Mungu (saww), ya kumpa habari juu ya tukio hilo. Nilipokwenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) nilimkabidhi ile barua naye akaisoma, mara nikaona ghadhabu katika uso wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), nikamwambia: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! hii ni sehemu ya mwenye kujilinda, ulinituma niwe pamoja na mtu ambaye umeniamrisha nimtii, nami nimefanya kama ulivyonituma.'Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Usimtuhumu Ali, hakika yeye ni sehemu yangu, na mimi ni sehemu yake, naye ni Walii wenu baada yangu.'

**Nasema:** al-Haythamiy ameitaja katika *Majmau* yake, katika Juz.9, uk.127, na amesema: "Ameipokea Ahmad na Bazar kwa ufupi." Na pia an-Nasaiy ameitaja katika *Khasa'is* yake kwa tofauti ndogo katika baadhi ya matamshi, katika uk. 23, na amesema humo:"Khalid bin Walid akamwandikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) barua na akaniamrisha nimshutumu – yaani Ali, nikampa ile barua na kumshutumu Ali (as), mara uso wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ukabadilika na akasema: 'Msinibughudhie Ali ewe Buraydah, hakika Ali ni sehemu yangu, na mimi ni sehemu yake, naye ndiye Walii wenu baada yangu."Na ameitaja tena al-Haythamiy kwa mara ya pili katika Juz. 9, uk. 128, amesema humo:"Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akatoka hali ameghadhibika, akasema: 'Wana nini watu ambao wanamtia doa Ali? Mwenye kumtia doa Ali amenitia doa mimi, na yeyote mwenye kujitenga na Ali amenitenga mimi. Hakika Ali ni sehemu yangu na mimi ni sehemu ya Ali, ameumbwa kutokana na udongo wangu, nami nimeumbwa kutokana na udongo wa Ibrahim, na mimi ni bora kuliko Ibrahim – mpaka aliposema: Ewe Buraydah! Hivi hujui kuwa Ali ana suria wengi kuliko huyo aliyemchukua, na kuwa yeye ndiye Walii wenu baada yangu?' Nikasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kwa haki ya uswahaba naomba ukunjue mkono wako ili nikupe kiapo cha utii katika Uislamu upya." Buraydah anasema: "Sikuondoka ila baada ya kuwa nimempa kiapo cha utii katika Uislamu." – Amesema: Ameipokea Tabaraniy katika *al-Awsat*.

**Nasema:** Pia al-Mutaqiy ameitaja kwa ufupi katika *Kanzul–Ummal*, katika Juz. 6, uk.154, na amesema: "AmeipokeaIbn Abi Shaybah kutoka kwa Abdullah bin Buraydah kutoka kwa baba yake."

**Musnad Imam Ahmad Hanbal, Juz. 1, Uk. 330:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Amru bin Maimuna kuwa alisema: "Wakati nikiwa nimeketi kwa Ibn Abbas mara alijiwa na watu tisa, wakasema: 'Ewe mtoto wa Abbas ima unyanyuke pamoja nasi na ima hawa ulionao watupishe.' Ibn Abbas akasema: 'Bali nanyanyuka pamoja nanyi.' Wakati huo alikuwa bado mzima hajapofuka, walikwenda pembeni na kuanza kuzungumza, na hatujui walizungumza nini. Mara alirudi huku akipukuta nguo yake na kusema: 'Ole wao, ole wao, wanawezaje kumtuhumu mtu mwenye mambo kumi –aliendelea kusimulia mpaka aliposema: Kisha alimtuma Fulani aende na Sura Tawba, akamtuma Ali nyuma yake kwenda kuichukua toka kwake (toka kwa huyo Fulani), akasema (saww): 'Haendi nayo isipokuwa mtu ambaye yeye ni sehemu yangu na mimi ni sehemu yake.'" Hadithi hii imetangulia kwa ukamilifu wake katika Mlango unaozungumzia Aya ya Utakaso, rejea huko.

**Nasema:** Pia ameipokea an-Nasaiy ndani ya*Khasa'isu* yake, katika uk. 8, na ameitaja al-Muhibu Tabari ndani ya *ar-Riyadh an-Nadhrah*, katika Juz. 2 uk. 203, na amesema: "Ameiandika kwa ukamilifu wake Ahmad na al-Hafidh Abul-Qasim ad-Damashqiy ndani ya *al-Muwafaqat* na ndani ya *al-Ar'bauna at-Twawali*." Na amesema: "Ameiandika an-Nasaiy kwa ufupi." Na ameitaja al-Haythamiy ndani ya *Maj'mau* yake katika Juz. 9, uk. 119, na amesema: "Ameipokea Ahmad na Tabaraniy ndani ya *al-Kabir* na ndani ya *al-Awsat* kwa muhtasari."

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 19:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Imran bin Huswin, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Hakika Ali ni sehemu yangu, na mimi ni sehemu yake, na yeye ndiye Walii wa kila muumini baada yangu.'"

**Khasa'isun-Nasaiy Uk.36:**

"Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Ama wewe ewe Ali, wewe ni ndugu yangu na baba wa watoto wangu, na wewe ni sehemu yangu, na mimi ni sehemu yako.'"

**Khasa'isun-Nasaiy Uk.19:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Habirah bin Maryam na Hani bin Hani, kutoka kwa Ali (as), amesema: "Wakati tulipotoka Makka mara alikuja binti ya Hamza huku akiita: 'Ewe ami yangu, ewe ami yangu!' Ali (as) akamchukua na kumbeba, akamwambia mkewe: 'Mtunze mtoto wa ami yako.' Naye akamchukua, na ndipo pakatokea mzozo kati ya Ali (as), Zayd na Ja'far (kila mmoja akitaka amtunze yeye), Ali (as) akasema: 'Mimi nimemchukua kwakuwa yeye ni mtoto wa ami yangu.' Ja'far akasema: 'Ni binti ya ami yangu na mama yake mdogo yuko chini yangu.' Na Zayd akasema: 'Ni binti ya ndugu yangu.' Ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawasuluhisha kwa kumpeleka kwa mama yake mdogo, na akasema: 'Mama mdogo ana nafasi ya mama mzazi.' Na akamwambia Ali: 'Wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa, na mimi ni sehemu yako.' Na akamwambia Ja'far: 'Umefanana na mimi kimaumbile na kitabia.' Na akamwambia Zayd: 'Wewe ni ndugu yetu na mtumishi wetu.'"

**Taarikh Ibn Jarir Tabari Juz. 2, Uk. 197:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abi Rafii kutoka kwa baba yake, kutoka kwa babu yake, amesema: "Wakati Ali bin Abu Talib (as) alipowauwa watu wa Alwiyah, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliliona kundi la Mushrikina wa Kikuraishi, akamwambia Ali (as): 'Washambulie.' Akawashambulia na akafanikiwa kulitawanya, na akamuua Amru bin Abdullah Jamhiy. Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaliona tena kundi la Mushrikina wa Kikuraishi, akamwambia Ali (as): 'Washambulie.' Akawashambulia na akafanikiwa kulitawanya, na akamuua Shaybah bin Maliki ambaye alikuwa ni mmoja kati ya wa Bani Amir bin Luay, ndipo Jibril (as) akasema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Hakika huu ndio msaada.'Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Hakika yeye ni sehemu yangu, na mimi ni sehemu yake.' Jibril (as) akasema:'Na mimi ni sehemu yenu ninyi.'Wakasikia sauti ikisema: 'Hapana upanga isipokuwa Dhulfiqar, wala hakuna kijana isipokuwa Ali.'"

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, uk. 172, na al-Mirqat cha Ali bin Sultan Juz. 2, uk. 568, katika ufafanuzi:**

“Wakati Ali bin Abu Talib (as) alipowauwa watu wa Alwiyah siku ya Uhudi, Jibril (as) alisema: ‘Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Hakika huu ndio msaada.’Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: ‘Hakika yeye ni sehemu yangu, na mimi ni sehemu yake.’ Jibril (as) akasema: ‘Na mimi ni sehemu yenu ninyi.’ – Wamesema: Ameiandika Ahmad katika *al-Manaqib*.

**Nasema:** Pia al-Haythamiy ameitaja katika*Majmau* yake, katika Juz. 6, uk. 114, na amesema: “Ameipokea Tabaraniy.” Pia al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzul-Ummal*, katika Juz. 6, uk. 400 kwakunukuu kutoka kwa Tabaraniy.

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, uk. 202:**

Amesema: Abu Said amepokea katika habari za utukufu wa unabii kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Ali (as):“Umepewa mambo matatu ambayo hajapewa yeyote hata mimi mwenyewe: Umepewa mkwe mfano wangu, wala mimi sijapewa mkwe kama mimi, umepewa mke mkweli mfano wa binti yangu, wala sijapewa mke mfano wake (Fatimah), na umepewa Hasan na Husain (as) kutoka katika mgongo wako, wala sijapewa kutoka katika mgongo wangu mfano wa hao wawili, lakini nyinyi ni sehemu yangu, na mimi ni sehemu yenu.”

**Kunuzul-Haqaiq cha al-MunawiUk. 37:**

Tamko lake ni: “Hakika Ali ni sehemu yangu, na mimi ni sehemu yake, naye ndiye Walii wa kila muumini.” – Amesema: Ni ya Tabaraniy.

**Kanzul-Ummal Juz. 3, uk. 123:**

Amesema: Kutoka kwa Ali (as) amesema: “Zayd bin Harithah alikwenda Makka, akamleta binti ya Hamza bin Abdul Muttalib, Ja’far bin Abu Talib akasema: ‘Namchukua mimi kwani mimi nina haki naye zaidi kwakuwa yeye ni binti wa ami yangu na mama yake mdogoyuko kwangu (ndiye mke wangu), na mama mdogo ni sawa na mama mzazi na ndiye mwenye haki zaidi.’Ali (as) akasema:‘Isipokuwa mimi nina haki naye zaidi kwani yeye ni bintiya ami yangu, na bintiya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) yuko kwangu (ndiye mke wangu), naye ana hakinaye zaidi, hakika mimi nanyanyua sauti yangu ili Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) asikie hoja zangu kabla hajatoka.’ Zayd akasema:‘Mimi nina haki naye zaidi, kwani nilisafiri kwenda (Makka) kumchukua, na nikamleta.’

“Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akatoka na kusema: ‘Mna jambo gani?’ Ali (as) akasema:‘Bintiya ami yangu, mimi nina haki naye zaidi, na binti ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) yuko kwangu, hivyo yeye ana haki zaidi ya kuwa pamoja naye kuliko mwingine yeyote.’ Ja’far akasema: ‘Mimi nina haki naye zaidi ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), kwanza ni binti ya ami yangu, pili mama yake mdogo yuko kwangu, na mama mdogo ni sawa na mama mzazi, naye ndiye mwenye haki naye zaidi kuliko mwingine yeyote.’ Zayd akasema:‘Mimi ndiye mwenye haki naye zaidi ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), kwani nilisafiri kwenda (Makka) kumchukua na nikamgharamikia, hivyo mimi ndiye mwenye haki naye zaidi.’

“Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: ‘Nitatoa hukumu kati yenu katika hili na katika mengine.’ Ali (as) anasema: ‘Aliposema: Na katika mengine, nikasema: Huenda Qur’ani imeteremka kwa sababu ya sisi kunyanyua sauti zetu. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: ‘Ama wewe

ewe Zayd bin Harithah, wewe ni mtumishi wangu na mtumishi wake.' Zayd akasema: 'Nimeridhia ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Mtume akasema: 'Ama wewe ewe Ja'far, wewe unafanana nami sana kiumbile na kitabia, na wewe unatokana na mti (ukoo) niliotokea.' Ja'far akasema: 'Nimeridhia ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Mtume akasema: 'Ama wewe ewe Ali, wewe ni chaguo langu namwaminifu kwangu, na wewe ni sehemu yangu, na mimi ni sehemu yako.' Nikasema: 'Nimeridhia ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Akasema:'Ama binti nimekwisharidhia achukuliwe na Ja'far kwani atakuwa pamoja na mama yake mdogo, na mama mdogo nisawa na mama mzazi.' Wakasema:'Tumekubaliewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.'" – Amesema: Ameiandika Adaniy, Bazar na Ibn Jariri.

**Nasema:** Na pia ameipokea at-Twahawiy kwa tamko tofauti, katika *Mushkilul-Athar*, katika Juz. 4 uk. 174, na pia ameipokea tena kwa tamko tofauti, kwa njia mbili nyingine, katika uk. 175. Na pia an-Nasaiy amepokea sehemu tu ya hadithi hii katika *Khasa'isu*yake, katika uk.20, na amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: 'Ama wewe ewe Ali, wewe ni chaguo langu na mwaminifu kwangu.'"

## MLANGO UNAOSEMA KUWA HAKIKA ALI (AS) NYAMA YAKE NI NYAMA YA MTUME (SAWW) NA DAMU YAKE NI DAMU YA MTUKUFU MTUME (SAWW)

**Taarikh Baghdad cha al-Khatib al-Baghdadiy Juz. 2, Uk. 204:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abul Abbas, amesema: "Nilikuwa kwa Mtume (saww) huku juu ya paja lake la kushoto akiwa amempakata mwanae Ibrahim, na juu ya paja lake la kulia amempakata Husain bin Ali (as), mara anambusu huyu na mara anambusu huyu, ndipo Jibril (as) akateremka kwake na wahyi kutoka kwa Mola wa walimwengu. Baada ya Jibril kuondoka Mtume (saww) akasema: Jibril amenijia kutoka kwa Mola Wangu, ameniambia: "Ewe Muhammad! hakika Mola Wako anakutolea salamu anakwambia: Wako ni mmoja si wote wawili, hivyo mtoe fidia mmoja wao kwa mwenyewe."Mtume (saww) akamwangalia Ibrahim akalia, na akamwangalia Husain (as) akalia, kisha akasema:'Hakika Ibrahim mama yake ni kijakazi, hivyo atakapofariki hakuna mwingine zaidi yangu atakayemhuzunikia. Ama mama yake na Husain (as) ni Fatimah na baba yake ni Ali (as) ambayeni nyamayangu na damu yangu. Atakapokufa atahuzunika binti yangu na mtoto wa ami yangu, na mimi pia nitamhuzunikia, na ni bora nihuzunike mimi kuliko wao wahuzunike. Ewe Jibril!Mchukue Ibrahim.'"- Itakuja kwa ukamilifuwake wakati wa kuzungumzia fadhila za Husain (as) Insha'Allah.

**Dhakhairul-Uqba Uk. 92:**

Amesema: Kutoka kwa Anas bin Maliki, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipanda mimbari akakumbusha maneno mengi kisha akasema: 'Yupo wapi Ali bin Abu Talib?' Akachupa kwake na kusema: 'Ni mimi hapa ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Akamkumbatia kifuani mwake na akambusu kwenye macho yake na akasema kwa sauti ya juu: 'Enyi Waislamu! Huyu ni ndugu yangu na mtoto wa ami yangu, huyu ni nyama yangu, damu yangu na unywele wangu, huyu ndio baba wa wajukuu zangu wawili Hasan na Husain mabwana wa vijana wa peponi.'" - Itakuja kwa ukamilifu wake katika milango inayofuata Insha'Allah.

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 9, uk. 111:**

Amesema: Na kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia Ummu Salama: 'Huyu ni Ali bin Abu Talib, nyama yake ni nyama yangu na damu yake ni damu yangu,

na yeye ana cheo kwangu sawa na cha Haruna kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu.'" - Amesema: Ameipokea Tabaraniy.

**Nasema:** Pia ameitaja al-Mutaqiy katika *Kanzul-Ummal*, katika Juz. 6, uk. 154, na amesema humo: "Ewe Ummu Salimu! -mpaka akasema: Ameiandikaal-Uqayliy kutoka kwa Ibn Abbas. Na pia ameitaja al-Munawi katika *Kunuzul-Haqaiq,* katika uk.161 kwa kunukuu kwa ufupi kutoka kwa Tabaraniy.

## MLANGO UNAOSEMA HAKIKA ALI (AS) NI NAFSI YA MTUKUFU MTUME (SAWW)

**Nasema:** Zimekwisha kutangulia habari nyingi katika Mlango unaozungumzia Maapizano, kuwa ilipoteremka kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **"Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wanawake zetu na wanawake zenu, na sisi wenyewe na nyinyi wenyewe,"**Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliwaita Ali, (as) Fatimah, Hasan na Husain (as), hivyo Ali (as) akawa ndiyo nafsi ya Mtume (saww), Fatimah ni wanawake zetu, na Hasan na Husain (as) ni watoto zetu. Hivyo hata kama pasingekuwa na dalili nyingine inayojulisha kuwa Ali (as) ni nafsi ya Mtume (saww) isipokuwa Aya hii tukufu, basi Aya hii ingetosha kutokana na tafsiri yake iliyotangulia huko nyuma. Lakini pamoja na hayo tunazo pia hadithi nyingine ambazo zajulisha hilo, nasi hapa tunataja sehemu tu ya hadithi hizo kwa haraka haraka, tunasema:

**Mustadrakus-Sahihain Juz. 2, uk. 120:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdur-Rahman bin Awfi, amesema: "Baada yaMtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuikomboa Makka alikwenda Twaif, akawazingira siku nane au saba, kisha aliwavamia asubuhi au jioni, kisha akateremka, kishaakaondoka, kisha akasema: 'Enyi watu hakika mimi nitawatangulia, na hakika mimi nakuusieni kukifanyia kheri kizazi changu, kwa mafikio yenu yatakuwa ni katika hodhi. Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu ipo mikononi Mwake, msimamisheSwala na mtoeZaka au la sivyo nimtume kwenu mtu anayetokana na mimi - au ambaye ni nafsi yangu - yeye atazipiga shingo za wale anaopigana nao na atazichukua mateka familia zao.'"Anasema: "Watu wakafikiri mtu huyo atakuwa Abu Bakr au Umar, mara akashika mkono wa Ali (as) na kusema:'Ni huyu."'

— Amesema: Hadithi hii ni yenye sanadi sahihi.

Nasema: Na al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzul-Ummal* Juz. 6, uk. 405, na pia Ibn Hajar ameitaja katika *Sawa'iqu* yake uk. 75, wote wamenukuu kutoka kwa Ibn Abi Shaybah. Na al-Haythamiy ameitaja katika*Majmau*yake Juz. 9 Uk. 134, na amesema:"Ameipokea Abu Ya'ala, na ameitaja pia katika uk. 164, na amesema: "Ameipokea Bazar."

**Al-Kashaf cha Zamakhshariy, katika tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: 'Enyi mlioamini! Akikujieni mpotovu na khabari yoyote, ichunguzeni.' Iliyopo katika Sura Hujurat:**

Amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimpeleka Walid bin Uqbah, ambaye ni ndugu wa Uthman kwa upande wa mama - mpaka aliposema: alimpeleka kwa Bani Mustaliq kama muhakiki, na kulikuwa na chuki binafsi kati yake (Walid) na wao (Bani Mustaliq), hivyo alipoanza kuziona nyumba zao walipanda wanyama wao na kuanza kwenda kumpokea kwa shangwe, lakini yeye alidhani hao ni wapiganaji wao wanakuja kumshambulia, hivyo akarejea kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kumwambia kuwa: 'Wameritadi na wamezuia kutoa Zaka.' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akakasirika na akaazimia kuwapiga, habari zilipowafikia (wale Bani Mustaliq) wakamfuata na kusema:'Tunajilinda kwa Allah kutokana na hasira Yake na hasira ya Mtume Wake.' Mtume akawatuhumu na kuwaambia: 'Lazima muache

(tabia hiyo) laa sivyo nitamtuma kwenu mtu ambaye kwangu mimi ni kama nafsi yangu, atawapiga wapiganaji wenu na atawateka dhuria wenu.' Kisha, akapiga mkono wake kwenye bega la Ali (as)."

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 19:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ubayya, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Lazima Bani Wali'awaache laa sivyo nitampeleka kwao mtu ambaye ni kama nafsi yangu, naye atatekeleza kwao amri yangu, atawauwa wapiganaji wao na atawateka dhuriya wao.'Mara Umari akaweka kitanga chake nyuma ya shingo yangu na kuniambia: 'Anamkusudia nani?' Nikasema: 'Anakukusudia wewe na rafiki yako (Abu Bakr).'Akasema: 'Anamkusudia nani?' Nikasema: 'Mshona viatu.' Na wakati huo Ali (as) alikuwa akishona kiatu."

**Nasema:** Ni kana kwamba mara ya kwanza Ubayya alimdhihaki Umari, akamwambia:'Anakukusudia wewe na rafiki yako (Abu Bakr).' Umari akahisi hilo kuwa kamfanyia dhihaka hivyo akamuuliza mara ya pili, naye akambainishia kwa uhakika kuwa anamkusudia Ali (as). al-Muhibu Tabari ametaja hadithi kama hii katika kitabu chake *ar-Riyadh an-Nadhrah*, katika Juz. 2, uk. 164, na amesema humo: "Kutoka kwa Zayd bin Nafii." Na amesema: "Ameiandika Ahmad katika *al-Manaqib*."

**Majmauz-Zawa'id ya al-Haythamiy Juz. 7, uk. 110:**

Amesema: Kutoka kwa Jabir bin Abdullah, amesema:"Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimpeleka Walid bin Uqbah, kwa Bani Wali'a -haditi ikaendelea mpaka aliposema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: 'Lazima Bani Wali'a waache, laa sivyo nitampeleka kwao mtu ambaye ni kama nafsi yangu, naye atawauwa wapiganaji wao na atawateka dhuriya wao, naye ni huyu.'Kisha akapiga mkono wake kwenye bega la Ali bin Abu Talib (as)." – Amesema: Ameipokea Tabaraniy katika *al-Awsat*.

**Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 400:**

Amesema: Kutoka kwa Amru bin Aas amesema: Wakati nilipofika kutoka kwenye vita vya Dhatus-Salasil, nilikuwa nadhani kwamba, hakuna yeyote anayependwa zaidi na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuliko mimi. Nikasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ni nani unayempenda zaidi kuliko watu wote? - Katika *Kanzul-Ummal* ametaja watu kadhaa mpaka Amru bin Aswi aliposema: Nikasema:'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Yupo wapi Ali?' Akawageukia Maswahaba zake na kusema:'Hakika huyu ananiuliza kuhusu nafsi yangu.'" – Amesema: Ameiandika Ibn Najari.

**Al-Istiab cha Ibn Abdul-Bari Juz. 2, uk. 464:**

Amesema: Maamar amepokea kutoka kwa Ibn Tawus, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Abdullah bin Hantab, amesema:"Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliuambia ujumbe wa Thaqif ulipofika kwake: 'Ni lazima msilimu au la sivyo nitamtuma kwenu mtu atokanaye na mimi – au ambaye ni sawa na nafsi yangu – naye atazipiga shingo zenu, atawateka dhuria wenu na atachukua mali zenu.' Umar akasema: 'Wallahi hakuna siku nilitamani uongozi isipokuwa siku hiyo, na nikawa najisemesha moyoni kuwa naomba mtu huyo awe ni mimi. Lakini alimgeukia Ali (as) akamshika mkono na kusema: Naye ni huyu.'"

**Nasema:** al-Muhibu Tabari ameitaja katika *ar-Riyadh an-Nadhrah*, katika Juz. 2, uk. 164, na amesema humo: "Mtu atokanaye na mimi, au alisema: Mtu ambaye ni sawa na nafsi yangu." Na akasema mwishoni: "Naye ni huyu, naye ni huyu." Mara mbili, kisha akasema: "Ameiandika Abdur-Razaq katika *Jamiu* yake, na pia Abu Amru na Ibn Siman."Kisha hapa kuna riwaya nyingine zinafaa kutajwa mwishoni mwa mlango huu, ya kwanza ni ile aliyoipokea al-Hakim katika*Mustadrak* yake:

**Mustadrakus-Sahihayn Juz. 3, uk. 126:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Abbas kwamba Mtukufu Mtume (saww) alisema katika hotuba yake aliyoitoa katika Hija yake ya kuaga: "Lazima nitawauwa mashujaa vitani." Jibril (as) akamwambia: "Au Ali (ndiye atakayewauwa)?" Akasema: "Ndiyo au Ali bin Abu Talib (as)."

Ya pili ni ile aliyoitaja al-Muhibu Tabari katika *ar-Riyadh an-Nadhrah*:

**ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, uk. 164:**

Amesema: Kutoka kwa Anas bin Malik amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Hakuna Nabii isipokuwa ana mfano wake katika ummah wake, na Ali ndiye mfano wangu."'Amesema: Ameiandika al-Qal'iy.

Ya tatu ni ile aliyoitaja al-Munawi katika *Faydhul-Qadir*, na al-Mutaqiy katika *Kanzul- Ummal*:

**Faydhul-Qadir Juz. 4 Uk. 356 katika matini, na Kanzul- Ummal Juz. 6, uk. 153:**

Na tamko lao ni: "Ali ni asili yangu na Ja'far ni tawi langu."

Wamesema: Ameipokea Tabaraniy na Dhiyau kutoka kwa Abdullah bin Ja'far.

## MLANGO UNAOZUNGUMZIA KAULI YA MTUKUFU MTUME (SAWW) ALIYOSEMA SIKU YA GHADIR KHUM KUHUSU ALI (AS): YEYOTE AMBAYE MIMI NI MTAWALA WAKE ALI (AS) NDIYE MTAWALA WAKE

**Sahih Tirmidhiy Juz. 2, uk. 298:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Shaabah, kutoka kwa Salamah bin Kuhaylu, amesema: Nilimsikia Abu Tufaylu akisimulia kutoka kwa Abu Sariha –au Zayd bin Arqam- kutoka kwa Mtukufu Mtume (saww) kuwa alisema: "Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake." – Amesema: Shaabah amepokea hadithi hii kutoka kwa Maymuna Abu Abdullah, kutoka kwa Zayd bin Arqam, kutoka kwa Mtukufu Mtume (saww).

**Nasema:** Pia Ali bin Sultan ameitaja katika *Mirqat* yake Juz. 5, uk. 568, katika ufafanuzi, kwa kunukuu kutoka katika *al-Jamiu*, kwamba Tirmidhiy na an-Nasaiy na Dhiyau wamepokea kutoka kwa Zayd bin Arqam kwamba Mtukufu Mtume (saww) alisema: "Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake."

**Sahih Ibn Majah Uk. 12, katika mlango wa fadhila za Maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa al-Barau bin Azib kuwa alisema: "Tulikuja pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika Hijja yake aliyohiji. Aliteremka njiani, akaamuru Swala iswaliwe, kisha akashika mkono wa Ali (as) na kusema: 'Je mimi si nina mamlaka zaidi kwa waumini kuliko waliyonayo juu ya nafsi zao?' Wakasema: 'Ndiyo.' Akasema: 'Je mimi si nina mamlaka zaidi kwa kila muumini kuliko aliyonayo juu

ya nafsi yake?' Wakasema: 'Ndiyo.' Akasema: 'Basi huyu ni mtawala wa kila ambaye mimi ni mtawala wake. Ewe Mungu Wangu, mpende ampendaye na mfanyiye uadui kila mwenye kumfanyia uadui.'"

**Nasema:** Pia Ahmad bin Hanbal ameipokea katika *Musnad* yake Juz. 4, uk. 281 kwa tamko hili: al-Barua amesema: "Tulikuwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika safari, ikanadiwa Swala ya jamaa na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akatengenezewa kivuli chini ya miti miwili, akaswali Dhuhri, kisha akaushika mkono wa Ali (as) na kusema: 'Si mnajua kuwa hakika mimi nina mamlaka kwa waumini kuliko waliyonayo juu ya nafsi zao?' Wakasema: 'Ndiyo.' Akasema: 'Si mnajua kuwa hakika mimi nina mamlaka zaidi kwa kila muumini kuliko aliyonayo juu ya nafsi yake?' Wakasema: 'Ndiyo.' Akasema: 'Basi yeyote ambaye mimi ni mtawala wake, Ali ndiye mtawala wake. Ewe Mungu Wangu, mpende ampendaye na mfanyiye uadui kila mwenye kumfanyia uadui.' Baada ya hapo akakutana na Umar, naye akamwambia: 'Hongera ewe mtoto wa Abu Talib sasa umekuwa mtawala wa kila muumini mwanaume na kila muumini mwanamke.'"

Kisha akasema Abu Abdur-Rahman –ambaye ni mtoto wa Ahmad bin Hanbal: "Alitusimulia Hadbah bin Khalid – akataja sanadi mpaka aliposema: Kutoka kwa al-Barau bin Azib kutoka kwa Mtukufu Mtume (saww) mfano wa hiyo."Na pia al-Mutaqiy ametaja hadithi kama ya Ahmad bin Hanbal katika *Kanzul-Ummal* Juz. 6, uk. 397, na amesema: "Ameiandika Ibn Abu Shaybah." Na al-Muhibu Tabari ametaja hadithi kama ya Ahmad bin Hanbal katika *ar-Riyadh an-Nadhrah* Juz. 2, uk. 169, na amesema: "Ameaindika Ibn Saman." Na ameiandika tena hadithi kama ya Ahmad bin Hanbal katika *Dhakhairu* yake, na akasema: "Ameiandika Ahmad katika *Musnad* yake." Na ameiandika katika *al-Manaqib* katika hadithi itokayo kwa Umar, na baada ya kauli: "mfanyie uadui yule mwenye kumfanyia uadui na mnusuru yule mwenye kumnusuru" ameongeza kauli yake: "Na mpende yule mwenye kumpenda." Shaabah amesema: "Au alisema: Na mchukie yule mwenye kumchukia."

**Sahih Ibn Majah Uk. 12, katika mlango wa fadhila za Maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww):**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Sabit –naye ni Abdur-Rahman – kutoka kwa Saad bin Abi Waqas, amesema: "Muawiya aliporudi kutoka katika moja ya safari zake, Saad aliingia kwake na wakamtaja Ali (as), Muawiya akamshutumu Ali, ndipo Saad akakasirika na akasema: 'Unasema haya kwa mtu ambaye nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.' Na nilimsikia akisema: 'Wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu.' Na nilimsikia akisema: 'Nitamkabidhi bendera kesho mtu ambaye Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanampenda.'"

**Nasema:** Na an-Nasaiy ameipokea ndani ya *Khasa'isu* yake uk. 4 kwa tofauti ndogo katika maneno, baada ya kutaja sanadi hadi kwa Abdur-Rahman bin Sabit kutoka kwa Saad, amesema: "Nilikuwa nimeketi na mara wakamshutumu Ali bin Abu Talib (as), nikasema: Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema mambo matatu kuhusu Ali (as), mimi kuwa na jambo moja kati ya hayo matatu ni jambo ninalolipenda sana kuliko ngamia mwekundu. Nilimsikia akisema: 'Hakika yeye kwangu mimi ana cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu.' Na nilimsikia akisema: 'Nitamkabidhi bendera kesho, mtu ambaye Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanampenda.' Na nilimsikia akisema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.'"

**Mustadrakus-Sahihayn cha al-Hakim Juz. 3, uk. 109:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Tufaylu kutoka kwa Zayd bin Arqam, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipokuwa anarejea kutoka Hijja ya kuaga, alipofika Ghadir Khum aliteremka

na akaamuru kufagiliwe chini ya miti na kukafagiliwa, akasema: 'Kana kwamba nimeitwa nami nimeitikia, hakika mimi nimewaachieni vizito viwili, kimoja ni kikubwa kushinda kingine, nacho ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na kizazi changu. Angalieni ni jinsi gani mtakavyoishi navyo baada yangu, hakika hivyo viwili havitoachana mpaka vitakaponikuta katika Hodhi.' Kisha akasema: 'Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Mtawala Wangu na mimi ni mtawala wa kila muumini.' Kisha akaunyanyua mkono wa Ali (as) na kusema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake. Ewe Mungu Wangu, mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui yule mwenye kumfanyia uadui.'"

Al-Hakim baada ya kutaja hadithi kwa urefu wake amesema: "Hadithi hii ni sahihi kwa mujibu wa sharti la mashekhe wawili, lakini hawajaiandika kwa urefu wake." Kisha akasema: "Ushahidi wake ni hadithi ya Salamah bin Kuhaylu kutoka kwa Abu Tufaylu, nayo ni sahihi kwa mujibu washarti la mashekhe wawili –akataja sanadi yake mpaka aliposema: Alitusimulia Muhammad bin Salamah bin Kuhaylu, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Abu Tufaylu, kutoka kwa Ibn Wathilah kuwa alimsikia Zayd bin Arqam akisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliteremka eneo lililopo baina ya Makka na Madina kwenye miti mikubwa mitano. Watu wakafagia uchafu uliokuwepo chini ya miti, kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliswali baada ya jua kukengeuka, kisha alisimama na kuwahutubia watu. Akamhimidi Mwenyezi Mungu na kumsifu, akakumbusha na kuwaidhi, akasema kadiri Mwenyezi Mungu alivyomuwezesha kusema, kisha akasema: 'Enyi watu! Hakika mimi ni mwenye kuwaachia ninyi mambo mawili, hamtapotea kama mtayafuata mambo hayo, nayo ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu na watu wa nyumba yangu kizazi changu.' Kisha akasema mara tatu: 'Hivi mnajua kuwa mimi ni mwenye mamlaka kwa waumini kuliko waliyonayo juu ya nafsi zao?' Wakasema: 'Ndiyo.' Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: ''Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake."

**Nasema:** Na pia ameipokea katika Juz. 3, uk. 533 kwa njia nyingine kutoka kwa Zayd bin Arqam, amesema: "Tulitoka pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mpaka tukafika Ghadir Khum. Akaamrisha pafagiliwe chini ya mti na pakafagiliwa. Ilikuwa ni siku yenye joto kali, hatujawahi kufikiwa na siku yenye joto kali kushinda siku ile. Mtume akaanza kwa kumhimidi na kumshukuru Mwenyezi Mungu, kisha akasema: 'Enyi watu! Hakika hajaletwa Nabii yeyote yule isipokuwa aliishi nusu ya umri alioishi Nabii wa kabla yake, na mimi ninakaribia kuitwa na kuitikia wito. Hakika mimi ni mwenye kuwaachieni vitu ambavyo ikiwa mtashikamana navyo hamtopotea baada yangu, navyo ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu.'Kisha akasimama na akashika mkono wa Ali (as), akasema: 'Enyi watu ni nani mwenye mamlaka zaidi kwenu kuliko hata mliyonayo juu ya nafsi zenu wenyewe?' Wakajibu: 'Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanajua zaidi.' Akasema: 'Yeyote ambayemimi ni mtawala wake basi Ali (as) ndiyemtawala wake.'" - Amesema: Hii ni hadithi yenye sanadi sahihi.

**Nasema:** Na al-Mutaqiykatika *Kanzul-Ummal*, katika Juz. 1, uk. 48 ametaja hadithi kama hadithi iliyotangulia iliyotajwa naal-Hakim ndani ya*Mustadrakus-Sahihayn*Juz. 3, uk. 109, na akasema: "Na Tabaraniy anayo ndani ya*al-Kabir* kutoka kwa Abu Tufaylu kutoka kwa Zayd bin Arqam."

**Mustadrakus-Sahihayn cha al-Hakim Juz. 3, uk. 116:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Khaythamah bin Abdur-Rahman, amesema: "Saad bin Maliki alipoambiwa na mtu: 'Hakika Ali (as) anakuona wewe ni mtu uliyemkhalifu.' Nilimsikia akisema: 'Naapa kwa Mwenyezi Mungu hakika hiyo ni rai yangu niliyoiona na rai yangu ilikuwa ya makosa. Hakika Ali bin Abu Talib (as) amepewa mambo matatu, mimi kupewa jambo moja kati ya hayo matatu ni jambo nilipendalo zaidi kushinda hata dunia na vyote vilivyomo. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimwambia

siku ya Ghadir Khum, baada ya kumhimidi na kumshukuru Mwenyezi Mungu alisema: 'Je mnatambua kuwa mimi nina mamlaka kwa waumini kushinda hata waliyonayo juu ya nafsi zao?' Tukasema: 'Ndiyo.' Akasema: 'Ewe Mungu Wangu, yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui.'Na akaletwa siku ya Khaibar akiwa mgonjwa wa macho, haoni, akamwambia Mtume (saww): 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mimi naumwa macho.' Akamtemea mate katika macho yake na akamwombea du'a wala hakuumwa na macho tena mpaka anauwawa, akapigana na kumletea ushindi wa Khaybari. Na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamtoa ami yake Abbas na wengine kutoka msikitini, Abbas akamwambia: 'Unatutoa hali sisi ni katika kundi lako na ami zako, na unamwacha Ali aendelee kuishi humo.' Akasema: 'Simimi niliyekutoeni na kumwacha yeye (Ali) aendelee kuishi humo, ni Mwenyezi Mungundiye aliyekutoeni ninyi nakumwacha yeye (Ali) aendelee kuishi humo.'"

**Mustadrakus-Sahihayn cha al-Hakim Juz. 3, uk. 371:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Rifaah bin Iyas Dhabiy kutoka kwa baba yake, kutoka kwa babu yake, amesema: "Tulikuwa pamoja na Ali (as) siku ya Jamali, akamtumia ujumbe Talha bin Abdullah kuwa tukutane, Talha alipokuja Ali (as) alimwambia: 'Nakuapiza kwa Mwenyezi Mungu, je hukumsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema: Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi huyu Ali ni mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui?' Akasema: 'Ndiyo nilimsikia.' Akasema: 'Kwa nini basi unanipiga vita?' Akasema: 'Sikuwa nimekumbuka.' Talha akaondoka." - Amesema: Na pia al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzul–Ummal*, katika Juz. 6, uk. 83 kwa tofauti ndogo, na amesema: "Ameiandika Ibn Asakiri."

**Mustadrakus-Sahihayn cha al-Hakim Juz. 3 Uk. 110:**

Amesema: Na hadithi ya Buraydah al-Aslamiy ni sahihi kwa mujibu wa sharti la mashekhe wawili – kisha akataja sanadi yake mpaka aliposema: Kutoka kwa Ibn Abbas, kutoka kwa Buraydah al-Aslamiy, amesema: "Nilikuwa vitani pamoja na Ali (as) huko Yemen -mpaka akasema: kisha nikaja kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) nikamtaja Ali kwa kumtoa kasoro. Mara nikaona uso wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ukibadilika, akaniuliza: 'Ewe Buraydah! Je mimi si ni mwenye mamlaka kwa waumini kuliko hata waliyonayo juu ya nafsi zao?' Nikasema: 'Ndiyo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Akasema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.'- Amesema: Akaitaja hadithi.

**Nasema:** Na pia ameipokea Ahmad bin Hanbal katika Juz. 5, uk.347, na pia al-Mutaqiy ameitaja kwa ufupi katika *Kanzul–Ummal*katika Juz. 6, uk. 154, na amesema: "Ameiandika Ahmad bin Hanbal, Ibn Haban, Samawayhi, al-Hakim, na Said bin Mansur kutoka kwa Ibn Abbas, kutoka kwa Buraydah." Pia al-Mutaqiy ameitaja mara ya pili katika *Kanzul–Ummal* Juz. 6, uk. 397, na pia ameipokea an-Nasaiy kwa njia mbili katika *Khasa'isu* yake uk. 22, kutoka kwa Ibn Abbas kutoka kwa Buraydah. Na Ibn Hajar ameitaja katika *Sawa'iq* yake uk. 26, na amesema kabla yake: "Dhahbiy amesema ni hadithi sahihi." Pia Ali bin Sultan ameitaja katika *Mirqat*yake, katika Juz.5, uk.568, na amesema: "Dhahbiy ameipokea kutoka kwa Buraydah na amesema ni hadithi sahihi."

**Mustadrakus-Sahihayn cha al-Hakim Juz. 2 Uk. 129:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Awanah, kutoka kwa Aamash kutoka kwa Saad bin Ubaydah, kutoka kwa Abdullah bin Buraydah al-Aslamiy, amesema: "Wakati nilipokuwa tunatembea pamoja na baba yangu, mara tukapita mbele ya watu ambao walikuwa wanamshutumu Ali (as) na

wakisema mambo mabaya kuhusu yeye, baba akasema: ‘Hakika mimi nilikuwa nikimshutumu Ali (as) na nilikuwa nina chuki binafsi dhidi yake. Na nilikuwa kwenye jeshi pamoja na Khalid bin Walid, walipopata ngawira Ali (as) alijichukulia suria kutoka kwenye khumsi. Na kulikuwa na chuki kati ya Ali (as) na Khalid, ndipo Khalid akasema: ‘Hii ni fursa yako.’ Kwani Khalid alikuwaanatambua chuki binafsiiliyokuwemo katika nafasi yangu dhidi ya Ali (as), hivyo akaniambia: ‘Nenda kwa Nabii (saww) ukamueleze hayo.’

Nilikwenda kwa Mtumewa Mwenyezi Mungu (saww) na nikamuhadithia, nilikuwa ni mtu mwenye kuinamisha kichwa pindi ninapo hadithia jambo, hivyo nilinyanyua kichwa changu na nikamhadithia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mambo ya kikosini, kisha nikamtajia jambo la Ali (as). Niliponyanyua kichwa tena nilikuta mishipa ya uso waMtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ikiwa myekundu kwa ghadhabu. Mtume (saww) akasema: ‘Yeyote ambaye mimi ni Walii wake basi hakika Ali ni Walii wake.’Kuanzia hapo ikaondoka chuki binafsi niliyokuwa nayo dhidi yake.”

Al-Hakim amesema: “Hadithi hii ni sahihi kwa masharti ya masheikh wawili lakini hawajaiandika kwa mtiririko huu.“ Kisha akasema:“Katika mlango huu hakuna hadithi iliyo sahihi kushinda hadithi hii iliyopokewa kutoka Abu Awanah, kutoka kwa Aamash kutoka kwa Saad bin Ubaydah.”Kisha akapokea kwa njia nyingine hadithi hii tuliyoitaja kutoka kwa Aamash kutoka kwa Saad bin Ubaydah, kutoka kwa mtoto wa Buraydah.

**Nasema:** Na pia ameipokea kwa ufupi Abu Na’im katika *Hilyatul-Awliyai*Juz. 4, uk. 23 kutoka kwa Buraydah, na tamko lake ni: “Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake.”Na pia al-Mutaqiy ameitaja kwa ufupi katika *Kanzul–Ummal*Juz. 6, uk. 152, na tamko lake ni: “Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake.” Na amesema: “Ameiandika Ahmad na an-Nasaiy kutoka kwa al-Barau, na pia Ahmad kaiandika kutoka kwa Buraydah, na pia Tirmidhiy, an-Nasaiy na Dhiyau wameiandika kutoka kwa Zayd bin Arqam.

Na pia Ahmad bin Hanbal ameiandika kwa muhtasari katika *Musnad* yake Juz. 5, uk. 358 na katika uk. 361 kutoka kwa Buraydah. Pia al-Muhibu Tabari ameitaja kwa ufupi kutoka kwa Buraydah katika *ar-Riyadh an-Nadhrah* Juz. 2, Uk. 172, na amesema: “Ameiandika Abu Hatim.” Na pia al-Munawi ameitaja kwa ufupi katika *Faydhul-Qadir* katika matini, katika Juz.. 6, Uk.218, na amesema:“Ameiandika Ahmad na an-Nasaiy na al-Hakim kutoka kwa Buraydah.” Na amesema katika ufafanuzi: “al-Haythamiy amesema katika sehemu moja:“Wapokezi wake ni watu waaminifu.” Na katika sehemu nyingine: “Wapokezi wake ni wapokezi wa hadithi sahihi.”

**Ad-Durul-Manthur ya As-As-Suyutiy: Mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: ‘Nabii ni mwenye mamlaka zaidi kwa Waumini kuliko nafsi zao.’ Iliyopo katika Sura Ahzab:**

Amesema: Ibn Abi Shaybah, Ahmad na an-Nasaiy wameandika kutoka kwa Buraydah kuwa alisema:, “Tulikuwa vitani pamoja na Ali (as) huko Yemen, mara nikaona kwake jambo lisilopendeza. Nilipofika kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) nikamtaja Ali (as) na kumshutumu. Mara nikauona uso wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) umebadilika, akasema: ‘Ewe Buraydah, je mimi si ni mwenyemamlaka zaidi kwa waumini kuliko hata waliyonayo juu ya nafsi zao?’ Nikasema ndiyo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, akasema: ‘Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake.”

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 4, Uk. 372:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Maimuna Abu Abdullah, amesema: “Zayd bin Arqam alisema huku nami nikiwa nasikia: ‘Tuliteremka pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika bonde ambalo

huitwa bonde la Khum, akaamrisha kuswali na akaswali huku kukiwa na joto kali. Akaanza kutuhutubia, lakini kutokana na jua kuwa kali sana ilibidiMtume wa Mwenyezi Mungu (saww) atengenezewekivuli kwa kutandaza nguo juu ya mti, akasema: 'Si mnajua au si mnashahidia kuwa hakika mimi ni mwenye mamlaka zaidi kwa kila muumini kushinda hata aliyonayo juu ya nafsi yake mwenyewe?'Wakasema: 'Ndiyo.' Akasema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mfanyie uadui yule mwenye kumfanyia uadui na mpende yule mwenye kumpenda.'"

**Nasema:** Na ameipokea katika Juz. 4, uk. 372 kwa matamshi mengine kutoka kwa MaimunaAbu Abdullah, amesema: "Nilikuwa kwa Zayd bin Arqam, akaja mtu kutoka hema la mbali na kumuuliza (Zayd), naye akamjibu: 'Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: Je mimi si ni mwenye mamlaka zaidi kwa kila muumini kushinda hata waliyonayo juu ya nafsi zao wenyewe? Wakasema: Ndiyo. Akasema: Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake.'" Maimuna anasema: "Wamenihadithia baadhi ya watu kutoka kwa Zayd kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Ewe Mungu wangu mpende yule mwenye kumpenda na mfanyie uadui yule mwenye kumfanyia uadui.'"

Na pia al-Haythamiy ameitaja katika *Majmau* yake, katika Juz. 9, uk. 104, na amesema: "Kutoka kwa Amru Dhiy Muri na Zayd bin Arqam, wamesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alituhutubia siku ya Ghadir Khum, akasema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende yule mwenye kumpenda na mfanyie uadui yule mwenye kumfanyia uadui. Mnusuru mwenye kumnusuru na msaidie mwenye kumsaidia.'" Kisha akasema: "Ameiandika Tabaraniy na Ahmad kutoka kwa Zayd peke yake - mpaka aliposema: Na Bazar."Pia al-Mutaqiyameitaja katika *Kanzul–Ummal*, katika Juz. 6, uk. 154, na amesema: "Ameiandika Tabaraniy kutoka kwa Amru Dhiy Muri na Zayd bin Arqam."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 4, Uk. 368:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Atwiyah al-Awfiy, amesema: "Nilimuuliza Zayd bin Arqam kwa kusema: Kungwi wangu amenihadithia kutoka kwako hadithi inayomhusu Ali (as) siku ya Ghadir Khum, mimi ningependa kuisikia kutoka kwako wewe mwenyewe. Akasema: 'Hakika nyinyi watu wa Iraq mnayo mliyonayo.' Nikamwambia: 'Wewe hutapata tatizo kutoka kwangu.' Akasema: 'Ndiyo, Tulikuwa Juhfa, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akatoka mbele yetu mchana huku akiwa kamshika Ali (as) mkono, akasema: Enyi watu!Si mnajua kuwa hakika mimi ni mwenye mamlaka kwa waumini kushinda hata waliyonayo juu ya nafsi zao wenyewe? Wakasema: Ndiyo. Akasema: Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake.' Nikamwambia: Je alisema: Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui yule mwenye kumfanyia uadui? Akasema: 'Hakika mimi nakupa habari kama nilivyosikia.'"

**Nasema:** Pia al-Mutaqiy ameipokea katika *Kanzul-Ummal*, katika Juz. 6, uk. 390, na amesema: "Kutoka kwa Atwiyah al-Awfiy kutoka kwa Zayd bin Arqam, kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliushika mkono wa Ali (as) siku ya Ghadir Khum katika ardhi inayoitwa Juhfa, kisha akasema: 'Enyi watu! Si mnajua kuwa hakika mimi ni mwenye mamlaka kwa waumini kushinda hata waliyonayo juu ya nafsi zao wenyewe?' Wakasema: 'Ndiyo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Akasema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake.' – Amesema: Ameiandika Ibn Jariri.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 1, Uk. 152:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ali (as) kwamba Mtukufu Mtume (saww) alisema siku ya Ghadir Khum: "Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake."

**Nasema:** Na pia al-Haythamiy ameitaja katika *Majmau* yake, katika Juz. 9, uk. 107, na amesema: "Ameipokea Ahmad." Kisha akasema: "Na wapokezi wake ni watu waaminifu."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 1, Uk. 330:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Amru bin Maimuna kuwa alisema: "Wakati nikiwa nimeketi kwa Ibn Abbas mara alijiwa na watu tisa, wakasema: 'Ewe mtoto wa Abbas ima unyanyuke pamoja nasi na ima hawa ulionao watupishe.' Ibn Abbas akasema: 'Bali nanyanyuka pamoja nanyi.' Wakati huo alikuwa bado mzima hajapofuka, walikwenda pembeni na kuanza kuzungumza, na hatujui walizungumza nini. Mara alirudi huku akipukuta nguo yake na kusema: 'Ole wao, ole wao, wanawezaje kumtuhumu mtu mwenye mambo kumi – alisimulia hadithi mpaka aliposema: Na akasema – yaani Mtume wa Mwenyezi Mungu: Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi huyu Ali ndiye mtawala wake.'" Hadithi hii imetangulia kwa ukamilifu wake katika Mlango unaozungumzia Aya ya utakaso, hivyo rejea huko.

**Nasema:** Pia ameipokea an-Nasaiy ndani ya *Khasa'isu* yake uk. 8, na ameitaja al-Muhibu Tabari ndani ya *ar-Riyadh an-Nadhrah*, katika Juz. 2 uk. 203, na katika *Dhakhairu* yake uk. 86, na amesema: "Ameiandika kwa ukamilifu wake Ahmad na al-Hafidh Abul-Qasim ad-Damashqiy ndani ya *al-Muwafaqat* na ndani ya *al-Ar'baunaat-Twawali*." Na amesema pia: "Na an-Nasaiy ameiandika kwa ufupi."Na ameitaja al-Haythamiy ndani ya *Maj'mau* yake Juz. 9, uk. 119, na amesema: "Ameipokea Ahmad na Tabaraniy ndani ya *al-Kabir* na ndani ya *al-Awsat* kwa muhtasari."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 5, Uk. 366:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Said bin Wahab, amesema: "Ali (as) aliwaapiza watu hivyo wakasimama watu watano –au sita – miongoni mwa Maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), wakashahidia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake.'"

**Nasema:** Ameipokea pia an-Nasaiy katika *Khasa'isu* yake uk. 22, na pia al-Haythamiy ameitaja katika *Majmau* yake Juz.9, uk. 104, na amesema: "Ameipokea Ahmad, na wapokezi wake ni wapokezi wa hadithi sahihi."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 1, Uk. 188:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Is'haqa, kutoka kwa Said bin Wahab na kutoka kwa Zayd bin Yathiu, wamesema: "Ali (as) aliwaapiza watu katika eneo la wazi (Rahbah), akasema:'Yeyote ambaye alimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiongea siku ya Ghadir Khum asimame.' Wakasimama watu sita kabla ya Said na watu sita kabla ya Zayd, wote wakashahidia kuwa wao walimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akimwambia Ali (as) siku ya Ghadir Khum: 'Je Mwenyezi Mungusi ana mamlaka zaidi kwa waumini kuliko hata waliyonayo juu ya nafsi zao wenyewe?' Wakasema: 'Ndiyo.' Akasema: 'Ewe MunguWangu, yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi huyu Ali ndiye mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui.'"

**Nasema:** al-Haythamiy ameitaja pia katika *Majmauz-Zawa'id* Juz.9, uk. 107, na amesema humo: "Wakasimama watu sita kabla ya Said na watu saba kabla ya Zayd." Kisha akasema: "Abdullah na Bazar wameipokea kwa ukamilifu zaidi."Na an-Nasaiy ameipokea pia katika *Khasa'isu* yake, katika uk.22 na katika uk. 40. Kisha Ahmad bin Hanbal baada ya kupokea hadithi iliyotajwa kutoka kwa Abu Is'haqa kutoka kwa Said bin Wahab, na kutoka kwa Zayd bin Yathiu, amepokea tena kutoka kwa Abu Is'haqa kutoka kwa

Amir Dhiy Murihadithi kama ya Abu Is'haqa kutoka kwa Said na Zayd, lakini humo ameongeza: "Na mnusuru mwenye kumnusuru na mtelekeze mwenye kumtelekeza." Kisha akapokea hadithi ya tatu kama hiyo kutoka kwa Abu Tufaylu kutoka kwa Zayd bin Arqam kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 1, Uk. 119:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdur-Rahman bin Abi Layla, amesema: "Nilimshuhudia Ali (as) akiwa katika eneo la wazi (Rahbah) akiwaapiza watu: 'Namuapiza kwa Mwenyezi Mungu, mtu yeyote aliyemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema siku ya Ghadir Khum: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi huyu Ali ndiye mtawala wake.' Asimame na kushahidia hilo."Abdur-Rahman anasema: "Wakasimama watu kumi na mbili waliokuwepo siku ya Badri, kana kwamba namuona mmoja wao, wakasema: 'Tunashahidia kuwa hakika sisi tulimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema siku ya Ghadir Khum: Je mimi si nina mamlaka zaidi kwa waumini kuliko hata waliyonayo juu ya nafsi zao wenyewe, na wake zangu ni mama zao? Wakasema: Ndiyo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Akasema: Basi yeyote ambaye mimi ni mtawala wake huyu Ali ndiye mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui.'"

**Nasema:** Na pia Khatib al-Baghadadiy ameipokea katika *Taarikh* yake, katika Juz. 14, uk. 236, na pia al-Haythamiy ameitaja katika *Majmau* yake, na amesema: "Ameipokea Abu Ya'ala na wapokezi wake ni wale walioaminiwa." Kisha akasema: "Na ameipokea Abdullah bin Ahmad." Na al-Mutaqiy ameitaja pia katika *Kanzul-Ummal*, katika Juz. 6, uk. 407, na amesema: "Ameipokea Abu Ya'ala, Ibn Jariri na Said bin Mansur." Na ameipokea Ibn Athir al-Jazriy katika *Usudul–Ghabah*, katika Juz. 4, uk. 27, na pia kaipokea at-Twahawi katika *Mushkilul-Athar*, katika Juz.2, uk. 308.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 1, Uk. 88:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ziyad bin Abi Ziyad, amesema: "Nilimsika Ali bin Abu Talib (as) akiwaapiza watu kwa Mwenyezi Mungu: 'Namuapiza kwa Mwenyezi MunguMwislamu yeyote aliyemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema aliyosema siku ya Ghadir Khum basi asimame.' Wakasimama watu kumi na mbili waliokuwepo siku ya Badri, na wakashahidia.

**Nasema:** al-Muhibu Tabari ameitaja katika *ar-Riyadh an-Nadhrah,* katika Juz. 2, uk. 170, na al-Haythamiy ameitaja katika *Majmau* yake, katika Juz. 9, uk. 106, na amesema: "Ameipokea Ahmad na wapokezi wake ni watu waaminifu."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 1, Uk. 84:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Zadhan bin Umar, amesema: "Nilimsika Ali (as) akiwaapiza watu katika eneo la wazi: 'Yeyote aliyemshuhudia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) siku ya Ghadir Khum akisema aliyosema, asimame.' Wakasimama watu kumi na tatu na wakashahidia kwamba wao walimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake.'

**Nasema:** Na pia al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzuli-Ummal*, katika Juz.6, uk.407, na amesema: "Ameipokea Ahmad bin Hanbal katika *Musnad* yake na Ibn Abi Aswim katika *as-Sunnah*.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 5, Uk. 370:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Zayd bin Arqam, amesema: "Ali (as) aliwataka watu watoe ushahidi, akawaambia: 'Namuapiza kwa Mwenyezi Mungu, yeyote ambaye alimsikia Mtume wa Mwenyezi

Mungu (saww) akisema: Ewe Mungu Wangu, yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake. Ewe MunguWangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui.' Wakasimama watu kumi na sita wakashahidia hilo."

**Nasema:** Pia al-Muhibu Tabari ameitaja katika *ar-Riyadh an-Nadhrah*, katika Juz.2, uk.170, na pia al-Haytahmiy ameitaja katika *Majmau* yake, katika Juz.9, uk. 106, na amesema mwishoni: "Na wakatoa ushahidi juu ya hilo, nami nilkuwa miongoni mwa wale walioficha ushahidi hivyo nikapofuka macho yangu." Kisha akasema:"Ameipokea Tabari katika *al-Kabir* na *al-Awsat*ikiwa bila kupofuka macho, kuficha ushahidi na dua yake Ali (as)."Kisha akasema: "Na katika riwaya nyingine iliyokokwake kuna: 'Ali (as) alikuwa amemuombea dua baya yeyote atakayeficha ushahidi."Kisha akasema: "Na wapokezi wa ndani ya*al-Awsat* ni watu waaminifu."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 4, Uk. 370:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Tufaylu, amesema: "Ali (as) aliwakusanya watu eneo la wazi kisha akawaambia: 'Namuapiza kwa Mwenyezi Mungu, Mwislamu yeyote aliyemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema yale aliyosema siku ya Ghadir Khum basi na asimame.' Wakasimama watu thelathini." Abu Na'im anasema: "Wakasimama watu wengi wakashahidia kwamba wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipomshika mkono Ali (as) aliwaambia watu: 'Je mnajua kuwa hakika mimi nina mamlaka zaidi kwa waumini kuliko hata waliyonayo juu ya nafsi zao?' Wakasema: 'Ndiyo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.'Akasema: "Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui.'"

Anasema: "Nikatoka, na katika nafsi yangu kulikuwa na kitu, nilipokutana na Zayd bin Arqam nikamwambia: Hakika nimemsikia Ali (as) akisema haya na haya. Akasema: 'Kitu gani unachokanusha? Hakika nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema hayo.'"

**Nasema:** Na pia an-Nasaiy ameipokea katika *Khasa'isu* yake, katika uk. 24 kwa njia mbili kutoka kwa Abu Tufaylu na kutoka kwa Amir bin Wathilah. Na al-Muhibu Tabari ameitaja pia katika *ar-Riyadh an-Nadhrah*, katika Juz. 2, uk.169, na amesema humo: "Wakasimama watu na wakatoa ushahidi."Na mwisho akasema:"Abu Na'im amesema: Nikamwambia Fari –yaani mtu ambaye yeye kapokea hadithi hii kutoka kwake: Kulikuwa na muda gani kati ya kauli na kifo chake? Akasema: 'Ni siku mia moja.'"Kisha akasema: "Ameiandika Abu Hatim na amesema: 'Anamaanisha kifo cha Ali bin Abu Talib (as).'"

**Nasema:** Inawezekana makusudio ya: 'Kulikuwa na muda gani kati ya kauli na kifo chake?'Ni: Kulikuwa na muda gani kati ya kauli ya Mtume (saww) siku ya Ghadir Khum: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiyemtawala wake.'Na kifo chake?Ndipo akasema: 'Ni siku mia moja.' Na Mwenyezi Mungu ndiye ajuaye zaidi.

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 5, Uk. 419:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Rabah bin Harith, amesema: "Lilikuja kundi la watu kwa Ali (as) katika eneo la wazi (Rahbah), wakasema: 'Asalam Alayka ewe bwana wetu.' Akawauliza: 'Vipi nitakuwa bwana wenu hali nyinyi ni Waarabu?' Wakajibu: 'Tulimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) siku ya Ghadir Khum akisema: Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake." Rabah anasema: "Walipoondoka nikawafuata na kuwauliza:'Ni akina nani hawa?' Wakasema:'Ni watu katika Ansari.'"

**Nasema:** Na pia baada ya hadithi hii bila kitenganishi ameipokea tena kwa njia nyingine kwa tofauti ndogo. Na pia al-Haythamiy ameitaja katika *Majmau* yake, katika Juz.9, uk.103, na amesema:"Ameipokea Ahmad na Tabaraniy isipokuwa yeye amesema: 'Wakasema: Tulimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake, basi Ali ndiye mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui.' Na ni huyu hapa Abu Ayub baina yetu.' Abu Ayub akaondoa kilemba chake toka usoni kisha akasema: 'Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake, basi Ali ndiye mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui.'" Kisha akasema:"Na wapokezi wa Ahmad ni watu waaminifu."

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal, Juz. 5, Uk. 350:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Buraydah kutoka kwa baba yake, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alitupeleka vitani na akamchangua Ali (as) kuwa kiongozi wetu, wakati tuliporudi akatuuliza: 'Mmeonaje ushirikiano wa rafiki yenu?'" Anasema: "Ima nilimshitakia au ni mwingine ndiye aliyemshitaki, nikanyanyua kichwa changu, kwani nilikuwa ni mtu mwenye kuinamisha kichwa wakati wa kuzungumza. Niliponyanyua nikakuta uso wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ukiwa mwekundu huku akisema: 'Yeyote ambaye mimi ni Walii wake basi Ali ndiye Walii wake.'"

**Nasema:** Pia an-Nasaiy ameipokea katika *Khasa'is* yake katika uk.21, pia al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzul–Ummal* Juz.6, uk.398, na amesema mwishoni mwa hadithi: "Basi kikaondoka kile kinyongo kilichokuwemo katika nafsi yangu dhidi yake. Na nikasema: Sintomtaja tena kwa ubaya." Na al-Haythamiy ameitaja katika *Majmau* yake katika Juz.9, uk.108, na amesema mwishoni mwa hadithi: "Kamwe sintokukosea tena kuhusu yeye." Kisha akasema:"Ameipokea Bazar, na wapokezi wake ni wapokezi wa hadithi sahihi."

**Tafsirul-Kabir cha Fakhru Razi, mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu: 'Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi.' Iliyoko katika Sura al-Maidah:**

Amesema: Kumi –yaani katika sababu za kuteremka Aya hii zilizotajwa na wafasiri: Aya hii imeshuka kueleza fadhila za Ali bin Abu Talib (as), na iliposhuka aya hii alishika mkono wake na kusema: "Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui." Na Umar alipokutana naye alisema: "Hongera ewe mtoto wa Abu Talib sasa umekuwa mtawala wangu na mtawala wa kila muumini mwanaume na muumini mwanamke." Amesema: Nayo – kuwa Aya hii imeshuka kueleza fadhila za Ali bin Abu Talib (as) - ndio kauli ya Ibn Abbas na al-Barau Ibn Azib na Muhammad bin Ali (as).

**Hilyatul-Awliyai cha Abu Na'im, Juz. 5, uk. 26:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Umayrah bin Saad, amesema: "Nilimshuhudia Ali (as) akiwa juu ya mimbari huku akiwaapiza Maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), akiwemo Abu Said, Abu Hurayra na Anas bin Malik, wakiwa pembezoni mwa mimbari. Ali (as) alikuwa juu ya mimbari na pembeni mwa mimbari kulikuwa na watu kumi na mbili, na hawa (niliowataja) wakiwa miongoni mwao, Ali (as) akasema: 'Nakuapizeni kwa Mwenyezi Mungu, je mlimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake? Wote wakasimama na kusema: 'Ewe MunguWetu, ndiyo tulimsikia.' Lakini mtu mmoja hakusimama, Ali (as) akamuuliza: 'Nilipi lililokuzuia kusimama?' Akasema: 'Ewe Amirul-Muuminina, ni utuuzima na kusahau.' Ali akase-

ma: 'Ewe MunguWangu ikiwa ameongopa basi mpe mtihani mzuri.' Hivyo hakufa isipokuwa baada ya kuwa naweupe kwenye macho, weupe ambaohauwezi kufichwa hata kwa kilemba."

**Nasema:** Mtu ambaye aliendelea kukaa na wala hakusimama kutoa ushahidi na akaombewa du'a baya na Imam Ali Amirul-Muuminina (as) ni Anas bin Malik, hiyo nikama lilivyotajwa jina lake wazi wazi katika baadhi ya riwaya. Huenda mwandishi wa*Hilyatul-Awliyai* hakutaka kutaja jina lake, na Allah ndiye mwenye kujua. Na al-Haythamiy ameitaja hadithi hii katika *Majmau* yake katika Juz.9, uk. 108, na amesema:"Ameipokea Tabari katika *al-Awsat* na *as-Saghir*." Na pia al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzul-Ummal* katika Juz.6, uk.403, na amesema:"Ameiandika Tabaraniy katika *al-Awsat."*

**Hilyatul-Awliyai cha Abu Na'im, Juz. 5, uk. 364, mwishoni mwa habari za Umar bin Abdul-Aziz:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwaYazid bin Umar bin Mawraq, amesema: "Nilikuwa Sham (sasa Syria) huku Umar bin Abdul-Aziz akiwapa watu hela, basi nami nikatangulia mbele yake, akaniuliza: 'Ni kutoka familia ya nani wewe?' Nikasema: Mimi ni kutoka kwa Makuraishi. Akasema: 'Ni kutoka kwa Mkuraishi yupi?' Nikasema: Ni kutoka katika ukoo wa Bani Hashim. Niliponyamaza akasema: 'Ni kutoka kwa Hashim yupi? Nikamwambia: Mimi ni mtumishi wa Ali (as). Akasema: 'Ni kutoka kwa Ali!?' Nikanyamaza, akaweka mkono wake kwenye kifua changu na kusema: 'Na mimi, Wallahi ni kipenzi cha Ali binAbu Talib (as), Mwenyezi Mungu autukuze uso wake.' Kisha akasema: 'Walinihadithia watu kadhaa kwamba walimsikia Mtume (saww) akisema: Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.' Kisha akasema: 'Ewe Muzahim unawapa kiasi gani watu kama yeye?' Muzahim akasema: 'Dirhamu mia moja au mia mbili.' Akasema: 'Mpe Dinari Khamsini.'"Ibn Abi Daud amesema: "Dinari sitini kwa sababu ya kumpenda kwake Ali bin Abu Talib (as), kisha akasema: 'Nenda katika mji wako utakuwa unaletewa mfano wa kile wanacholetewa watu mfano wako.'"

**Nasema:** Pia Ibn Athir ameitaja kwa tofauti ndogo katika *Usudul-Ghabah* katika Juz.5, uk. 383.

**Taarikh Baghdad cha al-Khatib al-Baghdadiy Juz. 7, Uk. 377:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Anas, amesema: "Nilimsikia Mtume (saww) akisema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui.'"

**Taarikh Baghdad cha al-Khatib al-Baghdadiy Juz. 8, Uk. 290:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Hurayra, amesema: "Yeyote atakayefunga siku ya kumi na nane ya mwezi wa Dhulhija ataandikiwa funga ya miezi sitini. Nayo ni siku ya Ghadir Khum, wakati Mtume (saww) alipochukua mkono wa Ali bin Abu Talib (as) na akasema: 'Je mimi si ni walii wa waumini?' Wakasema: 'Ndiyo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Akasema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake Ali ndiye mtawala wake.' Umar bin Khattab akasema: 'Hongera, hongera ewe mtoto wa Abu Talibsasa umekuwa mtawala wangu na mtawala wa kila mwislamu.' Ndipo Mwenyezi Mungu akateremsha: **'Leo nimewakamilishieni dini yenu…...'"**

**Nasema:** Na pia amepokea kama hii kwa njia nyingine.

**Taarikh Baghdad cha al-Khatib al-Baghdadiy Juz. 12, Uk. 343:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Fadhlu bin Rabii, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Mansuri, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa babu yake, kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake Ali ndiye mtawala wake.'"

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 21:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Tufaylu kutoka kwa Zayd bin Arqam, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipokuwa anarejea kutoka Hijja ya kuaga, alipofika Ghadir Khum aliteremka na akaamuru kufagiliwe chini ya miti na kukafagiliwa, kisha akasema: 'Kana kwamba nimeitwa nami nimeitikia. Hakika mimi nimewaachieni vizito viwili, kimoja ni kikubwa kushinda kingine, nacho ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na kizazi changu, watu wa Nyumba yangu. Angalieni ni jinsi gani mtakavyoishi navyo baada yangu, hakika hivyo viwili havitoachana mpaka vitakaponikuta katika Hodhi.' Kisha akasema: 'Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Mtawala Wangu na mimi ni mtawala wa kila muumini.' Kisha akaunyanyua mkono wa Ali (as) na kusema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake. Ewe Mungu Wangu, mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui yule mwenye kumfanyia uadui.' Nikamwambia Zayd: Kweli ulisikia hayo kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), akisema: 'Hakika hakukuwa na yeyote katika miti isipokuwa alimuona kwa macho yake na kusikia kwa masikio yake.'"

**Nasema:** Na al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzul–Ummal* katika Juz.16, uk.390, na amesema: "Ameiandika Ibn Jarir."Kisha akasema: "Kuna hadithi kama hiyo kutoka kwa Atwiyah al-Awfiy kutoka kwa Abu Said Khudriy nayo pia kaiandikaIbn Jarir."

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 22:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Saad, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake.'"

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 25:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Saad, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliushika mkono wa Ali (as), akaanza kuhutubu kwa kumhimidi na kumshukuru Mwenyezi Mungu kisha akasema: 'Hivi mnajua kwamba mimi nina mamlaka zaidi kwenu kuliko hata mliyonayo juu ya nafsi zenu?' Wakasema: 'Ndiyo, umesema kweli ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Kisha akaushika mkono wa Ali (as) na akaunyanyua juu, akasema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake. Ewe Mungu Wangu, mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui yule mwenye kumfanyia uadui.'"

**Nasema:** Na al-Haythamiy ameitaja pia kwa ufupi katika *Majmau* yake, katika Juz.9, uk.107, na amesema:"Ameipokea Bazar na wapokezi wake ni watu waaminifu."

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 25:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Saad, amesema: "Tulikuwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika njia ya Makka, naye alikuwa akielekea Makka. Alipofika Ghadir Kum watu walisimama, kisha akawarejesha waliokuwa wametangulia na akawangojea waliokuwa nyuma. Watu walipomkusanyikia, alisema: 'Enyi watu! Ni nani mtawala wenu? Wakasema mara tatu: 'Ni Allah na Mtume Wake.' Kisha akashika mkono wa Ali (as) akaunyanyua juu kisha akasema: "Yeyote ambaye Mwenyezi Mungu na Mtume Wake ni watawala wake basi huyu ndiye mtawala wake. Ewe Mungu Wangu, mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui yule mwenye kumfanyia uadui.'"

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 22:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Umayrah bin Saad kwamba yeye alimsikia Ali (as) akiwaapiza watu katika eneo la wazi kwamba yeyote aliyemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema:

"Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake, basi Ali ndiye mtawala wake," asimame. Wakasimama watu sita wakashahidia hilo.

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 23:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Sharik kutoka kwa Abi Is'haqa kutoka kwa Zayd bin Yathiu, amesema: "Nilimsikia Ali bin Abu Talib (as) akiwajuu ya mimbari yaKufahakisema: 'Hakika mimi namuapiza kwa Mwenyezi Mungu mtu yeyote –na wala asishahidie isipokuwa Sahaba wa Muhammad - ambaye alimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) siku ya Ghadir Khum akisema: Yeyote ambaye Mwenyezi Mungu na Mtume wake ni watawala wake basi Ali ndiye mtawala wake. Ewe Mungu Wangu, mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui yule mwenye kumfanyia uadui.'Wakasimama watu sita pembezoni mwa mimbari nyingine wakatoa ushahidi kwamba hakika wao walimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema hayo." Sharik anasema:"Nikamwambia Abu Is'haqa: Je umewahi kumsikia al-Barau bin Azib akisimulia haya kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)? Akasema: 'Ndiyo.'"

**Khasa'isun-Nasaiy Uk. 26:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Amru Dhiy Muri, amesema: "Nilimshuhudia Ali (as) akiwaapiza Maswahaba wa Mtume Muhammad (saww) katika eneo la wazi: 'Ni nani kati yenu alimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema aliyosema siku ya Ghadir Khum?' Wakasimama watu na kushahidia kwamba wao walimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Yeyote ambaye Mwenyezi Mungu na Mtume Wake ni watawala wake basi huyu Ali ndiye mtawala wake. Ewe Mungu Wangu, mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui yule mwenye kumfanyia uadui. Mpende mwenye kumpenda na mchukie mwenye kumchukia, na mnusuru mwenye kumnusuru."

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2 Uk. 169:**

Amesema: Kutoka kwake - yaani kutoka kwa Riyahi - amesema: "Wakati Ali (as) akiwa ameketi, mara alikuja mtu mwenye athari za safari. Mtu huyo akasema: 'Asalam Alayka ewe bwana wangu.' Ali akasema: 'Ni nani huyu?' Akasema: 'Ni Abu Ayub al-Answariy.' Ali (as) akasema: "Mwachieni njia.' Wakamwachia njia, Abu Ayub akasema: 'Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake, basi Ali ndiyemtawala wake.'"- Amesema: Ameiandika Baghawi katika *Muujamu* yake.

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, uk. 169:**

Amesema: Ibn Saman ameandika kutoka kwa Umar: "Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake, basi Ali ndiye mtawala wake. Na amesema katika uk. 70: Na kutoka kwa Umar, hakika yeye alisema: "Ali ni mtawala wa kila ambaye Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ni mtawala wake." Kisha akasema: kutoka kwa Salim: "Umar aliambiwa: 'Hakika wewe unamfanyia Ali (as) jambo ambalo humfanyii yeyote miongoni mwa Maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).' Akasema: 'Hakika yeye ni mtawala wangu.'"

**Nasema:** Hadithi hii ya mwisho ameitaja pia Ibn Hajar katika Sawa'iqu yake Uk. 26, na amesema: "Ameiandika ad-Daru Qutniy.

**As-Sawa'iqul-Muhriqah cha Ibn Hajar Uk. 102:**

Amesema: Imepokewa kwa Tabari na mwingine kwa sanadi sahihi kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alihutubia huko Ghadir Khum chini ya miti akasema: "Enyi watu! Hakika Mpole Mjuzi amenipa

habari kwamba hakuna Nabii yeyote isipokuwa aliishi nusu ya umri wa Nabii wa kabla yake, na mimi ninakaribia kuitwa na kuitikia wito, hakika mimi ni mwenye kuulizwa na ninyi ni wenye kuulizwa, basi mtasema nini?" Wakasema: "Tunashahidia kwamba umefikisha, umepigana jihadi na umetoa nasaha, tunamuomba Mwenyezi Mungu akulipe kheri."Akasema: "Si mnashahidia kwamba hapana Mugu isipokuwa Allah na kwamba Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake, na kwamba pepo Yake ni haki, na kwamba moto Wake ni haki, na kwamba mauti ni haki, na kwamba ufufuo baada ya mauti ni haki, na kwamba bila shaka Kiyama kitakuja, na kwamba Mwenyezi Mungu atawafufua walio makaburini?"Wakasema: "Ndiyo tunashahidia hayo." Akasema: "Ewe Mungu wangu kuwa shahidi."

Kisha akasema: "Enyi watu hakika Mwenyezi Mungu ni mtawala wangu na mimi ni mtawala wa waumini, na mimi nina mamlaka zaidi kwa waumini kuliko hata yale waliyonayo juu ya nafsi zao, hivyo yeyote ambaye Mwenyezi Mungu na Mtume Wake ni watawala wake basi huyu ni mtawala wake. Ewe Mungu wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui."

Kisha akasema: "Enyi watu! Hakika mimi nitawatangulieni, na hakika nyinyi mtakuja kwangu katika Hodhi, Hodhi ambayo ni pana usawa na umbali uliyopo baina ya Basra na Sanaa, ndani yake mna vikombe vya fedha sawa na idadi ya nyota, na mimi nitakuulizeni kuhusu vizito viwili pindi mtakapokuja kwangu, hivyo basi angalieni jinsi mtakavyoishi navyo baada yangu. Kizito kikubwa ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu, nayo ni kamba ambayo ncha yake mojaipo mikononi mwa Mwenyezi Mungu na ncha nyingine imo mikononi mwenu, basi shikamaneni nacho hamtopotea wala kubadilishwa. Na kingine ni kizazi changu, watu wa Nyumba yangu, hakika Mpole Mjuzi amenipa habari kwamba hivyo viwili havitotoweka mpaka vitakaponifikia katika Hodhi."

**Kanzul-Ummal Juz. 1, uk. 48:**

Na tamko lake ni: "Hakika mimi sijamkuta Nabii isipokuwa alipewa nusu ya umri wa Nabii aliyekuwa kabla yake. Na mimi ni karibu nitaitwa na kuitikia wito, basi mtasema nini?" Wakasema: "Umekwishatoa nasaha." Akasema: "Si mnashahidia kwamba hapana Mungu isipokuwa Allah na kwamba Muhammad ni mja wake na Mtume Wake, na kwamba pepo ni haki, na kwamba moto ni haki, na kwamba ufufuo baada ya mauti ni haki?" Wakasema: "Ndiyo tunashahidia hayo." Akasema: "Na mimi nashahidia pamoja nanyi, je mnasikia? Hakika mimi nitawatangulieni kwenye Hodhi, na nyinyi mtanikuta kwenye Hodhi, nayo upana wake ni sawa na umbali uliyopo baina ya Basra na Sanaa. Ndani yake mna vikombe vya fedha sawa na idadi ya nyota, hivyo angalieni jinsi mtakavyoishi na hivyo vizito viwili baada yangu."

Wakauliza:"Ni vipi hivyo vizito viwili ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?" Akasema: "Ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu, ncha yake moja imo mikononi mwa Mwenyezi Mungu na ncha yake nyingine imo mikononi mwenu, shikamaneni navyo wala hamtopotea. Na (kizito) kingine ni kizazi changu, hakika Mpole Mjuzi amenipa habari kwamba viwili hivi havitaachana mpaka vitakaponikuta kwenye Hodhi. Nimeviombea hilo (kutoachana) kwa Mola Wangu, hivyo basi msivitangulie mtaangamia, na wala msijitenge navyo mtaangamia, na wala msiwafundishe (Ahlul-Bayt) kwani wao ni wajuzi zaidi kuliko nyinyi. Yeyote ambaye mimi nina mamlaka zaidi kwake kuliko hata aliyonayo juu ya nafsi yake, basi afahamu Ali ndiyemtawala wake. Ewe MunguWangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui." – Amesema: Ameipokea Tabari katika *al-Kabir* kutoka kwa Abu Tufaylu kutoka kwa Zayd bin Arqam.

**Nasema:** Na pia al-Haythamiy ameitaja kwa tofauti ndogo katika *Majmau* yake, katika Juz. 9, uk. 163. Amesema: "Na kutoka kwa Zayd bin Arqam amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliteremka Juhfa kisha akawageukia watu. Akamhimidi na kumshukuru Mwenyezi Mungu, kisha akasema: 'Hakika mimi sijamkuta Nabii….." mpaka mwisho. Amesema: "Na katika riwaya fupi zaidi kuliko hii kuna: 'Ndani yake kuna vikombe vya dhahabu na fedha sawa na idadi ya nyota.' – mpaka aliposema: Na

katika riwaya nyingine: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliporejea kutoka katika Hijja ya kuaga aliteremka Ghadir Khum, akaamrisha kufagiliwe chini ya miti na kukafagiliwa, kisha akasimama na kusema: 'Kama kwamba nimeitwa na nimeitikia….'-Akasema mwishoni: 'Nikamuuliza Zayd: Je ulisikia hilo kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: Hakuna mtu yeyote aliyekuwepo kwenye miti isipokuwa alimuona kwa jicho lake na kumsikia kwa masikio yake.'"

**Kanzul–Ummal Juz. 1, Uk. 48:**

Na tamko lake ni: "Enyi watu! Hakika Mpole Mjuzi amenipa habari kwamba hatapewa umri Nabii yeyote isipokuwa nusu ya umri wa Nabii aliyekuwa kabla yake. Na mimi ni karibu nitaitwa na kuitikia wito, na hakika mimi ni mwenye kuulizwa na ninyi ni wenye kuulizwa, hivyo basi mtasema nini?"Wakasema: "Tunashahidia kwamba umefikisha, umepigana jihadi na umetoa nasaha." Akasema: "Si mnashahidia kwamba hapana Mungu isipokuwa Allah na kwamba Muhammad ni mja wake na Mtume Wake, na kwamba pepo yake ni haki, na kwamba moto wake ni haki, na kwamba mauti ni haki, na kwamba ufufuo baada ya mauti ni haki, na kwamba bila shaka Kiyama kitakuja, na kwamba Mwenyezi Mungu atawafufua walio makaburini?

"Enyi watu hakika Mwenyezi Mungu ni mtawala wangu na mimi ni mtawala wa waumini, na mimi nina mamlaka zaidi kwao kuliko hata yale waliyonayo juu ya nafsi zao, hivyo yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi huyu – Ali - ni mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui.

"Enyi watu! Hakika mimi nitawatangulieni, na hakika nyinyi mtakuja kwangu katika Hodhi ambayo ni pana sawa na umbali uliyopo baina ya Basra na Sanaa. Ndani yake mna vikombe vya fedha sawa na idadi ya nyota, na mimi nitakuulizeni kuhusu vizito viwili pindi mtakapokuja kwangu. Hivyo basi angalieni jinsi mtakavyoishi navyo baada yangu. Kizito kikubwa ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu, nayo ni kamba ambayo ncha yake moja ipo mikononi mwa Mwenyezi Mungu na ncha nyingine imo mikononi mwenu, basi shikamaneni nacho hamtopotea wala kubadilishwa. Na kingine ni kizazi changu, watu wa Nyumba yangu, hakika Mpole Mjuzi amenipa habari kwamba hivyo viwili havitotoweka mpaka vitakaponifikia katika Hodhi." – Amesema: Ameiandika al-Hakim Tirmidhiy katika *Nawadirul-Usul*, na Tabaraniy kaiandika katika *al-Kabir* kutoka kwa Abu Tufaylu kutoka kwa Hudhayfah bin Asid.

**Nasema:** Na pia al-Haythamiy ameitaja katika *Majmau* yake, katika Juz. 9, uk. 163, na akasema mwanzoni mwa hadithi: "Kutoka kwa Hudhayfah bin Asid, amesema: 'Wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipotoka katika Hijja ya kuaga aliwazuia Maswahaba zake katika eneo lenye miti iliyo mbali mbali, akawataka wateremke hapo, kisha akawatumia ujumbe kuwa wafagie miba iliyoko chini ya miti hiyo. Alikwenda katika miti hiyo akaswali hapo kisha akasimama na kusema: 'Enyi watu! Hakika Mpole Mjuzi amenipa habari…'Akasimulia hadithi kama ilivyotangilia, na akasema: 'Ameipokea Tabaraniy.'"Na pia al-Mutaqiy ameitaja mara ya pili katika *Kanzul–Ummal*Juz.3, uk. 61, na amesema: "Kutoka kwa Abu Tufaylu Amiru Ibn Wathilah, kutoka kwa Hudhayfah bin Asad al-Ghaffariy, amesema: 'Wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipotoka…"'Akasimulia hadithi kama ilivyotangilia kutoka kwa al-Haythamiy. Na Ibn Athir ameitaja pia katika *Usudul–Ghabah* Juz. 3, uk.92, amesema humo: "Kutoka kwa Abu Tufaylu Amiru bin Wathilah, kutoka kwa Hudhayfah bin Asid al-Ghaffariy na Amiru bin Layla bin Dhamrah; wamesema: 'Wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipotoka katika Hijja ya kuagana wala hakuhiji zaidi ya Hijja hiyo, alikuja mpaka akafika Juhfah -na hiyo ndiyo siku ya Ghadir Khum na hapo pana msikiti maarufu -akasema: 'Enyi watu! Hakika Mpole Mjuzi amenipa habari..'" mpaka mwisho kama ilivyotangulia. Na Ibn Hajar ameitaja pia kwa ufupi katika *Al-Isabah* yake Juz.4, Sehemu ya kwanza, uk.61.

**Kanzul–Ummal, Juz.6, Uk.153:**

"Ali bin Abu Talib ni mtawala wa kila ambaye mimi ni mtawala wake."

Amesema: Ameiandika Muhamiliy katika *al-Amaliy*yakekutoka kwa Ibn Abbas.

**Nasema:** Naal-Munawi ameitaja pia katika *Faydhul-Qadir* katika matini, katika Juz.4, uk. 358 na katika *Kunuzul–Haqaiq*uk.92, na pia kaitaja Ali bin Sultan katika *Mirqatu* yake katika ufafanuzi, katika Juz.5, uk.568.

**Kanzul–Ummal, Juz. 6, Uk. 153:**

Na tamko lake ni: "Tambueni kwamba Mwenyezi Mungu ni mtawala wangu na mimi ni mtawala wa kila muumini, hivyo yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake." – Amesema ameiandika Abu Na'im katika *Fadhailus-Sahabah* kutoka kwa Zayd bin Arqam pamoja na al-Barau bin Azib.

**Kanzul–Ummal, Juz.6, Uk.154:**

Na tamko lake ni: "Ewe Mungu Wangu!Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake. Ewe MunguWangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui. Mnusuru mwenye kumnusuru na msaidie mwenye kumsaidia." - Amesema: Ameipokea Tabaraniy kutoka kwa Habashiy bin Junadah.

**Nasema:** Na al-Haythamiy ameitaja pia katika *Majmau* yake katika Juz.9, uk.106, na amesema:"Kutoka kwa Habashiy bin Junadah, amesema: 'Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema siku ya Ghadir Khum: Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake."' Mpaka mwisho kama ilivyotangulia. Kisha akasema: "Ameipokea Tabaraniy na wapokezi wake ni watu walioaminiwa."Pia al-Muhibu Tabari ameitaja katika *ar-Riyadh an-Nadhrah*Juz.2, uk.169, na amesema: "Ameiandika al-Mukhlisu Dhahbiy.

**Kanzul–Ummal, Juz. 6, Uk. 154:**

Na tamko lake ni: "Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui."Amesema: Ameiandika Tabaraniy kutoka kwa Ibn Umar na Ibn Abu Shaybah, kutoka kwa Abu Hurayra na kwa Maswahaba kumi na wawili. Na Ahmad bin Hanbal, Tabaraniy na Said bin Mansuri wameiandika kutoka kwa Abu Ayub na kwa kundi la Maswahaba. Na al-Hakim ameiandika kutoka kwa Ali (as) na kwa Talha. Pia Ahmad bin Hanbal, Tabaraniy na Said bin Mansuri wameiandika kutoka kwa Ali (as) na kwa Maswahaba thelathini. Na Abu Na'im ameiandika katika *Fadhailus-Sahabah* kutoka kwa Saad. Na al-Khatib ameiandika kutoka kwa Anas.

**Kanzul–Ummal, Juz. 6, Uk. 154:**

Amesema: Kutoka kwa Maimuna Abu Abdullah, amesema: "Nilikuwa kwa Zayd bin Arqam, akaja mtu na kumuuliza (Zayd) kuhusu Ali (as), naye akamjibu: 'Hakika tulikuwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) safarini baina ya Makka na Madina, tukateremka sehemu inayoitwa Ghadir Khum. Mtu akaadhini kwa ajili ya kuwakusanya watu, na watu walipokusanyika alimhimidi Mwenyezi Mungu na

kumsifu kisha akasema: 'Enyi watu! Je mimi si ni mwenye mamlaka zaidi kwa kila muumini kushinda hata aliyonayo juu ya nafsi yake wenyewe?' Tukasema: 'Ndiyo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, sisi tunashahidia kuwa hakika wewe una mamlaka zaidi kwa kila muumini kushinda hata aliyonayo juu ya nafsi yake wenyewe.' Akasema: 'Hakika yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi huyu ndiye mtawala wake.' Akawa ameunyanyua mkono wa Ali (as), wala sijui kusudio lake isipokuwa alisema: 'Ewe Mungu Wangu mpende yule mwenye kumpenda na mfanyie uadui yule mwenye kumfanyia uadui.'" - Amesema: Ameiandika Ibn Jariri.

**Kanzul–Ummal, Juz. 6, Uk. 390:**

Amesema: Kutoka kwa Abu Dhuha kutoka kwa Zayd bin Arqam, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema:'Yeyote ambaye mimi ni walii wake basi Ali ni walii wake.'" - Amesema: Ameiandika Ibn Jariri.

**Kanzul–Ummal, Juz. 6, Uk. 397:**

Amesema: Kutoka kwa Abdur-Rahman bin Abi Layla, amesema: "Ali (as) alihutubia siku moja akasema: 'Namuapiza kwa Mwenyezi Mungu kiapo cha Uislam mtu yeyote ambaye alimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) siku ya Ghadir Khum akisema huku akiwa kanishika mkono: 'Je mimi si ni mwenye mamlaka zaidi kwenu enyi Waislamu kushinda hata mliyonayo juu ya nafsi zenu wenyewe? Wakasema: Ndiyo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Akasema: Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake. Ewe Mungu Wangu, mpende yule mwenye kumpenda na mfanyie uadui yule mwenye kumfanyia uadui. Mnusuru yule mwenye kumnusuru na mtelekeze yule mwenye kumtelekeza. Asimame na kutoa ushahidi.' Wakasimama watu kumi na kutoa ushahidi, lakini baadhi wakaficha ushahidi na hivyo hawakumaliza maisha ya dunia isipokuwa tayari walikuwa wameshapatwa na upofu na mbalanga."- Amesema: Ameiandika al-Khatib katika *al-Ifrad*.

**Kanzul–Ummal, Juz. 6, Uk. 397:**

Amesema: Kutoka kwa Ali (as) amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Je mimi si ni mwenye mamlaka zaidi kwa waumini kushinda hata waliyonayo juu ya nafsi zao wenyewe?' Wakasema: 'Ndiyo.' Akasema: 'Yeyote ambaye mimi ni walii wake basi huyu ndiye walii wake.'

— Amesema: AmeiandikaIbn Abi Aswim.

**Kanzul–Ummal, Juz. 6, Uk. 398:**

Amesema: Kutoka kwa Jabir bin Samrah, amesema: "Tulikuwa Juhfah kwenye bwawa la Khum, mara Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akatokeza mbele yetu huku akiwa kamshika mkono Ali (as), akasema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi huyu ndiye mtawala wake.'"

— Amesema: Ameiandika Ibn Abi Shaybah.

**Kanzul–Ummal, Juz.6, Uk.398:**

Amesema: Kutoka kwa Jabir bin Abdullah, amesema: "Tulikuwa Juhfah kwenye bwawa la Khum, na kulikuwa na watu wengi kutoka Juhaynah, Mazinah na Ghaffar, mara Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akatokeza mbele yetu kutoka kwenye hema, akaashiria mara tatu kwa mkono wake, akaushika mkono

wa Ali (as) na kusema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.'"- Amesema: Ameiandika Bazar.

**Kanzul–Ummal, Juz. 6, Uk. 399:**

Amesema: Kutoka kwa Jarir Bajaliy amesema: "Tulihudhuria msimu wa Hijja pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) - nayo ilikuwa Hijja ya kuaga - tupofika sehemu inayoitwa Ghadir Khum, akaadhini kwa ajili ya kuwakusanya watu, tukakusanyika Muhajirina na Ansar. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasimama katikati yetu na akasema: 'Enyi watu lipi mnaloshahidia?' Wakasema: 'Tunashahidia kwamba hapana Mungu isipokuwa Allah.' Akasema: 'Kisha nini?' Wakasema: 'Na kwamba Muhammad ni mja na Mtume Wake.' Akasema: 'Basi ni nani mtawala wenu?' Wakasema: 'Mwenyezi Mungu na Mtume wake ndiowatawala wetu.' Akasema: 'Ni nani mtawala wenu?' Kisha akapiga mkono wake kwenye kifupapanya cha mkono wa Ali (as) akamsimamisha akaondoa mkono wake kwenye kifupapanya na kumshika katika dhiraa yake na kusema: 'Yeyote ambaye Mwenyezi Mungu na Mtume Wake ni watawala wake basi huyu ni mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui. Ewe Mungu wangu, yeyote atakaye mpenda miongoni mwa watu basi kuwa kipenzi chake, na yeyote atakayembugudhi basi kuwa mbughudhi kwake.'" - Amesema: Ameipokea Tabari.

**Nasema:** al-Mutaqiy ameitaja katika *Kanzul–Ummal* kwa ufupi katika Juz.6, uk.154, na al-Haythamiy ameitaja kwa tofauti ndogo katika *Majmau* yake katika Juz.9, uk.106.

**Kanzul–Ummal, Juz. 6, Uk. 399:**

Amesema: Kutoka kwa Ali (as): "Hakika Mtume (saww) alifika kwenye mti huko Khum, kisha akatoka huku akiwa ameushika mkono wa Ali (as) akasema: 'Enyi watu! Si mnashahidia kwamba Mwenyezi Mungu ni Mola wenu?' Wakasema: 'Ndiyo.' Akasema: 'Si mnashahidia kuwa hakika Mwenyezi Mungu na Mtume wake wana mamlaka zaidi kwenu kuliko hata mliyonayo juu ya nafsi zenu wenyewe, na kwamba Mwenyezi Mungu na Mtume wake ni watawala wenu?' Wakasema: 'Ndiyo.' Akasema: 'Yeyote ambaye Mwenyezi Mungu na Mtume wake ni watawala wake basi huyu ni mtawala wake. Na nimewaachieni vitu ambavyo ikiwa mtavichukua basi hamtapotea baada yake, navyo ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu, ncha yake moja imo mikononi mwa Mwenyezi Mungu na ncha yake nyingine imo mikononi mwenu. Na watu wa Nyumba yangu (Ahlul-Bait).'"– Amesema: Ameiandika Ibn Jarir, Ibn Abi Aswim na Mahamiliy katika *al-Amaliy* yake na amesema ni hadithi sahihi.

**Kanzul–Ummal, Juz. 6, Uk. 403:**

Amesema: Kutoka kwa Amairu bin Saad, kwamba hakika Ali (as) aliwakusanya watu sehemu ya wazi na mimi nikiwa nashuhudia, akawaambia: "Namwapiza kwa Mwenyezi Mungu mtu yeyote aliyemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake' asimame." Wakasimama watu kumi na nane, wakashahidia kuwa wao walimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema hayo. - Amesema: Ameiandika Tabaraniy katika *al-Awsat.*

**Nasema:** al-Haythamiy pia ameitaja katika *Majmau* yake katika Juz.9, uk. 108, na amesema: Sanadi yake ni nzuri.

**Kanzul–Ummal, Juz. 6, Uk. 403:**

Amesema: Kutoka kwa Zayd bin Arqam amesema: "Ali (as) aliwaapiza watu kuwa yeyote aliyemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema siku ya Ghadir Khum: 'Si mnajua kuwa hakika mimi nina

mamlaka zaidi kwa waumini kuliko hata waliyonayo juu ya nafsi zao?' Wakasema: 'Ndiyo.' Akasema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui,'asimame. Wakasimama watu kumi na mbili wakashahidia hilo.

**Kanzul–Ummal, Juz. 6, Uk. 403:**

Amesema: Kutoka kwa Abu Is'haqa kutoka kwa Amru Dhiy Muri na Said bin Wahab na Zayd bin Yathiu, wamesema: "Tulimsikia Ali (as) akisema: 'Namwapiza kwa Mwenyezi Mungu yeyote yule aliyemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema aliyosema siku ya Ghadir Khum asimame.' Wakasimama watu kumi na tatu wakashahidia kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Je mimi si ni mwenye mamlaka zaidi kwa waumini kuliko hata waliyonayo juu ya nafsi zao?' Wakasema: 'Ndiyo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Akaushika mkono wa Ali (as) na kusema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui. Mpende mwenye kumpenda na mbughudhi mwenye kumbughudhi. Mnusuru mwenye kumnusuru na mtelekezemwenye kumtelekeza.'"

Amesema: Ameipokea Bazar na Ibn Jarir na Khalaiy katika *al-Khalaiyat*. Kisha akasema: al-Haythamiy amesema: "Ni sanadi yenye wapokezi waaminifu."

**Kanzul–Ummal, Juz. 6, Uk. 405:**

Amesema: Kutoka kwa Saad, amesema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema kuhusu Ali (as) mambo matatu, kuwa na moja tu kati ya hayo ni jambo nilipendalo zaidi kuliko hata kuwa na dunia na yote yaliyomo humo, nilimsikia akisema: 'Hakika wewe (Ali) kwangu mimi una cheo sawa na cheo cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu.' Na nikamsikia akisema: 'Nitamkabidhi bendera kesho mtu anayempenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanampenda yeye, na si mwenye kukimbia vitani.' Na nikamsikia akisema: 'Ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake.'" – Amesema: Ameiandika Ibn Jarir.

**Kanzul–Ummal, Juz. 6, Uk. 406:**

Amesema: Kutoka kwa Ali (as), kwamba Mtume (saww) alishika mkono wake (as) siku ya Ghadir Khum na akasema: "Ewe Mungu Wangu! Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake." – Amesema: Ameiandika Ibn Rahawayhi na Ibn Jarir.

**Al-Isabah Juz. 1, Sehemu ya kwanza, Uk. 319:**

Amesema: Katika kitabu kinachozungumzia utawalishaji, Ibn Uqdah amepokea hadithi ya Habib bin Badil bin Waraqau Al-Khuzaiy, kupitia riwaya ya Abu Maryam kutoka kwa Zur bin Habish, amesema: "Ali (as) alisema: 'Ni akina nani waliopo hapa miongoni mwa Maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)?' Wakasimama watu kumi na mbili akiwemo Qays bin Thabit na Habib bin Badil bin Waraqau, wakashahidia kwamba wao walimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema:'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake.'"

**Nasema:** Na pia ameitaja Ibn Athir al-Jazriy katika *Usudul-Ghabah* katika Juz. 1, uk. 368, amesema: "Siku moja Ali (as) alitoka kutoka katika kasri akapokewa na askari wa farasi waliokuwana panga, wakasema: 'Amani iwe juu yako ewe Amirul-Muuminina, amani iwe juu yako ewe mtawala

wetu na pia rehema za Mwenyezi Mungu na baraka zake viwe juu yako.' Ali (as) akasema: 'Ni akina nani waliopo hapa miongoni mwa Maswahaba wa Mtume (saww)?' Wakasimama watu kumi na mbili akiwemo Qaysu bin Thabit, Hashim Ibn Utbah, na Habib bin Badil bin Waraqau, wakashahidia kwamba wao walimsikia Mtume (saww) akisema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake.'"

**Al-Isabah Juz. 2, Sehemu ya kwanza, Uk. 57:**

Amesema: Ibn Uqdah amepokea hadithi katika kitabu kinachozungumzia utawalishaji, kutoka kwa Habah bin Juwayn, amesema: "Ilipotimu siku ya Ghadir Khum Mtume (saww) aliwaita watu ili wakusanyike. Akaitaja hadithi:'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake.' Akasema: 'Akaunyanyua mkono wa Ali (as) mpaka nikaziona kwapa zao, na mimi wakati huo nilikuwa ningali mushrik.'"

**Nasema:** Na pia Ibn Athir al-Jazriy ameitaja katika *Usudul-Ghabah*katika Juz. 1, uk. 368, na akasema: Amepokea kutoka kwa Yakub bin Yusuf -mpaka aaliposema: Kutoka kwa Habah bin Juwayn Al-Araniy Al-Bajaliy, amesema: "Ilipotimu siku ya Ghadir Khum Mtume (saww) aliwaita watu ili wakusanyike, ilikuwa ni nusu ya mchana, akamhimidi na kumshukuru Mwenyezi Mungu kisha akasema: 'Enyi watu!Je mnajuakwamba hakika mimi nina mamlaka zaidi kwenu kuliko hata mliyonayo juu ya nafsi zenu?' Wakajibu: 'Ndiyo.' Akasema: 'Basi yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiyemtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui.' Na akaushika mkono wa Ali (as) akaunyanyua juu mpaka nikaziona kwapa zao, na mimi wakati huo nilikuwa ningali mushriku."

**Al-Isabah Juz. 3, Sehemu ya kwanza, Uk. 29:**

Amesema: Ibn Uqdah amepokea hadithi katika kitabu kinachozungumzia utawalishaji, kupitia njia ya Amru bin Abdullah bin Ya'ala bin Murah, kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake, amesema: "Ali (as) alipofika Kufa aliwaapiza watu:'Yeyote aliyemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake' asimame. Wakamjibu watu kumi akiwemo Zayd au – Yazid - bin Sharahil Al-Answariy.

**Nasema:** Na pia Ibn Athir al-Jazriy ameipokea katika *Usudul-Ghabah*katika Juz. 5, uk. 6, amesema: "Abu Musa alitupa habari -mpaka aliposema: Alitusimulia Abu Abbas bin Uqdah - mpaka aliposema: Kutoka Amru bin Abdullah bin Ya'ala bin Murah, kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake, amesema: Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui.' Wakati Ali (as) alipofika Kufa aliwaapiza watu, wakamjibu watu kumi akiwemo Abu Ayub –aliyekuwa mmiliki wa nyumba ya Mtume (saww) - na Najiyah bin Amru Al-Khuzaiy." Na pia ameitaja Ibn Athir al-Jazriy katika *Usudul-Ghabah* katika Juz. 2, uk. 233.

**Al-Isabah Juz. 4, Sehemu ya kwanza, Uk. 16:**

Amesema: Ibn Uqdah amepokea kupitia kwa Amru bin Abdullah bin Ya'ala bin Murah, kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake, amesema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.' Wakati Ali (as) alipofika Kufa aliwaapiza watu, wakamjibu watu kumi na saba akiwemo Aamir bin Layla Al-Ghaffariy."

**Nasema:** Na pia ameitaja katika Juz. 6, uk. 223, na pia Ibn Athir al-Jazriy ameitaja katika *Usudul-Ghabah*katika Juz. 3 uk. 93, na baada ya kauli yake: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.' Amesema humo: 'Ewe Mungu Wangu, mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui.'

**Al-Isabah Juz. 4, Sehemu ya kwanza, Uk. 14:**

Amesema: Ibn Uqdah amepokea katika kitabu kinachozungumzia utawalishaji - kwa njia ya Musa bin Aktal bin Umayru an-Namiriy: Alinisimulia ami yangu Aamir bin Umayru, alisema: Akaitaja hadithi ya Ghadir Khum.

**Al-Isabah Juz. 4, Sehemu ya kwanza, Uk. 143:**

Amesema: Abu Abbas bin Uqdah amepokea katika njia kadhaa hadithi isemayo: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.' Kwa sanad inayofika kwa Ibrahim bin Muhammad -nahisi atakuwa ni Ibn Abi Yahya - kutoka kwa Ja'far bin Muhammad, kutoka kwa baba yake na kutoka kwa Ayman bin Nabil bin Abdullah bin Yamil, amesema:"Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.'" Kisha akasema: Na akairudia Abu Musa.

**Nasema:** Na ameitaja pia Ibn Athir al-Jazriy katika *Usudul-Ghabah*katika Juz. 3, uk.274, na amesema: "Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake."

**Al-Isabah Juz. 4, Sehemu ya kwanza, Uk. 169:**

Amesema: Katika kitabu kinachozungumzia utawalishaji, Ibn Uqdah amemtaja Abdur-Rahman bin Abdi Rabi Al-Answariy miongoni mwa waliopokea hadithi: "Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake." Na akaendelea kusimulia - kupitia njia ya Asbagh bin Nabatah - akasema: "Wakati Ali (as) alipowaapiza watu sehemu ya wazi: 'Yeyote aliyemsikia Mtume (saww) akisema aliyosema siku ya Ghadir Khum asimame, na wala asisimame isipokuwa yule aliyemsikia.' Walisimama watu kumi na kadhaa miongoni mwao ni Abu Ayub, Abu Zaynab, na Abdur-Rahman bin Abdu Rabi, wakasema: 'Tunashahidia kwamba sisi tulimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: Hakika Mwenyezi Mungu ni mtawala wangu na mimi ni mtawala wa waumini, hivyo basi yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake.'"

**Nasema:** Na ameitaja pia katikaJuz. 7, Sehemu ya kwanza, uk. 78, na amesema humo: "Wakasema: Tunashahidia kwamba sisi tulimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema -na aliushika mkono wako siku ya Ghadir Khum akaunyanyua juu na kusema: 'Si mnashahidia kuwa hakika mimi nimekwishafikisha?' Wakasema: 'Tunashahidia hilo.' Akasema: 'Basi yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake.'"

Na Ibn Athir al-Jazriy ameitaja katika *Usudul-Ghabah*katika Juz. 5, uk. 205, na akaongeza: "Ewe Mungu Wangu, mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui. Mpende mwenye kumpenda na msaidie mwenye kumsaidia na mbughudhi mwenye kumbughudhi." Na Twahawiy ameitaja pia katika *Mushkilul-Athar*katika Juz. 2, uk.307, na baada ya kipengele alichoongeza Ibn Athir, yeye ameongeza:"Mnusuru mwenye kumnusuru na mtelekeze mwenye kumtelekeza."

**Al-Isabah Juz. 4, Sehemu ya kwanza, Uk. 182:**

Amesema: Abu Abbas bin Uqdah amemtaja Abdur-Rahman bin Mudliju katika kitabu kinachozungumzia utawalishaji, na amepokea kupitia njia ya Musa bin Nadhir bin Rabii al-Hamswiy, amesema: Amenihadithia Saad bin Talib Abu Ghaylan, amesema: Amenihadithia Abu Is'haqa, amesema: Wamenihadithiawatu wengi ambao siwezi kuwahesabu kuwa: Hakika Ali (as) aliwaapiza watu katika eneo la wazi (Rahbah) alisema:"Ni nani aliyesikia kauli ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): 'Yeyote yule ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.'" Wakasimama kundi akiwemoAbdur-Rahman bin Mudliju wakashahidia kwamba wao wamesikia hayo kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). – Amesema: Ameiandika Ibn Shahin kutoka kwa Ibn Uqdah na akairudia Abu Musa.

**Nasema:** Na ameitaja pia Ibn Athir al-Jazriy katika *Usudul-Ghabah*Juz. 3 uk. 321, na amesema humo: "Wakashahidia kwamba wao walisikia hayo kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), na baadhi ya watu wakaficha kutoa ushahidi na hivyo kabla ya mauti kuwafikia walipatwa na upofu na maradhi, miongoni mwao ni Yazid bin Wadiah na Abdur-Rahman bin Mudliju."[526]

**Al-Isabah Juz. 7, Sehemu ya kwanza, Uk. 156:**

Amesema: Abu Abbas bin Uqdah amemtaja Abu Qudamah al-Answariy katika kitabu kinachozungumzia utawalishaji –ambacho humo amekusanya njia za hadithi: Yeyote yule ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.' Ameandika humo kwa njia itokayo kwaMuhammad bin Kathir kutoka kwa Fitr kutoka kwa Abu Tufail, amesema: "Tulikuwa kwa Ali (as) akasema: 'Namuapiza kwa Mwenyezi Mungu, ni nani aliyekuwepo siku ya Ghadir Khum.' Wakasimama watu kumi na saba miongoni mwao ni Abu Qudamah al-Answariy, wakashahidia kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu alisema hayo." - Amesema: Ameirudia Abu Musa.

**Nasema:** Na ameipokea pia Ibn Athir al-Jazriy katika *Usudul-Ghabah* Juz. 5 uk.276, baada ya kutaja sanad amesema hivi: "Kutoka kwa Abi Tufail amesema: 'Tulikuwa kwa Ali (as) akasema: Namuapiza kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, aliyekuwepo siku ya Ghadir Khum na asimame.' Wakasimama watu kumi na saba miongoni mwao Abu Qudamah al-Answariy wakasema: Tunashahidia kwamba sisi tulikutana pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika Hijja ya mwisho mpaka ulipotimu wakati wa adhuhuri akatoka Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaamrisha kuletwe miti, tukafunga na akatundika juu yake nguo, kisha akanadi kwa ajili ya Swala. Tukatoka na kuswali, kisha akasimama akamhimimdi na kumsifu Mwenyezi Mungu Mtukufu na akasema: 'Enyi watu mnatambua kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ni mtawala wangu na mimi ni mtawala wa Waumini, na mimi nina mamlaka zaidi kwenu kuliko hata mliyonayo juu ya nafsi zenu.' Alitamka hayo mara kwa mara nasi tukisema: 'Ndiyo.' Huku akiwa kaushika mkono wako alisema: 'Yeyote yule ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake. Ewe Mola wangu mpendemwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui.' Alirudia mara tatu."

**Usudul-Ghabah Juz. 1, uk. 308:**

Amesema: Na amepokea Abu Ahmad al-Askariy kwa sanadi yake kutoka kwa Ammarah bin Yazid kutoka kwa Abdullah bin Ulai kutoka kwa Zahriy -mpaka aliposema: Amesema: "Nimemsikia Aba Junaidah Jun'dai bin Amru bin Mazin akisema: Nilimsikia Mtume (saww) akisema: 'Yoyote mwenye kunizushia uongo kwa makusudi basi ajiandae makazi yake ni motoni.' Na wakati akiwa amekwisha ondoka kutoka katika Hijja ya mwisho na aliposhuka Khadir Khum alisimama mbele ya watu akawahutubia, akashika

[526] Na Anas bin Malik nimiongoni mwa waliopatwa na upofu kutokana na kuficha haki ya Ali (as).

mkono wa Ali (as) na nikamsikia akisema: 'Yeyote yule ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake. Ewe Mola Wangu, mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui.'" Abdullah anasema: Nikamwambia Zahriy: "Usizungumze haya ukiwa Sham masikio yako yatajaa matusi kwa kusikia matusi dhidi ya Ali (as)." Akasema: "Hakika nina fadhila zinazomuhusu Ali (as) lau kama nitasimulia fadhila hizo basi nitauwawa."

**Usudul-Ghabah Juz. 2, uk. 307:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Asbaghu bin Nabatah, amesema: "Ali (as) aliwaapiza watu siku ya mkusanyiko katika eneo la wazi (Rahba), akasema: 'Yeyote aliyesikia aliyoyasema Mtume (saww) siku ya Ghadir Khum na asimame, na wala asisimame isipokuwa yule aliyemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema.'Wakasimama kundi la watu kumi, miongoni mwao ni Abu Ayub al-Answariy, Abu Umrah bin Muhswin, Abu Zaynab, Sahal Ibn Hunayf, Khuzaymah bin Thabit, Abdullah bin Thabit al-Answariy, habashiy bin Junadah as-Saluliy, Ubayd bin Azib al-Answariy, Nu'man bin Ajalan al-Answariy, Thabit bin Wadiahal-Answariy, Abu Fadhalah al-Answariy na Abdur-Rahman bin Abdirabi, wakasema: Tunashahidia kwamba sisi tulimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Tambueni kwamba hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ni mtawala wangu na mimi ni mtawala wa Waumini, tambueni kuwa yeyote yule ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake. Ewe MunguWangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui. Mpende mwenye kumpenda na mchukie mwenye kumchukia na msaidie mwenye kumsaidia.'"

**Al-Imamah Was-Siyasah cha Ibn Qutaybah Uk. 93:**

Amesema: Wametaja kwamba mtu mmoja kutoka Hamadan anaitwa Burdam alifika kwa Muawiyah akamsikia Amru akimkashifu Ali (as) akamuuliza: "Ewe Amru hakika mababu zetu walimsika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Yeyote yule ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.' Je ni haki hayo au ni batili?" Amru akajibu: "Ni haki, na mimi nakuzidishia: Hakika hakuna yeyote katika Maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mwenye fadhila mfano wa fadhila za Ali (as)."Kijana yule akashtuka.

**Mushkilul-Athar cha at-Twahawi Juz. 2, uk. 307:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Muhammad bin Umar bin Ali (as), kutoka kwa baba yake Ali (as) kwamba Mtukufu Mtume (saww) alifika kwenye mti uliyopo Khum akatoka huku akiwa ameshika mkono wa Ali (as) na akasema: "Enyi watu si mnashahidia kwamba Mwenyezi Mungu ni Mola wenu?" Wakasema: "Ndiyo (tunashahidia)." Akasema: "Si mnashahidia kuwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake wana mamlaka zaidi kwenu kuliko hata mliyonayo juu ya nafsi zenu, na hakika Mwenyezi Mungu na Mtume wake ni watawala wenu?" Wakasema: "Ndiyo (tunashahidia)." Akasema: "Basi yeyote yule ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake. Hakika nimekuachieni ambavyo mkishikamana navyo kamwe hamtopotea baada yangu: Kitabu cha Mwenyezi Mungukilichomo mikononi mwenu na Ahlul-Bayt wangu."

**Faydhul-Qadir cha al-Munawi Juz. Uk. 218, katika ufafanuzi:**

Amesema: Na ameipokea hadithi ya Ghadir ad-Daylamiy kwa tamko hili: "Yeyote ambaye mimi ni Nabii wake basi Ali ni mtawala wake." Amesema: "Na kwa hili Abu Bakr amesema -katika aliyoandika ad-Daru al-Qutniy: "Ali ni kizazi cha Mtume wa Mwenyezi (saww)."

**Nasema:** Na pia ameitaja katika *Kunuzul-Haqaiq*uk. 147, na tamko lake humo ni: "Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake." Amesema: Ni riwaya ya ad-Daylamiy.

**Majmauz-Zawa'id cha al-Haythamiy Juz. 7 Uk. 17:**

Amesema: Kutoka kwa Ammar bin Yasir amesema: "Alisimama muombaji mbele ya Ali (as) akiwa katika rukuu ya Swala ya Sunna, mara akachomoa pete yake na kumpa yule muombaji, naye alikwenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na akamfahamisha juu ya tukio hilo, na ndipo ikateremka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hii Aya: **"Hakika walii wenu khasa ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walioamini ambao husimamisha Swala na hutoa Zaka na hali ya kuwa wamerukuu."** Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akaisoma na kisha akasema: 'Yeyote yule ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpendana mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui."'

– Amesema: Ameipokea Tabaraniy katika *al-Awsat*.

**Majmauz-Zawa'id cha al-Haythamiy Juz. 9, uk. 105:**

Amesema: Kutoka kwa Zayd bin Arqam, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliamrisha kuletwe miti pakafungwa kutoka juu na chini na kufunikwa, kisha akatuhutubia. Naapa kwa Mwenyezi Mungu hakuna kitu chochote kitakachotokea mpaka siku ya Kiyama isipokuwaalitueleza siku ile, kisha akasema: 'Enyi watu ni nani mwenye mamlaka zaidi kuliko mliyonayo juu ya nafsi zenu?' Tukajibu: 'Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wana mamlaka zaidi kuliko tuliyonayo juu ya nafsi zetu.' Akasema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi huyu ni mtawala wake.' -Akimaanisha Ali (as)- kisha akachukua mkono wake akaunyoosha kisha akasema: 'Ewe Mola Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui."' – Amesema: Ameipokea Tabaraniy, na al-Bazar ameipokea ikiwa kamili zaidi.

**Majmauz-Zawa'id cha al-Haythamiy Juz. 9, uk. 105:**

Amesema: Na kutoka kwa Daud bin Yazid al-Awdiy kutoka kwa baba yake amesema: "Abu Hurayra aliingia msikitini na mara watu wakamkusanyikia, akasimama mbele yake kijana mmoja na kusema: 'Nakuapizia kwa Mwenyezi Mungu, je ulimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake. Ewe Mola Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui?' Akajibu: 'Mimi nashahidia kuwa hakika nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake. Ewe Mola Wangu, mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui.'"

– Amesema: Ameipokea Abu Ya'ala na al-Bazar mfano wa hivyo, na Tabaraniy katika *al-Awsat*.

**Majmauz-Zawa'id cha al-Haythamiy Juz. 9, uk. 106:**

Amesema: Na kutoka kwa Malik bin al-Huwayrith amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.'" – Amesema: Ameipokea Tabaraniy na wapokezi wake ni watu wakweli.

**Majmauz-Zawa'id cha al-Haythamiy Juz. 9, uk. 107:**

Amesema: Na kutoka kwa Hamidi bin Amarah amesema: "Nilimsikia baba yangu akisema: Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema huku kashika mkono wa Ali (as): 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi huyu ni mtawala wake. Ewe Mola Wangu, mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui.'" – Amesema: Ameipokea al-Bazar.

**Majmauz-Zawa'id cha al-Haythamiy Juz. 9, uk. 108:**

Amesema: Na kutoka kwa Ibn Abbas amesema: "Hakika Mtume (saww) alisema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.'"– Amesema: Ameipokea al-Bazar katika hadith, na wapokezi wake ni watu wakweli.

**Majmauz-Zawa'id cha al-Haythamiy Juz. 9, uk. 108:**

Amesema: Kutoka kwa Abi Said amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.'" – Amesema: Ameipokea Tabaraniy katika *al-Awsat*. Kisha hapa pana hadithi nyingine zinafaa kutajwa mwishoni mwa mlango huu japokuwa hazina tamko: "Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake."

**Miongoni mwa hadithi hizo ni ile aliyoipokea Ahmad bin Hanbal katika Musnad yake Juz. 1, uk. 119:**

Kutoka kwa Abdur-Rahman bin Abi Layla amesema: Amenihadithia kwamba yeye alimshuhudia Ali (as) akiwa katika eneo la wazi (Rahbah) akasema: "Namuapiza kwa Mwenyezi Mungu, mtu yeyote aliyemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na alimshuhudia siku ya Ghadir Khum basi na asimame, na wala asisimame isipokuwa yule aliyemuona." Wakasimama watu kumi na mbili na wakasema: "Hakika tulimuona na kumsikia alipomshika mkono wake na kusema: 'Ewe Mola Wangu mpendemwenye kumpenda, mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui, mnusuru mwenye kumnusuru, na mtelekeze mwenye kumtelekeza.'Walisimama isipokuwa watu watatu ndio hawakusimama, akawaombea du'a baya na wakapatwa na maafa kutokana na du'a yake."

**Na pia miongoni mwa hadithi hizo ni ile aliyoipokea Ahmad bin Hanbal katika Musnad yake Juz.3, uk.71:**

Amepokea kwa sanadi itokayo kwa Abu Said al-Khidhriy, amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Asijizuie mtu yoyote kusimamisha haki (kutoa ushahidi) atakapoifahamu kwa kuhofia watu." Kisha Abu Said akalia na kusema: "Hakika naapa kwa Mwenyezi Mungu tuliishuhudia (haki) lakini hatukuisimamisha."

**Nasema:** Katika hadithi hii kuna ishara bayana kutoka kwa Abi Said kuhusu yale waliyoshuhudia siku ya Ghadir Khum lakini hawakuyasimamisha kwa kuhofia watu, ndio maana akalia kwa ajili ya hilo. Na Mwenyezi Mungu ndiye mjuzi zaidi.

**Na pia miongoni mwa hadithi hizo ni ile aliyoipokea Ibn al-Athir al-Jazriy katika Usudul-Ghabah Juz. 4, uk. 114, katika wasifu wa Amru bin Sharahil:**

Amesema: Imepokewa kutoka kwa Mtukufu Mtume (saww) kuwa alisema: "Ewe Mungu Wangu, mnusuru atakayemnusuru Ali. Ewe Mungu Wangu mkirimu atakayemkirimu Ali."

**Nasema:** Pia Ibn Hajar ameitaja katika*Al-Isabah* Juz. 4, uk. 305, pia al-Mutaqiy katika Kanzul-Ummal Juz. 6 Uk. 158, na akazidisha mwishoni: "Ewe Mungu wangu mtelekeze atakayemtelekeza Ali."

**Na pia miongoni mwa hadithi hizo ni ile aliyoipokea an-Nasaiy katika Khasa'isu yake Uk. 4 kwa njia yake:**

Kutoka kwa Aisha binti Saad amesema: Nilimsikia baba yangu akisema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) siku ya Juhfa, aliuchukua mkono wa Ali (as) akahutubia. Alianza kwa kumhimidi na kumshukuru Mwenyezi Mungu, kisha akasema: 'Enyi watu hakika mimi ni mtawala wenu.' Wakasema: 'Umesema kweli ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Akaushika mkono wa Ali (as) akaunyanyua na kusema: 'Huyu ndiye kipenzi changu na ndiye atakayefikisha dini yangu badala yangu, na mimi ni mwenye kumpenda yule mwenye kumpenda, na ni mwenye uadui na yule mwenye kumfanyia uadui.'"

**Na pia miongoni mwa hadithi hizo ni ile aliyoipokea al-Mutaqiy katika Kanzul-Ummal Juz. 6, uk. 155:**

Amesema: "Ewe Mungu Wangu! Msaidie yeye na yule atakayemsaidia, mrehemu yeye na yule atakayemrehemu, na mnusuru yeye na yule atakayemnusuru. Ewe MunguWangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui." Yaani Ali (as).

— Amesema: Ameiandika Tabaraniy kutoka kwa Ibn Abbas.

**Na miongoni mwa hadithi hizo ni ile aliyoitaja al-Haythamiy katika Majmau yake Juz. 9, uk. 107:**

Amesema: Na kutoka kwa Nadhir amesema: "Nilimsikia Ali (as) akisema siku ya Jamal kumwambia Talha: 'Nakuapiza kwa Mwenyezi Mungu ewe Talha, je ulimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: Ewe Mungu Wangu, mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui?' Akajibu:'Ndiyo (nilimsikia)', akakumbuka na kuondoka. – Amesema: Ameipokea al-Bazar.

**Na miongoni mwa hadithi hizo ni ile aliyoitaja al-Haythamiy katika Majmau yake Juz. 9, uk. 166:**

Amesema: Kutoka kwa Ummu Salamah amesema: "Fatimah (as) binti ya Mtume (saww) alikuja kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) huku akiwaongoza Hasan na Husain, mikononi mwake kulikuwa na bakuli la Hasan ambalo lilikuwa na chakula cha moto. Alipofika kwa Mtume (saww) na kuliweka bakuli mbele yake, Mtume alimuuliza: 'Yupo wapi Abu Hasan?' Akamjibu: 'Yupo nyumbani.' Akamwitaakakaa Mtume (saww) pamoja na Ali, Fatimah, Hasan na Husain (as) wakila chakula, Ummu Salamah anasema:'Siku ile Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hakuniita, kwani kabla ya siku hiyo hakuwahi kula chakula na mimi nipo isipokuwa mara zote aliniita. Alipomaliza aliwafunika nguo yake na kusema: Ewe MunguWangu mfanyie uadui yeyote mwenye kuwafanyia uadui, na mpende yeyote mwenye kuwapenda."' – Amesema: Ameipokea Abu Ya'ala na sanadi yake ni nzuri.

# MLANGO UNAOZUNGUMZIA KAULI YA UMAR NA ABU BAKR KWA ALI (AS): UMEKUWA MTAWALA WA KILA MUUMINI MWANAUME NA MUUMINI MWANAMKE

**Musnad Imam Ahmad bin Hanbal Juz. 4, uk. 281:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa al-Barau Ibn Azib amesema: “Tulikuwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika safari. Tukateremka Ghadir Khum -ameendelea kusimulia hadith kama ilivyotangulia katika mlango uliopita mwishoni mwa hadithi aliyoinukuu kutoka kwa Ibn Majah, mpaka aliposema: Akaushika -yaani Mtume (saww)- mkono wa Ali (as) na akasema: ‘Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake. Ewe Mungu Wangu, mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui.’ Baada ya hapo akakutana na Umar, naye akamwambia: ‘Hongera ewe mtoto waAbu Talib, sasa umekuwa mtawala wa kila muumini mwanaume na muumini mwanamke.’”

**Nasema:** Na pia imekwisha tangulia kwamba ni kundi kubwa lililojitokeza kunukuu hadithi hii, tumewataja huko nyuma kwa undani zaidi, rejea huko.

**Tafsirul-Kabir ya Fakhru Razi, mwishoni mwa tafsiri ya kauli ya Mtukufu: “Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola Wako Mlezi..” iliyoko katika Sura al-Maidah:**

Amesema –kama ilivyo katika mlango uliotangulia: Kumi –yaani katika sababu za kuteremka Aya hii zilizotajwa na wafasiri: Aya hii imeshuka kueleza fadhila za Ali bin Abu Talib (as), na iliposhuka aya hii, Nabii alishika mkono wake na kusema: “Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui.” Na Umar alipokutana naye alisema: “Hongera ewe mtoto wa Abu Talib, sasa umekuwa mtawala wangu na mtawala wa kila muumini mwanaume na muumini mwanamke.”

**Taarikh Baghdad cha al-Khatib al-Baghdadiy Juz. 8, uk. 290:**

Amepokea kwa njia yake –kama ilivyo katika mlango uliotangulia- kutoka kwa Abu Huraira kuwa alisema: “Yeyote atakayefunga siku ya kumi na nane ya Dhulhija (mfungo tatu) ataandikiwa malipo ya funga ya miezi sitini, nayo ni siku ya Ghadir Khum pale, Mtume (saww) aliposhika mkono wa Ali bin Abu Talib (as) na akasema: ‘Je mimi si ni mtawala wa Waumini?’ Wakajibu: ‘Ndiyo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.’ Akasema: ‘Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.’ Umar bin Khattab akasema: ‘Hongera, hongera ewe mtoto wa Abu Talib, sasa umekuwamtawala wangu na mtawala wa kila mwislamu.’ Na ndipoMwenyezi Mungu akateremsha:**‘Leo nimekukamilishieni dini yenu.’**”

**Nasema:** Na amepiokea kwa njia nyingine mfano wa hii.

**Faydhul-Qadir Juz. 6, uk. 217, katika ufafanuzi:**

Amesema: Abu Bakr na Umar waliposikia hayo -yaani kauli ya Mtume (saww): ‘Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake’: walisema: “Ewe mtoto wa Abu Talib, umekuwa mtawala wa kila muumini mwanaume na kila muumini mwanamke.”Hiyo ni kama alivyopokea ad-Daru al-Qutniy kutoka kwa Saad bin Abu Waqas.

**Nasema:** Na pia ameitaja Ibn Hajar katika *Sawa'iq*yake uk. 26.

**Dhakhairul-Uqba cha Tabari Uk. 68:**

Amesema: Kutoka kwa Umar, walikuja mabedui wawili mbele yake wakizozana, Umar akasema: "Hukumu kati yao ewe Aba Hasan." Ali (as) akahukumu kati yao, mmojawapo akasema: "Yaani tunahukumiwa na huyu kweli?!" Umar akachupa na kumvuta kwake na kumwambia: "Ole wako!Humjui huyu ni nani? Huyu ni mtawala wangu na mtawala wa kila muumini, na yeyote ambaye huyu si mtawala wake basi si muumini."

— Amesema: Ameiandika Ibn Siman katika kitabu *al-Muwafaqat*.

**Nasema:** Na pia ameitaja Ibn Hajar katika *Sawa'iqu* yake uk. 107, na akasema: "Ameiandika ad-Dar al-Qutniy."

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, uk. 170:**

Amesema: Na kutoka kwa Umar, alikuwa akibishana na mtu mmoja katika mas'ala, akamwambia: "Huyu aliyeketi awe mwamuzi kati yangu mimi na wewe." Akamuashiria Ali bin Abu Talib (as), mtu yule akasema: "Huyu mwenye kitambi?" Umar akanyanyuka kutoka alipokaa na akaanza kumvuta mpaka akamnyanyua kutoka chini, kisha akasema: "Unamjua ni nani huyu uliyemfanya mdogo? Huyu ni mtawala wangu na mtawala wa kila Mwislamu." – Amesema: Ameiandika Ibn Siman.

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, uk. 170:**

Amesema: Kutoka kwa Salim: Umar aliambiwa: "Hakika unamfanyia Ali jambo ambalo humfanyii yeyote mwingine kati ya Maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)." Akasema: "Hakika yeye ni mtawala wangu." – Amesema: Ameiandika Ibn Siman.

**Nasema:** Na pia ameitaja Ibn Hajar katika Sawa'iq yake uk. 26, na akasema: "Ameiandika ad-Dar al-Qutniy."

**Ar-Riyadh an-Nadhrah Juz. 2, uk. 170:**

Amesema: Kutoka kwa Umar, alisema: "Ali ni mtawala wa kila ambaye Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa ni mtawala wake."

—Amesema: Ameiandika Ibn Siman.

## MLANGO UNAOSEMA MTUKUFU MTUME (SAWW) ALIMFUNGA KILEMBA ALI (AS) SIKU YA GHADIR KHUM KWA MTINDO WANAOFUNGA MALAIKA

**Musnad Abi Daud at-Twayalasiy Juz. 1, uk. 23:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ali (as) kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alinifunga kilemba siku ya Ghadir Khum kwa mtindo wa kuteremsha nchayake nyuma yangu, kisha akasema: 'Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu alinipa msaada siku ya Badri na Hunain kupitia Malaika waliokuwa wamefunga vilemba kwa mtindo huu."

**Nasema:** Pia al-Bayhaqiy ameipokea katika *Sunan* yake Juz. 10, uk. 14. Na pia Ibn Hajar ameitaja katika *Al-Isabah*Juz. 4, Sehemu ya kwanza, uk. 41, na akasema humo: "Kwa kilemba cheusi, na ncha yake ikateremka kwenye mabega yangu." Akasema: Ameiandikaal-Baghawi.

**Kanzul-Ummal Juz. 8, uk. 60:**

Amesema: Kutoka kwa Ali (as) amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alinifunga kilemba siku ya Ghadir Khum, akateremsha ncha yake nyuma yangu." Amesema: Na katika tamko lingine: "Akateremshancha zake kwenye mabega yangu." Kisha akasema: "Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu alinipa msaada siku ya Badri na Hunain kupitia Malaika waliokuwa wamefunga vilemba kwa mtindo huu. Na akasema: Hakika kilemba ni kitambulisho kinachotofautisha kati ya ukafiri na imani." Na katika tamko lingine: "Kati ya Waislamu na Mushirikina." – Amesema: Ameiandika Ibn Abi Shaybah, Abu Daud at-Twayalasiy, Ibn Manii na al-Bayhaqiy.

**Usudul-Ghabah cha Ibn Athir Juz. 3, uk. 114:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abdul-A'ala bin Adiy, kwamba Mtume (saww) alimwita Ali bin Abu Talib (as) siku ya Ghadir Khum, akamfunga kilemba na akateremsha ncha ya kilemba nyuma yake kisha akasema: "Muwe mnajifunga hivi, kwani vilemba ni alama ya Uislamu navyo ni kitambulisho kinachotofautisha kati ya Waislamu na Mushirikina."

**Nasema:** Na pia al-Muhibu Tabari ameitaja katika *Riyadh an-Nadhrah* Juz. 2, uk. 217.

## MLANGO UNAOSEMA KUWA AYA: "EWE MTUME FIKISHA ULIYOTEREMSHIWA KUTOKA KWA MOLA WAKO." ILITEREMKA SIKU YA GHADIR KHUM KATIKA FADHILA ZA ALI (AS)

**Asbabun-Nuzul cha al-Wahidiy Uk. 150:**

Amesema: Alitupa habari Abu Said Muhammad bin Ali Swafar, alisema: Alitupa habari Hasan bin Ahmad al-Mukhlidiy, alisema: Alitupa habari Muhammad bin Hamdun bin Khalid, alisema: Alitupa habari Muhammad bin Ibrahim al-Khalutiy alisema: Alitupa habari Hasan bin Hamad Sajjadah, alisema: Alitupa habari Ali bin Abis kutoka kwa A'amash na Abu Hijab, kutoka kwa Atwiyah kutoka kwa Abu Said al-Khidriy, amesema: "Aya hii:**'Ewe Mtume fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola Wako.'** iliteremka siku yaGhadir Khum ikimuhusu Ali bin Abu Talib (as)."

**Tafsirul-Kabir ya Fakhru Razi, mwishoni mwa tafsiri ya kauli yake Mtukufu: 'Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola Wako.' iliyoko katika Sura al-Maidah:**

Amesema: Kumi –yaani katika sababu za kuteremka Aya hii zilizotajwa na wafasiri: Aya hii imeteremka kueleza fadhila za Ali bin Abu Talib (as), na iliposhuka aya hii alishika mkono wake na kusema: "Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake. Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda na mfanyie uadui mwenye kumfanyia uadui." Na alipokutana na Umar alisema: "Hongera ewe mtoto wa Abu Talib, sasa umekuwa mtawala wangu na mtawala wa kila muumini mwanaume na muumini mwanamke." – Amesema: Nayo ni kauli ya Ibn Abbas, al-Barau bin Azib na Muhammad bin Ali (as).

**Nasema:** Kauli yake: "Nayo ni kauli ya Ibn Abbas, al-Barau bin Azib na Muhammad bin Ali (as)." Yaani Aya hii kuteremka kwa sababu ya kuelezea fadhila za Ali (as) ndio kauli ya Ibn Abbas, al-Barau bin Azib na Muhammad bin Ali (as).

## MLANGO UNAOSEMA KUWA AYA: "LEO NIMEKUKAMILISHIENI DINI YENU" ILITEREMKA SIKU YA GHADIR KHUM

**Ad-Durul-Manthur cha As-Suyutiy, mwishoni mwa tafsiri ya kauli yake Mtukufu: 'Leo nimewakamilishieni dini yenu.' Iliyoko katika Sura al-Maidah:**

Ametaja kutoka kwa Ibn Mardawayhi na Ibn Asakir, wote hao wamepokea kutoka kwa Abi Said al-Khidriy amesema: "Wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipomsimika Ali siku ya Ghadir Khumna kumtangaza kuwa mtawala, Jibril alimshukia na Aya hii:**'Leo nimewakamilishieni dini yenu.'**"

**Ad-Durul-Manthur cha As-Suyutiy, mwishoni mwa tafsiri ya kauli yake Mtukufu: 'Leo nimewakamilishieni dini yenu.' Iliyoko katika Sura al-Maidah:**

Ametaja kutoka kwa Ibn Mardawayhi na al-Khatib na Ibn Asakir, wote wamepokea kutoka kwa Abu Huraira, amesema: "Ilipofika siku ya Ghadir Khum nayo ni siku ya kumi na nane katika mwezi wa Dhulhija (mfunguo tatu) Mtume (saww) alisema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.' Hapo Mwenyezi Mungu akateremsha Aya:**'Leo nimewakamilishieni dini yenu.'**"

**Taarikh Baghdad chaal-Khatib al-Baghdadiy Juz. 8, uk. 290:**

Amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abu Huraira amesema:"Yeyote atakayefunga siku ya kumi na nane ya Dhulhija (mfunguo tatu) ataandikiwa malipo ya funga ya miezi sitini, nayo ni siku ya Ghadir Khum pale, Mtume (saww) aliposhika mkono wa Ali bin Abu Talib (as) na akasema: 'Je mimi si ni mtawala wa Waumini?' Wakajibu: 'Ndiyo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Akasema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.' Umar bin Khattab akasema: 'Hongera, hongera ewe mtoto wa Abu Talib, sasa umekuwa mtawala wangu na mtawala wa kila Mwislamu.' Na ndipo Mwenyezi Mungu akateremsha: **'Leo nimekukamilishieni dini yenu.'"**

**Nasema:** Na amepiokea al-Khatib kwa njia nyingine mfano wa hii.

## MLANGO UNAOELEZA KUWA ADHABU ILIMTEREMKIA HARITH BIN NUUMAN PALE ALIPOKANUSHA MTUME (SAWW) KUMSIMIKA ALI (AS) SIKU YA GHADIR KHUM

**Nurul-Absar cha Shabalanjiy Uk. 71:**

Amesema: Imam Abu Is'haqa Tha'alabiy amenukuu katika *Tafsiir* yake kwamba Sufiyan bin Uyaynah aliulizwa kuhusu kauli yake Mtukufu: **"Muulizaji aliuliza juu ya adhabu itakayotokea"** iliteremka kwa sababu ya nani? Akamjibu mwenye kuuliza: "Hakika umeniuliza mas'ala ambayo hajaniuliza yeyote kabla yako. Amenihadithia baba yangu kutoka kwa Ja'far bin Muhammad, kutoka kwa baba zake (as) kwamba Mtume wa Mwenyezi (saww) alipokuwaGhadir Khum aliwaita watu nao wakakusanyika, akashika mkono wa Ali (as) na kusema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.' Habari zikaenea na kufika mpaka mjini na zikamfikia al-Harith bin Nuuman al-Fihriy. Akaja mpaka kwa Mtume wa Mwenyezi (saww) akiwa juu ya ngamia wake, alipofika akamuinamisha na akateremka na kusema: 'Ewe Muhammad! Kuhusu Mwenyezi Mungu Mtukufu umetuamrisha tushahidilie kwamba hakuna mungu apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, na kwamba hakika wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, tumekukubalia. Na umetuamrisha tuswali Swala tano, tumekukubalia. Na umetuamrisha kutoa Zaka, tumekubali. Na umetuamrisha tufunge Ramadhani, tumekubali. Na umetuamrisha kuhiji, tumekubali. Kisha bado haujaridhika kwa haya mpaka umenyanyua mkono wa mtoto wa ami yako na kumfanya bora juu yetu kwa kusema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.' Je jambo hili ni kutoka kwako au ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu?'

"Mtume (saww) akasema: 'Naapa kwa Yule ambaye hapana mungu apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye, hakika hili ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.'Al-Harith bin Nuumanakageuka na kuondoka huku akisema: 'Ewe MunguWangu ikiwa anayoyasema Muhammad ni kweli basi tuteremshie mvua ya mawe kutoka mbinguni au tuletee adhabu kali.'Kabla hajafika kwenye kipando chake, Mwenyezi Mungu Mtukufu akawa amemrushia jiwe ambalo lilitua juu ya kichwa chake na likatokea kwenye tundu lake la nyuma na kumuuwa, na Mwenyezi Mungu Mtukufu akateremsha:**'Muulizaji aliuliza juu ya adhabu itakayotokea. Kwa makafiri ambayo hapana awezaye kuizuia. Kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mwenye mbingu za daraja.'**"

**Nasema:** Ameitaja al-Munawi katika *Faydhul-Qadir* Juz. 6, uk. 217, na humoSufiyan hajasema: "Amenihadithia baba yangu kutoka kwa Ja'far bin Muhammad (as)."

# MLANGO UNAOSEMA KUWA HADITH YA GHADIR KHUM NI DALILI INAYOTHIBITISHA UKHALIFA WA ALI (AS) BAADA TU YA MTUKUFU MTUME (SAWW)

**Nasema:** Hakika hadithi ya Ghadir Khum ambayo tumetaja njia zake kadhaa katika Mlango unaozungumzia kauli ya Mtume (saww) kwa Ali (as): "Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake." Yenyewe ni miongoni mwa dalili za Mashia zenye nguvu zaidi na zilizobayanazaidikatika kuthibitisha ukhalifa wa Ali (as) na Uimamu wake baada tu ya Mtume (saww), na ili kuiwasilishakama dalili inahitaji kutaja mambo mawili: Sanadina hoja yake.

**Ama sanadi:** Hakika yenyewe ipo katika daraja ya juu kabisa ya usahihi na ubora, kwani hiyo ni hadithi mutawatiri (yenye wapokezi wengi) iliyopokewa na Maswahaba watukufu na wakubwa, miongoni mwao ni Ali (as), Ammar, Umar, Saad, Talha, Zayd bin Arqam, Barau bin Azib, Abu Ayub, Buraidah al-Aslamiy, Abu Said al-Khudriy, Abu Hurayra, Anas bin Maliki, hudhayfah bin Asid, Jabir bin Abdullah, Jabir bin Samrah, Ibn Abbas, Ibn Umar, Aamir bin Layla, habashiy bin Junadah, Jarir al-Bajaliy, Qaysu bin Thabit, Sahal bin Hanayfu, Khuzaymah bin Thabit, Ubaydullah Ibn Thabit Al-Ansariy, Thabit bin Wadiah Al-Ansariy, Abu Fadhalah Al-Ansariy, Ubaydu bin Azib Al-Ansariy, Nuuman bin Ajalan Al-Ansariy, habib bin Badil, Hashim bin Utbah, Habah bin Juwayn, Ya'ala bin Murah, Yazid bin Sharahil Al-Ansariy, Najiyah bin Amru al-Khuzaiy, Aamir bin Umayru, Ayman bin Nabil, Abu Zaynab, Abdur-Rahman bin Abdi Rabi, Abdur-Rahman bin Mudliju, Abu Qudamah Al-Ansariy, Abu Junaydah Junduu bin Amru bin Mazin, Abu Amrah bin Muhswin, Maliki bin Huwayrith, Ammarah, Amru Dhiy Mur, na wasiokuwa wao miongoni mwa watu wengi waliopokea hadithi ya Ghadir, nami nimeshindwa kuwataja majina yao kutokana na haraka.

Ibn Hajar katika *Tahdhibut-Tahdhib*Juz. 7, uk. 337 ametaja majina ya kundi la Maswahaba waliopokea hadithi ya Ghadir, kisha amesema katika uk. 329: "Na Ibn Jarir Tabariameikusanya hadithi inayozungumzia utawalishaji katika kitabu ambacho humo mna majina mengi ya aliowataja, na amesema ni hadithi sahihi." Kisha akasema: "Abu Abbas bin Uqdah amejikita katika kukusanya njia zake zote na hivyo akaiandika kutoka katika hadithi zaMaswahaba sabini au zaidi."

Na amesemakatika *Fat'hul-Bari*Juz. 8, uk. 76: "Na ama hadithi:'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.' Ameiandika Tirmidhiy na an-Nasaiy kwa njia nyingi sana, na amezikusanya njia hizo Ibn Uqdah katika kitabu *Mufrad*, na sanadi zake nyingi ni sahihi na nzuri.

Na al-Qunduziy katika kitabu chake Yanabiul-Mawaddah katika mlango wa nne ameitaja, amesema: "Na katika *al-Manaqib*, Muhammad bin Jarir Tabari mwandishi wa kitabu *Taarikh*, ameiandika habari ya Ghadir Khum kutoka katika njia sabini na tano, na ameitengea kitabu alichokiita '*Kitabu cha utawala*.'" Kisha akasema tena: "Abu Abbas Ahmad bin Muhammad bin Said bin Uqdah ameiandika habari ya Ghadir Khum, naameitengea kitabu alichokiita '*Kitabu cha utawalishaji*.' Ameitaja kutoka katika njiamia moja na tano." Kisha akasema: "Na amehadithia kuwa Allamah Ali bin Musa Ibn Ali bin Muhammad Abi Maaliy Juwayniy anayeitwa Imam wa Haram mbili – ambaye ni Ustadh Abi Hamid Ghazali - ameshangaa na kusema: 'Niliuona mjalada huko Baghdad ukiwa mkononi mwa Sahafundani yake mlikuwa na riwaya za Ghadir Khum, juu yake umeandikwa: Mjalada wa ishirini na nane wa njia za kauli yake (saww): Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake. Na unafuatiwa na Mjalada wa ishirini na tisa.

**Ama kuhusu hoja yake:** Nayo pia ipo katika daraja ya juu kabisa ya uthibitisho, hiyo ni baada ya kuchunguza vielelezo vilivyopo vya kimazingira na kimatamko. Hakika tamko neno '*Mawla*' katika lugha ya Kiarabu lina maana nyingi, kama vile mmililki, mtumwa, bwana, huria, mpenzi, jirani, mshirika na jamaa,

na katika maana hizo ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **“Na hakika mimi nawakhofia jamaa zangu baada yangu.”** Imesemekana kuwa wameitwa hivyo kwa sababu wao wanamfuata katika nasaba hivyo Walii ni ndugu. Na miongoni mwa maana zake ni mlinzi, imesemekana nayo ndiyo maana ya kauli yaMwenyezi Mungu Mtukufu: **“Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa walioamini. Na makafiri hawana mlinzi.”** Na pia ni rafiki, imesemekana nayo ndiyo maana ya kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **“Siku ambayo rafiki hatamfaa rafiki yake kwa chochote, wala hawatanusuriwa.”** Yaani rafiki hatamfaa rafiki. Pia humaanisha mrithi, nayo ndio maana ya kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **“Na kila mmoja tumemwekea warithi katika waliyoyaacha wazazi wawili na jamaa.”** Yaani warithi, na maana nyinginezo.

Na kati ya maana zake zilizokamili, mashuhuri zaidi na bayana zaidi ni mwenye mamlaka kwa mtu kuliko hata aliyonayo juu yake mwenyewe, *Mawla* kwa maana hii hutumika kwa kila aliyejuu mwenye cheo kikubwa ambaye amri yake hutiiwana maamuzi yake hutekelezwa. Hivyo utamwambia: ‘Wewe ni mwenye mamlaka kwangu kuliko hata niliyonayo juu ya nafsi yangu mwenyewe.’ Bali pia maana hii hutumikakumaanisha mwenye kumiliki mtumwa, kwani yeye ni mwenye mamlaka zaidi kwa mtumwa wake kuliko hata aliyonayo mtumwa juu yake mwenyewe, kwani bwana wake ndiye mwenye maamuzi katika mambo yake na kazi zake, na mtumwa ni mwenye kumtegemea yeye hawezi kufanya lolote. Na kuanzia hapa inasihi kusemwa: “Hakika neno ‘Mmiliki wa mtumwa’si maana nyingine yenye kujitegemea ya tamko ‘*Mawla*’, iliyo mkabala na ‘Mwenye mamlaka kwa mtu kuliko hata aliyonayo juu yake mwenyewe.’ Bali ni moja kati ya mifano yake halisi, na mifano yote miwili inakusanywa pamoja na ‘*Mawla*’, kama tulivyoashiria kuwa humaanisha kila aliyejuu mwenye cheo

kikubwa ambaye amri yake hutiiwa na maamuzi yake hutekelezwa. Hivyo kila ambaye yuko hivyohuwa ni *Mawla*kwa yule aliyechini yake, yaani ni mwenye mamlaka kwake kuliko hata aliyonayo juu yake mwenyewe, sawa mtu huyo awe ni mwenye kummiliki kama mtumwa wake kiasi kwamba akitaka kumuuza humuuza au la asiwe hivyo.

Kwa ujumla ni kuwa *Umawla* uliopo katika kauli ya Mtume (saww): “Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.”Haumaanishi maana nyingine isipokuwa ‘Mwenye mamlaka kwao kushinda hata waliyonayo juu yao wenyewe.” Kwa ibara nyingine ni Uimamu na uongozi, hayo yote ni kwa ushahidi wa viashiria yakinifu.

Miongoni mwa viashiria hivyo ni kauli yake (saww): “Je mimi si ni nina mamlaka zaidi kwa waumini kuliko hata waliyonayo juu ya nafsi zao wenyewe?” Baada ya Maswahaba zake kujibu: “Ndiyo” akasema: “Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.” Hiyo ni dalili bayana kuwa maana ya *Mawla* hapa ni kule kuwa na mamlaka zaidi kwao kuliko hata waliyonayo juu yao wenyewe. La sivyo kauli yake: “Je mimi si ni nina mamlaka zaidi kwa waumini kuliko hata waliyonayo juu ya nafsi zao wenyewe?” itakuwa ni upuuzi sana. Hiyo ni achilia mbali kwamba katika mapokezi mengi ya hadithi hii kumehusishwa herufi *Fau*iliyo wazi, mfano ni kauli yake: “Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ndiye mtawala wake.” Na hii (basi) inaonesha bayana uhusiano uliopo kati mafungu mawili ya sentensi, la kwaza la na la pili.

Pia miongoni mwa viashiria hivyo ni kauli yake (saww) iliyopo katika baadhi ya mapokezi yake kama ilivyotangulia: “Hakika Mwenyezi Mungu ni mtawala Wangu na mimi ni mtawala wa waumini, nina mamlaka zaidi kwao kuliko hata waliyonayo juu ya nafsi zao wenyewe, hivyo yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi huyu –yaani Ali - ndiye mtawala wake.” Akayafanya (saww) maneno “Nina mamlaka zaidi kwao kuliko hata waliyonayo juu ya nafsi zao wenyewe” kuwa ufafanuzi na tafsiri ya kauli yake: “Na mimi ni mtawala wa waumini.” Na hii pia ni dalili bayana kuwa maana ya neno *Mawla* hapa ni yeye kuwa na mamlaka zaidi kwao kuliko hata waliyonayo juu ya nafsi zao wenyewe.

Pia miongoni mwa viashiria hivyo ni kutamka kwake bayana: “Ni mwenye mamlaka kwake kuliko hata aliyonayo juu ya nafsi yake mwenyewe.” Kama ilivyo katika baadhi ya mapokezi ya hadithi hii, kama ilivyotangulia katika hadithi ya *Kanzul-Ummal* na al-Haythamiy ambayo ilianza kwa: Hakika mimi sijamkuta Nabii isipokuwa - mpaka aliposema: Kisha akaushika mkono wa Ali (as) na kusema: “Yeyote ambaye mimi ni mwenye mamlaka kwake kuliko hata aliyonayo juu ya nafsi yake mwenyewe basi Ali ndiye mtawala wake.” Kwa hakika nayo hiyo ni dalili bayana kuwa maana ya *Mawla* katika njia nyingine za hadithi zisizokuwa hii ni kuwa yeye ni mwenye mamlaka zaidi kwake kuliko hata aliyonayo juu ya nafsi yake mwenyewe, kwani hakika hadithi moja hufasiri nyingine.

Pia miongoni mwa viashiria hivyo ni kauli yake inayopatikana katika baadhi ya njia zake zilizojumuisha hadithi ya vizito viwili: “Hakuna Nabii yeyote isipokuwa aliishi nusu ya umri wa Nabii wa kabla yake. Hakika mimi sijamkuta Nabii isipokuwa alipewa nusu ya umri wa Nabii aliyekuwa kabla yake. Na mimi ninakaribia kuitwa na kuitikia wito, hakika mimi ni mwenye kuulizwa na ninyi ni wenye kuulizwa, basi mtasema nini?”

Hakika hii yote ni dalili yenye nguvu inayoonesha kwamba yeye (saww) hakuwa katika lengo lolote isipokuwa katika nafasi ya kumsimika Wasia na Khalifa na kumuainisha Imam wa baada yake ili watu wamfuate yeye, waongoke kwa muongozo wake na wafuate athari zake, na wala asiwaache holela pasipo na kiongozi yeyote huku wakimfuata kila mchungaji. Wala lengo lake haikuwa kubainisha kuwa yeyote ambaye mimi ni kipenzi chake au mlinzi wake au mfano wa hayo miongoni mwa maana za *walii*, basi Ali ni kipenzi chake au mlinzi wake. Kwani hakika kukusudia maana mfano wa hizi ni jambo lisilohitajikutajwakaribu na kifochake na karibu na muda wa kifo chake (saww), na kwamba hakika yeye anakaribia kuitwa na kuitikia wito, na mengineyo kama hayo.

Pia miongoni mwa viashiria hivyo ni kitendo cha Mtume (saww) na yote aliyoyafanya siku ile -yaani siku ya Ghadir Khum, hata ukiachilia mbali kiashiria cha kimatamshi -navyo ni dalili yenye nguvu na ushahidi mkubwa zaidi wenye kuonesha kwamba yeye (saww) alikuwa katika lengo la kumsimikaImam na Khalifa baada yake, na kwamba makusudio ya *Mawla* ni mwenye mamlaka zaidi kwao kuliko hata waliyonayo juu ya nafsi zao wenyewe, wala si maana nyingine.

Ufafanuzi wake ni kwamba sisi tutakapozingatia mazingira yaliyokuwepo alipoteremka katika sehemu ile baada ya kutoka katika Hijja yake, ni kwamba ilikuwa ni siku ya joto kali ambayo haijawahi kumtokea yeye wala Maswahaba zake siku yenye joto kali kuliko siku ile, - kama ilivyotangulia katika baadhi ya riwaya za al-Hakim kutoka kwa Zayd bin Arqam – pia ni kule kuwasimamisha kwake watu mpaka akawarudisha waliokuwa wamemtangulia na akawangojea waliokuwa nyuma, - kama ilivyotangulia katika baadhi ya riwaya za an-Nasaiy kutoka kwa Saad - mpaka watu wote wakakusanyika kwake, akaamrisha kufagiliwe chiniya miti mikubwa. Kukafagiliwa na kunyunyuziwa maji na akatengenezewa kivuli kwa kutumia nguo, – kama ilivyo katika riwaya nyingi za Zayd - kisha akamfunga Ali (as) kilemba kwa mtindo wanaofunga Malaika, - kama tulivyotaja habari zake huko nyuma katika mlango wenye kujitegemea - kisha akamshika mkono Ali (as) - baada ya kuwahutubia watu na kuwaeleza kuwa mauti yake na muda wa kifo chake umekaribia - akamnyanyua Ali kiasi ambacho mpokezi akaweza kuona kwapa zao - kama ilivyotangulia katika baadhi ya riwaya za Ibn Hajar katika *Al-Isabah* kutoka kwa Habah bin Juwayn - kisha ikateremka:**“Leo nimekukamilishieni dini yenu.”** Bali kabla yake iliteremka: “Ewe Mtume fikisha yaleuliyoteremshiwa kutoka kwa Mola Wako.” - kama ulivyosoma katika milango iliyozungumzia Aya hizo punde tu – tukichunguza yote hayo tutaona kwamba yote hayo hayakuwa na maana nyingine isipokuwa ni kumsimika Wasii na Khalifa wa Mtume (saww), na kwamba hakika yeye (saww) alikuwa katika zoezi la kumuainisha Imam baada yake na kuwafahamisha watu kwamba kiongozi wao ni Ali (as), na sio kwambayeyote ambaye mimi ni kipenzi chake au mlinzi wake basi Ali ni kipenzi chake na mlinzi wake.

Na pia miongoni mwa yanayotilia nguvu hilo ni kauli ya Abu Bakr na Umar kwa Ali (as): "Ewe mtoto wa Abu Talib, umekuwa mtawala wa kila muumini mwanamume na kila muumini mwanamke." Au kauli ya Umar: "Hongerahongera ewe mtoto wa Abu Talib, sasa umekuwa mtawala wangu na mtawala wa kila mwislamu." Au "Hongera hongera ewe mtoto wa Abu Talib, sasa umekuwa mtawala wangu na mtawala wa kila muumini wa kiume na kila muumini wa kike."

Hakika lau Mtume (saww) kwa kitendo chake kile na kwa kauli yake kwa Ali (as) asingekuwa amemwanzishia kipya ambacho kabla ya hapo hakikuwa kimethibiti kwake, basi Abu Bakr na Umar wasingemwambia Ali (as): "Sasa umekuwa mtawala wa kila muumini wa kiume na kila muumini wa kike."Na mfano wa hayo, kwanihakika ibara mfano wa hizi hazisemwi isipokuwa pale panapopatikana cheo na tukio jipya, kwani kabla ya hapo tayari Ali (as) alikuwa ni kipenzi kwa yule ambaye Mtume (saww) alikuwa ana mapenzi naye, au mlinzi kwa yule ambaye Mtume (saww) alikuwa ni mlinzi wake, na yote haya yapo wazi hayahitaji kuzidi kubainisha.

Kama ambavyo pia kukanusha kwa Harith bin Nuuman al-Fahriy kwa kusema:"Hakika umetuamrisha kadha wa kadha tumekubali. Kisha bado haujaridhika kwa haya mpaka umenyanyua mkono wa mtoto wa ami yako na kumfanya bora juu yetu." Nako kunatilia nguvu kwamba Mtume (saww) kwa kitendo chake pale na kauli yake hiyo alimteua Ali kuwa Khalifa, na akamuainisha kuwa Imam wa watu baada yake, na kitendo hicho hakikumridhisha Harith bin Nuuman hivyo akamshutumu Mtume (saww), naye akamjibu kwamba uteuzi ule ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na hapo Harith akaona hana budi ila ajiombee mwenyewe dua baya. Akajiombea na adhabu ikashuka kwake na Mwenyezi Mungu akamhilikisha. Lau ingekuwa makusudio ya Mtume (saww) ni kuwafikishia watu kwamba yeyote ambaye mimi ni kipenzi au mlinzi wake au mfano wa hayo basi Ali ni kama hivyo, jambo hilo lisingekuwa na umuhimu kwa daraja hili kiasi kwamba Harith asiweze kuridhishwa nalo na afikie hatua ya kujiombea dua mbaya na Mwenyezi Mungu amhilikishe.

Wanazuoni wa Kisunni wamejaribu kutoa hoja dhaifu ili kupinga kuwa Hadith ya Ghadir Khum ni dalili tosha juu ya ukhalifa wa moja kwa moja wa Ali (as) baada ya Mtume (saww).

Miongoni mwa hoja hizo ni: Hakika hakuna hata mmoja kati ya wanazuoni wa lughaya Kiarabu aliyewahi kusema kwamba *Maf'ala* huja kwa maana ya *Af'ala*, yaani neno *Mawla* kuja katika maana ya *Awla*.

**Jibu lake ni:** Nikana kwamba wao hawakusikia yale waliyoyasema wafasiri katika kauli ya Mwenyezi Munguiliyopo katika Sura Al-Hadid: **"Makaazi yenu ni Motoni, ndio bora kwenu."** Wanazuoni wa Sunni na Shia kama al-Kashaf, Jalalayn, Baydhawiy, Abi Suud, Tabarasiy, Tibyan na wengineo, wao wametaja tafsiri ya Aya hiyo kwa maana ya ndio bora kwenu, yaani ndiyo yanayostahili kwenu.

Na Akhtal anamsifu Abdul-Maliki bin Marwankwa kusema:

> "Makuraishi hawakupatamtu mwenye kufaa na mwenye kutosha katika jambo lao na mtukufu kushinda baba yako. Ushujaa wake haukuwa na mfano, na lau asingekuwa yeye basi watu wangezidi kutofautiana. Hivyo akawa mwenye mamlaka kwa watu wote, na mwenye kustahiki zaidi kuogopwa na kusifiwa kushinda Makuraishi wote."

Hivyo kamzungumzia kwa kutumia tamko *Mawla* – Khalifa ambaye amri yake ni yenye kutiiwa - kwa kumaanisha maana aliyokusudia. Na Akhtal ni mmoja wa malenga wa Kiarabu na ni miongoni mwa wasiotuhumiwa kwa maarifa, na si mwenye kuegemea kwenye madhehebu yoyote ya Kiislamu, bali yeye ni katika vinara wa lugha ya Kiarabu.

Na kadhalika Abu Ubayidah Maamaru Ibn al-Muthana ambaye yeye ni katika wanaotangulizwa mbele katika elimu ya lugha ya Kiarabu, na si mwenye kutuhumiwa katika kuijua kwake, ametaja maneno ya-

fuatayo katika kitabu chake kilichojumuisha *Tafsiru Gharibul-Qur'an* iliyo maarufu kwa jina la *al-Majaz* Juz. 2, uk. 254, katika tafsiri ya Aya iliyotajwa hapo juu: "*Hiya Mawlakum*: Yaani bora kwenu." Na akatolea ushahidi kupitia kauli ya Labid iliyopo katika *mualaqat* wake mashuhuri: "Kila upande kati ya pinde mbili ukawa unadhani kuwa wenyewe ndio unastahiki kuogopwa mbele yake na nyuma yake."

Katika sentensi hii: "Unastahiki kuogopwa" anakusudia kuwa mnyama huyu alichanganyikiwa akawa hatambui ni nyuma yake au ni mbele yake. Hakika huyu Abu Ubaydah Muhammad bin al-Muthana si mwenye kutuhumiwa kwa mapungufu katika elimu ya lugha ya Kiarabu na wala si mwenye kudhaniwa miongoni mwa wenye kuegemea kwa Amirul-Muuminina Ali (as) bali yeye anahesabiwa ni miongoni mwaMakhawariji.

Ibn Qutaybah Daynuriy katika *Gharibul-Qur'an Wamushkiluhu* Juz. 3, uk. 164 anasema hivi: "*Maawakum naru hiya mawlakum*, yaani ndipo mnapostahili." Kisha akatolea ushahidi kutumia kauli ya Labid iliyotajwa. Na imekuja katika *Sharhu Mualaqat Labid* cha Zawzaniy uk. 106 chapa ya Beirut ya mwaka 1377 Hijriyyahsawa na mwaka 1958 Miladiyyah, katika kufafanua maelezo haya amesema:"Tha'lab amesema: 'Hakika neno *Mawla* katika ubeti huu ina maana ya mwenye haki zaidi na kitu, kama kauli yake Mtukufu: *Maawakum naru hiya mawlakum*, yaani ndio stahili yenu.'"

Kadhalika imekuja katika *Sahih Bukhari* kuwa tafsiri ya *Hiya Mawlakum* ni stahili yenu, kama alivyoitaja Ibn Hajar al-Asqalaniy katika *Fat'hul-BariSharhul-Bukhar* Juz. 8, uk. 482, na amesema: "Na hivyo ndivyo alivyosema Abu Ubaydah." Na katika baadhi ya nakala za *Bukhari*:"Ndio stahili yenu, na hayondio maneno ya Abu Ubaydah."

Na kadhalika imepokewa kutoka kwa Abu Bakr Muhammad bin Qasim Anbariy katika kitabu chake maarufukwa jina la*Tafsirul-Mushkili Fil-Qur'an*, anapotajaaina za *Mawla* anasema:"Hakika *Mawla* ni Walii, na pia *Mawla* ni mwenye haki zaidi na kitu." Na akatolea ushahidimaana hiyo kupitia Aya iliyotajwa na pia ubeti wa Labid:"*Walikuwa ni wenye kustahiki haki wakaitafuta mpaka wakaipata na wala hawakulegalega wala kuchoka.*"

Na Fakhru Razi ametaja kutoka kwa Kalbiy, Zujaj, Farau na Abi Ubaydah kwamba wao wameifasiri aya hii kwa maana ya panapowastahili.

Zaidi ya hapo ni kwamba hata kama pasingekuwepo na Aya wala riwaya wala mtaalamu wa lugha ya Kiarabualiyetamka bayana kuwa *Mawla* imekuja kwa maana mwenye haki zaidi ispokuwa tu kauli ya Mtume (saww): "Je mimi si ni mwenye mamlaka zaidi kwa waumini kuliko hata waliyonayo juu ya nafsi zao wenyewe? Wakasema: Ndiyo. Akasema: Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake." Au kauli yake (saww): "Hakika Mwenyezi Mungu ni mtawala wangu na mimi ni mtaala wa waumini, na mimi nina mamlaka zaidi kwao kuliko hata waliyonayo juu ya nafsi zao wenyewe. Hivyo, yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake." ingetosha kuwa dalili inayothibitisha kuwa neno *Mawla* limekuja kwa maana ya mwenye kustahiki zaidi, kwani hakika makusudio ya hadithi hizo mbili si jingine isipokuwa maana hiyo. Hiyo ni kutokana na kiashiria ambacho ni kauli yake (saww): "Je mimi si ni mwenye mamlaka zaidi.." Na kauli yake: "Na mimi nina mamlaka zaidi kwao."

Na miongoni mwa hoja hizo ni: Hakika *Mawla* ingekuwa inamaanisha mwenye haki zaidi basi ingefaa kutumika kila moja wapo sehemu ya mwenzie, na hivyo ingesihi kauli ya mwenye kusema: "*Hadha Mawla Bizayd*" badala ya kauli yake: "*Awla Bizayd*" au "*Awla Zayd*" badala ya kauli yake: "*Mawla Zayd*." Na lililo wazi ni kuwa hilo halisihi.

**Jibu lake ni:** Hakika *Mawla* humaanisha mwenye haki zaidi pale inapoambatana na herufi *Bau*, na lililo wazi ni kwamba hapo husihi kutumika kila mojawapo sehemu pa mwenzie, hivyo utasema: "*Hadha*

*Mawla Bizayd*" yaani "*Awla Bizayd.*" Au utasema: "*Hadha Awla Bizayd*" yaani "*Mawla Zayd*." Ndiyo neno *Awla* wakati mwinginehutumika kwa maana ya mwenye mamlaka zaidi kwake kuliko hata aliyonayo juu ya nafsi yake. Kama ilivyotangulia katika kauli yake (saww):"Je mimi si ni mwenye mamlaka zaidi kwa waumini kuliko hata waliyonayo juu ya nafsi zao wenyewe?" Na wakati mwingine hutumika kwa maana ya mwenye haki zaidi kuliko mwingine, kama ilivyo katika kauli yake Mtukufu:**"Hakika watu wenye haki zaidi na Ibrahim ni wale waliomfuata yeye"** yaani watu wenye hakizaidi naye kuliko wengine ni wale waliomfuata. Au kama ilivyo katika kauli yake (saww): "Mwenye haki zaidi na maiti ni yule mwenye haki zaidi ya kumrithi."Yaani mwenye haki zaidi kati yao na mwenye kufaa zaidi kati yao ni yule mwenye haki zaidi ya kumrithi. Hivyo maana ya mwanzo huzingatia cheo na daraja kubwa, lakini maana ya pili haizingatii hilo bali hutumika hata kwa wenye kulingana cheo au hata kwa walio chini zaidi kicheo.

Na pia miongoni mwa hoja hizo ni: Hakika kama neno *Mawla* lililopo katika kauli ya Mtume (saww): "Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake." Tutalitafsiri kwa maana ya mwenye mamlaka zaidi kwao kuliko hata waliyonayo juu ya nafsi zao wenyewe na si kwa maana ya msaidizi au kipenzi au mfano wa hayo, basi hilo litaleta uharibifu mkubwa, fedheha ya uhasama na dosari kubwa kwa Maswahaba wengi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) miongoni mwa Muhajirina na Ansari.

**Jibu lake ni:** Hakika kukosea Maswahaba wengi katika jambo makhususi si jambo lisilokubalika kiakili, na hakika madai ya kwamba watu wote walikongamana katika kumpa kiapo cha utiiAbu Bakr, na kwamba hakika yeye Mtume (saww) alisema: "Hakika ummah wangu hauwezi kukongamana katika kosa."Madai yote ya kwanza na ya pili hayakubaliki.

Ama dai la kwanza ni kwa kuwa Ijmai haikutimia, kama tutakavyoona hilo katika muhtasari wa maneno ya Ibn Qutaybah, ama ufafanuzi wake unahitaji kurejea vitabu vikubwa vya historia.

Ama madai ya pili ni kwa kuwa usemi huo:"Hakika ummah wangu hauwezi kukongamana katika kosa." Si hadithi inayokubalika na makundi yote mawili, yaani Sunni na Shia, ili usihi kuwa dalili wakati wa mjadala, bali wenyewe ni hadithi iliyozushwa ya uwongo aliyoiweka muwekaji kwa lengo la kuhalalisha yale waliyoyatenda Maswahaba wengi baada ya Mtume (saww). Hakika yalitokea mambo makubwa zaidi katika ummah wa Musa (as) wakati wa uhai wake kabla ya kufa kwake, kushinda yale yaliyotokea katika ummah wetu baada ya kufa kwa Mtume wetu (saww). Hakika baada ya Musa (as) kuwalingania watu wake katika tawhid (kumpwekesha Mwenyezi Mungu) kwa muda mrefu kwa kuwatolea miujiza ya mkono mweupe na fimbo ambayo kwayo alipasua bahari na kuyameza yote yaliyotendwa na wachawi, baada ya miujiza hiyo na aina nyingine za miujiza mfano wa hiyo, walimwaminiMwenyezi Mungu, wakamwabudu na kumpwekesha, kisha aliwaacha kwa muda mdogo kwa ajili ya kwenda kuzungumza na Mola Wake na akawaachia Harunambaye ni ndugu wa Musa (as) na mshirika wake katika unabii kwa muktadha wa kauli yaMwenyezi Mungu:**"Na tukampa yeye katika neema zetu ndugu yake Harun kuwa ni Nabii."**

Na Musa (as) alikuwa ameshawaamrisha wamtii Harun (as) na watende atakayowaagiza. Alipotoweka Musa (as), walikongomana katikakumkhalifu Harun (as) isipokuwa wachache miongoni mwao, na wakakaribia kumuuwa. Walimuacha Harun (as) na wakamchukua ndama na kumwabudu kwa kumshirikisha Mwenyezi Mungu Mtukufu. Yote haya waliyafanya kwa kupotezwa na Samiriy. Ikiwa iliwezekana kwa ummah wa Musa (as) kukongamana katika kumfanya ndamakuwa Mungukwa kumshirikisha Mwenyezi Mungu Mtukufu na kumuacha Harun baada yakukaribia kumuuwa, bila shaka inawezekana pia kwa Maswahaba wengi kufanya kosa la kumfanyaAbu Bakr Khalifa na kumuacha Ali (as) Wasii wa Mtume (saww) baada ya kukaribia kumuuwa kama alivyotaja hilo Ibn Qutaybah katika *al-Imamah Was-Siyasah* katika kisa cha kumpa kiapo cha utii Ali (as).

Amesema: "Na hakikaAbu Bakr aliwatafuta watu ambao hawakutoa kiapo cha utii kwake, akamtuma Umar kwa Ali (as) akaja akawaita - walikuwa nyumbani kwa Ali (as) - wakakataa kutoka hivyo akaamrisha kuni ziletwena akasema: 'Naapa kwa yule ambaye nafsi ya Umar imo mikononi mwake, ni lazima mtoke laa sivyo nitaichoma moto pamoja na waliomo humo.' Akaambiwa: 'Ewe baba Hafsa, hakika humo (ndani ya nyumba) yumo Fatimah.' Akasema:'Hata akiwemo.' Wakatoka na kutoa kiapo cha utii isipokuwa Ali."

Ameendelea kusimulia mpaka aliposema: "Umar akamwendea Abu Bakr na kumwambia: 'Je hauchukui kwa nguvu kiapo cha utii kutoka kwa huyu aliyekupinga? - Ameendelea kusimulia mpaka aliposema: Kisha Umar akasimama na kwenda akiwa pamoja na kundi la watu, mpaka walipofika mlangoni kwa Fatimah (as) wakagonga mlango, Fatimah aliposikia sauti zao akanadi kwa sauti ya juu: 'Ewe baba yangu Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mangapi yanatukuta baada yako kutoka kwa mtoto wa Khattab na mtoto wa Abu Quhafa!' Jamaa waliposikia sauti yake na kilio chake wakaondoka huku wakilia na nyoyo zao zikihofu na vifua vyao vikikaribia kupasuka. Lakini Umar akiwa na watu kadhaa walibaki na wakamtoa Ali (as) na kumpeleka kwa Abu Bakr, wakamwambia: 'Mpe kiapo cha utii.' Akasema: 'Ikiwa sintofanya hilo basi kipi kitatokea?' Wakasema: "Wallahi tunaapa kwa kwa Mwenyezi Mungu ambaye hakuna Mungu isipokuwa Yeye, tutakata shingo yako.' Akasema: 'Kwa hiyo mtamuuwa mja wa Mwenyezi Mungu na ndugu wa Mtume Wake.' Umar akasema: 'Ama mja wa Mwenyezi Mungu ni sawa, na ama kuhusu ndugu wa Mtume Wake hapana.' Wakati wote huo, Abu Bakr alikuwa kimya hazungumzi chochote, ndipo Umar akamwambia: 'Je una amri yoyote kuhusu yeye?'Akasema:'Simchukii kwa chochote maadamuFatimah yupo upande wake.' Ndipo Ali (as) akaenda kwenye kaburi la Mtume wa Mwenyezi Munguhuku akipiga kelele kwa kulia na kuita: 'Ewe mtoto wa ami yangu hakika watu wamenidhoofisha na wamekaribia kuniuwa.'........"mpaka mwisho.

**Nasema:** Ni kana kwamba Umar bin Khattab alikuwa amesahau ule udugu aliyouunga Mtume (saww) kati ya Maswahaba zake, na amesahau kuwa hakika yeye (saww) aliunga udugu kati yake mwenyewe na Ali bin Abu Talib (as) kama ulivyosoma hilo katika mlango usemao: "Ali ni ndugu wa Mtume (saww)". Hivyo Umar akakanusha udugu huo baada ya kifo cha Mtume (saww) ikiwa bado ni muda mchache tu tangu kufariki kwake (saww), hivyo akasema: 'Ama mja wa Mwenyezi Mungu ni sawa, na ama kuhusu ndugu wa Mtume Wake hapana.'

Vyovyote iwavyo ni kwamba, ikiwa iliwezekana kwa ummah wa Musa (as) kukongamana katika kumfanya ndama kuwa Mungu kwa kumshirikisha Mwenyezi Mungu baada ya kuona miujiza mbalimbali ya wazi, na kumuacha Harun (as) baada ya kukaribia kumuua, basi pia inawezekana kwa urahisi zaidi kwaMaswahaba wengi kufanya kosa la kumfanyaAbu BakrKhalifa na kumuacha Ali (as) baada ya kukaribia kumuua.

Na sababu ya urahisi huo ni kwamba huyo waliye jitenga mbali naye ambaye ni Ali (as), ukimlinganisha na Harun hakuwa na ukaribu zaidi wa nasaba kwa Mtume (saww) kushinda ule aliokuwa nao Harun (as) kwa Musa (as), kwa nini isiwe hivyo wakati Harun (as) alikuwa ni ndugu wa Musa (as) kinasaba namshirikawake katika amri na unabii wake kama tulivyotaja.[527] Lakini Ali (as) alikuwa ni mtoto wa ami ya Mtume (saww) katika nasaba na pia alikuwa ni Khalifa wake kwa ummah wake lakini si mshirika wake katika unabii wake,[528]kama ambavyo yule waliyemkimbilia ambaye ni Abu Bakr alikuwa na haraka zaidi kushinda hatawaliyoifanya watu wa Musa (as). Kwa nini isiwe hivyo

[527] Ambapo watu wa Musa (a. S.) walikuwa na yakini kwamba Musa ametoka tu kwenda mlimani kuongea na Mola Wake, lakini atarudi na watakabiliana naye – hawakuogopa hilo. – **Mhariri**

[528] Na ummah wa Muhammad (s.a.w.w.) walikuwa na yakini kwamba yeye (s.a.w.w.) amekwisha kufariki na hatorudi tena, hivyo ni rahisi kutokuwa na sababu ya kuhofia kumuasi Ali (a. S.). –Utakapoisoma mifano miwili hii kwa ulinganisho bila taasubi, utapata picha halisi ya jinsi historia zinavyopinduliwa**,** ukweli kufanywa batili na batili kufanywa ndio kweli **– Mhariri**

wakati yule ndama alikuwa ni kiwiliwili chenye sauti kama ilivyokuja katika Qur'ani, lakiniAbu Bakr alikuwa ni kiumbe mwenye roho anazungumza na kuhutubia? Zaidi ya hapo ni kwamba watu wa Musa (as) walimfanya ndama kuwa mungu mwenye kuabudiwa, lakini kundi la Maswahaba walimfanya Abu Bakr kuwa Khalifa mwenye kutiiwa si mshirika pamoja na Mwenyezi Mungu Mtukufu, na hata kama hilo ni dogosana ukilinganisha na kumshirikisha Mwenyezi Mungu, lakini hizi ni sababu zinazoonesha uwezekano wa Maswahaba wengi kufanya kosa kwa urahisi zaidi la kumfanya Abu Bakr Khalifana kumuacha Ali (as).

Kwa ujumla ni kwamba, mwenye kutaamali katika maudhui hii haoni kuwa ni jambo geni lililo mbali na akili, lile walilotenda Maswahaba wengi baada ya Mtume (saww) licha ya kuwepo tamko la Mtume juu ya uimamu wake. Hiyo ni baada ya kutokea mfano wa hilo kwa watu wa Musa (as) pale walipomuacha Harun (as) japokuwa tayari kulikuwa na tamko juu yake. Hakika yatakapochunguzwa yale maelezo mengi yaliyopokewa kutoka kwa Mtume (saww) ambayo yote yanaonesha yale yote waliyoyatenda Maswahaba zake baada yake, atagundua kuwa maelezo hayo ni ishara bayana inayokaribia kuwa tamko na wala si ishara tu, kwanialiwapa habari kuwa wapo watu katika Maswahaba zake wataritadi kwa visigino vyao baada ya yeye kuachana nao, na kuwa wao watazusha watakayoyazusha baada yake. Na ni suala lililowazi kwamba hakuna kitu kilichotokea toka kwa Maswahaba wake baada yake isipokuwa ni kuacha kwao tamko nyuma ya migongo yao na kujitenga mbali na Ali (as) kwa visingizio tofauti, kama vilekuwa na umri mdogo[529]- kama alivyoelezea Ibn Qutaybah katika al-*Imamah Was-Siyasah* anapozungumzia kitendo cha Ali (as) kukataa kumpa Abu Bakr kiapo cha utii.

Au kwa kumuonea husuda kutokana nakuwa na fadhila nyingi kama vile yeye kuwa mtu wa kwanza aliyesilimu na kuswali, au yeye kuwa mmoja kati ya wale ambao Mtume (saww) aliapizana na Wakristo kupitia wao, bali ni kwamba Mwenyezi Mungu ndani ya Kitabu Chake amemfanya nafsi ya Mtume (saww) na akasema:**"Na nafsi zetu"**, au kuwa kwake mmoja kati ya wale walioteremshiwa Aya ya utakaso, au yeye kuwa mhusika wa hadithi ya cheo, au hadithi ya bendera ya siku ya Khaibari, au hadithi ya ndege wa kuchoma, au hadithi ya kuunga udugu, au hadithi ya kufunga milango yote ya msikiti isipokuwa mlango wake, na fadhila nyingine nyingi ambazo zinamfanya awe mwenye kuhusudiwa na watu wengi isipokuwa wachache wale ambao Mwenyezi Mungu amewathibitishia uongofu Wake.

Au kwa kuwa yeye ni mkali katika dini ya Mwenyezi Mungu, shujaa wa vita ambaye aliwauwa mabwana na makomandoo wa Kiarabu, kiasi kwamba dini haikusimama isipokuwa kwa upanga wake, hivyoWaarabu wakamfanyia uadui. Wakati wa uhai wa Mtume (saww) hawakuweza kumfanyia uovu wowote, lakini Mtume (saww) alipofariki wakatumia fursa na wakasaidiana katika kumpokonya mamlaka kutoka mikononi mwake. Na mengineyo mengi miongoni mwa sababu.

Hizi hapa baadhi ya njia za maelezo yanayoonesha kuwa watu miongoni mwa Maswahaba wataritadi baada ya Mtume (saww), sisi hapa tutakomea kutaja kwa ufupi tu yale yaliyopokewa na waandishi wa *Sahih* na si wengineo.

Bukhari katika *Sahih* yake katika kitabu kinachozungumzia mwanzo wa uumbaji, katika mlango wa kauli ya Mwenyezi Mungu: **"Na Mwenyezi Mungu akamfanya Ibrahimu khalili"**, amepokea kwa sanadi yake kutoka kwa Ibn Abbas kutoka kwa Mtume (saww) kuwa alisema: "Hakika nyinyi mtafufuliwa mkiwa pekupeku, uchi na wapweke. Kisha akasoma:**"Kama tulivyoanza umbo la mwanzo tutalirudisha tena. Ni ahadi iliyo juu yetu. Hakika Sisi ni watendao."** Na wa kwanza atakayevishwa nguo

[529] Mbona suala la umri mdogo wa Ali (a. S.) linajitokeza katika mas'ala za maslahi na vyeo tu, ndio amekuwa hakustahili kwa kuwa alikuwa mdogo! Mbona katika mas'ala za uwajibikaji mzito kama wa vita, wakubwa hao hawakumwambia asiwajibike kwa vile ni mdogo! Mathalan vita vya Khaybar ama vya Khandaq, pale Amr bin Abd al-Wudd aliponadi: 'huyu Ali ni mtoto, nataka atoke mtu mkubwa,' na walikuwepo wakubwa hao mashuhuri lakini hawakutoka! Huyo mtoto ndiye aliyeleta ushindi kote! **"…..Basi mna nini ninyi? Mnahukumu vipi nyie? (10:35) - Mhariri**

siku ya Kiyama ni Ibrahim, na hakika kuna watu miongoni mwa Maswahaba zangu watavutwa upande wa kushoto, nitasema: ‘Maswahaba zangu, Maswahaba zangu.’Atasema: ‘Hakika wao hawakuacha kuritadi kwa kurudi nyuma kwa visigino vyao tokea ulipoachana nao.’ Nitasema kama alivyosema mja mwema: **‘Na mimi nilikuwa shahidi juu yao nilipokuwa nao. Na uliponifisha ukawa Wewe ndiye Muangalizi juu yao. Na Wewe ni shahidi juu ya kila kitu. Ukiwaadhibu basi hao ni waja Wako. Na ukiwasamehe basi Wewe ndiye Mwenye nguvu na Mwenye hikima.’”**

Na pia ameipokea kwa sanadi nyingine kwa matamko yenye kukaribiana katika kitabu kinachozungumzia mwanzo wa uumbaji, katika mlango wa kauli ya Mwenyezi Mungu: **“Na mtaje Maryam katika Kitabu.”**Na katika kitabu cha tafsiri katika mlango wa: **“Na nilikuwa shahidi juu yao.”** Amesema humo:“Nitasema: Ewe Mola, Maswahaba zangu. Atasema: Hakika wewe hujui waliyozua baada yako. Hapo nitasema kama alivyosema mja mwema:**‘Na mimi nilikuwa shahidi juu yao nilipokuwa nao.’**” mpaka mwisho.

Na pia ameipokea katika kitabu cha tafsiri katika mlango wa:**“Kama tulivyoanza umbo la mwanzo tutalirudisha tena.”** Na katika kitabu kinachozungumzia uwanja wa hesabu, katika Mlango unaozungumzia jinsi ufufuo utakavyokuwa. Na pia katika kitabu kinachozungumzia uwanja wa hesabu, katika Mlango unaozungumzia Hodhi, humo ameipokea kwa njia mbalimbali. Na pia katika kitabu kinachozungumzia fitna, hadithi ya pili.

Na pia Muslim ameipokea katika *Sahih* yake katika kitabu cha twahara, katika mlango unaosema kuwa ni mustahabu kurefusha uso katika udhu. Na katika kitabu kinachozungumzia fadhila, katika mlango wa kuthibitisha Hodhi ya Mtume wetu, humo ameipokea kwa njia mbalimbali. Na pia katika kitabu kinachozungumzia pepo, katika Mlango unaozungumzia kutoweka kwa dunia.

Na pia Tirmidhiy ameipokea katika *Sahih* yake Juz. 2, uk. 68, kwa njia mbili, na katika Juz. 2, uk. 199 kaipokea kwa njia mbili nyingine. Na an-Nasaiy ameipokea katika *Sahih* yake Juz. 1, uk. 195. Na pia ameipokea Ibn Majah katika *Sahih*yake katika milango ya ibada, katika uk. 226.

Pamoja na haya pia kuna ishara ya wazi iliyopokewa kutoka kwa Mtume (saww) kumhusuAbu Bakr, kuwa yeye atazua atakayozua baada yake (saww), kwani Imam Maliki bin Anas katika *Sahih* yake inayoitwa *al-Muwatwa* katika kitabu kinachozungumzia jihadi, katika uk. 197, amepokea kwa sanadi yake kutoka kwa Abi Nadhiru bwana wa Umar bin Ubaydullah kwamba zilimfikia habari kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema kuwaambia mashahidi wa Uhudi: “Hawa mimi ni shahidi juu yao.” Abu Bakr akasema: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, je sisi si ni ndugu zao tumesilimu kama walivyosilimu na tukapigana jihadi kama walivyopigana?” Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: “Ndiyo, lakini sijui ni lipi mtakalozusha baada yangu.” Abu Bakr akalia, kisha akalia tena, kisha akasema: “Hivi kweli sisi tutakuwa hivyo baada yako!”

**Nasema:** Na jambo la kushangaza ni kwamba wanazuoni wa Kisuni baada ya kushindwa kujadili sanadi za hadithi hizi zinazosema kuwa watu miongoni mwa Maswahaba wataritadi, wao wamezitafsiri kuwa kuna watu miongoni mwa mabedui watakataa kutoa Zaka, kama Maliki bin Nuwayrah na wengineo ambao waliishi nje ya Madina na wala hawakumuona Mtume (saww) umri wake wote isipokuwa mara moja au mbili au inayo karibiana na hiyo.

Hakika tafsiri hii iko mbali na makusudio katika maneno mawili: Kwanza ni katika neno “kuritadi,” hakika Mtume (saww) alitoa tamko – kama ulivyotambua hilo kutokana na riwaya mutawatiri - na akatangaza bayana kwamba yeye ni mwenye mamlaka zaidi kwa waumini kuliko hata waliyonayo juu ya nafsi zao, na Maswahaba zake wakakiri hilo, kisha akasema: “Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake – yaani mwenye mamlaka zaidi kwake kuliko hata aliyonayo juu ya nafsi yake - basi Ali ni mtawala wake,

hiyo ni baada ya kuwazindua juu ya kukaribia kufa kwake kama ilivyotangulia, na hali hiyo ni kiashiria yakinifu kinachoonesha kuwa yeye (saww) alikuwa katika nafasi ya kutoa wasia na kumtangaza Khalifa. Kisha akafariki na kwenda kwa Mola Wake, na huku nyuma Maswahaba zake wakamuasi na wakaliacha tamko nyuma ya migongo yao na wakamfanya Abu Bakr Khalifa kwa kubadili na kumfuata mtu ambaye si yule walioambiwa.

Wakaishambulia nyumba ya Fatimah (as) na wakakaribia kuichoma moto pamoja na wale waliokuwemondani yake. Humo alikuwemo bibi mbora kushinda wanawake wote, ambaye yeyote atakayemuudhi basi atakuwa amemuudhi Mtume (saww), kama utakavyosikia mahali pake. Na wakamtoa Ali (as) na wakakaribia kumuuwa kama ulivyosikia, naye ni ndugu wa Mtume (saww), mkwe wake, mtoto wa ami yake na baba wa wajukuu zake. Na ni miongoni mwa wale ambao Mwenyezi Mungu amewaondoshea uchafu na kuwatakasa barabara, naye kwa Mtume (saww) ana cheo sawa na cheo cha Harun (as) kwa Musa (as). Hivyo neno“kuritadi” lililopo katika maelezo hayo yaliyotangulia kulitafsiri kwa maana yamatukio haya mabaya ni bora na inastahiki zaidikuliko kulitafsiri kwa maana ya mabedui waliokataa kutoa Zaka.

Pili ni katika neno “Maswahaba.”Hakika kulitafsiri neno hili kwa maana ya yule aliyesuhubiana na Mtume (saww) katika safari zake, nyumbani, vitani, katika faragha yake na katika mikusanyiko yake, naalikuwa akihudhuria pamoja naye kwenye Swala tano, katika jamaa na ijumaa, na wala hajawahi kuachana naye katika kikao chochote, mtu kama vileAbu Bakr, Umar, Uthman, Abdur-Rahman bin Awf, Saad bin Abi Waqas, Abu Ubaydah bin Jarah na mfano wa hao, hakika tafsiri hiyo ndio iliyo karibu zaidi na neno husika kuliko kulitafsiri kwa maana ya watu ambao hawakuishi isipokuwa nje ya Madina na wala hawakumuona Mtume (saww) katika umri wao wote isipokuwa mara moja au mbili au inayokaribiana na hiyo.

Naapa kwa umri wangu, hakika haya yote yako wazi hayahitaji kurefusha maneno, kuendelea kuvunja hoja au kudhihirisha, isipokuwa ni kwamba yule ambaye Mwenyezi Mungu hajampa nuru hawezi kuwa na nuru yoyote, na yule ambayeMwenyezi Mungu ameupofoa moyo wake kamwe hana dawa zaidi ya moto. Mwenyezi Mungu anasema:**“Na tumeiumbia Jahannamu majini wengi na watu. Wana nyoyo, lakini hawafahamu kwazo. Na wana macho, lakini hawaoni kwayo. Na wana masikio, lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama nyama howa, bali wao ni wapotofu zaidi. Hao ndio walioghafilika.”**

Na tuhitimishe maneno yetu kwa beti za Hassan bin Thabit Al-Ansariy katika kisa cha Ghadir. Hakika yeye alikuja kwa Mtume (saww) akamuuliza: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu unaniruhusu katika kisimamo hiki kusema yale yanayomridhisha Mwenyezi Mungu?” Akamwambia: “Sema ewe Hassan kwa jina la Mwenyezi Mungu.” Akasimama kwenye ardhi na Waislamu wakamkusanyikia kusikia maneno yake, akaanza kusema:

“Mtume wao aliwaita siku ya Ghadir Khum

na ninamsikia Mtume akinadi.

Akasema: Basi ni nani mwenye mamlaka kwenu

na Walii wenu? Wakajibu bila kuonekana asiyejua.

Mungu Wako ndiye Mwenye mamlaka kwetu na

wewe ndiye Walii wetu, na wala leo hutapata uasi kutoka kwetu.

Akamwambia simama ewe Ali, hakika mimi nimekuridhia

baada yangu kuwa Imam na kiongozi.

Hivyo yeyote ambaye mimi ni mwenye mamlaka kwake

basi huyu ni mtawala wake, hivyo kuweni watetezi

wa kweli kwake na wenye kumtawalisha.

Hapo akaomba, Ewe Mungu Wangu mpende mwenye kumpenda

na mfanyie uadui yule mwenye kumfanyia Ali uadui."

Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akamwambia: "Ewe Hassan! utaendelea kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu (Jibril) wakati wote utakapotunusuru kwa ulimi wako." – Wameyataja hayo wanahistoria wengi kutoka pande zote mbili.

Kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na neema zake, imetimia juzuu ya kwanza ya kitabu chetu kinachoitwa: **Fadhila za watukufu watano kutoka katika Sahihi sita**.

Na tunaomba swala na salamu za Mwenyezi Mungu zimwendee Mtume Muhammad na Aalii zake ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na kuwatakasa barabara.

Inayofuata ni juzuu ya pili, itakayoanza na Mlango unaozungumzia kauli ya Mtume (saww): **"Ali ni Walii wenu baada yangu."**

# BIBLIOGRAFIA


1. *Sahih Bukhari*cha Muhammad bin Ismail. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Khayriyyah huko Misri, mwaka 1320.
2. *Sahih Muslim*cha Imam Muslim bin al-Hajaj Nisaburiy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na Bulaqu, mwaka 1320.
3. *Sahih Tirmidhiy*cha Muhammad bin Isa. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na Bulaqu, mwaka 1292.
4. *Sahih an-Nasaiy*cha Ahmad bin Shuaybuan-Nasaiy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Maymaniyyah huko Misri, mwaka 1312.
5. *Sahih Abi Daud*cha Abi Daud Sijistaniy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Kastaliyyah, mwaka 1280.
6. *Sahih Ibn Majah al-Qazuwiniy*. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Faruqiy huko Delhi.
7. *Mustadrakus-Sahihayn* cha al-Hafidh Abu Abdullah Muhammad bin Abdullah Nisaburiy, mashuhuri kwa jina la al-Hakim. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na Majlis Dairatul-Maarif an-Nidhamiyyah, huko Haidar Abad Dukn, mwaka 1324.
8. *Musnad Imam Ahmad bin Hanbal*. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Maymaniyyah huko Misri, mwaka 1313.
9. *Muwata Imam Malik bin Anas*. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Hajariyyah huko Misri, mwaka 1280.
10. *Musnad Imam Abi Hanifah Nuuman*. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na Muhammady huko Lahore India, mwaka 1306.
11. *Musnad*ya Imam Abu Abdillah Muhammad bin Idirisa Shafiy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Khaliliy huko Urhu India, mwaka 1306.
12. *al-Adab al-Mufrad* cha Abu Abdullah Muhammad bin Ismail Bukhari, mwandishi wa *Sahih Bukhari*. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Khaliliy huko Urhu India, mwaka 1306.
13. *Musnad Abi Daud Twayalasiy* cha al-Hafidh Sulayman bin Daud. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na Majlis Dairatul-Maarif an-Nidhamiyyah, huko Haidar Abad Dukn, mwaka 1321.
14. *Sunan ad-Daramiy* cha al-Hafidh Abi Muhammad Abdullah bin Abdur-Rahman ad-Daramiy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Iitidal, huko Damascus, mwaka 1349.
15. *as-Sunan al-Kubra* cha al-Hafidh Abu Bakr Ahmad bin Husain bin Ali al-Bayhaqiy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na Majlis Dairatul-Maarif an-Nidhamiyyah, huko Haidar Abad Dukn, mwaka 1344.
16. *Sunan* ya Hafidh Abil-Hasan Ali bin Umar ad-Daruqutuniy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Ansariy huko Delhi.

17. *Hilyatul-Awliyai* cha Abu Naiim, ambaye ni al-Hafidh Ahmad bin Abdullah al-Isbahaniy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na as-Saadah huko Misri, mwaka 1351.

18. *Fat'hul-Bariy Fii Sharhil-Bukhariy* cha al-Hafidh Shahabud-Din Abil-Fadhli al-Asqalaniy, maarufu kwa jina la Ibn Hajar. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na Mustafal-Babiy al-Halbiy na watoto wake, huko Misri, mwaka 1378.

19. *at-Tabaqat al-Kubra* cha Muhammad bin Saad, Katib al-Waqidiy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na Baril huko Lidan, mwaka 1322.

20. *Taarikh Baghdad* cha al-Hafidh Abi Bakri Ahmad bin Ali al-Khatib al-Baghdadiy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na as-Saadah jirani na Mkoa wa Misri, mwaka 1349.

21. *Taarikh al-Umam Wal-Muluki* cha Imam Abi Ja'far Muhammad bin Jarir Tabariy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Istiqamah huko Cairo Misri, mwaka 1357.

22. *Mushkilatul-Athar* cha Abu Ja'far Twahawi, Ahmad bin Muhammad al-Misriy al-Hanafiy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na Majlis Dairatul-Maarif an-Nidhamiyyah, huko Haidar Abad Dukn, mwaka 1333.

23. *Sharhu Maanil-Athari* cha Abi Ja'far Twahawi. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Mustafaiy, mwaka 1300.

24. *al-Athar* cha Muhammad bin Hasan Shaybaniy, mwanafunzi wa Abu Hanifa. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na An'wari Muhammady huko Lahoro India.

25. *Usudul-Ghabah* cha Izzud-Din Abul-Hasan Ali bin Muhammad, maarufu kwa jina la Ibn Athir. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Wahabiyyah huko Misri, mwaka 1285.

26. *al-Istiaab* cha al-Hafidh Abi Umar Yusuf bin Abdullah, maarufu kwa jina la Ibn Abdul-Bari. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na Dairatul-Maarif huko Haidar Abad Kusini mwa India, mwaka 1336.

27. *Al-Isabah* cha al-Hafidh Shahabud-Din Ahmad bin Ali bin Muhammad al-Asqalaniy, maarufu kwa jina la Ibn Hajar. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala iliyochapishwa huko Misri kwa kufuata chapa ya mwaka 1853 Miladiyyah huko Calcutta.

28. *Tahdhibut-Tahdhib* cha Sheikhul-Islam Shahabud-Din Ahmad bin Ali bin Hajar al-Asqalaniy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala iliyopigwa chapa na Majlis Dairatul-Maarif an-Nidhamiyyah, huko Haidar Abad Dukn, mwaka 1325.

29. *Mizanul-Itidal* cha al-Hafidh Shamsud-Din Muhammad bin Ahmad, maarufu kwa jina la Dhahbiy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na as-Saadah jirani na Mkoa wa Misri, mwaka 1325.

30. Tafsiri ya Qur'ani inayoitwa *Jamiul-Bayan* ya Imam Abi Ja'far Muhammad bin Jarir Tabariy aliyefariki mwaka 310. Nimechukua hadithi kutoka kwenye chapa ya kwanza iliyopigwa chapa na al-Kubra huko Bulaqu Misri, Mwaka 1323.

31. Tafsiri ya Qur'ani inayoitwa *al-Kashaf An Haqaiq Ghawamidhut-Tanzil* ya Mahmudu bin Umar

Zamakhshariy aliyefariki mwaka 528. Nimechukua hadithi kutoka kwenye chapa ya kwanza iliyopigwa chapa na Mustafa Muhammad, Mwaka 1354, Mmiliki wa maktaba kubwa ya kibiashara huko Misri.

32. Tafsiri ya Qur'ani inayoitwa *Mafatihul-Ghaybi* ambayo ni mashuhuri kwa jina la *Tafsirul-Kabir* ya Imam Muhammad Razi Fakhrud-Din, mtoto wa Allamah Dhayaud-Din Umar, maarufu kwa jina la Hatibu wa Ray, aliyefariki mwaka 606. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na Darut-Twabaah al-Amirah.

33. Tafsiri ya Qur'ani inayoitwa *ad-Durul-Manthur Fii Tafsiri Bil-Maathuri* ya Imam mkubwa Jalalud-Din Abdur-Rahman Abu Bakri Suyutiy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Maymaniyyah huko Misri, mwaka 1314.

34. *Asbabun-Nuzul* cha Sheikh Imam Abul-Hasan Ali bin Ahmad mashuhuri kwa jina la al-Wahidiy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na Hindiyyah huko Ghaydhun-Nuwabiy, mwaka 1315.

35. *Qusasul-Anbiyai*kinachoitwa *Araisut-Tijan*cha Ahmad bin Muhammad bin Ibrahim Thaalabiy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Haydariy huko Bombay, mwaka 1294.

36. *Khasa'isu Amiril-Muuminin Ali bin Abu Talib (as)* cha al-Hafidh al-Hujah Abu Abdur-Rahman Ahmad bin Shuaybu an-Nasaiy mwandishi wa *Sahih an-Nasaiy*. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na at-Taqadumu al-Ilmiyyah huko Misri, mwaka 1348.

37. *Al-Imamah Was-Siyasah* cha Abu Muhammad Abdullah bin Muslim, maarufu kwa jina la Ibn Qutaybah. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Futuhul-Adabiyyah, mwaka 1331.

38. *Majmauz-Zawa'id* cha al-Hafidh Nurud-Din Ali bin Abu Bakr al-Haythamiy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyochapishwa mwaka 1352, ambayo ilichapishwa na mmiliki wa maktaba al-Qudsiy Hasamud-Din al-Qudsiy.

39. *Kanzul-Ummal* cha al-Mutaqiy al-Hindiy. Asili ya kitabu ni *Jam'ul-Jawamiu* cha al-Hafidh Suyutiy, hadithi zake zilikuwa zimeandikwa kwa kufuata utaratibu wa alfabeti, ndipo al-Mutaqiy akazipangilia kwa kufuata mfumo wa vitabu vya Fiqhi na akakiita *Kanzul-Ummal Fii Sunanul-Aqwali Wal-Af'ali*. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na Dairatul-Maarif an-Nidhamiyyah huko Haidar Abad Dukn, mwaka 1312.

40. *Faydhul-Qadir* cha Allamah Abdur-Rauf al-Munawi, nacho ni ufafanuzi wa *al-Jamiu as-Saghiru* cha Suyutiy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Mustafa mmiliki wa maktaba kubwa ya kibiashara huko Misri, mwaka 1356.

41. *Kunuzul-Haqaiq Fii Ahadith Khayrul-Khalaiq* cha Allamah Abdur-Rauf al-Munawi. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyochapishwa huko Istanbul mwaka 1285, kwa uhariri wa Hafidh Husain al-Halmiy.

42. *ar-Riyadh an-Nadhrah* cha al-Hafidh Ja'far Ahmad bin Abdullah, mashuhuri kwa jina la al-Muhibu Tabariy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa ya kwanza iliyopigwa chapa na al-Itihadi al-Misriy.

43. *Dhakhairul-Uqbah* cha al-Hafidh Abu Ja'far Ahmad bin Abdullah, mashuhuri kwa jina la al-Muhibu Tabariy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyochapishwa mwaka

1356, ambayo ilichapishwa na mmiliki wa maktaba al-Qudsiy Hasamud-Din al-Qudsiy.

44. *Sawa'iqul-Muhriqah* cha Shahabud-Din Ahmad bin Hajar al-Haythamiy. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Maymaniyyah huko Misri, mwaka 1312.

45. *Mirqatul-Mafatihi* cha Ali bin Sultan Muhammad al-Qariu, nacho ni ufafanuzi wa *Mishkatul-Maswabihi* cha al-Khatib at-Tabriziy Waliyud-Din Muhammad bin Abdullah. Na *al-Mishkatu* ni ufafanuzi wa *al-Maswabihu* cha Abu Muhammad Husain bin Mas'ud al-Farau al-Baghawi. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Maymaniyyah huko Misri, mwaka 1309.

46. *Nurul-Absari* cha Aalim al-Fadhil Sheikh Shabalanjiy, anayeitwa Muuminu. Nimechukua hadithi kutoka kwenye nakala ya chapa iliyopigwa chapa na al-Maymaniyyah huko Misri, mwaka 1322.

# OORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A. S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A. S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashariyyah
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera

31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a. S)
38. Adhana
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusherehekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mtume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mtume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mtume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi

64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Huduma ya Afya katika Uislamu

97. Sunan an-Nabii
98. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
99. Shahiid Mfiadini
100. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
101. Ujumbe - Sehemu ya Pili
102. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
103. Ujumbe - Sehemu ya Nne
104. Kumswalia Nabii (s.a.w.w.)
105. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
106. Hadithi ya Thaqalain
107. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
108. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
109. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
110. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
111. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
112. Safari ya kuifuata Nuru
113. Fatima al-Zahra
114. Myahudi wa Kimataifa
115. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
116. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
117. Muhadhara wa Maulamaa
118. Mwanadamu na Mustakabali wake
119. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
120. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
121. Khairul Bariyyah
122. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
123. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
124. Yafaayo kijamii
125. Tabaruku
126. Taqiyya
127. Vikao vya furaha
128. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
129. Visa vya wachamungu

130. Falsafa ya Dini
131. Kuhuzunika na Kuomboleza - Azadari
132. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
133. Kuonekana kwa Allah
134. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
135. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
136. Ushia ndani ya Usunni
137. Maswali na Majibu
138. Mafunzo ya hukmu za ibada
139. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
140. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
141. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
142. Abu Huraira
143. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
144. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
145. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Pili
146. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
147. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
148. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
149. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a. S)
150. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
151. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
152. Uislamu Safi
153. Majlisi za Imam Husein Majumbani
154. Uislam wa Shia
155. Amali za Makka
156. Amali za Madina
157. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
158. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
159. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
160. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
161. Umoja wa Kiislamu na Furaha
162. Mas'ala ya Kifiqhi

163. Jifunze kusoma Qur'ani
164. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
165. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
166. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
167. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
168. Uadilifu katika Uislamu
169. Mahdi katika Sunna
170. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
171. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
172. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
173. Vijana na Matarajio ya Baadaye
174. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
175. Ushia – Hoja na Majibu
176. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
177. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a. S.)
178. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
179. Takwa
180. Amirul Muuminina ('as) na Makhalifa
181. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (a. S.)
182. Kuelewa Rehma ya Mwenyezi Mungu
183. Mtazamo kuhusu msuguano wa kimadhehebu
184. Upotoshaji Dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
185. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
186. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah kwa Imam Ali (a. S.)
187. Uongozi wa kidini – Maelekezo na utekelezaji wa Kijamii

# KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba'Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

MUHTASARI

# MUHTASARI